# WAULIZE WANAOFAHAMU

## KIMEANDIKWA NA: MUHAMMAD TIJANI AS-SAMAWI AT-TUNISI

### KIMETARJUMIWA NA: MUSABAH SHABAN MAPINDA

### UTANGULIZI:

### ALLAMAH SAYYID SAEED AKHTAR RIZVI

Kwa Jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu. Kitabu kilichopo mikononi mwako ni tafsiri ya kitabu cha Kiarabu kiitwacho Fas'alu Ahladh-Dhikr kilichoandikwa na Shaikh Muhammad Tijani Samawi wa Tunisia. Ndani ya Kitabu hiki ameelezea mkusanyiko wa itikadi za Kiislamu kwa namna zilivyo ndani ya Qur'an na Sunna Tukufu ya Mtume **(s.a.w.w)**. Kitabu hiki ni kama vile vya mwanzo, nacho kimepata umaarufu hasa kutokana na jinsi mwandishi alivyozichambua itikadi hizo kwa mujibu wa mtazamo wa Sunni na Shia, kisha akayabainisha maeneo wanayohitilafiana. Kwa mara nyingine tena mimi binafsi sikusita kumuomba Shaikh Musabah Shaban Mapinda kukitafsiri kitabu hiki katika lugha ya Kiswahili kutoka kwenye asili yake ya lugha ya Kiarabu. Sababu iliyoifanya Tasisi zetu isimamie kazi hii ni kama zile za mwanzo, ambayo inatokana na maombi ya Maulamaa wengi katika Afrika Mashariki kututaka tukifasiri kitabu hiki kiingie kwenye lugha ya Kiswahili. Namshukuru Shaikh Musabah kwa kuifanya kazi hii kwa moyo mmoja. Nimeiangalia pamoja naye tafsiri hii kwa makini kuhakikisha kuwa maudhui yake ya asili hayakupotoshwa katika lugha ya Kiswahili. Shaikh Tijani Samawi ameandika vitabu vifuatavyo, Thummah-Tadaytu, Li Akuna Ma'as-Sadiqin na Fa'salu Ahladh-Dhikr, na Sheikh Musabah Shaban Mapinda amezitafsiri vitabu zote tatu za mwandishi huyu chini ya Tasisi ya Ahlul-Bayt (a.s) Assembly of Tanzania (ABATA) kwa lugha ya kiswahili viitwavyo Hatimaye Nimeongoka, Hi Niwe Pamoja Na Wakweli na Waulizeni Wanaofahamu, vilivyo pangwa katika kompyuta na Ahlul-Bayt (a.s) Assembly of Tanzania na kuchpishwa na Bilal Muslim Mission of Tanzania.

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu tena kwani vitabu zetu "Hatimaye Nimeongoka na Hi Niwe Pamoja Na Wakweli "kimependwa mno na wasomaji na hivyo kutupa ari ya kuchapisha hiki ulichonacho mkononi. Ushahidi wa kupendwa kwa kitabu hicho ni shukurani na pongezi tunazozipokea toka kwa wasomaji kwa namna mbalimbali ikiwemo kutuandikia barua n.k. BILAL na ABATA zinatoa shukurani kwa mfasiri na wale wote waliosaidia kwa njia moja au nyingine katika uchapishaji wa kitabu hiki. Wa Ma Tawfeeqi IlIa Billah Sayyid Saeed Akhtar Rizvi Dar-es-salaam 29th Zilqaadah, 1422 13th Feb, 2001.

## DIBAJI

### KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU, MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU

Sifa njema anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa Walimwengu, na Sala njema na salamu zimshukie Bwana wetu Muhammad aliyetumwa awe ni Rehema kwa walimwengu, ni Bwana wa waliotangulia hapo mwanzo na waliokuja baadaye. Naye ametakasika kutokana na kila kinachochukiza, na (Sala na Salamu) ziwashukie (watu wa) kizazi chake waliowema tena watakatifu, (ambao) ndiyo bendera ya uongofu na taa iondowayo kiza (tena wao) ndiyo viongozi wa Waislamu.

Ama Ba'd, Haya ni masuali niliyoyaandaa hasa kwa Waislamu wanaofanya utafiti, wakiwemo Waislamu wa Madhehebu ya Sunni ambao wanadhani kwamba wao peke yao ndiyo wanaoshikamana na Sunna sahihi ya Mtume, Sala njema na Salamu zimshukie (yeye Mtume) na watu wa kizazi chake waliotakasika, (na zaidi ya hapo) wao Sunni wanashikilia (msimamo) wa kuwapinga wasiokuwa wao miongoni mwa Waislamu wengine na huwataja kwa majina mabaya. Na kwa hakika kumetumwa vikundi vipya katika sehemu mbali mbali za nchi za Kiislamu kwa jina la kutetea Sunna ya Mtume Muhammad **(s.a.w.w)** na kwa Jina la kunusuru sunna na kuwatetea Masahaba, na kumeandikwa vitabu vingi kuwashutumu na kuwakufurisha Mashia na Maimamu wao na kuwakejeli wanavyuoni wao, navyo vyombo vya habari vya Ulimwengu vimeeneza fikra hii kwenye nchi zote za Ulimwengu wa Kiislamu na zile zisizokuwa za Kiislamu (kiasi kwamba) leo mazungumzo ya watu yamekuwa ni juu ya "Usunni na Ushi'a." Mara nyingi nimekuwa nikikutana katika minasaba mbali mbali na baadhi ya vijana wenye taaluma miongoni mwa Waislamu wa kweli ambao wanajiuliza na kuuliza kuhusu uhakika wa Shi'a na upotovu wao, hali ya kuwa ni wenye kuchanganyikiwa kati ya mambo wayaonayo na kuishi nayo pamoja na rafiki zao miongoni mwa Mashi'a, na yale wanayoyasikia na kuyasoma kuhusu Mashi'a na wanashindwa kufahamu haki inapatikana wapi. Nilipata kuzungumza na baadhi yao na nikawazawadia kitabu changu (kiitwacho) "Thummah-Tadaitu", Nanamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba wengi miongoni mwao na (hasa) baada ya majadiliano na utafiti, wanaongoka kwa kuufahamu ukweli na wanaufuata. Lakini hali hii inabakia kwa kikundi kidogo miongoni mwa vijana ambao inatokezea kukutana nao, ama waliobakia huenda wasipate nafasi kama hii ya kukutana nao, basi watabakia ni wenye fikra iliyochanganyikiwa baina ya maoni yanayopingana.

Japokuwa kuna dalili zinazokinaisha na hoja madhubuti ndani ya kitabu (kiitwacho) Thummah-Tadaitu na kitabu (kiitwacho) Ma'as-Sadiqina, lakini vitabu hivyo havitoshelezi kukabili mashambulizi na madai mengi (ya uongo) ambayo yanadhaminiwa kipesa na baadhi ya nchi ovu kutokana na mafuta (waliyonayo) na dollar (walizonazo) kwa kupitia njia mbali mbali za upashaji habari. Pamoja na yote hayo, sauti ya haki itaendelea kuvuma katikati ya makelele yanayoudhi, na nuru itabakia inang'ara katikati ya kiza nene, kwani ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya kweli na hapana budi itimie. Mwenyezi Mungu anasema:

يُرِيدُونَ لِيُطْفِئُوا نُورَ اللَّـهِ بِأَفْوَاهِهِمْ وَاللَّـهُ مُتِمُّ نُورِهِ وَلَوْ كَرِهَ الْكَافِرُونَ ﴿٨﴾

"Wanataka kuizima nuru ya Mwenyezi Mungu kwa vinywa vyao, naye Mwenyezi Mungu ataikamilisha nuru yake japokuwa makafiri watachukia." (Qur'an 61:8).

Na amesema Mwenyezi Mungu akibainisha kwamba matendo yao haya yatashindwa na kuwageukia wao wenyewe.

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا يُنفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ لِيَصُدُّوا عَن سَبِيلِ اللَّـهِ ۚ فَسَيُنفِقُونَهَا ثُمَّ تَكُونُ عَلَيْهِمْ حَسْرَةً ثُمَّ يُغْلَبُونَ ۗ وَالَّذِينَ كَفَرُوا إِلَىٰ جَهَنَّمَ يُحْشَرُونَ ﴿٣٦﴾

"Bila shaka wale waliokufuru hutoa mali zao ili kuzuwiya (watu wasiamini) njia ya Mwenyezi Mungu, basi watazitoa (mali hizo) kisha zitakuwa majuto juu yao, hatimaye watashindwa, na wale waliodumu katika ukafiri watakusanywa katika Jahanamu". (Qur'an, 8:36).

Kwa ajili hiyo basi, imekuwa ni wajibu kwa Wanachuoni waandishi na wanafikra kuwabainishia watu mambo yanayowatatiza na kuwaongoza kwenye njia ya sawa. Mwenyezi Mungu amesema:

إِنَّ الَّذِينَ يَكْتُمُونَ مَا أَنزَلْنَا مِنَ الْبَيِّنَاتِ وَالْهُدَىٰ مِن بَعْدِ مَا بَيَّنَّاهُ لِلنَّاسِ فِي الْكِتَابِ ۙ أُولَـٰئِكَ يَلْعَنُهُمُ اللَّـهُ وَيَلْعَنُهُمُ اللَّاعِنُونَ ﴿١٥٩﴾ إِلَّا الَّذِينَ تَابُوا وَأَصْلَحُوا وَبَيَّنُوا فَأُولَـٰئِكَ أَتُوبُ عَلَيْهِمْ ۚ وَأَنَا التَّوَّابُ الرَّحِيمُ ﴿١٦٠﴾

"Bila shaka wale wanaoficha tuliyoyateremsha miongoni mwa hoja zilizowazi na uongofu, baada ya sisi kuubanisha kwa watu ndani ya kitabu, hao anawalaani Mwenyezi Mungu na kinawalaani kila chenye kulaani. Isipokuwa wale waliotubu na wakarekebisha (mienendo yao) na kubainisha (waliyokuwa wakiyaficha) basi hao nitawapokea na mimi ni Mwenye kupokea Toba na ni Mwenye huruma." (Qur'an 2:159-160).

Basi ni kwa nini wanachuoni hawasemi na kufanya uchunguzi juu ya maudhui haya kwa bidii na utakaso wa moyo kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Na iwapo Mwenyezi Mungu ameteremsha hoja zilizo wazi na uongofu, na ameikamilisha dini na kuitimiza neema (yake kwetu), na ikiwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ameifikisha amana (aliyokabidhiwa) na ameufikisha ujumbe (aliotumwa) na akatoa nasaha (njema) kwa ajili ya umma, basi ni za nini tofauti hizi na uadui, bughudha na kuitana majina mabaya na baadhi yetu kuwakufurisha wengine? Mimi hapa kwa upande wangu ninasimama msimamo ulio wazi ili niwaambie Waislamu kwamba, "Hakuna uokovu wala umoja na wala mafanikio wala pepo isipokuwa kwa kurejea kwenye misingi miwili ya asili (ambayo ni) Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Watu wa kizazi cha Mtume **(s.a.w.w)**, na (pia tutafanikiwa) kwa kupanda ndani ya meli ya uokovu, nayo ni ile Meli ya watu wa nyumba ya Mtume **(s.a.w.w)**. Maneno haya (nisemayo) siyo maneno niliyoyazusha mimi, bali ni maneno ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake **(s.a.w.w)** yaliyomo ndani ya Qur'an na Sunna tukufu ya Mtume.

Kwa hakika leo hii Waislamu wanakabiliwa na mitazamo miwili kuifikia njia ya umoja unaotakiwa.

**Kwanza**: Ni kwa Ah-lus-Sunnati Wal-Jama'a kuyakubali Madh-hebu ya watu wa nyumba ya Mtume **(s.a.w.w)** ambayo yanafuatwa na Shia Imamiyyah Al-Ithna'Ashariyyah peke yao. Kwa maana hiyo yawe ni Madh-

hebu ya tano kwao wao, na watumie mfumo wake wa Kifiq-hi kama wanavyotumia katika Madh-hebu manne ya Kiislamu. Wasiyatie dosari wala kuwatuhumu vibaya kwa chochote (watu) wanaoyakubali Madh-hebu hayo ya (Shia), na wawaachie wasomi na wanafikra uhuru wa kuchagua Madhehebu wanayoyaafiki. Katika kufuata mwenendo huu, ni wajibu kwa Waislamu Masunni na Mashia, kuyakubali Madh-hebu mengine ya Kiislamu ya Kiibadhi na Zaidiyyah.

Bila shaka mwelekeo huu utauepushia umma wetu mizozo mingi na mifarakano, ingawaje hautafikia kiwango cha ufumbuzi utakaoondosha matatizo ya kihistoria ambayo yamekuwepo tangu karne nyingi (zilizopita). **Pili**: Ni kwa Waislamu wote kushikamana kwenye itikadi moja iliyowekwa na kitabu cha Mwenyezi Mungu na Mtume wake **(s.a.w.w)** na hilo litawezekana kwa njia moja, njia iliyonyooka nayo ni kuwafuata Maimamu wa Nyumba ya Mtume **(s.a.w.w)** ambao Mwenyezi Mungu amewaondolea uchafu na akawatakasa mno, na ni kwa sababu hii Waislamu wote Masunni na Mashia wameafikiana juu ya kuwa Maimamu wa nyumba ya Mtume ni wajuzi mno (wa dini), ni wenye kutangulia kwa kila kitu ikiwa ni pamoja na ucha Mungu, utakatifu, kutosheka, tabia njema, elimu na matendo (mema). Kwa upande mwingine, Waislamu wametofautiana kuhusu Masahaba wa (Mtume).

Basi hebu Waislamu na wayaache yale waliyotofautiana ndani yake na wafuate kile walichoafikiana juu yake kwa mujibu wa kauli ya Mtume (isemayo), "**Acha kinachokutia mashaka, ufanye kisichokutia mashaka**". Basi Umma wa (Kiislamu), na ushikamane kwenye jambo hilo na uwe kitu kimoja kwenye kanuni ya msingi ambayo ndiyo nguzo ya kila kitu alichokiasisi Mtume pale aliposema; "**Nimeacha kati yenu vizito viwili ambavyo mkishikamana navyo kamwe hamtapotea, kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu watu wa nyumba yangu**" Sahih Muslim.

Kwa kuwa hadithi hii ni Sahihi kwa pande zote mbili (Sunni na Shia) bali kwa Waislamu wote pamoja na tofauti za Madhehebu zao, basi ni kwa nini sehemu fulani ya Waislamu hawaitekelezi? Na lau Waislamu wote wangeitekeleza hadithi hii basi ingeleta umoja miongoni mwao, tena umoja wa Kiislamu wenye nguvu ambao usingetikiswa na upepo wala kubomolewa na kimbunga na wala usingechafuliwa na vyombo vya habari wala maadui wa Uislamu wasingefanya umoja huo ushindwe. Kwa mujibu wa itikadi yangu huo ndiyo ufumbuzi pekee utakaowaokoa Waislamu na kuwakwamua, na ufumbuzi mwingine kinyume cha huu ni upotovu na ni kauli za uongo. Na kwa yeyote atakayeifuatilia Qur'an na Sunna ya Mtume na akaifuatilia historia ya (Uislamu) kisha akayazingatia (hayo) kwa akili yake, bila shaka atakubaliana nami juu ya (maoni yangu) haya. Ama mtazamo wa kwanza ukishindikana na ulishindikana kufaulu tangu siku aliyofariki Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** Masahaba walipohitilafiana na jambo hili ndilo lililosababisha Umma (wa Kiislamu) ugawanyike na kutawanyika.

Kwa kuwa katika karne nyingi zilizopita umma (wa Kiislamu) umeshindwa kurejea kwenye muelekeo wa pili ambao ni kushikamana na Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Kizazi cha Mtume **(s.a.w.w)** tangu zamani

katika zama za Bani Ummaya na Bani Abbas na sasa hivi katika zama zetu (umma pia umeshindwa kufanya hivyo) kutokana na vyombo vya habari kupotosha ukweli na kuwahukumu upotovu na ukafiri wafuasi wa Watu wa nyumba ya Mtume **(s.a.w.w)**, basi hakuna njia iliyobakia mbele yetu isipokuwa kukabiliana wazi wazi na kuidhihirisha haki kwa kila aipendaye. Hali ya kuwa tukiulenga mfumo wa Qur'an Tukufu kwani inatoa sababu za kuthibitisha kwa kusema: "Waambie leteni hoja zenu ikiwa ninyi ni wa kweli" (Qur'an, 2:111).

Hoja na dalili hazifanywi kwa nguvu wala kwa kutumia mali, wala hazivunjwi kwa vivutio na vitisho kwa watu waliohuru ambao nafsi zao wamemkabidhi Mwenyezi Mungu peke yake, hawakuridhia na hawataridhia cho chote badala ya haki japokuwa kufanya hivyo kutawalazimu kupoteza nafsi. Basi laiti Wanachuoni wa umma (wa Kiislamu) leo hii wangekutana wakafanya mkutano ili wayatafiti mas-ala haya kwa mioyo mikunjufu na akili zenye mazingatio na nia njema, na hayo wakayafanya kwa ajili ya kuhudumia umma wa Kiislamu, na wakatenda haya ili kuondosha mifarakano na kutibu majeraha ya umma wa Kiislamu na kuimarisha umoja wake, basi hapana shaka umoja huu utakuja bila kizuwizi cho chote, wapende au wasipende kwani Mwenyezi Mungu amemuweka kwa ajili ya jambo hili Imamu kutoka katika kizazi cha Mtume **(s.a.w.w)** ambaye ataijaza (dunia) haki na uadilifu kama ambavyo (leo hii) imejazwa dhulma na ujeuri.

Imam huyu ni kutoka katika kizazi kitukufu, na imekuwa kama kwamba Mwenyezi Mungu mtukufu ameupa mtihani umma huu kwa muda wote wa kuwepo kwake, mpaka pale muda wake utapokaribia ataudhihirishia umma kosa la uchaguzi wake, na ataupa fursa ya kurejea kwenye haki na kufuata njia ya asili ambayo Mtume Muhammad **(s.a.w.w)** aliilingania na alikuwa akisema: "**Ewe Mwenyezi Mungu! waongowe watu wangu kwani wao hawafahamu**". Na mpaka utakapofika wakati huo mimi "ninatoa kitabu changu hiki "**Fas-Alu Ahl-Ladhikri**" ambacho kimekusanya maswali na majibu kwa mujibu wa msimamo na mafundisho ya Maimamu wa Nyumba ya Mtume **(s.a.w.w)** Huenda Waislamu wakafaidika kwayo katika kila nchi ya Kiislamu na kisha wafanye (juhudi) ya kuunganisha maoni kwa ajili ya kuandaa umoja unaotafutwa.

Hayatakuwa mafanikio yangu isipokuwa (nimetegemea) kwa Mwenyezi Mungu, kwake yeye ndiko ninakotegemea na kwake ndiko nitakakorejea. Ewe Mola wangu nikunjulie kifua changu na uniwepesishie jambo langu na ufungue fundo ulimini kwangu wapate kufahamu maneno yangu. Namuomba Mwenyezi Mungu mtukufu anikubalie kazi yangu hii, na ajaalie kheri na baraka ndani yake, kwani kazi hii ni kama tofali moja tu kwa ajili ya ujenzi wa mshikamano na umoja. Nasema hivi kwa sababu leo hii Waislamu bado wako mbali mno na haki ndogo ya binadamu na kutendeana mema miongoni mwao. Nimeyashuhudia hayo mwenyewe wakati wa safari zangu nyingi za kutembelea nchi za Kiislamu au nchi ambazo wapo Waislamu, na safari ya mwisho ni ya hivi karibuni katika Bara Hindi ambalo wakazi wake ni zaidi ya Waislamu milioni mia mbili, robo yao ni Mashia na robo tatu yao ni Masunni. Kwa hakika nimeyasikia mengi kutoka kwao, lakini niliyoyashuhudia yanashangaza na yanatisha. Na kwa kweli

nilisikitika na nikalia juu ya hatima ya umma huu (sijuwi itakuwaje). Ilikuwa karibu moyo wangu ukate tamaa lau siyo matumaini na imani (yangu).

Haraka baada ya kurudi kwangu kutoka India, nilituma barua ya wazi kwa Mwanachuoni wa India ambaye ndiye marejeo ya **Ah-Lis-Sunnah Wal-Jama'a**, katika nchi hiyo: **Sayyid Abul-Hasan An-Nadawi**, na nilimuahidi kuichapisha pamoja na jawabu lake lakini sikupata jawabu mpaka sasa. Nami naichapisha (barua hiyo) katika utangulizi wa kitabu hiki ili iwe ni uthibitisho wa kihistoria utakaotushuhudia mbele ya Mwenyezi Mungu na mbele ya watu kwamba sisi ni miongoni mwa wanaolingania umoja. Doctor Muhammad At-Tijani As-Samawi

## KWA JINA LA MWENYE ENZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU

## KISHA SALA NA SALAMU ZIMSHUKIE MBORA WA MITUME NA AALI ZAKE WATUKUFU

### BARUA YA WAZI KWA MWANACHUONI WA INDIA, SAYYID ABUL-HASAN AN-NADAWI

Amani ya Mwenyezi Mungu ikushukieni na Rehema na Baraka zake zikushukieni. Amma Ba'ad: Mimi Muhammad At-Tijani As-Samawi, Mtunisia, ambaye Mwenyezi Mungu amenineemesha kwa uongofu na mafanikio, nayakubali Madh-hebu ya watu wa nyumba ya Mtume baada ya uchunguzi (uliochukua muda) mrefu na kabla ya hapo nilikwa (mfuasi wa Madh-hebu ya) Malik. Si hivyo tu, bali nilikuwa miongoni mwa wafuasi wa Tariqa mashuhuri ya Kisufi huko Afrika ya Kaskazini iitwayo "AT-TIJAN1YYAH". Hatimaye nikaufahamu ukweli wakati wa safari yangu iliyofana kwenda kwa Wanachuoni wa Kishia, na niliandika kuhusiana na safari hiyo kitabu nilichokiita, "THUMMAH-TADAITU", kilikamilika kuchapishwa huko kwenu India kwa lugha nyingi kutokana na ukarimu wa Majimau Al-ilmiyyi Al islamiyyi, na kwa ajili ya munasaba (huu) niliitwa kuitembelea India. Ewe Bwana wangu mpendwa, nilifika India kwa matembezi mafupi, na matarajio yangu yalikuwa ni kukutana nanyi kutokana na sifa zenu ninazozisikia na kutokana na kufahamu kwangu kwamba ninyi ndio mategemeo kwa AH-LIS-SUNNAT WAL-JAMA'A. Lakini nilishindwa kufanya hivyo kutokana na umbali na kukosa muda, na nikatosheka kwa kuzuru Bombay, Puna, Jabal Pur na miji mingine iliyoko Gujarat. Nilihuzunika sana kutokana na mambo niliyoyaona huko India (hasa) kutokana na uadui na bughudha iliyoko baina ya Ahli-Sunnah Wal-Jama'a, na ndugu zao Waislamu wa Kishia. Kwa hakika nilikuwa nikisikia kwamba wao hupigana na hupata wakati mwingine wakauana na kumwaga damu za watu wasio na kosa lolote kutoka pande mbili hizi eti kwa niaba ya (kutetea) Uislamu. Mimi nilikuwa siamini (haya) huku nikiitakidi kuwa habari hizo zimepewa mno sura isiyo yake, lakini niliyoyaona na kuyasikia wakati wa ziyara yangu kwa kweli yanashangaza na nimeyakinisha kwamba huko kuna makusudio mabaya na ushauri wa hatari unaoundwa dhidi ya Uislamu na Waislamu ili kuwamaliza wote Masunni na Mashia. Miongoni mwa mambo yaliyozidisha uwazi wa yakini yangu na kuimarisha ufahamu

wangu (juu ya hayo) ni ule mkabala uliopita baina yangu na kundi la wanachuoni wa Kisunni wakiongozwa na Sheikh Azizur -Rahman Mufti wa Al-Jamaatul-Islamiyyah, na mkutano wetu ulikuwa ndani ya Msikiti wao huko Bombay na wao ndiyo walioniita.

Baada tu ya kufika, dharau, tuhuma na matusi na kuwalaani Mashia (Wafuasi) wa kizazi cha nyumba ya Mtume vilianza, na walikuwa wamekusudia kunitisha na kuniudhi kwa kuwa walikuwa wanajua kwamba mimi nimeandika kitabu kinachotoa wito wa kushikamana na Madh-hebu ya Ahlul-Bait (a.s). Lakini mimi nilifahamu makusudio yao na nikaimiliki nafsi yangu na nilitabasamu hali ya kuwa nikisema: "Mimi ni mgeni kwenu ninyi, nanyi ndiyo mlioniita na nimekuja kwa haraka kuitika wito, basi je mumeniita ili mnitukane na kunishutumu, na Je, hii ndiyo tabia ambayo Uislamu umekufundisheni. Basi walinijibu kwa kujiamini kabisa kwamba, mimi hata siku moja sijapata kuwa Muislamu kwa sababu mimi ni Shia na Mashia hawana Uislamu wowote, na waliapa kuthibitisha jambo hilo. Mimi nilisema, "Mcheni Mwenyezi Mungu enyi ndugu zangu, Mola wetu ni mmoja na Mtume wetu ni mmoja na Kitabu chetu ni kimoja na Qibla chetu ni kimoja, na Mashia wanampwekesha Mwenyezi Mungu na wanautumikia Uislamu kwa kumfuata Mtume na Watu wa nyumba yake, wanasali Sala (Tano) wanatoa zaka na wanahiji kwenye nyumba tukufu ya Mwenyezi Mungu, basi vipi inajuzu kwenu ninyi kuwakufurisha wao? Walinijibu, "Ninyi Hamuamini Qur'ani, ninyi ni WANAFIKI mnatumia TAQIYYAH, na Imam wenu amesema: "Taqiyyah ni Dini yangu na ni Dini ya wazazi wangu" Nanyi ni kikundi cha Kiyahudi alichokianzisha Abdallah ibn Saba'a Myahudi."

Niliwaambia hali ya kuwa nikitabasamu, "Hebu tuwaache Mashia na zungumzeni nami binafsi, kwani mimi nilikuwa (wa Madhehebu ya) Malik kama ninyi, na baada ya uchunguzi wa muda mrefu niliyakinisha kwamba Watu wa nyumba ya Mtume ndiyo wenye haki na ndiyo bora kuwafuata. Basi Je, mnayo hoja ya kunijadili au kuniuliza ni ipi dalili yangu na hoja yangu ili pengine tuweze kuelewana miongoni mwetu?" Walisema: "Ahlul-Bait (Watu wa Nyumba ya Mtume) ni wakeze Mtume na wewe huna ukijuacho ndani ya Qur'ani." Nikasema: "Bila shaka Sahih Bukhar na Sahih Muslim zinafundisha kinyume cha mlivyotaja! Wakasema: "Yote yaliyomo ndani ya Bukhari na Muslim na vitabu vingine vya Kisunni miongoni mwa hoja mnazozitoa ni katika uzushi wa Mashia waliouweka vitabuni kwetu."

Niliwajibu hali ya kuwa nacheka; "Ikiwa Mashia wamefikia kiasi cha kuingiza uzushi ndani ya vitabu vyenu, basi vitabu hivyo havina maana tena na pia Madhehebu yenu ambayo yamesimama juu ya vitabu hivyo!!" Walinyamaza wakakosa hoja, lakini mmoja wao alikusudia kuleta fujo na chuki kwa mara nyingine akasema: "Ye yote asiyeamini Ukhalifa wa Makhalifa waongofu (ambao ni) Sayyidina Abu Bakri, Sayyidna Umar na Sayyidna Uthman, Sayyidna Ali, Sayyidina Muawiyyah na Sayyidna Yazid (r.a) basi huyo siyo Muislamu. Nilishangaa kwa maneno haya ambayo sijasikia mfano wake maishani mwangu nayo ni kumkufurisha asiyeamini Ukhalifa wa Muawiyyah na Yazid, na nilisema kimoyo moyo: "Ni jambo linaloingia akilini Waislamu kumuombea radhi Abubakar, Omar na Uthman jambo hili limezoeleka, ama kumuombea radhi Yazid kabisa sijasikia

(popote) isipokuwa India na niliwageukia nikawauliza: "Je mnakubaliana na huyu juu ya maoni yake? Wote kwa pamoja wakajibu "Ndiyo". Hapo ndipo nilipofahamu ya kuwa hakuna faida ya kuendeleza mazungumzo, na nikafahamu pia kwamba hakuna kingine isipokuwa wanataka kuniudhi (nikasirike) ili wapate kunishambuha na pengine waniuwe kwa madai ya kuwatukana Masahaba, nani ajuaye (nia zao)? Niliona machoni mwao (ishara ya) shari, nikamuomba rafiki yangu aliyenileta kwao anitoe haraka, akanitoa huku akisikitika na kunitaka radhi kwa yaliyotokea. Mtu huyu hakuwa na kosa alikuwa akifuatilia mkutano huo kwa kutaka kufahamu ukweli, ni kijana mwenye heshima (akiitwa) Sharafud-Din ambaye anamiliki Maktaba na Kiwanda cha uchapishaji cha Kiislamu mjini Bombay. Basi yeye ni shahidi wa yote yaliyopita baina yetu katika majadiliano yaliyotajwa, na hakuficha kutoridhika kwake na watu hawa ambao yeye alikuwa akiamini kwamba wao ni miongoni mwa Wanachuoni wakubwa.

Niliwaacha hali ya kuwa nimechukia na kusikitika juu ya hali ambayo imewafikia Waislamu na hasa wale wanaosimamia vituo vya uongozi na kujiita kuwa ni Wanachuoni, na nilisema moyoni kuwa, ikiwa hali ya Wanachuoni iko kwenye kiwango hiki cha ung'ang'anizi wa kipofu, basi hali itakuwaje kwa watu wa kawaida na wale wasiojua kitu? Hapo ndipo nilipofahamu ni vipi yamekuwa yakizuka mapambano na vita ambavyo ndani yake damu iliyoharamishwa humwagwa na kuvunja heshima na utukufu (wa watu) kwa jina la kuutetea Uislamu, na nililia juu ya hatima ya umma huu uliogawanyika na kuangamia, umma ambao Mwenyezi Mungu Mtukufu ameubebesha jukumu la uongofu na Mtume wa Mwenyezi Mungu vile vile ameubebesha jukumu la kuifikisha nuru kwenye nyoyo zenye kiza zinazohitaji kupata nuru inayong'ara na kwa wakati huo huo katika India peke yake kuna watu wapatao milioni mia saba wanaabudia asiyekuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na wanamtukuza Ng'ombe na Masanamu. Badala ya juhudi za Waislamu kuunganika ili wawaongowe na kuwaongoza na kuwatoa kwenye kiza watu hao na kuwapeleka kwenye nuru ili wasilimu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mola wa Walimwengu, tunawaona Waislamu leo hii hasa India wao ndiyo wenye haja ya uongofu na kujisahihisha.

Kwa sababu hii wewe Bwana wangu (Sayyid Abul-Hasan An-Nadawi) ninaleta kwenu barua yangu nikikulinganieni kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma Mwenye kurehemu na kwa jina la Mtume wake Mtukufu na kwa jina la Uislamu Mtukufu na kwa kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu (Aliposema) "Shikamaneni katika Dini ya Mwenyezi Mungu na wala msifarakane." (Qur'an 3:103).

Nakulinganieni msimame msimamo wa Muislamu shujaa ambaye haogopi kutekeleza la Mwenyezi Mungu na (haogopi) lawama ya mwenye kulaumu na wala ubinafsi haumchukui wala vikundi (havimchukui) kumpeleka namna apendavyo shetani na wafuasi wake. Nakulinganieni msimame msimamo safi ulio wazi, kwani ninyi ni miongoni mwa wale ambao Mwenyezi Mungu amewabebesha jukumu (la uongozi) muda wote mtakaokuwa mkizungumza kwa niyaba ya Uislamu katika nchi hiyo. Mwenyezi Mungu hatakuridhieni iwapo mtasimama msimamo wa

mtazamaji mwenye kuridhika na yale yanayotokea huku na huko miongoni mwa misiba inayosababisha kupoteza (maisha ya watu) wasio na makosa miongoni mwa Waislamu wa Kisunni na Kishia. Mwenyezi Mungu atakuulizeni siku ya Qiyama kwa kila dogo na kubwa, na atakuhesabuni kutokana na kila linalopita na linalokuja kwa kuwa Hawawi sawa wale wanaojua na wale wasiojua, kwani kwa kiwango cha bidii mtu afanyacho ndivyo yatavyokuwa mafanikio, na kwa kadiri ya kiwango cha utukufu ndivyo yajavyo mambo matukufu. Na maadam ninyi ndiyo mnaowaongoza wanachuoni wa India, basi jukumu lenu ni kubwa na bila shaka neno litokalo kwenu huenda ndani yake kukawa na mafanikio kwa umma (wa Kiislamu) nchini India kama ambavyo huenda kukawa na maangamivu ya mali na watu (likitumika vibaya), basi mcheni Mwenyezi Mungu enyi watu wenye akili! Na kwa kuwa Mwenyezi Mungu amewapa Wanachuoni daraja ya kwanza baada ya Malaika akasema:

شَهِدَ اللَّـهُ أَنَّهُ لَا إِلَـٰهَ إِلَّا هُوَ وَالْمَلَائِكَةُ وَأُولُو الْعِلْمِ قَائِمًا بِالْقِسْطِ ۚ لَا إِلَـٰهَ إِلَّا هُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١٨﴾

"Mwenyezi Mungu ameshuhudia ya kwamba, hapana aabudiwaye kwa haki ila yeye tu na Malaika na wenye elimu (wameshuhudia hivyo), (Yeye) ni Mwenye kusimamia uadilifu." (Qur'an, 3:18).

Na ikiwa Mwenyezi Mungu anatuamuru sote kwa kusema: "Na pimeni kipimo kwa haki na wala msipunguze kipimo". (Qur'an, 55:9).

Iwapo wafasiri wanaona umuhimu wa kufanya uadilifu katika vipimo vya kimaadda ambavyo vina viwango maalum, basi mwaonaje hali ya kufanya uadilifu katika mambo ya kiitikadi, ambayo yanamvutano baina ya haki na batili na kwa mambo hayo ya kiitikadi ndipo mahala unapotegemea uongofu wa watu na uokovu wa watu wote? Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema; "Na mtakapohukumu basi hukumuni kwa uadilifu". Na amesema tena; "Ewe Daud bila shaka sisi tumekufanya uwe Khalifa (msimamizi) katika nchi, basi hukumu baina ya watu kwa haki na wala usifuate matamanio yatakupotosha kutoka njia ya Mwenyezi Mungu." Hapana shaka Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: "Sema kweli japokuwa ni dhidi ya nafsi yako, sema kweli japokuwa ni chungu." Ewe Bwana wangu Mtukufu, nakuiteni kwenye Kitabu cha Mwenyezi Mungu, na sunna ya Mtume wake, semeni kweli wazi wazi kwa sauti kubwa japokuwa ni chungu itakushuhudieni mbele ya Mwenyezi Mungu. Naapa kwa Mola wako hivi kwenu ninyi Mashia siyo Waislamu? Hivi kweli mnaitakidi kwamba wao ni makafiri? Je wafuasi wa Watu wa nyumba ya Mtume ambao wanampwekesha Mwenyezi Mungu na kumtukuza zaidi kuliko vikundi vyote kwa usemi wao wa kuwa hafanani na chochote kwa kumtakasa kutokana na kufanana, na kutokana na kuwa hana umbo na mwili. Si hivyo tu bali wanamuamini Mtume wake Muhammad **(s.a.w.w)** na wanamuheshimu mno kuliko vikundi vyote wasemapo kuwa, "Yeye Mtume ni Maasum moja kwa moja hata kabla ya kupewa utume". Je, hawa ndiyo munaowahukumu kuwa ni makafiri? Je, wale wanaomtawalisha Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini na wanawapenda kizazi cha Mtume na kuwatawalisha kama alivyowatambulisha Ibn Mandhur ndani ya "Lisanul-A'rab" katika mada ya Shia, basi je ninyi mwasema kwamba wao

siyo Waislamu? Je, Mashia hawa ambao wanatekeleza wajibu wa Sala kwa namna iliyo bora, na wanatoa Zaka na kuzidisha juu yake Khumsi ya mali zao kwa ajili ya kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wanafunga (saumu ya) mwezi wa Ramadhani na nyingine na wanahiji nyumba Tukufu ya Mwenyezi Mungu na kuyatukuza mambo matukufu ya Mwenyezi Mungu, kadhalika wanawaheshimu Mawalii wa Mwenyezi Mungu na kujiepusha na maadui wa Uislamu, hivyo kwenu ninyi watu hawa ni washirikina?

Je, hivi watu wasemao kuwa Uimamu hasa ni (haki) wa Maimamu kumi na wawili kutoka katika watu wa nyumba ya Mtume ambao Mwenyezi Mungu amewaondolea uchafu na amewatakasa sana sana, na Mtume wa Mwenyezi Mungu aliwataja kama alivyotoa Bukhari na Muslim na wengineo katika Sahihi za Ahlu-Sunnah, hivi watu hawa kwenu ninyi ni watu waliotoka nje ya Uislamu? Je hivi kuna siku ambayo Waislamu wamekuwa hawautambui Uimamu na wala hawakubali sawa sawa liwe hilo katika uhai wa Mtume au baada ya kufa kwake mpaka kufikie kuihusisha nadharia ya Uimamu kwa Waajemi na Majusi? Na je hivi mnasema kwa kujiamini kuwa, "Ni Kafiri asiyekubali Uimamu wa Yazidi ibn Muawiyyah ambaye uovu wake unaeleweka kwa Waislamu wote? Na itoshe uovu na udhalimu wa Yazidi kwa maelezo walioafikiana Waislamu wote kutokana na yeye kuruhusu kufanyika maasi kwenye mji Mtakatifu wa Madina kwa kutumia jeshi lake na askari wake kufanya wayatakayo mjini humo ili wachukuwe viapo vya utii (kutoka kwa watu) kwa nguvu kama kwamba (watu hao) ni watumwa wake. Si hivyo tu, bali wa Yazid waliwaua maelfu ya Masahaba watukufu na Tabiina, wakavunja heshima za wanawake na wasichana wa Kiislamu waliojihifadhi kiasi walizaliwa kutokana na uchafu huo idadi ya watoto ambao hakuna awezaye kuidhibiti isipokuwa Mwenyezi Mungu.

Na yamtosha Yazidi aibu mbaya mno na udhalim wa kudumu kule kumuuwa Bwana wa vijana wa peponi na kuwateka Mabinti wa Mtume na kuyachokora meno ya Husein (a.s) kwa kijiti kisha kuimba kwake beti za ushauri ambazo ni maarufu akasema, "**Laiti wazee wangu (waliouawa) katika Badri wangeshuhudia...**" Mpaka akafikia kusema: "**Banu Hashim walichezea Ufalme, hakuna habari yeyote iliyokuja wala Ufunuo ulioshuka.**" Ni wazi kabisa kwamba hakuamini utume wa Muhammad **(s.a.w.w)** wala Qur'an Tukufu, basi je, ni kweli mnaafiki kumkufurisha anayejitenga na Yazid? Na baba yake Muawiyyah ambaye alikuwa akimlaani Ali (a.s) na huamuru alaaniwe, bali na (alikuwa) akimuuwa kila anayekataa kufanya hivyo miongoni mwa Masahaba wema kama alivyomfanyia Hujr ibn Adiyy Al-Kindi na jamaa zake, na (tendo la kumlaani Ali a.s) aliliusia likawa ni sunna iliyofuatwa kwa miaka sabini hali ya kuwa (Muawiyyah) anaijua kauli ya Mtume **(s.a.w.w)** aliposema "Yeyote atakayemtukana Ali, basi kanitukana mimi, na atakayenitukana mimi amemtukana Mwenyezi Mungu". Kama ambavyo zilivyoandika Sahih za Ahli-Sunnah kwa ziyada ya matendo aliyoyatenda miongoni mwa mambo yanayopingana na Uislamu kwa kuwauwa watu wema wasio na kosa ili achukue kwao kiapo cha utii kwa ajili ya mwanawe Yazid. Vilevile kumuua kwake, Hassani ibn Ali (a.s) kwa kumtumia Ju'da binti Ash-ath, na maovu

mengine mengi yanatajwa na historia kwa Masunni kama ambavyo pia yanashuhudiwa na wafuasi wa Imam Ali (a.s).

Mimi, ewe Bwana wangu, sikudhani kwamba ninyi mnaafikiana na hayo, vinginevyo basi na tuyaache kama yalivyo, na ikifika hapo basi hapatabakia baada ya hayo kipimo wala akili, wala sheria na wala hekima pia dalili. Na Mwenyezi Mungu anasema: "Enyi mlioamini mcheni Mwenyezi Mungu na kuweni pamoja na wakweli." (Qur'an, 9:119).

Namuapa Mwenyezi Mungu, bila shaka mwanachuoni wa Kipakistan Abul-A'ala Al-Maududi, Mwenyezi Mungu amrehemu amesema kweli alipotaja katika kitabu chake kiitwacho, "Ukhalifa na lifetime" katika ukurasa wa 106 akimnukuu Al-Hasan Al-Basri aliposema, "Mambo manne alikuwa nayo Muawiyyah, lau angekuwa na jambo moja miongoni mwa hayo lingetosha kumuangamiza.

1) Kuchukua ukhalifa bila ya mashauriano ya Waislamu na hali wamo miongoni mwao waliobakia Masahaba na wenye nuru ya ubora.

2) Kumpa Ukhalifa baada yake mwanawe mlevi ambaye alikuwa akivaa hariri na kupiga magitaa.

3) Kumfanya Ibn Ziyad kuwa ni mwana wa baba yake na hali Mtume **(s.a.w.w)** amesema: "**Mtoto ni wa kitanda na mzinifu mwanaume atapata jiwe.**"

4) Kumuua kwake Hujr na Jamaa za Hujr, basi ole wake kwa kumuua Hujr na jamaa zake Hujr (akakariri mara tatu).

Basi Mwenyezi Mungu amrehemu Abu A'ala Al-Maududi, aliyepasua ukweli, na lau angetaka angeongeza zaidi ya mambo haya manne yakawa mambo arobaini lakini aliona kwamba hayo yanatosheleza kumuangamiza Muawiyyah. Huenda Maududi alikuwa akichelea hisia za watu ambao wamejifunza kwa watangulizi wao kumtukuza Muawiyya, kumuheshimu na kumuombea radhi, bali hata mwanawe Yazid vile vile (kutukuzwa n.k.) kama nilivyosikia mimi mwenyewe binafsi toka kwa Wanachuoni wenu huko India. Lahaula wala Quwwata Illa Billahil-'Aliyyil-Adhim.

Kutokana na yote hayo mimi pia nilichelea hisia za wale watu walioniita wasije wakanivamia, basi sikuwatajia chochote katika matukio hayo. Kwa hiyo ewe bwana wangu, ninakulinganieni muwe na msimamo ulio wazi mkitafuta radhi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa msimamo huo, kwani Mwenyezi Mungu haichelei haki, na wala sikutakeni mkiri makosa ya watu hawa wala kuisambaza aibu yao kwa kuwa historia inatutosheleza sisi na ninyi kutuhadharisha juu ya hayo. Lakini kinachotakiwa kutoka kwenu ni kukiri na muwafahamishe wafuasi wenu kwamba, "Watu ambao hawaukubali Uimamu wa watu hawa (Muawiyya Yazid, Abubakr, Omar na Uthman) na wala hawawatawalishi, wao ni Waislamu wanaostahiki heshima na jambo hilo halina shaka, museme ya kwamba Mashia ni wenye kudhulumiwa siku zote kwani wao hawakuufuata na kuukubali Uimamu wa mti uliolaaniwa ambao Mwenyezi Mungu ameupigia mfano ndani ya Qur'ani. Basi ni lipi kosa la Mashia kwa Mola wenu, ikiwa Mtume **(s.a.w.w)** anawaamuru Waislamu kuwafuata Watu wa nyumba yake baada yake, mpaka akawafanya wao kuwa ni kama Safina ya Nuh, anaokoka mwenye kupanda ndani yake na anaangamia anayeikwepa. Na ni lipi kosa la Mashia ikiwa walitekeleza amri ya Mtume aliposema: "**Nimekuachieni vizito**

**viwili, Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Kizazi changu, vitu ambavyo mkishikamana navyo kamwe hamtapotea baada yangu.**" Kama ambavyo zinashuhudia Sihah za Sunni ukiachilia mbali vitabu vya Kishia. Badala ya kuwashukuru (Mashia) na kuwatanguliza na kuwaboresha juu ya wengine kwa kufuata kwao maamrisho ya Mtume **(s.a.w.w)**, tunawashutumu na kuwakufurisha na kujitenga nao, jambo hili siyo uadilifu wala haliingii akilini.

Ewe Bwana wangu, hebu tuachane na kauli za kijinga na za uongo ambazo haziwezi kusimamisha dalili wala hoja na hazina uzito kwa wanataaluma miongoni mwa watoto wa umma wetu kwamba, "Eti Mashia wanayo Qur'ani yao, au eti wao wanasema kwamba aliyepewa Utume ni Ali, au kwamba Abdallah ibn Sabaa' Myahudi ndiye muanzilishi wa Ushia."Na mengineyo miongoni mwa kauli dhaifu ambazo Mwenyezi Mungu anashuhudia kuwa hayo ni miongoni mwa uzushi wa maadui wa Uislamu na maadui wa Ahlul-Bait na wafuasi wao. Na hayo ni mambo hayakuzushwa isipokuwa ni kutokana na ubinafsi mpotovu na ujinga wenye kero iliyopita kipimo. Ewe Bwana wangu mpendwa mimi nauliza, "Wana daraja iliyoje wanachuoni wa India kuliko ile ya wanachuoni wa Az-Har Tukufu waliotoa Fat-wa inayoruhusu kufanya Ibada kwa mujibu wa Madhehebu ya Shia Imamiyyah tangu miaka thelathini iliyopita? Na miongoni mwa Wanachuoni wa Az-Har kuna aonaye kuwa fiqihi ya Mashia ya Jaa'fari ambayo wanaitumia Mashia ni pana yenye manufaa na iko karibu mno na Roho ya Uislamu kuliko Madhehebu nyinginezo ambazo zinaitegemea. Na anayewaongoza Wanachuoni hawa (kwa fikra hii) ni Mtukufu Marehemu Sheikh Mahmud Shal-Tut Mwenyezi Mungu amrehemu, ambaye aliiongoza Az-har katika uhai wake.

Je hivi wanachuoni kama hawa hawaujui Uislamu na Waislamu? Au wanachuoni wa India ni wajuzi mno kuliko wanachuoni hao? Mimi siwadhanieni kabisa kwamba ninyi mnasema namna hiyo...!! Ewe Bwana wangu Mtukufu, mategemeo yangu kwenu ni thabiti na moyo wangu kwenu uko wazi kwa mapenzi na huruma, na hapo zamani nilikuwa kama ninyi nimefunikwa sioni haki wala Ahlul-Bait (a.s) na wafuasi wao. Mwenyezi Mungu akaniongoza kuelekea kwenye haki ambayo hapana baada yake ila upotovu, na nikawa huru kutokana na minyororo ya ung'ang'anizi na kufuata kama kipofu, na nilifahamu kwamba wengi wa Waislamu bado wamefunikwa na habari zisizo na ukweli na za uzushi. Kampeni zilizoandaliwa kuwapa baadhi ya watu utukufu wasiostahili zinawazuwia (Waislamu) kuufikia ukweli ili wote wapate kupanda meli ya uokovu na washikamane na kamba imara ya Mwenyezi Mungu, na hakuna tofauti kama mjuavyo baina ya Sunni na Shia isipokuwa ni katika yale waliyotofautiana kwa ajili ya Ukhalifa baada ya Mtume, na msingi wa tofauti ni itikadi yao kuhusu Masahaba, nao Masahaba (r.a) walitofautiana kati yao mpaka wakalaaniana, kupigana na kuuana wao kwa wao. Ikiwa kutofautiana kati yao ni kutoka katika Uislamu basi Masahaba ndiyo wa mwanzo kutuhumiwa kwa tuhuma hii na Mwenyezi Mungu apishe mbali. Mimi siitakidi kwamba ninyi mnayaridhia hayo, na uadilifu unakulinganieni msiridhiye Mashia kutolewa nje ya Uislamu, kama ambavyo Mashia wana desturi ya kuwatukuza Ahlul-Bait (a.s) na kuwaheshimu vile vile Masunni

wanayo desturi ya kuwatukuza Masahaba wote, na misimamo hii miwili iko mbali mbali.

Basi ikiwa Mashia kwa desturi yao hiyo wanakosea, basi Masunni ndiyo watakaokuwa wanakosea zaidi (katika desturi yao) kwani Masahaba wote wanawatanguliza Ahlul-Bait (a.s) kuliko nafsi zao, na huwatakia rehma kama wamtakiavyo rehma Mtume **(s.a.w.w)**. Na hatumfahamu yeyote miongoni mwa Masahaba (r.a) aliyeitanguliza nafsi yake au aliyejitukuza juu ya watu wa nyumba ya Mtume **(s.a.w.w)** katika elimu au matendo mema. Basi wakati umefika kuliondosha giza la kihistoria kwa wafuasi wa Ahlul-Bait (a.s), kushirikiana nao, kuunga udugu, kusaidiana kwa mema na kumcha Mwenyezi Mungu na imetosha kwa umma huu kumwaga damu na kusambaza fitna. Huenda Mwenyezi Mungu Mtukufu akaunganisha kupitia kwenu kauli (ya umoja) na kuuondoa utengano, akalitibu jeraha hili na akauzima moto wa fitina na kumdhalilisha shetani na kundi lake na mtakuwa ninyi mbele ya Mwenyezi Mungu ni wenye kufaulu hasa kwa kuwa ninyi mnatokana na kizazi kitukufu kama ninavyosikia.

Basi fanyeni hayo ili mpate kufufuliwa pamoja nao. "Na hakika umma wenu ni mmoja nami ndiye Mola wenu." "Na waambie, fanyeni Mwenyezi Mungu ataona matendo yenu na Mtume wake na waumini". Mwenyezi Mungu akuwafikisheni ninyi na sisi kwa mambo ambayo ndani yake kuna kheri ya nchi na waja, Mwenyezi Mungu akujaalieni ninyi na sisi kuwa miongoni mwa wenye kutenda (mema) wenye utakaso kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Nakutumieni kwa heshima yenu pamoja na barua hii nakala ya kitabu changu "Thummah-Tadaitu" ambacho nilikitunga maalumu kuhusiana na maudhui haya, hiyo ni zawadi yangu kwenu huenda kikapata kukubalika mbele yenu. Was-salaam Alaikum Warahmatullahi Taala wa Barakatuh. Muhammad Tijani As-Samawi At-Tunisi.

1

# WAULIZE WANAOFAHAMU

(QUR. 16:43 NA 21:7) Bila shaka aya hii Tukufu inawaamuru Waislamu kuwarejea watu wenye kumbukumbu kwa kila linalowatatiza ili wapate kuufahamu muelekeo ulio sawa, kwani Mwenyezi Mungu amewaandaa (wenye kumbukumbu) kwa ajili hiyo baada ya kuwafunza, basi wao ndiyo waliobobea katika elimu na ndiyo wanaofahamu Ta'wili ya Qur'an. Kwa hakika aya hii ilishuka kuwatambulisha Ahlul-Bait (a.s) nao ni Mtume Muhammad, Ali, Fatma, Hasan na Husein, na hili lilitendeka katika zama za Mtume. Amma baada ya Mtume **(s.a.w.w)** mpaka kitakaposimama Qiyama (wenye kumbukumbu) ni hawa hawa watano waliotajwa ambao ndiyo Ahlul-Kisaa na huongezwa kwa hao, Maimamu tisa kutoka katika kizazi cha Hussein (a.s) ambao Mtume wa Mwenyezi Mungu amewabainisha katika Minasaba mbali mbali na akawaita kuwa ni Maimamu wa uongofu na ni taa ziondoazo kiza na wao ndiyo wenye kumbukumbu, na ndiyo waliobobea katika elimu, Mwenyezi Mungu amewarithisha elimu ya kitabu. Riwaya hizi zimethibiti na ni sahihi tena mutawatir kwa Mashia tangu zama za Mtume **(s.a.w.w)**, na wamezieleza baadhi ya wanachuoni wa Kisunni, na wafasiri wao wamekiri kwamba kushuka kwa aya hii kunawahusu Ahlul-Bait (a.s). Ninawataja miongoni mwa wanachuoni hawa kwa kutolea mfano:

1) Im1)Imam Thaa'labi katika Tafsiri yake (alipozunhumzia) maana ya aya hii katika Surat An-NahliNahl.

2) Tafsirul-Qur'an ya ibn Kathir Juzuu ya pili ukurasa 570570.

3) Tafsirut-Tabari, Juzuu ya kurni na nne ukurasa 109.

4) Tasirul-Alusi iitwoyo Ruhul-Maani Juzuu ya kumi na nne ukurasa wa 134.

5) Tafsirul-Qurtubi Juzuu ya kumi na moja ukurasa 272.

6) Tafsirul-Hakim iitwayo Shawa-Hidut-Tanzil, Juzuu ya kwanza ukurasa 334.

7) Tafsir At-Tustari, itwayo Ih-QaaQul-Haq, Juzuu ya tatu ukurasa 482.

8) Yanahi'ul-Mawaddah cha Al-Qanduzi Al-Hanafi ukurasa wa 51 na 140.

Na ilivyokuwa wenye kumbukumbu kwa dhahiri ya aya ni Ahlul-Kitab miongoni mwa Mayahudi na Wakristo, basi imetulazimu juu yetii kubainisha wazi kwamba wao sio waliokusudiwa katika aya hiyo Tukufu.

**Kwanza**; Kwa sababu Qur'an Tukufu imewataja (Mayahudi na Wakristo) mara nyingi katika aya nyingi kwamba wao waliyageuza maneno ya Mwenyezi Mungu na wakakiandika kitabu kwa mikono yao, na wakasema kuwa kimetoka kwa Mwenyezi Mungu ili wakiuze kwa thamani ndogo. na (Qur'an) imeshuhudia uongo wao na kuigeuza kwao haki, basi haiwezekani wakati huo huo iwaamrishe Waislamu warejee kwao (Mayahudi na Wakristo) katika Mas-ala wasiyoyajua.

**Pili**: Bukhari ameeleza katika Sahih yake ndani ya Kitabus-Shahadah mlango usemao, "Hawaulizwi washirikina". Juzuu ya tatu uk. 163. Kutoka kwa Abuhurairah: Amesema Mtume **(s.a.w.w)**: "Msiwaamini Ah-lil-Kitab na wala msiwapinge (kuwaambia kuwa ni waongo) semeni tumemuamini

Mwenyezi Mungu na yaliyoteremshwa (toka kwake)[1]. Hii inafundisha kutowarejea (Ahlul-kitab) katika mas-ala na (lililopo) ni kuwaacha na kuwapuuza, kwa sababu kutowaamini na kisha kutokuwapinga kunakanusha lengo la kuwauliza ambalo linasubiri jawabu sahihi. Tatu: Bukhari ameeleza ndani ya Sahih yake katika Kitabut-Tauhidi mlango wa kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo: "Kila siku yeye yumo katika mambo." Juzuu ya nane ukurasa 208 kama ifuatavyo: Kutoka kwa Ibn Abbas amesema: "Enyi kongamano la Waislamu, vipi mnawauliza Ah-Lul-Kitab na hali kitabu chenu alichokiteremsha Mwenyezi Mungu kwa Mtume wenu **(s.a.w.w)** ndicho chenye maelezo halisi ya Mwenyezi Mungu na hakikuharibiwa, Mwenyezi Mungu amekusimulieni kwamba Ah-Lul-Kitab wamekwisha badilisha na kugeuza (yaliyoteremshwa) katika vitabu vya Mwenyezi Mungu (vilivyotangulia) wakaandika kwa mikono yao kisha wakasema hayo ni kutoka kwa Mwenyezi Mungu ili wayauze kwa thamani ndogo, je hajakukatazeni yale yaliyokufikieni katika elimu kuwauliza hao? Basi fahamuni, namuapa Mwenyezi Mungu; hatujamuona mtu miongoni mwao akikuulizeni kuhusu yaliyoteremshwa kwenu." Nne: Lau leo hii tutawauliza Ah-Lul-Kitab miongoni mwa Wakristo bila shaka watadai kuwa Isa ni Mungu na Mayahudi wanawapinga (Wakristo kwa madai hayo) na wala hawamkubali (Isa) japo kwa Utume, na kila mmoja wao anaupinga Uislamu na Mtume wa Uislamu, na wanasema kuwa (yeye Mtume) ni muongo na ni mzushi.

Kwa yote hayo basi haiwezekani ifahamike maana iliyomo katika aya kwamba Mwenyezi Mungu ametuamrisha tuwaulize wao, na ilipokuwa Ah-Lud-Dhikr katika dhahiri ya aya ni wao Ah-Lul-Kitab miongoni mwa Wayahudi na Wakristo, basi hapana shaka hali hii haikanushi kwamba aya hii imeshuka kwa watu wa Nyumba ya Mtume kama ambavyo imethibiti kwa 33 Mashia na Masunni kwa njia sahihi. Kwa hiyo inafahamika kutoka katika aya hiyo kwamba, Mwenyezi Mungu ameirithisha elimu ya Kitabu ambacho ndani yake hakuacha kitu kwa hawa Maimamu ambao amewateua kutoka miongoni mwa waja wake ili watu wawarejee katika Tafsiri na Ta'awiili, na kwa kufanya hivyo uongofu wao utathaminiwa iwapo watamtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Kwa kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na hekima yake imetukuka alitaka watu wote wawanyenyekee wateule wanaotoka miongoni mwao, ambao aliwachagua na akawafunza elimu ya Kitabu ili hali za watu ziwe katika nidhamu. Basi lau watu hawa hawangekuwepo miongoni mwa watu, nafasi ingekuwa wazi mbele ya wenye kujigamba (kuwa wanafahamu), na wajinga na hata kila mmoja angefanya kulingana na matamanio yake na mambo ya watu yangevurugika maadam kila mmoja aweza kudai kuwa ni mjuzi zaidi kuliko mwingine. Ili nitoe hoja baada ya mimi kukinaika kwamba Ah-Lul-Bait ndiyo "Ah-Lud-Dhikri" nitauliza maswali ambayo hayana jawabu kwa Ahlis-Sunnah Wal-Jamaa, au yanayo majibu lakini mwenye kujikalifisha kujibu majibu yake hayana hoja iwezayo kukubaliwa na mtu mtafiti mwenye kutaka uthibitisho imara. Ama jawabu lake la kweli, lipo kwa hawa Maimamu watakatifu

1. Sahihi Al-Bukhari, Juz.3, Uk.163.

ambao wameijaza dunia elimu na maarifa na pia wameijaza matendo mema na mafanikio.

## MLANGO WA KWANZA: YALE YANAYOMUHUSU MUUMBA MTUKUFU

Swali la Kwanza: Kumuona Mwenyezi Mungu na Kumfanyia Mwili Mwenyezi Mungu katika kitabu chake kitukufu anasema:"Macho hayamfikii (kumuona)". (Qur 'an, 6:103).

(Hakuna chochote chenye mfano wake) (Qur'an 42:11). Na anasema Mwenyezi Mungu kumwambia Musa alipotaka kumuona: "Kamwe hutaniona" (Qur'an 7:143.) Basi ni vipi (enyi Masunni) mnazikubali hadithi zilizopokewa ndani ya Sahih Bukhari na Sahih Muslim kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu anajidhihirisha kwa viumbe wake nao watamuona kama wauonavyo Mwezi mpevu? Na kwamba Mwenyezi Mungu anashuka mpaka kwenye mbingu ya dunia kila usiku na ataweka unyayo wake motoni nao utajaa na kwamba ataonesha mguu wake ili waumini wamtambue na kwamba anacheka na kushangaa, na mengineyo miongoni mwa riwaya ambazo zinamfanya Mwenyezi Mungu kuwa ni mwili wenye harakati na mabadiliko, ukiwa na mikono miwili, miguu miwili na ana vidole vitano, ameziweka mbingu kwenye kidole cha kwanza, ardhi kwenye kidole cha pili, mti kwenye kidole cha tatu, cha nne maji na udongo na kwenye kidole cha tano ameweka viumbe vingine vilivyobakia na anayo nyumba anayoishi ndani yake na Muhammad ataomba ruhusa kuingia humo mara tatu. Ametukuka Mwenyezi Mungu kwa Utukufu mkubwa kutokana na hayo (hayuko hivyo) utakasifu ni wa Mola wako Mola aliyetukuka kutokana na sifa wanazomzifu. Jawabu la swala hili liko kwa Maimamu waongofu na Taa ziondoshazo kiza nalo ni kumtakasa kikamilifu Mwenyezi Mungu Mtukufu kutokufanana na umbile na sura na mwili na kumshabihisha na kumuwekea mpaka.

Imam Ali (a.s) anasema: "**Sifa njema anastahiki Mwenyezi Mungu ambaye wasemaji hawafikii upeo wa sifa zake, wala wenye kuhesabu hawawezi kudhibiti neema zake, wala hawawezi kutekeleza vilivyo haki yake wenye kujitahidi, wala haziwezi kumfikia fikra zozote, na haziwezi kumtambua vilivyo akili mahiri, Mwenyezi Mungu ambaye sifa zake hazina mpaka, wala hasifiki kwa sifa za vilivyopo, na hana wakati unaohesabika wala muda wenye kikomo... Basi mwenye kumsifu Mwenyezi Mungu Mtukufu atakuwa kamfanyia mwenzi na Mwenye kumfanyia mwenzi, kamfanyia wa pili, na Mwenye kumfanyia wa pili kamgawa mafungu, na amgawaye mafungu basi hamjui Mwenyezi Mungu. Asiyemjua hakika kamuashiria na mwenye kumuashiria kamjaalia mipaka, na mwenye kumjaalia mipaka amemuhesabu, na atakaesema yumo ndani ya kitu fulani, basi kamuambatanisha, na atakayesema yuko juu ya nini kamtoa. Yupo siyo kwa kuzuka, yupo siyo kutokana na kutokuwepo, yu pamoja na kila kitu si kwa wenza naye si kila kitu siyo kwa kumfanya si kitu, mtendaji siyo kwa harakati na vifaa, anaona wakati hakuna kinachomuona miongoni mwa viumbe wake**". Kwa hakika nimeyaelekeza macho ya wachunguzi miongoni mwa vijana wenye taaluma kwenye hazina alizoziacha Imam Ali (a.s), zilizokusanywa ndani ya Nah-Jul-Balaghah ambacho ni kitabu madhubuti

hakitanguliwi ila na Qur'an, na ni kitabu ambacho kwa bahati mbaya hakifahamiki kwa watu wengi kutokana na kampeni, vitisho na vizuizi vilivyowekwa na watawala wa Banu Umayyah na Banu Abbas dhidi ya kila kile ambacho kina uhusiano na Ali ibn Abitalib. Sitakuwa nimezidisha nitakaposema kwamba ndani ya Nahjul-Balaghah kuna elimu nyingi na mafunzo mengi ambayo watu (wataendelea) kuyahitaji siku zote, na ndani ya Nahjul-Balaghah kuna elimu ya akhlaq, elimu ya jamii, uchumi na miongozo madhubuti katika elimu za dunia na teknolojia na zaidi ya hapo kuna falsafa, tabia, siasa na hekima.

Kwa hakika nimeyathibitisha hayo mimi mwenye we ndani ya Insha niliyotoa kwenye Chuo Kikuu cha Sirbun, Insha ambayo ilijadiliwa juu ya maudhui nne nilizozichagua kutoka ndani ya Nahjul-Balaghah na kutokana na maudhui hizo nilipata shahada ya "Udaktari". Basi lau Waislamu wangeifuata Nahjul-Balaghah kikamilifu wakayachambua mas-ala yote yaliyomo na kila nadharia, bila shaka (Nahjul-Balaghah) ni bahari yenye kina kirefu, kwani kila aizamiapo mtafiti hutoa ndani yake Lulu na Marjan.

**Ufafanuzi**: Iko tofauti iliyo wazi kati ya Aqida mbili: Aqida ya Ahlus-Sunnah Wal-Jamaa ambayo inamfanya Mwenyezi Mungu Mtukufu kuwa na mwili, umbo na sura kama kwamba yeye ni mtu anayetembea na anashuka (kutoka juu) na mwili wake unahifadhiwa na anayo nyumba (anamoishi) na mengineyo miongoni mwa mambo yanayochukiza. Mwenyezi Mungu ametakasika mno, yu mbali na mambo hayo. Aqida ya Mashia ambao wanamtakasa Mwenyezi Mungu na kutomfananisha na kumfanyia mwili, na wanasema kuwa haiwezekani kabisa kumuona (Mwenyezi Mungu) hapa duniani wala akhera. Nami binafsi naamini kwamba riwaya wanazotolea hoja Ahlus-Sunnah Wal-Jamaa zote ni uchafuzi wa Myahudi katika zama za Masahaba, kwani Kaabul-Ahbar Myahudi ambaye alisilimu katika zama za Omar bin Al-Khatab ndiye aliyeingiza itikadi hizi ambazo Wayahudi wanaziamini (na alifanikiwa kwa) kupitia njia za baadhi ya Masahaba wepesi (wa kuhadaika) kama vile Abu-Hurairah na Wahab ibn Munabbah. Basi ziko riwaya nyingi za aina hiyo zilizopokelewa ndani ya Bukhari na Muslim kutoka kwa Abu-Hurairah, na imekwishatangulia katika uchunguzi uliopita namna gani Abu-Hurairah asivyotenganisha hadithi za Mtume na hadithi za Myahudi Kaabul-Ahbar kiasi kwamba Umar bin Khatab alimpiga na kumzuwia asisiimulie riwaya kuhusu suala la Mwenyezi Mungu kuumba mbingu na ardhi katika siku saba. Na madam Ahlis-Sunnah Wal-Jamaa wanaziamini Sahih Bukhari na Muslim na kuvifanya kuwa ni vitabu sahihi mno, na maadam hawa wanamtegemea Abu-Hurairah kiasi kwamba amekuwa ndiyo tegemeo la wanachuoni wa hadithi (wa Kisunni) na yeye (Abu-Hurairah) kwa Masunni ndiyo mpokezi wa Uislamu (katika hadithi). Basi kwa hali kama hii haiwezekani kwa Masunni kubadili itikadi yao isipokuwa kama watajikomboa kutokana na kufuata kiupofu, na wakarejea kwa Maimamu waongofu (ambao) ni kizazi cha Mtume nao ndio mlango wa mji wa Elimu ambao huendewa. Wito huu hauwahusu Wazee na Masheikh, bali kijana mwenye taaluma miongoni mwa Masunni, pia ni miongoni mwa wajibu alionao (kijana) ni kujinasua kutokana na kufuata kiupofu na afuate hoja na dalili.

**Swali la Pili**: Uadilifu wa Mwenyezi Mungu na kutenza nguvu Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema ndani ya Kitabu chake kitukufu:

﴿وَقُلِ الْحَقُّ مِن رَّبِّكُمْ فَمَن شَاءَ فَلْيُؤْمِن وَمَن شَاءَ فَلْيَكْفُرْ﴿٢٩﴾

"Na waambie, huu ni ukweli utokao kwa Mola wenu, basi anayetaka naamini na anayetaka naakufuru" (Qur'an, 18:29).

﴿لَا إِكْرَاهَ فِي الدِّينِ قَد تَّبَيَّنَ الرُّشْدُ مِنَ الْغَيِّ﴿٢٥٦﴾

"Hakuna kulazimishwa katika dini, uongofu umekwisha bainika kutokana na upotofu" (Qur'an 2:256).

﴿فَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا يَرَهُ ﴿٧﴾ وَمَن يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُ ﴿٨﴾

"Na anayefanya wema (hata) kwa kiasi cha chembe ndogo ataona malipo yake, na anayefanya uovu (hata) kwa kiasi cha chembe ndogo ataona malipo yake" (Qur'an 99:7-8).

﴿لَّسْتَ عَلَيْهِم بِمُصَيْطِرٍ ﴿٢٢﴾

"Bila shaka wewe ni mkumbushaji tu, wewe siyo mwenye kuwatenza Nguvu" (Qur'an 88:22).

Basi vipi mnakubali hadithi zilizopokelewa katika Sahih Bukhari na Sahih Muslim kwamba eti Mwenyezi Mungu amewakadiria waja wake matendo yao kabla hajawaumba? Bukhari ameeleza katika Sahih yake amesema: "Walijadiliana Adam na Musa (a.s), Musa akamwambia Adam, Ewe Adam wewe ni baba yetu umetuingiza makosani na umetutoa peponi. Adam akamwambia Musa, Ewe Musa Mwenyezi Mungu amekuteua na akakuandikia (mambo yako) kwa mkono wake, Je, wanilaumu kwa jambo alilonikadiria Mwenyezi Mungu kabla hajaniumba kwa miaka arobaini? Basi Adam akamhoji Musa mara tatu."

Kama ambavyo Muslim amepokea katika Sahihi yake amesema: "Hakika mmoja wenu hukusanywa umbile lake tumboni mwa mama yake kwa siku arobaini kisha katika muda huo anakuwa pande la damu, katika muda kama huo (tena) anakuwa pande la nyama, na katika muda kama huo hutumwa Malaika kupulizia ndani yake roho na huamrishwa mambo manne: Kuandika rizqi yake, muda wake, kazi yake na kuwa ni mwema au muovu, basi naapa kwa ambaye hapana Mola asiyekuwa yeye, hakika mmoja wenu atatenda matendo ya watu wa peponi mpaka pasiwe baina yake na pepo ila dhiraa moja, basi yatamtangulia maandiko (aliyoandikiwa) atatenda tendo la watu wa motoni aingie motoni, na kwamba mmoja wenu atatenda matendo ya watu wa motoni mpaka pasiwe baina yake na moto ila dhiraa moja, basi yatamtangulia maandiko (aliyoandikiwa) atatenda tendo la watu wa peponi aingie peponi.

Ni kama alivyopokea Muslim katika Sahih yake kutoka kwa Bibi Aisha mama wa waumini amesema, "Mtume wa Mwenyezi Mungu aliitwa kwenye jeneza la mtoto mdogo miongoni mwa Ansar, nikasema, Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu amefaulu huyu ni ndege miongoni mwa ndege wa peponi hakufanya uovu na wala hakuufikia, Mtume akasema, au kinyume cha hivyo ewe Aisha, hakika Mwenyezi Mungu aliumbia pepo watu wake na akawaumba watu kwa ajili ya pepo hali wakiwa migongoni mwa baba zao, na ameuumbia moto watu wake na akawaumba watu kwa ajili ya moto hali wakiwa migongoni kwa baba zao." Bukhari amepokea

katika Sahih yake kwamba, mtu mmoja alisema "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu Je, wanafahamika watu wa Peponi kutokana na watu wa Motoni? Mtume akasema ndiyo, (yule mtu) akasema, basi ni kwa nini wanafanya amali? Akasema, kila mmoja anatenda kwa lile aliloumbiwa au kwa lile analorahisishiwa."

Umetakasika Mola wetu, na sifa njema ni zako, utukufu ni wako na umeepukana mno na dhulma hii, basi vipi tuzisadiki hadithi hizi zinazopingana na kitabu chako kitukufu ambacho ndani yake umesema na kauli yako ni ya kweli.?

﴿إِنَّ اللَّـهَ لَا يَظْلِمُ النَّاسَ شَيْئًا وَلَـٰكِنَّ النَّاسَ أَنفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿٤٤﴾﴾

"Bila shaka Mwenyezi Mungu hawadhulumu watu chochote lakini watu wanajidhulumu nafsi zao" (Qur'an 10:44).

﴿إِنَّ اللَّـهَ لَا يَظْلِمُ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ ﴿٤٠﴾﴾

"Hakika Mwenyezi Mungu hadhulumu (malipo japo) yenye uzito wa chembe ndogo (Qur'an 4:40).

"Na Mola wako hamdhulumu yeyote" (Qur'an 18:49).

﴿وَمَا ظَلَمَهُمُ اللَّـهُ وَلَـٰكِنْ أَنفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿١١٧﴾﴾

"Mwenyezi Mungu hakuwadhulumu wao lakini (wao) wazidhulumu nafsi zao" (Qur'an, 3:117).

﴿فَمَا كَانَ اللَّـهُ لِيَظْلِمَهُمْ وَلَـٰكِن كَانُوا أَنفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿٧٠﴾﴾

"Basi Mwenyezi Mungu hakuwa ni mwenye kuwadhulumu lakini wao wamekuwa ni wenye kuzidhulumu nafsi zao" (Qur'an 9:70, 29:40, 30:9).

﴿وَمَا ظَلَمْنَاهُمْ وَلَـٰكِن كَانُوا هُمُ الظَّالِمِينَ ﴿٧٦﴾﴾

"Hatukuwadhulumu lakini wao walikuwa wakizidhulumu nafsi zao" (Qur'an, 43:76).

﴿ذَٰلِكَ بِمَا قَدَّمَتْ أَيْدِيكُمْ وَأَنَّ اللَّـهَ لَيْسَ بِظَلَّامٍ لِّلْعَبِيدِ ﴿٥١﴾﴾

"Hayo (ni malipo) kwa yale yaliyotangulizwa na mikono yake na kwamba Mwenyezi Mungu hakuwa ni Mwenye kuwadhulumu waja." (Qur'an, 8:51).

﴿مَّنْ عَمِلَ صَالِحًا فَلِنَفْسِهِ وَمَنْ أَسَاءَ فَعَلَيْهَا وَمَا رَبُّكَ بِظَلَّامٍ لِّلْعَبِيدِ ﴿٤٦﴾﴾

"Yeyote mwenye kufanya wema basi ni kwa ajili ya nafsi yake, na yeyote (atayefanya) uovu basi ni juu yake na Mola wako si mwenye kuwadhulumu waja" (Qur'an, 41:46).

Na kama alivyosema ndani ya hadithi takatifu, "Enyi waja wangu. mimi nimeiharamisha dhulma juu ya nafsi yangu mwenyewe na nikaifanya kuwa ni haramu kati yenu basi musidhulumiane". Itakuwaje basi Muislamu aliyemuamini Mwenyezi Mungu na uadilifu wake na huruma yake asadiki kwamba Mwenyezi Mungu amewaumba viumbe na akawaamulia baadhi yao (wapate) Pepo na wengine Moto kwa kutaka kwake yeye Mwenyezi Mungu, na akawakadiria matendo yao ikawa kila mmoja amefanyiwa wepesi (kutenda) lile aliloumbiwa kama zilivyo riwaya hizi zinazopinga Qur'an Tukufu na asili ya maumbile ambayo Mwenyezi Mungu amewaumbia watu, na (zinapingana na) akili na ukweli na nafasi ya haki za mwanaadamu! Vipi tutaiamini Dini hii ambayo inaviza akili na kwamba

mtu huyu ni kinyago anayeendeshwa na mikono yenye uwezo namna inavyotaka, ili hatimaye imtupe ndani ya tanuru (la moto) - itikadi hii ndiyo ile ambayo inazuia akili ya mtu kuvumbua, kufanya maendeleo na kushindana, mambo ambayo huleta maajabu. (Itikadi hii inamviza) mtu abakie amedumaa mwenye kuridhika katika hali aliyomo na alichonacho kwa madai kwamba anawepesishiwa kwa yale aliyoumbiwa.

Vipi tutayakubali mapokezi haya ambayo yanagongana na akili iliyosalimika na yanatupatia picha kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu ni muvimba mwenye kugandamiza na amewaumba waja wake madhaifu kisha awatupe motoni si kwa lolote isipokuwa kwa kuwa yeye anafanya akitakacho! Basi je wenye akili watamuita Mungu huyu kuwa ni mwenye hekima au mwenye huruma au muadilifu? Itakuwaje kama tutazungumza na watu wataalamu na wenye elimu miongoni mwa wasio Waislamu, kisha wakafahamu kwamba Mola wetu anasifa hizi, na kwamba dini yetu imewahukumu watu kabla ya kuzaliwa kwao kuwa ni waovu, basi Je, wataukubali Uislamu na wataingia katika dini ya Mwenyezi Mungu kwa wingi? Ewe Mola umetakasika, bila shaka hizi ni kauli za uongo zilizopandikizwa na Banu Umayyah na wakazisambaza kwa haja zao, na mchunguzi yeyote anafahamu siri ya hayo, kwani ni uzushi mtupu unaopingana na maneno yako, na haiwezekani kwa Mtume wako kukuzulia mambo yanayopingana na ufunuo wako ambao ulimfungulia, hasa kwa kuwa imethibiti kwamba Mtume **(s.a.w.w)** amesema:

"**Itakapokufikieni hadithi itokayo kwangu, ilinganisheni na kitabu cha Mwenyezi Mungu, ikilingana na kitabu hicho ichukuweni na ikienda kinyume na kitabu cha Mwenyezi Mungu ipigeni ukutani (itupeni haifai)**".

Hadithi zote hizi na nyingine nyingi mfano wa hizi zinapinga Qur'an na zinapingana na akili, basi na zitupwe wala zisishughulikiwe japokuwa zimepokewa na Bukhari na Muslim kwani wawili hawa hawakuwa wamehifadhika kutokana na makosa. Inatutosheleza dalili moja tu kuyapinga madai haya maovu, nayo ni kutumwa kwa Manabii na Mitume kutoka kwa Mwenyezi Mungu kuja kwa viumbe wake, na kwa muda wote wa historia, ya wanaadamu (Mitume walikuja) kurekebisha maovu ya waja (wa Mwenyezi Mungu) na kuwabainishia njia iliyonyooka na wawafundishe kitabu, hekima na wawabashirie pepo wakiwa wema na wawaonye kuwa, kuna adhabu ya Mwenyezi Mungu motoni kama watakuwa waovu.

Miongoni mwa uadilifu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu na huruma yake kwa viumbe wake ni kwamba, hatawaadhibu isipokuwa wale aliowapelekea Mtume na akawasimamishia hoja, anasema Mwenyezi Mungu:

مَّنِ اهْتَدَىٰ فَإِنَّمَا يَهْتَدِي لِنَفْسِهِ ۖ وَمَن ضَلَّ فَإِنَّمَا يَضِلُّ عَلَيْهَا ۚ وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَىٰ ۗ وَمَا كُنَّا مُعَذِّبِينَ حَتَّىٰ نَبْعَثَ رَسُولًا ﴿١٥﴾

"Yeyote anayeongoka, bila shaka anaongoka kwa manufaa ya nafsi yake, na anayepotea bila shaka anapotea kwa hasara ya nafsi yake, wala hatabeba mbebaji mzigo wa mwingine, basi hatukuwa wenye kuwaadhibu (viumbe) mpaka tupeleke Mtume" (Qur'an, 17:15).

Basi kama riwaya hizi ambazo wameziandika kina Bukhari na Muslim zinazosema kwamba Mwenyezi Mungu amewaandikia waja wake matendo

yao kabla hajawaumba na akawaamulia baadhi yao pepo na wengine moto kama tulivyoeleza hapo kabla, na kama ambavyo Ahlis-Sunnah Wal-Jamaa wanavyoamini, mimi nasema, kama riwaya hizo ni sahihi, basi bila shaka kutumwa kwa Mitume na kuteremshwa kwa Vitabu kunakuwa ni aina ya upuuzi!! Na Mwenyezi Mungu ameepukana mno kufanya mambo ya upuuzi, na hawa waaminio hivi hawakumtukuza Mwenyezi Mungu (anavyostahiki kutukuzwa). Kwa hiyo haifai kabisa kwetu sisi kusema maneno kama haya. Ewe Mola wetu umetakasika na huu (usemwao juu yako) ni uzushi mkubwa.

تِلْكَ آيَاتُ اللَّـهِ نَتْلُوهَا عَلَيْكَ بِالْحَقِّ ۗ وَمَا اللَّـهُ يُرِيدُ ظُلْمًا لِّلْعَالَمِينَ ﴿١٠٨﴾

"Hizo ni aya za Mwenyezi Mungu tunakusomea kwa haki, na Mwenyezi Mungu hataki kuwadhulumu walimwengu." (Qur'an, 3:108).

Amma jawabu la utata huu unaohusu kumtakasa Mwenyezi Mungu Mtukufu kutokana na dhulma na upuuzi, linapatikana kutoka kwa Maimamu waongofu ambao ni taa ziondoazo kiza, na wao ndiyo mwangaza wa Ummah.

Hebu basi na tumsikilize mlango wa mji wa elimu Amiri wa waumini Ali ibn Abi Talib (a.s), anawafafanulia watu itikadi hii ambayo imeendelea kutokutambulika kwa baadhi ya Waislamu ambao wameuacha mlango huo yeye anasema alipoulizwa na mmoja wa wafuasi wake, "Je, kwenda kwetu Shamu kulikuwa kunatokana na Qadhaa (maamuzi) ya Mwenyezi Mungu na Qadar yake?" Anajibu Imam Ali (a.s):

"**Ole wako, huenda wewe umedhania kuwa Qadhaa ya kulazimisha na Qadar yenye kuwajibishwa, na lau ingekuwa hivyo thawabu na adhabu vingebatilika, ahadi na maonyo vingetenguka, hakika Mwenyezi Mungu amewaamuru waja wake kwa kuwahiyarisha na akawakataza kwa kuwatahadharisha. Akawalazimisha (kufanya mambo) mepesi na wala hakuwalazimisha (mambo) mazito. Akatoa (malipo) mengi kwa (matendo) kidogo na wala hawakumuasi hali ya kuwa ni mwenye kushindwa na hawakumtii hali ya kuwa ni mwenye kulazimisha. Wala hakuwatuma Mitume kwa ajili ya mchezo tu na hakuteremsha vitabu kwa waja ili iwe ni upuuzi, wala hakuumba mbingu na ardhi na vilivyomo bure bure tu. "Hizo ni fikra za wale waliokufuru basi ole wao waliokufuru kutokana na adhabu ya moto.** " Amesema kweli Imam (a.s) basi, ole wao kutokana na adhabu kali ya Mwenyezi Mungu wale wanaomnasibishia Mwenyezi Mungu kufanya upuuzi na dhulma.

Ni vizuri kusema na haki husemwa, ya kwamba Ahlus-Sunna Wal-Jamaa wanamtakasa Mwenyezi Mungu kwa kumuepusha na upuuzi na dhulma, basi iwapo utamuuliza mmoja wao huenda kamwe asimnasibishe Mwenyezi Mungu na dhulma kwa utukufu wake, lakini huenda yeye mwenyewe akajikuta anaona vibaya kuzikataa hadithi zilizotolewa na Bukhari na Muslim na wakati huo huo akaziamini kwamba ni sahihi, kwa ajili hiyo utamuona wakati unamjadili kwa mantiki inayoingia akilini atadai kwamba hiyo kwa Mwenyezi Mungu siyo dhulma kwani yeye ni Muumba, na Muumba anawafanyia viumbe wake vile atakavyo, kwani yeye haulizwi kuhusu ayatendayo nao viumbe wataulizwa. Wakati utakapomuuliza kwa kusema. Ni vipi Mwenyezi Mungu anamhukumu kiumbe kuingia motoni

kabla ya kumuumba, eti kwa kuwa amemuandikia uovu na mwingine amemhukumia pepo kabla ya kumuumba kwa kuwa kamuandikia wema? Basi je, hiyo siyo dhulma kwa wawili hao kwa sababu yule atakayeingia peponi haingii humo kwa ajili ya matendo yake bali Mwenyezi Mungu kamchagulia, na vile vile atakayeingia motoni haingii humo kwa makosa aliyoyatenda bali Mwenyezi Mungu amemkadiria. Je, katika hali hiyo siyo dhulma na ni jambo linalopingana na Qur'ani? Jawabu lake atakuambia; "Hiyo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu anafanya atakavyo." Huwezi kufahamu msimamo wake unaopingana; na hii bila shaka ni kwa sababu anampa Bukhari na Muslim daraja ya usahihi kama Qur'an, na anasema kuwa vitabu sahihi baada ya kitabu cha Mwenyezi Mungu ni Bukhari na Muslim.

Ndani ya Bukhari na Muslim kuna maajabu na misiba ambayo Waislamu wamekumbwa na mtihani huo. Hakika Banu Umayyah na baada yao Banu Abbas wamefaulu sana kueneza uzushi wao na itikadi zao ambazo zinaafikiana na siasa zao mbaya, na athari zao zimebakia mpaka leo hii, kwani Wailsamu wanazizingatia kuwa ni urithi bora kwa kuwa (wanaona) ni mkusanyiko wa hadithi sahihi za Mtume kama wanavyodai. Lau Waislamu wangefahamu kiwango ambacho (Banu Ummayah na Banu Abbas) walivyomzulia Mtume **(s.a.w.w)** kwa ajili ya kutimiza malengo yao ya kisiasa, basi wasingezisadiki kabisa hadithi hizo na hasa zile zinazopingana na kitabu cha Mwenyezi Mungu.

Na kwa kuwa Mwenyezi Mungu amechukua jukumu la kuihifadhi Qur'an Tukufu, na Masahaba walikuwa wameihifadhi na wakawa wanaiaridhi kwa Mtume **(s.a.w.w)** ndiyo maana (Banu Umayyah na Banu Abbas) hawakuweza kuigeuza wala kuibadilisha, na kwa hali hiyo basi wakaigeukia Sunna takatifu wakaweka waliyoyataka kwa ajili ya yule wamtakaye, khususan kutokana na uadui wao dhidi ya watu wa nyumba ya Mtume **(s.a.w.w)** ambao ndiyo walinzi wa Qur'an na Sunna. Walizua hadithi kwa kila tukio wakainasibisha kwa Mtume **(s.a.w.w)** na wakairemba kwa Waislamu (na kuwambia) hadithi hizi ni sahihi kuliko nyinginezo, na watu wakazikubali kwa nia njema hali wakipokezana hadithi hizo kwa kurithiana kizazi baada ya kizazi tena kwa uadilifu kabisa. Mimi nasema kwamba Mashia nao ni mateka wa uharibifu na uzushi (uliofanywa) katika hadithi nyingi ambazo zinanasibishwa kwa Mtume **(s.a.w.w)** au kwa mmoja wa Maimamu watukufu (a.s).

Uingizaji huo wa hadithi na ufichaji wa ukweli huo hawajasalimika nao Mashia wala Masunni muda wote wa historia (ya Uislamu), lakini Shia wanajipambanua kutokana na Ah'li Sunna Wal-Jamaa kwa vitu vitatu ambavyo vimewapambanuwa Mashia kutokana na makundi mengine ya Kiislamu kwani itikadi yao imejitokeza kuwa salama na yenye kuafikiana na Qur'an, Sunna na Akili. Vitu hivyo vitatu ni hivi vifuatavyo:

**Jambo la kwanza**: Mashia wametoshelezwa na (uongozi wa) watu wa nyumba ya Mtume **(s.a.w.w)**, hawamtangulizi yeyote juu yao, na kila mmoja wetu anafahamu ni kina nani hawa watu wa nyumba ya Mtume ambao Mwenyezi Mungu amewaondolea uchafu na amewatakasa mno. **Jambo la Pili**: Idadi ya Maimamu wa nyumba ya Mtume ambao ni kumi na wawili, uhai wao na athari zao viliendelea kwa muda wote wa karne tatu na

wameafikiana wao kwa wao katika kila hukumu na hadithi, na hawakutofautiana kwa chochote, jambo ambalo liliwafanya wafuasi wao kuwa ni wajuzi katika kila nyanja za elimu na maarifa kwa uwazi bila ya kupingana katika itikadi na mengineyo.

**Jambo la Tatu**: Kukubali na kukiri kwa Mashia kwamba vitabu (vya hadithi) walivyonavyo vinaweza kuwa na mambo yaliyo sawa na mengine yenye makosa , na hawana kitabu sahihi isipokuwa Qur'an ambayo haitofikiwa na batili mbele wala nyuma yake. Basi inakutosha kufahamu kwa mfano kwamba, kitabu kikubwa (cha hadithi) kwao ni Usulul-Kafi wao wanasema kwamba humo kuna maelfu ya hadithi za uongo, na kwa hiyo basi utawakuta wanachuoni wao na Mujtahidina wao ni wenye bidii kutafiti na kuchambua (hadithi) hawachukui katika kitabu hicho ila hadithi iliyothibiti kwa Matni na Sanad na ile isiyopingana na Qur'an wala akili. Ama kwa upande wa Ahlul-Sunna Wal-Jamaa wao wamejilazimisha (kufuata) vitabu walivyoviita kuwa ni Sihah Sita kwa kuzingatia kwamba kila kilichomo humo ni sahihi na wengi wao (Masunni) wanarithishana rai hii bila ya utafiti wala uchunguzi. Hapana shaka kwamba, nyingi kati ya hadithi hizi ambazo zimepokelewa ndani ya vitabu hivi hazisimami kwenye dalili za kielimu na ndani yake mna kufru ya wazi wazi na mambo yanayopingana na Qur'an na mwenendo wa Mtume na matendo yake na yanaitia aibu heshima ya Mtume. Kwa mtu mwenye kutafiti inamtosha asome kitabu cha Sheikh wa Kimisri aitwaye Mahmud Abur-Rayyah kiitwacho, Adh-wau Alas-sunnatil Muhmmadiyyah ili afahamu kikoje kiwango cha Sihahi hizo sita. Al-Hamdulillah leo wapo vijana wengi wanaochunguza na wamejikomboa kutokana na minyororo hiyo, wanatofautisha kati ya (hadithi) dhaifu na yenye nguvu. Kwa hali hiyo basi hata Masheikh wenye kung'ang'ania hizo Sihahi sasa hivi wengi miongoni mwao wanazipinga Sihahi hizo, siyo kwa sababu wamekuta kuwa baadhi ya hadithi ni dhaifu, bali zimekutwa hoja wazisemazo Mashia zinazohusu hukumu za kifiqhi au kuhusu akida za mambo ya ghaibu, basi hapana hukumu au itikadi waisemayo Mashia isipokuwa utaikuta imethibiti ndani ya moja ya Sihahi sita za Masunni.

Katika hali ya majadiliano, mmoja wa baadhi ya wenye ung'ang'anizi aliniambia; "Madamu ninyi (Mashia) mnaitakidi kwamba hadithi za Bukhari siyo Sahihi, basi ni kwa nini mwazitolea hoja dhidi yetu?" Nilijibu, "Siyo kila kilichomo ndani ya Bukhari kinapingwa, ukweli ni ukweli tu na batili ni batili tu nasi tunawajibika kuchekecha ukweli na kuuchuja." Akasema, "Je, wewe unayo darubini maalum ambayo kwayo unafahamu (hadithi) sahihi kutokana na ile ya uongo?" Nikasema, "Mimi sina zaidi kuliko uliyonayo wewe, lakini zile ambazo wameafikiana Masunni na Mashia ndiyo sahihi kwa sababu usahihi wake umethibiti kwa pande zote mbili. Sisi tunawawajibishia kama walivyojiwajibishia nafsi zao, na zile walizotofautiana hata kama zitasihi kwa mmoja wao basi haulazimishwi upande wa pili kuzikubali kama ambavyo siyo lazima kwa mtafiti wa upande mmoja kuzikubali na kuzitolea hoja kama ambavyo mtafiti asiyefungamana na upande wowote halazimiki kuzikubali na kuzitolea ushahidi. Mimi nakupigia mfano mmoja unaohusu hali hiyo ili kusiwe na tatizo katika maudhui hii na ili usirejewe ukosoaji kama huo kwa njia

nyingine tofauti". Mashia wanadai kwamba Mtume **(s.a.w.w)** alimuweka Ali kuwa Khalifa wa Waislamu huko kwenye bonde la Khum siku ya tarehe kumi na nane Mwezi wa Mfunguo Tatu baada ya Hijja yake ya mwisho na alisema Mtume kuhusu mnasaba huo, "Yeyote ambaye mimi nilikuwa mtawala wake basi huyu hapa Ali ni mtawala wake, Ewe Mwenyezi Mungu msaidie atakayemtawalisha (Ali) na umpige vita atakayempiga vita (Ali)." Tukio na hadithi hii wameinakili wengi miongoni mwa wanachuoni wa Kisunni katika Sihahi zao na Musnad zao na vitabu vyao vya tarekhe, basi hapo inawezekana kwa Mashia kutoa hoja dhidi ya Masunni.

Masunni wanadai kwamba Mtume **(s.a.w.w)** alimbainisha Abubakar awasalishe watu wakati Mtume akiwa anaumwa ugonjwa uliopelekea mauti yake na akasema: "Mwenyezi Mungu na Mtume wake na waumini hawamkubali mwingine isipokuwa Abubakar." Tukio hili na hadithi hii haimo ndani ya vitabu vya Kishia, bali wao wanapokea (hadithi isemayo) kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu alituma ujumbe aitwe Ali (a.s) Aisha naye akatuma ujumbe aitwe Baba yake, na Mtume alipotambua hilo alimwambia bibi Aisha, "Hakika ninyi ni kama yule mwanamke aliyemtamani Yusuf (a.s) kisha Mtume alitoka ili akawasalishe watu na akamuondosha Abubakr. Basi haiwezekani na wala siyo uadilifu kwa Masunni kutoa hoja dhidi ya Mashia kwa tukio au hadithi waliyopwekeka nayo hasa hasa iwapo riwaya zenyewe zinapingwa na ukweli na historia, kwani Mtume wa Mwenyezi Mungu alimteua Abubakr awe katika jeshi la Usama chini ya uongozi wa Usama, na inafahamika kwamba kiongozi wa jeshi katika jeshi ndiye anakuwa Imamu wa Sala. Imethibiti kihistoria kwamba Abubakr hakuwepo Madina wakati wa kifo cha Mtume **(s.a.w.w)** bali alikuwa Sunhi akijiandaa kutoka na kiongozi wake Usama ibn Zaid ambaye alikuwa na umri wa miaka kumi na saba. Basi vipi katika hali kama hii itawezekana kwetu sisi kusadiki kwamba Mtume **(s.a.w.w)** alimchagua kuongoza Sala?

Itawezekana tu iwapo tutaisadiki kauli ya Omar ibn Khatab kwamba, Mtume anaweweseka hajui atendalo na alisemalo. Na jambo hili (la Mtume kuweweseka) halina nafasi kabisa kwa Mtume, haliwezekani na wala Mashia hawalisemi kabisa. Hivyo basi kwa mtafiti hapa na amche Mwenyezi Mungu katika utafiti wake wala yasimzuge mapenzi akaiacha haki akafuata mapenzi akajikuta amepotea njia ya Mwenyezi Mungu, bali wajibu wake ni kufuata haki japo haki hiyo anayo mwingine. Na (anawajibika) kuikomboa nafsi yake isiwe yenye kuzolewa na matamanio na ubinafsi, ili awe miongoni mwa wale aliowasifu Mwenyezi Mungu Mtukufu katika kauli yake aliposema

الَّذِينَ يَسْتَمِعُونَ الْقَوْلَ فَيَتَّبِعُونَ أَحْسَنَهُ أُولَـٰئِكَ الَّذِينَ هَدَاهُمُ اللَّـهُ وَأُولَـٰئِكَ هُمْ أُولُو الْأَلْبَابِ ﴿١٨﴾

"Wabashirie (wema) waja wangu ambao husikiliza maneno kisha wakafuata yaliyo mazuri hao ndiyo ambao aliowaongoa Mwenyezi Mungu na hao ndiyo wenye akili" (Qur'ani 39:18).

Kwa hiyo haiingii akilini Mayahudi watakaposema "Haki iko kwetu". Na Wakristo nao waseme: "Haki iko kwetu"', Waislamu nao waseme "Haki tunayo sisi" hali ya kuwa wote hawa wanahitilafiana katika itikadi na sheria.

Basi hapana budi kuwa yule anayetafiti achunguze kauli ya dini zote na azilinganishe mpaka haki imbainikie. Na haingii akilini vile vile Masunni waseme kwamba; "Haki iko pamoja nao", na Mashia nao waseme kwamba "Haki iko kwao peke yao". Hali ya kuwa (wawili hawa) wanahitilafiana katika baadhi ya mafundisho na hukumu. Haki ni moja tu haigawiki!! Kwa hiyo hapana budi kwa mtu anayetafiti afanye bidii na achunguze vile vile kauli za pande mbili hizi na azilinganishe na aipe akili yake uamuzi mpaka ukweli umbainikie, na huo ndiyo mwito wa Mwenyezi Mungu kwa kila kikundi kinachodai ukweli pindi aliposema: "Waambie leteni hoja zenu ikiwa ninyi ni wakweli". (Qur'an 2:111).

Wingi siyo dalili ya kuwa kwenye haki, bali kinyume chake ndiyo sahihi, Mwenyezi Mungu anasema:

وَإِن تُطِعْ أَكْثَرَ مَن فِي الْأَرْضِ يُضِلُّوكَ عَن سَبِيلِ اللَّـهِ إِن يَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ وَإِنْ هُمْ إِلَّا يَخْرُصُونَ ﴿١١٦﴾

"Na kama utawatii wengi wa (hawa) waliomo katika nchi watakupoteza kutoka kwenye njia ya Mwenyezi Mungu" (Qur'ani 6:116)

na Amesema tena

وَمَا أَكْثَرُ النَّاسِ وَلَوْ حَرَصْتَ بِمُؤْمِنِينَ ﴿١٠٣﴾

"Na watu wengi hawatakuwa wenye kuamini hata kama utajitahidi vipi" (Qur'ani 12:103).

(Hali hii) ni kama ambavyo maendeleo ya kielimu na teknolojia na uchumi siyo dalili ya kwamba watu wa magharibi wako kwenye haki na wale wa Mashariki wako kwenye batili. Mwenyezi Mungu anasema:

فَلَا تُعْجِبْكَ أَمْوَالُهُمْ وَلَا أَوْلَادُهُمْ إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّـهُ لِيُعَذِّبَهُم بِهَا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَتَزْهَقَ أَنفُسُهُمْ وَهُمْ كَافِرُونَ ﴿٥٥﴾

"Zisikufitini mali zao wala watoto wao hakika Mwenyezi Mungu anataka awaadhibu kwa hizo (mali) katika maisha ya dunia na zitoke roho zao hali ya kuwa ni makafiri. (Qur'ani 9:55).

Kauli ya Ahlud-dhikri juu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu Imam Ali (a.s) anasema: "Sifa njema anastahiki Mwenyezi Mungu ambaye anayajua mambo yaliyofichikana, na dalili zilizo wazi zimemtambulisha yeye.

Amefichikana kwa jicho la mwenye kuona, hapana jicho la asiyemuona linalo mkanusha, wala hakuna moyo wa aliyemthibitisha utakaomuona. Ametangulia kwa utukufu hapana cho chote kitukufu kuliko yeye na yu karibu mno. hakuna kilicho karibu kuliko yeye na utukufu wake haukumtenga mbali na viumbe wake na wala ukaribu wake haukuwalinganisha kwake katika daraja. Akili hazikupewa uwezo wa kutambua ukomo wa sifa zake, na wala hazikuzuiliwa ulazima wa kumfahamu. Basi ni yeye ambaye dalili za ulimwengu zinashuhudia juu ya kukiri kwa moyo wenye upinzani. Ametukuka mno Mwenyezi Mungu na yu mbali na yale wayasemayo wenye kumfananisha na wale wampingao." Anaendelea kusema: "Kila sifa njema ni zake Mwenyezi Mungu ambaye hapana hali yo yote iliyomtangulia na hakuna asemwaye kuwa ni wa pekee ila ni yeye. Na kila mwenye nguvu asiye yeye ni dhalili, na kila mwenye uwezo asiye yeye basi yu dhaifu. Na kila Mfalme ambaye si yeye basi yuko

chini ya Ufalme wake. Na kila mjuzi ambaye si yeye ni mwenye kujielimisha. Na kila mwenye kuweza ambaye si yeye huwezwa na hutenzwa nguvu. Na kila asikiaye ambaye si yeye hasikii sauti nyepesi na hufanywa kiziwi kwa sauti kubwa na hasikii kilicho mbali, na kila aonaye asiye yeye haoni aina ya vitu vilivyofichikana na haoni viwiliwili laini, na kila aliye dhahiri asiye yeye basi kafichikana. Kila aliyefichikana asiye yeye yu dhahiri. Hakuumba alivyo viumba ili kuimarisha Ufalme, wala si kwa kuchelea matokeo ya zama, wala kwa kutaka msaada wa mshirika mshauri, wala mshirika mwingi wa fahari wala mpinzani mwenye kuchukiza, lakini wote hao ni viumbe wenye kuchungwa na ni waja wanyonge. Hakuingia ndani ya vitu asemwe kuwa yumo humo, na hakuwa mbali akasemwa kajitenga navyo.

Hakikumshinda kiumbe alichokianzisha wala kuendesha alichokiumba, wala hakupatikana na kushindwa kwa vile alivyoviumba, na wala hakuingiwa na utatanishi ndani ya yale aliyoyahukumu na kukadiria bali ni maamuzi bora. Na elimu iliyothabiti na ni jambo lililosadikishwa, mwenye kutumainiwa pamoja na kuadhibu, na mwenye kuogopewa pamoja na neema. Hana mwanzo wala mwisho, yeye ndiyo wa mwanzo yupo na ni mwenye kubaki bila ya ukomo, zimeinama nyuso kwa ajili yake na midomo yampwekesha. Fikra haziwezi harakati na wala viungo na vifaa. Hasemwi alianza kuwa lini, hakuwekewa kikomo kwa tamko wala mpaka, yu dhahiri hasemwi anatokana na nini. Ametukuka Mwenyezi Mungu kutokana na mwenendo wa wanaomuwekea mipaka miongoni mwa sifa za kukadiria na ukomo wa eneo na asili ya makazi na kumfanyia makao, ukomo kwa waja wake umewekwa na umenasibishwa kwa wasiokuwa yeye. Hakuumba vitu kutokana na asili ya milele wala vyanzo vya milele, bali ameumba alivyoviumba akaviwekea ukomo wake. Na ameumba alivyoumba na akavifanyia maumbile mazuri hapana kinachoshindikana kwake wala haumnufaishi utiifu wa chochote, elimu yake kwa wafu waliokwishapita ni kama elimu yake kwa waliobakia hai na elimu yake kwa vilivyomo mbinguni juu ni kama elimu yake kwa vilivyomo ndani ya ardhi chini kabisa.

2

# WAULIZE WANAOFAHAMU

## MLANGO WA PILI KATIKA MAMBO YANAYOMUHUSU MTUME (s.a.w.w).

**Swali la Pili**: Isma ya Mtume **(s.a.w.w)**. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema kuhusu ustahiki wa Mtume wake Muhammad **(s.a.w.w)**

"Na Mwenyezi Mungu atakulinda kutokana na watu**.**" (Qur'an, 5:67), na amesema tena:

وَمَا يَنطِقُ عَنِ الْهَوَىٰ ﴿٣﴾

"Na wala hasemi kwa matamanio (ya nafsi yake) isipokuwa ni ufunuo uliofunuliwa kwake." (Qur'an, 53:3).

Na akasema tena,

وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانتَهُوا ﴿٧﴾

"Na yale anayokupeni Mtume basi yachukuweni, na yale anayokukatazeni komeni (msiyafanye)." (Qur'an, 59:7).

Aya zote hizi zinajulisha wazi juu ya Isma (kuhifadhika) kwake Mtume **(s.a.w.w)** moja kwa moja katika kila kitu. Ama ninyi (Ahlus-Sunnah Waljamaa) mnasema kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** ni Maasum (amehifadhika) katika kufikisha Qur'an tu, na mambo mengine yeye ni kama watu wengine, anakosea na anapatia, na mnatolea ushahidi ili kuthibitisha kukosea kwa Mtume katika minasaba mbali mbali kwa hadithi mnazopokea ndani ya vitabu vyenu. Ikiwa hali ndiyo iko namna hii (kama mnavyodai) basi hoja yenu iko wapi na dalili yenu ni ipi kuhusu madai yenu ya kushikamana na kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna ya Mtume wake maadam Sunna hii kwenu ninyi haikuhifadhika na inawezekana kukawa na makosa ndani yake? Na kwa msingi huu basi, kushikamana na Kitabu na Sunna kwa mujibu wa itikadi zenu hakusalimiki kuwa na makosa, na hasa tutakapofahamu kwamba Qur'an yote imefasiriwa na kubainishwa na Sunna ya Mtume. Basi hoja yenu ni ipi inayothibitisha kuwa tafsiri yake (Mtume) na ubainishaji wake haukuwa umekwenda kinyume na kitabu cha Mwenyezi Mungu? Mmoja wa Masunni aliniambia alipokuwa akielezea maoni haya (akasema): "Bila shaka Mtume **(s.a.w.w)** alikhalifu hukumu nyingi zilizomo katika Qur'an kutegemeana na vile Maslahi yanavyopelekea."

Mimi nilisema katika hali ya kushangaa: "Nipe mfano mmoja juu ya yeye kuikhalifu Qur'an." Alijibu akasema: "Qur'an inasema:

الزَّانِيَةُ وَالزَّانِي فَاجْلِدُوا كُلَّ وَاحِدٍ مِّنْهُمَا مِائَةَ جَلْدَةٍ ﴿٢﴾

Mzinifu mwanamke na mzinifu mwanamume wapigeni kila mmoja wao mijeledi mia moja". (Qur'an, 24:2).

wakati ambapo Mtume aliwahukumu mzinifu mwanamume na mzinifu mwanamke wapigwe mawe jambo ambalo halimo ndani ya Qur'an." Mimi nilisema: "Bila shaka kupigwa mawe ni hukumu ya yule mwenye hifadhi (mwenye mke au mume) atakapozini awe mwanamume au mwanamke na mijeledi ni kwa mjane atapozini, awe mwanamke au mwanamume". Sunni yule akasema: "Ndani ya Qur'an haikutajwa mjane au aliyehifadhika, kwani Mwenyezi Mungu hakuhusisha (aina ya mzinifu) bali ametumia tamko

mzinifu mwanamke na mzinifu mwanamume bila ya kuhusisha". Mimi nikasema: "Kwa hiyo kwa msingi huu basi kila hukumu ya moja kwa moja iliyomo katika Qur'an na Mtume akaihusisha hivi yeye Mtume atakuwa ameikhalifu Qur'an? Na kwa msingi huu ndiyo maana wewe unasema kuwa Mtume ameikhalifu Qur'an katika hukumu zake nyingi? Alijibu hali ya kuwa kachanganyikiwa: "Qur'an peke yake ndiyo imehifadhiwa kwa kuwa Mwenyezi Mungu amechukua jukumu la kuihifadhi, ama Mtume yeye ni mtu tu, anakosea na kupatia kama ambavyo Qur'an inasema juu ya stahiki yake, Waambie sikuwa mimi ila ni mtu mfano wenu ninyi." Nikasema: "Basi ni kwa nini tunaswali Asubuhi, Adhuhuri, Alasiri, Magharibi na I'sha, na hali ya kuwa Qur'an imetumia tamko Sala bila ya kuzihusisha nyakati zake?".

Alijibu: "Ndani ya Qur'an kuna (aya isemayo), Bila shaka sala imekuwa kwa waumini ni faradhi iliyowekewa wakati maalum. Na Mtume ndiye aliyebainisha nyakati za Sala." Nikasema: "Basi ni kwa nini unamsadiki katika (kubainisha) nyakati za sala na unampinga juu ya hukumu ya kumpiga mawe mzinifu?" Alijaribu kwa juhudi zake kunitosheleza kwa njia ya falsafa mbovu zinazopingana ambazo haziwezi kusimama kwenye dalili ya kiakili wala kimantik, kama pale aliposema: "Hatuwezi kuwa na mashaka juu ya Sala kwa sababu Mjumbe wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** alisali muda wote wa uhai wake tena kila siku mara tano, ama kumpiga mawe mzinifu hatuwezi kuwa na utulivu (wa nafsi) kwani hakufanya jambo hilo katika uhai wake isipokuwa mara moja au mara mbili." Na kama alivyosema (tena huyu Sunni) kwamba, "Mtume hakosei pale Mwenyezi Mungu anapomuamuru jambo fulani, ama wakati anapohukumu kwa fikra yake, basi yeye anakuwa hakuhifadhika kutokana na makosa, na kwa sababu hiyo basi Masahaba walikuwa wakimuuliza kila jambo kwa kumwambia, Je, jambo hilo linatoka kwake au ni linatoka kwa Mwenyezi Mungu, na pindi akiwaambia kuwa ni jambo lililotoka kwa Mwenyezi Mungu basi mara moja hulitekeleza bila ya kufanya mjadala. Ama akisema kuwa jambo hilo ni kutoka kwangu (yaani kwake Mtume), hapo humjadili na kumpa nasaha na yeye hukubali nasaha zao na maoni yao. Na wakati mwingine Qur'an hushuka kuafiki maoni ya baadhi ya Masahaba na kukhalifu maoni yake kama ilivyo katika qadhiya ya mateka wa Badri, na qadhiya nyinginezo mashuhuri".

Nilijaribu kwa kadiri ya uwezo wangu kumkinaisha lakini bila mafanikio, kwani wanachuoni wa Kisunni wanaamini hivyo (juu ya Isma) na vitabu vyao vimejaa maelezo kama haya yanayoifedhehesha Isma ya Mtume na kumfanya kuwa ni mtu mwenye kiwango cha chini kuliko mtu mwenye akili pevu au chini ya kiwango cha kamanda wa kiaskari au hata chini ya kiwango cha Sheikh wa Tariqa kwa masufi. Sintakuwa nazidisha nitakaposema kuwa wamemuweka Mtume **(s.a.w.w)** chini ya kiwango cha mtu wa kawaida, tutaposoma baadhi ya riwaya zilizomo ndani ya sihahi za Ahlus-Sunnah wal-Jamaa itatubainikia wazi ni kwa kiasi gani athari za Kibanu Umayyah zimekita mizizi yake katika akili za Waislamu tangu zama (walizotawala) na zimebakia mpaka nyakati zetu hizi.

Tukitafiti madhumuni na lengo la hayo, huenda tukatoa matokeo yasiyo na shaka na machungu, lakini kwa ufahamisho matukio yenyewe ni haya:

Ni kwamba jamaa hao waliowatawala Waislamu katika zama za dola ya Bani Umayyah wakiongozwa na Muawiyyah ibn Abi Sufiyani hata siku moja hawakuamini kwamba Muhammad ibn Abdillah ni mjumbe aliyetumwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu au ni Nabii wa kweli wa Mwenyezi Mungu. Dhana yenye nguvu kwa (watu hao) walikuwa wakiitakidi kuwa yeye Mtume ni mchawi aliyewashinda watu na ameimarisha ufalme wake kwa msaada wa wanyonge miongoni mwa watu, na hasa hasa watumwa ambao waliutia nguvu wito wake na wakamsaidia. Hii siyo dhana tu kwani baadhi ya dhana ni dhambi, lakini tunaposoma ndani ya vitabu vya historia ili tupate kumfahamu Muawiya na mazingira yake, na yote aliyoyafanya muda wote wa uhai wake hasa muda wa utawala wake, basi inakuwa ni hakika (yaani ni kweli wala si dhana tena) hakuna njia ya kuikwepa. Sote tunafahamu kuwa Muawiya ni nani na baba yake Abu Sufiyan ni nani na mama yake (Muawiya) Hindu ni nani (katika historia yao dhidi ya Uislamu). Basi Muawiya ni muachwa huru mwana wa muachwa huru ambaye ujana wake aliumaliza akiwa chini ya malezi ya baba yake na (alikuwa) chini ya mafunzo ya majeshi yaliyoandaliwa kumshambulia Mtume na kuumaliza wito wake (ujumbe wa Uislamu) kwa juhudi zake zote mpaka mbinu zake zote ziliposhindwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu akamshinda (yeye Muawiya) na baba yake, akasalimu amri bila ya kuwa ni mwenye kuamini. Lakini Mtume **(s.a.w.w)** kwa ukarimu wake na utukufu wa tabia yake alimsamehe na akamwita kuwa ni muachwa huru. Na baada ya Mtume kufariki, baba yake Muawiyah (Abu Sufiyan) alijaribu kuzusha fitna ili aumalize kabisa Uislamu, hilo alilifanya pale alipomjia usiku Imam Ali (a.s) kumchochea afanye mapinduzi dhidi ya Abubakr na Omar na akawa anamtia tamaa ya mali na watu (wa kumsaidia), lakini Imam Ali (a.s) alifahamu makusudio yake akamfukuza. Hivyo basi (Abu Sufiyan) alibakia katika maisha ya chuki dhidi ya Uislamu na Waislamu katika uhai wake wote mpaka pale Ukhalifa ulipohamia kwa mtoto wa ami yake Bwana Uthman ibn Af-faan. Hapo ndipo alipodhihirisha yaliyokuwa (yamejificha) ndani ya nafsi yake ambayo ni ukafiri na unafiki akasema: "Enyi watoto wa Umayyah, udakeni (muung'ang'anieni) Ukhalifa kama udakwavyo mpira, amma hakika kwa yule ambaye Abu Sufiyan anamuapia, hakuna pepo wala moto." Ibn Asakir ameandika ndani ya kitabu chake juzuu ya sita ukurasa wa 407 kuwa, "Imepokewa kutoka kwa Anas kwamba, Abu Sufiyan aliingia kwa Uthman, baada ya kuwa amepofuka akasema: "Hivi hapa kuna yeyote (asiyekuwa miongoni mwetu Banu Umayyah)? Wakasema, Hapana, Abu Sufiyan akasema, "Ewe Mwenyezi Mungu lifanye jambo hili (la Uislamu) liwe ni jambo la kijahiliyyah, na Ufalme huu uwe ni Ufalme wenye kupokonywa, na uimarishe utawala wa Banu Umayyah."

Ama mwanawe Abu Sufiyan yaani Muawiyah, na huyo Muawiya ni nani? Simulia wazi wazi wala hakuna kosa (kumueleza Muawiya alivyo) na matendo yake aliyoyafanya dhidi ya ummati wa Muhammad **(s.a.w.w)** katika muda wote wa ugavana wake huko Shamu na baadaye alipoukalia Ukhalifa kwa nguvu na shinikizo, na mengineyo waliyoyataja wanahistoria ikiwa ni pamoja na (yeye Muawiyah) kuidhalilisha Qur'an na Sunnah na kuchupa kwake mipaka ambayo imewekwa na sheria. Hakika Muawiyah

alitenda matendo ambayo kalamu inastahi kuyaandikia na ulimi nao unastahi kuyatamka kutokana na ubaya na uchafu wa matendo hayo. Kwa hakika tumeacha kuyataja (matendo yake) kwa kuzingatia hisia za ndugu zetu miongoni mwa Ahlus-Sunnah wal-Jamaa na wale ambao nyoyo zao zimeyeyushwa na mapenzi ya kumpenda Muawiyah na kumtetea mtu huyu. Lakini hapa hatujaacha kutaja undani wa mtu (huyu) na itikadi yake kumhusu Mtume **(s.a.w.w)** kwani itikadi yake haiko mbali na ile itikadi ya baba yake, na itikadi hiyo aliinyonya ndani ya maziwa ya mama yake aliyekuwa akiitwa Hindu mla maini (ya Sayyidna Hamza ibn Abdul-Mut-Talib) tena (Mama huyo) alikuwa mashuhuri kwa uzinifu na uchafu, kama ambavyo alivyoyarithi hayo toka kwa baba yake ambaye ni mkuu wa wanafiki ambaye Uislamu haukupata njia ya kuingia moyoni mwake. Na kama tulivyokwisha ufahamu undani wa baba yake, basi huyu hapa mwanawe naye anaeleza undani wake kwa maelezo yale yale lakini kwa njia yake (inayoonyesha) ujanja na unafiki.

Amepokea Zubair bin Bakar kutoka kwa Mutawaf bin Mughirah bin Shuuba At-Thaqafi amesema: "Niliingia mimi na baba yangu kwa Muawiyah, na baba yangu alikuwa akienda kwa (Muawiya) na kuzungumza kwake kisha huja akamtaja Muawiyah na akili yake na hupendezwa na mambo ayaonayo kwake. Basi usiku mmoja alikuja (kutoka kwa Muawiyah) akakataa kula chakula cha jioni, na nikamuona ni mwenye huzuni. Nikamsubiri kwa muda na nikahisi kuna jambo lililotokea juu yetu au katika kazi yetu nikamwambia, mbona nakuona ni mwenye huzuni tangu usiku ulipoingia?" Akasema: "Ewe Mwanangu, hakika nimetoka kwa mtu mbaya kuliko watu wote". Nikamwambia, "Ni nani huyo?" Akasema, "Nimemwambia Muawiyah na nilikua naye faragha ya kwamba, Hakika wewe umekwisha fikia lengo lako ewe Amriul-Muuminina, lau utaonesha uadilifu na ukaeneza wema, kwani wewe sasa hivi ni mtu mzima na lau utawaangalia nduguzo Bani Hashim, ukashirikiana vyema na kizazi chao, Wallahi leo hii hawana cho chote unachokiogopa toka kwao, na kwa kufanya hivyo kwako utabakia utajo (mwema) na thawabu zake."

Muawiyah akanijibu, "Haiwezekani kabisa, ni utajo gani ninaotarajia kuwa utabakia (baada yangu)? Alitawala ndugu wa kizazi cha Taim akafanya uadilifu na akatenda aliyoyatenda, lakini alipokufa basi na utajo wake nao ukafa, isipokuwa ikawa husema msemaji, Abubakr. Kisha alitawala ndugu wa kizazi cha Adiyyi, akajitahidi na kuimarika kwa miaka kumi, basi Wallahi alipokufa na utajo wake nao ukafa isipokuwa aseme msemaji, Umar. Hatimaye alitawala ndugu yetu Uthman, akawa ametawala mtu ambaye hakuwepo yeyote mwenye mfano katika nasaba yake, akatenda aliyoyatenda naye akatendewa, Wallahi alipokufa utajo wake nao ulikufa ikawa yanatajwa aliyofanyiwa. Lakini kwa hakika ndugu wa kizazi cha Hashim anapigiwa makelele kila siku mara tano (katika adhana) Ash-hadu Anna Muhammadan Rasulullah. Sasa basi, ni tendo gani na ni utajo gani utakaobakia sambamba na utajo huu? Koma (kunishauri jambo kama hilo) na Wallahi (hakuna kingine kitakachobaki) isipokuwa kuwaangamiza tu." Umepata hasara na umefedheheka ewe muovu uliyetaka kuuangamiza utajo wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kwa juhudi zako zote,lakini juhudi zako zimeshindwa kwa sababu Mwenyezi Mungu anakufuatia nyendo zako na ni

yeye aliyesema: "Na tumeutukuza utajo wako". Basi kamwe wewe si mwenye uwezo wa kuufuta utajo wake ambao Mwenyezi Mungu ameutukuza, Mola mwenye nguvu na utukufu, basi fanya vitimbi vyako na uwakusanye jamaa zako, wewe huna uwezo wa kuizima nuru ya Mwenyezi Mungu kwa mdomo wako na Mwenyezi Mungu ataikamilisha nuru yake licha ya chuki za unafiki wako, uliimiliki nchi mashariki mpaka magharibi na wakati ulipokufa na utajo wako nao ukafa ila akutaje mwenye kukutaja kwa matendo yako maovu ambayo kwayo ulitaka kuubomoa Uislamu kama yalivyokuja hayo kupitia kauli ya Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**. Na umebakia utajo wa Muhammad ibn Abdillah ndugu wa (kizazi cha) Hashim kwa karne na zama zote mpaka hapo Mwenyezi Mungu atakapoiondosha ardhi na vilivyoko juu yake. Na kila amtajapo Mtume (yeyote) mwenye kumtaja humsalia yeye na kizazi chake licha ya chuki zako na chuki za Banu Umayyah ambao walijaribu kwa kuongozwa na wewe kukiangamiza kizazi cha Hashim na utukufu wao, basi (njama hizo) hazikuwaongezea isipokuwa utukufu na utajo mwema. Amma ninyi (enyi Banu Umayyah) mtakutana na Mwenyezi Mungu siku ya Qiyama hali ya kuwa amekukasirikieni kwa yale mliyoyazusha ndani ya sheria yake na atakulipeni mnachostahiki.

Tukiongeza juu ya hawa (tuliokwisha wataja) ni mtoto wao Yazid ibn Muawiyah asiye na haya, muovu mnywa pombe na anayedhihirisha ufasiqi na uovu wazi wazi, basi yeye tunamkuta ndiye wa mwisho aliyebeba itikadi ile ile ambayo ameirithi kwa baba yake Muawiyah na babu yake Abu Sufiya, kama ambavyo amerithi kutoka kwao ukatili na uovu na kunywa pombe na kutopea katika uzinifu na kucheza kamari. Na lau hata asingekuwa na sifa zote hizi mbaya, Muawiya hakustahiki kumrithisha (Yazid) Ukhalifa na kumtawalisha juu ya shingo za Waislamu, na hali ya kuwa wote wanamfahamu fika. Muawiyah alifanya hayo hali ya kuwa (akijua) miongoni mwa Waislamu walikuwemo masahaba watukufu kama vile Hussein ibn Ali Bwana wa vijana wa peponi. Na hapana shaka kwamba Muawiyah alimaliza muda wa uhai wake (katika) kutoa mali yake ambayo aliipata kwa njia za haramu ili auangamize Uislamu na Waislamu wa kweli. Bila shaka tumekwisha ona ni jinsi gani alikuwa akitaka kuufuta utajo wa Muhammad **(s.a.w.w)** na hilo hakuweza ndipo alipowasha moto wa vita dhidi ya Imam Ali ambaye ni ibn ammi ya Mtume na ni wasii wake mpaka akamuua na akaushika Ukhalifa kwa nguvu, udanganyifu na unafiki. Aliweka Sunna yake chafu na akawaamuru wawakilishi wake katika kila nchi wamlaani Ali (a.s) pamoja na watu wa nyumba ya Mtume **(s.a.w.w)** kwenye mimbari na ndani ya kila Sala.Kwa kufanya hivyo (bila shaka) alikuwa akikusudia kumlaani Mtume wa Mwenyezi Mungu, na hila zake ziliposhindwa alikufa bila kulitimiza lengo lake isipokuwa alimuweka mwanawe na akamtawalisha juu ya Ummah ili aendeleze malengo yake aliyoyaweka yeye Muawiyah na baba yake Abu Sufiyan. Ni malengo gani hayo? Hapana kingine bali ni kuuangamiza Uislamu na kurudisha mambo kwenye zama za ujinga.

Yazid muovu asiye na haya aliukumbatia Ukhalifa na akaziimarisha nguvu zake kwa ajili ya kuuangamiza Uislamu kama yalivyokuwa mapenzi ya baba yake. Hivyo basi alianza kwa kulihalalishia jeshi lake kuuvamia mji

wa Mtume **(s.a.w.w)**, jeshi lake la kikafiri likafanya lilivyofanya, na kwa muda wa siku tatu yalifanyika mauaji makubwa kwa maelfu ya Masahaba wema na baada ya hapo alifuatishia kumuua Bwana wa vijana wa peponi na kiliwazo cha Mtume **(s.a.w.w)** na watu wote wa nyumba ya Mtume ambao ndiyo nuru ya ummahma akawateka wanawake watukufu wa nyumba ya Mtume. "Hakika sisi ni Milki ya Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea." Na lau Mwenyezi Mungu asingempunguza umri wake, angeumaliza Uislamu na Waislamu. Jambo muhimu (tunalolikusudia) katika utafiti huu ni kuidhihirisha wazi itikadi ya Yazid kama tulivyoidhihirisha wazi itikadi ya baba yake na babu yake.

Wanahistoria wamesimulia kwamba, baada ya tukio baya la kuuvamia mji wa Madina na kuwauwa Waislamu wema elfu kumi isipokuwa wanawake na watoto, na (katika tukio hilo) bikra za kiasi cha wasichana elfu moja ziliharibiwa na wanawake wapatao elfu moja walishika mimba bila ya kuwa na waume. Kisha watu waliobakia walifanya Baiah wakiwa ni watumwa wa Yazid na aliyekataa aliuawa. Yazid zilipomfikia habari za maovu hayo ambayo yanamfanya mtu alie (kwa uchungu) na wala historia haijapata kuyashuhudia ambapo hata Wamongolia na Watataar... na Waisraeli (hawajapata kutenda hayo), Yazid alifurahi na akaonesha kufurahia msiba uliompata Mtume wa Uislamu na ndipo aliposema kauli ya Ibn Az-Zub-ari, kauli ambayo aliisema baada ya tukio la Uhd akasema: "Laiti wazee wangu (waliouawa) siku ya Badri wangeshuhudia khofu (iliyowapata) Khaz-Raji kutokana na tukio la vita, basi wangejitokeza wakafurahi, kisha wangesema, Ewe Yazid usihuzunike, bila shaka tumemuuwa Bwana Mtukufu miongoni mwa watukufu wao na tumelipa kisasi cha Badri na tumelingana".Aliendelea akasema, "Iwapo sintaacha kuwaadhibu kizazi cha Ahmad (Muhammad) kwa yale yaliyotendeka (hapo kabla). Bani Hashim walicheza (mchezo wa) Ufalme, hakuna habari yoyote iliyokuja wala hapakushuka Wahyi."

Basi ikiwa babu wa Yazid (Abu Sufiyan) ambaye ndiye adui wa kwanza wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake anasema wazi wazi kwamba, "Udakeni (Ukhalifa) enyi Banu Umayyah kama udakwavyo mpira, basi kwa yule ambaye Abu Sufiyan anamuapia. hakuna pepo wala moto." Na iwapo baba wa Yazid (Muawiyah) ambaye ni adui wa pili wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake (naye) anasema wazi wazi (pale anapomsikia Muadhini anashuhudia kwamba Muhammad ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu) yeye aseme "Ni utajo gani utakaobakia (kwangu) sambamba na (utajo) huu, basi koma Wallahi nitaendelea kuwaangamiza tu." Kama mtoto (wao) Yazid ambaye ni adui wa tatu wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake naye anasema wazi wazi kwamba "Banu Hashim walicheza (mchezo wa) Ufalme, hakuna habari iliyokuja wala Wahyi ulioshuka." Nasi tunapokuwa tumezifahamu itikadi za watu hawa juu ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake na (itikadi zao) juu ya Uislamu, na tukawa tumefahamu matendo yao maovu ambayo kwayo walitaka kubomoa nguzo za Uislamu na kumchafua Mtume wa Uislamu. Isitoshe hali hiyo, bali matendo mengine tumeacha kuyataja kwa nia ya kufupisha maelezo, kwani lau tungetaka kupanua zaidi tungejaza mkusanyiko mkubwa (wa kitabu) kinachohusu matendo ya Muawiyah peke yake ambayo yamebakia kuwa ni aibu na fedheha kwake

wakati wote japokuwa walijaribu kuyaficha. Baadhi ya wanachuoni waovu ambao walikuwa wakikirimiwa na Banu Umayyah, macho yao yalipofuka wakaiuza akhera yao kwa thamani ya dunia yao, na haki wakaifunika kwa batili hali yakuwa wanafahamu na Waislamu wengi walibakia kuwa mateka wa uovu huu na uzushi huu. Na lau mateka hawa wangefahamu ukweli kabisa wasingemtaja Abu Sufiyan na Muawiyah na Yazid isipokuwa kwa kuwalaani na kujitenga nao. Lakini jambo muhimu katika utafiti huu mfupi ni kufikia kwenye kiwango cha namna zilivyo athari za watu hawa (Banu Umayyah) na wafuasi wao na vipenzi vyao (katika kuuvuruga Uislamu), ambao waliwatawala Waislamu kwa muda wa miaka mia moja Hapana shaka kwamba athari ya wanafiki hawa ilikuwa kubwa kwa Waislamu, kwani waliwageuza itikadi zao, mienendo yao, tabia zao na mahusiano yao mpaka ibada zao, kiasi kwamba ni namna gani tutaweza kueleza ni jinsi gani umma wa Kiislamu uliacha kuitetea haki na kuwafanyia uhaini Mawalii wa Mwenyezi Mungu na (kinyume chake ikawa ni) kusimama pamoja na maadui wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake **(s.a.w.w)**.

Ni jinsi gani tutaweza kueleza namna Muawiya aliyeachwa huru, mtoto wa muachwa huru na mwenye kulaaniwa mtoto wa aliyelaaniwa alivyoweza kuufikia Ukhalifa ambao unawakilisha cheo na Ukhalifa wa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**, tutawezaje kulieleza hili wakati wanahistoria wanatupotosha eti kwamba watu walikuwa wakimwambia Omar ibn Khatab, "Lau tungekuona unapotoka tungekurekebisha kwa panga zetu." Ni wanahistoria hao hao ndiyo wanaotueleza habari za Muawiyah aliyetwaa cheo cha Ukhalifa kwa nguvu na mabavu, na hotuba yake ya kwanza anayoisema mbele ya Masahaba wote kama ifuatavyo; "Bila shaka mimi sikuwapigeni eti kwa ajili mswali wala kwa ajili mfunge, lakini (nimekupigeni) ili niwatawaleni na sasa mimi huyu hapa ni mtawala wenu."

Hakuna (Sahaba) yeyote miongoni mwao anayejaribu kutingishika wametulia tulii, wala hapana aliyempinga (Muawiyah kwa kauli hiyo) bali anatamba kiasi kwamba wanahistoria wanauita mwaka huo aliotawala Muawiya kuwa ni mwaka wa umoja, na kwa kusema kweli huo ulikuwa ndiyo mwaka wa kusambaratika kwa Waislamu. Kisha tunawaona Masahaba baada ya hayo (aliyowatendea Muawiya) wanakubali awatawalishie mwanawe muovu Yazid ambaye anafahamika kwao wote, hawakupinga wala kujitetea isipokuwa wachache ambao Yazid aliwauwa katika tukio la uvamizi wa Madina na akachukua baia kwa wale waliobakai (tena kwa nguvu) akawafanya kuwa watumwa wake. Basi ni jinsi gani tutayaeleza yote hayo, kwani tunachokikuta baada ya hayo ni kwamba waovu wa kibanu Umayyah kama Marwan ibn Al-Hakam na Walid ibn Uqbah na wengineo waliutwaa Ukhalifa kwa niaba ya kuwaongoza waumini. Kwa kupitia viongozi wa aina hiyo mambo yaliharibika yakafikia hatua ya kuushambulia mji wa Mtume wa Mwenyezi Mungu na wakatenda mjini humo matendo machafu, na vitu vitakatifu vikavunjiwa heshima zake, (kama hayo hayakutosha) bali waliiunguza nyumba tukufu ya Mwenyezi Mungu (Al-Kaaba) na waliwauwa ndani ya Haram hiyo Masahaba wema. Kwa amri ya hao (waitwao kuwa) viongozi wa waumini mambo yalifikia hata kuimwaga damu ya Mtume wa Mwenyezi Mungu pale walipomuuwa kiliwazo cha Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** Husein ibn Ali (a.s) na

kizazi chake na wakawateka mabinti zake, (basi kwa yote hayo) hakuna yeyote aliyeshituka miongoni mwa watu wa umma wa Kiislamu wametulia na wala Bwana wa vijana wa peponi Imam Husein (a.s) hakupata wa kumtetea.

Na kwa hao waliojiita viongozi wa waumini walifikia hatua ya kukichana kitabu cha Mwenyezi Mungu na kisha wakakiambia, "Utakapokutana na Mola wako siku ya ufufuo mwambie ewe Mola wangu Walid alinichanachana." Tendo hili alilitenda Walid wa ukoo wa Banu Umayyah. Mambo hayakuishia kupitia kwao hao viongozi wa waumini, bali walimlaani Ali ibn Abi Talib juu ya minbari na wakawaamuru watu wamlaani katika kila nchi, na hali hakuna wanachokikusudia kwa tendo hilo isipokuwa kumlaani Mtume wa Mwenyezi Mungu, wakati yote haya yanatendeka watu walitulia kimya hakuna aliyeshtuka miongoni mwao, na aliyekataa kumlaani Ali (a.s) aliuawa, akasulubiwa na kuteswa kama onyo kwa wengine. Mambo yalifikia kwa viongozi hao wa waumini kunywa pombe hadharani na kuzini, kufanya mambo ya upuuzi, kuimba na kucheza n.k Basi ikiwa mambo ya umma wa Waislamu yalifikia kiwango kama hiki cha kuporomoka katika maadili yao na udhalili kama huu, basi hapana budi kuna mambo ambayo yaliathiri itikadi yao, na hili ndilo jambo muhimu katika utafiti huu kwani linafungamana na maudhui ya Ismah na heshima ya Mtume Mtukufu **(s.a.w.w)**. Jambo la kwanza linalotufanya tuwe waangalifu hapa ni kwamba, Makhalifa watatu Abubakr, Umar na Uthman walizuwia hadithi za Mtume **(s.a.w.w)** zisiandikwe wala kusimuliwa.

Basi huyu hapa Abubakr anawakusanya watu na anawaambia, "Hakika ninyi mnasimulia hadithi toka kwa Mtume **(s.a.w.w)** ambazo ndani yake mnatofautiana, na watu watakaokuja baada yenu watahitilafiana mno. Hivyo basi msisimulie cho chote toka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, na yeyote atakaye kuulizeni mwambieni kuwa baina yetu kuna Kitabu cha Mwenyezi Mungu, ihalalisheni halali yake na muiharamishe haramu yake." Kama alivyofanya Abubakr, Umar bin Khatab naye aliwazuwiya watu wasisimulie hadithi za Mtume **(s.a.w.w)**. Qur-Zatu ibn Kaab anasema: "Umar bin Khatab alipotutuma kwenda Iraq alitushindikiza na akatuambia; Je, mnafahamu ni kwa nini nimekushindikizeni? Wakasema, bila shaka kwa kutuheshimu tu. Umar akasema: Pamoja na hilo, bila shaka ninyi mtawafikia watu wa kijiji (fulani) wanao mvumo kwa kusoma Qur'an kama mvumo wa nyuki, basi msiwazuwiye kwa hadithi mtawashughulisha isomeni Qur'an na mpunguze maelezo ya hadithi za Mtume wa Mwenyezi Mungu, nami niko pamoja nanyi." Mpokeaji wa hadithi hii anasema: "Basi sikunakili hadithi yoyote kamwe baada ya maneno ya Umar." Alipofika Iraq watu walimkimbilia wakimuuliza juu ya hadithi (za Mtume), Qur-zah akawaambia, "Umar alitukataza kufanya hivyo." Kama ambavyo Abdur-Rahman ibn Auf alisema kwamba, "Umar bin Khatab aliwakusanya masahaba toka sehemu mbali mbali kwa ajili ya kuwazuwia kuzizungumza hadithi za Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa watu na akawaambia, "Bakieni hapa kwangu na wala msiachane nami muda wote wa uhai wangu." Masahaba hao hawakuondoka mpaka alipokufa. Vile vile amelieleza jambo hili Al-khatib Al-bagh-dadi na Addhahabi ndani ya Tadh-kiratul-hufadh kwamba Umar ibn Khatab aliwafunga jela Masahaba watatu hapo Madina

nao ni, Abud-dir-dai na ibn Mas-ud na Abu Masud Al-ansari kwa kosa la kunakili kwa wingi hadithi (za Mtume **s.a.w.w**). Pia Umar aliwaamuru Masahaba wamletee kila kitabu kilichomo mikononi mwao miongoni mwa vitabu vya hadithi, basi wao wakadhani kwamba yeye anataka kuvisahihisha viwe katika hali ambayo hapatakuwa na tofauti ndani yake, wakamletea vitabu vyao yeye akavichoma moto vyote. Kisha baada yake alikuja Uthman akaiunganisha sera yao kwa kuwatangazia watu wote kwamba "Si halali kwa mtu yeyote kueleza hadithi ambayo hakuisikia katika zama za Abubakr wala katika zama za Umar!!"

Baadaye ilifika zamu ya Muawiyah ibn Abi Sufiyan alipokalia cheo cha Ukhalifa, akapanda kwenye mimbar akasema, "Enyi watu ole wenu kusimulia hadithi toka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**, msisimulie isipokuwa zile hadithi zilizotajwa katika zama za Umar." Kwa hiyo basi hapana budi kwamba kuna siri ya kuzuwia hadithi alizozisema Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** (hasa) zile ambazo hazikubaliani na malengo ya zama hizo (za watawala hao), vinginevyo basi ni kwa nini hadithi za Mtume ziendelee kuzuwiwa kuandikwa kwa muda huu mrefu na isipatikane ruhusa ya kuziandika mpaka zama za Umar ibn Abdil-Aziz (r.a) ndipo ilipopatikana ruhusa ya kuziandika. Kwa mujibu wa maelezo yaliyotangulia kutokana na uchunguzi kuhusu maelezo halisi yaliyo bayana juu ya Ukhalifa, ambayo Mtume **(s.a.w.w)** aliyatangaza mbele ya ushuhuda wa watu wengi tunapata matokeo yanayomaanisha kwamba, Abubakr na Umar -walizuwia mapokezi ya hadithi kutoka kwa Mtume **(s.a.w.w)** kwa kuhofia kusambaa kwa maelezo hayo (ya Mtume kuhusu Ukhalifa) katika miji au katika vijiji vya jirani na yangewadhihirishia ukweli huo. Hapo kabla tumekwisha zungumza katika maudhui haya na tumeuweka wazi ukweli huu ndani ya kitabu chetu Liakuna Maas-Sadiqin, basi na arejee (kitabu hicho atakaye) ili kuong,eza uthibitisho.

La kushangaza miongoni mwa mambo ya Umar ibn Al-Khatab ni ile misimamo yake inayopingana hasa katika kila jambo linalohusiana na suala la Ukhalifa. Kuna wakati tunamkuta yeye ndiye aliyeisimamia baia ya Abubakar na akawalazimisha watu wautii (Ukhalifa huo) kwa nguvu, na akauhukumu kuwa eti ulitimia pasipo kutegemea bali Mwenyezi Mungu aliikinga shari yake. Wakati mwingine (tunamkuta Umar) anateua watu sita kwa ajili ya Ukhalifa anasema, "Lau watamtawalisha Alah (akiwa na maana ya Ali ibn Abi Talib) basi atawaongoza kwenye njia ya sawa." Basi maadam (Umar) anakiri kwamba Ali ndiye mtu pekee ambaye atawapeleka watu kwenye haki, basi ni kwa nini hakumbainisha wazi wazi na mambo yakamilike na kwa ajili hiyo awe ametoa mchango mzuri kwa umma wa Muhammad? Lakini kinyume chake, tunamuona anajichanganya na kukipa uwezo mkono wa Abdur-rahman anaposema, "Lau Salim aliyeachwa huru na Abu Hudhaifah angekuwa hai ningemtawalisha juu yenu." Na la kushangaza zaidi kuliko yote katika mambo ya Abu Hafsah (Umar) ni kule kuzuwia kwake kuzungumzwa hadithi za Mtume **(s.a.w.w)** na kuwafunga Masahaba hapo Madina kwa kuwazuwia wasitoke nje ya mji huo, na pia kuwakataza wajumbe watokao kwake kwenda miji mingine wasiwazungumzie watu sunna ya Mtume, na (miongoni mwa aliyoyatenda)

ni kuvichoma moto vitabu vilivyokuwa mikononi mwa Masahaba ambavyo vinazungumzia hadithi za Mtume **(s.a.w.w)**.

Je, Umar ibn Khatab hakufahamu kwamba Sunna ya Mtume ndiyo inayobainisha Qur'an Tukufu? Je, hakusoma kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu aliposema:

وَأَنزَلْنَا إِلَيْكَ الذِّكْرَ لِتُبَيِّنَ لِلنَّاسِ مَا نُزِّلَ إِلَيْهِمْ ﴿٤٤﴾

"Na tumekuteremshia wewe ukumbusho (Qur'an) ili uwabainishie watu yale yaliyoteremshwa kwao." (Qur'an, 16:44).

Au (yeye Umar) alifahamu yaliyomo ndani ya Qur'an ambayo, Mtume **(s.a.w.w)** aliyeteremshiwa hiyo Qur'an hakuyafahamu? Mambo kama haya ndiyo wayatakayo watu waliochanganyikiwa ambao wanasema kwamba eti Qur'an mara nyingi ilikuwa ikishuka kuunga mkono maoni ya Umar, na iliyapinga maoni ya Mtume **(s.a.w.w)**. "Ni maneno mabaya yatokayo vinywani mwao, bila shaka hawana wanachokijua." Siku zote nilikuwa nikishangaa nisomapo ndani ya Bukhari juu ya upinzani wa Umar kutokubali riwaya za Ammar ibn Yasir hasa hasa ile ya mafunzo ya Mtume kwake (Ammar) juu ya nama ya kutayammamu. Kama ambavyo ninashangaa kutokana na kauli ya Ammar kwa kumuogopa Umar anasema, "Ukitaka sitaisimulia hadithi hiyo." Basi inabainika wazi kwamba Umar alikuwa mkali dhidi ya kila anayesimulia hadithi za Mtume na humtaabisha. Ikiwa Masahaba miongoni mwa Maquraishi wanamuogopa Khalifa huyo, kiasi kwamba hawatoki nje ya Madina na wakitoka hawanakili (na kusimulia) hadithi za Mtume, kisha Khalifa huyo anavichoma vitabu vyao ambavyo ndani yake walikusanya hadithi (za Mtume) na pasiwepo mtu hata mmoja wa kusema kitu (kutokana na tendo hilo), basi Ammar ibn Yasir ana thamani gani? Ni mgeni, mtoka mbali, na alikuwa akichukiza mbele ya Maquraishi kwa kusimama kwake pamoja na Ali ibn Abi Talib na kumpenda kwake Ali ibn Abi Talib (a.s)?

Tunaporudi kidogo kwenye uchunguzi (wa Mas-ala yanayostaabisha), na hasa ile siku ya Al-Khamisi ambayo ilikuwa kabla ya kufariki kwa Mtume **(s.a.w.w)** na siku hiyo ndiyo ile ambayo Ibn Abbas ameiita kuwa ni "Siku ya Msiba". Ameiita hivyo kwa sababu, wakati Mtume **(s.a.w.w)** alipowaamuru waliokuwepo mbele yake wamletee karatasi na kidau cha wino ili awaandikie maandiko ambayo kwayo kamwe hawatapotea, tunaona katika siku hiyo Umar ibn Khatab ndiye aliyempinga Mtume **(s.a.w.w)** na kumtuhumu kwamba "Anaweweseka" Mungu apishe mbali. Na akasema yeye Umar "Kinatutosha kitabu cha Mwenyezi Mungu." Tukio hili ameliandika Bukhari na Muslim, ibn Majah, An-Nasai, Abu Dawud na Imam Ahmad na wengineo miongoni mwa wana historia wengi. Sasa basi, iwapo Umar anathubutu kumzuwiya Mtume wa Mwenyezi Mungu asiandike hadithi zake mbele ya watu wengi wakiwemo Masahaba na watu wa nyumba ya Mtume na kumtuhumu kuwa anaweweseka, na kisha (kuonesha) ushupavu huo ambao historia haijapata kutambua mfano wake, basi hiyo haishangazi na wala siyo ajabu kwa Umar ibn Khatab kuendelea tena kwa nguvu baada ya kufariki Mtume **(s.a.w.w)** kuwazuwiya watu kunakili hadithi za Mtume **(s.a.w.w)** kwa juhudi zake zote hali ya kuwa ni Khalifa mwenye nguvu na anamiliki uwezo, na hapana shaka kwamba alikuwa nao wasaidizi miongoni mwa Masahaba wengi ambao wanao

uwezo katika makabila na jamaa wa kutosha, na ni katika wale ambao walimfuata Mtume kwa sababu ya tamaa au khofu au unafiki, tumekwisha waona hawa kutokana na wingi wao wanaunga mkono ile kauli ya Umar eti kwamba Mtume anaweweseka, walishiriki kumzuia Mtume **(s.a.w.w)** kuandika maandiko yake.

Mimi naamini kwamba hiyo ndiyo iliyokuwa sababu ya msingi kwa Mtume kunyamaza asiandike maandiko hayo kwani yeye alifahamu kwa kupitia Wahyi kutoka kwa Mola wake kwamba, kuna njama zenye nguvu na huenda zitatishia ukamilifu wa malengo ya Uislamu iwapo maandiko hayo yataandikwa. Maandiko hayo aliyotaka kuyaandika Mtume **(s.a.w.w)** yalikuwa na lengo la kuulinda Umma wake usiingie katika upotevu, lakini kumbe walikuwepo wenye njama (dhidi yake) wakageuza lengo (lililokusudiwa) na ikawa kama kwamba maandiko hayo yakiandikwa itakuwa ni sababu ya kupotea na kuacha Uislamu. Basi ni kwa nini Mtume wa Mwenyezi Mungu asibadilishe (hivyo alivyotaka kuandika yaani akaacha kuandika) na wakati yeye yuko katika hali hiyo ya maradhi juu ya kitanda cha mauti (akaacha kuandika) kutokana na Wahyi toka kwa Mola wake, Wahyi ambao unasikika katika masikio yake, na kuujaza moyo wake masikitiko na huzuni juu ya Umma wake ambao umefikwa na kauli yake (Mwenyezi Mungu). "Basi ikiwa (Muhammad) atakufa au atauawa mtarudi nyuma kwa visigino vyenu?" Hii aya haikushuka bure bure tu bali ni matokeo ya kweli ambayo Mwenyezi Mungu alikwishafahamu uovu wao na magenge yao na vitimbi vyao. Mwenyezi Mungu yeye ndiye anayefahamu hiana ya macho na yale yaliyojificha katika nyoyo.............. Bali Mwenyezi Mungu amemwambia Mtume wake toka hapo mwanzo kama ifuatavyo:

وَيَوْمَ يَعَضُّ الظَّالِمُ عَلَىٰ يَدَيْهِ يَقُولُ يَا لَيْتَنِي اتَّخَذْتُ مَعَ الرَّسُولِ سَبِيلًا ﴿٢٧﴾ يَا وَيْلَتَىٰ لَيْتَنِي لَمْ أَتَّخِذْ فُلَانًا خَلِيلًا ﴿٢٨﴾ لَّقَدْ أَضَلَّنِي عَنِ الذِّكْرِ بَعْدَ إِذْ جَاءَنِي وَكَانَ الشَّيْطَانُ لِلْإِنسَانِ خَذُولًا ﴿٢٩﴾ وَقَالَ الرَّسُولُ يَا رَبِّ إِنَّ قَوْمِي اتَّخَذُوا هَٰذَا الْقُرْآنَ مَهْجُورًا ﴿٣٠﴾ وَكَذَٰلِكَ جَعَلْنَا لِكُلِّ نَبِيٍّ عَدُوًّا مِّنَ الْمُجْرِمِينَ وَكَفَىٰ بِرَبِّكَ هَادِيًا وَنَصِيرًا ﴿٣١﴾

"Na siku ambayo dhalimu atajiuma mikono yake na huku anasema; Laiti ningelishika njia pamoja na Mtume, Ee Mola wangu! Laiti nisingelimfanya fulani kuwa rafiki, amenipoteza nikaacha ukumbusho baada ya kunifikia na kweli shetani ni mwenye hiana kwa mwanadamu. Na Mtume alikuwa akisema: Ewe Mola wangu! hakika watu wangu wameifanya hii Qur'ani ni kitu kilichohamwa, na vivi hivi tumemfanyia kila Nabii adui miongoni mwa waovu na Mola wako mlezi anatosha kuwa mwenye kuongoa na mwenye kunusuru." (Qur'an, 25, 27-31).

Jambo ambalo hatuwezi kulikwepa katika uchunguzi huu ni hayo matokeo yenye uchungu tuliyoyafikia, nayo ni kwamba Abu Sufiyani na Muawiyah wasingekuwa wajeuri dhidi ya Mtume **(s.a.w.w)** lau si msimamo wa Umari wa kijeuri aliokuwa akiufanya mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu hasa tunapouchunguza mwenendo wake muda wote wa uhai wa Mtume **(s.a.w.w)** na upinzani wake aliokuwa akiuonesha katika matukio mbali mbali. Kwa hali hii hatuna budi kupata matokeo yanayomaanisha kwamba, kulikuwa na njama kubwa zilizoandaliwa ili kuudhalilisha utu wa Mtume Mtukufu na kumtia doa, pia kumfanya aonekane mbele ya watu

wasiomfahamu kwamba yeye ni mtu wa kawaida tu au chini kuliko hapo na kwamba yeye wakati mwingine anatawaliwa na ubinafsi na matamanio yake yanampotosha na kumtoa kwenye haki. Yote hayo lengo lake ni kuwapotosha watu wamuone kwamba yeye siyo Maasumu (yani hakuhifadhika kutokana na madhambi).

Dalili ya hilo ni kwamba Umar amempinga Mtume mara nyingi na eti Qur'ani ikaja kumuunga mkono Umar mpaka ikafikia Mwenyezi Mungu kumkemea Mtume wake naye Mtume akalia na kusema:"Lau Mwenyezi Mungu angelituteremshia maangamizo basi asingeokoka kutokana na maangamizo hayo isipokuwa mwana wa Khatab (yaani Umar) Tukio hili linahusu mateka wa Badri. Au kama isemwavyo kwamba, Umar alikuwa akimwamuru Mtume wa Mwenyezi Mungu kuwaweka wake zake kwenye hijabu, wakati Mtume alikuwa hafanyi hivyo mpaka Qur'an ikamuunga mkono Umar na kumwamrisha Mtume wa Mwenyezi Mungu awaweke wake zake kwenye hijab. Au kama isemwavyo kwamba shetani hakumuogopa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu lakini alimwogopa Umar na kumkimbia na mengineyo miongoni mwa riwaya potofu zinazoangusha heshima ya Mtume **(s.a.w.w)** na kupandisha juu heshima ya Masahaba. Kwa hakika Umar alifanikiwa mno katika lengo lake hili mpaka watu wamesimulia (Mwenyezi Mungu awafedheheshe watu hao) Eti wanasema kwamba; mjumbe wa Mwenyezi Mungu alikuwa akiutilia mashaka utume wake na hilo limo ndani ya hadithi wanayoisimulia isemayo kuwa, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amesema: "**Jibril alikawia kuja kwangu mpaka nikadhani kwamba yeye sasa atashuka kwa Umar bin Khatab.**"

Mimi naamini kwamba hadithi kama hizi na nyingine mfano wa hizi, ziliwekwa katika zama za Muawiyah ibn Abu Sufiyan aliposhindwa kufuta ukweli unaomhusu (fadhila za) Ali ibn Abi Talib akaona azushe fadhila za Abubakr, Umar na Othman ili anyanyue zaidi daraja zao mbele ya macho ya watu kuliko daraja ya Ali, na alilifanya hilo kwa malengo mawili:

1) Ni kuirudisha chini heshima ya Ali ibn Abi Talib (Abu Turab) kama alivyomwita yeye ili kuwapotosha watu na kuwafanya Makhalifa watatu waliomtangulia kuwa wao ni bora zaidi kuliko yeye.

Lengo la pili la kuzua kwake hadithi ilikuwa ni kuwafanya watu wakubali kinyume na maamrisho ya mjumbe wa Mwenyezi Mungu na usia wake unaohusu suala la Ukhalifa ambao ni haki ya watu wa nyumba ya Mtume, hususan Hassan na Husein ambao waliishi katika kipindi cha Muawiyah. Basi ilipokuwa imewezekana kwa Makhalifa watatu wa mwanzo kwenda kinyume na maamrisho ya Mtume kuhusu (ukhalifa wa) Ali je, ni kwa nini isiwezekane Muawiyah ambaye ni wanne wao naye asiweze kwenda kinyume na maamrisho ya Mtume juu ya watoto wa Ali? Kwa hakika mwana wa Hindu (Muawiyah) amefanikiwa sana katika mipango yake, na dalili (ya mafanikio yake) ni kuwa leo hii sisi tunapozungumzia elimu ya Ali (a.s) na ushujaa wake na udugu alionao kwa Mtume na ubora na fadhila zake kwa Uislamu na Waislamu, basi mbele yetu husimama mtu ambaye husema, "Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema, Lau itapimwa imani ya umma wangu kulinganisha na imani ya Abubakr basi imani ya Abubakr itakuwa nzito." Na mwingine naye atatuambia, "Umar Al-Faruq ndiye aliyetenganisha baina ya haki na batili".

Na mwingine naye atasimama mbele na kutuambia, "Uthman Dhun-Nurain ndiye ambaye Malaika wa Mwenyezi Mungu walimstahi."

Yeyote mwenye kufuatilia uchunguzi huu atakuta kwamba, Umar ibn Al-Khatab amechukua nafasi ya simba katika mlango wa ubora, na hayo hayakuja ghafla bali ni kutokana na misimamo yake ya upinzani wa mara kwa mara dhidi ya Mtume **(s.a.w.w)**. Maquraish walimpenda na hasa kwa mchezo alioucheza katika kumtweza Amirul-Muuminina na Bwana wa Mawasii Ali ibn Abi Talib kwa kumnyang'anya Ukhalifa, na kuwapa Maqureish walitolee uamuzi vile wapendavyo kiasi cha kupupiwa na waachwa huru na waliolaniwa miongoni mwa Bani Umayyah, na hapana shaka Maquraish wote wakiongozwa na Abubakr wanafahamu kwamba shukurani zote zinarejea kwa Umar katika kuwatawalisha wao juu ya Waislamu. Hivyo basi Umar ndiye shujaa wa upinzani dhidi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu na ndiye aliyemzuwia Mtume wa Mwenyezi Mungu asimuandikie Ali usia wa Ukhalifa, na ni yeye aliyewakemea watu na kuwatia shaka juu ya kifo cha Mtume wao ili wasije kumtangulia kwa kumpa baia Ali. Si hivyo tu bali Umar ndiye shujaa wa Saqifa aliyethibitisha baia ya Abubakr na huyo huyo Umar aliyewaonya wale waliopinga (Baia ya Abubakr) na wakajizuwia ndani ya nyumba ya Ali (akawaonya) kwa kwaambia kwamba, "Ataiunguza nyumba hiyo na waliomo ndani, ikiwa tu hawatatoka kwenda kula kiapo cha utii kwa Abubakr". Ni yeye pia aliyewalazimisha watu wampe baia Abubakr kwa nguvu na shinikizo, na ndiye ambaye alikuwa akiteua magavana na kuwapa vyeo wakati wa Ukhalifa wa Abubakr, bali hatutakuwa tumetia chumvi tutakaposema kwamba yeye ndiye alikuwa mtawala mtendaji hata katika Ukhalifa wa Abubakr mwenyewe. Wanahistoria wamesimulia kwamba, wenye kuimarishwa imani zao katika dini (Muallafatul-Qulubi) walipomjia Abubakar ili wachukue sehemu yao ambayo Mwenyezi Mungu ameifaradhisha kwa ajili yao kufuatana na mazowea waliyokuwa nayo wakati wa Mtume **(s.a.w.w)**, Abubakar aliwaandikia barua juu ya jambo hilo wakaenda kwa Umar ili wakapokee (sehemu hiyo) kutoka kwake, basi (Umar) akaichana barua hiyo na akasema, "Hatuna haja nanyi kwani Mwenyezi Mungu amekwisha uimarisha Uislamu na hana haja nanyi, kwa hiyo mkislimu (mtasalimika) vinginevyo upanga ndiyo utakaoamua baina yetu na ninyi".

Watu hao walirudi kwa Abubakr wakamwambia, "Hivi wewe ndiyo Khalifa au yeye? Akasema: "Bali ni yeye apendapo Mwenyezi Mungu". Kisha akayapitisha aliyoyaamua Umar. Na mara nyingine Abubakar aliwaandikia barua Masahaba wawili (kuwapa) sehemu ya ardhi na akaituma barua hiyo kwa Umar ili aipitishe, Umar akaitemea mate na kuifuta, wale wakamshutumu na wakarudi kwa Abubakar huku wanalaumu na wakamwambia Abubakar "Sisi hatufahamu, hivi wewe ndiyo Khalifa au Umar?" Abubakar akasema, "Ni yeye." Baadaye Umar alikuja hali amemkasirikia Abubakar na akamwambia, "Huna haki ya kuwapa ardhi hawa." Abubakr akamwambia Umar, "Hakika nilikwisha kuambia kwamba wewe ndiwe mwenye nguvu kuliko mimi juu ya jambo hili hakika wewe umenishinda nguvu." Mpaka hapa inatubainikia siri ya cheo alichokuwanacho Umar ibn Khatab mbele ya Maquraish wote na mbele ya

Bani Umayyah kwa upande wao, kiasi kwamba wamemuita shujaa na mwenye kupata Il-Ham na kuwa ndiyo Faaruq na muadilifu bila mipaka hadi wakamboresha juu mno kuliko hata Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**. Bila shaka tumekwishaona itikadi ya Umar juu ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** kuanzia siku ya mapatano ya Hudaibiyah hadi siku ya msiba (wa siku ya Al-Khamisi) basi ongeza juu ya hayo kwamba, yeye aliwazuwia Masahaba kutabaruku kwa athari za Mtume wa Mwenyezi Mungu, akaukata mti wa Baiyatur- Ridh-wan, kama ambavyo alitawasali kupitia kwa Abbas ambaye ni ammi yake Mtume **(s.a.w.w)** ili awaoneshe watu kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu alikwisha kufa na mambo yake yamemalizika hakuna faida hata kumkumbuka. Basi hapana lawama juu ya Mawahabi wasemao maneno kama haya, kwani siyo maneno mapya kama baadhi ya watu wanavyodhani. Mpaka hapa (utaona) mlango umefunguliwa kwa maadui wa Uislamu na Mustashrikina "Orientalists" ili waone kuwa Muhammad alikuwa mtu hodari tu, aliyewafahamu watu wake kuwa ni waabudu sanamu wamelelewa ndani ya ibada ya Masanamu, basi akawaondolea masanamu na kuwabadilishia jiwe jeusi (Hajarul-As-Wad).

Baada ya yote haya tunamuona Umar kuwa ndiyo shujaa wa kupinga kuandikwa kwa hadithi za Mtume kiasi kwamba anawafunga Masahaba hapo Madina na wengine anawazuwia kusimulia hadithi na anavichoma moto vitabu vya hadithi kwa pupa yake kwamba Sunna ya Mtume isije ikasambaa miongoni mwa watu. Kadhalika kwa kupitia hali hiyo tunafahamu kwamba ni kwa nini Imamu Ali (a.s) alibakia nyumbani (mwake) hatoki ila pale anapoitwa kwenda kutatua swali gumu lililowashinda Masahaba, na wala Umar hakumshirikisha Imamu Ali (a.s) katika madaraka wala utawala na hata katika majukumu ya kutuma ujumbe (wala jeshi) na alizuwiwa hata mirathi ya bibi Fatma (a.s) na akawa hana cho chote ambacho kingewafanya watu wawe na hamu naye, na kwa ajili hiyo basi, wanahistoria wanataja kuwa alilazimika kutoa baia baada ya mauti ya bi Fatma (a.s) baada ya kuwaona watu wamempuuza. Ni kwa nini watu wasikubughudhi (ewe Ali) hali ya kuwa uliwauwa mashujaa wao (wa kikafiri) na ukausambaratisha umoja wao, ukazibomoa ndoto zao, na hukuwaachia heshima yo yote katika jamii yao wala hukuwachia chochote katika nyanja za wema. Pamoja na yote hayo wewe ndiye mwana wa ammi ya mteule wa Mwenyezi Mungu na mtu wa karibu mno kwake, nawe ndiye mume wa Fatma (binti yake Mtume ambaye ni) mwanamke bora kuliko wanawake wote ulimwenguni pia (wewe) ni baba wa wajukuu wawili (wa Mtume) mabwana wa vijana wa peponi, isitoshe wewe ndiwe wa mwanzo wao kusilimu na mwenye elimu nyingi kuliko (Masahaba) wote.

Si hivyo tu bali ammi yako Hamza ndiye bwana wa mashahidi, na Jaafar At-tayyar ni nduguyo kwa baba na mama, pia baba yako ndiye mlezi wa Mtume **(s.a.w.w)**, kadhalika Maimamu waliobarikiwa wote wanatokana na kizazi chako. Umewatangulia.wenye kutangulia na umewazidi waliodhaniwa kuwa wao ndiyo, ulikuwa ni simba wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake na ulikuwa ndiyo upanga wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake **(s.a.w.w)**, na uliaminiwa na Mwenyezi Mungu na Mtume wake **(s.a.w.w)** uende ukaifikishe Suratul-baraa, kwani hakuaminiwa mwingine (kuipeleka sura hiyo) asiyekuwa wewe. Wewe ulikuwa ndiyo Sid-diqul-

Akbar, hawezi kudai sifa hiyo mtu mwingine baada yako ila atakuwa ni muongo, kama ambavyo wewe ndiyo yule Faruqul-Akbar ambaye huiweka haki mahali pake, na kisha haki hiyo ikafahamika kutoka katikati ya rundo la batili. Ni wewe ambaye ulikuwa ndiyo elimu iliyo wazi na minara inayong'ara, hufahamika kwa akupendaye imani ya muumini na kwa yule anayekubughi (hufahamika) unafiki wa munafik. Wewe ndiyo mlango wa mji wa elimu, mwenye kukujia ataufikia mji huo, hivyo basi hapana shaka kwamba, yeyote atakayedai kuingia mjini kupitia kwa asiyekuwa huyo ni muongo. Je, ni nani miongoni mwao anayo hisa mfano wa hisa uliyonayo wewe ewe Abul-hasan, na ni nani miongoni mwao ana ubora kama ubora wako ndiyo dalili? Kwa hiyo, iwapo utukufu unachokitambulisho hapana shaka wewe ndicho kitambulisho chake, kwani ubora wako uko kwenye ngazi ya juu. Bila shaka walikuhusudu kwa yale aliyokujaalia Mwenyezi Mungu miongoni mwa fadhila zake, na kwa hakika walikutenga wakati Mwenyezi Mungu alipokuhusisha kuwa karibu naye. Basi watafahamu wale waliodhulumu ni mgeuko gani watakaogeuka(siku hiyo).

Sasa hivi kalamu imetusogeza karibu ili tuweze kuzungumza na Amirul-Muuminina (Ali ibn Abitalib) aliyedhulumiwa akiwa hai au amekufa ambaye ni kiigizo chema kwa nduguye Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** kwani naye ni mwenye kudhulumiwa akiwa hai au amekufa, kutokana na yeye kuyamaliza maisha yake ya Utume hali akipigana jihadi na kuunasihi (umma), huku akiwahangaikia waumini, alikuwa mpole kwao tena mwenye huruma. (Lakini katika hao), wako waliomkabili kwa maneno machafu katika ile saa ya mwisho (wa uhai wake) wakamtuhumu kuwa anaweweseka na wakamjibu majibu yaliyomchukiza walipomuasi na kumpinga wakati alipompa uongozi wa jeshi Usama, si hivyo tu bali wakakimbilia Saqifa kwa ajili ya (kugombea) Ukhalifa na wakauacha mwili wa Mtume (alipofariki) na wala hawakujishughulisha na maandalizi ya kumkosha Mtume wala kumvalisha sanda. Baada ya kufariki kwake Mtume **(s.a.w.w)** walimfanyia mambo ya kumdhalilisha mbele za watu na kuiporomosha heshima yake pia kumuondolea "Isma" ambayo Qur'an na hali halisi vinashuhudia yote hayo, (na walifanya) haya yote kwa ajili ya kutafuta utawala usiodumu na dunia yenye kutoweka. Kwa hiyo basi, kwa kupitia utafiti huu, tumeufahamu msimamo wa baadhi ya masahaba dhidi ya utukufu wa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** katika lengo lao la kuufikia Ukhalifa.

Bila shaka watawala wa Bani Umayyah wakiongozwa na Muawiyyah ibn Abi Sufiyan, wao waliupata Ukhalifa kwa kurithiana na wakaimarika kwa Ukhalifa huo na wala yeyote miongoni mwao hakupata kufikiri kwamba siku moja Ukhalifa utawatoka. Sasa basi ni kwa nini Banu Umayyah waliendelea kuitweza heshima ya Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** na kuzua riwaya za kuporomosha cheo chake? Mimi ninaamini kuwa, kuna sababu mbili za msingi nazo nihizi zfuatazo: Sababu ya Kwanza: Bila shaka lengo la kuitweza heshima ya Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** ilikuwa ni kuwadhalilisha Bani Hashim ambao walikuwa wamejipatia heshima na utukufu miongoni mwa makabila ya Kiarabu kwa kupatikana Nabii anayetokana na Bani Hashim, hususani pale tunapofahamu ya kwamba Umayyah (Babu wa Bani Umayyah) alikuwa akishindana na

nduguye Hashim (Babu wa Bani Hashim), na (huyu Umayyah) akimhusudu (Hashim) kwa kufanya kila mbinu ili amuuwe. Ongeza zaidi ya hilo ni kwamba, Ali (a.s) ndiye Bwana wa Bani Hashim baada ya Mtume **(s.a.w.w)** bila kupingwa, na Waislamu wa pande zote wanafahamu kero ya Muawiyah dhidi ya Ali (a.s) na vita alivyopigana (Muawiyah) dhidi ya Ali ili amnyang'anye Ukhalifa. Na baada ya Ali kuuawa Muawiyyah akaendelea kumtukana na kumlaani Ali juu ya mimbari (misikitini), kwa hiyo ili kumuondolea Mtume **(s.a.w.w)** heshima yake, kwa mujibu wa imani ya Muawiyah ilikuwa ni, kwanza aiangushe heshima ya Ali kama ukweli wenyewe ulivyo ya kuwa, kumtukana na kumlaani Ali ni kuelekeza (matusi na laana) kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**.

Sababu ya Pili: Bila shaka kuivunja heshima ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ndani yake iko namna inayowatakasa watawala wa Banu Umayyah kutokana na matendo ya aibu na maovu waliyokuwa wakiyatenda kama yalivyoandikwa katika historia (na kueleza namna walivyokuwa). Iwapo Mtume wa Mwenyezi Mungu (kama wamtazamavyo wao Banu Umayyah) ni mtu mwenye kupenda mambo ya upuuzi na wanawake kiasi kwamba hali hiyo inampelekea kusahau wajibu wake, na (eti Mtume) alikuwa anampenda mmoja wa wanawake hao mpaka anafikia kushindwa kuwa muadilifu baina yao, nao (wakeze) wanamtumia ujumbe kumtaka afanye uadilifu. Baada ya yote hayo. watu wa kawaida (wasiokuwa Mitume) kama vile Muawiya na Yazid na wengine mfano wa hao hawana lawama (kwa kutenda hayo maovu waliyoyatenda). Ndani ya hii sababu ya pili, inajificha hatari ya kuwa Banu Umayyah walitengeneza hadithi nyingi zinazodaiwa kuwa zilisimuliwa kutoka kwa Mtume **(s.a.w.w)** ambazo zimekuwa miongoni mwa hukumu (za sheria) zinazotumika ndani ya Uislamu, na Waislamu wamezichukulia moja kwa moja kuwa ni miongoni mwa kauli na matendo ya Mtume **(s.a.w.w)** na zimekuwa ni sunna ya Mtume kwa Waislamu. Nitatoa baadhi ya mifano kuhusu hadithi hizo miongoni mwa hadithi chafu ambazo ziliwekwa ili kuudhalilisha Utukufu wa Mtume na kuangusha daraja yake, na wala sitaki kuifanya maudhui hii iwe pana, bali nitafupisha tu kwa yale waliyoyaandika Bukhari na Muslim katika vitabu vyao nazo ni hadithi zenye fedheha kwa lengo la kumuaibisha Mtume **(s.a.w.w)**.

1). Bukhari ameandika katika kitabul-Ghusli mlango usemao, Atakapojamii kisha akirudia, Amesema Anas, "Mtume alikuwa akiwazungukia wakeze usiku katika saa moja pia mchana na walikuwa kumi na moja. Akasema: Nikamwambia Anas: Je, alikuwa akiweza kufanya hivyo? Akasema: Tulikuwa tukizungumza kwamba yeye alipewa nguvu za watu thelathini". Hebu tuiangalie sote kwa pamoja hadithi hii yenye fedheha ewe msomaji, hadithi ambayo inatuonyesha kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** alikuwa katika hali ya uroho wa kujamii (kwa kiasi hiki), anawajamii wanawake kumi na moja kwa saa moja na anawajamii usiku na mchana tena kwa haraka namna hii kisha bila hata ya kukoga josho la jimai ya kwanza bali anamjamii mke wa pili akiwa na maji ya yule wa kwanza. Ni juu yako ewe msomaji upime na ufikiri itakuwaje mtu kumvamia mkewe kama mnyama bila kuwepo vitangulizi wala maandalizi, na tunashuhudia hata kwa wanyama kwamba suala la jimai huchukua muda mrefu na linahitaji vitangulizi na maandalizi, basi iweje kwa Mtume huyu Mtukufu

afanye kama hivyo (ilivyoelezwa ndani ya hadithi hiyo bila kuwepo maandalizi ya jimai n.k.)? Kwa hakika Mwenyezi Mungu awalaani (waliozuwa mambo haya dhidi ya Mtume) ni waongo tena wamepotea. Na kwa kuwa Waarabu katika zama hizo na wanaume (kwa jumla) walikuwa hawajaacha kujifakhirisha kwa nguvu za jimai na waliliona jambo hilo kuwa ni alama ya uanaume ndiyo maana waliweka kisa hiki dhidi ya Mtume **(s.a.w.w)**.

Kamwe Mtume hakutenda hayo, kwani yeye ndiye aliyesema kuwa "Musiwavamie wake zenu kama wanyama, wekeni mjumbe baina yenu na wao." Basi mfano wa riwaya kama hizi ndizo ambazo maadui wa Uislamu huzichukulia kuwa hoja dhidi ya Mtume **(s.a.w.w)** na kumuelezea kuwa yeye alikuwa mtu aliyezama katika mambo ya kijinsia, kujamiana na kupenda wanawake na tuhuma nyinginezo. Hebu tumuulize huyo Anas ibn Malik aliyekieleza kisa hiki. "Je, ni nani aliyemuambia kisa hicho? Ni nani aliyemjulisha kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** ana jamii wakeze kumi na moja kwa saa moja? Je, ni Mtume ndiye aliyemueleza jambo hilo? Na je, inakubalika kwa mmoja wetu kuwasimulia watu namna anavyomjamii mkewe? Au wakeze Mtume ndio waliokuambia hayo (ewe Anas)? Basi je, inakubalika kwa mwanamke Muislamu kuwaelezea wanaume namna anavyojamiiwa na mumewe? Au Anas yeye ndiye aliyempeleleza Mtume na kufuatilia faragha zake na wakeze na akachungulia kupitia matundu ya milango (akagundua hilo)? Namuomba Mwenyezi Mungu aniepushe na mawazo ya kishetani, na Mwenyezi Mungu awalaani wazushi hao. Mimi sina shaka kwamba watawala wa Banu Umayyah na Banu Abbas ambao ni mashuhuri kwa kuwa na wanawake na vijakazi wengi, wao ndiyo walioweka visa vyenye mfano kama huu ili kuhalalisha matendo yao (maovu).

2) Bukhari ameandika katika Sahihi yake ndani ya juzuu ya tatu ukurasa wa 132 na pia Muslim ndani ya Sahihi yake katika juzuu ya saba ukurasa wa 136 wamesema: "Bibi Aisha amesema, Wakeze Mtume **(s.a.w.w)** walimtuma Fatma binti ya Mtume **(s.a.w.w)** aende kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, alipofika akabisha hodi, na wakati huo Mtume alikuwa amelala pamoja nami ndani ya shuka yangu, Mtume akamkaribisha binti yake, Fatima akasema, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu hakika wakezo wamenituma kwako wanakutaka uwe muadilifu kutokana na (kuegama kwako upande) binti ya Abu Quhafa, wakati huo mimi nimenyamaza tu: bibi Aisha akasema: Mtume akamwambia bibi Fatma; Ewe binti yangu hukipendi nikipendacho mimi, bibi Fatma akasema kwa nini (nisikipende) Mtume akasema basi mpende huyu (Aisha).."

Kisha hadithi inaendelea na inasema, "Mpaka wakeze Mtume wakamtuma kwa mara ya pili bibi Zainab binti Jahshi ambaye ni mke wa Mtume, wakimuelekeza afanye uadilifu (kwa kuegama kwake) kwa binti ya Abu Quhafah (yaani Aisha) na akaingia kwa Mtume na hali Mtume kalala pamoja na Aisha na amejifunika shuka ya Aisha na akiwa katika mazingira kama yale aliyomkuta nayo bibi Fatma, basi akamtaka Mtume awe muadilifu kuhusu binti ya Abu Quhafah kwa niaba ya wakeze Mtume. Hatimaye (bibi Zainab) akamrukia bibi Aisha na kumtukana, naye bibi Aisha akajitetea nafsi yake akamtukana Zainab mpaka Mtume

akamnyamazisha na kisha Mtume akatabasamu na akasema: L'Bila shaka huyo ndiye binti Abubakr." Nasikitika sana kusema kwamba, hadithi hizi chafu ambazo zinamfanya Mtume wa Mwenyezi Mungu kuonekana kuwa ni mtu anayefuata matamanio ya nafsi yake na hana uadilifu baina ya wakeze, wakati ambapo Qur'an iliyokuja kwa kupitia ulimi wake inasema "Na mkichelea kuwa hamtafanya uadilifu basi mke mmoja anatosha, au wekeni wajakazi ambao mikonoyenu ya kuume imewamiliki". Itakuwaje basi Mtume **(s.a.w.w)** amkaribishe binti yake ambaye ni mwanamke bora kuliko wanawake wote aingie (chumbani) kwake na Mtume yuko katika hali ile amelala na mkewe na amejifunika shuka ya mkewe, na Mtume asinyanyuke akakaa au kusimama bali anabaki kalala hata amwambie, "Ewe binti yangu hukipendi nikipendacho?" Pia wakati mkewe Zainab anapoingia na kumtaka awe muadilifu (matokeo yake) Mtume anatabasamu na kusema: "Bila shaka huyo ndiyo binti Abubakr."

Ewe msomaji mpendwa hebu iangalie fedheha hii wanayomsingizia Mtume wa Mwenyezi Mungu ambaye ni kiigizo chema kwa uadilifu na usawa, na wakati huo huo wanasema eti uadilifu ulitoweka alipokufa Umar ibn Khattab na wanamfanya Mtume wa Mwenyezi Mungu kuwa ni mtu asiyejali tabia njema, hafahamu jambo la aibu ni lipi wala utu ni kitu gani. Kuna hadithi nyingi mno ndani ya vitabu vya Kisunni, mfano wa hii (iliyotangulia) ambazo makusudio ya wapokezi wake kwa undani ni kuonyesha ubora wa Sahaba au bibi Aisha mwenyewe kwa kuwa tu yeye ni binti ya Abubakr, na kwa hali hii wanamdhalilisha Mtume hali ya kuwa wanajua au hawajui. Na kama ilivyotangulia ndani ya uchunguzi (huu) kwamba hadithi hizi zimewekwa ili kuaibisha utukufu wa Mtume **(s.a.w.w)**. Sasa hebu itazame hadithi ya tatu inayofanana na hii (iliyotangulia).

3) Muslim ndani ya kitabu chake katika mlango unaohusu fadhila za Uthman ibn Affan ameandika hadithi toka kwa Aisha mkewe Mtume **(s.a.w.w)** na yeye Uthman, wawili hawa wameeleza kwamba, Abubakr alibisha hodi nyumbani kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** na hali Mtume kalala kitandani kwake amejifunika shuka ya Aisha, Mtume akamkaribisha Abubakar na Mtume akabakia kama alivyokuwa na akamtekelezea Abubakr shida yake (iliyomleta) kisha akaondoka, halafu Umar alibisha hodi na Mtume akamkaribisha hali ya kuwa katika hali ile ile ya mwanzo na akamtimizia shida yake akaondoka, Uthman akasema; hatimaye nilibisha hodi mimi basi Mtume akakaa na akamwambia Aisha; jifunike nguo zako, mimi nikamaliza shida yangu kwa Mtume kisha nikaondoka, Aisha akasema, Ewe Mtume wa Mwenyezi mungu mbona sikukuona ukibabaika (walipoingia) Abubakr na Umar (r.a) kama ulivyobabaika kwa Uthman? Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema, bila shaka Uthman ni mtu mwenye haya nami nilichelea lau ningemkaribisha nikiwa katika hali ile asingenifikishia shida yake". Hadithi hii inafanana na hadithi nyingine iliyo andikwa na Bukhari na Muslim kuhusu fadhila za Uthman ibn Affan na inaeleza kwamba, "Mapaja ya Mtume wa Mwenyezi Mungu yalikuwa wazi bila nguo, mara akabisha hodi Abubakr, Mtume hakuyafunika mapaja yake na ndivyo alivyofanya alipoingia Umar, hatimaye alipobisha hodi Uthman, Mtume akayafunika mapaja yake na kuziweka vizuri nguo zake, bibi Aisha alipomuuliza Mtume juu ya jambo

hilo, Mtume akamwambia Aisha, kwa nini nisimstahi mtu Malaika wa Mwenyezi Mungu wanamstahi?"

Mwenyezi Mungu awalaani Banu Umayyah ambao wamemdhalilisha Mtume wa Mwenyezi Mungu ili wamtukuze bwana wao.

4) Muslim ameandika ndani ya sahih yake katika mlango wa Wujubul-Ghusli Bil-tiqail-khitaanain, kwamba imepokewa kutoka kwa bibi Aisha mke wa Mtume **(s.a.w.w)** amesema: "Kuna mtu mmoja alimuuliza Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** kuhusu mtu aliyemuingilia mkewe kisha akakidhi haja yake, je, wote wawili wanawajibika kukoga (wakati swali linaulizwa) bibi Aisha alikuwa kakaa (hapo anasikiliza), basi Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema, "Hakika Mimi na huyu (Aisha) huwa tunafanya hivyo kisha tunakoga." Nakuachia wewe ewe msomaji uichunguze mwenyewe hadithi hii, hivi ni kweli ilifikia kiasi cha Mtume kumpenda mkewe Aisha akawa anasimulia namna ya jimai yake kwa watu mahsusi na kwa kila mtu? Kuna hadithi chungu nzima za Aisha binti Abubakr kama hizi ambazo ndani yake zinagusa heshima ya Mtume na kuiangusha thamani yake, kwani mara nyingine anaeleza kwamba Mtume alikuwa akiweka shavu lake juu ya shavu la (Aisha) ili achungulie ngoma inayochezwa na Msudani (yaani mtu mweusi). Na mara nyingine (Mtume) humbeba begani kwake, na wakati mwingine hushindana naye na Aisha humshinda Mtume kisha Mtume anasubiri mpaka Aisha aliponenepa ndipo alipomshinda na hatimaye akasema: "Ushindi huu niliokushinda ni kwa zile mara mbili ulizonishinda". Na kuna wakati mwingine Mtume alilala chali huku wanawake wakipiga madufu na zumari za shetani nyumbani kwake na Abubakr akawakaripia. Zipo hadithi chungu nzima zenye mambo ya aibu mfano wa hizi ambazo hazina lengo isipokuwa kumuabisha Mtume wa Uislamu. Kwa mfano hadithi isemayo kwamba, Mtume **(s.a.w.w)** alifanyiwa uchawi kiasi kwamba akawa hajui akifanyacho wala akisemacho mpaka akawa anadhani kwamba anawaendea wakeze wakati hawaendei" na kama riwaya zisemazo kuwa Mtume **(s.a.w.w)** alikuwa akiamka na janaba mwezi wa Ramadhani na kwamba hulala Mtume mpaka anakoroma usingizini kisha husimama akaswali bila kutawadha. Mtume huwa anasahau ndani ya sala yake kiasi kwamba hajui ni rakaa ngapi ameswali na Mtume wa Mwenyezi Mungu hafahamu nini hatima yake siku ya Qiyama na atafanyiwa nini na kwamba yeye Mtume alikuwa akikojoa wima na Sahaba anasogea mbali kisha Mtume humwita Sahaba huyo asogee karibu mpaka amalize kukojoa. Naam (miongoni mwa hadithi hizo) kutoka kwa mkewe Aisha binti Abubakr zimefikia hatua mbaya ya kumdhalilisha Mtume wa Mwenyezi Mungu eti kwamba yeye alijizuwia nafsi yake mwenyewe na akawazuwia Waislamu waliokuwa pamoja naye ili watafute mkufu wa mwana Aisha, ulimpotea na (Waislamu) wakiwa hawana maji mpaka ikabidi watu wamshitaki Aisha kwa Abubakr, ikamlazimu baba yake Aisha aje kumkemea Aisha na kumlaumu na wakati yote haya yanatendeka Mtume amelala usingizi mapajani kwa mkewe. Hebu isome riwaya hii kwa urefu.

Bukhari ameandika ndani ya Sahihi yake katika Babut-tayamum, na Muslim naye vile vile kaandika ndani ya Sahih yake katika Babut-tayammum imeelezwa toka kwa bibi Aisha kwamba yeye amesema, "Tulitoka pamoja na Mtume **(s.a.w.w)** katika baadhi ya safari zake hata

tulipofika jangwani pasipo maji mkufu wangu ulikatika, Mtume wa Mwenyezi Mungu akasimama kuutafuta, watu wote wakasimama pamoja naye na walikuwa sehemu isiyo na maji na hawana (akiba ya) maji, basi watu wakamjia Abubakr wakasema: Je, huyaoni aliyoyafanya Aisha, amemsimamisha Mtume wa Mwenyezi Mungu na watu alionao hali ya kuwa wapo mahala pasipo na maji na wala wao hawana (akiba ya) maji. Basi Abubakr akaja na (akamkuta) Mtume wa Mwenyezi Mungu ameweka kichwa chake mapajani mwangu amelala akasema, Umemzuwia Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** hali ya kuwa watu wako mahala pasipo na maji na hawana maji? Bibi Aisha anasema, Abubakr akanikemea na akasema aliyoyataka Mwenyezi Mungu ayaseme kiasi kwamba akawa ananichokoa kiunoni nami sikujizuia kutikisika isipokuwa mahala alipolala mjumbe wa Mwenyezi Mungu (yaani) mapajani mwangu. Basi Mtume alilala mpaka asubuhi bila ya maji na ndipo Mwenyezi Mungu alipoteremsha aya ya kutayammam. Usaid ibn Al-Hudhair ambaye ni miongoni mwa watu wenye haiba akasema, Hii siyo baraka yenu ya kwanza enyi kizazi cha Abubakr. Aisha akasema tukaagiza (aletwe) yule ngamia niliyekuwa nimepanda tukaukuta mkufu chini yake." Basi hivi kweli muumini anayeufahamu Uislamu ataamini kwamba Mtume **(s.a.w.w)** anapuuza jambo la Sala kwa kiwango hiki, na anawazuwia Waislam hali ya kuwa hawako mahala penye maji na hawana maji na yote hayo kwa ajili ya kutafuta mkufu wa mkewe ambao umempotea? Si hivyo awaache Waislamu wanasikitikia kupotea (kwa wakati wa) Sala na (hatimaye) wamshitakie kwa Abubakr na katika kipindi hicho hicho Mtume amekwenda kulala mapajani kwa mkewe na usingizi umemkolea hata asitambue kuja kwa Abubakr na kumkemea Aisha na kumchokoa kiunoni? Basi vipi itawezekana kwa Mtume huyu kuwaacha watu wakihangaika kwa ajili ya kukaribia (ibada ya) Sala hali yeye amelala mapajani kwa mkewe?

Hapana shaka kwamba hadithi hizi zilizuliwa katika zama za Muawiya ibn Abi Sufiyan na kwa kweli hazina chimbuko lolote (ndani ya Uislamu), vinginevyo basi tutalieleza namna gani tukio kama hili ambalo lilihudhuriwa na masahaba wengi na Umar akawa halijui tukio hili wakati alipoulizwa namna ya kutayammam, kama walivyoandika Bukhari na Muslim ndani ya vitabu vyao katika mlango wa kutayammam? Jambo muhimu katika utafiti wote huu ni kutaka kufahamu kwamba njama dhidi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** zilikuwa ni njama mbaya na chafu zinazotumika kumuaibisha na kuporomosha hadhi yake mpaka kufikia kiwango cha mmoja wetu leo hii hawezi kuridhia binafsi yake aonekane kuwa na mwenendo kama huu na vitendo kama hivi (ukiachilia mbali uovu ambao umeenea kila mahali). Basi sisi Waislamu tunamuangalia vipi Mtume huyu mtukufu ambaye historia ya wanaadamu imemtambua (kwa wema) na anashuhudiwa na Mola mwenye nguvu na utukufu kwamba yeye ni mwenye hadhi kubwa mno kwa tabia njema? Kwa hakika ninavyoamini mimi ni kwamba, njama hizi zilianza baada ya Hija ya kuaga na hasa baada ya Mtume **(s.a.w.w)** kumsimika Imam Ali (a.s) kuwa Khalifa wake siku ya Ghadir khum. Hapo ndipo wale wenye tamaa ya ukubwa walipofahamu ya kwamba sasa hakuna lakufanya isipokuwa ni upinzani na ukaidi dhidi ya agizo (yaani uteuzi huo) kwa gharama yoyote ile japokuwa itapelekea

kurudi nyuma kwa visigino vyao (yaani kutoka katika dini). Hiyo ni tafsiri ya matukio iliyoanza kujitokeza kwa kumpinga Mtume **(s.a.w.w)** katika kila maamrisho yake (aliyoyatoa) na inathibitika hali hiyo kuanzia pale Mtume alipoandika maandiko ya kumpa Usamah uongozi wa jeshi, na matokeo yake ni watu kutokwenda kwenye jeshi aliloliandaa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** mwenyewe, na pia matukio yaliyofuatia baada ya Mtume kufariki. Miongoni mwa matukio hayo ni kuwalazimisha watu wale kiapo cha utiifu kwa nguvu na kuwatishia kuwachoma moto wale waliogoma, wakiwemo Ali, Fatma, Hassan na Hussein (a.s). Bali hali ilikuwa mbaya mno kiasi cha kuwazuwia watu kunakili hadithi za Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** kiasi kwamba vitabu ambavyo ndani yake tayari Sunna ya Mtume **(s.a.w.w)** ilikwisha andikwa vilichomwa moto. Si hivyo tu bali wako baadhi ya masahaba walitiwa gerezani ilimradi wasisimulie hadithi za Mtume **(s.a.w.w)**, mpaka ikafikia (kiwango) cha kuwauwa Masahaba ambao walikataa kutoa zaka kwa Abubakr kwa sababu yeye siye Khalifa waliyempa kiapo cha utii katika zama za Mtume wao kabla hajafariki.

(Haikuishia hapo tu bali) ilifikia kiwango cha kupora haki za bibi Fatma binti ya Mtume **(s.a.w.w)** ikiwa ni pamoja na shamba la Fadak, mirathi, Khums na kisha kumtuhumu kwamba yeye ni muongo kutokana na madai yake yanayohusu haki zake. Ilifikia wakati ambapo Imam Ali (a.s) alitengwa mbali mno na kila aina ya majukumu ya Kiislamu, na badala yake walitawalishwa juu ya shingo za Waislamu watu waovu na wanafiki miongoni mwa Bani Umayyah, na mambo yalivuka mpaka kwani Masahaba walizuiliwa kutabaruku kwa kumbukumbu za Mtume **(s.a.w.w)**. Utadhani hayo hayatoshi,. bali ilifikia hatua ya kufanya jaribio la kulifuta jina la Mtume **(s.a.w.w)** kwenye Adhana na kuushambulia mji wa Madina yenye Nuru kwa jeshi la kikafiri, jeshi ambalo lilifanya namna litakavyo mjini humo. Na ilifikia kuipiga nyumba tukufu (ya Mwenyezi Mungu) kwa mizinga, kuichoma moto na kuwauwa humo Masahaba, na ikafikia kukiua kizazi kitukufu cha Mtume **(s.a.w.w)** na kukitukana, kukilaani na watu kuwalazimisha kufanya hivyo, na hatimaye ilifikia kuwaua na kuwasambaratisha wote wanaowapenda watu wa nyumba ya Mtume kwa kuwafuatilia, mpaka ikafikia kuwa dini ya Mwenyezi Mungu ni jambo la mchezo na ni upuuzi na Qur'an ikawa inachanwa na kupuuzwa.

Njama hizo bado zinaendelea mpaka leo na athari zake na nguvu zake zinatembea ndani ya umma wa Kiislamu, na maadam kuna Waislamu wanaomtakia radhi Muawiyah na Yazid, na wanayatakasa matendo yao kuwa eti walifanya jitihada katika dini na kwamba watalipwa ujira kwa matendo hayo mbele ya Mwenyezi Mungu, na maadam wapo watu wanaoandika vitabu na makala mbali mbali dhidi ya wafuasi wa nyumba ya Mtume, kisha kuwavurumishia kila aina ya shutuma na matusi watu hao, na maadam kuna watu wanaohalalisha kuwaua wafuasi wa nyumba ya Mtume ndani ya nyumba Tukufu ya Mwenyezi Mungu tena katika msimu wa Hija, basi njama hizo (dhidi ya Mtume **s.a.w.w**) bado zinaendelea na zitabakia kuendelea mpaka hapo atakapotaka Mwenyezi Mungu. Nami siwezi kuzionesha zote au kuzidhibitisha kwa ufafanuzi wake kila upande, lakini ninajaribu juhudi yangu tena kwa unyenyekevu ili kumtakasa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** kutokana na riwaya zenye fedheha ambazo

amesingiziwa na ninamtetea yeye na Isma yake, na ninajaribu kuwatosheleza Waislamu wenye maarifa na walio huru (kifikra) kwamba, Mtume huyu ambaye Mwenyezi Mungu alimtuma ili awaongoe wanadamu wote na akamfanya kuwa mwangaza na taa inayong'ara, ni Mtume Mtukufu mno na ni mbora mno aliyetakasika sana sana, ni mkamilifu mno kuliko watu (wengine). Mwenyezi Mungu ndiye aliyemuumba (kwa sifa hizo) hivyo basi haiwezekani kwetu sisi kuzinyamazia riwaya ambazo undani wake hazikulengwa isipokuwa kuivunja heshima yake na kuporomosha utukufu wake.

Haiwezekani na haitawezekana kwetu sisi kuzikubali riwaya hizi japokuwa Ahlu-Sunnah Wal-Jamaa wamezikubali na wakaziandika ndani ya Sihahi zao na Musnad zao, haiwezekani (tukazikubali) hata kama wataafikiana (kuzikubali) walimwengu wote, kwani kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu aliposema, "Hakika wewe uko juu ya labia tukufu" hiyo ndiyo kauli ya ufumbuzi na uamuzi wa msingi, na baada ya kauli hiyo hapana kingine isipokuwa ni upotofu na uzushi. Na hii ifuatayo ndiyo kauli ya Mashia kumhusu Bwana wa viumbe wote ambaye ni muokozi wa wanaadamu kutokana na upofu na upotofu (uliozushwa dhidi ya) kiongozi wa umma anayeongoza watu kwenye amani na usalama, basi enyi wenye akili hebu fanyeni mazingatio.

3

# WAULIZE WANAOFAHAMU

## KAULI YA AHLU-DHIKRI KUHUSU MTUME (S.A.W.W)

Imam Ali (a.s) anasema: "Mpaka karama za Mwenyezi Mungu zikamfikia Muhammad **(s.a.w.w)**, akamtoa kutoka kwenye maoteo yenye asili bora, na mahala penye mapandio yenye nasaba tukufu, (akamtoa) kutoka katika mti ambao Mitume wake wametokana nao, na kutokana na mti huo (Mwenyezi Mungu) ameteua wawakilishi wake, kizazi cha Mtume ndiyo bora kuliko vizazi vyote, na ukoo wake ndiyo bora kuliko koo zote, na mti wake ndiyo bora kuliko miti yote, umeota mahala patakatifu na ukachanua mahala pema, una matawi marefu na matunda yasiyodhurika kwa chochote kile. Basi yeye Mtume ndiyo kiongozi wa yeyote anayemcha Mungu, naye ndiye jicho la mwenye kuongoka, ni taa ing'arayo mwanga wake na ni miali ambayo nuru yake imechomoza, yeye ni mwenge ambao mng'ao wake ni wenye kumeta, mwendo wake ni wenye msimamo na Sunna yake ni uongofu, maneno yake ndiyo upambanuzi na hukumu yake ni yenye uadilifu. Mwenyezi Mungu alimtuma akiwa ni miongoni mwa Mitume katika muda muafaka kwani ulikuwa ni wakati wa upotofu na matendo ya kijinga miongoni mwa watu. Mtume akatoa nasaha kikamilifu, akapita katika njia (ya haki) na akalingania (watu) kwa hekima na mawaidha mazuri ... Makazi yake ni makazi bora na chimbuko lake ni chimbuko tukufu lililomo ndani ya asili bora na makazi ya amani. Kwa hakika nyoyo za (watu) wema zimegeuziwa upande wake na macho yamemwelekea. Kwa sababu yake Mtume, chuki baina ya watu zimezimwa na uadui nao umeangamizwa, na kwa ajili yake udugu (Kiislamu) umeunganika na ukabomolewa uhusiano (na kufru). Kupitia kwa Mtume mnyonge ameheshimika na amedhalilishwa mwenye kiburi, maneno yake ndiyo ubainifu na ukimya wake ni usemi (tosha). (Mwenyezi Mungu) amemtuma kwa hoja zilizokamilika, na mawaidha yenye kuponya, na wito ulio mzuri, kwa Mtume amezidhihirisha sheria zilizokuwa zimesahaulika na kwake yeye amekemea uzushi uliokuwa umeingizwa (katika dini) na kwake akazibainisha hukumu kwa ufafanuzi. Alimtuma pamoja na mwangaza, na akamtanguliza kwa kumtukuza kwake yeye Mtume, akaondosha maovu na akawashinda wenye kuipinga haki, na akayawepesisha yaliyo mazito na akazidhalilisha itikadi mbaya mpaka akautenga mbali upotovu kutokana na njia ya haki.

# MLANGO WA TATU

## YANAYOWAHUSU WATU WA NYUMBA YA MTUME (S.A.W.W)

### SWALI LA TATU: AHLUL-BAIT (WATU WA NYUMBA YA MTUME) NI KINA NANI?

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّـهُ لِيُذْهِبَ عَنكُمُ الرِّجْسَ أَهْلَ الْبَيْتِ وَيُطَهِّرَكُمْ تَطْهِيرًا ﴿٣٣﴾

Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu, enyi Watu wa Nyumba ya Mtume, na kukusafisheni baarabara. (Qar'an, 33:33).

Ahlu-Sunna Wal-Jamaa, wanasema kwamba aya hii ilishuka kwa ajili ya wake za Mtume **(s.a.w.w)**, na wanatolea ushahidi wa madai hayo kulingana na mfumo wa aya zilizo itangulia aya hii na zinazoifuatia. Kwa mujibu wa madai yao ni kwamba Mwenyezi Mungu amewaondolea uchafu wakeze Mtume na amewatakasa kikamilifu. Na miongoni mwa hao Ahli-Sunnah wapo wanaowaongeza juu ya wakeze Mtume **(s.a.w.w)** Imam Ali, Fatma, Hassan na Husein (a.s). Lakini ukweli ulivyo na kama ulivyonukuliwa, kadhalika akili na historia vinaikataa tafsiri hii, kwani Ahlu-Sunnah haohao wanazo riwaya ndani ya vitabu vyao (zisemazo) kwamba aya hii ilishuka kuwahusu watu watano tu nao ni: Mtume Muhammad **(s.a.w.w)**, Ali, Fatma, Hasan na Husein (a.s), na kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** ndiye aliyewahusisha hao na nafsi yake tukufu kwenye aya hii pale alipomuingiza Ali, Fatma, Hasan na Hussein pamoja na yeye mwenyewe ndani ya kisaa (shuka) na akasema: "Ewe Mwenyezi Mungu hawa ndiyo watu wangu basi waondolee uchafu na uwatakase kikamilifu." (Tafsiri) hiyo wameiandika wanachuoni wengi wa Kisunni, mimi nitawataja baadhi yao tu:

1) Muslim ndani ya Sahihi yake katika mlango wa Fadhail-Ahlil-Bait Juz. ya 2 uk. 368.

2) At-Tirmidhi ndani ya Sahih yake Juzuu ya 5 uk. 30.

3) Musnadul-Imam Ahmad ibn Hanbal Juzuu 1 uk. 330.

4) Mustad-rak-Al-Hakim Juzuu 3 uk. 123.

5) Khasaisul-Imamin-Nasai uk. 49.

6) Tal-Khisud-dhahabi Juzuu 2 uk. 150.

7) Mu'ujamut-Tabrani Juzuu 1 uk. 65.

8) Shawahidut-Tanzil ya Al-Hakimul-Haskani Juz.2 uk.ll

9) Bukhari ndani ya Tarikhul-Kabir Juz. 1 uk. 69

10) Al-Isabah ya ibn Hajar Al-Asqalani Juzuu 2 uk. 502.

11) Tadh-Kiratul-Khawas ya ibn Al-jauzi uk. 233.

12) Tafsirul-Fakhrir-Razi Juz. 2 uk. 700.

13) Yanabiul-Mawaddah ya Al-Qanduzi Al-Hanafi
uk. 107.

14) Manaqibul-Khawar-Zami uk. 23.

15) As-siratul-Halabiyyah Juz.3 uk. 213.

16) As-siratud-dah-laniyyah Juz. 3 uk. 329.

17) Usudul-ghabah ya ibnul-Athir Juz. 2 uk. 12. jl8) Tafsirut-Tabari Juz. 22 uk.6.

19) Ad-durul-Manthur ya Suyuti Juz. 5 uk. 198.

20) Tarikhu ibn A'sakir Juz. 1 uk. 185.

21) Tafsirul-Kashaf ya Az-Zamakhshari Juz. 1 uk.193

22) Ah-kamul-Qur'an ya ibn Arabi Juz. 2 uk. 166.

23) Tafsirul-qur-Tubi Juz. 14 uk. 182.

24) As-sawaiqul-Muhriqah ya ibn Hajar uk. 85.

25) Al-Istiiabu ya ibn Abdibarri Juz. 3 uk. 37.

26)Al-Iqdul-Farid ya ibn Abd rabih Juz. 4 uk. 311.

27) Muntakhabu Kanzil-Ummal Juz. 5 uk. 96.

28)Masabihus-Sunnah ya Al-baghwi Juz. 2 uk. 278.

29)As-babun-nuzul ya Al-wahidi uk. 203.

30)Tafsiru ibn Kathir Juz. 3 uk. 483.

Wako wengine wasiokuwa hawa miongoni mwa wanachuoni wa Ahlul-sunnah Wal-jamaa, wengi tu hatukuwataja lakini tumetosheka na idadi hii. Sasa basi ikiwa wanachuoni wote hawa wanakiri kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu ndiye aliyebainisha makusudio ya aya hii, je zina nafasi gani kauli za wengine wasiokuwa Mtume miongoni mwa Masahaba na Tabiina au wafasiri ambao wanataka kuipeleka maana ya aya hiyo kinyume na vile atakavyo Mwenyezi Mungu na Mtume wake eti kwa lengo la kutaka kumridhisha Muawiyah na kutumainia (mali) aliyonayo? Kama ambavyo Mtume **(s.a.w.w)** amepata kuwaashiria watu nyumba yake kwa mara nyingine na akawahusisha kwamba wao ndio Ahlul-bait na siyo wengine wasiokuwa wao, napo ni pale iliposhuka kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo:

فَقُلْ تَعَالَوْا نَدْعُ أَبْنَاءَنَا وَأَبْنَاءَكُمْ وَنِسَاءَنَا وَنِسَاءَكُمْ وَأَنفُسَنَا وَأَنفُسَكُمْ ثُمَّ نَبْتَهِلْ فَنَجْعَل لَّعْنَتَ اللَّـهِ عَلَى الْكَاذِبِينَ ﴿٦١﴾

"Basi waambie njooni tuwaite wanetu na wanenu, na wanawake wetu na wanawake wenu na sisi wenyewe na ninyi wenyewe, kisha tuapizane na tuombe laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie waongo" (Qur'an, 3:61).

Bwana Mtume alimwita Ali, Fatma, Hassan na Husein na akasema "Hawa ndiyo wanetu na sisi wenyewe na wanawake wetu, basi njooni ninyi wenyewe na wanenu na wanawake zenu."

Na katika riwaya ya Muslim amesema: "**Ewe Mwenyezi Mungu hawa ndiyo watu wangu**."

Na wale wanachuoni wa Ahli-Sunna Wal-Jamaa ambao nimewataja katika rejea zilizotangulia vile vile wote wanakiri kuwa aya hii (Qur'an, 3:61), ilishuka kuwahusu watu watano hawa waliotajwa, rehma na amani za Mwenyezi Mungu ziwashukie wote. Ifahamike kwamba, wakeze Mtume **(s.a.w.w)** waliyafahamu makusudio ya aya hiyo tukufu, (Qur'an, 33:33).

Na ndiyo maana hakuna mmoja wao aliyedai kwamba yeye ni miongoni mwa Ahlul-Bayt (a.s) na hasa hasa wakitanguliwa na Ummu Salamah na mwana Aisha, kwani kila mmoja wao (wawili hawa) ameleta riwaya (isemayo) kwamba aya hii inamuhusu Mtume wa Mwenyezi Mungu, Ali, Fatma, Hassan na Husein (a.s), na wameandika juu ya kukiri kwa wake za Mtume kuhusu aya hiyo, Muslim, Tir-midhi, Al-Hakim, Tabari, Suyuti na Ibnul- Athir na wengineo.

Zaidi ya yote hayo ni kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** aliondoa utatanishi na mush-keli huu, kwani yeye alifahamu kwamba Waislamu wataisoma Qur'an na kuwafahamu Ahlul-Bait kutokana na mtiririko wa aya zilizotangulia na zinazofuatia ambazo zinawaonya wake wa Mtume, hivyo akawahi kuufundisha umma (wake) makusudio ya aya ya kuwaondolea uchafu na kuwatakasa (watu wa nyumba ya Mtume) pale alipodumu kwa mfululizo wa muda wa miezi sita (baada ya kushuka aya hii) kwa kupita kwenye mlango wa (nyumba ya) Ali, Fatma, Hasan na Hussein kabla ya kuanza kusali kwa kusema: (Bila shaka Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu enyi watu wa nyumba ya Mtume na kukutakaseni sana sana, basi amkeni mkasali Mwenyezi Mungu akurehemuni. Suala la Bwana Mtume kuwahi kuufundisha umma wake ni

jambo aliloliandika Tir-midhi katika Sahih yake Juz. 5 uk. 31, Al-hakim katika Mustad-rak Juz. 3 uk. 158, Ad-dhahabi ndani ya Tal-khisi yake, Ahmad ibn Hanbal ndani ya Musnad yake Juz. 3 uk. 259, Ibnul-athir ndani ya Usudul-ghabah Juz. 5 uk. 521 na Al-Has-Kani katika Shawahidut-tanzil Juz. 2 uk. 11, As-suyutti ndani ya Ad-durul-manthur Juz. 5. uk. 199, Tabari katika tafsiri yake Juz. 22 uk. 6, Al-baladhuri ndani ya Ansabul-Ash-raf Juz. 2 uk. 104, ibn Kathir katika tafsiri yake Juz. 3 uk. 483 na Haithami katika Majmauz- zawaid Juz. 9 uk. 168 na wengineo.

Zaidi ya hawa wanachuoni wa Kisunni tukiwaongeza Maimamu wa nyumba ya Mtume na wanachuoni wa Kishia ambao hawana shaka juu ya kuhusika kwa Mtume, Ali, Fatma Hassan na Husein katika aya hii tukufu, basi hakuna nafasi yoyote ya kujitetea watakayokuwa nayo wapinzani miongoni mwa maadui wa Ahlul-Bait na wafuasi wa Muawiyah na Banu Umayyah ambao wanataka kuizima nuru ya Mwenyezi Mungu kwa kutumia vinywa vyao na Mwenyezi Mungu (bila shaka) ataitimiza nuru yake (ing'ae) japokuwa makafiri watachukia. Kwa hakika wamedhihirisha wazi hao wanaofasiri aya hizo kinyume cha tafsiri ya Mtume **(s.a.w.w)** kwamba, wao ni miongoni mwa wanaojipendekeza kwa watawala wa Banu Umayyah na Bani Abbas hapo zamani mpaka sasa, kwani (wafasiri) hao ni miongoni mwa watu wenye chuki ambao hawampendi Ali japo watajificha kwa mavazi ya Uanachuoni na Ufaqihi. Tunasema hivi kwa sababu akili peke yake tu inatosha kupata uamuzi wa kutokuwaingiza katika aya hii yaani (kuondolewa uchafu na kuwatakasa) wakeze Mtume **(s.a.w.w)**.

1) Kwa mfano tukimchukua Ummul-Muuminina Aisha ambaye yeye anadai kuwa ni kipenzi mno kwa Mtume kuliko wakeze wengine na ni wa karibu mno kwa Mtume kiasi kwamba wake wengine wa Mtume walimuonea wivu na wakamtumia ujumbe (Mtume) wa kumtaka awe muadilifu kwa sababu ya binti Abi Quhafah, kama tulivyotangulia (kueleza) hakuthubutu na wala hakuna aliyethubutu miongoni mwa watetezi wake na wampendao si miongoni mwa waliopita wala wale waliofuatia (hakuna aliyethubutu) kusema kuwa Bibi Aisha alikuwa ndani ya Kisaa siku iliposhuka aya hiyo. Basi ni utukufu ulioje wa Muhammad **(s.a.w.w)** katika maneno yake na vitendo vyake na ni utukufu ulioje wa hekima yake pale alipowafunika ndani ya Kisaa mpaka Ummul-Muuminina Ummu Salamah ambaye ni mke wa Mtume alitaka kuingia pamoja nao ndani ya Kisaa na akamuomba mumewe ambaye ndiye Mtume wa Mwenyezi Mungu (naye aingie), lakini Mtume akamzuwia kuingia na akamwambia, "Wewe uko kwenye kheri".

2) Kisha aya hii kwa maf-humu yake makh'sus na ile ya jumla inajulisha juu ya "Isma" (ambayo ni kuhifadhika kutokana na kila aina ya madhambi), kwani kuondolewa uchafu kunakusanya kila aina ya dhambi, maasi na uovu, madogo na makubwa, na hasa itakapoongezewa utakaso huo kuwa unatoka kwa Mola Mtukufu mwenye nguvu.

3) Na iwapo Waislamu hujitoharisha kwa maji na udongo tahara ya kimwili ambayo haivuki zaidi ya nje ya miwili, basi Mwenyezi Mungu amewatakasa Ahlul-Bait kwa tahara ya kiroho iliyosafisha akili na moyo, na haukuachiwa nafasi yoyote ushawishi wa shetani wala kutenda maovu. Kwa

hiyo nyoyo zao (Ahlul-Bait) ni safi, zimetakasika, zenye ukweli wa dhati kwa Muumba wao katika kila harakati zao na utuvu wao.

4) Kwa yote hayo watu hawa wamekuwa kiigizo kwa watu wote katika ucha Mungu, ukweli, elimu, upole, ushujaa, utu, utakasifu, kuipa nyongo dunia na kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na historia haikupata kuandika maasi au dhambi ya yeyote miongoni mwao muda wote wa uhai wao. Na kama mambo yako kama hivyo, hebu na turejee kwenye mfano wa kwanza unaohusu wakeze Mtume **(s.a.w.w)** na (tumuone) Mwanaisha ambaye amefikia daraja tukufu na cheo cha juu na umaarufu mkubwa ambao hakuna mke yeyote wa Mtume **(s.a.w.w)** aliyeufikia. Haiwezekani kabisa kuzifikia sifa kemkem za bibi Aisha binti Abubakr hata kama sifa zao (wake wengine wa Mtume) zitakusanywa pamoja, na hivi ndivyo wasemavyo Ahlus-Sunnah kuhusu sifa za Mwanaisha pia Ahlus-Sunnah wanaamini kwamba nusu ya dini inatokana kwake (Bibi Aisha) peke yake.

Tukishikamana na ukweli bila ya chuki wala kupendelea, hivi kweli inaingia akilini kwamba Mwanaisha ametakasika hana madhambi wala maasi? Au tuseme kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu alimuondolea Mwanaisha hifadhi na kizuwizi (cha kutofanya dhambi) baada ya kifo cha mumewe (ambaye) ni Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**? Basi hebu na tuuangalie kwa pamoja ukweli halisi ulivyo. Bibi Aisha katika zama za uhai wa Mtume **(s.a.w.w)** Tunapoyafanyia uchunguzi maisha yake na mumewe, tunayakuta madhambi na maasi mengi (aliyoyatenda). Mara nyingi alikuwa akifanva njama yeye na bibi Hafsa dhidi ya Mtume **(s.a.w.w)** mpaka akamlazimisha Mtume kujinyima kitu alichohalalishiwa na Mwenyezi Mungu. Maelezo ya jambo hilo yamo ndani ya Bukhari na Muslim, na wawili hao walisaidiana dhidi ya Mtume **(s.a.w.w)** kama zilivyolithibitisha jambo hilo sihah na tafsiri zote, na Mwenyezi Mungu ameyataja matukio yote mawili ndani ya kitabu chake kitukufu.

Vile vile ni kama ilivyokuwa wivu ukitawala moyo na akili zake na akawa hana heshima wala adabu mbele ya Mtume **(s.a.w.w)**, kuna wakati alimwambia Mtume **(s.a.w.w)** pale Mtume alipomtaja bibi Khadija mbele yake, (bibi Aisha akasema) "Kuna uhusiano gani kati yangu na Khadija, hakika yeye alikuwa bibi Kizee mwenye midomo myekundu na Mwenyezi Mungu amekubadilishia (mke) bora kuliko yeye." Na kwa ajili hii Mtume wa Mwenyezi Mungu alikasirika mpaka nywele zake zikatikisika. Kuna wakati fulani mmoja kati ya wakeze Mtume **(s.a.w.w)** alimpelekea Mtume sahani ambayo ndani yake mlikuwa na chakula ambacho Mtume alikuwa akikipenda, bibi Aisha (kwa wivu aliokuwa nao) akaivunja sahani hiyo na chakula chake mbele ya Mtume **(s.a.w.w)**.

Kuna mara nyingine tena bibi Aisha alimwambia Mtume, "Hivi wewe ndiye unayedai kuwa ni Mtume wa Mwenyezi Mungu? Pia ipo siku ambayo Mama Aisha alikasirika mbele ya Mtume na akamwambia Mtume, "Fanya uadilifu." Baba yake alikuwepo mahala hapo akampiga mpaka damu zikamtiririka. Na kutokana na wingi wa wivu (aliokuwa nao) alimdanganya Asmaa binti Nu'uman alipokuwa bi harusi nyumbani kwa Mtume akamwambia, "Mtume humfurahia sana mwanamke ambaye akiingia kwake amwambie, "Najilinda kwa Mwenyezi Mungu kutokana nawe". Lengo la

Mama Aisha ilikikiwa kinyume cha hivyo, bali ni alitaka mwanamke huyo asiye na kosa aachike, na Mtume alimuacha kwa sababu ya maneno haya. Kutokana na adabu yake mbaya mbele ya Mtume **(s.a.w.w)**, ilifikia mahali ambapo Mtume alikuwa akiswali naye bibi Aisha amenyoosha miguu yake kwenye Qibla, na Mtume akisujudu huisogeza pembeni ndipo (bibi Aisha) huikunja, Mtume akisimama yeye huionyoosha miguu yake kwenye Qibla yake. Kuna kipindi fulani walikula njama yeye na Mama Hafsa dhidi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** ikapelekea (njama hiyo kumfanya Mtume) ajitenge na wakeze kwa sababu ya njama hiyo kwa muda wa mwezi mmoja kamili Mtume analala kwenye jamvi. Iliposhuka kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo:

"Na umuahirishe umtakaye miongoni mwao na umsogeze umtakaye" (Qur 33:51). Aisha alimwambia Mtume bila hata aibu "Simuoni Mola wako isipokuwa anaweka mbele matamanio yako".

Mama Aisha alipokuwa akikasirika (na ni mara nyingi alikuwa akikasirika) huacha jina la Mtume **(s.a.w.w)** na hutaja jina la Muhammad na hupata akasema: "Ewe Mlezi wa Ibrahim. (Kwa kweli) Aisha alimuudhi Mtume wa Mwenyezi Mungu mara nyingi na kumpa taabu, lakini Mtume **(s.a.w.w)** ni mpole mwenye huruma, na tabia yake ni tukufu na subira yake ni kubwa, mara nyingi alikuwa akimwambia Aisha, "Ewe Aisha shetani wako kisha kukuvaa" na mara nyingi alikuwa akisikitika kutokana na makemeo ya Mwenyezi Mungu kwake Aisha na Hafsa binti Umar, na ni mara nyingi Qur'an ilishuka kwa sababu yake, Mwenyezi Mungu amesema kuwaambia Aisha na Hafsa:

إِن تَتُوبَا إِلَى اللَّـهِ فَقَدْ صَغَتْ قُلُوبُكُمَا ﴿٤﴾

"Iwapo mtatubia kwa Mwenyezi Mungu itakuwa kheri kwenu kwa hakika nyoyo zenu zimepotoka" (Qur'an 66:4). Aya hii inamaanisha kwamba amepotoka na kuiacha haki na amesema tena Mwenyezi Mungu:

وَإِن تَظَاهَرَا عَلَيْهِ فَإِنَّ اللَّـهَ هُوَ مَوْلَاهُ وَجِبْرِيلُ وَصَالِحُ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمَلَائِكَةُ بَعْدَ ذَٰلِكَ ظَهِ يرٌ
﴿٤﴾

"Na kama mtasaidiana dhidi ya (Mtume) basi Mwenyezi Mungu ndiye msaidizi wake na Jibril na Waislamu wema, na zaidi ya hayo Malaikapia watasaidia". (Qur'an, 66:4).

Ni onyo la wazi kutoka kwa Mola Mtukufu (kuwaonya) Mama Aisha na Hafsa ambaye mara nyingi alikuwa akimfuata Aisha na kutekeleza anayomuamrisha. Na amesema tena Mwenyezi Mungu kuwaambia wawili hawa

عَسَىٰ رَبُّهُ إِن طَلَّقَكُنَّ أَن يُبْدِلَهُ أَزْوَاجًا خَيْرًا مِّنكُنَّ مُسْلِمَاتٍ مُّؤْمِنَاتٍ ﴿٥﴾

"Mtume akikupeni talaka Mola wake atampa badala yenu wanawake wengine walio bora kuliko ninyi Waislamu tena waumini." (Qur'an, 66:5).

Aya hizi zilishuka kumuhusu Mama Aisha na Hafsa kwa ushahidi wa Umar ibn Khatab kama ilivyokuja katika Bukhari. Basi aya hii pekee inajulisha kuwa, kuna wanawake waumini miongoni mwa Waislamu ambao ni bora kuliko Aisha. Kuna wakati fulani Mtume **(s.a.w.w)** alimtuma Aisha pale Mtume alipotaka kumposa dada wa kiongozi wa kabila la Kalbi, Mtume akamtaka Aisha aende akamtazame mwanamke huyo, na aliporudi

wivu ulikuwa umeusonga moyo wake, Bwana Mtume **(s.a.w.w)** akamuuliza, "Umemuonaje ewe Aisha? Aisha akasema "Sikuona uzuri wowote." Mtume **(s.a.w.w)** akamwambia Aisha, "Hakika umeona uzuri, hapana shaka umemuona msichana bora na umesisimka ukamuogopa." Basi Aisha akasema; "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu kwako wewe hapana siri na ni nani mwenye kukuficha." Yote aliyoyafanya Aisha kumfanyia Mtume **(s.a.w.w)** miongoni mwa njama (mbali mbali) mara nyingi alikuwa akimshirikisha Hafsa binti Umar, na la kushangaza ni kwamba tunakuta kuwa maelewano na mtiririko kamili kati ya wanawake wawili Aisha na Hafsah ni kama ulivyo mtiririko (wa ushirikiano) na maelewano baina ya baba zao Abubakr na Umar, isipokuwa kwa wanawake Aisha mara nyingi alikuwa na nguvu na hana woga na ndiye mwenye kuharakia (mambo), na yeye Aisha ndiye aliyekuwa akimkokota Hafsah nyuma yake katika kila kitu, wakati huo huo baba yake (Aisha) Abubakr alikuwa dhaifu mbele ya Umar, ambapo Umar alikuwa na nguvu na hana woga na ndiye mwenye kuchukua hatua ya mwanzo katika kila kitu.

Kwa hakika tumeona katika maelezo yaliyopita kwamba (Abubakr) hata katika ukhalifa wake, Umar ndiye aliyekuwa mtawala mtendaji. Wanahistoria wamesimulia ya kwamba, Aisha alipokusudia kutoka kwenda Basra kumpiga Imam Ali (a.s) katika vita ambayo iliitwa vita ya Jamal, aliwapelekea ujumbe wakeze Mtume **(s.a.w.w)** akiwataka watoke pamoja naye, basi hakuna aliyekubali mwito huo miongoni mwao isipokuwa Hafsa bint Umar ambaye alijiandaa na akaazimia kutoka, lakini kaka yake Bwana Abdallah ibn Umar akamkataza na akaenda kumwita ndipo akavunja safari yake.[47] Kwa ajili hiyo basi Mwenyezi Mungu alikuwa akiwaonya Aisha na Hafsa kwa pamoja katika kauli yake aliposema: "Na kama mtasaidiana dhidi yake (Mtume) basi Mwenyezi Mungu ndiye msaidizi wake na Jibril na Waislamu wema, na zaidi ya hayo Malaika pia watamsaidia." Na vile vile kauli yake aliposema: "Iwapo mtatubia kwa Mwenyezi Mungu (itakuwa kheri kwenu) kwa hakika nyoyo zenu zimepotoka." Kwa hakika Mwenyezi Mungu aliwapigia (Aisha na Hafsa) mfano wa hatari sana katika Surat-tahrim ili Mwenyezi Mungu awafahamishe Waislamu wengine ambao wanaamini kwamba Mama huyu wa waumini ataingia peponi bila ya hesabu wala adhabu, eti tu kwa kuwa ni mke wa Mtume **(s.a.w.w)**. Sivyo kabisa, Mwenyezi Mungu amewajulisha waja wake wanaume kwa wanawake kwamba hali ya kuoana hainufaishi wala haidhuru mbele ya Mwenyezi Mungu, bali ni matendo ya mtu mwenye we (ndiyo yatakayomsaidia).

Mwenyezi Mungu anasema: "Mwenyezi Mungu amewapigia mfano wale waliokufuru kwa mkewe Nuhu na mkewe Lut, walikuwa chini ya waja wetu miongoni mwa waja wetu wema wawili hao (Nuh na Lut) basi (wanawake hao) wakawafanyia hiyana waume zao, hawakuweza kuwakinga kwa lolote (kutokana na adhabu) mbele ya Mwenyezi Mungu, na wakaambiwa ingieni motoni pamoja na wenye kuingia (humo). Surat-tah-riim, aya ya kumi. Mwenyezi Mungu amepiga mfano kwa wale walioamini (akamtaja) mke wa Firaun pale aliposema:

رَبِّ ابْنِ لِي عِندَكَ بَيْتًا فِي الْجَنَّةِ وَنَجِّنِي مِن فِرْعَوْنَ وَعَمَلِهِ وَنَجِّنِي مِنَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿١١﴾
وَمَرْيَمَ ابْنَتَ عِمْرَانَ الَّتِي أَحْصَنَتْ فَرْجَهَا فَنَفَخْنَا فِيهِ مِن رُّوحِنَا وَصَدَّقَتْ بِكَلِمَاتِ رَبِّهَا وَ كُتُبِهِ
وَكَانَتْ مِنَ الْقَانِتِينَ ﴿١٢﴾

"Ewe Mola wangu! nijengee nyumba peponi na uniokoe kutokana na Firaun na matendo yake (machafu) na uniokoe kutokana na watu madhalimu. Na Mariamu binti wa Imran aliyejihifadhi tupu yake, tukampulizia humo roho yetu (inayotoka kwetu) na akayasadikisha maneno ya Mola wake na vitabu vyake na alikuwa miongoni mwa (watu) wanyenyekevu." (Qur.66:ll-12).

Kutokana na hali hii basi inabainika kwamba kuoana na urafiki japokuwa kuna ubora mwingi lakini hausaidii (chochote) kuepukana na adhabu ya Mwenyezi Mungu isipokuwa (kuoana huko na urafiki) kutakapo jitambulisha kwa matendo mema, vinginevyo basi adhabu itakuwa maradufu, kwani uadilifu wa Mwenyezi Mungu ni kutomuadhibu aliye mbali ambaye hakusikia wahyi (kwa kiwango) kama cha yule ambaye Qur'an inashuka nyumbani mwake, na haitakuwa sawa adhabu ya mtu aliyeifahamu haki kisha akaipinga aadhibiwe kama mjinga ambaye hakutambua haki. Ewe msomaji sasa hivi hebu angalia baadhi ya riwaya zenye ufafanuzi ili upate kumfahamu vyema mwanamke huyu aliyechukua nafasi kubwa ya kumtenga Imam Ali kutoka kwenye Ukhalifa na akampiga vita kwa kila aina ya nguvu na vitimbi. Vile vile ili upate kufahamu kwamba ile aya ya kuondolewa uchafu na kutakaswa haimhusishi kabisa Mama Aisha kwa umbali wa masafa ya mbingu na ardhi, na kwamba Ahlu-Sunnah wengi wao ni mateka wa uharibifu na uzushi (wa Banu Umayyah) na wanawafuata Banu Umayyah hali yakuwa wao hawafahamu.

4

# WAULIZE WANAOFAHAMU

## UMMUL-MU'MININA AISHA ANAISHUHUDIA NAFSI YAKE

Hebu na tumsikie bibi Aisha mwenyewe analeta riwaya (inayomuhusu) na ni namna gani (tutaona) wivu ulivyo mkosesha lengo lake na kisha ni jinsi gani alionesha tabia mbaya mbele ya Mtume **(s.a.w.w)**.

Anasema bibi Aisha: "Safiyah mkewe Mtume alimletea Mtume **(s.a.w.w)** chakula alichomtengenezea wakati Mtume akiwa nyumbani mwangu, nilipomuona mjakazi (analeta chakula hicho) nilianza kutetemeka na nikashindwa kujizuwia, kisha nikaipiga sahani (ya chakula) na nikaitupa (chini). Mtume wa Mwenyezi Mungu akaniangalia na nilifahamu hasira (iliyojitokeza) usoni mwake, basi nikasema, Najilinda kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu asije nilaani leo hii." Mtume akasema: "Badilisha." Nikasema, kafara yake ni kitu gani ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu?" Mtume akasema, "Ni chakula kama chakula chake (kilichokuwa humu) na chombo kama chombo chake". Na kuna mara nyingine ameleta riwaya inayomuhusu yeye mwenyewe amesema: "Nilimwambia Mtume, anakutosha Safiyyah (kwa jambo) kadha wa kadha," Mtume akaniambia, "Kwa hakika umesema jambo (ambalo) lau litachanganywa na maji ya bahari lingeyaharibu." Subhanallah!!!. Ana hali gani Ummul-Muminina, yuko mbali mno na tabia njema na haki ambazo Uislamu umezifaradhisha katika kuharamisha kuteta na uzushi? Na hapana shaka kwamba kauli yake aliposema, "Anakutosha Safiyyah (kwa jambo) kadha wa kadha, na kauli ya Mtume aliposema kuwa neno hilo lau litachanganywa na maji ya bahari lingeyaharibu," jambo hilo alilolisema Aisha kuhusu mke mwenziwe Bibi Safiyyah inaonesha lilikuwa ni jambo la kutisha na lilikuwa jambo la hatari. Mimi naamini kwamba wapokezi wa hadithi waliliona kuwa ni baya na la kutisha basi wakalibadilisha kwa ibara ya "kadha wa kadha" kama ilivyo kawaida yao kwa mambo kama haya.

Huyu hapa tena Aisha Ummul-Muminina anaeleza kwa mara nyingine wivu wake kwa wakeze Mtume anasema: "Sikumuonea wivu mwanamke yeyote isipokuwa wivu huo utakuwa chini ya wivu niliomuonea "Mariyah" na hiyo ni kwa sababu alikuwa mzuri mno na Mtume wa Mwenyezi Mungu alimpenda, mwanzoni alipokuja naye alimfikishia kwenye nyumba ya Harithah ibn Nuuman, na tulitishika kutokana naye lakini mimi nilishindwa kuvumilia, ndipo Mtume wa Mwenyezi Mungu alipomuhamishia Aliyah, kisha akawa huenda huko. Jambo hilo lilikuwa zito mno kwetu sisi na Mwenyezi Mungu akamruzuku (Mtume) kutokana na Mariyah mtoto wa kiume nasi akatunyima". Kama ambavyo wivu wa bibi Aisha ulivuka mipaka kutoka kwa mke mweziwe bibi Mariyah hadi kwa mtoto mdogo Ibrahim. Aisha amesema: "Ibrahim alipozaliwa Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuja naye kwangu akasema, Hebu muangalie namna alivyofanana nami, basi mimi nikasema, Sioni kufanana kokote, Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema: Hivi huoni weupe wake na mwili wake? Nikamwambia, Yeyote aliyenyweshwa mazima ya kondoo huwa mweupe na hunenepa". Wivu wa Mwanaisha ulivuka mipaka yote na hauelezeki hasa pale

ulipomfikisha kumdhania vibaya na kumtilia wasi wasi na mashaka Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**, kwani mara nyingi alikuwa akijifanya kalala wakati Mtume anapolala nyumbani kwa Aisha, lakini kumbe humchunga mumewe na kumchunguza mahali alipo katika giza na kumfuatilia popote anapokwenda. Hebu ione riwaya hii inayotoka ulimini mwa Mama Aisha riwaya ambayo ameiandika Muslim ndani ya sahihi yake na Imam Ahmad ndani ya Musnad yake na wengineo.

Amesema: "Ilipokuwa ni usiku wangu ambao Mtume **(s.a.w.w)** alikuwa kwangu, alirudi akaweka nguo zake, akavua viatu vyake akaviweka mbele ya miguu yake na akakunjua shuka yake juu ya kitanda chake kisha akalala, basi muda si mrefu alidhani mimi nimepitiwa na usingizi, alichukua nguo zake taratibu na akavaa viatu vyake taratibu halafu akafungua mlango akatoka kisha akaufunga mlango taratibu. Pale pale nami nikavaa nguo yangu na nikafunga shuka yangu nikatoka kumfuata nyuma yake mpaka akafika Baqii. Hapo akasimama kwa muda mrefu kisha akanyanyua mikono yake mara tatu, kisha akageuka nami nikageuka, akakaza mwendo nami nikakaza mwendo, akaongeza mwendo nami nikaongeza mwendo, alifika nami nimeshafika nikawa nimemtangulia nikaingia ndani, hakuna nilichofanya ila nililala, basi akaingia na akasema, Una nini ewe Aisha mbona unahema namna hii?. Nikamwambia, "Hapana lolote." Mtume akasema: "Lazima utaniambia vinginevyo Mwenyezi Mungu atanieleza." nikasema, "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, namuapia baba yangu na mama yangu, basi nikamueleza hali ilivyokuwa. Akasema, "Wewe ndiyo ule weusi niliouona mbele yangu"? Nikasema, "'Ndiyo." Akanipiga kifuani pigo lililonipa maumivu, kisha akasema, "Hivi ulidhani Mwenyezi Mungu na Mtume wake watakudhulumu..."? Na kuna mara nyingine bibi Aisha alisema, "Nilimkosa Mtume wa Mwenyezi Mungu basi nikadhani amekwenda kwa baadhi ya wajakazi wake, basi nikamtafuta, ghafla nikamuona amesujudu hali ya kuwa anasema, "Ewe Mola nisamehe" Na mara nyingine amesema, "Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu alitoka nyumbani mwangu usiku, basi nikaona wivu, aliporudi akayaona mambo ninayoyafanya, Mtume akasema, Una nini ewe Aisha je, umeona wivu? Nikasema, kwa nini mtu kama mimi nisione wivu kwa mtu kama wewe?! Basi Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema: Hivi shetani wako kisha kuchukua? Riwaya hii ya mwisho inajulisha wazi kwamba, bibi Aisha kila alipokuwa na wivu alikuwa anabadilika kutoka katika hali yake ya kawaida na kufanya mambo ya ajabu kama vile kuvunja vyombo au kuchanachana mavazi.

Na ndiyo maana katika riwaya hii anasema, "Mtume alipokuja na akaona ninayoyafanya akasema, hivi shetani wako kisha kuchukua"? Hapana shaka kwamba shetani wa Aisha alikuwa akimchukua na kumzingira mara nyingi, na (shetani huyo) aliukuta moyo wa Aisha kuwa ni njia miongoni mwa njia za wivu. Imepokewa toka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema kwamba: "**Wivu kwa mwanamume ni imani na kwa mwanamke ni kufru.**" Tafsiri yake ni kwamba: mwanamume anamuonea wivu mkewe kwa kuwa kisheria haifai awe na mshirika yeyote kwa mke huyo, ama mwanamke hana haki ya kuwa na wivu kwa mumewe kwa kuwa Mwenyezi Mungu amemruhusu mwanamume kuoa zaidi ya mke mmoja.

Basi mwanamke mwema anayefuata hukumu za Mwenyezi Mungu Mtukufu humpokea mke mwenziwe kwa moyo mkunjufu, kama isemwavyo leo hii hasa pale mumewe akiwa muadilifu mwenye msimamo na anamuogopa Mwenyezi Mungu. Je, nini fikra yako kuhusu uadilifu na msimamo wa Bwana aliyembora wa utu na kigezo cha ukamilifu, uadilifu na tabia njema? Sisi tunakuta kuna tofauti bayana kuhusu penzi la Mtume kwa Aisha na vile wasemavyo Ahlus-sunnah Wal-jamaa, eti kwamba Aisha alikuvva ni kipenzi mno kwa Mtume kuliko wakeze wengine, na kwamba alikuwa bora mno mbele yake mpaka kiasi wanaleta riwaya kwamba baadhi ya wake za Mtume walizitoa nauba zao (siku anazostahiki Mtume kuwa kwao) kwa Aisha walipofahamu kwamba Mtume **(s.a.w.w)** anampenda mno bibi Aisha na havumilii kumkosa!!!. Je, hivi kweli inawezekana katika hali kama hii (tuliyoeleza juu ya Mama Aisha tukampata mtu kuutakasa na kuupa tafsiri (nyingine) wivu wa bibi Aisha usiokuwa na kipimo?

Ukweli unavyoonekana, ni kinyume cha alivyokuwa akifanya bibi Aisha, kwani wake wengine wa Mtume wao ndiyo wangestahiki kumuonea wivu Aisha kwa kuwa Mtume kampenda mno na kuegemea kwake kama wanavyodai na kueleza katika riwaya. Sasa, ni kitu gani kinachohalalisha wivu wa bibi Aisha.?

Historia haikusimulia isipokuwa hadithi zake na vitabu vya Sirah vimejaa sifa zake na kwamba yeye ndiye kipenzi cha Mtume wa Mwenyezi Mungu, mwenye kujipendekeza ambaye Mtume alikuwa hawezi kutengana naye. Mimi naitakidi kwamba, yote hayo yametokana na Banu Umayyah ambao walimpenda bibi Aisha na wakamtukuza pale alipoyatumikia maslahi yao na akawatengenezea riwaya za yale wayapendayo, pia alimpiga vita adui yao Ali ibn Abi Talib (a.s). Mimi naamini kwamba, Mtume **(s.a.w.w)** hakuwa akimpenda Aisha kutokana na hayo aliyomtendea, kama tulivyotangulia kueleza!! Basi itakuwaje Mtume wa Mwenyezi Mungu ampende mtu ambaye ni muongo, anateta, kufitinisha na kumtilia mashaka Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kuwadhania kuwa wanafanya dhulma? Itakuwaje basi Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** ampende mtu ambaye anampeleleza na anatoka nyumbani mwake bila ruhusa ya Mtume ili tu atake kufahamu Mtume anakwenda wapi?

Itakuwaje kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ampende mtu ambaye anawatukana wakeze mbele yake japokuwa wamekwisha kufa? Ni vipi Mtume atampenda mtu ambaye anamchukia mwanawe Ibrahim na kumsingizia mama wa Ibrahim bibi Mariyah kuwa katenda dhambi?" Ni vipi Mtume wa Mwenyezi Mungu atampenda mtu anayejiingiza kati ya Mtume na wakeze kwa kuzua uongo na mara nyingine kueneza chuki na kusababisha Mtume kuwataliki wakeze? Itakuwaje basi Mtume wa Mwenyezi Mungu ampende mtu ambaye anamchukia binti yake Fatmah, na anamchukia nduguye Mtume na mtoto wa ami yake Ali ibn Abi Talib kiasi kwamba (bibi Aisha anashindwa kulitamka jina la Imam Ali, na wala tu nafsi yake haimfurahii Ali kwa wema. Yote haya na zaidi ya haya yalifanyika katika zama za uhai wa Mtume **(s.a.w.w)**, ama baada ya kufa kwake, na ni haki yasimuliwe wala hapana ubaya. Matendo yote haya Mwenyezi Mungu na Mtume wake waliyachukia na wala hawakumpenda aliyeyatenda, kwani Mwenyezi Mungu yeye ndiye haki na Mtume wake

alikuwa akiitekeleza haki hiyo, hivyo basi hawawezi kumpenda mtu asiyekuwa kwenye haki.

Hapo baadaye kwa kupitia utafiti uliotangulia tutafahamu kwamba, Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** alikuwa hampendi Bibi Aisha, bali alipata kuutahadharisha ummati wake kutokana na fitina ya bibi Aisha. Kuna wakati fulani niliwauliza baadhi ya Masheikh sababu za Mtume **(s.a.w.w)** kumpenda kupita kiasi Bibi Aisha peke yake kuliko wake wengine, walinipa majibu mengi na yote hayo hayakuwa na maana yeyote. Mmoja wao alisema: "Kwa kuwa Aisha alikuwa mzuri kisha mdogo na ndiye bikra pekee ambaye Mtume alimuoa na nakushirikiana na mwingine kwa bibi Aisha ila yeye Mtume peke yake". Mwingine akasema, "Kwa kuwa alikuwa ni binti ya Abubakris -Sidiq ambaye alikuwa pamoja na Mtume pangoni". Wa tatu alisema: "Hiyo ni kwa sababu Mama Aisha alihifadhi nusu ya dini kutoka kwa Mtume, kwa hiyo ni mjuzi mwenye kufahamu". Na wanne alisema, "Ni kwa sababu Jibril alipata kuja akiwa katika sura yake (bibi Aisha) na Jibril alikuwa haji kwa Mtume ila Mtume awapo nyumbani kwa Aisha".

5

# WAULIZE WANAOFAHAMU

Kama uonavyo ewe msomaji kwamba, madai yote hayana ushahidi wowote na wala akili na ukweli ulivyo havikubaliani. Sisi tutaleta ushahidi ili kuyatengua (madai hayo). Kama Mtume **(s.a.w.w)** alikuwa akimpenda kwa kuwa yeye ni mzuri na kuwa yeye ni bikra pekee aliyepata kumuoa, basi ni jambo gani lililomzuwia Mtume kuowa wanawake bikra na wazuri ambao walikuwa bora kwa wema na uzuri na walikuwa wakipigiwa mfano (kwa uzuri) katika makabila ya Kiarabu wakati yeye Mtume alikuwa akiwafahamu' Na juu ya hayo wanahistoria wanautaja wivu wa Aisha kwa Zainab binti Jah-shi na Safiyyah binti Huyayi na Mariyah Al-Qibtiyyah kwa sababu wao walikuwa wazuri zaidi kuliko yeye. Ibn Saad ndani ya Tabaqat yake Juzuu ya 8 uk.148 na Ibn Kathir katika tarekh yake wameleta riwaya kwamba, Mtume **(s.a.w.w)** alimuoa Mulaikah binti Ka'b, na bibi huyu alikuwa akifahamika kwa ubora na uzuri, basi Aisha akamwendea bibi huyu (nyumbani kwake) kisha akamwambia: "Hivi huoni haya kuolewa na mtu ambaye amemuua baba yako?" (Kutokana na ushawishi huu) bibi yule akamwambia Mtume: "Najilinda kwa Mwenyezi Mungu kutokana nawe." (Neno hilo likamchukiza) Mtume **(s.a.w.w)** akamtaliki bibi huyo, kisha jamaa zake wakaja kwa Mtume **(s.a.w.w)** wakamwambia "Huyu ni mtoto mdogo naye hana hiyari, kwa hakika amehadaiwa mrejee" Mtume **(s.a.w.w)** akakataa, na baba wa binti huyu aliuawa siku ya Fat-hi Maka, aliuawa na Khalid ibn Walid mahala paitwapo Khindimah.

Riwaya hii inatujulisha wazi kwamba makusudio ya Mtume wa Mwenyezi Mungu haikuwa kuoa mabinti wadogo tena wazuri, vinginevyo (kama malengo yake yangekuwa ni kuoa watoto wadogo tena wazuri) asingeachika Mulaikah binti Ka'b hali yakuwa ni msichana mdogo na bora tena mzuri kama ambavyo riwaya hii na nyinginezo zinavyotuonesha njia alizozitumia Aisha kuwahadaa wanawake waumini wasio na kosa lolote na (kusababisha) wasiolewe na Mtume wa Mwenyezi Mungu? Na (huyu bi Mulaikah) alitanguliwa na kuachika kwa As-ma binti Nuuman pale Aisha alipomuonea wivu akamwambia kuwa: "Mtume humfurahia sana mwanamke pindi akiingia kwake akamwambia, najilinda kwa Mwenyezi Mungu kutokana nawe." (Bibi Aisha pia) anamchochea huyu bi Mulaikah hisia za mauaji ya baba yake na kwamba aliyemua ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na anamwambia, "Huoni haya kuolewa na mtu aliyemuua Baba yako?" Maskini binti huyu hakuwa na jawabu lolote isipokuwa ni kumchukia Mtume wa Mwenyezi Mungu, unadhani angejibu nini binti huyo wakati ambapo watu walikuwa bado wapo kwenye zama za ujinga na wakichukua kisasi na kumcheka asiyechukua kisasi kwa ajili ya baba yake? Kilichobaki tujiulize na tunayo haki ya kujiuliza, Ni kwa nini Mtume **(s.a.w.w)** aliwaacha wanawake hawa wawili bila kosa lolote na ambao walikuwa muhanga wa vitimbi na hadaa za Aisha?

Kabla ya kufanya kitu cho chote, hatuna budi tufahamu katika akili zetu kwamba, Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** ni Maasum (hafanyi dhambi) na wala hamdhulumu yeyote wala hafanyi ila ni haki, basi (kama ni hivyo) hapana budi kwa kuwataliki (kina mama hao) kuna hekima ambayo

Mwenyezi Mungu na Mtume wake ndiyo wanaoifahamu kama ambavyo Mtume hakumtaliki Aisha pamoja na matendo yake, vile vile kuna hekima yake. Pengine huenda tunaweza kuwa na msimamo wa jambo fulani katika hekima hiyo katika uchambuzi ufuatao. Ama kwa upande wa yule mwanamke wa kwanza ambaye ni Asma binti Nuuman, bila shaka kutotumia kwake busara kunadhihirika pale hila za Aisha zilipomchemsha, basi neno lake la kwanza alilomkabili nalo Mtume wa Mwenyezi Mungu wakati alipomnyooshea mkono wake likawa "Ninajilinda kwa Mwenyezi Mungu kutokana nawe". Pamoja na uzuri wake na ubora wake Mtume hakumbakisha kutokana na ujinga wake (wa kutofikiri). Ibn Saad na wengineo anasema ndani ya Tabaqat yake Juz.8 uk.145.

Imepokewa kutoka kwa ibn Abbas amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu alimuoa Asma binti Nu'uman na (bibi huyu) alikuwa mzuri mno miongoni mwa wanawake wa zama zake na alikuwa ametimia." Basi huenda Mtume **(s.a.w.w)** alitaka kutufundisha kwamba akili pevu ni bora kuliko uzuri, kwani ni mara ngapi mwanamke mzuri ujinga wake umempelekea kufanya uchafu?.

Ama kwa upande wa yule mwanamke wa pili ambaye ni Mulaikah bint Ka'ab aliyebeuliwa na Aisha kwa kuambiwa kuwa mumewe ndiye aliyemuua baba yake, Mtume hakutaka mwanamke huyu maskini (ambaye alikuwa na umri mdogo asiye na uamuzi kama walivyoshuhudia hayo jamaa zake aishi pamoja na) Aisha mwenye vitisho na mawazo yaliyo komaa mambo ambayo huenda yangesababisha matatizo makubwa hasa hasa kutokana na Aisha ambaye asingempa nafasi ya kufurahi na Mtume **(s.a.w.w)**. Na hapana shaka kwamba zipo sababu nyingine ambazo Mtume wa Mwenyezi Mungu anazijuwa na kwetu zimefichikana. Jambo la muhimu ni kufahamu kwamba, Mtume **(s.a.w.w)** alikuwa havutiki kwa uzuri na matamanio ya mwili na kijinsiya kama walivyodhania baadhi ya watu wajinga na baadhi ya Mustashrikina[58] ambao wanasema eti lengo la Muhammad lilikuwa ni kujipatia wanawake wazuri. Kwa hakika tumeona jinsi gani Mtume wa Mwenyezi Mungu alivyowataliki wanawake hawa wawili bila kujali udogo wao na uzuri wao, kwani walikuwa wazuri mno katika zama zao kama ilivyoandikwa katika vitabu vya historia na vitabu vya hadithi. Kwa hiyo kauli ya anayedai kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa akimpenda Aisha kwa umri wake mdogo na uzuri wake inapingwa na haikubaliki. Ama wale wasemao kwamba Mtume alimpenda Aisha kwa sababu ni binti ya Abubakr, jambo hili siyo sahihi, lakini tunaweza tu kusema kwamba Mtume alimuoa Aisha kwa sababu ya Abubakr, kwa kuwa Mtume aliwaoa wanawake kutoka katika makabila mbali mbali kwa sababu za kisiasa ili kuziunganisha nyoyo (za watu hao) na kuyaelekeza mapenzi na huruma kwa makabila hayo badala ya (kueneza) ugomvi na chuki. Hapana shaka kwamba Mtume alimuoa dada yake Muawiyah, Ummu Habibah binti Abi Sufiyan, wakati ambapo huyu Abu Sufiyan alikuwa ni adui namba moja wa Mtume **(s.a.w.w)** na alifanya hivyo kwa kuwa yeye (Mtume) siyo mtu mwenye chuki pia yeye ndiye rehma kwa walimwengu. Huruma na upole wa (Mtume **s.a.w.w**) vilivuka kutoka kwenye makabila ya Kiarabu mpaka akafikia hadi ya kuwaolea Mayahudi

na Wakristo na hata Waqibt (wa Misri) ili awaunganishe watu wa dini wao kwa wao.

Jambo muhimu linalotupasa sisi kulifahamu kupitia maarifa tuyasomayo ndani ya vitabu vya Sira ni kwamba Abubakr ndiye aliyemtaka Mtume **(s.a.w.w)** amuoe binti yake Aisha, kama ambavyo Umar naye alimtaka Mtume **(s.a.w.w)** amuowe binti yake Hafsah, Mtume **(s.a.w.w)** alikubali kwani moyo wake uko wazi kuwaenea walimwengu wote. Mwenyezi Mungu anasema:

وَلَوْ كُنتَ فَظًّا غَلِيظَ الْقَلْبِ لَانفَضُّوا مِنْ حَوْلِكَ ﴿١٥٩﴾

"Na lau ungekuwa (wewe Muhammad) ni mkali na mwenye moyo mgumu bila shaka wangekukimbia." (Qur'an, 3:159).

Tukizirejea riwaya ambazo amezitaja Aisha na akasema katika riwaya hizo kwamba, "Mtume **(s.a.w.w)** hakukaa muda mrefu ila alidhani kuwa nimepitiwa na usingizi, akachukua nguo yake taratibu na akafungua mlango akatoka kisha akaufunga." Basi tunafahamu uongo wa madai ya kwamba Mtume alikuwa hawezi kuvumilia kwa kumkosa Aisha.

Matokeo ya utafiti huu siyo natija ya kubahatisha iliyoundwa kimawazo tu (bila ushahidi) sivyo kabisa, bali inao ushahidi ndani ya vitabu vya Kisunni. Muslim ameandika riwaya ndani ya Sahih yake, na wengineo ndani ya Sihah zao za Kisunni kwamba, Umar ibn Khatab amesema, "Wakati Mtume wa Mwenyezi Mungu alipojitenga mbali na wakeze, niliingia msikitini nikawakuta watu wakiwa wanawaza na wanasema, Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amewataliki wakeze, na tukio hili lilitokea kabla hawajaamriwa kuwa na hijab, basi Umar akasema, hapana budi nilitambue jambo hilo leo. Akasema, nikaingia kwa Aisha nikamwambia, Ewe binti Abubakr hivi hadhi yako imefikia kiasi cha kumuudhi Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**"?

Aisha akasema, "Ewe Mwana wa Khatab kuna uhusiano gani kati yangu na wewe kamuulize binti yako" Omar akasema: "Nikaingia nyumbani kwa Hafsah binti Umar nikamwambia, Ewe Hafsah hivi hadhi yako imefikia kiasi cha kumuudhi Mtume wa Mwenyezi Mungu, Wallahi bila shaka wewe unajua kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu hakupendi na lau siyo mimi Mtume wa Mwenyezi Mungu angekwisha kukuacha, Hafsah akalia sana" Bila shaka riwaya hii inatujulisha wazi kwamba hapana shaka kuwa Mtume **(s.a.w.w)** alimuoa Hafsah binti Umar si kwa sababu ya kumpenda, lakini ni kwa maslahi ya kisiasa ambayo hali halisi ilipelekea iwe hivyo. Miongoni mwa mambo yanayotuongezea uhakika wa kukubalika kwa mtazamo tulionao katika kuyapata matokeo mazuri ya uchambuzi huu ni kwamba, Umar ibn Khatab anamuapa Mwenyezi Mungu kuwa Mtume **(s.a.w.w)** hampendi Hafsah, na Umar anatuongezea uhakika tena kwamba binti yake Hafsah yeye pia anafahamu ukweli huu wenye uchungu, pale alipomwambia, "Wallahi hakika wewe unafahamu kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu hakupendi." Basi baada ya hayo hakuna shaka yoyote inayobakia kwetu sisi kwamba kuolewa kwa Hafsah kulikuwa ni kwa ajili ya maslahi ya kisiasa (hasa) pale Umar aliposema: "Lau si mimi Mtume wa Mwenyezi Mungu angekwisha kukuacha."

Kwa hiyo riwaya hii inatufanya tuifikirie vile vile sababu iliyomfanya Mtume kumuoa Aisha binti Abubakr na kuonesha kwamba Mtume alisubiri

na akavumilia maudhi yote ya Aisha kwa ajili ya Abubakr, vinginevyo kwa Hafsah itakuwa ni afadhali zaidi Mtume ampende yeye kwani hapakuwa na mambo mengi yaliyotokana naye aliyoyafanya kumuudhi Mtume, tena kwa kiwango kikubwa kuliko mambo aliyoyatenda Aisha binti Abubakr. Na tukiuchunguza ukweli halisi na tukazipuuza riwaya zilizozushwa ambazo Banu Umayyah wamezitengeneza kuhusu ubora wa Aisha, bila shaka tutakuta kwamba, Mtume wa Mwenyezi Mungu mara nyingi alikuwa akikerwa na Aisha na mara nyingi alikuwa akimgombeza. Hapa tunanakili riwaya moja aliyoiandika Bukhari na wanachuoni wengi wa hadithi wa Kisunni inayoeleza kiwango cha kero ambayo alikuwa akiionesha Ummul-Muuminina Aisha mbele ya mumewe (ambaye ni) Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**. Bukhari amethibitisha ndani ya Sahih yake katika juzuu ya saba katika mlango wa "Kauli ya mgonjwa, hakika ninaumwa, au Eeh kichwa changu. " Amesema: Nilimsikia Qasim ibn Muhammad amesema: "Aisha alisema, Eeh, kichwa changu!" Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema, "Lau hali hiyo ingekupata nami nikawa ni hai basi ningekutakia msamaha na kukuombea dua" Aisha akasema,"Ole wangu, Wallahi hakika nikuonavyo wewe (naona) unapenda nife, na lau nitakufa bila shaka jioni (usingejali bali) ungeendelea kufurahi na baadhi ya wake zako." Je, riwaya hii inakujulisha juu ya Mtume kumpenda Aisha?

Mwisho tunafupisha (kwa kusema) kwamba, hakika Banu Umayyah wakiongozwa na Muawiya ibn Abi Sufiyan wanamchukia Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**, na tangu pale Ukhalifa ulipowazungukia walifanya (kila njia) kuubadilisha ukweli kinyumenyume, wakawapandisha (kwa ubora) watu fulani fulani mpaka wakawafikisha kwenye daraja la kusifiwa na kutukuzwa, wakati ambapo (watu hao) katika zama za uhai wa Mtume **(s.a.w.w)** walikuwa ni watu wa kawaida tu wala hawakuwa na lolote la maana. Na wakati huo huo Banu Umayyah waliwanyanyasa watu wengine ambao walikuwa katika daraja tukufu na yenye heshima katika siku za uhai wa Mtume **(s.a.w.w)**. Mimi naamini kwamba, kipimo chao pekee katika kuwapandisha daraja baadhi ya watu na kuwanyanyasa wengine hakuna isipokuwa ni ule uadui wao mkali na chuki yao isiyo na kipimo dhidi ya Mtume Muhammad na watu wa nyumba yake (ambao ni) Ali, Fatmah, Hasan na Husein (a.s). Na kwa hali hiyo kila mtu ambaye alikuwa mpinzani wa Mtume **(s.a.w.w)** na watu wa nyumba yake ambao Mwenyezi Mungu amewaondolea uchafu na amewatakasa sana sana, Banu Umayyah walimpandisha daraja na kumtengenezea riwaya na ubora kemkem, walimkumbatia na kumpa vyeo na zawadi nyingi na hatimaye akawa mwenye hadhi kwa kutukuzwa na watu na kuheshimiwa.

Ama kila yule aliyekuwa akimpenda Mtume **(s.a.w.w)** na akimtetea, wao walifanya kila juhudi kumuangusha na kumzushia maovu ya uongo na kumtengnezea riwaya ambazo zinakanusha heshima yake na ubora wake. Kwa hakika hali kama hii ndiyo iliyomfanya Umar ibn Khatab akawa ndiyo kiongozi mkuu wa Uislamu katika zama za utawala wa Banu Umayyah, Umar ambaye alikuwa akimpinga Mtume **(s.a.w.w)** katika kila maamrisho yake mpaka akamtuhumu Mtume **(s.a.w.w)** kwamba anaweweseka wakati wa mwisho wa uhai wake Mtume **(s.a.w.w)**.

Ama Ali ibn Abi Talib ambaye kwa Mtume **(s.a.w.w)** alikuwa na cheo kama kile cha Nabii Harun kwa Nabii Musa, na ambaye alikuwa akimpenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Mwenyezi Mungu na Mtume wake wakimpenda (Ali) ambaye ni mtawala wa kila muumini, zilipofika zama za utawala wa Banu Umayyah akawa analaaniwa kwenye Minbar za Waislamu kwa muda wa miaka themanini. Hali kama hii (katika dola ya Banu Umayyah) Aisha ambaye alimsonga koo Mtume **(s.a.w.w)** na akaasi amri zake nyingi kama ambavyo (kwa kumuasi Mtume) alimuasi Mola wake na akampiga vita wasii wa Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na kwa fitina yake hiyo kubwa ambayo Waislamu waliifahamu, alisababisha mauaji ya maelfu ya Waislamu. basi mwanamke huyu akawa ndiyo mwanamke mashuhuri katika Uislamu na eti watu wajifunze kwake hukumu za dini. Ama bibi Fatmah Zahra mwanamke bora ulimwenguni, ambaye Mwenyezi Mungu Mtukufu hukasirika pindi Fatmah anapokasirika na huwa radhi Mwenyezi Mungu pindi Fatmah anapokuwa radhi, huyu akawa ni mtu aliyesahauliwa kabisa, kiasi kwamba alipofariki alizikwa usiku tena kwa siri. Na kabla ya hapo alitishiwa kuchomwa moto, na walimkamua tumbo lake kwa kumbana na mlango mpaka ujauzito ukampromoka, na kutokana na mazingira haya hakuna hata Muislamu mmoja katika Masunni anayefahamu japo riwaya moja aliyoipokea Fatmah kutoka kwa baba yake.

Hali ni hiyo hiyo (kwa shinikizo la Banu Umayyah) Yazid ibn Muawiyah na Ziyad mwana wa baba yake na mwana wa Mar-wan na Haj-Jaj na mwana Al'as na wengineo miongoni mwa waovu waliolaaniwa kwa mujibu wa Qur'an kupitia ulimi wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, wote hawa wakawa ndiyo viongozi wa waumini na watawala wa mambo yao. Ama Hassan na Husein ambao ni mabwana wa vijana wa peponi na ni kiliwazo cha Mtume katika umma huu na ambao ni Maimamu wanaotokana na kizazi cha Mtume **(s.a.w.w)** ambao ndiyo ngome ya umma huu, wao wakawa ni wenye kufukuzwa, kutiwa magerezani na kuuawa kwa kutiliwa sumu. Mazingira ni yale yale, yule mnafiki Abu Sufiyan ambaye hapana vita yoyote iliyotokea dhidi ya Mtume isipokuwa yeye alikuwa ni kiongozi wa vita hiyo, huyu akawa mwenye kusifiwa na kushukuriwa mpaka ikasemwa eti Mtume kasema: "Yeyote atakayeingia ndani ya nyumba ya Abu Sufiyan atakuwa katika amani."

Kinyume chake Bwana Abu Talib ambaye ni mlezi wa Mtume **(s.a.w.w)** na alimlinda Mtume kwa uwezo wake wote, na yeye ndiye aliyetumia uhai wake akiwapinga jamaa zake na watu wake kwa ajili ya kufanikisha mwito wa mtoto wa nduguye kiasi kwamba aliishi miaka mitatu ndani vikwazo vya kiuchumi pamoja na Mtume kwenye viunga vya mji wa Maka, na aliificha imani yake kwa ajili ya maslahi ya Uislamu, ili tu zipatikane njia za yeye kuwa pamoja na Maquraish wasiwaudhi Waislamu kwa namna wanavyotaka, na hilo ni kama ilivyokuwa kwa yule Muumini wa jamaa ya Firaun aliyeficha imani yake, Abu Talib huyu malipo yake yakawa eti yumo ndani ya moto wenye joto hafifu na akiweka humo mguu wake mafuta yaliyoko katikati ya mifupa yake yatachemka. Kadhalika hali ni hiyo hiyo kwa Muawiya ibn Abi Sufiyan, ambaye ni muachwa huru mwana wa muachwa huru na ni mwenye kulaaniwa mwana wa aliyelaaniwa, mtu ambaye lizichezea hukumu za Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na wala

hakuzipa uzito unaostahiki, ambaye aliwauwa watu wema wasio na kosa lolote ili tu apate kuyatimiza malengo yake maovu, mtu ambaye alimtukana Mtume wa Mwenyezi Mungu mbele ya macho na masikio ya Waislamu, mtu huyu akawa anaitwa ndiye mwandishi wa wahyi, na wanasema eti kwamba Mwenyezi Mungu amewaamini juu ya wahyi wake Jibril, Muhammad na Muawiyah, huyu akawa husifiwa kuwa yeye ni mwenye hekima, siasa na mnadhimu bora. Watu kama Abu Dharri Al-ghifari ambaye hapakuwepo mkweli kuliko yeye, huyu akaonekana kuwa ndiyo mwenye fitina. akapigwa na kufukuzwa na kuondolewa mjini Madina akapelekwa "Rabdhah."

Nao Salmaan Al-Farisi, Miqdad, Ammar, Hudhaifah na Masahaba wote wema ambao walimtawalisha Ali na wakamfuata, kwa hakika walipambana na mateso na walitawanywa ovyo na kuuawa. Kutokana na mazingira haya basi, wafuasi wa Makhalifa, wafuasi wa Muawiyah na wafuasi wa madhehebu ambayo yaliundwa na tawala za kidhalimu, wao ndiyo waitwao "Ahl-lus-sunnah Wal-jamaa" ambao (kwa mtazamo wao)wanajiona kuwa ni wao pekee ndiyo wanaoutekeleza Uislamu ipasavyo na yeyote anayewapinga wanamuona kuwa yu miongoni mwa makafiri, hata kama atakuwa ni mfuasi wa Maimamu wema wa nyumba ya Mtume waliotakasika. Ama wafuasi wa Maimamu wa nyumba ya Mtume **(s.a.w.w)**, ambao wamemfuata (Ali) ambaye ni mlango wa elimu na mtu wa kwanza kusilimu, ambaye haki huzunguka pamoja naye popote alipo, na wakawafuata watu wa nyumba ya Mtume **(s.a.w.w)** ambao ni Maimamu Maasum, basi hawa wakawa ndiyo (huitwa) watu wa bid'a na upotofu, na yeyote mwenye kuwapinga na kuwapiga vita huyo ndiyo Mwislamu sawa sawa. "Lahaula wala quwwata illa billahil-aliyyil-adhim. " Amesema kweli Mwenyezi Mungu pale aliposema:"Na wanapoambiwa, msifanye uharibifu ulimwenguni wao husema, Sisi ni watenda mema, Hakika wao ni waharibifu lakini hawatambui. Na wanapoambiwa aminini kama walivyoamini watu, husema, Oh hivi sisi tuamini kama walivyoamini wapumbavu". Hakika wao ndiyo wapumbavu lakini hawatambui" (Qur'an 2:11-13).

6

# WAULIZE WANAOFAHAMU

Na tukirejea kwenye maudhui ya Mtume **(s.a.w.w)** kumpenda Aisha kwa kuwa eti alihifadhi kutoka kwa Mtume nusu ya dini, na yeye Mtume alikuwa akisema, "Chukuweni nusu ya dini yenu kutoka kwa kijanajike hiki chekundu". Hadithi hii haifai wala haina msingi wowote wa kusihi kwake, wala haiwezi kulingana na hadithi ambazo zimepokewa kutoka kwa yeye Aisha (akielezea) miongoni mwa hukumu zinazochekesha na kuhuzunisha, hadithi ambazo (ukweli ulivyo) Mtume wa Mwenyezi Mungu kamwe hakuzisema. Basi hebu na tutosheke na mfano mmoja juu ya hayo unaohusu suala la kumnyonyesha mtu mzima, hadithi ambayo Aisha alikuwa akiieleza kuwa imetoka kwa Mtume **(s.a.w.w)** na ni hadithi ambayo Muslim ameithibitisha ndani ya Sahihi yake, na Maliki naye ndani ya Muwatta yake na ni hadithi ambayo tumetosheleza juu ya uchunguzi wetu kuhusiana nayo ndani ya kitabu chetu "Liakuna Maas-Sadiqin" basi atakaye ufafanuzi na uthibitisho wa uwazi wa mambo na akirejee kitabu hicho. Na itoshe tu kuhusu riwaya hii mbaya ya kwamba wakeze Mtume wote waliyapinga matumizi yake na wakaikanusha mno kiasi kwamba hata huyo aliyeipokea alibakia kwa mwaka zima anaogopa kuitaja kutokana na ubaya wake na kutokuwa na haya. Na tutakapoirejea Sahihi Bukhari katika mlango usemao, "Sala hupungnzwa mtu akitoka nyumbani mwake " amesema: Kutoka kwa Az-zuhri, naye kutoka kwa Ur-wah, amepokea toka kwa Aisha (r.a) amesema: "Hapo mwanzo Sala ilifaradhishwa rakaa mbili, Sala ya safari ikabakishwa (kuwa rakaa mbili) na Sala isiyo ya safari ikakamilishwa (kuwa rakaa nne). Az-Zuhri akasema nikamwambia Ur-Wah, mbona Aisha anakamilisha (rakaa nne katika safari)? Akasema, Anabadilisha kama alivyobadilisha Uthman" Riwaya hii ameithibitisha Muslim ndani ya Sahihi yake katika mlango wa Sala ya wenye safari na kuipunguza.

Kwa maelezo yaliyowazi zaidi ni kama ilivyo ndani ya Bukhari amesema: "Imepokewa kutoka kwa Az-zuhri, naye kutoka kwa Ur-wah naye kutoka kwa Aisha kwamba, hapo mwanzo Sala ilifaradhishwa rakaa mbili, basi Sala ya safari ikabakishwa kuwa rakaa mbili na Sala isiyo ya safari ikakamilishwa (kwa rakaa nne) Az-zuhri akasema, nikamuuliza Ur-wah mbona Aisha anakamilisha (rakaa nne) katika safari? akasema: "Amebadilisha kama alivyobadilisha Uthman." Bila shaka ni kupingana kuliko dhahiri, yeye mwenyewe bibi Aisha ndiye aliyepokea kwamba Sala ya msafiri ilifaradhishwa rakaa mbili, lakini ni yeye huyo huyo anafanya kinyume cha vile alivyofaradhisha Mwenyezi Mungu na alivyofanya Mtume wake, na anabadilisha na kuzigeuza hukumu za Mwenyezi Mungu na Mtume wake ili aimarishe sunna ya Uthman, na kwa sababu hizi basi tunakuta ndani ya Sihah za Ahlis-Sunnah wal-jamaa mna hukumu nyingi lakini hawazitumii kwa kuwa wao mara nyingi wanatumia (hukumu) zilizoanzishwa na Abubakr na zile zilizoanzishwa na Ummar, Uthman, Aisha na zile alizoanzisha Muawiyah ibn Abi Sufiyan na Masahaba wengineo. Sasa basi iwapo kijanajike hiki chekundu ambacho kwake inapatikana nusu ya dini kinafanya mabadiliko katika hukumu za Mwenyezi Mungu vile kinavyopenda, mimi siamini kwamba mumewe ambaye ni

Mtume wa mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** anakiridhia, na katika hali hiyo awaamuru watu wakifuate. Wakati huo huo kumekuja riwaya ndani ya Sahihi Bukhari na Sihah nyigine za Masunni zikiashiria kwamba, kukifuata (kijanajike chekundu hicho) ndani yake kuna maasi dhidi ya Mwenyezi Mungu, na tutakutosheleza kwa hilo utapofika wakati wake apendapo Mwenyezi Mungu.

Ama wale wasemao kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** alikuwa akimpenda bibi Aisha kwa sababu Jibril alimjia Mtume akiwa na picha ya bibi Aisha kabla hata hajamuoa, na kwamba Jibril alikuwa haingii kwa Mtume ila awapo nyumbani kwa bibi Aisha, riwaya hizi zinawachekesha hata wenda wazimu, kwa sababu mimi binafsi sifahamu iwapo picha hiyo aliyokuja nayo Jibril ilikuwa ni ya Photograph au ya kuchora, wakati ambapo Ahlus-sunna wanazo riwaya kwamba, Abubakr ndiye alimtuma Aisha aende kwa Mtume akiwa na chombo kilichotiwa tende ili tu Mtume amuangalie Aisha, na Abubakr yeye ndiye aliyemtaka Mtume **(s.a.w.w)** amuoe Binti yake huyo, basi je, kulikuwa na haja gani kwa Jibril kushuka na picha yake wakati Mwanaisha anaishi umbali wa mita chache tu kutoka nyumbani kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**? Mimi naamini kwamba bibi Mariyah Al-qibtiyyah aliyekuwa akiishi Misri akiwa mbali na Mtume **(s.a.w.w)** na hapana yeyote aliyekuwa akitazamia kuja kwake, yeye ndiye aliyestahiki kuwa Jibril ashuke na picha yake na ambashirie Mtume **(s.a.w.w)** kwamba Mwenyezi Mungu atamruzuku kutokana naye Ibrahim.

Lakini riwaya hizi ni miongoni mwa uzushi wa Aisha ambaye alikuwa hapati kitu cha kujifaharisha kwa wake wenzi isipokuwa visa ambavyo mawazo yake huvizusha, au riwaya hizo ni katika uzushi wa Banu Umayyah kwa kupitia ulimi wa bibi Aisha ili wapate kuyatukuza mambo yake mbele ya watu wenye akili finyu. Ama kusema kwamba Jibril alikuwa haingii nyumbani kwa Mtume akiwa kalala isipokuwa nyumbani kwa Aisha riwaya hii ni mbaya kuliko ile ya kwanza, kwani kinachofahamika katika Qur'an ni kuwa, Mwenyezi Mungu alimkemea bibi Aisha pale alipokula njama dhidi ya Mtume wake, akamkemea kwa kumjulisha kwamba, "Jibril na Waumini wema na Malaika baada ya msaada wake (Mwenyezi Mungu) watamsaidia (Mjumbe wa Mwenyezi Mungu). Basi kauli za Masheikhe wetu si chochote isipokuwa ni dhana na mawazo yao tu, na kwa hakika dhana haitoshelezi cho chote mbele ya haki, basi waambie je mnayo elimu yoyote ile muitoe kwetu sisi, (hamna) bali hakuna mnachokifuata isipokuwa ni dhana na hamna chochote ila mnazua tu. Aisha baada ya kufariki Mtume **(s.a.w.w)** Ama tunapoyasoma maisha ya Ummul-Muminina Aisha binti Abubakr baada ya mumewe kufariki (roho yangu iwe fidia yake) na baada ya mambo kumkalia vizuri na baba yake kuwa ndiyo Khalifa na kiongozi juu ya umma wa Kiislamu, hapo ndipo bibi Aisha akawa yeye ndiye mwanamke bora katika dola ya Kiislamu kwa kuwa mumewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na baba yake ni Khalifa wa Mtume wa Mwenyezi Mungu.

Kwa kuwa yeye anaamini au anadhani kuwa ndiye mbora miongoni mwa wakeze Mtume **(s.a.w.w)**, si kwa chochote bali kwa kuwa Mtume alimuoa akiwa bikra, na Mtume hakupata kuoa mwanamke bikra ila yeye, kisha Mtume **(s.a.w.w)** alifishwa na yeye bibi Aisha akiwa katika umri wa ujana,

kwani umri wake ulikuwa miaka kumi na minane siku Mtume alipofishwa kwa mujibu wa makadirio ya juu na riwaya zilizo mashuhuri. Na wala hakuishi pamoja na Mtume isipokuwa miaka sita au minane kwa tofauti za riwaya, kwani miaka ile ya mwanzo aliimaliza akicheza michezo ya kitoto hali yakuwa ni mke wa Mtume **(s.a.w.w)** na katika hali hiyo kama alivyomueleza Burairah mjakazi wa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** aliposema kuhusu Aisha: "Hakika yeye ni msichana mdogo akilala na kuuacha unga uliokandwa na matokeo yake huja mnyama miongoni mwa wanyama wafugwao na kula ule unga uliokandwa." Naam miaka kumi na minane kwa msichana aliyefikia umri wa kuvunja ungo kama isemwavyo hivi leo, na aliyetumia nusu ya umri wake akiwa pamoja na Mtume na akiwa miongoni mwa wakewenza wanaofikia kumi au tisa, na (siyo wakeze Mtume tu alioishi nao bibi Aisha nyumbani kwa Mtume) bali kuna mwanamke mwingine ambaye tumeghafilika kumtaja aliyekuwepo katika zama za maisha ya bibi Aisha. Mwanamke huyo alikuwa ni tishio kwa Aisha kuliko mkemwenziwe yeyote, kwani upendo wa Mtume **(s.a.w.w)** kwake ulikuwa hauna mfano naye si mwingine bali ni Fatmah ambaye ni binti ya Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** aliyemzaa kwa bibi Khadija, na Khadija huyu Mkuu ni nani? Huyo ni Khadija ambaye Jibril alimtolea salam na kumbashiria nyumba peponi isiyokuwa na fujo wala makelele Khadija ambaye ilikuwa haiwezekani kupita tukio lolote isipokuwa Mtume **(s.a.w.w)** humtaja Khadija, na hapo ndipo Aisha maini humkata na moyo kumuwaka kwa wivu, kwa hasira zake hufura na kupoteza muruwa wake, akawa hutukana kwa lile aonalo linafaa na bila kujali heshima na uhusiano uliopo kati yake na mumewe.

Hebu na tumsikilize yeye mwenyewe bibi Aisha anasimulia juu ya Khadija kama alivyopokea Bukhari, Ahmad, Tirmidhi na Ibn Majah: Amesema bibi Aisha, "Sikumuonea wivu mke yeyote wa Mtume wa Mwenyezi Mungu kama nilivyomuonea wivu Khadija na hii ni kwa sababu Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa akimtaja mara nyingi na kumsifu, basi nilimwambia (Mtume) ni kwa jambo gani unamtaja ajuza huyu miongoni mwa maajuza wa Kiquraish mwenye kona za midomo myekundu, na amekwisha kufa zamani, hapana Mwenyezi Mungu amekubadilishia mbora kuliko yeye." Bibi Aisha anasema, (ghafla) uso wa Mtume ulibadilika sana na nilikuwa siuoni kubadilika hivyo ila unaposhuka Wahyi na akasema (Mtume): "Wallahi Mwenyezi Mungu hajanibadilishia mke bora kuliko yeye (Khadija), kwa hakika aliniamini wakati watu waliponipinga na alinisadiki wakati watu waliponikatalia na aliniruhusu nitumie mali yake wakati watu waliponinyima na Mwenyezi Mungu aliniruzuku watoto kwake wakati alininyima watoto kwa wanawake wengine." Hapana shaka kwamba jibu la Mtume **(s.a.w.w)** kwa Aisha linabatilisha madai ya wale wasemao kwamba Aisha alikuwa bora mno na akipendwa mno miongoni mwa wake wa Mtume **(s.a.w.w).** Na ubaya zaidi ni kwamba, Aisha aliongeza wivu na chuki kwa Khadija pale Mtume wa Mwenyezi Mungu alipomkemea kwa kemeo hili na akamjulisha kwamba Mola wake hajambadilisha mke bora kuliko Khadija. Ni kwa mara nyingine tena Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** anatufahamisha kwamba yeye hafuati matamanio na wala hapendi (kwa sababu ya) uzuri na bikra, kwani

Khadija [a.s] kabla ya Mtume **(s.a.w.w)** alikuwa kisha olewa mara mbili na alikuwa mkubwa zaidi ya Mtume kwa miaka kumi na mitano, lakini pamoja na hayo Mtume alimpenda mno wala hakuacha kumtaja, na kwa hali hii naapa kuwa hii ndiyo tabia ya Mtume **(s.a.w.w)** ambaye hupenda kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na huchukia kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.

Kwa hiyo basi kuna tofauti kubwa kati ya riwaya hii ya kweli na zile riwaya zilizoundwa ambazo zinadai kwamba Mtume **(s.a.w.w)** alikuwa akimpenda mno Aisha mpaka wakeze wanamtumia ujumbe kumtaka awe muadilifu kuhusu Binti ya Abu Quhafah. Na hebu tumuulize Ummul-Muminina Aisha ambaye hakupata kumuona Bibi Khadija japo mara moja katika uhai wake wala hakukutana naye, ni vipi anamsema kuwa ni kikongwe mwenye kona za midomo myekundu? Na je, hii ndiyo tabia ya mwanamke Muumini wa kawaida ambaye inaharamishwa kwake kumteta mwenzake awapo hai, basi vipi itakuwa hali kwa yule aliyekwisha kufa na kufika mbele ya Mola wake? Basi hali itakuwaje ikiwa mke wa Mtume wa Mwenyezi Mungu ndiye atetwaye, mke ambaye Jibril alikuwa akishuka nyumbani mwake na kumbashiria kupata nyumba yenye utulivu peponi? Na kwa kutilia mkazo ni kwamba, chuki na wivu uliokuwa ukifukuta ndani ya moyo wa Aisha kwa sababu ya Khadija ilikuwa ni lazima ufure na upate mahali pa kupumulia, vinginevyo bibi Aisha angepasuka!! Kwa hiyo basi Aisha hakupata (mahali pa kushushia pumzi zake) isipokuwa hapo mbele yake alikuweko Fatmah binti ya Khadija ambaye ni mtoto wa kambo wa bibi Aisha na ambaye alikuwa katika umri unaolingana naye au anamzidi kidogo kwa (mujibu wa) tofauti ya riwaya. Bila shaka vile vile kwamba lile pendo la kweli la Mtume **(s.a.w.w)** kwa Khadija lilitengenezeka na kuimarika kwa binti yake wa pekee Fatmah, kwani ndiye yeye peke yake aliyeishi pamoja na baba yake akiwa amebeba sifa njema kutoka kwa Khadija ambazo Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa akizipenda, Mtume akawa humwita (Fatmah) mama wa baba yake.

Bibi Aisha alizidi wivu kumuona Mtume wa Mwenyezi Mungu anamtukuza na kumwita kuwa yeye ni mwanamke bora kuliko wanawake wote ulimwenguni na ni mwanamke bora kati ya wanawake wa peponi. Kisha Mwenyezi Mungu akamruzuku Mtume kutokana na Binti yake huyu mabwana wa vijana wa peponi Hasan na Husein, na ndiyo maana Aisha akawa humuona Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** anakwenda kwa Fatmah na kukesha huko kwa ajili ya kuwalea wajukuu zake na anasema: "Wanangu hawa wawili ni viliwazo vyangu katika umma huu." Ikawa huwabeba mabegani kwake, na yote hayo humuongezea Aisha wivu kwa kuwa yeye ni mgumba. Kisha Aisha alizidi wivu mpaka akamuingiza katika wivu huo mume wa Fatmah baba wa Hasan na Husein, si kwa lolote bali ni kwa sababu ya Mtume akimpenda mno mume wa Fatmah na kumtanguliza mbele kuliko baba yake Aisha kwa kila hali, basi hapana shaka kwamba, bibi Aisha alikuwa akiishi katika mazingira haya. Hatimaye anamuona mwana wa Abu-Talib (Ali) anafuzu kila mara dhidi ya baba yake (Aisha) na anakuwa mbele kwa kupendwa na Mtume **(s.a.w.w)** na kumtanguliza juu ya wengine.

Aisha hakika alikuwa akifahamu kwamba baba yake alirudi akiwa ameshindwa katika vita ya Khaibar yeye pamoja na aliokuwa nao katika

jeshi, na kwamba Mtume **(s.a.w.w)** alihuzunishwa na jambo hilo na akasema: "Kesho nitampa bendera mtu ambaye anampenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanampenda mtu huyo, ni shujaa wala si mwoga." Na mtu huyo alikuwa ni Ali ibn Abu Talib mume wa Fatmah, kisha Ali alirudi baada ya kushinda vita ya Khaibar akiwa na Safiyyah binti Huyayi ambaye Mtume **(s.a.w.w)** alimuoa na kwa hilo moyo wa Aisha ukawa kama umepigwa na radi. Kadhalika Aisha alifahamu kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** alimtuma baba yake akiwa na Suratul-Baraah ili akaifikishe (awasomee) Mahujaji, lakini baadaye Mtume alimtuma Ali ibn Abi Talib amfuate na akaichukue kutoka kwa Abubakr, na huyo baba yake Aisha akarudi huku analia na kumuuliza Mtume sababu (ya kumrudisha). Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** akamjibu, "Hakika Mwenyezi Mungu ameniamuru asifikishe Surah hiyo isipokuwa mimi au mmoja katika watu wa nyumba yangu."

Bila shaka vile vile bibi Aisha alikuwa akifahamu kwamba Mtume **(s.a.w.w)** alimtawaza mwana wa ammi yake Ali (a.s) awe ni Khalifa kwa Waislamu baada yake, na akawaamuru Masahaba na wake zao wampongeze kwa kupata uongozi kwa waumini, na baba yake Aisha alikuja akiwa miongoni mwa watu wa mwanzo mwanzo huku akisema: "Pongezi pongezi ewe Mwana wa Abu Talib, leo umekuwa kiongozi wa kila Muumini mwanaume na Muumini wa kike." Bila shaka Bibi Aisha alikuwa akifahamu kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu alimpa uamiri jeshi kijana mdogo mwenye umri wa miaka kumi na saba juu ya baba yake, na Mtume akamuamuru baba yake Aisha aende akiwa chini ya uongozi wa kijana na huyu na aswali nyuma yake. Hapana shaka kwamba Ummul-Muuminina Aisha alijihusisha kikamilifu katika matukio haya, kwani (yaonekana) alikuwa amekamia makusudio ya baba yake ya kugombea Ukhalifa na njama hizo zilikuwa zikipikwa na viongozi wa makabila katika Maquraish. Kwa hiyo basi alikuwa akizidisha chuki na ubaya dhidi ya Ali na Fatmah, na akijaribu kwa kila juhudi kuingilia kati ili kubadilisha msimamo kwa ajili ya maslahi ya baba yake kwa njia mbali mbali na kwa gharama yoyote ile.

Bila shaka tumekwisha muona ni jinsi gani alivyomwita baba yake eti kwa niyaba ya Mtume na akamuamuru aswalishe watu, baada ya yeye Bibi Aisha kugundua kwamba Mtume **(s.a.w.w)** amemwita Ali ili amkabidhi jukumu hilo, na Mtume alipoifahamu njama hiyo alilazimika kutoka (kwenda msikitini) na hapo ndipo Abubakr alipompisha Mtume **(s.a.w.w)** akawasalisha watu hali ya kuwa amekaa, na akamkemea kwa kumwambia. "Hakika ninyi ndiyo wale wanawake waliomfanyia vitimbi Yusuf' akiwa na maana kwamba, Vitimbi vya Aisha ni vikubwa. Na mtu yeyote mwenye kufanya uchambuzi ndani ya tukio hili ambalo bibi Aisha mwenyewe amelisimulia kwa njia ya riwaya zenye kutofautiana na kupingana, atakuta kuna mgongano ulio wazi kwani ilivyo ndivyo ni kwamba Mtume **(s.a.w.w)** alikuwa kisha muandaa baba yake Aisha na kumuamuru atoke katika jeshi chini ya uongozi wa Usamah ibn Zaidi kabla ya kuswaliwa kwa Sala hiyo siku tatu kabla. Inavyofahamika moja kwa moja ni kwamba, kiongozi wa jeshi ndiye Imamu katika Sala, kwa hiyo Usamah alikuwa ni Imam wa Abubakr ndani ya msafara wa jeshi hilo.

Bibi Aisha alipokwishafahamu jambo hilo aliona kuwa ni udhalili kwa baba yake na aliyajua makusudio ya Mtume **(s.a.w.w)**, na hasa alipogundua kwamba Mtume hakumchagua Ali ibn Abi Talib kuwemo ndani ya jeshi hilo ambalo alikuwa ameliandaa ili ndani ya jeshi hilo wawemo vigogo wa Muhajirina na Ansar ambao kwa Maquraish walikuwa ni watu watukufu na wenye daraja kubwa.

Isitoshe mama Aisha alikwisha fahamu kama ambavyo wengi wa masahaba walikwisha fahamu kuwa siku za kuishi Mtume **(s.a.w.w)** zimebakia za kuhesabu, na huenda bibi Aisha aliungana na maoni ya Umar ibn Khattab kwamba sasa Mtume anaweweseka hajui alifanyalo. Kwa sababu hiyo wivu wake mkali ukamlazimisha kufanya vile aonavyo ili mradi tu akinyanyue cheo cha baba yake dhidi ya Ali Bin Abi Talib ambaye ni mgomvi wake.

Kutokana na yote haya ndiyo maana bibi Aisha alikanusha kuwa Mtume aliusia kuwa Ali ni Khalifa, na kwa sababu hiyo alitaka kuwakinaisha watu wenye mawazo finyu kwamba Mtume **(s.a.w.w)** alikufa akiwa amempakata na ameegemea kifuani kwake, na pia ndiyo maana akasimulia kwa kusema kwamba, "Mtume alipokuwa mgonjwa alimwambia (bibi Aisha) niitie baba yako na nduguyo ili niwaandikie maandiko kwani huenda akadai mwenye kudai, na Mwenyezi Mungu na Mtume wake na waumini hawamkubali yeyote isipokuwa Abubakr." Basi Je, kuna mwenye kumuuliza bibi Aisha, "Ni jambo gani lililomzuwia asiwaite?".

7

# WAULIZE WANAOFAHAMU

## MSIMAMO WA AISHA DHIDI YA AMIRUL-MUUMININA ALI (A.S.)

Kwa mtafiti yeyote juu ya msimamo wa bibi Aisha dhidi ya Abul-Hasan Ali (a.s), atakuta mambo ya ajabu na ya kushangaza na hataweza kupata tafsiri yoyote kwa mambo hayo isipokuwa ni wivu na uadui dhidi ya watu wa nyumba ya Mtume **(s.a.w.w)**. Historia imezisajili chuki na bughdha za bibi Aisha kwa Imam Ali, chuki ambazo hazina mfano, na zilifikia kiasi cha bibi Aisha kushindwa hata kulitamka jina la Imam Ali (a.s) na wala hataki hata kumuona, na aliposikia kuwa watu wamempa baia Imamu Ali kuwa Khalifa baada ya kuuawa Uthman akasema: 'Natamani lau mbingu ingeifunika ardhi kabla hajaukalia Ukhalifa mwana wa Abutalib." Hapo ndipo bibi Aisha alipofanya kila njia kumuangamiza Imam Ali na akaongoza jeshi kubwa ili kumpiga Ali (a.s) na hatimaye zilipomfikia habari kwamba Imamu Ali amefariki alisujudu sijda ya kumshukuru Mwenyezi Mungu. Je, kwa nini hamuwashangai pamoja nami Masunni ambao wanasimulia ndani ya vitabu vyao kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Ewe Ali hatakupenda isipokuwa Muumini na hatakuchukia isipokuwa mnafiki"** Kisha wanasimulia ndani ya Sihah zao na Musnad zao na vitabu vyao vya historia kwamba bibi Aisha akimchukia Imam Ali kiasi cha kushindwa hata kulitamka jina lake. Basi je, huo si ushahidi unaotoka kwao juu ya hali halisi ya mwanamke (huyu)? Kama ambavyo Bukhari anavyosimulia ndani ya Sahihi yake kwamba, Mtume **(s.a.w.w)** amesema: "**Fatmah ni sehemu itokanayo nami, yeyote mwenye kumkasirisha (atakuwa) kanikasirisha mimi, na mwenye kunikasirisha mimi basi hakika kamkasirisha Mwenyezi Mungu**."

Kisha Bukhari huyo huyo anasimulia kwamba, Fatmah alikufa hali ya kuwa amemkasirikia Abubakr na mpaka amefariki hakumsemesha. Je, huo sio ushahidi utokanao na wao (Ahlul-Sunnah) kwamba Mwenyezi Mungu na Mtume wake wamemkasirikia Abubakr? Ukweli unafahamika kwa kila mwenye akili. Ndiyo maana Mimi siku zote nasema kwamba, ukweli hapana budi uonekane japokuwa watu waovu watauficha na kwa namna yoyote (ukweli utadhihiri) japokuwa watetezi wa Banu Umayyah watajaribu kuuvuruga, kwani hoja ya Mwenyezi Mungu imesimama juu ya waja wake tangu siku Qur'an iliposhuka mpaka siku ya Qiyama "Kila sifa njema anastahiki kusifiwa Mwenyezi Mungu Mola wa walimwengu. " Imam Ahmad ibn Hambal amesimulia kwamba, "Siku moja Abubakr alikuja na kubisha hodi kwa Mtume **(s.a.w.w)**, na kabla hajaingia aliisikia sauti ya Aisha imeparama juu anamwambia Mtume **(s.a.w.w)**, Wallahi mimi nafahamu kwamba, Ali unampenda mno kuliko mimi na baba yangu." Alikariri maneno hayo mara mbili au tatu.... Mambo ya Aisha na chuki yake dhidi ya Imam Ali yalifikia kiasi kwamba siku zote Aisha alikuwa akijaribu kumtenganisha Ali na Mtume **(s.a.w.w)** kwa njia zozote anazoziweza.

Na amesimulia Ibn Abil-hadid kwamba, Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** siku moja alimsindikiza Imam Ali, basi mazungumzo yao yakawa

marefu, na bibi Aisha alikuwa akija nyuma yao mpaka akaingia katikati yao na akawaambia mnazungumza nini nyie mbona mmerefusha (mazungumzo)? Mtume alikasirika kutokana na (tendo) hilo. Vile vile amesimulia kwamba bibi Aisha wakati fulani alimwendea Mtume **(s.a.w.w)** hali yakuwa anazungumza na Ali, akapiga kelele na akasema, "Kuna nini baina yangu mimi na wewe ewe mwana wa Abutalib? Hakika mimi ninayo siku moja tu kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu." Mtume **(s.a.w.w)** alichukia. Ni mara nyingi bibi Aisha amemchukiza Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** kwa matendo yake yanayotokana na wivu mkali, tabia yake ngumu na maneno yake yanayoudhi. Je, hivi ni kweli Mtume wa Mwenyezi Mungu anamridhia Muumini mwanaume au Muumini wa kike ambaye moyo wake umejaa chuki na bughudha dhidi ya mwana wa ammi yake na Bwana wa kizazi chake ambaye Mtume amesema kumuhusu yeye kuwa, "Anampenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanampenda."

Na akasema Mtume juu ya Ali (a.s). "Yeyote mwenye kumpenda Ali basi bila shaka kanipenda mimi, na yeyote mwenye kumchukia Ali basi bila shaka kanichukia mimi" Tulieni majumbani mwenu wala msioneshe mapambo yenu. Mwenyezi Mungu Mtukufu amewaamuru wakeze Mtume **(s.a.w.w)** watulie majumbani mwao na wala wasitoke hali wamedhihirisha mapambo yao, na akawaamuru wasome Qur'an, wadumishe Sala, watoe Zaka na wamtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake **(s.a.w.w)**. Wakeze Mtume **(s.a.w.w)** wote waliitumia na kuifuata amri ya Mwenyezi Mungu na amri ya Mtume wake ambaye naye aliwakataza wakeze kabla ya kufa kwake na kuwahadharisha aliposema; "Ni nani kati yenu atakayepanda ngamia na watambwekea mbwa wa Hauab?" Wakeze Mtume wote (walifuata amri) isipokuwa Aisha ambaye alivunja amri zote na kupuuza maonyo (ya Mtume **(s.a.w.w)**. Wanahistoria wanaeleza kwamba Hafsah binti Umar alitaka kutoka pamoja na Aisha, lakini nduguye Hafsah Bwana Abdallah alimhadharisha na akamsomea aya (inayohusu katazo la kutoka) basi akavunja azma yake ya kutoka, Amma Aisha yeye alipanda ngamia na wakambwekea mbwa wa Hauab. Twaha Husein ndani ya kitabu chake kiitwacho, "Al-fitnatul-kubra anasema: "**Aisha alipita mahala penye maji, mara mbwa wa mahala hapo wakambwekea na akauliza kuwa maji haya ni ya mahali gani? Akaambiwa kuwa hapo ni Hauab**."

Alitishika sana na akasema; "Nirudisheni, nirudisheni hakika nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akisema na mbele yake walikuwepo wakeze (akatuambia) Ni nani kati yenu atakayebwekewa na mbwa na Hauab? Abdallah ibn Zubair akaja akamtuliza bibi Aisha na akamletea watu hamsini katika Baniamir wakamuapia viapo vya uongo kwamba maji haya siyo maji ya Hauab. Mimi naamini kwamba riwaya hii iliwekwa katika zama za utawala wa Bani Umayyah ili kumpunguzia Ummul-Muuminina uzito wa maasi yake, hali yakuwa wakitegemea kwamba Ummul-Muuminina (Aisha) atasameheka baada ya mtoto wa dada yake Bwana Abdallah ibn Zubair kumhadaa na kumletea watu hamsini wakamuapia kwa Mwenyezi Mungu na kumpa ushahidi wa uongo kwamba maji yale siyo maji ya Hauab. Kwa hakika ni upuuzi mtupu, wanataka (hao Banu Umayyah) kuzipamba riwaya kama hizi kwa watu wenye akili finyu ili wawakinaishe kwamba Aisha

alihadaiwa alipopita kwenye maji hayo na kusikia sauti za mbwa, na hatimaye akaulizia kuhusu mahali hapa na akaambiwa kuwa ni Hauab kisha akatishika na kusema nirudisheni nirudisheni.

Lakini je, watu hawa wapumbavu ambao waliweka riwaya hii wanaweza kumtakia msamaha Aisha katika maasi yake dhidi ya amri ya Mwenyezi Mungu iliyoshuka ndani ya Qur'ani juu ya wajibu wa yeye Aisha kutulia nyumbani mwake au wanaweza kumpa udhuru kwa kukiuka amri ya Mtume wa Mwenyezi Mungu iliyomtaka akae nyumbani mwake na asipande ngamia, kabla ya kufika mahali penye mibweko ya mbwa katika maji ya Hauab? Je, hivi (watu hawa) wanamuona Ummul-Muumina Aisha atasameheka baada ya kupinga nasaha ya Ummul-Muuminina Ummu-Salamah ambaye wanahistoria wanamtaja kuwa alimwambia bibi Aisha (alipoazimia kutoka): "Je, (Aisha) unakumbuka siku Mtume alipofika kwenye maji upande wa kaskazini nasi tukiwa pamoja naye kisha akakaa feragha na Ali akawa anazungumza naye kwa kipindi kirefu, mara wewe ukataka kuwavamia (kwenye mazungumzo yao), mimi nikakukataza ukanipinga na ukawavamia, lakini punde si punde ulirudi huku unalia, mimi nikakuuliza una nini? Ukasema, nimewaendea wakiwa wanazungumza nikamwambia Ali, miye kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu sina isipokuwa siku moja katika siku tisa, basi huniachii siku yangu ewe mwana wa Abu Talib? Mtume amenitazama hali ya kuwa uso wake ni mwekundu amekasirika, kisha akaniambia rudi ulikotoka, Wallahi yeyote hambughudhi (huyu Ali) ila huwa ametoka nje ya imani basi nimerudi hali yakuwa nina juta." Bibi Aisha akasema, "Jambo hilo nalikumbuka." Ummu-Salamah akasema; ninakukumbusha vile vile, tulikuwa mimi na wewe pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** akatuambia: "Nani kati yenu atakayepanda ngamia, na atabwekewa na mbwa wa Hauab? Huyo atakuwa ameacha njia ya sawa." Sote tukasema, Twajilinda kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake kutokana na hilo, kisha Mtume akakupiga mgongoni kwako na akasema, Ole wako ewe kijanajike chekundu, usije kuwa wewe." Aisha akasema "Hilo nalikumbuka.

"Ummu Salama akasema: "Je, unakumbuka siku alipokuja baba yako akiwa pamoja na Umar, nasi tukasimama tukaingia ndani, nao wakapita wakawa wanazungumza na Mtume kuhusu mambo yao mpaka ikafikia wakasema, "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, bila shaka sisi hatufahamu muda utakaoishi pamoja nasi, basi lau utatujulisha ni nani utakayetuachia baada yako kusudi awe ndiyo mategemeo yetu." Mtume akawaambia: "Amma mimi namuona mahala pake, lau nitafanya (kama mtakavyo) mtatofautiana juu ya mtu huyo kama walivyotofautiana wana wa Israil juu ya Haruna." Baba yako na Umar wakanyamaza na kisha wakaondoka, na walipoondoka sisi tukatoka mpaka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, kisha wewe ukamwambia nawe ulikuwa shupavu mno kwake kuliko sisi (ukasema); "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu ni nani basi utakayewaachia?" Mtume akasema, "Ni yule anayeshona viatu." Tukatoka nje tukamuona Ali. wewe ukasema, "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu simuoni isipokuwa Ali." Mtume akasema "**Huyo ndiye**. " Aisha akasema: "Ndiyo nakumbuka jambo hilo.'" Ummu Salamah akamwambia Aisha: "Basi baada ya yote haya ni utokaji gani utokao ewe Aisha"? Aisha

akasema: "**Sitoki kwa jingine lolote isipokuwa kwa ajili ya kuleta mapatano baina ya watu**".

Ummu Salamah akamkataza Aisha asitoke na akamkemea sana, akamwambia, "Bila shaka nguzo ya Uislamu ikipinda hainyooshwi na wanawake na ikivunjika haitengenezwi na wao, ukomo wa sifa za wanawake ni kuinamisha macho na kulinda heshima zao, utasema nini ewe Aisha lau kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu atakuona umepanda ngamia wako unakwenda kutoka kituo hadi kituo kingine, Wallahi lau ningekwenda kwa mwendo wako (huu) kisha nikaambiwa ingia ndani ya pepo ya Fir-daus, hakika ningeona haya kukutana na Muhammad hali yakuwa nimevua hijabu aliyonivalisha. kama ambavyo Aisha Ummul-Muumina hakukubali kusikia nasaha ya masahaba wengi wenye nia njema (pia nasaha ya ummu Salama hakuikubali). Tabari anasimulia ndani ya Tariikh yake kwamba, Jariyah ibn Qud-damah As-suudi alimwambia bibi Aisha, "Ewe Ummul Muuminina, Wallahi kuuawa Uthman ibn Af-fanni ni jambo jepesi kuliko kutoka kwako nyumbani mwako kwenda kupigana hali ya kuwa umepanda ngamia huyu aliyelaaniwa, kwa hakika wewe ulikuwa na sitara kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na umeivua sitara yako na heshima yako umeifedhehesha, kwa hakika anayeona hivi unavyopigana vita basi bila shaka anaona kukuuwa wewe ni sawa tu, basi iwapo umekuja kwetu kwa hiyari yako mwenyewe, basi rudi nyumbani kwako, na ikiwa uumekuja kwa kulazimishwa. basi waombe msaada watu hawa vvakusaidie. Ummul-muuminina Aisha (awa) kiongozi mkuu.

Wanahistoria wanaeleza kuwa, bibi Aisha alikuwa ndiyo kiongozi mkuu, yeye ndiye aliyekuwa akitawalisha (viongozi katika jeshi lake hilo) na kuwauzulu pia kutoa amri zote, mpaka kuna wakati Tal-ha na Zubair walipohitilafiana kuhusu uongozi wa Sala na kila mmoja wao akitaka awasalishe watu, bibi Aisha aliingilia kati na kuwauzulu wote wawili kisha akampa uongozi mtoto wa dada yake (Bibi Aisha) bwana Abdallah ibn Zubair awasalishe watu. Ni yeye bibi Aisha aliyekuwa akituma wajumbe wapeleke barua zake alizokuwa akizisambaza katika miji mingi kuomba msaada dhidi ya Imam Ali ibn Abi Talib na pia akichochea (ndani ya barua hizo) chuki na upinzani wa zama za ujinga. Ilifikia kiwango ambacho alifanikiwa kuandaa jeshi la watu elfu ishirini au zaidi linalotokana na watu wasiofikiri miongoni mwa Waarabu na watu wenye tamaa, (wote hawa) ni kwa ajili ya kumpiga vita na kumuangamiza jemedari wa waumini (Ali ibn Abi Talib). bali alichochea fitina mbaya ambayo ilisababisha watu wengi wauawe kwa kisingizio cha kumtetea Ummul-Muuminina na kumsaidia.

Wanahistoria wanasema kwamba, watu wa Aisha walipomfanyia khiyana Uthman ibn Hunaif aliyekuwa mtawala wa Basra na hatimaye wakamteka yeye na watu wake sabini waliokuwa wakilinda nyumba ya hazina (Baitul-Mali), kisha waliwaleta mpaka kwa Aisha akaamuru wauawe. watu hao walichinjwa kama achinjwavyo mbuzi. Na inasemekana watu hao walikuwa mia nne, na pia inasemwa kuwa ndiyo watu wa kwanza miongoni mwa Waislamu kukatwa shingo zao katika mazingira hayo. As-sha'abi amesimulia kutoka kwa Muslim ibn Abi Bakrah nave toka kwa baba yake amesema: "Wakati Twal-ha na Zubair walipofika Basra mimi nilibeba upanga wangu nikitaka kuwasaidia, nikaenda kwa Aisha nikamkuta anatoa

amri na kukemea, si hivyo tu kumbe mambo yote yalikuwa chini ya mammlaka yake, hapo hapo nikaikumbuka hadithi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** niliyomsikia akisema: Kamwe hawawezi kufanikiwa watu ambao mambo yao yanaendeshwa na mwanamke, pale pale nikaondoka na nikawaacha." Kama ambavyo Bukhari ameandika kutoka kwa Abi Bakrah kauli yake isemayo: "Hakika Mwenyezi Mungu amenipa manufaa ya neno siku ya (vita vya) Jamal, Mtume alipopata habari kwamba Wafursi wamemtawalisha binti ya Kisra akasema: Kamwe hawawezi kufanikiwa watu ambao wamempa mwanamke mammlaka ya mambo yao."

Miongoni mwa mambo yanayochekesha na kumfanya mtu alie kwa wakati mmoja ni kwamba, Aisha Ummul-Muuminina alitoka nyumbani mwake hali ya kuwa anamuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, kisha yeye huyo huyo aliwaamuru Masahaba watulizane majumbani mwao, kwa kweli ni jambo la kushangaza!! Basi yalikuwaje yote haya ewe bwana, je unayajua? Amepokea Ibn Abil-hadid Al-muutazili ndani ya Shar-h Nahjul-balagha na pia wanahistoria wengine wanasema kwamba, Aisha alipokuwa Basra aliandika barua kumuandikia Zaid ibn Sauhan Al-abadi akasema ndani ya barua hiyo: "Kutoka kwa Aisha Ummul-Muuminina binti Abi-bakris-sidiq, mke wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, kwenda kwa mwanawe mpendwa Zaid ibn Sauhan, amma ba'ad. Bakia nyumbani mwako na uwatenganishe watu (wasihusiane) na mwana wa Abu Talib, na (nataka) zinifikie habari nizipendazo kutoka kwako, kwani mimi nakutumainia mno miongoni mwa watu wangu, Was-Salaam." Mtu huyu mwema (Zaid ibn Sauhan) akamjibu mama Aisha kama ifuatavyo: (Barua) kutoka kwa Zaid ibn Sauhan kwenda kwa Aisha binti Abubakr ama ba'ad, bila shaka Mwenyezi Mungu amekuamuru jambo (linalokuhusu) nasi akatuamuru jambo(linalotuhusu) amekuamuru utulizane nyumbani mwako na ametuamuru sisi (tupigane) jihad, kwa hakika barua yako imenifikia ukiniamuru nifanye kinyume cha vile alivyoniamrisha Mwenyezi Mungu, na nitakuwa nimefanya yale Mwenyezi Mungu aliyokuamrisha wewe (kama nitatii amri yako) na wewe umekwisha fanya yale aliyoniamrisha mimi, kwa hiyo mimi siwezi kutii amri yako na barua yako haina jawabu."

Tukio hili linatubainishia kwamba Aisha hakutosheka na uongozi wa jeshi la ngamia peke yake. bali aliazimia kuwa amirijeshi wa waumini wote duniani, na kwa yote haya yeye ndiye aliyekuwa akiwahukumu Talha na Zubair ambao Umar ibn Khatab alikuwa amewapendekeza kwa ajili ya Ukhalifa. sasa basi, bibi Aisha kwa kuutaka uongozi (mkuu) alijihalalishia mwenyewe kuwasiliana na viongozi wa makabila na watawala, akawataka msaada na kuwapa matumaini ya mambo mbali mbali. Kutokana na yote hayo bibi Aisha alifikia daraja hiyo na umashuhuri huo mbele ya Banu Umayyah, akawa yeye ndiye anayetazamwa na kutukuzwa mbele ya wote na pia nguvu zake na upinzani wake vikawa vinaogopewa. Kwa hiyo ikiwa mashujaa na watu mashuhuri miongoni mwa mashujaa wanakimbia na kukwepa safu (ya mapambano) mbele ya Imam Ali ibn Abi Talib na wala hawawezi kusimama mbele yake, cha kushangaza Aisha alisimama kidete akachochea (vita) na kupiga makelele na akatamba. Kutokana na sababu hii basi akili (za watu) zilichanganyikiwa na wanahistoria walioufahamu msimamo wa bibi Aisha katika vita ndogo ya Jamal walishangazwa kabla ya

kufika kwa Imam Ali, na pia katika vita kubwa ya Jamal baada ya kufika kwa Imam Ali na kumtaka mama Aisha arudi kwenye kitabu cha Mwenyezi Mungu (wafanye sulhu), lakini bibi Aisha alikataa na akang'ang'ania vita vipiganwe tena kwa ukaidi ambao hauna tafsiri isipokuwa kama tutaufahamu wivu mkali na chuki ambayo Ummul-Muuminina ameibeba dhidi ya wanawe (Waumini) waliojitolea kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake **(s.a.w.w)**.

Onyo la Mtume **(s.a.w.w)** kwa Aisha na fitina yake.

Bila shaka Mtume **(s.a.w.w)** alikuwa akifahamu kwa undani mipango na njama zilizokuwa zikimzunguka kila upande, na hapana shaka kwamba alifahamu athari na fitina waliyonayo wanawake dhidi ya wanaume, kama ambavyo Mtume **(s.a.w.w)** alifahamu kwamba vitimbi vya wanawake ni vikubwa vinakaribia kung'oa milima. Na hasa alifahamu kuwa mkewe Aisha yeye ndiye muhusika mkuu katika njama hizi za hatari kutokana na wivu na chuki aliyonayo katika nafsi yake dhidi ya Khalifa wake na wasii wake kwa upande mmoja na watu wa nyumbani mwake Mtume kwa upande wa pili. Basi kwa nini Mtume asifahamu hali yakuwa yeye binafsi aliishi katika mazingira (yanayomuonesha wazi) msimamo wa bibi Aisha na uadui wake dhidi yao, kiasi kwamba wakati fulani Mtume alikuwa akikasirika na wakati mwingine uso wake ulikuwa ukimbadilika, na akijaribu mara nyingi kumtosheleza (kumkinaisha) bibi Aisha kwamba ampendaye Ali ni mpenzi wa Mwenyezi Mungu na yule amchukiaye Ali ni mnafiki, na Mwenyezi Mungu anamchukia mtu huyo. Lakini wapi hadithi hizo za Mtume hazikuweza kupenya ndani ya nafsi hizo ambazo hazikuitambua haki kuwa ni haki isipokuwa kwa manufaa yake, na hazikutambua ukweli kuwa ni ukweli isipokuwa ukitokana nazo. Ndiyo maana basi, Mtume **(s.a.w.w)** aliweka msimamo kutokana na kufahamu kwake kwamba (bibi Aisha) yeye ndiyo ile fitina aliyoiweka Mwenyezi Mungu katika umma huu ili aupe mtihani (umma huu) kwa fitina hiyo kama zilivyotahiniwa nyumati zilizotangulia. Mwenyezi Mungu anasema:

الم ﴿١﴾ أَحَسِبَ النَّاسُ أَن يُتْرَكُوا أَن يَقُولُوا آمَنَّا وَهُمْ لَا يُفْتَنُونَ ﴿٢﴾

"Alif Lam Mim, Je watu wanadhani wataachwa (wasitiwe msukosuko) kwa kuwa wanasema tumeamini, basi ndiyo wasijaribiwe. (Qur'an, 29:1-2).

Kwa hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu aliutahadharisha umma wake kutokana na bibi Aisha mara nyingi mpaka siku moja alisimama na akaielekea nyumba ya bibi Aisha akasema: "Hapa ndipo itakapoanzia fitina, hapa ndipo itakapoanzia fitina pale pembe la Shetani litakapochomoza." Bukhari katika Sahih yake ndani ya mlango uliokuja kuzungumzia nyumba za wakeze Mtume amesema: "Imepokewa toka kwa Nafii naye kutoka kwa Abdallah (r.a) amesema: Mtume **(s.a.w.w)** alisimama kuhutubia akaiashiria nyumba ya Aisha akasema: "Hapa ndipo itakapoanzia fitina (mara tatu) wakati pembe la Shetani litakapochomoza."

Kama ambavyo Muslim ndani ya Sahihi yake ameandika mapokezi kutoka kwa Ikrimah ibn Ammar kutoka kwa Salim naye kutoka kwa Ibn Umar amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu alitoka katika nyumba ya Aisha akasema: "**Chanzo cha kufru kitaanzia hapa wakati pembe la Shetani litakapochomoza**". Hakuna mazingatio yoyote kwa nyongeza waliyoiongeza waliposema, "Yaani eti Mtume alikusudia upande wa

mashariki" kwani ni wazi kabisa kwamba tamko hilo limewekwa ili kumpunguzia (mzigo) Ummul-Muuminina na kumuepusha na tuhuma hii. Na imekuja ndani ya Sahihi Bukhari vile vile, amesema: "Wakati Talha, Zubair na Aisha walipokwenda Basra, Imam Ali alimtuma Ammar ibn Yasir na Hasan ibn Ali kisha wakapanda juu ya mimbari, Hasan ibn Ali akapanda juu zaidi kwenye mimbar na Ammar akawa chini ya Hasan, basi sisi tukakusanyika kisha nikamsikia Ammar anasema, Bila shaka Aisha amekwenda Basra na Wallahi yeye ni mke wa Mtume wenu duniani na akhera. Lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu amekupeni mtihani ili ajue je, mtamtii Mwenyezi Mungu au Aisha?" Allahu Akbar!! Habari hii vile vile inajulisha kwamba katika kumtii Aisha ni kumuasi Mwenyezi Mungu na kumuasi Aisha na kusimama dhidi yake ni kumtii Mwenyezi Mungu.

Vile vile tunaona ndani ya hadithi hii kwamba wasimuliaji miongoni mwa Banu Umayyah wameongeza neno jingine katika, "Hakika yeye (Aisha) ni mke wa Mtume wenu duniani na akhera", ili tu wawapotoshe watu wa kawaida kwamba eti Mwenyezi Mungu amemsamehe (Aisha) madhambi yake yote aliyoyatenda na amemuingiza katika pepo yake na kumuozesha kipenzi chake Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** kama sivyo, basi Ammar amefahamu kutoka wapi kwamba Aisha ni mke wa Mtume huko Akhera? Hizi ndizo hila za mwisho walizotumia wazushi miongoni mwa wazushi wa riwaya katika zama za Banu Umayya, kwani kila walipoikuta hadithi inayotajwa sana na watu ambayo hakuna uwezekano wa kuikanusha au kuipinga walikuwa wakifanya makusudi kabisa kuongezea sentensi au neno kwenye hadithi hiyo, au kugeuza baadhi ya matamko yake ili kuipunguza makali au kupoteza maana inayohusika kwenye hadithi hiyo, kama walivyofanya hayo kwenye hadithi isemayo, "Mimi ndiyo mji wa elimu na Ali ndiyo mlango wake na Abubakr ndiyo msingi wake, na Umar ndiyo kuta zake na Uthman ndiyo paa lake." Nyongeza iliyopo kwenye hadithi hiyo haifichikani kwa watu wachunguzi wenye uadilifu, kwani waadilifu na watu wanaochunguza wanaweza kuzitengua nyongeza hizo ambazo sehemu kubwa zinajulisha juu ya ubovu wa akili za wazushi hao na kutokuwa kwao na hekima na mwangaza wa hadithi za Mtume **(s.a.w.w)**.

Hapana shaka kwamba wataiona kauli isemay'o kuwa Abubakr ni msingi wa mji huo, maana yake ni kuwa elimu yote ya Mtume wa Mwenyezi Mungu imetokana na elimu ya Abubakr na hii ni kufru, kama ambavyo kusema Umar ni kuta za mji huo, maana yake ni kwamba Umar yuko pale kuzuia watu kuingia kwenye mji huo, yaani anawazuia kuifikia elimu, na kusema kwamba Uthman ni paa la mji huo, moja kwa moja (kauli) hiyo ni batili, kwani hakuna mji wenye paa na haiwezekani. Kama ambavyo wachunguzi wataona kwamba Ammar anamuapa Mwenyezi Mungu kwamba Aisha ni mke wa Mtume **(s.a.w.w)** duniani na akhera, hii ni kusema mambo wasiyoyajua, basi iweje Ammar aapie kitu asichokijua? Je, anayo aya katika kitabu cha Mwenyezi Mungu inayomjulisha hilo au yeye ndiye aliyeachiwa jukumu hilo na Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**?

Bila shaka usahihi wa hadithi unabakia kuwa Aisha alikwenda Basra, na kwamba yeye ni mke wa Mtume wenu, lakini Mwenyezi Mungu amekupeni mtihani ili apate kubaini iwapo mtamtii yeye Mwenyezi Mungu au Aisha.

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia akili, na kwa akili hizo tukaweza kupambanua haki kutokana na batili, na akatubainishia njia kisha akatutahini kwa mambo mbali mbali ili iwe ni hoja dhidi yetu siku ya malipo.

8

# WAULIZE WANAOFAHAMU

## MWISHO WA UCHAMBUZI

Kilicho muhimu katika uchambuzi wote uliotangulia japokuwa ni kwa mukhtasari ni kwamba, Ummul-Muuminina Aisha binti Abubakr mkewe Mtume **(s.a.w.w)** hakuhesabiwa kuwa miongoni mwa Ahlul-bait ambao Mwenyezi Mungu amewaondolea uchafu na amewatakasa sana sana, na kuwahifadhi kutokana na kila dhambi na baada ya utakaso huo wakawani "Maasum". Na itoshe tu kwamba, bibi Aisha siku za mwisho wa uhai wake alizitumia kwa kilio, huzuni na majuto kwa kukumbuka matendo yake hayo, alikuwa akilia na huenda Mwenyezi Mungu Mtukufu atamsamehe makosa yake, kwani ni yeye peke yake ndiye ajuaye siri ya mpepeso wa macho na yaliyofichikana katika nyoyo za waja wake na ndiye ajuaye ukweli wa nia zao. Hakuna kinachofichikana kwa Mwenyezi Mungu ardhini wala mbinguni, wala mtu mwingine yeyote hataweza kuwahukumia pepo wala moto viumbe wa Mwenyezi Mungu, kwani kufanya hivyo ni kujilazimisha usiloliweza au usilolijuwa. Mwenyezi Mungu amesema:

لِّلَّـهِ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَإِن تُبْدُوا مَا فِي أَنفُسِكُمْ أَوْ تُخْفُوهُ يُحَاسِبْكُم بِهِ اللَّـهُ فَيَغْفِرُ لِمَن يَشَاءُ وَيُعَذِّبُ مَن يَشَاءُ وَاللَّـهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢٨٤﴾

"Vyote vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini ni vya Mwenyezi Mungu, na kama mtadhihirisha yaliyomo ndani ya nyoyo zenu au mtayaficha, Mwenyezi Mungu atakuhisabuni kwa hayo kisha amsamehe amtakaye (kwa kuwa katubia) na amuadhibu amtakaye (kwa kuwa hakutubia) na Mwenyezi Mungu ni mwenye uwezo juu ya kila kitu (Qur'an, 2:284).

Hivyo basi, kwa ajili hii si juu yetu sisi kumtakia radhi bibi Aisha wala kumlaani, lakini tunalazimika kutokumfuata wala kuyabariki matendo yake, na tutazungumza yote hayo wazi wazi ili ukweli ufahamike kwa watu, huenda wakaongoka kwenye njia ya haki. Imam Ali (a.s) amesema: "Msiwe watukanaji wala wenye kulaani, lakini semeni matendo yao yalikuwa kadhaa wakadhaa ili upatikane ushahidi wa kutosha. Kauli ya Ahlud-dhikr juu ya Ahlul-bait. Imam Amirul-Muuminina Ali (a.s) ambaye ni Bwana wa kizazi kitakatifu cha Mtume **(s.a.w.w)** anasema: "Namuapa Mwenyezi Mungu, hakika mimi nafahamu vyema namna ya kufikisha ujumbe, kutimiza miadi, kukamilisha maneno na kwetu sisi watu wa nyumba ya Mtume ndiko kwenye milango ya hekima na mwangaza wa mambo.

Wako wapi wale wanaodai kwamba wao ndiyo waliobobea katika elimu kinyume chetu, ni waongo na ni dhulma dhidi yetu (kudai hivyo) kwani Mwenyezi Mungu ametutukuza sisi na akawatweza wao, akatupa sisi na wao akawanyima, na akatuingiza sisi na wao akawatoa, kwetu sisi ndiko huombwa uongofu na huondoshwa upofu, bila shaka Maimamu wanatokana na Maquraish na wamepandikizwa katika tumbo hili la Hashim, basi haufai Uimamu kwa mwingine asiyekuwa wao na wala haukubaliki utawala kutoka kwa asiyekuwa wao. Sisi ndiyo wenyewe na ndiyo tunaostahiki (uongozi) nasi ndiyo hazina na ndiyo milango (ya kuingilia), hayaingiwi majumba isipokuwa kwa kupitia milango yake, basi yeyote mwenye kuyaendea

majumba bila kupitia milangoni mwake huyo huitwa mwizi." Kisha Imam Ali (a.s) anawataja Ahlul-bait anasema: "**Ndani yao Ahlul Bayt ndimo ulimo utukufu wa Qur'an na wao ndiyo hazina ya wingi wa rehma, watamkapo hutamka kweli na wanaponyamaza siyo kwamba wameshindwa.**"

Wao ndiyo uhai wa elimu na ndiyo kifo cha ujinga, subira yao itakuelezeni upeo wa elimu yao, na kujizuwia kwao kutakuelezeni hekima ya mantiq waliyonayo. Hawaendi kinyume na haki wala hawahitilafiani katika haki, wao ndiyo nguzo za Uislamu na ndiyo matumaini ya amani, kwao wao haki imerudi kwenye asili yake na upotofu umeondoka mahala ulipokuwa na hoja zake nazo zimetoweka. Wameizingatia dini kwa mazingatio ya utambuzi na kuilinda na siyo kwa mazingatio ya kusikia na kuelezwa, kwani wapokezi wa elimu ni wengi lakini walinzi wake ni wachache.

Kizazi cha Mtume ndiyo bora ya vizazi, na ukoo wake ndiyo bora ya koo zote, na mti wake (nasaba) ni bora ya miti, umeota mahala patakatifu na ukachanua mahala pema, una matawi marefu na matunda yasiyoweza kufikiwa. Sisi ndiyo mti wa Utume na kituo cha Utume na mahala wapishanapo Malaika, nasi ni kituo cha elimu na ndiyo chemchem ya hekima, mwenye kutuangalia na kutupenda huyo anasubiri rehma, na adui yetu na mwenye kutuchukia anasubiri adhabu. Sisi ni watukufu, na kizazi chetu ni kizazi cha Manabii na kundi letu ni kundi la Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kundi la wenye kutupinga ni kundi la shetani na mwenye kutulinganisha sisi na adui yetu huyo si katika sisi.

Mnakwenda wapi na mnageukia wapi hali yakuwa dalili zimethibiti na ishara zipo wazi na minara imesimikwa, namna gani mnababaishwa? Vipi mnababaika hali yakuwa kizazi cha Mtume wenu kipo miongoni mwenu nao ndiyo walioshikamana na haki, na wao ndiyo viongozi wa dini na ndiyo ndimi za kweli, basi waheshimuni kwa heshima nzuri ya Qur'an na muwaendee kama awaendavyo ngamia mwenye kiu. Enyi watu yachukuweni hayo kutoka kwa Mtume wa mwisho aliposema: "Bila shaka anakufa mwenye kufa miongoni mwetu (watu wa nyumba ya Mtume) lakini yeye si maiti, na anachakaa mmoja wetu lakini si kwamba amechakaa, hivyo basi msiseme msiyoyajua, hapana shaka haki imo ndani ya yale muyapingayo. Mtakaseni ambaye ninyi hamna hoja yoyote dhidi yake nami ndiye huyo, je sikukitumia kati yenu kizito kikubwa na ninakuachieni kizito kidogo na nimeisimika kati yenu bendera ya imani?" Waangalieni watu wa nyumba ya Mtume wenu, mshikamane na kizazi chao na mfuate nyayo zao, hapana shaka hawatakutoeni nje ya haki na wala hawawezi kukurudisheni kwenye maangamizi, wakisimama nanyi simameni, wakinyanyuka nanyi nyanyukeni, wala msiwatangulie mtapotea na wala msiache kuwafuata mtaangamia.

Hizi ni kauli za Imam Ali (a.s) kuhusu kizazi kitukufu (cha watu wa nyumba ya Mtume) ambao Mwenyezi Mungu amewaondolea uchafu na amewatakasa mno. Na lau tutazifuatilia kauli za Maimamu miongoni mwa wanawe (a.s) ambao walikuwa wakizungumza mbele za watu kama vile (kauli za) Imam Hasan, Imam Husein, Zainul-Abidiin, Jaafar As-Sadiq na Imam Riza amani ya Mwenyezi Mungu iwashukie wote, tutawakuta wote

wanasema maneno ya namna hiyo hiyo na wanawaongoza watu katika kila zama na kila mahali (wafuate) kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi cha Mtume **(s.a.w.w)** kwa lengo la kuwaokoa kutokana na upotevu na kuwaingiza kwenye uongofu. Zaidi ya hapo ni kwamba, historia ndiyo shahidi bora juu ya kuhifadhika kwa watu wa nyumba ya Mtume, kwani haikusajili kwao isipokuwa elimu, uchamungu, utambuzi, ukarimu, upole na usamehevu na kila tendo alipendalo Mwenyezi Mungu na Mtume wake **(s.a.w.w)**. Kama ambavyo historia ni shahidi bora vile vile kwamba, watu wema katika umma huu na wachamungu miongoni mwa watu wa Tasawaf, Masheikh wa Tariqa, Maimamu wa madhehebu na wanachuoni wema wa zamani na zama hizi wote hawa wanakiri juu ya ubora wa Maimamu wa kizazi cha Ali na kutangulia kwao kielimu, matendo na kuhusika kwao kwa Mtume **(s.a.w.w)** kiukoo na utukufu. Na kwa yote haya basi si vyema kwa Muislamu yeyote kuwachanganya Ahlul-Bait ambao Mwenyezi Mungu amewaondolea uchafu na amewatakasa sana, na ambao Mtume aliwaingiza ndani ya Kisaa, haiwezekani kabisa kuwachanganya na wake wa Mtume **(s.a.w.w)**. Je, huoni kwamba Maimamu wa hadithi kama vile Muslim, Bukhari, Tirmidhi, Imam Ahmad, Nasai na wengineo wakati wanapothibitisha hadithi za ubora katika vitabu vyao na Sihah zao, huwa wanatenga mlango maalum wa ubora wa watu wa nyumba ya Mtume mbali na watu wengine miongoni mwa wake wa Mtume **(s.a.w.w)**.

Kama ilivyokuja ndani ya Sahih Muslim kwenye mlango wa ubora wa Ali ibn Abi Talib aliposema: "Imepokewa kutoka kwa Zaid ibn Ar-Qam kwamba, Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema, Fahamuni ya kwamba hakika mimi nakuachieni vizito viwili, kimoja wapo ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu, ni kamba ya Mwenyezi Mungu, yeyote mwenye kuifuata atakuwa kwenye uongofu na yeyote mwenye kuiacha atakuwa kwenye upotofu, kisha akasema, na watu wa nyumba yangu, nakukukumbusheni Mwenyezi Mungu kuhusu watu wa nyumba yangu. Sisi tukasema, je wakeze ni miongoni mwa watu wa nyumba yake? Akasema hapana, Namuapa Mwenyezi Mungu bila shaka mwanamke huwa pamoja na mume kwa kipindi fulani, kisha humtaliki na akarejea kwa baba yake na jamaa zake, watu wa nyumba yake Mtume ni wale wenye asili naye na ukoo wake ambao imeharamishwa kwao sadaka baada yake" Kama ulivyokuja ushahidi wa Bukhari na Muslim kwamba Aisha yeye anatokana na kizazi cha Abubakr na siyo katika kizazi cha Mtume **(s.a.w.w)** (walipozungumzia) tukio la kushuka aya ya kutayammam. Basi wa nini ung'ang'anizi huu utokanao na baadhi wapinzani ambao wanatumia kila gharama kuihuisha fitina na kuugeuza ukweli ambao hauna shaka ndani yake? Wanawatukana Mashia si kwa lolote isipokuwa kwa sababu wao hawazikubali fadhila hizo za Ummul-Muuminina, lakini ni kwa nini hawavitukani vitabu vyao na wanachuoni wao waliowatoa wakeze Mtume kuwa siyo katika watu wa nyumba ya Mtume?.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّـهَ وَقُولُوا قَوْلًا سَدِيدًا ﴿٧٠﴾ يُصْلِحْ لَكُمْ أَعْمَالَكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ
ذُنُوبَكُمْ وَمَن يُطِعِ اللَّـهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ فَازَ فَوْزًا عَظِيمًا ﴿٧١﴾

"Enyi mlioamini muogopoeni Mwenyezi Mungu na mseme maneno ya kweli. Atakutengenezeeni vizuri matendo yenu na atakusameheni madhambi

yenu, na yeyote anayemtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake bila shaka amefanikiwa mafanikio makubwa." (Qur'an, 33:71).

## MLANGO WA NNE

### YANAYOWAHUSU MASAHABAKWA UJUMLA

ila shaka hukumu zote za kisheria na itikadi za Kiislamu zimetufikia kwa kupitia kwa Masahaba, kwa Waislamu wote duniani hapana yeyote anayedai kwamba, yeye anamuabudu Mwenyezi Mungu kwa kupitia Qur'an na Sunna (moja kwa moja) isipokuwa Masahaba, wao ndio njia ya kumfikisha kwenye misingi hii miwili muhimu Na kwa kuwa Masahaba walihitilafiana baada ya Mtume **(s.a.w.w)**, wakatengana, kutukanana na kulaaniana, wakapigana mpaka wakauwana wao kwa wao, basi kwa hali hii haiwezekani kwetu sisi kuzichukua hukumu (za sheria) bila ya kuzijadili wala kuzichambua, kuzichunguza na (nyingine) kuzikanusha. Kama ambavyo hatuwezi (pia) kuwaunga mkono au kuwapinga bila ya kuzifahamu hali zao na kusoma historia yao na waliyovatenda katika zama za uhai wa Mtume **(s.a.w.w)** na baada ya kufa kwake, na tumchuje (miongoni mwao) yule mwenye kutenda haki na yule mwenye kutenda uovu, na kati ya muumini na yule mwenye matendo machafu na mwenye moyo safi na mnafiki, na (pia) tufahamu wale waliogeuka na wale walioshukuru. Na kwa masikitiko mengi ni kuwa, Ahlul-Sunnah hawalikubali jambo hilo na wanalizuwia kwa nguvu zote kuwakosoa Masahaba na kuonesha dosari zao, na wao Ahlul-Sunnah wanawaombea radhi kwa Mwenyezi Mungu Masahaba wote, na zaidi ya hapo wanawatakia rehema kama wamtakiavyo rehma Mtume Muhammad na watu wa kizazi cha Mtume Muhammad **(s.a.w.w)** wala hawamtoi sahaba yeyote. Suala wanalotupiwa Ahlul-Sunnah Wal-Jamaa ni kuwa: Je, hivi kuwakosoa Masahaba na kuonesha dosari zao kunasababisha mtu kutoka nje ya Uislamu au maana yake ni kwenda kinyume cha Qur'an na Sunnah?

Kwa kujibu suala hili sina budi kuonesha matendo na kauli za baadhi ya masahaba katika zama za uhai wa Mtume **(s.a.w.w)** na baada ya kufariki kwake, na (nitaonesha hayo) kwa kupitia maelezo yaliyotajwa na wanachuoni wa Kisunni ndani ya Sihah zao na Musnad zao na vitabu vyao vya historia, (pia) nitatosheka na (vitabu) vyao bila ya kutaja kitabu chochote miongoni mwa vitabu vya Kishia, kwani wao Mashia msimamo wao kwa baadhi ya Masahaba unaeleweka hauhitaji ziada ya maelezo au ufafanuzi. Na ili nipate kuondoa utata na ili mpinzani asiwe na hoja yoyote atakayoitoa dhidi yangu ninasema: "Bila shaka wakati tutakapokuwa tukizungumza juu ya Masahaba katika mlango huu, basi makusudio ni baadhi ya Masahaba na siyo wote, na huenda baadhi hii wakawa ndiyo wengi au wachache." Basi haya ndiyo tutakayo yafahamu kwa kupitia uchambuzi (huu) Inshaa Allah Taala, kwani wengi wa watu wanaoeneza chuki wanatudhania sisi tuko dhidi ya Masahaba, na kwamba sisi tunawashutumu Masahaba na kuwatukana, na yote haya wanayafanya ili wawatie mashaka wasikilizaji na wawakatize wale wanaofanya uchambuzi kutafuta haki, wakati ambapo sisi tunajiepusha mbali na (suala) la kuwatukana Masahaba na kuwashutumu, bali (ukweli) sisi tunawaombea radhi Masahaba wenye moyo safi ambao Qur'an imewaita kuwa ni "Wenye

kushukuru" na vile vile sisi tunajitenga mbali na Masahaba waliorudi kinyume nyume kwa visigino vyao, ambao (waliritadi) wakageuka nyuma baada ya Mtume **(s.a.w.w)**, na wakasababisha upotevu kwa Waislamu wengi, na hata hawa (licha ya kugeuka kwao) hatuwatukani wala hatuwashutumu, bali lililopo ni kwamba tunayaweka wazi matendo yao ambayo wanahistoria na wanachuoni wa hadithi wameyataja ili kweli iwadhihirikie wenye kuchunguza, na (kwa bahati mbaya) ndugu zetu Masunni jambo hili hawaliridhii na wanaliona kuwa ni matusi na ni shutma.

Iwapo Qur'ani tukufu ambayo ni maneno ya Mwenyezi Mungu na haichelei kusema ukweli, (yenyewe) ndiyo iliyotufundisha kwamba miongoni mwa Masahaba wamo wanafiki, wengine waovu, wengine madhalimu na wamo waongo, wengine washirikina na wengine waligeuka kinyume nyume na wamo wengine wanamuudhi Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Naye Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** ambaye hasemi lolote kwa matamanio yake na lawama ya mwenye kulaumu haimtishi Mtume (atendapo) kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, ndiye yeye Mtume **(s.a.w.w)** ametufungulia mlango na akatufahamisha kwamba miongoni mwa Masahaba wamo wenye kuritadi, na kuna wenye kutengua ahadi na wengine wenye kutoka katika dini na wamo wenye kuacha njia ya dini na miongoni mwao wataingia motoni na wala usahaba hautawanufaisha kitu, bali itakuwa ni hoja dhidi yao na adhabu yao itakuwa mara dufu katika siku ambayo haitofaa mali wala watoto. Basi itakuwaje katika hali kama hii ambayo inashuhudiwa na Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna ya Mtume wake Mtukufu, wao Masunni wanataka kuwazuia Waislamu wasizungumze na kujadili juu ya Masahaba kwa sababu haki isidhihirike na Waislamu wapate kuwafahamu mawalii wa Mwenyezi Mungu na kisha wawafuate kama ambavyo kwa njia hii watawafahamu maadui wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kisha wawapinge?.

Siku moja nilikuwa katika mji mkuu wa Tunisia ndani ya Msikiti mkubwa miongoni mwa Misikiti ya mji huo, baada ya kumaliza kusali sala ya faradhi, Imam alikaa katikati ya mzunguko wa watu waliokuwa wakisali (Msikitini hapo) na akaanza darasa lake kwa kuwatukana na kuwakufurisha wale watu ambao wanawashutumu Masahaba wa Mtume **(s.a.w.w)** na aliendelea kwa kusema: "Jihadharini na watu ambao wanawataja kwa ubaya Masahaba kwa madai eti ya utafiti wa kielimu na kutaka kuifahamu haki, watu hao wanastahiki laana ya Mwenyezi Mungu na Malaika na watu wote. Wanataka kuwatia shaka watu katika dini yao, hali ya kuwa Mtume **(s.a.w.w)** amesema: "**Itakapokufikieni hadithi inayohusu Masahaba wangu basi nyamazeni (msiisimulie) kwani namuapa Mwenyezi Mungu, lau ninyi mtatoa (katika njia ya dini) thamani ya dhahabu kama mlima wa Uhudi msingeweza kufikia sehemu moja ya kumi ya mmoja wao**." Mtu mmoja aliyekuwa kafuatana nami alimkatiza kwa kusema: "Hadithi hii siyo sahihi, na Mtume amesingiziwa" Imamu yule na baadhi ya waliokuwepo walihamaki na wakatugeukia hali ya kuwa wamekasirika, basi mimi nikayaangalia mazingira hayo na kumtuliza Imamu na nikamwambia: "Ewe bwana wangu Sheikh Mtukufu, hivi ni lipi kosa la Mwislamu ambaye atasoma ndani ya Qur'ani kauli (ya Mwenyezi Mungu) isemayo:

وَمَا مُحَمَّدٌ إِلَّا رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِن قَبْلِهِ الرُّسُلُ ۚ أَفَإِن مَّاتَ أَوْ قُتِلَ انقَلَبْتُمْ عَلَىٰ أَعْقَابِكُمْ ۚ وَمَن يَنقَلِبْ عَلَىٰ عَقِبَيْهِ فَلَن يَضُرَّ اللَّـهَ شَيْئًا ۗ وَسَيَجْزِي اللَّـهُ الشَّاكِرِينَ ﴿١٤٤﴾

"Na Muhammad hakuwa ila ni Mtume, wamepita kabla yake Mitume (wengi) basi akifa au akiuawa ndiyo mtarudi nyuma muwe makafiri kama zamani? Na yeyote atakayerudi nyuma kwa visigino vyake hatamdhuru Mwenyezi Mungu chochote, na Mwenyezi Mungu atawalipa wanaomshukuru, (Qur'an, 3:144).

Je, anakosa gani Muislamu ambaye anasoma ndani ya Sahihi Bukhari na Sahihi Muslim kauli ya Mtume **(s.a.w.w)** kuwaambia Masahaba wake kwamba; "**Siku ya Qiyama mtachukuliwa muelekezwe upande wa kushoto, kisha mimi nitasema (wanapelekwa) wapi? Nitaambiwa Wallahi (wanapelekwa) motoni, mimi nitasema: Ewe Mola wangu! hawa ni Sahaba wangu, nitaambiwa, hakika wewe hujui ni mambo gani waliyoyazusha baada yako, hakika wao hawakuacha kurudi nyuma tangu ulipowaacha, kisha nitasema atokomee atokomee yeyote aliyebadilisha (dini) baada yangu, nami sioni atakayeokoka miongoni mwao isipokuwa wachache mno.**"

Wakinisikiliza mimi kwa utulivu mno na baadhi yao waliniuliza ikiwa mimi nina hakika na kuwepo kwa hadithi hii ndani ya Sahihi Bukhari. Nami niliwajibu, "Ndiyo, nina hakika kama ambavyo nina hakika kuwa Mwenyezi Mungu ni mpweke hana mshirika na Muhammad ni Mtumwa wake na ni Mtume wake." Yule Imam alipogundua athari yangu kwa waliohudhuria kutokana na kuhifadhi kwangu hadithi ambazo nilizitaja, alisema kwa utulivu: "Sisi tumesoma kwa Masheikh wetu (Mwenyezi Mungu awarehemu) kwamba fitina imelala basi Mwenyezi Mungu amlaani yeyote mwenye kuiamsha."

Mimi nikasema: "Ewe Bwana wangu fitina siku zote haijalala, lakini sisi ndio tumelala, basi na yule aamkaye miongoni mwetu na kufungua macho yake ili aifahamu haki ninyi mnamtuhumu kuwa anaamsha fitina, na kwa hali yoyote ile Waislamu wanatakiwa kufuata Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna ya Mtume wake **(s.a.w.w)** na wala siyo maneno wayasemayo Masheikh ambao wanawatakia radhi kina Muawiyah na Yazid na Ibnul-Aa's. Yule Imam alinikatiza kwa kusema, "Je, hivi wewe humtakii radhi bwana wetu Muawiyah (r.a) ambaye ndiye mwandishi wa Wahyi? Nikasema: "Maudhui hii ni ndefu kuifafanua, na iwapo utataka kufahamu maoni yangu kuhusu jambo hilo, basi mimi nakuzawadia kitabu changu "Thummah-Tadaitu" huenda kikakuamsha kutoka kwenye usingizi wako na kikayafungua macho yako kuhusu baadhi ya mambo ya haki."

Basi yule Imam aliyakubali maneno yangu pamoja na ile zawadi yangu huku akiwa anasita, lakini baada ya mwezi mmoja aliniandikia barua nzuri akimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumuongoza kwenye njia yake iliyonyooka na akadhihirisha kuwafuata na kushikamana na watu wa nyumba ya Mtume **(s.a.w.w)**, nami nilimuomba niitangaze barua yake hiyo katika chapa ya tatu (ya kitabu changu hicho) kutokana na kuwemo ndani ya barua hiyo mambo ya maana na upendo na roho safi ambayo pindi alipoifahamu haki aliikumbatia, na inaonyesha ukweli kwamba wengi miongoni mwa Masunni huielekea haki kwa kiasi cha kuondoa pazia tu

(machoni pao). Lakini Imam huyo alinitaka niizuwie barua yake wala nisiitangaze, kwani inataka muda wa kutosha ili kuwatosheleza (kwa hoja) wale watu ambao wanasali nyuma yake na yeye anapendekeza wito wake uwe wa amani bila ya fitina na vurugu kwa mujibu wa mtazamo wake. Tunarudi kwenye maudhui ya kuzungumzia Masahaba, ili tuudhihirishe ukweli unaouma, ambao Qur'an imeusajili na pia Sunna ya Mtume. Hebu tuanze kwa maneno ya Mwenyezi Mungu ambayo hayatafikwa na batili mbele yake wala nyuma yake kabla na kwani yenyewe ndiyo uamuzi ulio na uadilifu na ndiyo kauli bayana.

Mwenyezi Mungu anasema:

وَمِمَّنْ حَوْلَكُم مِّنَ الْأَعْرَابِ مُنَافِقُونَ وَمِنْ أَهْلِ الْمَدِينَةِ مَرَدُوا عَلَى النِّفَاقِ لَا تَعْلَمُهُمْ نَحْنُ نَعْلَمُهُمْ سَنُعَذِّبُهُم مَّرَّتَيْنِ ثُمَّ يُرَدُّونَ إِلَىٰ عَذَابٍ عَظِيمٍ ﴿١٠١﴾

"Na miongoni mwa watu wa Madina wapo waliobobea katika unafiki, huwafahamu (kuwa ni wanafiki) sisi tunawafahamu, tutawaadhibu mara mbili kisha watarudishwa kwenye adhabu kubwa". (Qur'an, 9:101).

يَحْلِفُونَ بِاللَّهِ مَا قَالُوا وَلَقَدْ قَالُوا كَلِمَةَ الْكُفْرِ وَكَفَرُوا بَعْدَ إِسْلَامِهِمْ وَهَمُّوا بِمَا لَمْ يَنَالُوا ﴿٧٤﴾

"Wanaapa kwa Jina la Mwenyezi Mungu (kwamba) hawakusema, na hakika wamekwisha sema neno la ukafiri na wakakufuru baada ya (kudhihirisha) Uislamu wao (wa uongo) na wakaazimia mambo ambayo hawakuweza kuyafikia" (Qur'an, 9:74).

وَمِنْهُم مَّنْ عَاهَدَ اللَّهَ لَئِنْ آتَانَا مِن فَضْلِهِ لَنَصَّدَّقَنَّ وَلَنَكُونَنَّ مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿٧٥﴾ فَلَمَّا آتَاهُم مِّن فَضْلِهِ بَخِلُوا بِهِ وَتَوَلَّوا وَّهُم مُّعْرِضُونَ ﴿٧٦﴾ فَأَعْقَبَهُمْ نِفَاقًا فِي قُلُوبِهِمْ إِلَىٰ يَوْمِ يَلْقَوْنَهُ بِمَا أَخْلَفُوا اللَّهَ مَا وَعَدُوهُ وَبِمَا كَانُوا يَكْذِبُونَ ﴿٧٧﴾

"Na miongoni mwao (hao wanafiki) wapo waliomuahidi Mwenyezi Mungu kuwa, akitupatia katika fadhila zake tutatoa sadaka na tutakuwa miongoni mwa wanaotenda mema, lakini alipowapa hizo fadhila zake walizifanyia ubakhili na wakapinga, basi (Mwenyezi Mungu) akawalipa unafiki ndani ya nyoyo zao mpaka siku ya kukutana naye kwa sababu ya kukhalifu kwao waliyomuahidi Mwenyezi Mungu na kwa sababu ya kusema uongo." (Qur'an, 9:75-77).

الْأَعْرَابُ أَشَدُّ كُفْرًا وَنِفَاقًا وَأَجْدَرُ أَلَّا يَعْلَمُوا حُدُودَ مَا أَنزَلَ اللَّهُ عَلَىٰ رَسُولِهِ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٩٧﴾

"Mabedui wamezidi sana katika ukafiri na unafiki, na wameelekea zaidi wasijuwe mipaka ya yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu juu ya Mtume wake, na Mwenyezi Mungu ni mjuzi na mwenye hekima." (Qur'an, 9:97).

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَقُولُ آمَنَّا بِاللَّهِ وَبِالْيَوْمِ الْآخِرِ وَمَا هُم بِمُؤْمِنِينَ ﴿٨﴾ يُخَادِعُونَ اللَّهَ وَالَّذِينَ آمَنُوا وَمَا يَخْدَعُونَ إِلَّا أَنفُسَهُمْ وَمَا يَشْعُرُونَ ﴿٩﴾ فِي قُلُوبِهِم مَّرَضٌ فَزَادَهُمُ اللَّهُ مَرَضًا وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ بِمَا كَانُوا يَكْذِبُونَ ﴿١٠﴾

Na miongoni mwa watu wapo (wanafiki) wasemao tumemuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho na hali ya kuwa wao si wenye

kuamini, wanataka kumdanganya Mwenyezi Mungu na wale walioamini, lakini hawadanganyi isipokuwa nafsi zao hali yakuwa hawatambui, ndani ya nyoyo zao mna maradhi na Mwenyezi Mungu amewazidishia maradhi, basi watapata adhabu iumizayo kwa sababu ya kule kusema kwao uongo." (Qur'ani, 2:8-10).

إِذَا جَاءَكَ الْمُنَافِقُونَ قَالُوا نَشْهَدُ إِنَّكَ لَرَسُولُ اللَّـهِ ۗ وَاللَّـهُ يَعْلَمُ إِنَّكَ لَرَسُولُهُ وَاللَّـهُ يَشْهَدُ إِنَّ
الْمُنَافِقِينَ لَكَاذِبُونَ ﴿١﴾ اتَّخَذُوا أَيْمَانَهُمْ جُنَّةً فَصَدُّوا عَن سَبِيلِ اللَّـهِ ۚ إِنَّهُمْ سَاءَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ
﴿٢﴾ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ آمَنُوا ثُمَّ كَفَرُوا فَطُبِعَ عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ فَهُمْ لَا يَفْقَهُونَ ﴿٣﴾

"Wanapokujia wanafiki husema: tunashuhudia ya kuwa, kwa yakini wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu anajua kuwa wewe ni Mtume wake na Mwenyezi Mungu anashuhudia kuwa hakika wanafiki ni waongo, wamevifanya viapo vyao kuwa ngao za kujikinga, wakazuwia njia ya Mwenyezi Mungu, hakika ni mabaya waliyokuwa wakiyafanya, na hayo ni kwa kuwa waliamini kisha wakakufuru, basi muhuri ukapigwa juu ya nyoyo zao, hivyo basi hawafahamu chochote" (Qur'ani, 63:1-3).

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ يَزْعُمُونَ أَنَّهُمْ آمَنُوا بِمَا أُنزِلَ إِلَيْكَ وَمَا أُنزِلَ مِن قَبْلِكَ يُرِيدُونَ أَن يَتَحَاكَمُوا
إِلَى الطَّاغُوتِ وَقَدْ أُمِرُوا أَن يَكْفُرُوا بِهِ وَيُرِيدُ الشَّيْطَانُ أَن يُضِلَّهُمْ ضَلَالًا بَعِيدًا ﴿٦٠﴾ وَإِذَا قِيلَ
لَهُمْ تَعَالَوْا إِلَىٰ مَا أَنزَلَ اللَّـهُ وَإِلَى الرَّسُولِ رَأَيْتَ الْمُنَافِقِينَ يَصُدُّونَ عَنكَ صُدُودًا ﴿٦١﴾ فَكَيْفَ إِذَا
أَصَابَتْهُم مُّصِيبَةٌ بِمَا قَدَّمَتْ أَيْدِيهِمْ ثُمَّ جَاءُوكَ يَحْلِفُونَ بِاللَّـهِ إِنْ أَرَدْنَا إِلَّا إِحْسَانًا وَتَوْفِيقًا ﴿٦٢﴾

"Huwaoni wale wanaodai kwamba wameamini yale yaliyoteremshwa kwako na yaliyoteremshwa kabla yako, wanataka wakahukumiwe kwa Taaghuti (dhalimu) na hali wameamrishwa kumkataa Taaghuti, naye shetani anataka kuwapoteza upotofu ulio mbali, na wanapoambiwa njooni katika yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu na njooni kwa Mtume utawaona wanafiki wanajitenga nawe mbali kabisa, basi itakuwaje utakapowafikia msiba kwa sababu ya yale iliyoyatanguliza mikono yao? Kisha wakakujia wakiapa kwa Mwenyezi Mungu, Hatukutaka ila wema na mapatano" (Qur'ani, 4:60-62).

إِنَّ الْمُنَافِقِينَ يُخَادِعُونَ اللَّـهَ وَهُوَ خَادِعُهُمْ وَإِذَا قَامُوا إِلَى الصَّلَاةِ قَامُوا كُسَالَىٰ يُرَاءُونَ النَّاسَ
وَلَا يَذْكُرُونَ اللَّـهَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿١٤٢﴾

"Bila shaka wanafiki hutaka kumdanganya (hata) Mwenyezi Mungu, naye atawaadhibu kwa sababu ya kudanganya kwao, na wanaposimama kusali husimama kwa uvivu, wanawaonesha watu (kuwa wanasali) wala hawamkumbuki Mwenyezi Mungu ila kidogo." (Qur'ani, 4:142).

وَإِذَا رَأَيْتَهُمْ تُعْجِبُكَ أَجْسَامُهُمْ ۖ وَإِن يَقُولُوا تَسْمَعْ لِقَوْلِهِمْ ۖ كَأَنَّهُمْ خُشُبٌ مُّسَنَّدَةٌ ۖ يَحْسَبُونَ كُلَّ
صَيْحَةٍ عَلَيْهِمْ ۚ هُمُ الْعَدُوُّ فَاحْذَرْهُمْ ۚ قَاتَلَهُمُ اللَّـهُ ۖ أَنَّىٰ يُؤْفَكُونَ ﴿٤﴾

"Na unapowaona miili yao inakupendeza, na kama wakisema unasikiliza usemi wao, lakini wao ni kama boriti zilizotegemezwa, wanadhani kila kishindo kiko juu yao, hao ni maadui jihadhari nao, Mwenyezi Mungu awaangamizie mbali, ni vipi wanapotoka kutoka kwenye haki? (Qur'ani, 63:4).

"Bila shaka Mwenyezi Mungu anawajua wale wanaojizuwia miongoni mwenu wasiende vitani, na wale wanaowaambia ndugu zao, njooni kwetu (msiende kwa Muhammad) wala hawaendi katika mapigano ila kidogo tu, wanakufanyieni choyo, lakini inapokuja hofu utawaona wanakutazama, macho yao yanazunguka kama yule aliyezimia kwa mauti, lakini hofu yao inapoondoka wanakuudhini kwa ndimi zao kali wanaifanyia choyo kheri hao hawakuamini, kwa hivyo Mwenyezi Mungu ameviondoshea thawabu vitendo vyao, na hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi." (Qur'ani, 23:18-19).

وَأَنزَلْنَا مِنَ السَّمَاءِ مَاءً بِقَدَرٍ فَأَسْكَنَّاهُ فِي الْأَرْضِ وَإِنَّا عَلَىٰ ذَهَابٍ بِهِ لَقَادِرُونَ ﴿١٨﴾ فَأَنشَأْنَا
لَكُم بِهِ جَنَّاتٍ مِّن نَّخِيلٍ وَأَعْنَابٍ لَّكُمْ فِيهَا فَوَاكِهُ كَثِيرَةٌ وَمِنْهَا تَأْكُلُونَ ﴿١٩﴾

"Na wapo miongoni mwao wanaokusikiliza, hata wanapoondoka kwako huwaambia wale waliopewa elimu, (Mtume) amesema: nini sasa hivi, hao ndio ambao Mwenyezi Mungu amewapiga muhuri nyoyoni mwao na wakafuata matamanio ya nafsi zao" (Qur'ani, 47:16).

أَمْ حَسِبَ الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِم مَّرَضٌ أَن لَّن يُخْرِجَ اللَّهُ أَضْغَانَهُمْ ﴿٢٩﴾ وَلَوْ نَشَاءُ لَأَرَيْنَاكَهُمْ
فَلَعَرَفْتَهُم بِسِيمَاهُمْ وَلَتَعْرِفَنَّهُمْ فِي لَحْنِ الْقَوْلِ وَاللَّهُ يَعْلَمُ أَعْمَالَكُمْ ﴿٣٠﴾

"Je, wale wenye maradhi nyoyoni mwao wanadhani kwamba Mwenyezi Mungu hataidhihirisha bughudha yao, na kama tungependa tungekuonesha (watu hao) na ungewatambua kwa alama zao, lakini utaweza kuwafahamu kwa namna ya msemo (wao) na Mwenyezi Mungu anavifahamu vitendo vyenu" (Qur'ani, 47:29-30).

"Watakuambia wale waliokaa nyuma (wasiende vitani) miongoni mwa mabedui (watajidai kutoa nyudhuru) mali zetu na watu wetu walitushughulisha, basi tuombee msamaha, wanasema kwa ndimi zao yasiyokuwamo ndani ya mioyo yao." Kwa hiyo aya hizi zilizobayana kutoka ndani ya kitabu cha Mwenyezi Mungu, maelezo ambayo aya zimeyabainisha kuhusu unafiki wa baadhi yao na miongoni mwao wamo ambao walijificha ndani ya safu za Masahaba wema mpaka ukafichikana unafiki wao hata kwa mwenyewe Mtume lau si wahyi wa Mwenyezi Mungu kumtambulisha. Lakini sisi siku zote kuhusu jambo hili tunapingana na Masunni, kwani wao wanasema; "Tunahaja gani kuzungumzia wanafiki ambao Mwenyezi Mungu amewalaani, na Masahaba siyo miongoni mwa hawa (wanafiki), au husema, wanafiki siyo miongoni mwa Masahaba."Je, wanafiki hawa ni kina nani basi. ambao zimeshuka aya zaidi ya mia moja na khamsini kwa ajili yao ndani ya Surah za At-Taubah na Munafiqiina. " Watakujibu: "Hao ni Abdallah bin Ubai na Abdallah bin Abi Sallul." Na baada ya majina haya hawana jina jingine zaidi. Su-bhanallah!! Ikiwa Mtume **(s.a.w.w)** mwenyewe nafsi yake hakuwafahamu wengi miongoni mwa wanafiki, basi itakuwaje unafiki ukomee kwa ibn Ubai na ibn Abi Sallul ambao wanafahamika kwa Waislamu wote?

Ikiwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** aliwatambua baadhi yao na akawabainisha majina yao kwa Hudhaifah ibn Al-yamani kama mnavyosema, na kisha Mtume akaamuru asitangaze unafiki wao, kiasi kwamba Umar ibn Khattab alikuwa akimuuliza Hudhaifah zama za utawala wake Umar juu ya nafsi yake kuwa je, yeye ni miongoni mwa wanafiki? Na

je, Mtume alimtaja jina lake? Yote haya ni kwa mujibu wa maelezo yenu ndani ya vitabu vyenu na ikiwa Mtume **(s.a.w.w)** alitoa alama za wanafiki ambazo kwazo watatambulikana, nazo ni kumbughudhi Ali ibn Abi Talib, kwa mujibu wa riwaya zilizomo vitabuni mwenu hapana shaka wengi miongoni mwa hawa ni Masahaba ambao ninyi mnawaombea radhi na kuwapandisha daraja (za juu) na wengine licha ya bughudha dhidi ya Ali ibn Abi Talib, bali bughudha hiyo iliwafikisha mahali pa kumpiga vita Ali na walimuua na kumlaani angali hai na baada ya kufa yeye mwenyewe Ali na watu wa nyumba yake na wampendao, na wote waliotenda haya ni masahaba wema kwenu ninyi. Hekima ya Mtume **(s.a.w.w)** ilimfanya amfundishe Hudhaifa majina ya wanafiki kwa upande mmoja, na Mtume pia akawapa Waislamu alama za wanafiki kwa upande wa pili, ili asimamishe hoja dhidi ya watu wasijesema baada yake kuwa hakika sisi hatukuwa tunalijuwa jambo hili. Hatuoni maana yoyote wakati Masunni wanaposema "Sisi tunampenda Ali (r.a)."

Sisi tunawaambia Masunni kwamba "Kamwe ndani ya moyo wa Muumini hayakutani mapenzi ya kumpenda Walii wa Mwenyezi Mungu na mapenzi ya kumpenda adui wa Mwenyezi Mungu, kwani yeye mwenyewe Imam Ali (a.s) amesema: **Hawezi akawa miongoni mwetu yule anayetulinganisha sisi na maadui zetu**."

Ifahamike kwamba Qur'ani wakati ilipozungumzia Masahaba, iliwazungumzia kwa sifa mbali mbali na alama mbali mbali zenye kuthibiti, na inapowatoa miongoni mwao wale Masahaba wema wenye kushukuru, basi bila shaka watakaosalia Qur'an imewataja kuwa ni waovu, au ni wenye khiyana, au ni wenye kujifanya wanyonge, au wenye kutoka katika dini, au ni wenye kugeuka au wanamtilia mashaka Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na ni wenye kukimbia mapambano dhidi ya makafirina na au wanadhoofisha wenzao kwenye jihadi au ni wapinzani wa haki, au ni waasi wa amri za Mwenyezi Mungu na Mtume wake, au ni wenye kukimbilia upuuzi na biashara na kuacha sala, au ni wenye kusema wasiyoyatenda, au wanajifaharisha kwa Uislamu wao mbele ya Mtume, au nyoyo zao ni ngumu hazikumnyenyekea Mwenyezi Mungu kwa utajo wake na haki iliyoteremka, au watakuwa ni wenye kunyanyua sauti zao juu ya sauti ya Mtume **(s.a.w.w)** au ni wale wanaomuudhi Mtume wa Mwenyezi Mungu au ni wenye kuwasikiliza wanafiki. Hebu na tutosheke na kiasi hiki kidogo, kwani kuna aya nyingi hatukuzitaja ili tufupishe maelezo. Lakini ili ipatikane faida, hatuna budi kutaja baadhi ya aya ambazo zimekuja kuhusiana na kuwashutumu Masahaba ambao walisifika kwa sifa hizo, lakini kwa baraka za kisiasa baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** na baada ya wahyi kukatika, wote hawa wakawa ni waadilifu na eti haifai kwa yeyote miongoni mwa Waislamu kuzungumza cho chote kuhusiana nao ikiwa ni kuwakosoa au kutia dosari.

9

# WAULIZE WANAOFAHAMU

## BUKHARI AMEANDIKA KATIKA SAHIHI YAKE

Bukhari ameandika katika sahihi yake juzuu ya nne mlango wa vitu alivyokuwa akiwapa Mtume wale wanaoimarishwa nyoyo zao, ndani ya Kitabul Jihadi Was-sair.

Imepokewa kutoka kwa Anas ibn Malik kwamba, "Wakati Mwenyezi Mungu alipomjaalia Mtume wake ghanima katika mali za Hawazin, aliwapa baadhi ya watu miongoni mwa Maquraishi, Ansari wakasema, Mwenyezi Mungu amsamehe Mtume wa Mwenyezi Mungu, anawapa Maquraishi na anatuacha sisi na hali panga zetu zinadondoka damu yao? Basi Mtume **(s.a.w.w)** akawakusanya hapo Qubbah na hakumuacha yeyote kisha akawaambia, Zikoje khabari zilizonifikia kutoka kwenu? Waliporudia usemi wao kwa Mtume, Mtume **(s.a.w.w)** akasema: Hakika mimi nawapa watu ambao hivi karibuni walikuwa katika ukafiri je, hamridhii watu wende na mali nanyi murudi majumbani kwenu mkiwa pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu? Basi Wallahi mtakachorudi nacho ni bora kuliko watakachorudinacho.Wakasema, Kwa nini tusiridhike ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, hakika tumeridhia. Basi Mtume akawaambia, Hakika ninyi mtakuja ona upendeleo baada yangu, basi vumilieni mpaka mkutane na Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwenye Hauz, Anas alisema, Hatukuvumilia[1].

**Tunajiuliza**: Je, hivi miongoni mwa Ansari wote kulikuwa na mtu japo mmoja aliyeongoka ambaye aliridhia alichokifanya Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** na akaamini kwamba Mtume hafuati matamanio ya nafsi yake wala hawezi kuacha haki? Na je, aliifahamu kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kuhusu kusudio hili aliposema:

فَلَا وَرَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ حَتَّىٰ يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لَا يَجِدُوا فِي أَنفُسِهِمْ حَرَجًا مِّمَّ ا
قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُوا تَسْلِيمًا ﴿٦٥﴾

"Naapa kwa haki ya Mola wako hawawezi kuwa waumini (wa kweli) mpaka wakufanye wewe kuwa ni hakimu katika yale wanayokhitilafiana, kisha wasione uzito nyoyoni mwao juu ya hukumu uliyoitoa na wanyenyekee kabisa." (Qur'ani, 4:65).

Je, alikuwemo miongoni mwao aliyemtetea Mtume **(s.a.w.w)** wakati waliposema: "Mwenyezi Mungu amsamehe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Hakuna, hapakuwa na yeyote miongoni mwao aliyekuwa na kiwango cha imani iliyowajibishwa na aya tukufu, na kule kusema kwao baada ya usemi wa Mtume kuwa, "Kwa nini tusiridhike ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, hakika tumeridhika." Ukweli haikuwa kwa kutosheka (na maelezo ya Mtume **s.a.w.w**) na ndiyo maana ulikuja ushahidi wa Anas naye akiwa yu miongoni mwao pale aliposema, "Mtume alituusia kuvumilia lakini hatukuvumilia."

---

1. Sahihi Bukhari Juz.4 uk.60.

Bukhari ameandika ndani ya Sahihi yake katika juzuu ya tano, Babu ghaz-watil-hudai-biyyah katika Kitabul-maghazii. imesimuliwa kutoka kwa Ahmad ibn Ishkab, ametusimulia Muhammad ibn Fazail kutoka kwa Al-ala ibn Al-musayyab kutoka kwa baba yake amesema, "Nilikutana na Al-Bar-raa ibn A'zib (r.a) nikasema: Hongera, umefuzu, ulikuwa sahaba wa Mtume **(s.a.w.w)** na ukampa baia chini ya mti. Akasema: **Ewe Mwana wa ndugu yangu, hakika wewe hujuwi tuliyoyazua baada yake**"[1].

Bila shaka Al-Barraa ibn A'zib amesema kweli, kwani wengi wa watu hawayafahamu waliyoyazua Masahaba baada ya Mtume wao kufariki, na miongoni mwake ikiwa ni kumdhulumu wasii wake na Ibn Ammi yake Mtume na kumtenga kwenye ukhalifa, pia walimdhulumu binti ya Mtume Fatimatuz-Zahraa na kumtishia kumchoma moto, na kupora haki yake miongoni mwa zawadi na urithi na khumsi, na pia waliukhalifu Usia wa Mtume na kubadilisha hukumu za sheria. Si hivyo tu bali walichoma moto vitabu vya Sunna ya Mtume na kuidhibiti isisimuliwe, kadhalika walimuudhi yeye Mtume **(s.a.w.w)** kwa kuwalaani na kuwauwa watu wa nyumba ya Mtume, kuwatenga na kuwatawanya kisha kuwapa uongozi wanafiki na waovu miongoni mwa maadui wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Basi yote hayo na mengineyo miongoni mwa waliyoyazusha Masahaba baada ya Mtume na yakabakia hayafahamiki kwa watu wengi ambao hawakufahamu ukweli isipokuwa yale yaliyopendekezwa na chuo cha Makhalifa (yaani Usunni), na yanayo kila namna ya mabadiliko katika hukumu za Mwenyezi Mungu na Mtume wake (kwa kuingizwa) ijtihadi mbali mbali za watu zilizoitwa kuwa ni Bid 'a nzuri.

Kwa Munasaba huu tunawaambia Masunni, "Enyi ndugu zetu msidanganyike kwa usahaba na kusuhubiana (na Mtume) basi huyu hapa Al-Bar-raa ibn Azib ambaye ni miongoni mwa watu wa mwanzo ambao walimpa baia Mtume **(s.a.w.w)** chini ya mti, anamwambia mtoto wa nduguye hali halisi ilivyo kwamba, usikudanganye usahaba wangu wala baia yangu chini ya mti, hakika wewe hujuwi niliyoyazua baada ya Mtume, na Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema:

إِنَّ الَّذِينَ يُبَايِعُونَكَ إِنَّمَا يُبَايِعُونَ اللَّـهَ يَدُ اللَّـهِ فَوْقَ أَيْدِيهِمْ فَمَن نَّكَثَ فَإِنَّمَا يَنكُثُ عَلَىٰ نَفْسِهِ وَمَنْ أَوْفَىٰ بِمَا عَاهَدَ عَلَيْهُ اللَّـهَ فَسَيُؤْتِيهِ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿١٠﴾

"Bila shaka wale wanaokupa baia kwa hakika wanambai Mwenyezi Mungu, msaada wa Mwenyezi Mungu uko juu yao, basi yeyote avunjaye ahadi hii anaivunja kwa kuidhuru nafsi yake..." (Qur'an, 48:10).

Na ni idadi kubwa ya Masahaba walivunja ahadi mpaka hata Mtume alimuusia Ibn Ammi yake Ali kuwapiga (waliovunja ahadi) kama yalivyokuja hayo katika vitabu vya historia.

Bukhari katika Sahih yake ndani ya juzuu ya kwanza na ya tatu katika mlango, Idhaa Nafaran-nasu Anil-Imam fi Salatil-jumuah ndani ya Kitabul-jumuah ameandika kama ifuatavyo. Ameeleza Jabir ibn Abdillah (r.a) amesema: "Ulifika msafara kutoka Sham umebeba vyakula na sisi tunasali pamoja na Mtume **(s.a.w.w)** sala ya Ijumaa, watu wakakimbia isipokuwa

1. Sahihi Bukhari Juz.5 uk.66.

watu kumi na wawili, hapo ndipo iliposhuka aya hii isemayo: "Na waionapo biashara au (vitu) vya upuuzi huvikimbilia na wakakuacha umesimama..."[1].

Huu ni mfano mwingine wa Masahaba wanafiki ambao hawamuogopi Mwenyezi Mungu wala kumnyenyekea. bali wanakimbia kutoka kwenye Sala ya Ijumaa ili wakaone msafara na biashara na wanamuacha Mtume wa Mwenyezi Mungu amesimama mbele ya Mwenyezi Mungu akitekeleza Faradhi yake kwa unyenyekevu mkubwa. Basi je, hawa ni Waislamu waliokamilika imani yao? Au wao ndio wanafiki wanaodharau Sala, na wasimamapo husiama kwa uvivu? Na hawaepukani miongoni mwao isipokuwa wale waliodumu pamoja na Mtume **(s.a.w.w)** kuikamilisha Sala ya Ijumaa na idadi yao ilikuwa kumi na wawili tu. Yeyote atakayefuatilia hali za Masahaba na kuchunguza habari zao, huenda akashangaa kwa matendo yao, na hapana shaka kwamba kukimbia kwao kutoka kwenye sala ya Ijumaa kulirudia mara nyingi, na kwa hiyo basi kitabu cha Mwenyezi Mungu kimelisajili tendo hilo kwa kusema: "Waambie kilichopo kwa Mwenyezi Mungu ni bora kuliko mambo ya upuuzi na biashara." Ili ufahamu vyema ewe msomaji Mtukufu kiwango cha heshima yao kwenye sala hii ambayo Waislamu wa leo wanaiheshimu zaidi kuliko wao, hebu basi iangalie riwaya hii ifuatayo.

Bukhari ameandika ndani ya Sahihi yake katika juzuu ya tatu mlango uitwao: Majaa Fil-gharsi" ndani ya Kitabul-Wakalah. Imepokewa kutoka kwa Sahl ibin Said (r.a) kwamba: "**Hakika sisi tulikuwa tunafurahi katika siku ya Ijumaa, kwani tulikuwa na bibi Kizee fulani akichukua mizizi ya mmea uitwao 'Salaq' ambayo tulikuwa tukiipanda katika maeneo yetu, basi (kizee huyo) huiweka ndani ya chungu chake na kutia humo mbegu za Shairi. Sifahamu zaidi bali yeye alisema hakuna ndani yake mafuta, basi tukisha sali Ijumaa tunamtembelea na hutusogezea chakula hicho, tulikuwa tukifurahi siku ya Ijumaa kwa ajili hiyo, na tulikuwa hatuli wala hatupumziki isipokuwa baada ya sala ya Ijumaa**" -[2].

Ni maajabu yaliyoje kwa Masahaba hawa ambao hawaifurahii siku ya Ijumaa kwa kukutana na Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** na kusikiliza hotuba yake na mawaidha yake na kusali nyuma ya Mtume wao, wala hawafurahi kukutana wao kwa wao na mengine yaliyomo ndani ya siku hiyo ikiwa ni miongoni mwa baraka na rehma. Lakini Masahaba wanafurahia siku ya Ijumaa kwa ajili ya chakula maalum kilichoandaliwa na bibi kizee, na lau leo hii Muislamu fulani angesema kuwa siku ya Ijumaa anafurahi kwa ajili ya chakula, basi bila shaka angeonekana ni miongini mwa wasogeza wakati wasiojali dini!! Na tutakapotaka nyongeza ya uchunguzi na kufuatilia, tutawakuta wenye kushukuru (miongoni mwa Masahaba) ambao Qur'an Tukufu imewasifu ni wachache mno na idadi yao haizidi kumi na wawili, na hawa ndiyo (Masahaba) wema ambao hawakukimbia kufuata mambo ya upuuzi na biashara na kuiacha sala, na ndiyo hao hao ambao waliimarika katika Jihadi pamoja na Mtume **(s.a.w.w)** mahala pengi miongoni mwa nyanja nyingi ambazo masahaba wengine

1. Sahihi Bukhari Juz.l uk.225 na Juz.3 uk.6 na 7.
2. Sahih Bukhari Juz.3 uk. 73.

walikimbia na waligeuka nyuma wakatokomea. Bukhari ameandika ndani ya Sahihi yake juzuu ya nne katika mlango wa Yanayochukiza miongoni mwa mizozo na tofauti katika vita, Kitabul-Jihad Was-Sair, Imepokewa toka kwa Al-Bar-raa ibn Azib amesema: "Mtume **(s.a.w.w)** alimuweka Abdallah ibn Jubair (kuwa kiongozi) wa askari wa miguu siku ya Uhdi, na walikuwa watu hamsini, Mtume akasema, Mkituona tumeshambuliwa msiondoke mahala penu mpaka niwatumieni habari, akasema, Wallahi niliwaona wanawake wanakimbia na miundi yao inaonekana na bangiri zao wakipania nguo zao, basi watu wa Abdallah ibn Jubayr wakasema: 'Ghanimah' yaani Mali hizo, jamaa zenu wameshinda sasa mnangoja nini? Abdallah ibn Jubayr akawaambia: Je, mmesahau alivyokuambieni Mtume wa Mwenyezi Mungu, wakasema, Wallahi tutawafuata watu hao ili tupate ngawira. Walipowafuata mwenendo wao uligeuzwa na wakashambuliwa, hapo ndipo walipokimbia na Mtume akawa anawaita lakini hapakubaki pamoja na Mtume isipokuwa watu kumi na wawili, makafiri wakawauwa miongoni mwetu watu sabini..."[1].

Na tukishayafahamu yale waliyoyaeleza wanahistoria kuhusu vita hivi (vya Uhdi) kwamba Mtume **(s.a.w.w)** alitoka akiwa na Masahaba elfu moja na wote wakiwa wamehamasika kwa Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu, lakini wakiwa wamehadaika kwa ushindi walioupata katika vita vya Badri, lakini ghafla waliasi amri ya Mtume **(s.a.w.w)** na wakasababisha mashambulizi haya mabaya ambayo waliuawa watu sabini akiwemo Hamza ammi yake Mtume **(s.a.w.w)**, na (Masahaba) wengine wakakimbia na hapakubaki pamoja na Mtume **(s.a.w.w)** katika uwanja wa vita isipokuwa watu kumi na wawili kama anavyosema Bukhari. Ama wanahistoria wengine wanashuka chini ya idadi hii mpaka watu wanne, tu. nao ni Ali ibn Abi Talib ambaye aliwazuwia washirikina akimlinda Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** kwa mbele na Abud-dajjanah akimlinda Mtume kwa nyuma na Talha na Zubair na inasemekana Sahal ibn Hunaif. Kutokana na mazingira haya tunaifahamu vema kauli ya Mtume wa Mwenyezi Mungu aliposema, "Sioni atakayesalimika miongoni mwao isipokuwa mfano wa idadi ya ngamia wasiomchunga" Baadaye yatakuja maelezo kuhusu hadithi hii.

Sasa basi kama Mwenyezi Mungu Mtukufu amewakamia kwa moto watakapokimbia vita, akasema,

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذَا لَقِيتُمُ الَّذِينَ كَفَرُوا زَحْفًا فَلَا تُوَلُّوهُمُ الْأَدْبَارَ ﴿١٥﴾ وَمَن يُوَلِّهِمْ يَوْمَئِذٍ
دُبُرَهُ إِلَّا مُتَحَرِّفًا لِّقِتَالٍ أَوْ مُتَحَيِّزًا إِلَىٰ فِئَةٍ فَقَدْ بَاءَ بِغَضَبٍ مِّنَ اللَّـهِ وَمَأْوَاهُ جَهَنَّمُ ۖ وَبِئْسَ الْمَصِيرُ
﴿١٦﴾

"Enyi mlioamini mkutanapo vitani na wale waliokufuru basi msiwageuzie migongo mkakimbia, na atakayegeuka siku hiyo akakimbia isipokuwa ageukaye kwa kushambulia au ili akaungane na sehemu nyingine za jeshi la Waislamu, vinginevyo atastahiki ghadhabu za Mwenyezi Mungu na mahala pake ni moto wa jahanam napo ni mahala pabaya pa kurejea." (Qur'ani, 8:16).

1. Sahih Bukhari Juz. 4 uk.26.

Basi ikoje daraja ya Masahaba hawa ambao wanaikimbia sala kwa ajili ya mambo ya mchezo na biashara na wanaikimbia Jihadi kwa hofu ya mauti na kumuacha Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** peke yake akiwa katikati ya maadui? Na katika hali zote mbili, walikimbia na kugeuka wote na Mtume hakubakia isipokuwa na watu kumi na wawili kwa makadirio ya juu, basi wana hali gani Masahaba enyi wenye kufikiri? Huenda baadhi ya wachunguzi wanaposoma hadithi mfano wa riwaya kama hizi wanayaona mambo haya kama ni madogo na wanadhani kuwa ni matukio ya kipuuzi ambayo Mwenyezi Mungu ameyasamehe na kwamba Masahaba hawakurudia tena kufanya hivyo.

Sivyo kabisa, bila shaka Qur'ani tukufu itatupatia ukweli unaotisha, hakika Mwenyezi Mungu amesajili kukimbia kwao siku ya Uhd kwa kusema: "Na kwa hakika Mwenyezi Mungu alikukamilisheni miadi yake mkawaua kwa idhini yake, mpaka mliporejea na mkagombana katika shauri lile na mkaasi baada ya yeye kukuonesheni mliyoyapenda. Wako miongoni mwenu wanaopenda dunia na wako miongoni mwenu wanaopenda akhera, kisha (Mwenyezi Mungu) akakuwekeni mbali nao ili akujaribuni, naye sasa amekusameheni, na Mwenyrzi Mungu ni Mwenye ihsani nyingi juu ya wanaoamini. Kumbukeni mlipokuwa mkikimbia mbio wala ninyi hamumngoji yeyote hali Mtume alikuwa anakuiteni nyuma yenu, (Mwenyezi Mungu) akakupeni huzuni juu ya huzuni, na ili msihuzunike (sana) kwa yale yaliyokupoteeni, wala kwa misiba iliyokupateni na Mwenyezi Mungu anayajua yote mnayoyatenda." (Qur'ani, 153).

Aya hizi zilishuka baada ya vita vya Uhdi ambavyo Waislamu walishambuliwa vibaya kwa sababu ya kupenda kwao starehe za dunia hasa wakati walipowaona wanawake wanapania nguo zao, miundi yao na bangiri zinaonekana kama alivyoeleza Bukhari. Wakamuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake **(s.a.w.w)** kama ilivyoeleza Qur'ani, basi je, Masahaba walilizingatia tukio hilo na wakatubia kwa Mwenyezi Mungu na kumuomba msamaha na hawakurudia tena kosa kama hilo? Sivyo kabisa, hakika wao hawakutubu na walirudia kosa kubwa zaidi kuliko hilo katika vita ya Hunain ambayo ilitokea mwishoni mwa uhai wa Mtume **(s.a.w.w)**, na idadi yao katika vita hiyo ilikuwa ni watu elfu kumi na mbili kama wanahistoria walivyoeleza. Pamoja na wingi wao walijitetea kwa kukimbia na hawakugeuka nyuma kama kawaida yao, wakamuacha Mtume wa Mwenyezi Mungu katikati ya maadui wa Mwenyezi Mungu miongoni mwa washirikina akiwa na watu tisa au kumi miongoni mwa Bani Hashim wakiongozwa na Ali ibn Abi Talib kama alivyoeleza Al-yaa'qubi katika tarikh yake na wengineo.

Sasa basi ikiwa kukimbia kwao siku ya Uhd lilikuwa ni jambo baya, hapana shaka kwamba, siku ya Hunain lilikuwa ni jambo baya zaidi na lenye kuchukiza mno, kwani wenye kusubiri ambao waliimarika pamoja na Mtume siku ya Uhdi walikuwa watu wanne katika elfu moja nayo ni sawa na mtu mmoja katika kila watu mia mbili na hamsini. Ama siku ya Hunain waliosubiri na wakaimarika walikuwa kumi katika idadi ya Masahaba elfu kumi na mbili nayo ni sawa na mtu mmoja katika kila watu elfu moja na mia mbili. Na iwapo vita vya Uhdi vilikuwa mwanzoni mwa Hijra na kwamba watu wengi walikuwa bado wachache na ndiyo hivi karibuni

walikuwa katika zama za ujinga, basi ni ipi sababu yao katika vita ya Hunain ambayo ilitokea mwishoni mwa mwaka wa nane wa Hijra ya Mtume? Ilikuwa imebaki miaka miwili tu katika uhai wa Mtume, lakini pamoja na ukubwa wa idadi yao na maandalizi yao walikimbia bila kumgeukia Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**. Qur'an Tukufu inabainisha wazi msimamo wao mbaya na kukiambia kwao katika vita hivyo kwa kusema:

وَيَوْمَ حُنَيْنٍ إِذْ أَعْجَبَتْكُمْ كَثْرَتُكُمْ فَلَمْ تُغْنِ عَنكُمْ شَيْئًا وَضَاقَتْ عَلَيْكُمُ الْأَرْضُ بِمَا
رَحُبَتْ ثُمَّ وَلَّيْتُم مُّدْبِرِينَ ﴿٢٥﴾ ثُمَّ أَنزَلَ اللَّـهُ سَكِينَتَهُ عَلَىٰ رَسُولِهِ وَعَلَى الْمُؤْمِنِينَ وَأَنزَلَ جُنُودًا لَّمْ
تَرَوْهَا وَعَذَّبَ الَّذِينَ كَفَرُوا وَذَٰلِكَ جَزَاءُ الْكَافِرِينَ ﴿٢٦﴾

"Na siku ya Hunain ambapo wingi wenu ulikupandisheni kichwa lakini haukukufaeni chochote na ardhi ikawa finyu juu yenu ingawa ilikuwa na nafasi kisha mkakimbia, hatimaye Mwenyezi Mungu akateremsha utulivu kwa Mtume wake na juu ya waumini, na akateremsha majeshi ambayo hamkuyaona na akawaadhibu wale waliokufuru na hayo ndiyo malipo ya makafiri." (Qitr'ani, 9:25-26).

Mwenyezi Mungu anabainisha kwamba alimuimarisha Mtume wake na wale waliosubiri pamoja naye kwenye vita kwa kuwateremshia utulivu, kisha akawatia nguvu kwa jeshi la Malaika wakapigana pamoja nao na akawapa ushindi dhidi ya Makafiri, wala hakukuwa na haja ya msaada wa wale walioritadi ambao waliwakimbia maadui kwa hofu ya kufa, na kwa kufanya hivyo wakamuasi Mola wao na Mtume wao, na kila Mwenyezi Mungu alipowapa mtihani aliwakuta ni wenye kushindwa!! Bukhari ameandika ndani ya Sahih yake katika juzuu ya tano mlango wa kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo; "Na siku ya Hunain ulikupandisheni kichwa wingi wenu na haukuwasaidieni chochote," Kitabul-Maghazi kwamba: Abu Qatadah amesema:"Ilipokuwa siku ya Hunain, nilimuangalia mtu fulani miongoni mwa Waislamu anapigana na mtu fulani miongoni mwa washirikina na mwingine miongoni mwa washirikina anamvizia Muislamu kwa nyuma ili amuue, basi nikafanya haraka kumuendea yule anayemvizia, basi akanyanyua mkono wake ili anipige upanga (nikamuwahi) nikampiga mkono wake nikaukata kisha akanishika na kunikumbatia kwa nguvu sana mpaka nikaogopa kisha akaniachia na akatoka nikamsukuma na kumuua. Waislamu walielemewa (wakakimbia) nami nikawa pamoja nao, basi mara ghafla (nikamuona) Umar ibn Khatab akiwa ndani ya kundi la watu nikamwambia, Mbona hivi," watu wamepatwa na nini? akasema, Hiyo ni amri ya Mungu. (Sahih Bukhari Juzuu ya 5 uk.101).

Wallahi mambo aliyoyafanya Umar siku hiyo ni ajabu, lakini huyu ndiye Umar ambaye mbele ya Masunni anaonekana kuwa ni shujaa mno miongoni mwa Masahaba kama siyo shujaa kupita wote kabisa. Kwa mujibu wa Masunni, wao wanamuona kwamba eti ni mtu ambaye kupitia kwake Mwenyezi Mungu aliutia nguvu Uislamu na kwamba Waislamu hawakuutangaza wazi wazi Uislamu ila baada ya kusilimu kwa Umar. Hapana shaka historia imetupatia msimamo sahihi na wa kweli na ni jinsi gani Umar alivyokimbia siku ya Khaibar, pale Mtume alipomtuma aende

katika mji wa Khaibar akauteke (uwe chini ya himaya ya Kiislamu) na akamtuma pamoja na jeshi akashindwa yeye pamoja na wanajeshi wake na wanajeshi aliofuatana nao wakarudi hali wakimtuhumu kwa woga na yeye akiwatuhumu wao kwa woga. Kama ambavyo aligeuka na akakimbia siku ya Hunain yeye na waliokimbia au huenda alikuwa ni wa kwanza kukimbia na watu wakamfuata kwa kuwa yeye alikuwa ndiye shujaa wao, na ndiyo maana tunamuona Abu Qatada anamgeukia Umar kati ya maelfu ya watu waliokimbia anamuuliza kana kwamba anashangazwa akamwambia, "Watu wamepatwa na nini?"

Umar ibn Khatab siyo tu alikimbia jihadi na kumuacha Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** katikati ya maadui miongoni mwa washirikina, bali alimdanganya Abu Qatada kwa kumwambia; "Hiyo ni amri ya Mwenyezi Mungu...!" Je, hivi Mwenyezi Mungu ndiye aliyemuamuru Umar ibn Khatab akimbie vita? Au amemuamrisha kusimama imara na kusubiri ndani ya vita na asikimbie? Kwani Mwenyezi Mungu amesema kumwambia Umar na wenzake, "Enyi mlioamini mtakapokutana vitani na wale waliokufuru msiwakimbie." (Qur'ani, 8:15).

Kama ambavyo Mwenyezi Mungu alichukua ahadi kwa Umar na kwa wenzake kwa jambo hilo ambalo limekuja ndani ya Qur'ani kwamba: "Na kwa yakini walikwisha fanya ahadi na Mwenyezi Mungu zamani ya kwamba, hawatageuza migongo (yao watakapokuja makafiri kuwashambulia) na ahadi ya Mwenyezi Mungu itaulizwa." Basi vipi baba Hafsa akimbie vita na kudai kuwa hiyo ni amri ya Mwenyezi Mungu? Hakika yuko mbali na aya hizi zenye kubainisha ukweli, au (tuseme), "Katika nyoyo zao kuna makufuli?" Hapa sisi hatukusudii kuichunguza hali ya Umar ibn Khatab kwani tutamtengea mlango maalum wa kwake, lakini hadithi ya Bukhari inaathiri na haikutupa nafasi ya kuacha kuleta dokezo juu ya Umar kwa haraka kabla ya kufika wakati wake, na kilicho cha muhimu sasa hivi ni ushahidi wa Bukhari kwamba, pamoja na wingi wa idadi ya masahaba lakini walikimbia siku ya vita vya Hunain, na yeyote anayesoma vitabu vya historia kuhusu vita hivyo yatamdhihirikia mambo ya ajabu mno.

Iwapo amri ya Mwenyezi Mungu Masahaba wengi hawakuitii kama tulivyokwishaona hapo kabla, basi siyo ajabu kwao kupinga amri za Mtume **(s.a.w.w)** hali ya kuwa yu hai. Ama amri zake baada ya kufa kwake (naapa kwa baba yangu na mama yangu) na nimeyakuta mambo mengi yanayotokana nao ikiwa ni pamoja na kupuuza (maamrisho) na kuzibadilisha (hukumu zake). Hakika hapana ubaya kuyasimulia hayo. Masahaba na maamrisho ya Mtume **s.a.w.w**) zama za uhai wake. Hebu na tuanze na maamrisho ambayo Mtume aliyaamrisha zama za uhai wake, maamrisho ambayo yalipambana na kutotiiwa na uasi kutoka kwa hawa Masahaba. Sisi hatutazungumzia ila yale tu aliyoyaandika Bukhari ndani ya Sahihi yake ili tufupishe maelezo, hatutajishughulisha na Sihah zingine za Kisunni kwasababu hapana shaka kabisa katika sahihi zingine kuna ibara nyingi mno zilizowazi na zilizofafanuliwa vyema. Bukhari ameandika ndani ya Sahih yake, juzuu ya tatu mlango wa sharti za jihadi na mapatano na wapiganaji, Kitabus-Shurut. Baada ya Bukhari kukileta kisa cha Hudaibiyyah na upinzani wa Umar ibn Al-khat-tab kwa kitu ambacho Mtume wa Mwenyezi Mungu amekiwafiki, na pia kukitilia mashaka mpaka

akamwambia Mtume waziwazi, "Hivi wewe siye Nabii wa Mwenyezi Mungu wa kweli?"... Mpaka mwisho wa tukio Bukhari anasema: "Alipomaliza suala la kuandika Sul-hu ya Hudaibiyyah Mtume wa Mwenyezi Mungu alisema kuwaambia Masahaba wake, Simameni mchinje kisha mnyoe. Akasema; Wallahi hakuna mtu aliyesimama miongoni mwao mpaka akarudia mara tatu, hakuna aliyesimama. Mtume akaingia ndani kwa Ummu Salamah akamuelezea yaliyomkuta kutoka kwa watu." (Sahih Bukhari Juz.3 uk.182).

Je, hushangai ewe msomaji kutokana na Masahaba kutotii na kuasi kwao amri ya Mtume **(s.a.w.w)**, hata baada ya kurudia mara tatu ikawa hakuna mtu yeyote miongoni mwao aliyemuitikia Mtume? Mahala hapa, sina budi kuueleza mjadala uliofanyika baina yangu na baadhi ya wanachuoni huko Tunis baada ya kutoka kitabu changu kiitwacho Thummah-Tadaytu, na kwa kuwa wao walisoma ndani yake ufafanuzi wangu juu ya Sul-hu ya Hudaibiyyah, basi wao kwa upande wao walitoa uchambuzi kuhusu sehemu hii kwa kusema: "Ikiwa Masahaba waliasi amri ya Mtume **(s.a.w.w)** ya kuchinja na kunyoa, hawakuitekeleza amri yake yeyote mbona Ali ibn Abi Talib alikuwa pamoja nao naye hakuitekeleza amri ya Mtume **(s.a.w.w)**. Mimi niliwajibu kama ifuatavyo:

**Kwanza**: Ali ibn Abi Talib alikuwa hahesabiwi kuwa ni miongoni mwa Masahaba, bali yeye ni ndugu wa Mtume wa Mwenyezi Mungu na Ibn Ammi yake Mtume na ni mume wa Binti yake na baba wa watoto wa Mtume. Kwa hakika Ali alikuwa pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu upande mmoja na watu wengine walikuwa upande mwingine, basi mpokezi wa hadithi ndani ya Sahih Bukhari anaposema kwamba Mtume **(s.a.w.w)** aliwaamuru Masahaba wake kuchinja na kunyoa, basi Abul-Hasan (a.s) hakuhesabiwa kuwa miongoni mwao, kwani yeye yu katika daraja ya Harun kwa Musa. Je, hamuoni kwamba sala ya Mtume haiwi kamili mpaka iongezwe juu yake sala ya kizazi cha Mtume, na Ali ndiyo Bwana (kiongozi) wa kizazi cha Muhammad bila mpinzani yeyote? Hivyo basi Abubakr, Umar, Uthman na Masahaba wote sala zao hazisihi mpaka ndani yake uwemo utajo wa Ali ibn Abi Talib pamoja na Muhammad ibn Abdillah.

**Pili**: Bila shaka Mtume **(s.a.w.w)** siku zote alikuwa akimshirikisha nduguye Ali kuhusu mnyama wa kuchinja, kama hali hiyo ilivyotokea katika Hija ya mwisho wakati Ali alipofika kutoka Yemen na Mtume akamuuliza; "Je, umechinja kichinjo gani ewe Ali?" Akasema, "Kile alichochinja Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**." Basi Mtume akamshirikisha katika kichinjo chake. Tukio hili wamelieleza wanahadithi wote na wana historia, basi hapana budi kuwa alikuwa pia mshirika wake siku ya Hudaibiyyah. Tatu: Hapana shaka Ali ndiye alikuwa muandishi wa mapatano siku ya Hudaibiyyah kwa imla ya Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** na hakumpinga Mtume kwa lolote muda wote wa uhai wake, siyo katika munasaba wa Hudaibiyyah wala sehemu nyingine, na Historia haikusajili kwamba yeye Ali (a.s) alipinga amri ya Mtume au kuasi japo mara moja, hapana kabisa hakufanya hivyo na wala hakukimbia hata mara moja kwenye vita na kumuacha nduguye na Ibn Ammi yake katikati ya maadui, bali alikuwa siku zote akijitolea nafsi yake.

Kwa kifupi ni kwamba, Ali ibn Abi Talib yeye ni kama nafsi ya Mtume na ndiyo maana Mtume alikuwa akisema: "Haifai kwa mwingine yeyote kuwa na janaba msikitini isipokuwa mimi na Ali." Wengi wa hao niliokuwa nikijadiliana nao walitosheka kwa maelezo niliyoyaleta na wakakiri kwamba Ali ibn Abi Talib hakwenda kinyume na amri ya Mtume wa Mwenyezi Mungu katika uhai wake. Bukhari ameandika katika Sahihi yake juzuu ya nane, mlango wa Karahiyatul-khilaf Kitabul-i'tisam bil-kitabi Was-Sunnah. Imepokewa kutoka kwa Abdallah ibn Abbas amesema: "Pindi mauti yalipomkabili Mtume **(s.a.w.w)** alisema, na hali yakuwa nyumbani humo wamo watu, akiwemo Umar ibn Khat-tab, Mtume akasema: Nipeni karatasi na kidawati nikuandikieni maandiko ambayo kamwe hamtapotea baada yake. Umar akasema, Bila shaka Mtume amezidiwa na maradhi, nanyi mnayo Qur'ani, basi kinatutosha Kitabu cha Mwenyezi Mungu. Wakahitilafiana watu waliokuwemo ndani ya nyumba, na wakazozana, wengine wanasema mpeni Mtume wa Mwenyezi Mungu akuandikieni maandiko ambayo hamtapotea baada yake, na wengine wanasema alivyosema Umar. Walipozidisha hitilafu yao na makelele mbele ya Mtume **(s.a.w.w)**, Mtume akasema Niondokeeni. Basi Ibn Abbas siku zote akawa husema, Hakika msiba mkubwa kuliko yote ni ule uliopita baina ya Mtume na baina ya kuwaandikia maandiko yale kutokana na hitilafu zao na fujo zao"[1].

Na hii ni amri nyingine ya Mtume wa Mwenyezi Mungu ambayo Masahaba waliikabili kwa kuipinga na kuiasi na kumtia dosari Mtume **(s.a.w.w)**. Kwa kuongezea ni kwamba, Umar ibn Khatab alisema mbele ya Mtume **(s.a.w.w**) alipowataka wamletee karatasi na kidawati ili awaandikie maandiko ambayo yatawazuwia wasipotee Umar akasema: "Bila shaka Mtume anaweweseka" Mwenyezi Mungu atulinde (kutokana na matamko ya aina hiyo).

Lakini Bukhari aliistahi ibara hiyo na kuibadilisha kuwa "Maradhi yamemzidi" kwa kuwa tu aliyesema ni Umar ibn Khatab. Na utamuona pindi anapolipuuzia jina la Umar ndani ya riwaya hii husema, "Wakasema Mtume wa Mwenyezi Mungu anaweweseka, na huku (kupinda mapokezi ya hadithi) ndiyo uaminifu wa Bukhari katika kunakili hadithi. (Baadaye tutamtengea mlango wake maalum). Kwa hali yoyote ile, wengi wa wanachuoni wa hadithi na wanahistoria wameeleza kuwa, Umar ibn Khatab ndiye aliyesema "Bila shaka Mtume wa Mwenyezi Mungu anaweweseka." Na ndipo Masahaba wengi wakamfuatia wakasema kama alivyosema yeye mbele ya Mtume **(s.a.w.w)**. Sisi tunajaribu kuiangalia hali halisi ya msimamo huo unaotisha na sauti kali, wingi wa makelele na kuhitilafiana kwao mbele ya Mtume **(s.a.w.w)**, na iwe kwa namna yoyote ile iliyoelezwa katika riwaya hii, lakini riwaya haielezi ukweli halisi wa jinsi ya tukio namna lilivyokuwa isipokuwa kidogo tu, kama ambavyo tutakaposoma kitabu cha historia kinachoeleza maisha ya Musa [(a.s)], kitabu hicho kieleze kwa namna yoyote ile, lakini hakiwezi kufikia ufafanuzi wa filamu ya sinema tunayoishuhudia kwa macho. Bukhari ameandika ndani ya Sahih yake, juzuu ya saba, mlango wa Yanayoruhusiwa miongoni mwa ghadhabu

1. Sahihi Bukhari Juz.8 uk.161 na Juz. 1 uk.37 na Juz.5 uk.138.

na kuwa mkali kwa ajili ya amri ya Mwenyezi Mungu Kitabul-adab, amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** alijenga kijichumba kilichotengenezwa kwa makuti au jamvi, basi Mtume **(s.a.w.w)** alitoka akaswali mahala hapo watu wakamfuata kisha wakaja usiku mwingine, walipofika Mtume akakawiya hakutoka, wakapaza sauti zao na wakaugonga mlango, (Mtume) akawatokea hali ya kuwa mwenye ghadhabu akawaambia hamukuacha kutenda kitendo chenu mpaka nikadhani kwamba hii itafaradhishwa kwenu, basi nendeni mukaswali majumbani mwenu kwani sala iliyo bora ni ile aswaliyo mtu nyumbani mwake isipokuwa sala ya faradhi"[1].

Kwa masikitiko makubwa ni kwamba, Umar ibn Khatab alikwenda kinyume na amri ya Mtume **(s.a.w.w)** na akawakusanya watu kwenye sala ya Sunna katika zama za Ukhalifa wake akasema kwa tendo hilo kuwa, "Hakika hii ni Bid'a na ni Bid'a nzuri. " Kwenye uzushi wake huu, walimfuata Masahaba wengi ambao walikuwa wanayakubali maoni yake na kumuunga mkono kwa kila alifanyalo na alisemalo. Ni Ali ibn Abi Talib na watu wa nyumba yake tu ndiyo waliomkhalifu Umar nao ndio ambao walikuwa hawafanyi isipokuwa kwa mujibu wa maamrisho ya kiongozi wao ambaye ni Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** na hawakumkubali mwingine badala yake. Kama ikiwa kila Bid'a ni upotevu na kila upotevu ni motoni, basi unafikiria nini juu ya mambo yaliyozushwa ili kupinga maamuzi ya Mtume **(s.a.w.w)**?

Bukhari ameandika katika Sahih yake juzuu ya tano mlango wa Ghaz-watu Zaidi ibn Haritha Kitabul-maghazi. Imepokewa kutoka kwa Ibn Umar (r.a) amesema, "Mtume wa Mwenyezi Mungu alimpa uamirijeshi Usama juu ya watu, lakini wakapinga (Usama) kupewa uamirijeshi, Mtume akasema, Ikiwa mnapinga uamiri wake kwa hakika mlikwishaupinga uamirijeshi wa baba yake kabla yake, namuapa Mwenyezi Mungu hakika baba yake alistahiki mno uamiri na alikuwa ni mtu nimpendaye, na huyu ni miongoni mwa watu niwapendao baada ya baba yake."[2]. Kisa hiki wamekieleza wanahistoria kwa upana, na wameeleza jinsi Mtume wa Mwenyezi Mungu alivyowalaani waliobakia nyuma wasiende kwenye msafara wa Usamah ambaye ni kijana mdogo aliyekuwa hajafikia hata umri wa miaka kumi na saba, na Mtume alimpa uamiri wa jeshi ambalo ndani yake alikuwemo Abubakr, Umar, Talhah, Zubair na Abdur-rahman ibn A'ufi na wakuu wengine wa Kiquraish wote. Lakini katika jeshi hilo Mtume hakumtia humo Ali ibn Abi Talib wala Sahaba yeyote aliyekuwa akimpenda Ali [(a.s)].

Kama ilivyo kawaida ya Bukhari, siku zote hufupisha matukio na huzikata hadithi ili kulinda heshima ya viongozi waliopita miongoni mwa Masahaba, pamoja na hali hiyo ndani ya hayo aliyoyaandika yanatosha kwa mwenye kutaka kuifikia haki. Bukhari pia ameandika ndani ya Sahih yake juzuu ya pili mlango wa Onyo kwa anayefululiza kufunga usiku na mchana Kitabus-Saum. Imepokewa kutoka kwa Abuhurairah amesema:"Mtume **(s.a.w.w)** alikataza kufululiza katika saumu, mtu mmoja miongoni mwa

---

1. Sahih Bukhari Juz. 7 uk. 99 na Juz. 2 uk. 252 na Juz. 4 uk. 168.
2. Sahihi Bukhari Juzuu ya 5 uk. 84.

Waislamu akamwambia Mtume, Mbona wewe unafululiza ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Mtume akasema: **Nani kati yenu aliye kama mimi? Mimi nikilala Mola wangu hunilisha na kuninywesha. Walipokataa kuacha kufululiza Mtume alifululiza pamoja nao siku moja kisha siku nyingine hatimaye wakauona mwezi, Mtume akasema; Lau (mwezi) ungechelewa ningekuongezeeni.**"[1] Hili ni kama onyo kwao walipokataa kuacha kufululiza.

Wakoje Masahaba hawa ambao Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** anawakataza kitu hawakatazikі na anakariri katazo lake lakini hawasikii. Je, hawakusoma kauli ya Mwenyezi Mungu aliposema:

وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانتَهُوا وَاتَّقُوا اللَّـهَ إِنَّ اللَّـهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٧﴾

"Anayokupeni Mtume yachukuweni, na anayokukatazeni yaacheni, mcheni Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu**.**" (Qur'ani, 59:7).

Pamoja na onyo la Mwenyezi Mungu kwa yeyote anayemkhalifu Mtume wake, kuwa (atamuadhibu) adhabu kali, baadhi ya Masahaba hawayapi uzito wowote makemeo na maonyo ya Mwenyezi Mungu.

Iwapo hali yao ndiyo hii, basi hapana shaka juu ya unafiki wao japokuwa walijionesha kuwa wanasali sana, na kufunga na kuwa wakali katika dini mpaka wakafikia daraja ya kuharamisha kukutana na wake zao ili tu wasije kwenda Mina na huku dhakari zao zikidondoka manii, na wakigomea yale ambayo Mtume wa Mwenyezi Mungu anayatenda kama ilivyotangulia katika uchambuzi uliopita. Bukhari ameandika ndani ya Sahih yake juzuu ya tano, mlango wa Mtume kumpeleka Khalid ibn Walid kwa Bani Judhaimah Kitabul-maghazi. lmepokewa kutoka kwa Az-zuhri naye toka kwa Salim nave kapokea kutoka kwa baba yake amesema: "Mtume **(s.a.w.w)** alimtuma Khalid ibn Walid kwenda kwa Bani Judhaimah, Khalid aliwaita kwenye Uislamu ikawa hawakuweza kutamka vizuri hicho, "Tumesilimu," bali wakawa wanasema, Swaba 'naa, basi Khalid akaanza kuwauwa na kuwateka, na akampa kila mmoja wetu mateka wake kiasi kwamba siku moja Khalidi alimuamuru kila mtu miongoni mwetu amuuwe mateka wake mimi nikasema; Wallahi mimi simuuwi mateka wangu wala mtu yeyote katika jamaa zangu hatamuuwa mateka wake. Tulipofika kwa Mtume na tukamuelezea hali hiyo, alinyanyua mikono yake juu kisha akasema: "Ewe Mwenyezi Mungu hakika najitakasa kwako kutokana na yale aliyoyatenda Khalid akasema hivyo mara mbili."[2] Wanahistoria wamelielezea tukio hili kwa upana zaidi, na wametaja namna Khalid alivyotenda maasi haya mabaya yeye mwenyewe na wale waliomtii miongoni mwa baadhi ya Masahaba, na hawakufuata maamrisho ya Mtume yanayokataza kumuua mtu yeyote aliyesilimu. Kwa hakika ni maasi makubwa ambayo yalimwaga damu ya watu isiyo na makosa, na hasa kwa kuwa Mtume **(s.a.w.w)** alimuamuru Khalid awalinganie kwenye Uislamu na hakumuamuru kuwaua. Khalid ibn Walid, ulimzidi ufahari wa zania za kijahiliya (kabla

1. Sahih Bukhari Juzuu 2 uk.243.
2. Sahih Bukhari Juz.5 uk.107 na Juz.8uk.118.

kuja Uislamu) na chuki ya kishetani ikambeba, kwani hawa Bani Judhaimah walipata kumuua ammi yake Khalid aliyekuwa akiitwa Al-Fakih ibn Al-Mughirah katika zama za Kijahiliyyah, ndiyo maana Khalid akawahadaa watu hao akawaambia wekeni silaha zenu chini kwani watu wamekwisha silimu hakuna hatari yoyote ni amani tupu kisha akaamrisha (wakakamatwa) wakafungwa mikono na waliuawa watu wengi miongoni mwao.

Baada ya Masahaba wengi wema kutambua makusudio ya Khalid, walikimbia kutoka kwenye jeshi hilo wakaenda kwa Mtume **(s.a.w.w)** na wakampa habari zilivyo, Mtume wa Mwenyezi Mungu alijitakasa kutokana na tendo la Khalid, na akamtuma Ali ibn Abi Talib akaenda lipa fidia za damu iliyomwagwa huko na mali iliyoharibiwa. Na ili kulifahamu (vyema) tukio hili kwa ufafanuzi, si vibaya kuyasoma maandiko aliyoyaandika Abbas Mahmud Al-I'qad katika kitabu chake kiitwacho, Abqariyyatu Khalid ukurasa wa 57 na 58 lakini ameeleza kwa njia ya kupotosha maelezo kama ifuatavyo: Baada ya ushindi wa Maka, Mtume alielekeza umuhimu wa kueneza dini kwa kuzisafisha sehemu za majangwani zinazoizunguka Maka kutokana na ibada za masanamu, hivyo basi alituma vikosi kwenda kwenye makabila ya sehemu hizo ili kuyalingania Uislamu na kupata uhakika wa nia za makabila hayo. Miongoni mwa vikosi hivyo ni kile cha Khalid kwenda kwa Bani Judhaimah na kikosi hicho kilikuwa na watu karibu mia tatu na hamsini wakiwemo Muhajirina na Ansari na Bani Sulaim, na Mtume aliwatuma wakalinganie dini wala hakuwaamuru kupigana. Hawa Bani Judhaimah walikuwa ni kitongoji kikali mno zama za Jahiliyyah na wakiitwa kuwa ni "Walamba Damu" na miongoni mwa watu waliouawa na Bani Judhaimah zama hizo ni Alfakihu ibn Al-Mughirah na nduguye ambao wote ni ammi zake Khalid ibn Walid, na wengine waliouawa na Bani Judhaimah ni mzazi wa Abdur-Rahman ibn Auf, na Malik ibn Rashid na nduguze watatu miongoni mwa Bani Sulaim (wote hawa) waliuawa mahala pamoja, na wengine (waliuawa) kutoka makabila mengine mbali mbali.

Khalid ibn Walid alipofika kwa Bani Judhaimah wao walifahamu kuwa miongoni mwa watu waliokuja na Khalid wamo Bani Sulaim, basi wakabeba silaha zao na wakajiandaa kwa vita kisha wakakataa kuteremka kwenye vipando vyao. Khalid akawauliza, "Je, ninyi ni Waislamu?" Inasemekana baadhi yao walimjibu ndiyo, na wengine walimjibu wakasema, "Saba'naa Saba'naa" yaani tumekwisha aacha kuabudu sanamu. Kisha akawauliza, "Nini basi maana ya kubeba kwenu silaha?" Wakasema, "Bila shaka baina yetu na baadhi ya jamaa wa Kiarabu kuna uadui, tumechelea kuwa labda ninyi ndiyo hao hiyo ndiyo sababu ya sisi kuchukua silaha." Basi Khalid akawaambia, "Wekeni silaha chini kwani watu wamekwisha silimu." Mtu mmoja miongoni mwao aitwaye Jahdam akawapigia ukelele wenziwe akasema, "Ole wenu enyi kizazi cha Judhaimah huyo ni Khalid, Wallahi hakuna jambo litakalotokea baada ya kuweka silaha isipokuwa mtatekwa, na hakuna kitakachotokea baada ya kutekwa isipokuwa ni kuuawa, Wallahi mimi kamwe siweki silaha yangu chini." Basi wenziwe waliendelea kumrai mpaka akawa miongoni mwa walioweka silaha zao na wengine wakatawanyika. Hapo ndipo Khalid alipoamuru wakamatwe wakafungwa mikono wakauawa. Bani Sulaim na Waarabu wengine wakamtii Khalid katika mauaji hayo, lakini Muhajirina na

Ansari wakamkemea Khalid na kumwambia asimuuwe yeyote isipokuwa iwe imeamuriwa na Mtume **(s.a.w.w)** kuwa auawe. Hatimaye habari zikamfikia Mtume, basi alinyanyua mikono juu mbinguni na akasema mara tatu; "Ewe Mwenyezi Mungu najitakasa kwako kutokana na matendo aliyoyafanya Khalid ibn Walid" na akamtuma Ali ibn Abi talib aende kwa Banu Judhaimah akalipe fidia ya damu iliyomwagwa na mali zao zilizoharibiwa. Kwa hakika Masahaba wengi wakubwa walichukizwa na tukio hilo, ikiwa ni pamoja na wale waliokuwepo kwenye kikosi hicho na wale ambao hawakuwepo. Abdur-rahman alikasirika sana mpaka akamtuhumu Khalid kwamba aliwauwa jamaa hao kwa makausudi ili alipe kisasi cha ammi zake." Mwisho wa kunukuu maneno ya Al-Iq-Qad.

Basi haya ndiyo aliyoyataja Al-Iqqa'd kwa njia ya kupotosha ndani ya kitabu chake kiitwacho Ab-Qariyatu Khalid. Huyu Al-iqa'ad ni kama walivyo wasomi wengi wa Kisunni, baada ya kukisimulia kisa hiki kwa ukamilifu anatafuta sababu za kupoza na kumpamba Khalid ibn Walid, lakini ni sababu ambazo hazisimami na kuwa dalili za kumtakasa Khalid kutokana na matendo yake, wala akili iliyosalimika haiwezi kuzikubali sababu hizo. Na huyu Al-iqad hana sababu yoyote isipokuwa ni kule kuandika, Abqariyatu Khalid kwa maana ya Ushujaa wa Khalid. Kwani kila alichokileta miongoni mwa sababu ni dhaifu mfano wa nyumba ya buibui na yeyote azisomaye ataona ubovu na unyonge wa utetezi uliomo. Basi vipi anamtetea Khalid hali yakuwa yeye mwenyewe ameshuhudia katika maneno yake kuwa Mtume **(s.a.w.w)** aliwatuma kwenda kulingania watu na hakuwaamrisha kufanya mauaji, na amekiri kwamba Banu Judhaimah waliweka sialaha zao chini baada ya kuwa walikuwa wamezibeba wakati Khalid alipowahadaa kwa kuwaambia, "Wekeni silaha chini, kwani watu wamekwisha silimu." Amekiri pia kwamba, Jahdam ambaye alikataa kuweka silaha na akawaonya jamaa zake kwamba Khalid atawageuka pale alipowaambia, "Ole wenu huyo ni Khalid, Wallahi hakuna jambo litakalotokea baada ya kuweka silaha zenu isipokuwa kutekwa na hakuna litakalotokea baada ya kutekwa isipokuwa ni kuuawa, Wallahi siweki silaha yangu kamwe." Al-iqad amesema kwamba, Bani Judhaimah hawakuacha kumrai mwenzao mpaka akaweka silaha yake, na kitendo chao hiki kinajulisha juu ya Uislamu wa watu hawa na nia yao njema.

Sasa iwapo Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** aliwatuma kulingania watu dini na wala hakuwaamuru kuua kama ulivyoshuhudia wewe Iqa'ad, basi Khalid anazo sababu zipi zilizomfanya aende kinyume na amri za Mtume **(s.a.w.w)**? Hili ni tatizo sifikirii kama unaweza kulitatua ewe iqa'ad. Na kama watu hawa waliweka silaha zao na wakatangaza Uislamu wao .na wakamzidi jamaa yao aliyekuwa ameapa kutokuweka silaha yake na hatimaye wakamkinaisha kama ulivyo kiri wewe I'qaad, basi ni ipi hiyo sababu iliyomfanya Khalid awafanyie khiana na kuwaua hali kawafunga na hawana hata silaha? Hapana shaka wewe umesema kwamba, "Khalid aliamrisha wafungwe na kuwaelekeza kwenye panga na kuwaua." Hapa umezua tatizo jingine na sikufikiria kwamba unaweza kupata ufumbuzi wake ewe Iqa'ad. Na je, hivi Uislamu umewaamuru Waislamu kuwaua watu ambao hawajawashambulia? Tena kwa kukadiria tu kwamba jamaa hao hawakutangaza Uislamu wao, sivyo kabisa hii ndiyo hoja

wanayoitumia Mustashirikina Orientalist Kisha umekiri mara nyingine kwamba Mtume **(s.a.w.w)** hakumuamuru Khalid kuwaua jamaa hao pale uliposema kwamba: "Muhajirina na Ansari walimkemea Khalid asimuue yeyote isipokuwa iwe ni amri ya Mtume **(s.a.w.w)** kuwaua." Basi sababu gani uliyonayo ewe Iqa'ad hata umtakase Khalid? Inatosha kuwa ni jibu dhidi ya Iqa'ad ya kwamba yeye amebatilisha sababu zake yeye mwenyewe na kuzipinga zote pale alipokiri kwa kusema: "**Na kwa hakika Masahaba wengi wakubwa walichukizwa na tukio hilo, ikiwa ni pamoja na wale waliokuwepo kwenye kikosi hicho na wale ambao hawakuwepo**." Basi iwapo Masahaba wakubwa walishinikiza kumpinga Khalid mpaka wakakimbia kutoka kwenye jeshi lake na wakamshitakia kwa Mtume **(s.a.w.w)**, na kama Abdur-rahman ibn Auf alimshutumu Khalid kuwa aliwaua jamaa hao kwa makusudi ili alipe kisasi cha ammi zake kama alivyoshuhudia hayo I'qaad, na iwapo Mtume **(s.a.w.w)** alinyanyua mikono yake juu mbinguni na akasema mara tatu: "Ewe Mwenyezi Mungu, mimi najitakasa kwako kutokana na aliyoyafanya Khalid ibn Walid."

Na (vile vile) kama Mtume **(s.a.w.w)** alimtuma Ali akiwa na mali ambayo aliitoa fidia kwa damu na mali za Bani Judhaimah zilizoharibiwa mpaka akawaridhisha kama alivyoshuhudia Iqa'ad, hii inajulisha kwamba jamaa hao walisilimu, lakini Khalid aliwadhulumu na kuwashambulia. Sasa je, kuna yeyote mwenye kuuliza amuulize Iqa'ad anayejaribu kumtaksa Khalid kwamba, "Je, yeye Iq a'ad' anajua zaidi kuliko Mtume wa Mwenyezi Mungu ambaye alijitakasa mbele ya Mwenyezi Mungu mara tatu kutokana na vitendo vya Khalid? Au anajua mno kuliko wale Masahaba wakubwa ambao walimkemea Khalid? Au anajua mno kuliko wale Masahaba waliokuwepo kwenye tukio na wakakimbia kutoka kwenye kikosi hicho kutokana na uzito wa yale waliyoyaona miongoni mwa matendo yake mabaya? Au anajua mno kuliko Abdurrahman ibn A'uf ambaye alikuwa pamoja na Khalid katika kikosi hicho, na hapana shaka anamtambua vyema Khalid kuliko Iqa'ad, lakini alimshutumu kwa mauaji ya jamaa hao kwa makusudi ili alipe kisasi cha Ammi zake? Mwenyezi Mungu autokomeze ung'ang'anizi wa kipofu na chuki za kijinga ambavyo vinageuza ukweli. Iwe iwavyo, pamoja na Bukhari kulifupisha tukio hili na kuliandika kwa mistari minne, lakini hicho kidogo alichokiandika kimetosheleza kuufahamu mwenendo wa Khalid na Masahaba wengine ambao walimtii katika mauaji ya Waislamu wasio na hatia, na Iqa'ad amewataja kwa kusema: "Banu Sulaim na wengine miongoni mwa Waarabu aliokuwa nao Khalid, walimtii katika mauaji ya Banu Judhaimah." Lakini Bukhari hawakuwaondoa katika Masahaba waliomtii Khalid ila watu wawili au watatu waliokimbia kutoka katika jeshi na kurudi kwa Mtume na kumshitaki Khalid. Ewe Iqa'ad huwezi kabisa kutukinaisha kwamba Muhajirina na Ansar ambao idadi yao ilikuwa mia tatu na hamsini kama ulivyobainisha hivyo wewe mwenyewe eti hawakumtii Khalid katika mauaji ya jamaa hao, na kuwa walikimbia wote kutoka kwenye jeshi, hili halikubaliki kwa mtafiti yeyote yule. Lakini hilo ni jaribio lako la kulinda heshima ya waliopita miongoni mwa Masahaba na kuufunika ukweli kwa gharama yoyote ile, lakini fahamu kwamba sasa wakati umefika wa kuondoa kifuniko hicho na kuitambua haki.

Huyu Khalid ibn Walid anayo mauaji mengi mabaya aliyoyafanya ambayo historia imetusimulia hasa yale ya siku alipofika Bat-tah wakati Abubakr alipomteua aongoze jeshi kubwa lenye Masahaba wakubwa wakubwa wa mwanzoni. Huko kwa mara nyingine alimfanyia khiyana Malik ibn Nuwairah na watu wake walipoweka silaha zao chini, yeye akafunga mikono kisha wakauawa hali ya kuwa wamefungwa, na kisha Khalid akamuingilia mke wa Malik aliyekuwa akiitwa Laila Ummu Tamim katika usiku ule ule aliouawa mumewe. Umar ibn Khat-tab aliposimama kumrudishia kisasi akamwambia:"Umemuua mtu Muislamu kisha umemuingilia mkewe, Wallahi nitakupiga kwa mawe ewe adui wa Mwenyezi Mungu." Lakini Abubakr alisimama upande wa Khalid kumtetea akamwambia Umar "Mwache Khalid bila shaka yeye amejitahidi akakosea." Na hili ni tukio jingine ambalo kulifafanua inachukua muda na kwa kweli ni halifai hata kulieleza. Basi ni mara ngapi mwenye kudhulumiwa hunyang'anywa haki yake kwa kuwa anayemdhulumu ana nguvu? Na ni mara ngapi dhalimu hutetewa uovu wake kwa kuwa ni tajiri na yu karibu na mtawala?

Basi huyu Bukhari wakati anaeleza kisa cha Banu Judhaimah anakikata na anasema: "Mtume alimpeleka Khalid kwa Banu Judhaimah akawaita kwenye Uislamu, wakashindwa kutamka vizuri kuwa "Tumesilimu, Aslamnaa bali wakawa wanasema; Saba 'anaa, Saba 'anaa " Ewe Bukhari, hawa Banu Judhaimah walikuwa ni Waajemi au walikuwa Waturuki, Wahindi au Wajerumani mpaka wasiweze kusema, "Aslamnaa, yaani Tumesilimu? Au wao ni miongoni mwa Makabila ya Kiarabu ambayo Qur'ani ilishuka kwa lugha yao? Lakini ung'ang'anizi wa kipofu na njama kubwa ambazo zimepita ili tu kuilinda heshima ya Masahaba ndizo zilizomfanya Bukhari aseme maneno kama haya kwa lengo la kumtakasa Khalid ibn Walid. Huu nao ni utata, kwani anasema: "Khalid akawauliza ninyi ni Waislamu?" Kisha I'qaad anasema, "Inasemekana baadhi yao walimjibu ndiyo, na baadhi yao walimjibu, Saba'anaa Saba'naa...

Neno hili Inasemekana linajulisha wazi kwamba watu hawa kina Iqa'ad, Bukhari n..k.. hung'ang'ania kitu ambacho huenda kikawachanganya mawazo watu ili wapate kumtakasa Khalid ibn Walid, kwa kuwa Khalid ibn Walid ndiyo upanga ulio tayari kutumiwa na mtawala, naye ndiye mtetezi wa Ukhalifa wa mabavu ambaye pamoja na wafuasi wake ndiyo watekelezaji wa nguvu zenye kupambana na kila yule ambaye nafsi yake inamuambia kuwa atoke na apinge yote yaliyopitishwa na mashujaa wa Saqifah siku aliyofariki Mtume **(s.a.w.w)**.

10

# WAULIZE WANAOFAHAMU

## UTENDAJI WA MASAHABA KUHUSU MAAMRISHO YA MTUME (s.a.w.w) BAADA YA KUFARIKI KWAKE

### NAMNA WALIVYOIPOTOSHA SUNNA YA MTUME (s.a.w.w)

Bukhari ameandika katika Sahihi yake, juzuu ya kwanza Babu tadh-yius-salah. Imepokewa toka kwa Ghailan, Anas ibn Malik amesema: "**Sikioni chochote miongoni mwa mambo ambayo yalikuwepo zama za Mtume (s.a.w.w)." Akaambiwa, "Sala (ipo)" akasema: "Je, hivi hamjaipoteza kwa kuyaacha yaliyomo ndani ya Sala**?" Na amesema: nilimsikia Az-zuhri anasema: "**Niliingia kwa Anas ibn Malik alipokuwa Damascus nikamkuta analia, nikamwambia kitu gani kinakuliza? Akasema: sikioni chochote vitu nilivyovifahamu isipokuwa hii sala, na hii sala imekwisha puuzwa**."[1]

Kama ambavyo Bukhari ameandika katika juzuu ya kwanza mlango wa fadhila za sala ya alfajiri kwa jamaa, amesema: "**Ametusimulia A'amash, amesema: Nilimsikia Salim, kasema:Nilimsikia Ummud-dar-dai akisema, alikuja kwangu Dar-dai hali yakuwa amekasirika, nikamwambia, Kito gani kimekukasirisha? Akasema, Wallahi sikioni chochote katika umma wa Muhammad ila ni kwamba wote wanasali tu**." [2].

Na ameandika Bukhari ndani ya juzuu ya pili Babul-khuruji Ilal-musalla bighair minbar kutoka kwa Abu Said Al-khudri amesema: "Mtume **(s.a.w.w)** alikuwa akitoka kwenda kusali siku ya Idil-fitri au Al-az'ha, basi kitu cha kwanza alichokuwa akianza ni sala kisha baada ya hapo huwapa mawaidha watu, hivyo basi watu waliendelea kufanya hivyo mpaka siku moja nilitoka na Mar-wan akiwa ndiyo amiri wa Madina, katika sala ya Idul-az-ha au Idid-fitr, basi (Mar-wan) akataka kupanda juu ya Minbar kabla ya kusali, nikaivuta nguo yake naye akaivuta kisha akapanda na akahutubu kabla ya sala, baadaye nikamwambia "Wallahi mmebadilisha.

"Akasema: "Ewe Abu Said yamekwisha toweka uyajuwayo wewe." Nikamwambia "Wallahi niyajuwayo mimi ni bora kuliko yale nisiyoyajua." Akasema: "Hakika watu walikuwa hawakai kwa ajili yetu baada ya sala, ndiyo maana mimi nikaifanya hotuba kabla ya Sala."[3] Ni vipi Masahaba katika zama za Anas ibn Malik na zama za Abud-dardai pia katika zama za Mar-wan zama ambazo ziko karibu mno na zama za uhai wa Mtume **(s.a.w.w)**, wanabadilisha Sunna za Mtume na kupuuza kila kitu mpaka sala kama ulivyosikia? Si hivyo tu bali wamezigeuza Sunna za Mtume **(s.a.w.w)** kwa maslahi yao yasiyo na maana na hasa kwa kuwa, Banu Umayyah walijitengenezea Sunna ya kumtukana na kumlaani Ali na watu wa nyumba ya Mtume. Waliwatukana juu ya mimbari kila baada ya khutba, kwa ajili hiyo watu wengi wakawa hutawanyika siku ya Idul-az-ha au Idul-fitr kila

---

1. Sahih Bukhari Juz 1. uk.134.
2. Sahih Bukhari Juz. 1 uk.159.
3. Sahih Bukhari Juz. 2 uk.4.

inapomalizika sala kwa kuwa walikuwa hawapendi kumsikia Imam wao anamlaani Ali ibn Abi Talib na watu wa nyumba ya Mtume. Kwa sababu hiyo basi, Banu Umayyah wakafanya makusudi hasa kubadilisha Sunna ya Mtume na wakatanguliza hotuba kabla ya Sala katika sikukuu hizo mbili ili wapate fursa ya kumtukana na kumlaani Ali mbele ya Waislamu wote na yote hayo ni kuonesha chuki yao. Kiongozi wa hawa wote ni Muawiyah ibn Abi Sufiyani, yeye ndiye aliyewawekea mwenendo huo ambao waliufanya kuwa ni miongoni mwa sunna tukufu ambayo kwayo wakijikurubishia kwa Mwenyezi Mungu.

Kuna baadhi ya wanahistoria wamesimulia kwamba, mmoja wa Maimamu wao alikamilisha hotuba yake siku ya Ijumaa na akasahau kumlaani Ali akawa anateremka kutoka kwenye mimbari ili aje kusalisha, basi ghafla watu wakawa wanapiga kelele kutoka kila upande, "Umeacha Sunna, umesahau Sunna." Sunna gani hiyo? Naam kwa masikitiko makubwa basi, hii ndiyo Bid'a iliyozushwa na Muawiyyah ibn Abi Sufiyan na ilidumu kwa miaka themanini ikizunguka kwenye mimbari za Waislamu na makovu yake yamebakia hadi leo. Pamoja na yote hayo Ahlus-Sunna Wal-Jamaa wanamuombea radhi Muawiyyah na wafuasi wake, na wala hawawezi kumkosoa wala kumtia kombo kwa madai ya kuwaheshimu Masahaba. Kila sifa njema zinamstahiki Mwenyezi Mungu, watafiti wenye moyo safi miongoni mwa Umma wa Kiislamu sasa wameanza kufahamu haki kutokana na isiyo kuwa haki, na wengi kati yao wameanza kujinasua kwenye kifungo cha masahaba ambacho hakuna aliyekitebgeneza isipokuwa Muawuya na wafuasi wake na wale wampendao. Sasa hivi Masunni wameanza kuzinduka kutokana na tatizo hili, ingawaje wakati huo wanawatetea Masahaba wote kiasi cha kumlaani mwenye kumkosoa mmoja miongoni mwa Masahaba. Iwapo Masunni utawaambia kwamba "Bila shaka laana yenu hii mnayolaani pia inamkumba Muawiya ibn Abi Sufyaan kwani yeye Muawiya kwa kufanya hivyo alikusudia moja kwa moja kumtukana Mtume wa Mwenyezi Mungu ambaye amesema: Yeyote atakaye mtukana Ali, basi hakika amenitukana mimi basi atakuwa amemtukana Mwenyezi Mungu." Basi hapo utawaona wanachanganyikiwa na kushindwa kujibu na hatimaye husema vitu ambavyo ikiwa vina maana Fulani basi maana hiyo itakuwa ni mawazo duni na ung'anga'nizi wa kipofu ambao unakera.

Kwa mfano baadhi yao husema: Huu ni uongo uliofanywa na Shia, na baadhi yao husema, Ee Bwana hao ni Masahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** wanao uhuru wa kuwasema Masahaba wenzao namna watakavyo, amma sisi hatuna daraja hata ya kuwakosoa. Umetakasika ewe Mwenyezi Mungu na sifa njema ni zako, kwa hakika maneno yako yamenifahamisha katika Qur'an Tukufu juu ya ukweli ambao ilikuwa vigumu mimi kuufahamu na kuamini, na kila nilipokuwa nikisoma maneno yako yasemayo kwamba:

وَلَقَدْ ذَرَأْنَا لِجَهَنَّمَ كَثِيرًا مِّنَ الْجِنِّ وَالْإِنسِ ۖ لَهُمْ قُلُوبٌ لَّا يَفْقَهُونَ بِهَا وَلَهُمْ أَعْيُنٌ لَّا يُبْصِرُونَ
بِهَا وَلَهُمْ آذَانٌ لَّا يَسْمَعُونَ بِهَا ۚ أُولَـٰئِكَ كَالْأَنْعَامِ بَلْ هُمْ أَضَلُّ ۚ أُولَـٰئِكَ هُمُ الْغَافِلُونَ ﴿١٧٩﴾

Na bila shaka tumewaumbia moto wa Jahannam wengi katika majini na wanadamu (kwani) wanazo nyoyo lakini kwa nyoyo hizo hakuna wanachokifahamu, na wanayo macho, lakini hawaoni kwa macho hayo, na

wanayo masikio lakini hawasikii kwa masikio hayo. Basi hao ni kama wanyama, bali wao ni wapotofu zaidi, hao ndio walioghafilika" (Qur'ani, 7:179).

Nisomapo maneno hayo nashangaa moyoni mwangu na ninasema ni vipi itakuwa hivyo? Je, inawezekana mnyama asiyesema akawa ameongoka kuliko mtu? Inawezekana mtu akachonga jiwe kisha akaliabudia na kuliomba riziki na msaada? Lakini namshukuru Mwenyezi Mungu, kushangaa kwangu kumetoweka baada ya kupanuka mawasiliano yangu na watu, na niliposafiri kwenda India nimeona maajabu makubwa, nimewaona madaktari katika elimu ya viumbe wanaofahamu umbile la mtu na viungo vyake. lakini bado wanaabudu ng'ombe, lakini lau jambo hili baya lingefanywa na watu wajinga miongoni mwa Wahindu udhuru wao ungekubalika, lakini utamuona mwana taaluma mzuri miongoni mwao anaabudia ng'ombe, jiwe, bahari, jua na mwezi!! Kwa hali hii huna la kufanya baada ya (kuona haya) isipokuwa ukubali na ufahamu maana inayojulishwa na Qur'ani kuhusu watu ambao wao ni wapotevu mno kuliko mnyama.

Ushahidi wa Abud-dharri kuhusu baadhi ya Masahaba Bukhari ameandika ndani ya juzuu ya pili mlango wa Man ud-diyat Zakatuhu falaisa Bikanzin, Imepokewa kutoka kwa Al-Ahnaf ibn Qais amesema: "Nilikaa na watu miongoni mwa Maquraishi, basi alikuja mtu mwenye nywele na nguo zilizochakaa pia na hali yake mpaka akasimama mbele yao akasalimia kisha akasema, Wabashirie kuwa (watachomwa) kwa mawe yaliyochemshwa katika moto wa jahannam, kisha yatawekwa juu ya chuchu ya maziwa ya mmoja wenu na kutokea kwenye sehemu inayoanzia shingo katika bega na kuwekwa (tena) kwenye sehemu inayoanzia shingo katika bega na kutokea kwenye chuchu, kisha (mtu huyo) akageuka na akakaa kwenye nguzo, nami nikamfuata nikakaa naye na hali yakuwa simfahamu kuwa ni nani, basi nikamwambia mimi sioni isipokuwa jamaa wamechukizwa kwa maneno uliyoyasema. Akasema: Bila shaka hao hawafahamu chochote, kipenzi changu aliniambia ndiye aliyeniambia... Mimi nikamwambia ni nani huyo kipenzi chako?

Akasema Mtume **(s.a.w.w)** aliniambia: Ewe Abudharri wauona (mlima wa) Uhd? Nikaliangalia jua na muda wa mchana uliobakia na hali ya kuwa nahisi kwamba Mtume anataka kunituma kwa shida aliyonayo, nikamwambia, Naam, Akasema: Mimi sipendi kuwa na dhahabu mfano wa Uhud (bali nikiwa nayo) nitaitoa yote isipokuwa dinari tatu. Watu hawa hawana akili, bali wanaikusanya (mali ya) dunia, hapana Wallahi siwaombi dunia yao wala sitaki wanilipie deni mpaka nitakapokutana na Mwenyezi Mungu Mtukufu[1].

Bukhari pia ameandika katika juzuu ya saba, Babul-haudh Waqaulullahi Taala In-naa A'atainakal-kawthar. Imepokewa toka kwa At'a ibn Yasar kutoka kwa Abu Hurairah kwamba, Mtume **(s.a.w.w)** amesema: "Kuna wakati mimi nitakuwa nimesimama (siku ya Qiyama), ghafla watafika jamaa, nami nitakapowatambua atatokea mtu kati yangu na wao, atasema Njooni, Mimi nitasema, Waende wapi? Atasema Wallahi motoni, Nitasema

1. Sahih Bukhari Juz. 2 uk.112.

Yalikuwaje mambo yao? Atasema, Hakika wao waligeuka baada yako kinyumenyume.

Kisha jamaa wengine watafika mpaka nitapowafahamu, atatoka mtu kati yangu na wao atasema, Njooni, Nitasema waende wapi? Atasema Wallahi motoni, Nitasema Yalikuwaje mambo yao? Atasema: Hakika wao waligeuka baada yako kinyumenyume, Sitamuona miongoni mwao anayesalimika isipokuwa wachache tu." Na imepokewa kutoka kwa Abu Said Al-khudri kwamba: Siku hiyo patasemwa: "Bila shaka wewe hufahamu waliyoyazusha baada yako, basi mimi nitasema na aangamie, aangamie aliyebadilisha baada yangu."[1]

Kama alivyoandika Bukhari katika juzuu ya tano mlango wa Ghaz-watul-Hudaibiyyah na kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo, "Kwa hakika Mwenyezi Mungu amewapa radhi Waumini waliofungamana nawe chini ya mti." Imepokewa kutoka kwa Al-alaa ibn Al-musayyab naye kapokea kwa baba yake amesema: "Nilikutana na Al-barra ibn A'zib (r.a) nikamwambia, pongezi wewe ulisuhubiana na Mtume **(s.a.w.w)** na ukampa baia chini ya mti, akasema, Ewe mtoto wa ndugu yangu hakika wewe hujuwi tuliyoyazua baada yake."[2]

Na huo ni ushahidi mkubwa utokao kwa Sahaba mkubwa ambaye kwa uchache alikuwa mkweli kwa nafsi yake na watu, na ushahidi wake unakuja kutia nguvu maneno aliyoyasema Mwenyezi Mungu kuwahusu Masahaba alipowaambia, "(Muhammad) akifa au akiuawa mtageuka nyuma kwa visigino vyenu." Na unatia nguvu maneno aliyoyasema Mtume **(s.a.w.w)**, "Nitaambiwa, hakika wao walirudi baada yako kinyume nyume." Huyu Al-barraa ibn Azib ni Sahaba Mtukufu miongoni mwa wale wa mwanzo ambao walimpa baia Mtume **(s.a.w.w)** chini ya mti, yeye anaishuhudia nafsi yake na za wengine miongoni mwa Masahaba kwamba, wao walizusha baada ya kufa Mtume **(s.a.w.w)** ili watu wasije danganyika kutokana na Masahaba, na alibainisha wazi kwamba kuwa sahaba wa Mtume **(s.a.w.w)** na kumpa baia chini ya mti ambako kumeitwa kuwa ni Baia'tur-ridh-wan vitu hivi havizuwii Sahaba kupotoka na kuritadi baada ya Mtume **(s.a.w.w)**.

Bukhari ameandika katika juzuu ya nane mlango wa kauli ya Mtume **(s.a.w.w)** isemayo. Mtafuata mwenendo wa watu waliopita kabla yenu. Imepokewa kutoka kwa Ataa ibn Yasar, kutoka kwa Abu Said Al-Khudri naye kutoka kwa Mtume **(s.a.w.w)** amesema: "Mtafuata mwenendo wa waliopita kabla yenu hatua baada ya hatua na dhiraa baada ya dhiraa, mpaka hata wakiingia kwenye shimo la kenge nanyi mtawafuata." Tukamwambia Mtume, "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu hao ni Mayahudi na Wakristo?" Mtume akasema, "Ni kina nani basi (kama si hao)?"[3] Ushahidi wa historia kuhusu Masahaba Baada ya Qur'ani na Sunna tunao ushahidi mwingine ambao huenda ukawa bayana na wazi zaidi, kwani unatambulikana kwa watu walioishi katika kipindi hicho na wakaushuhudia na kuwa nao sambamba, na hatimaye ukawa ni historia na ni matukio yaliyohifadhiwa. Tutaposoma vitabu vya historia vya Ah-lusunna Wal-

---

1.Sahih Bukhari Juz.7 uk.209.

2.Sahihi Bukhari Juz.5 uk.66.

3.Sahih Biikhari Juz.8 uk. 151.

Jamaa kama vile Tabari, Ibnul-Athir, Ibn Sa'ad, Abul-Fidai, Ibnu Qutaibah na wengineo tutaona maajabu makubwa na tutafahamu kwamba, wayasemayo Masunni juu ya uadilifu wa Masahaba na kwamba haifai kumkosoa yeyote miongoni mwao ni maneno yasiyoweza kusimamisha dalili,wala akili iliyosalimika haiwezi kukubali isipokuwa (kwa watu) wang'ang'anizi ambao kiza limewazibia mwangaza kiasi ambacho hawawezi kutofautisha baina ya Mtume Muhammad ambaye ni Ma'asum, hatamki kwa matamanio na wala hafanyi kitu isipokuwa ni cha haki tu. Wanashindwa kutofautisha kati yake na Masahaba wake ambao Qur'ani imeshuhudia juu ya unafiki na uovu wao na uchache wa uchamungu walionao, ndiyo maana utawaona Masunni wanawatetea Masahaba zaidi ya vile wanavyomtetea Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**.

Nakupigia mfano kuhusu hilo. Wakati unapomwambia mmoja wao kwamba (maonyo yaliyomo katika) Sura ya Abasa Watawalla hayakukusudiwa kwa Mtume **(s.a.w.w)**, bali aliyekusudiwa ni mmoja wa Masahaba wakubwa ambaye Mwenyezi Mungu alimlaumu kwa kiburi chake na kuchukizwa kwake alipomuona yule kipofu masikini. Hapo utamuona (Sunni) hakubaliani na tafsiri hii na atasema, "Muhammad hakuwa ila ni mtu tu, kwani ni mara nyingi alikosea na Mola wake akamlaumu mahala pengi tu, yeye hakuhifadhika isipokuwa katika kufikisha Qur'ani. Basi huu ndiyo mtazamo wa Masunni kumhusu Mtume wa Mwenyezi Mungu. Lakini iwapo wewe utasema kwamba, "Umar ibn Khatab alikosea alipozusha sala ya tarewehe ambayo Mtume wa Mwenyezi Mungu alikataza isisaliwe Msikitini na akawaamuru watu wasali majumbani mwao mmoja mmoja sala ya sunna (yaani isiyo ya faradhi), hapo utamuona Sunni anamtetea Umar ibn Khatab kwa nguvu na hakubali majadiliano bali atasema: "Hiyo ni Bid'a nzuri", na atajaribu kwa juhudi zake zote kumtafutia sababu (ya kumuepushia kosa) pamoja na kuwepo kwa tamko la Mtume **(s.a.w.w)** inalokataza.

Na ukimwambia kwamba, "Umar alizuwia haki ya Muallafatul-Qulubi haki ambayo Mwenyezi Mungu aliipitisha ndani ya Kitabu chake kitukufu." Pia utamuona anasema, "Bila shaka Bwana wetu Umar alifahamu kwamba Uislamu umekwishapata nguvu, ndiyo maana aliwaambia hao wanaoimarishwa nyoyo zao katika dini kwamba: Hatuna haja nanyi, naye (Umar) alikuwa akifahamu maana za Qur'ani zinavyoeleza kuliko watu wote! Loh! (ewe bwana) halikushangazi jibu kama hili? Kuna mtu mmoja miongoni mwa Masunni kwa hakika yeye amevuka mpaka pale nilipomwambia; "Hebu tuachane na Bid'a nzuri na hao wanaoimarishwa nyoyo zao katika dini, Je, utamteteaje Umar pale alipoanza kutoa onyo kwamba angeliichoma moto nyumba ya Bibi Fatmah pamoja na waliomo, isipokuwa (watasalimika tu) iwapo watatoka kwenda kula kiapo cha utii (kwa Abubakr)?" Huyu bwana alinijibu wazi wazi (bila woga akasema): "Anayo haki (ya kufanya hivyo) kwani lau asingefanya hivyo watu wengi miongoni mwa Masahaba wangejizuwia (kutoa baia) wakabaki kwa Ali ibn Abi Talib na fitina ingetokea." Watu kama hawa kuzungumza nao haisaidii wala kunufaisha kitu, na kwa masikitiko makubwa nasema kwamba, "Wengi wa Masunni wana mawazo ya aina hii, kwani wao hawaitambui haki isipokuwa kupitia kwa Umar ibn Khatab na matendo yake, kwa hiyo

wameigeuza kanuni na wakawa huitambua haki kupitia kwa watu, wakati kinachotakiwa ni kuwatambua watu kupitia kwenye haki. Itambue haki utawatambua watu wa haki kama alivyosema Imam Ali (a.s).

Kisha kanuni hii imeenea kwa Masunni na ikamvuka Umar ibn Khatab mpaka ikawafikia Masahaba wote, na wote ni waadilifu haiwezekani kwa mtu yeyote kuwakosoa au kuwapinga, kwa maana hiyo basi Masunni wameweka pazia zito na kizuwizi kigumu kwa mchunguzi anayetaka kufahamu haki, utamuona hawezi kukwepa wimbi moja mpaka yanapomkumba mawimbi mengi na hawawezi kukwepa hatari yeyote mpaka hatari nyingi zinapozuia njia yake, na masikini hawezi kufikia ukingoni kwa amani isipokuwa atapokuwa miongoni mwa wenye azma, subira na ushujaa. Tukirudi kwenye maudhui ya historia ni kwamba, baadhi ya Masahaba wamevuliwa nguo zao, siri zao za moyoni kukashifika na ulidhihiri ukweli wao ambao walijaribu kwa juhudi zao zote kuuficha mbele za watu, au watetezi wao na wafuasi wao walijaribu kuuficha au unaweza kusema kuwa watawala waovu na mashabiki wao ndiyo waliojaribu kila namna kuficha ukweli huo. Kitu cha kwanza kukitupia macho ni msimamo wa Masahaba hawa juu ya Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** waliouonyesha mapema baada ya kufariki kwake, na ni vipi walimuacha na hawakushughulika kumuandaa, kumkosha na wala kumvika sanda na hatimaye kumzika, bali walikimbilia kwenye mashauriano yao katika Klabu ya Bani Saidah, wakagombana na kushindana ni nani aupate Ukhalifa ambao walikuwa wakimfahamu fika muhusika wake kisheria ambaye walikula kiapo cha utii kwake katika zama za uhai wa Mtume **(s.a.w.w)**.

Kinachotuthibitishia kwamba watu hawa waliitumia fursa ya kutokuwepo kwa Ali na Bani Hashim ambao utu wao haukuwapa nafasi ya kuuacha mwili wa Mtume **(s.a.w.w)** ukiwa umefunikwa eti tu wakagombee Ukhalifa katika Saqifah, kwa ajili hiyo jamaa hawa wakapitisha haraka haraka maamuzi kuhusu Ukhalifa kabla Bani Hashim hawajamaliza kazi yao tukufu ya kumuandaa Mtume kwa ajili ya mazishi ili hatimaye wawalazimishe kukubali matokeo hayo, na wasiweze kusema chochote wala kutoa hoja hasa kwa kuwa jamaa hao waliokuwa Saqifa walikwisha kukubaliana kumuua yeyote atakayejaribu kutengua kile walichokipitisha, eti kwa madai ya kuwadhibiti wapinzani na kutuliza machafuko. Wanahistoria wanaeleza mambo ya ajabu yaliyotokea katika siku hizo yaliyofanywa na hao Masahaba ambao baadaye walikuwa ndiyo Makhalifa wa Mtume **(s.a.w.w)** na pia wakawa ndiyo maamiri wa Waumini. Miongoni mwa mambo hayo ni kama vile kuwalazimisha watu kutoa Baia (kiapo cha utii) kwa kuwapiga na kuwatisha kwa nguvu na kuihujumu nyumba ya Bibi Fatmah kisha kuikashifu nyumba hiyo na pia kumbana tumbo lake (Bibi Fatimah) kwenye mlango ambao alikuwa yuko nyuma yake mpaka mimba yake ikaporomoka.

Si hivyo tu bali walimtoa nje Ali hali ya kuwa kafungwa na kumuonya kuwa watamuua iwapo atakataa kutoa Baia, na walimpokonya Bibi Fatmah haki zake ikiwa ni pamoja na zawadi (ya Fadak) na mirathi yake na sehemu ya Qaraba  wa Mtume kiasi kwamba, Bibi Fatimah amekufa hali ya kuwa amewakasirikia waliomfanyai hayo na akiwaombea katika kila Sala (waangamizwe), na (Mwana Fatmah) alizikwa usiku tena kwa siri na hao

jamaa hawakuhudhuria jeneza lake!! Vile vile jamaa hao wa Saqifah, waliwaua Masahaba waliokataa kutoa zaka kwa Abubakr kutokana na kusita kwao ili tu wafahamu sababu za Ali kutokuwa Khalifa, kwani wakijuwacho wao ni kuwa yeye ndiye waliyempa Baia (ya kuwa Khalifa wao) zama za uhai wa Mtume **(s.a.w.w)** huko kwenye Bonde la Khum. Pia miongoni mwa mambo waliyoyafanya ni kama vile kuhalalisha mambo ya haramu, kuivuka mipaka ya Mwenyezi Mungu na kuwaua watu wema miongoni mwa Waislamu kisha wakawaingilia wake zao bila kuheshimu kipindi cha Eda. Walibadilisha hukumu za Mwenyezi Mungu na Mtume wake zilizojengeka kwa msingi wa Kitabu Qur'an na Sunnah wakaweka badali yake hukumu za ijitihadi zitakazotumikia maslahi yao binafsi.

Na kama vile kunywa kwao pombe na kudumu kwenye zinaa hali yakuwa ni viongozi wa Waislamu na ni watawala ndani ya Waislamu, vile vile kumuondosha Abudharri Al-Ghifari na kumfukuza kutoka Madina mji wa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** mpaka akafa akiwa peke yake (na alifanyiwa hivyo) bila ya kosa lolote alilolitenda, walimpiga Ammar mpaka wakampasua, walimpiga Abdallah ibn Mas-udi mpaka wakamvunja mbavu zake, na pia wakawauzulu Masahaba wema kwenye madaraka na kuwatawalisha waovu miongoni mwa Banu Umayyah ambao ni maadui wa Uislamu. Na (miongoni mwa mambo yao) ni kama vile kuwatukana na kuwalaani watu wa nyumba ya Mtume ambao Mwenyezi Mungu amewaondolea uchafu na amewatakasa mno, na pia kuwaua wale wanaowafuata watu wa nyumba ya Mtume miongoni mwa Masahaba wema. Na kama vile kukalia kwao Ukhalifa kwa shinikizo la nguvu, mauaji, vitisho na kumdhibiti yeyote anayewapinga kwa njia mbali mbali kama vile kumuua kwa kumvamia au kumtilia sumu na mengineyo. Na miongoni mwa hayo ni kuushambulia mji wa Mtume kwa jeshi la Yazid. likafanya lilivyotaka bila kujali kauli ya Mtume aliyosema: "Bila shaka mji wangu huu wa Madina ni mji mtukufu, basi yeyote atakayezua ndani yake tukio la uovu laana ya Mwenyezi Mungu na Malaika na watu wote iwe juu yake." Na kama vile kuipiga kwao nyumba ya Mwenyezi Mungu kwa Manjaniq na kuichoma moto nyumba hiyo tukufu ya Mwenyezi Mungu, na ndani yake waliwaua baadhi ya Masahaba.

Na kama vile kumpiga kwao vita Amirul-Muumina Ali ambaye ni Bwana wa Mawasii na ndiye kiongozi wa kizazi kitukufu ambaye mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa na cheo cha Harun kwa Musa, (walimpiga vita) katika vita vya Jamal, vita ya Siffin, na vita ya Nah-rawan (yote hayo) kwa sababu ya tamaa duni na dunia yenye kutoweka. Na kama vile kuwaua mabwana wawili wa vijana wa peponi, Imam Hasan kwa kumtilia sumu na Imam Husein kwa kumchinja, haikuwatosha hali hiyo bali walikiandama na kukiuwa kizazi cha Mtume **(s.a.w.w)** chote, na hakusalimika isipokuwa Ali ibn Husein, na matendo yao mengine yanayomfanya mtu atoe machozi, nami naiepusha kalamu yangu isiyaandike. Masunni wanayajua mengi miongoni mwa hayo na ndiyo maana huwa wanajaribu kwa juhudi zao zote kuwazuiwia Waislamu kusoma vitabu vya historia na kuchunguza maisha ya Masahaba. Niliyoyataja sasa hivi kutoka katika vitabu vya historia miongoni mwa maovu na machafu hapana shaka ni matendo ya Masahaba, basi

haiwezekani kwa mtu mwenye akili baada ya kuyasoma haya akaendelea kuwatakasa masahaba na kuhukumu kuwa wao ni waadilifu ila kama atakuwa hana akili. Pamoja na yote tuliyoyayaeleza sisi tunangalia kwa makini mno na, tunauthamini uadilifu wa baadhi ya Masahaba na usafi wao, uchamungu wao na kumpenda" kwao Mwenyezi Mungu na Mtume wake **(s.a.w.w)**, na msimamo wao zama za Mtume **(s.a.w.w)** mpaka walipokufa na hawakubadilisha kamwe, basi Mwenyezi Mungu awaridhie na awape makazi karibu na mpenzi wao na Mtume wao Muhammad **(s.a.w.w)**.

Masahaba hawa ni watukufu na ni bora, hawezi kuifedhehesha heshima yao mfedheheshaji, au akawazulia mwenye kuzua, na kwa hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu amewasifu mahala pengi ndani ya Kitabu chake kitukufu, kama ambavyo Mtume ameutukuza usuhuba wao na ikhlasi yao si mara moja. Na kama ambavyo historia haikusajili kwao isipokuwa msimamo Mtukufu uliojaa utu, wema, ushujaa, uchamungu na kujinyima (mambo ya dunia) kwa ajili ya dhati ya Mwenyezi Mungu. Basi pongezi ni zao na marejeo yao ni kwenye mabustani ambayo milango yake iko wazi kwa ajili yao na radhi ya Mwenyezi Mungu kwao ni kubwa na hayo ndiyo malipo ya wenye kushukuru, na wenye kushukuru kama kilivyosema Kitabu cha Mwenyezi Mungu. usisahau kuwa ni wachache mno. Ama wale waliojisalimisha na imani haikuingia mioyoni mwao na wakasuhubiana na Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** kwa tamaa (ya mambo fulani) na kwa khofu au kwa haja ya nafsi zao, Qur'ani imewalaumu na kuwaonya, naye Mtume **(s.a.w.w)** amewahadharisha na amewalaani mahala pengi, na historia nayo imeyasajili matendo yao na misimamo yao mibaya. Watu hawa basi, hawastahiki heshima ya aina yoyote wala cheo chochote, achilia mbali kuwatakia radhi (kitu ambacho kinafanya) tuwaweke daraja ya Mtume na Mashahidi na watu wema. Kwa hiyo basi, huu ndiyo msimamo wa haki ambao unapima mizani kwa uadilifu wala hauchupi mipaka aliyoiweka Mwenyezi Mungu kwa waja wake kwamba, wawatawalishe (viongozi) waaminifu na wawapinge (viongozi) waovu na wajitenge nao mbali. Mwenyezi Mungu anasema:"

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ تَوَلَّوْا قَوْمًا غَضِبَ اللَّـهُ عَلَيْهِم مَّا هُم مِّنكُمْ وَلَا مِنْهُمْ وَيَحْلِفُونَ عَلَى الْكَذِبِ
وَهُمْ يَعْلَمُونَ ﴿١٤﴾ أَعَدَّ اللَّـهُ لَهُمْ عَذَابًا شَدِيدًا إِنَّهُمْ سَاءَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٥﴾ اتَّخَذُوا أَيْمَانَهُمْ
جُنَّةً فَصَدُّوا عَن سَبِيلِ اللَّـهِ فَلَهُمْ عَذَابٌ مُّهِينٌ ﴿١٦﴾ لَّن تُغْنِيَ عَنْهُمْ أَمْوَالُهُمْ وَلَا أَوْلَادُهُم مِّنَ
اللَّـهِ شَيْئًا أُولَـٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿١٧﴾ يَوْمَ يَبْعَثُهُمُ اللَّـهُ جَمِيعًا فَيَحْلِفُونَ لَهُ
كَمَا يَحْلِفُونَ لَكُمْ وَيَحْسَبُونَ أَنَّهُمْ عَلَىٰ شَيْءٍ أَلَا إِنَّهُمْ هُمُ الْكَاذِبُونَ ﴿١٨﴾ اسْتَحْوَذَ عَلَيْهِمُ
الشَّيْطَانُ فَأَنسَاهُمْ ذِكْرَ اللَّـهِ أُولَـٰئِكَ حِزْبُ الشَّيْطَانِ أَلَا إِنَّ حِزْبَ الشَّيْطَانِ هُمُ الْخَاسِرُونَ
﴿١٩﴾ إِنَّ الَّذِينَ يُحَادُّونَ اللَّـهَ وَرَسُولَهُ أُولَـٰئِكَ فِي الْأَذَلِّينَ ﴿٢٠﴾ كَتَبَ اللَّـهُ لَأَغْلِبَنَّ أَنَا وَرُسُلِي إِنَّ
اللَّـهَ قَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٢١﴾ لَّا تَجِدُ قَوْمًا يُؤْمِنُونَ بِاللَّـهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ يُوَادُّونَ مَنْ حَادَّ اللَّـهَ وَرَسُولَهُ وَلَوْ
كَانُوا آبَاءَهُمْ أَوْ أَبْنَاءَهُمْ أَوْ إِخْوَانَهُمْ أَوْ عَشِيرَتَهُمْ أُولَـٰئِكَ كَتَبَ فِي قُلُوبِهِمُ الْإِيمَانَ وَأَيَّدَهُم بِرُوحٍ
مِّنْهُ وَيُدْخِلُهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا رَضِيَ اللَّـهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ
أُولَـٰئِكَ حِزْبُ اللَّـهِ أَلَا إِنَّ حِزْبَ اللَّـهِ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٢٢﴾

Je, huwaoni wale ambao wamewatawalisha watu aliowakasirikia Mwenyezi Mungu? Hao si miongoni mwenu wala si miongoni mwao, na huapa viapo vya uongo na hali wanajua kuwa ni uongo. Mwenyezi Mungu amewaandalia adhabu kali, kwa hakika waliyokuwa wakiyatenda ni mabaya kabisa. Wamefanya viapo vyao kuwa ngao (yao) wakawazuwia (watu) njia ya Mwenyezi Mungu, basi watapata adhabu ifedheheshayo, mali zao na watoto wao hawatawafaa kitu mbele ya Mwenyezi Mungu, hao ndiyo watu wa motoni watakaa humo milele. (Wakumbushe) siku atakayowafufua Mwenyezi Mungu wote wamuapie (viapo vya uongo) kama wanavyoapa kwenu na wanadhani ya kwamba wamepata kitu! Kwa hakika wao ndio waongo kabisa. Shetani amewatawala akawasahaulisha kumkumbuka Mwenyezi Mungu, hao ndiyo kundi la shetani, fahamuni kwamba bila shaka kundi la shetani ndilo lenye kupata hasara. Hakika wale wanaompinga Mwenyezi Mungu na Mtume wake hao ndiyo miongoni mwa watakaodhalilika. Mwenyezi Mungu amekwishaandika yakuwa bila shaka nitashinda Mimi na Mitume wangu, hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye nguvu, mwenye kushinda. Huwezi kuwakuta watu wanaomuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho kuwa wanawapenda wale wanaompinga Mwenyezi Mungu na Mtume wake, hata kama watakuwa ni baba zao au watoto wao au ndugu zao au jamaa zao, hao ndiyo ambao Mwenyezi Mungu ameithibitisha imani nyoyoni mwao na akawatia nguvu kwa roho itokayo kwake, na atawaingiza katika mabustani yapitayo mito ndani yake, humo watakaa daima, Mwenyezi Mungu amewawia radhi na wao wanamridhia, hao ndiyo kundi la Mwenyezi Mungu, Fahamuni! bila shaka kundi la Mwenyezi Mungu ndilo lenye kufaulu, (58:14-22).

Arnesema kweli Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Nami siachi fursa kuandika katika makusudio haya kwamba, Mashia ndiyo wako kwenye ukweli, kwani wao hawampendi yeyote isipokuwa ni kwa ajili ya Mtume Muhammad na watu wa nyumba yake na Masahaba waliopita kwenye njia ya Mtume na watu wa nyumba yake, na ( hawa Mashia wanawapenda) waumini ambao waliwafuata hao kwa wema mpaka siku ya mwisho. Amma wasiokuwa Mashia miongoni mwa Waislamu wanawapenda Masahaba wote bila kujali wanaompinga Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na mara nyingi hutolea ushahidi kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo:

وَالَّذِينَ جَاءُوا مِن بَعْدِهِمْ يَقُولُونَ رَبَّنَا اغْفِرْ لَنَا وَلِإِخْوَانِنَا الَّذِينَ سَبَقُونَا بِالْإِيمَانِ وَلَا تَجْعَلْ فِي قُلُوبِنَا غِلًّا لِّلَّذِينَ آمَنُوا رَبَّنَا إِنَّكَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿١٠﴾

"Ewe Mola wetu! tusamehe sisi na ndugu zetu waliotutangulia katika imani, wala usijaalie ndani ya nyoyo zetu undani kuwafanyia wale walioamini, Ewe Mola wetu! hakika wewe ni mpole mwenye huruma." (Qur'ani, 59:10).

Na kwa ajili hiyo basi utawaona Masunni wanawaombea radhi Ali (a.s) na Muawiyyah bila kujali aliyoyatenda Muawiyah miongoni mwa matendo ambayo yaweza kusemwa ni kufru na upotofu na ni kumpiga vita Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na nimetaja katika maelezo yaliyopita habari hizo si vibaya kuzirejea kama ifuatavyo: Mtu mmoja miongoni mwa wacha Mungu alizuru kaburi la Sahaba Mtukufu Hujri ibn Adiyyi Al-kindi,

akamkuta kaburini hapo mtu fulani analia sana, akamdhania kuwa huyo ni miongoni mwa Mashia akamuuliza; "Kwa nini unalia?" Yule mtu akajibu, "Namlilia Sayyidna Hujri Radhi yallahu anhu. " akasema: "Ni yepi yaliyompata?" Akasema: "Aliuawa na Sayydna Muawiyah Radhiyallahu anhu. " Akamwambia: "Kwa nini alimuuwa?" Akajibu:"Kwa sababu alikataa kumlaani Sayidina Ali Radhiyallahu anhu.

Yule mtu mwema akamwambia yule aliyekuwa akilia: "Nami nakulilia wewe radhi ya Mungu ikufikie." Basi faida gani ya kupokezana huku kwa kuwapenda Masahaba wote mpaka tunawaona Masunni hawamswalii Mtume Muhammad na kizazi chake isipokuwa wataongeza juu yake Masahaba wake wote. Si Qur'an iliyowaamuru kufanya hivyo wala Mtume wa Mwenyezi Mungu hakuwataka kufanya hivyo wala yeyote miongoni mwa Masahaba hakulisema jambo hilo (ilivyo sawa ni kwamba), sala ya Mtume ilikuwa ni kwa Muhammad na kizazi cha Muhammad kama ilivyoshuka Qur'ani na kama alivyoifundisha Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**. Kama nitakuwa nashaka juu ya kitu fulani, basi sina na sitakuwa nashaka kwamba, Mwenyezi Mungu amewataka waumini kuwapenda Al-Qurba ambao ni watu wa nyumba ya Mtume na akafanya upendo huo kwao kuwa ni faradhi kama ndiyo malipo ya ujumbe wa Mtume Muhammad, akasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

قُل لَّا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا إِلَّا الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبَىٰ ﴿٢٣﴾

"Waambie sikuombeni malipo (yoyote kwa kazi hii ya Utume) isipokuwa muwapende Qaraba (zangu), (Qur'an, 42:23).

Hapana shaka Waislamu wote wameafikiana bila tofauti kati yao juu ya kuwapenda watu wa nyumba ya Mtume (a.s), lakini Waislamu wametofautiana juu ya kuwapenda wasiokuwa hao, na Mtume **(s.a.w.w)** amesema: "**Wacha lenye kukutia shaka ufanye lisilokutia shaka.**" Kauli ya Mashia juu ya kuwapenda watu wa nyumba ya Mtume na wanaowafuata haina shaka, na (amma) kauli ya Masunni juu ya kuwapenda masahaba wote, ina mashaka ndani yake, basi itakuwaje kwa Muislamu awapende maadui wa watu wa nyumba ya Mtume ambao waliwauwa na eti awatakie radhi maadui hao? Je, huu si utata unaochukiza?

Hebu wachana na kauli za watu waliochanganyikiwa na baadhi ya Masufi ambao wanadai kwamba, mtu hawezi kuutakasa moyo wake wala hawezi kuijuwa imani ya kweli mpaka pale itakapokuwa haikubakia moyoni mwake chembe ndogo ya kuwabughudhi waja wa Mwenyezi Mungu wote miongoni mwao wakiwa ni Mayahudi, Wakristo na Walahidi na Washirikina, na (hawa jamaa) wanazo kauli za ajabu zinazoshangaza kuhusiana na jambo hili ambazo zinaambatana na zile za wabashiri miongoni mwa watu wa Kanisa la Kikiristo ambao wanawadanganya watu kuwa "Mwenyezi Mungu ni upendo na dini ni upendo, basi yeyote mwenye kuwapenda viumbe wa Mungu hana haja ya kusali na kufunga na kuhiji na mengineyo." Mambo hayo kwa hakika naapa ni uzushi ambao Qur'ani na Sunna havikubaliani nao wala akili haikubali. Qur'ani inasema: "Huwezi kuwakuta watu wamuaminio Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho wanawapenda watu wanaompinga Mwenyezi Mungu na Mtume wake." Na amesema tena:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الْيَهُودَ وَالنَّصَارَىٰ أَوْلِيَاءَ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ وَمَن يَتَوَلَّهُم مِّنكُمْ فَإِنَّهُ مِنْهُمْ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿٥١﴾

"Enyi mlioamini msiwafanye Mayahudi na Wakristo kuwa walinzi wa maslahi (yenu), wao kwa wao ni marafiki, basi yeyote atakayewatawalisha miongoni mwenu yeye atakuwa miongoni mwao, bila shaka Mwenyezi Mungu hawaongozi watu madhalimu." (Qur'an, 5:51).

Na amesema tena Mwenyezi Mungu:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَّخِذُوا آبَاءَكُمْ وَإِخْوَانَكُمْ أَوْلِيَاءَ إِنِ اسْتَحَبُّوا الْكُفْرَ عَلَى الْإِيمَانِ وَمَن يَتَوَلَّهُم مِّنكُمْ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٢٣﴾

"Enyi mlioamini, msiwafanye baba zenu na ndugu zenu kuwa walinzi wa maslahi yenu ikiwa watauboresha ukafiri kuliko imani, na yeyote miongoni mwenu atakayewafanya kuwa walinzi wa maslahi yake (yote) hao ndio madhalimu." (Qur'an, 9:23).

Na pia amesema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَّخِذُوا عَدُوِّي وَعَدُوَّكُمْ أَوْلِيَاءَ تُلْقُونَ إِلَيْهِم بِالْمَوَدَّةِ وَقَدْ كَفَرُوا بِمَا جَاءَكُم مِّنَ الْحَقِّ... ﴿١﴾

"Enyi mlioamini msiwafanye adui zangu na adui zenu kuwa walinzi wa maslahi yenu na mukawapenda hali yakuwa wameikanusha haki iliyokujieni." (Qur'an, 60:1).

Naye Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Haikamiliki imani ya Muumini mpaka yawe mapenzi yake ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na chuki yake iwe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu**." Pia amesema: "**Hayakutani ndani ya moyo wa Muumini, mapenzi ya kumpenda Mwenyezi Mungu na mapenzi ya kumpenda adui wa Mwenyezi Mungu**." Hadithi zinazohusu jambo hili ni nyingi mno, na akili yatosha peke yake kuwa ni dalili, kwani Mwenyezi Mungu ameijaza imani (katika nyoyo za) waumini na akaipamba ndani ya nyoyo zao, na akachukia kwao kufru na uovu na uasi, hivyo basi mtu anaweza kumchukia mwanawe au baba yake au nduguye kwa sababu ya kupinga haki na kudumu katika njia ya shetani, na anaweza kumpenda na kumfanya rafiki mtu baki asiye na uhusiano naye isipokuwa udugu wa Kiislamu.

Kutokana na yote haya basi ni wajibu mapenzi yetu na urafiki wetu uwe kwa wale ambao Mwenyezi Mungu ameamrisha tuwapende, kama ambavyo ni wajibu ghadhabu zetu na chuki yetu na kujitenga kwetu kuwe juu ya wale ambao Mwenyezi Mungu ameamrisha tujitenge nao. Na kwa ajili hiyo basi, ndiyo maana tumemtawalisha Ali na Maimamu ambao ni miongoni mwa wanawe bila ya kuwa sisi tunauhusiano nao hapo kabla ya kuwapenda, na kuwapenda wao ni kwa sababu Qur'ani na Sunna na historia na akili hazikuachia nafasi yoyote ya kuwatilia mashaka ya aina yoyote.

Na kwa ajili hiyo pia kujitenga kwetu na Masahaba ambao walipora haki ya Ali katika Ukhalifa, kumekuja bila ya kuwepo uhusiano fulani uliotangulia wa kuwachukia, na hayo ni kwa sababu Qur'ani na Sunna na historia na akili vimetuachia sisi mashaka makubwa kuhusu wao. Na kwa kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** ametuamrisha kwa kusema: "**Acha linalokutia shaka ufanye lisilokutia shaka**." Basi haifai kwa

Muislamu kufuata jambo lolote lenye mashaka, akaacha Qur'ani ambayo haina shaka ndani yake. Kama ambayo ni wajibu juu ya kila Muislamu kujikomboa kutoka katika kifungo alichofungwa na kufuata kwake bila kujua bali aipe akili yake maamuzi bila kujali mawazo ya hapo kabla na chuki iliyojificha ndani, kwani nafsi na shetani ni maadui wa hatari wanaompambia mwanaadamu matendo yake mabaya akayaona kuwa mazuri.

Uzuri ulioje wa maneno aliyoyasema Imam Busairi ndani ya Burdah: "Ipinge nafsi na shetani uviasi (viwili hivi), bila shaka nasaha (yao) wanakudanganya, basi wachukie." Ni wajibu juu ya Waislamu kumuogopa Mwenyezi Mungu kuhusu waja wake wema miongoni mwao, ama wale ambao hawakuwa miongoni mwa wachamungu basi hawana heshima yoyote (wanayostahiki) kwani Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: "Si uteti kuzungumza habari za mtu muovu" ili Waislamu wapate kuyafahamu mambo yake wasije wakadanganyika kwake na wasijempa utawala. Pia Waislamu wanawajibika leo hii wawe wakweli kwa nafsi zao na waangalie hali yao inavyotia uchungu na huzuni na udhalili walio nao, wasitosheke na kujifaharisha kwa sifa za wakubwa zao waliopita, lau kama viongozi wetu waliopita wangekuwa kwenye haki kama tunavyodhania leo hii, basi sisi tusingefikia kwenye matokeo haya ambayo moja kwa moja yamekuja kutokana na kugeuka ambako kulitokea katika Ummah baada ya kufariki kwa Mtume wake. Roho yangu na roho za Walimwengu ziwefidia kwake.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُونُوا قَوَّامِينَ بِالْقِسْطِ شُهَدَاءَ لِلَّـهِ وَلَوْ عَلَىٰ أَنفُسِكُمْ أَوِ الْوَالِدَيْنِ وَالْأَقْرَبِينَ إِن يَكُنْ غَنِيًّا أَوْ فَقِيرًا فَاللَّـهُ أَوْلَىٰ بِهِمَا فَلَا تَتَّبِعُوا الْهَوَىٰ أَن تَعْدِلُوا وَإِن تَلْوُوا أَوْ تُعْرِضُوا فَإِنَّ اللَّـهَ كَانَ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرًا ﴿١٣٥﴾

"Enyi mlioamini kuweni wenye kusimamisha uadilifu, wenye kushuhudia kwa ajili ya Mwenyezi Mungu japokuwa (ushahidi huo) ni dhidi ya nafsi zenu au wazazi wenu na jamaa zenu, akiwa tajiri au masikini, Mwenyezi Mungu anawastahikia zaidi, basi msifuate matamanio mkaacha kufanya uadilifu, na kama mkipotosha (ushahidi) au mkajitenga, basi Mwenyezi Mungu anajua yale mnayoyatenda." (Qur 'an, 4:135).

11

# WAULIZE WANAOFAHAMU

## KAULI YA AHLUL-DHIKRI KUHUSU BAADHI YAMASAHABA

Imam Ali (a.s) amesema akiwazungumzia Masahaba hawa wanaohesabiwa kuwa ni miongoni mwa (watu) wa mbele:

"**Niliposimamia Ukhalifa, kuna kundi lililotengua (kiapo chake) na kundi jingine lilitoka, na wengine wakafanya ujeuri, kama kwamba wao hawakuyasikia maneno ya Mwenyezi Mungu aliposema, Hayo ni makazi ya akhera tunawapa wale wasiotaka ukubwa katika nchi wala uovu, na marejeo (mema) ni kwa ajili ya wamchao Mwenyezi Mungu. Bila shaka Wallahi Wallahi, waliyasikia maneno hayo na wakayafahamu, lakini dunia imewapendeza machoni mwao na mapambo yake yamewafurahisha**.[1]".

Na amesema tena Imam Ali (a.s) kuwahusu hao Masahaba: "**Wamemfanya shetani kuwa ndiyo msimamizi wa mambo yao, naye amewafanya wao kuwa ni washirika (wake) basi ametaga (mayai) na kuyaangua ndani ya nyoyo zao na anatambaa ndani ya akili zao, basi (shetani) anaona kwa kutumia macho yao na anazungumza kwa kupitia ndimi zao, akawapoteza na kuwapambia maovu yakawa ndiyo matendo ya yeyote aliyeshirikishwa na shetani ndani ya utawala wake na akazungumza batili kwa ulimi wake.**"[2]

Na amesema tena Imam (a.s) juu ya Sahaba mashuhuri Amri ibn Al-'as:

"**Anashangaza mwana wa Nnabighah, hakika amesema (mambo) batili na ametamka uovu, ama (na ifahamike kwamba) kauli mabaya ni kusema uongo, hakika yeye akizungumza husema uongo, na akiahidi huenda kinyume na ahadi, na akiomba (kitu) hulazimisha (apewe) na anapoombwa ni bakhili, ana hiyana kwenye ahadi na anakata udugu.**"[3]

Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema **(s.a.w.w)**:

"**Alama za mnafiki ni tatu: Akizungumza husema uongo, na akiahidi huenda kinyume na ahadi na akiaminiwa hufanya khiyana**."

Ewe msomaji fahamu kwamba: machafu yote haya na zaidi kuliko haya yanapatikana kwa Amru ibn Al-'as.

Na amesema Imam Ali (a.s) akimsifu Abu Dharri Al-Ghifari na wakati huo huo akamshutumu Uthman ibn Affan pamoja na washirika wake ambao walimfukuza Abudharri na kumpeleka mahala paitwapo Ar-rabdhah kisha kutomruhusu kurudi Madina mpaka akafa huko akiwa peke yake.

"**Ewe Abudharri, hakika wewe umechukizwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, basi mtarajie huyo ambaye kwa ajili yake umechukizwa, bila shaka jamaa hawa walikuogopa juu ya dunia yao, nawe uliwachelea kwa ajili ya dini yako, kwa hiyo viache mikononi mwao vitu ambavyo kwavyo walikuogopa na uwakimbie ukiwa na kile ambacho wewe uliwachelea wao kwa ajili yake, hakika wanakitaka mno hicho**

---

1.Nahjul-Balagha uk.90.
2.Nahjul-Balagha uk.96.
3.Nahjul-Balagha uk.200.

**ulichowazuwia, nawe umetosheka mno na hicho waliochokuzuwilia, na hivi karibuni utajua ni nani atakayepata faida kisha (ni nani) mwingi wa husuda, na lau mbingu na ardhi zingekuwa zimeshikana juu ya mja kisha (mja huyu) akamcha Mwenyezi Mungu, basi Mwenyezi Mungu angemjalia mja huyo njia katika mbingu na ardhi. Usiwe na kiliwazo kingine isipokuwa haki, na kisikufanye mpweke chochote isipokuwa batili, basi lau ungeikubali dunia yao wangekupenda na lau ungekata sehemu (katika dunia) wangekupa amani**."[1]

Amesema Imam Ali (a.s) kuhusu Mughirah ibn Al-akhnas ambaye naye ni miongoni mwa Masahaba wakubwa:

"**Ewe mwana wa aliyelaaniwa aliyekatikiwa, na (ewe mwana wa) mti ambao hauna mizizi wala matawi, Wallahi Mwenyezi Mungu hajamtukuza yule ambaye wewe unamtetea, na wala hatosimama yule ambaye wewe unamnyanyua, hebu tuondokee, Mwenyezi Mungu ayaangamize makazi yako, kisha azidishe mashaka yako, kamwe Mwenyezi Mungu asikubakishie muda wa kubakia kwako**."[2] Na amesema Imam (a.s) kuwahusu Tal-ha na Zubair, ambao ni Masahaba mashuhuri waliompiga vita Imam Ali baada ya kuwa wamempa baia na hatimaye wakatengua baia yao:

"Wallahi hawakunikuta na aibu ya aina yoyote ile, na wala hawakufanya uadilifu kati yangu na wao, na kwa hakika wao wanaitetea damu ambayo wao ndiyo walioimwaga...Hapana shaka hilo ndilo kundi lililoasi, ndani yake yumo jamaa (wa karibu yangu (yaani Zubair) na yumo nyoka, madai yao si kweli bali kuna jambo walitakalo, hapana shaka mambo yako wazi na hakika uovu umeondoka toka mahala pake na ulimi wake umekatika kutoka mahala pake pa uchochezi Ni nyie mlionijia mbio mbio kama mwanamke mwenye watoto anavyowakimbilia wanawe na huku mnasema, "Baia Baia" lakini mimi nikakikunja kiganja changu ninyi mkakinyoosha, nikautoa mkono wangu nanyi mkauvuta, Ewe Mwenyezi Mungu hakika wawili hawa wameniasi na wamenidhulumu, wametengua kiapo chao kwangu, wamewavuruga watu dhidi yangu, nakuomba uyafungue waliyoyafunga na wala usiwakubalie waliyoyaamua na uwaoneshe ubaya wa waliyoyategemea na kuyafanya. Niliwataka wajirekebishe kabla ya mapambano, na hapo vitani niliwataka wawe mbali wakanipinga na kuukataa msamaha wangu.

Na amesema Imam Ali (a.s) ndani ya barua aliyowaandikia Zubair na Tal-ha: "**Enyi Masheikh wawili badilisheni maoni yenu (mujisahihishe) kwani sasa hivi jambo kubwa litakalowafika ni aibu kabla ya fedheha na moto havijakutana... Was-salaam.**"[3]

Na amesema kuhusu Marwan ibn Al-hakam wakati alipomteka katika vita ya Jamal kisha akamwachia huru, na huyu Marwan ni miongoni mwa watu waliombai Imam Ali kisha akatengua baia yake: Anasema Imam Ali: "**Sina haja na baia yake, hakika kiganja chake ni kiganja cha Kiyahudi, lau atanibai kwa kiganja chake hatimaye atatengua kimya kimya, ama huyu (Marwan) atamiliki uongozi kama mbwa arambavyo pua yake**

1.Nahjul-Balagha u. 299.
2.Nahjul-Balagha uk. 306.
3. Nahjul-Balagha uk. 626.

**(muda mchache) naye ni baba wa watawala wanne, na kutokana naye na wanawe hao umma (wa Kiislamu) utakumbana na siku nyekundu. matatizo na umwagaji damu.** "

Na amesema Imam [(a.s)] kuhusu Masahaba ambao walitoka pamoja na bibi Aisha kwenda Basrah katika vita ya Jamal na katika hao walikuwemo Talha na Zubair: "**Wakatoka hali ya kuwa wanaikokota heshima ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) kama akokotwavyo mjakazi anaponunuliwa wakaielekeza Basra, wao wakawazuwia wake zao majumbani mwao, na wakamtoa nyumbani kwa ajili yao na wasiokuwa wao mtu ambaye Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) alimzuwia asitoke, wakiwa ndani ya jeshi ambalo hapana mwanaume yeyote aliyekuwa ndani ya jeshi hilo isipokuwa (hapo kabla) alikuwa amenitii na kunipa kiapo cha utii kwa hiyari yake mwenyewe bila kulazimishwa. Wakamshambulia muwakilishi wangu na muweka hazina wa nyumba ya mali ya Waislamu hapo Basra na wengineo miongoni mwa wakazi wa mji huo, wakauwa watu kadhaa hali yakuwa wamefungwa. na wengine wakawauwa baada ya kuwahadaa. Basi Wallahi lau wasingemuuwa miongoni mwa Waislamu isipokuwa mtu mmoja ambaye kumuuwa kwake iwe kuwa ametenda kosa lolote, hakika ingenihalalikia mimi kulipiga jeshi hilo lote, kwani walipomfikia hawakupinga (kuuawa kwake) wala hawakumtetea kwa ulimi wala kwa mkono, achilia mbali ile hali ambayo wao wamewauwa Waislamu kwa kiasi cha idadi ambayo waliyoingia nayo dhidi yao**.[1]

Na amesema Imam [(a.s)] kuhusu bibi Aisha na wafuasi wake miongoni mwa Masahaba katika vita ya Jamal: "**Ninyi mmekuwa askari wa mwanamke na wafuasi wa mnyama, akipiga kelele ninyi mnaitikia na akijeruhiwa mnakimbia, tabia yenu ni mbaya, ahadi yenu ni yenye kuvunjika na dini yenu ni unafiki**."[2]

"**Ama fulani umemtangulia mtazamo wa wanawake wenziwe, anayo chuki inayotokota kifuani mwake mfano wa chungu kinachotokota, lau angeitwa ili atende kwa mwingine kama haya yaliyomleta kwangu asingefanya, na kwangu mimi anayo heshima yake ile ile ya mwanzo (kwa kuwa ni mke wa Mtume) na malipo (yake) yapo kwa Mwenyezi Mungu**." (Nahjul-Balagha uk. 334).

Pia Imam Ali [(a.s)] alisema kuhusu Maquraishi wote, na hapana shaka alikuwa akiwakusudia Masahaba.

"**Ama sisi kuwekwa kando kuhusiana na cheo hiki (cha Ukhalifa) wakati sisi ndio watukufu kwa nasaba na watu wa karibu mno na Mtume kimafungamano, yote hayo ni kwa sababu ya choyo na chuki katika nafsi za watu lakini hukumu ya yote hayo iko kwa Mwenyezi Mungu na marejeo ni kwake siku ya Kiyama Kwa hakika mambo ya dunia hii yananichekesha na kuniliza, hasa kuhusu huyu mwana wa Abu Sufiyan, hapana shaka ametenda mambo yanayoshangaza na kuzidisha mashaka. Jamaa hawa walitaka kuizima nuru ya Mwenyezi Mungu kutoka kwenye taa yake na kuziba mbubujiko toka kwenye asili**

1.Nahjid-Balagha uk.370.
2.Nahjul-Balagha uk.98.

**yake, na wakanichanganyia kinywaji kibaya, iwapo yataondoka matatizo kwetu na kwao nitawapasha ukweli halisi, vinginevyo basi usiwajutie kwani hakuna shaka Mwenyezi Mungu anayajua wayatendayo**."[1] Na alisema katika maana kama hii maneno yafuatayo alipokuwa akimzika bibi Fatma hali yakuwa akimwambia Mtume wa Mwenyezi Mungu. "**Binti yako atakueleza namna Umma wako walivyosaidiana kuubomoa (Ukhalifa), basi muulize akueleze jinsi ya hali (ilivyokuwa) hali hii (imetokea) hata haujapita muda mrefu (toka kufariki kwako) na wala utajo wako haujatoweka..**."[2]

Na amesema Imam Ali [(a.s)] ndani ya barua aliyomuandikia Muawiya:

"**Wewe bila shaka neema zimekupa kiburi na shetani amechukua sehemu ya kwako wewe na amefikia malengo yake kupitia kwako, anazunguka (mwilini mwako) mzunguko wa roho na damu, tangu lini enyi kina Muawiyah, mmekuwa viongozi wa raia na watawala wa mambo ya Umma pasina kuwa kuna unyayo uliotangulia wala heshima tukufu? Tunajilinda kwa Mwenyezi Mungu kutokana na kushikilia mwenendo wa waovu waliotangulia, nakuonya kuwa wewe ni mwenye kuendelea kudanganyika kwa matamanio umekuwa tofauti kati ya nje yako na ndani yako, kwa hakika wewe Muawiyah umeitaka vita, basi hebu waache watu pembeni unitokee mimi, na yaache makundi haya mawili (langu na lako) yasipigane (utoke wewe na mimi) ili apate kutambulikana ni yupi kati yetu aliyemzoefu moyoni mwake na ambaye macho yake yamefumbwa. Basi (fahamu ya kwamba), mimi ndiye baba Hasan, ndiye niliyemuua babu yako, mjomba wako na nduguyo, nikawavunja vunja siku ile ya Badri, na ule upanga (niliowavunjia bado) ninao, na moyo ule ule (wa siku ile) nilipopambana na adui yangu (bado ni ule ule) kamwe sijabadili dini wala sijazusha Mtume mwingine (zaidi ya Muhammad) na ni bila shaka nipo kwenye dini ambayo mliikataa kwa hiyari yenu na mkaingia bila kupenda...**"[3] Imam [(a.s)] anaendelea kusema:

"**Ama kauli yako (kusema) kwamba, sisi ni kizazi cha Abdu Manafi ni kweli, sisi ndio wao, lakini Umayyah halinganishwi na Hashim, na wala Harbu (babu yake Muawiyah) yeye si kama Abdul-Mutalib, na wala Abu-Sufiyan si (sawa kwa ubora) kama Abu Talib, wala Muhajir (aliyetoka Maka mwanzoni anajikusudia yeye mwenyewe Imam a.s) si kama muachwa huru (anamkusudia Muawiyah) wala mwenye nasaba takatifu si kama mwenye nasaba ya kubandikizwa, wala atendaye haki si sawa na mpotoshaji, wala Muumini si sawa na muovu, kwa kweli badali mbaya ni ya yule anayefuata waliomtangulia ambao wameporomokea ndani ya moto wa Jahannam.**

**Mikononi mwetu (tumeshika) utukufu wa Utume ambao kwao tumemuinamisha mwenye nguvu na tukamnyanyua mnyonge, na pale Mwenyezi Mungu alipowaingiza Waarabu ndani ya dini yake kwa wingi, basi Umma huu ulijisalimisha kwa hiyari yake na wengine kwa**

---

1.Nahjul-Balagha uk.348.
2.Nahjul-Balagha uk.460.
3.Nahjul-Balagha uk. 526.

**kulazimika, hivyo ninyi mlikuwa miongoni mwa walioingia katika dini ima kwa matumaini fulani au kwa kuogopa, na (kwa kweli) wamefaulu wale waliotangulia kwa sababu ya kutangulia kwao na Muhajirina wa mwanzo wamejichukulia ubora wao."**[1]

"**Kwa hakika umetuita kwenye usuluhishi wa Qur'ani na wewe si miongoni mwa watu wa Qur'ani, (fahamu kwamba) sisi hatukukuitikia wewe (matakwa yako) lakini tumeiitika Qur'ani katika hukumu yake Wassalaam....**"[2]

"Waambie, ukweli umekwisha fika na bila shaka uongo ni wenye kuondoka." (Qur'ani, 17:81).

---

1.Nahjul-Balagha uk.533.
2.Nahjul-Balagha uk.595.

12

# WAULIZE WANAOFAHAMU

## MLANGO WA TANO

### UNAWAHUSU MAKHALIFA WATATU ABUBAKR, UMAR, NA UTHMAN

Bila shaka Masunni kama tulivyotangulia kueleza, hawakubali kabisa kumkosoa Sahaba yeyote kati ya Masahaba wa Mtume **(s.a.w.w)** na wanaamini kwamba, Masahaba wote ni waadilifu. Na iwapo kuna mwanataaluma yeyote aliye huru ataandika juu ya kukosoa matendo ya baadhi ya Masahaba, basi Masunni humshutumu, si hivyo tu, bali humkufurisha japo mwanataaluma huyo atakuwa ni miongoni mwa wanachuoni wao. Hali hii ndiyo iliyowapata baadhi ya wanachuoni huru wa Kimisri na wasio Wamisri, na mfano wa wanachuoni hao ni Sheikh Mahmud Abur-rayyah mwandishi wa kitabu kiitwacho Adh-wau Alas-sunnatil-Muhammadiyyah na kitabu kingine kiitwacho, Shaykhul-Mudhirah, na mwingine ni Qadhi Shaykh Muhammad Amin Al-antaki mwandishi wa kitabu kiitwacho, Limadha Ikhtartu Madh-haba Ahlil-Bait na mwingine ni Sayyid Muhammad ibn Aqil, ambaye alitunga kitabu kiitwacho, An-nasaihul-hafiyah liman yatawallaa Muawiyah. Bali zaidi ya hapo, baadhi ya waandishi wa Kimisri walifikia kiasi cha kumkufurisha Sheikh Mahmud Shal-tut, ambaye alikuwa ni Sheikh wa Chuo cha Azhar, pale tu alipotoa fat-wa kuruhusu kufanya ibada kwa mujibu wa Madhehebu ya Ja'afariyyah.

Sasa ikiwa Sheikh wa Azhar na Mufti wa miji ya Misri anashutumiwa kwa kiasi tu cha kuyakubali kwake Madhehebu ya Kishia ambayo yananasibishwa kwa mwalimu wa Maimamu wa Kisunni ambaye ni Imam Jaafar As-sadiq, basi unafikiri atakuwa na hali gani mtu aliyeyakinai (akaingia) ndani ya Madhehebu haya baada ya kuchunguza na kutosheka na akayakosoa Madhehebu ambayo hapo kabla yeye alikuweko na aliyarithi kutoka kwa baba zake na babu zake? Basi jambo kama hili ndilo ambalo Masunni hawalipi nafasi kabisa, na wanaamini kabisa kuwa (kumkosoa Sahaba) ni kutoka katika dini na ni kutoka katika Uislamu, na hali hii inaleta maana kwa mujibu wa madai yao kwamba, Uislamu umo ndani ya Madhehebu manne tu na mengine yote ni batili. Bila shaka fikra hizo ni fikra zilizoganda, zinafanana na akili ambazo Qur'an inatusimulia, akili za watu ambao walipinga wito wa Mtume tena kwa nguvu, pale Mtume alipowaita wampwekeshe Mwenyezi Mungu na waache kuabudia miungu mingi mbali mbali. Mwenyezi Mungu anasema:

وَعَجِبُوا أَن جَاءَهُم مُّنذِرٌ مِّنْهُمْ وَقَالَ الْكَافِرُونَ هَٰذَا سَاحِرٌ كَذَّابٌ ﴿٤﴾ أَجَعَلَ الْآلِهَةَ إِلَٰهًا وَاحِدًا إِنَّ هَٰذَا لَشَيْءٌ عُجَابٌ ﴿٥﴾

"Walishangaa alipowafikia muonyaji kutoka miongoni mwao, na makafiri wakasema huyu ni mchawi tena muongo, hivi kweli anawafanya miungu wengi awe Mungu mmoja, bila shaka hili ni jambo la kushangaza." (Qur'ani, 38:4 - 5).

Kutokana na yote hayo, mimi naamini kwamba kuna mashambulizi mabaya ambayo yataelekezwa kwangu kutoka kwa hao wang'ang'anizi (wa fikra za Kisunni) ambao wamejifanya kuwa wao ndiyo wanaowasimamia wenzao, basi ikawa kwamba hana haki yeyote yule kutoka kwenye mambo ambayo yamezoweleka kwao japo mazowea haya kama yatakuwa hayana uhusiano wowote na Uislamu. Sasa kama si hivyo ni vipi mtu anayewakosoa Masahaba katika matendo yao ahukumiwe kuwa ni kafiri na ametoka katika dini, wakati ambapo misingi ya dini na matawi yake havina kabisa uhusiano na suala la kuwakosa Masahaba? Baadhi ya watu wenye chuki za Kimadh-heb walikuwa wanaeneza uvumi katika mawazo yao eti kitabu changu kiitwacho Thummah-Tadaitu kinafanana na kitabu cha Salman Rushdie, ili tu wawazuwie watu kukisoma, bali zaidi ya hayo wakiwahimiza kumlaani mwandishi wake.

Bila shaka huo ni uchafuzi na ni uzushi na uongo mkubwa ambao Mwenyezi Mungu atamuadhibu mtu kwa ajili hiyo, kwani itakuwaje akilinganishe kitabu (changu) Thummah-Tadaitu ambacho kinaligania kwenye kauli ya Isma ya Mtume **(s.a.w.w)** na kumtakasa na kuwafuata Maimamu wa nyumba ya Mtume ambao Mwenyezi Mungu amewaondolea uchafu na amewatakasa mno? Iweje yeye akilinganishe na kitabu cha Aya za Shetani ambacho mwandishi wake mwenye kulaaniwa anaushutumu Uislamu na Mtume wa Uislamu **(s.a.w.w)** ndani ya kitabu hicho, pia anaiona dini ya Kiislamu kuwa ni maneno ya Shetani? Mwenyezi Mungu anasema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُونُوا قَوَّامِينَ بِالْقِسْطِ شُهَدَاءَ لِلَّـهِ وَلَوْ عَلَىٰ أَنفُسِكُمْ ﴿١٣٥﴾

"Ehyi mlioamini kuweni wenye kusimamia' uadjlifu, wenye kushuhudia kwa ajili ya Mwenyezi Mungu japokuwa (ushahidi huo) ni dhidi ya nafsi zenu." (Qur'an, 4:135).

Na kwa ajili ya aya hii tukufu, mimi sijali isipokuwa (nataka) radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu na siogopi lawama ya mwenye kulaumu maadamu ninatetea Uislamu sahihi na ninamtakasa Mtume wake Mtukufu kutokana na kila kosa japokuwa kwa kufanya hivyo italazimu kuwakosoa Masahaba (waitwao kuwa) watukufu na hata kama watakuwa ni wale Makhalifatur-rashiduna kwani Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** ndiye bora mno anayestahiki kutakaswa kuliko kiumbe mwingine yeyote. Msomaji yeyote mwenye akili iliyohuru atafahamu kutoka katika vitabu vyangu viwili nilivyoandika kwamba, lengo lililokusudiwa ni nini, kwani siyo suala la kuwakosoa tu Masahaba, bali ni kwa kiwango cha kumtetea Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** na Isma yake na kuondoa mashaka ambayo (watawala wa) Banu Umayyah na Banu Abbas wameyaambatanisha kwenye Uislamu na kwa Mtume wa Uislamu katika kipindi cha karne za mwanzoni ambazo waliwatawala Waislamu katika kipindi hicho kwa nguvu na wakaigeuza dini ya Mwenyezi Mungu vile ambavyo yalivyowatuma malengo yao mabaya, siasa zao butu na matamanio yao machafu.

Njama zao hizi kubwa kwa kweli zimeiathiri sehemu kubwa ya Waislamu ambao waliwafuata kwa nia njema na wakakipokea kila kile kilichosimuliwa (katika hadithi) miongoni mwa riwaya ambazo ni zenye kubadilisha (ukweli) na zingine za uongo zikawa ndizo za kweli na kwamba huo ndiyo Uislamu na ni wajibu kwa Waislamu kufanya ibada zao kwa

mujibu wa riwaya hizo bila ya kuzihoji. Na lau Waislamu wangetambua ukweli wa mambo ulivyo wasingewathamini kabisa watawala hao na riwaya zao. Kisha lau historia ingetuletea riwaya zisemazo kwamba Masahaba walikuwa wakitekeleza amri za Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** na kuacha makatazo yake" bila ya kumjadili wala kuyapinga maamuzi yake, na kwamba hawakumuasi zama za mwisho wa maisha yake, basi tungewahukumu kuwa ni waadilifu wote na wala tusingefanya uchunguzi juu ya suala hili (la Masahaba) wala tusingesema chochote.

Ama ukweli ulivyo ni kwamba, miongoni mwao (Masahaba) wamo waongo na wanafiki na miongoni mwao wamo mafasiki kwa mujibu wa Qur'ani na Sunna sahihi iliyothibiti. Pia wamo Masahaba waliohitilafiana mbele ya Mtume **(s.a.w.w)** na wakamuasi kuhusu amri (yake) ya kuwaandikia maandiko mpaka wakamtuhumu kwamba anaweweseka, na wakamzuwia kuandika (maandiko hayo). Hawakufuata maamrisho yake pale alipompa uamiri wa jeshi Usamah, na walihitilafiana juu ya suala la Ukhalifa baada yake mpaka wakapuuza kumkosha Mtume na kumuandaa na kumzika, na wakagombana kwa sababu ya Ukhalifa, baadhi yao wakaridhia na wengine wakapinga. (Masahaba) walikhitilafiana katika kila kitu baada ya Mtume **(s.a.w.w)** mpaka wakafikia kukufurishana wao kwa wao na kulaaniana wao kwa wao na kujitenga baadhi yao kuwatenga wengine.

(Na kutokana nao) Dini ya Mwenyezi Mungu ambayo ni moja ikawa na madhehebu mengi na maoni yanayotofautiana, kwa hali hii hapana budi tufanye uchunguzi juu ya kiini (cha yote haya) na migawanyiko ambayo imeuchelewesha umma bora uliotolewa kwa watu na kuuporomosha chini ukawa ni umma dhalili usiojua kitu na unaodharaulika mno duniani. Leo hii unavunjiwa heshima yake na sehemu zake takatifu kukaliwa (kwa mabavu), mataifa yake kufanywa makoloni na wananchi wake kufukuzwa na kutawanywa (huku na huko) kutoka katikati ya nchi zao, na wala umma huu hauwezi kuwazuwia wavamizi hawa wala hata kujitoa aibu usoni pake. Ufumbuzi pekee ninavyoamini mimi kuhusu tatizo hili sugu ni kujikosoa kikweli kweli, tuache kuridhika na kujitapa kwa yale yasemwayo kufanywa na hao waliotutangulia ambao hawakubaliki na wamechakaa, wamekuwa ni makumbusho ambayo yako tupu hayana faida hakuna hata anaye yazuru. Ukweli unatuita tukafanye uchunguzi wa kina juu ya sababu za maradhi yetu, kubakia kwetu nyuma, kufarikiana kwetu na kushindwa kwetu mpaka tuweze kuugundua ugonjwa na kisha tuutafutie dawa itakayotuponyesha kabla ya kutumaliza sisi na kuwapata wenzetu wanaokuja.

Hili ndilo lengo linalokusudiwa, na Mwenyezi Mungu peke yake ndiye mwenye kuabudiwa naye ndiye mwenye kuwaongoa waja wake kwenye njia iliyonyooka maadamu lengo letu ni sahihi. Basi una maana gani upinzani wa wale wanaopinga na wale wenye kung'ang'ania ambao hawafahamu isipokuwa kutukana na kushutumu eti kwa hoja ya kuwatetea Masahaba? Watu hawa sisi hatuwalaumu wala hatuwachukii, bali tunawahurumia kwa hali yao hiyo, kwani wao masikini kilichowazuwia (kufahamu) ni dhana zao njema kwa Masahaba. Dhana hiyo imewazuwia wasiweze kuufikia ukweli, wamefanana mno na watoto wa Mayahudi na Wakristo ambao wamefanya dhana njema kwa baba zao na babu zao, na hawakuzilazimisha nafsi zao kufanya juhudi ya kuchunguza ukweli wa

Uislamu, wamebakia wanaamini tu yasemwayo na viongozi wao waliotangulia kwamba Muhammad ni muongo na wala siyo Nabii. Mwenyezi Mungu anasema:

وَمَا تَفَرَّقَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ إِلَّا مِن بَعْدِ مَا جَاءَتْهُمُ الْبَيِّنَةُ ﴿٤﴾

"Na hawakufarakana wale waliopewa kitabu ila baada ya kuwafikia ukweli" (Qur'an 98:3).

Baada ya kupita karne nyingi imekuwa ni vigumu leo hii kwa Muislamu kumtosheleza Myahudi au Mkristo juu ya itikadi ya Kiislamu, basi unafikiriaje juu ya mtu atakayewaambia kwamba Taurati na Injili ambazo wanapokezana (ni vitabu) vilivyobadilishwa na kisha akawatolea juu ya hilo ushahidi wa Qur'an, basi je, Muislamu huyu atampata mwenye kumsikiliza kutoka kwao? Hali ni hiyo hiyo kwa Muislamu wa kawaida ambaye anaamini kuwa Masahaba wote ni waadilifu na akaing'ang'ania fikra hiyo bila ya dalili yoyote, basi je itawezekana kwa mtu yeyote kumkinaisha kinyume cha hivyo? Ikiwa watu hawa (Masunni) hawawezi hata kumkosoa Muawiyah na mwanawe Yazid na wengine wengi kama hawa ambao wameuharibu Uislamu kwa matendo yao machafu, basi utakuwa na hali gani iwapo utakapowasemesha kuhusu Abubakar, Umar na Uthman ambao ni As-sidiq na Al-faruq na yule aliyestahiwa na Malaika, au (ukawasemesha) kuhusu Aisha Ummul-Muuminina mke wa Mtume **(s.a.w.w)** na ni binti ya Abubakar, (Aisha) ambaye tumemzungumzia katika mlango uliopita kwa mujibu wa mapokezi yaliyopokelewa juu yake na waandishi wa sihahi zinazotegemewa kwa Masunni? Na sasa imefika zamu ya kuwazungumzia Makhalifa watatu ili tupate kuonesha baadhi ya matendo yao ambayo yamesajiliwa na Sihahi za Kisunni na Musnad zao na vitabu vya historia vinavyotegemeka kwao, kwanza tubainishe kwamba usemi wa kuwa Masahaba wote ni waadilifu siyo sahihi, na kwamba uadilifu haupatikani hata kwa Masahaba (wanaozingatiwa kuwa ni) wema.

Hatimaye tutawaonesha ndugu zetu Masunni kwamba kukosoa (tunakokusudia) siyo kwa kutukana na kushutumu, bali (makusudio) ni kiasi cha kuweza kuondoa pazia ili kuufikia ukweli kama ambavyo (maelezo hayo ya kukosoa) siyo miongoni mwa uzushi na uongo wa wapinzani (wa dini) kama wanavyodai watu wengi bali yote ni kutoka ndani ya vitabu ambavyo (wao Masunni) wamevihukumu kuwa ndiyo vitabu sahihi na wakashikamana navyo. Abubakr Sidiq katika zama za uhai wa Mtume **(s.a.w.w)** Bukhari amethibitisha ndani ya sahihi yake juzuu ya sita ukurasa arobaini na sita Kitabu Tafsir Surah Al-Hujurat amesema: "Ametusimulia Nafii ibn Umar, naye amepokea kwa Ibn Abi Mulaikah amesema: Ilikuwa karibu watukufu wawili waangamie, Abubakar na Umar (r.a), walipaza sauti zao mbele ya Mtume **(s.a.w.w)** pale ulipokuja msafara wa Bani Tamim, mmoja wao alimuashiria Aqraa ibn Habis ndugu wa Bani Mujashi'i, na mwingine akamuashiria mtu mwingine, Nafii akasema, jina lake silikumbuki, basi Abubakar akasema kumwambia Umar hakuna ulichokusudia ila kunipinga, Umar akasema sikukusudia kukupinga, basi sauti zao zikapaa katika majibizano hayo, Mwenyezi Mungu akateremsha aya isemayo, Enyi mlioamini msipaze sauti zenu, Ibn Zubair amesema basi Umar alikuwa hamsikilizishi Mtume **(s.a.w.w)** baada ya kushuka aya hii

mpaka Mtume amuulize na hilo hakulieleza toka kwa baba yake yaani Abubakar."

Kama ambavyo Bukhari ameandika ndani ya sahihi yake juzuu ya nane ukurasa wa 145 Kitabul-I'tisami Bil-kitabu Was-sunnah Babu Mayukrahu minat-ta'amuq Wat-tanazu'u amesema: "Ametueleza Waqi'i kutoka kwa Nafii ibn Umar kutoka kwa Abu Mulaikah amesema: Ilikuwa karibu watukufu wawili waangamie (yaani) Abubakar na Umar pale ujumbe wa Bani Tamim ulipofika kwa Mtume **(s.a.w.w)**, mmoja wao akamuashiria Aqraa ibn Habis At-tamimi Al-handhali ndugu wa Bani Mujashi'i, na mwingine akamuashiria mwingine, basi Abubakar akasema kumwambia Umar, bila shaka umekusudia kunipinga, Umar akasema, Sikukusudia kukupinga, basi sauti zao zikapaa mbele ya Mtume **(s.a.w.w)**, ikashuka aya isemayo: Enyi mlioamini musipaze sauti zenu zaidi ya sauti ya Mtume na wala msiseme naye kwa sauti ya nguvu kama mnavyosemezana ninyi kwa ninyi visije kuporomoka vitendo vyenu na hali ninyi hamjui, kwa hakika wale wanaoangusha sauti zao mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, hao ndiyo Mwenyezi Mungu amezisafisha nyoyo zao kwa kumcha Mungu, basi wanayo maghfira na ujira mkubwa."

Ibn Abi Mulaikah amesema, "Zubair amesema: Basi Umar baada ya hapo na hakumueleza hilo baba yake yaani Abubakar, akawa akizungumza na Mtume **(s.a.w.w)** humzungumza kama ndugu ampaye siri hakumsikilizisha jambo Mtume mpaka amuulize. Kama ambavyo Bukhari amethibitisha ndani ya sahihi yake juzuu ya tano ukurasa 116 Kitabul-maghazi Wafdu Bani Tamim amesema: "Ametusimulia Hisham ibn Yusuf kwamba Ibn Juraij aliwasimulia kutoka kwa Ibn Abi Mulaikah kwamba, Abdallah ibn Zubair aliwaeleza kuwa ulifika kwa Mtume **(s.a.w.w)**, ujumbe kutoka kwa Bani Tamim, Abubakar akasema, Mpe Uamiri Al-Qa'aqa'a ibn Ma'abad ibn Zurarah, Umar akasema Hapana, mpe uamiri Aqra'a ibn Habis, Abubakar akasema huna nia nyingine ila kunipinga. Umar akasema; sikukusudia kukupinga, wakajibizana mpaka sauti zao zikapaa juu ikashuka aya kuhusu tukio hilo isemayo: Enyi mlioamini, msitangulize kusema lenu mbele ya (neno la) Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Mpaka mwisho wa aya.

Kinachoonekana wazi hapa kupitia riwaya hii ni kwamba Abubakar na Umar hawakufanya heshima mbele ya Mtume **(s.a.w.w)** kwa mujibu wa adabu za Kiislamu, na walijitanguliza mbele ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake bila idhini, wala Mtume hakuwaomba watoe maoni yao kuhusu kumpa uamiri mtu yeyote miongoni mwa Bani Tamim, kisha wasitosheke na hali hiyo mpaka wakazozana mbele ya Mtume na zikapaa sauti zao mbele yake bila ya heshima wala kujali mambo yanayowalazimu katika (kuonesha) tabia na adabu (njema) ambazo haiwezekani kwa yeyote miongoni kwa Masahaba kukosa kuzifahamu au kujifanya hazifahamu baada ya Mtume kumaliza muda wa uhai wake akiwalea na kuwafundisha. Lau tukio hili lingekuwa limetokea mwanzoni mwa kuja kwa Uislamu tungewatakia samahani Masheikh hawa wawili juu ya tendo lao hilo, na tungejaribu kupata baadhi ya tafsiri. Lakini riwaya hizi zinathibitisha mambo ambayo hayatoi nafasi ya kuwa na mashaka kwamba tukio hili lilitokea mwishoni mwa uhai wa Mtume **(s.a.w.w)**, kwani ujumbe wa Bani Tamim ulifika kwa Mtume **(s.a.w.w)** mwaka wa tisa wa Hijra, na baada ya

hapo Mtume hakuishi isipokuwa miezi michache, kama ambavyo wanashuhudia pia wanahistoria na wanachuoni wa hadithi ambao wameeleza juu ya kufika kwa ujumbe huo kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu. Isitoshe hili ni tukio ambalo Qur'ani imelizungumza ndani ya sura za mwisho pale inaposema: "Utakapokuja msaada wa Mwenyezi Mungu na ushindi, utawaona watu wanaingia katika dini ya Mwenyezi Mungu kwa wingi."

Ikiwa mambo yako namna hii, ni vipi wenye kutoa udhuru wanatoa udhuru kuhusu msimamo wa Abubakar na Umar (namna ulivyokuwa) mbele ya Mtume **(s.a.w.w)**, na lau riwaya ingeishia kueleza msimamo waliouonesha Masahaba hawa wawili, basi tusingepata nafasi ya kukosoa, lakini Mwenyezi Mungu ambaye hastahi chochote katika haki amelisajili tukio hilo na akateremsha Qur'ani kuhusiana nalo itakayokuwa ikisomwa, na ndani yake yamo maonyo na makemeo kwa Abubakar na Umar kwamba, matendo yao yataporomoka iwapo watarudia tendo kama hilo, kiasi kwamba mpokezi wa riwaya ya tukio hili ameanza maneno yake kwa kusema: "Karibu watukufu wawili waangamie, (akimaanisha) Abubakar na Umar."

Mpokezi wa riwaya inayohusu tukio hili ambaye ni Abdallah ibn Zubair anajaribu kutukinaisha kwamba Umar baada ya kushuka aya hii kuhusu tendo lake kwamba yeye Umar anapomzungumza na Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** akawa hamsikilizishi sauti yake mpaka Mtume humuuliza pamoja na kwamba hakumwambia babu yake Abubakar. Lakini historia na matukio ambayo wameyataja wana hadithi yanathibitisha kinyume cha hivyo, na inatosha ukumbuke ile siku ya alhamisi kabla ya kufariki Mtume **(s.a.w.w)** kwa siku tatu, tunamkuta Umar mwenyewe alitamka ile kauli yake mbaya akasema: "Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu anaweweseka, kinatutosha kitabu cha Mwenyezi Mungu." Kwa sababu yake watu wakahitilafiana, wapo wanaosema sogeeni kwa Mtume akuandikieni, na wengine wanasema kama alivyosema Umar, basi walipozidisha vurugu na kukhitilafiana, Mtume wa Mwenyezi Mungu akawaambia, Ondokeni haifai kufanya makelele mbele yangu." Maana ya wingi wa fujo, makele, kuhitilafiana na kugombana inajulisha kwamba, wao walivuka kila mipaka ambayo Mwenyezi Mungu aliwawekea katika suratul-huj-rati kama ilivyotangulia.

Haiwezekani kututosheleza kwamba, kutofautiana kwao na vurugu zao eti zilikuwa kwa kunong'ona kwenye masikio, bali inafahamika kutokana na yote hayo kwamba wao walipaza sauti zao mpaka hata wanawake ambao walikuwa nyuma ya pazia na hijabu walishiriki katika fujo na wakasema: "Sogeeni kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** akuandikieni maandiko." Umar akawambia: "Ninyi ndiyo kama wale wanawake waliomfanyia vitimbi Yusuf, anapokuwa (Mtume) mgonjwa mnalia na akipona mnamfanyia vitimbi."

Mtume akasema kumwambia Umar, "Waacheni, kwani wao ni bora kuliko ninyi." Na tunachokifahamu katika yote haya ni kwamba, wao hawakufuata maamrisho ya Mwenyezi Mungu katika kauli yake aliposema: "Enyi mlioamini msitangulize (kusema lenu) mbele ya (neno la) Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na wala msipaze sauti zenu zaidi ya sauti ya

Mtume." Hawakukiheshimu cheo cha Mtume na wala hawakufanya adabu pale walipomtuhumu kuwa anaweweseka. Hapo kabla Abubakr alikwisha kutamka maneno machafu mbele ya Mtume **(s.a.w.w)** pale alipomwambia Ur-wah ibn Mas-oud, "Amsas bibidhril-laab." Na Al-QastaJani ambaye ndiye aliyeisherehesha sahihi Bukhari amesema katika kuifafanua ibara hii kwamba, suala la kufyonza Bidhri ni miongoni mwa matusi makubwa mno kwa Waarabu.

Sasa basi, ikiwa maneno kama haya yanatamkwa mbele ya Mtume **(s.a.w.w)** basi nini maana ya kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu aliposema: "Na wala msiseme naye kwa sauti ya nguvu kama mnavyosemezana ninyi kwa ninyi.?" Na ikiwa Mtume wa Mwenyezi Mungu ana tabia njema ya hali ya juu kama alivyomsifu Mola wake, na itakapokuwa Mtume ni mwingi wa haya kuliko mwali aliye ndani kama walivyoyathibitisha haya Bukhari na Muslim. Masheikh hawa wawili Bukhari na Muslim wamebainisha wazi kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** hakuwa muovu wala mwenye kueneza maovu na alikuwa akisema: "Hakika mbora wenu ni mzuri wenu kwa tabia." Basi imekuwaje Masahaba wake hao waliokuwa karibu yake mno hawakuathirika kwa tabia hii tukufu? Zaidi ya yote haya ni kwamba, Abubakr hakutekeleza amri ya Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** pale Mtume alipompa uamiri Usamah bin Zaid na Abubakr akawa miongoni mwa askari walio chini ya uamiri wa Usamah (lakini Abubakar hakutii amri hiyo) na Mtume **(s.a.w.w)** aliwakemea mno wale waliobakia nyuma (wasiende pamoja na Usamah katika jeshi hilo) mpaka akasema: "Mwenyezi Mungu amlaani yeyote atakayebaki nyuma asitoke na jeshi la Usamah." Haya aliyasema baada ya kumfikia habari yeye Mtume juu ya upinzani wa wapinzani dhidi yake kutokana na kumpa uamiri Usamah ibn Zaid, jambo ambalo wanahistoria wengi wamelitaja.

Hali ni kama hiyo kwamba, Abubakr alikimbilia Saqifah na akashiriki kumtenga Ali ibn Abi Talib kutoka kwenye Ukhalifa, na (yeye Abubakar alipokuwa akikimbilia Saqifah) aliuacha mwili wa Mtume na wala hakuona umuhimu wa kumkosha na kumvisha sanda na kufanya maandalizi (yanayohusika) na hatimaye kumzika, bali aliyaacha yote hayo kwa kugombea cheo cha Ukhalifa na uongozi ambao ndiyo iliyokuwa hamu yake. Kama ni hivyo uko wapi huo usahaba na urafiki unao daiwa (kuwa alikuwa nao Abubakar kwa Mtume)?

Na je, iko wapi tabia njema (anayostahiki kuwa nayo)? Mimi unanishangaza sana msimamo wa Masahaba hawa kuhusu Mtume wao ambaye alimaliza muda wa uhai wake akiwaongoza na kuwalea (malezi bora), na kuwapa nasaha mbali mbali Mtume ambaye "Yanamuhuzunisha yanayokutaabisheni, anakuhangaikieni na ni mpole na mwenye huruma kwa walioamini." Matokeo yake walimuacha juu ya kitanda cha mauti na wao wakakimbilia Saqifah ili kumchagua mmoja wao awe Khalifa wao. Na sisi leo hii tunaishi katika karne ya ishirini, karne ambayo tunaisema kuwa ni karne mbaya, na kwamba eti tabia za watu zimeharibika na miongozo nayo imetelekezwa. Lakini pamoja na hayo hapana shaka Waislamu (wa leo hii) anapokufa jirani yao hufanya haraka kumshughulikia mpaka wanamsitiri

kaburini mwake hali ya kuwa wakitekeleza kauli ya Mtume **(s.a.w.w)** aliposema: "Kumkirimu maiti ni kumzika."

Bila shaka Amirul-Muuminina Ali ibn Abi Talib aliyaumbua matukio hayo waliyoyatenda pale aliposema: "Amraa Wallahi, hakika mwana wa Abu Qahafah (Abubakr) aliuvaa (aliutwaa) Ukhalifa hali ya kuwa anafahamu kwamba nafasi yangu juu Ukhalifa ni sawa na mkono (mshikio) ulioko kwenye jiwe la kusagia." Kisha baada ya hapo, Abubakr aliruhusu nyumba ya bibi Fatmah ihujumiwe na kutishiwa kuchomwa moto ikiwa hawakutoka humo kwenda kumbai Abubakr wale wote waliopinga (Ukhalifa wake) na yalitokea yaliyotokea miongoni mwa mambo ambayo wanahistoria wameyataja ndani ya vitabu vyao na wapokezi nao wakayanakili zama hadi zama nyingine. Nasi tutakubainishia ewe msomaji sehemu tu ya hayo, na ni juu ya mwenye kutaka ziyada kuvisoma vitabu vya historia.

13

# WAULIZE WANAOFAHAMU

## ABUBAKR BAADA YA UHAI WA MTUME (s.a.w.w)

### NAMNA ALIVYOMPINGA BIBI FATMAH, KWA KUMNYANG'ANYA HAKI YAKE

Bukhari amethibitisha ndani ya sahih yake juzuu ya tano ukurasa 82 Kitabul-Maghazi Babu Ghaz-watukhaibar amesema: "Imepokewa kutoka kwa Ur-wah naye kutoka kwa Aisha kwamba Fatmah (a.s) binti ya Mtume **(s.a.w.w)** alituma ujumbe kwa Abubakr akimuomba ampe mirathi yake kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** miongoni mwa mali ambazo Mwenyezi Mungu alimpa Mtume hapo Madina na Fadak na sehemu iliyobaki katika khumsi ya Khaibar. **Abubakar akasema: Bila shaka Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: Sisi (Mitume) haturithiwi tunachokiacha ni sadaka, hakika watakula kizazi cha Muhammad katika mali hii, na kwa hakika Wallahi sibadilishi chochote katika sadaka ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) kutoka katika hali iliyokuwa nayo katika zama za Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w) na nitaitumia kama alivyoitumia Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w)**. Basi Abubakar akakataa kumpa chochote bibi Fatmah (a.s) na ndipo bibi Fatimah alipomkasirikia Abubakar kuhusu jambo hilo na hakumsemesha mpaka alipofariki, na aliishi miezi sita tu baada ya kufariki Mtume **(s.a.w.w)**."

Bibi Fatmah alipofariki, mumewe (ambaye ni Sayyidna Ali ibn Abi Talib) alimsalia na akamzika usiku wala hakumruhusu Abubakr kuhudhuria maziko hayo. Katika uhai wa bibi Fatmah (a.s) Imam Ali (a.s) alikuwa akithaminiwa mno na watu, lakini alipofariki watu wakampuuza Imam Ali, ndipo alipotaka mapatano na Abubakar na akambai, na kabla ya miezi hiyo sita alikuwa hakumbai.

Naye Muslim ameandika ndani ya sahihi yake, juzuu ya pili Kitabul-jihad mlango unaohusu kauli ya Mtume, "La Nuurathu Mataraknahu Sadaqah" Imepokewa toka kwa Ummul-Muuminina Aisha (r.a) kwamba, baada ya kufa Mtume bibi Fatmah (a.s) binti ya Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** alimuomba Abubakr, mirathi yake katika alivyoviacha Mtume **(s.a.w.w)** na mali aliyompa Mwenyezi Mungu, basi Abubakar akasema: "**Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema, Haturithiwi tulichokiacha ni Sadaka**." Basi Fatmah binti ya Mtume wa Mwenyezi Mungu akakasirika na akakata mawasiliano na Abubakar na alibakia hivyo mpaka akafariki. Na aliishi miezi sita tu baada ya Mtume **(s.a.w.w)**, Aisha amesema: "**Fatmah alikuwa akimuomba Abubakr ampe sehemu yake iliyoachwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu katika Khaibar na Fadak na sadaka yake iliyoko Madina, basi Abubakar alimkatalia Fatmah na kusema, Siwezi kuacha chochote ambacho Mtume alikifanya ila nami nitakifanya, kwani mimi nachelea ikiwa nitaacha kitu katika mambo yake nitapotea**."

Ama sadaka ya Mtume **(s.a.w.w)** ya pale Madina, Umar aliitoa kwa Ali na Abbas, na ile ya Khaibar na Fadak, Umar alizizuwiya na akasema: "**Hizo**

**ni sadaka za Mtume wa Mwenyezi Mungu, zilikuwa ni haki yake ambayo inamuhusu yeye na mambo yake, usimamizi wake uko chini ya yeyote atakayetawala, basi zimebakia hivyo hadi leo**."

Pamoja na kuwa Masheikh hao wawili (Bukhari na Muslim) kuikata riwaya hii na kuifupisha ili ukweli usije ukaonekana kwa wale wanaotafiti, lengo lao wamekusudia kulinda heshima ya Makhalifa hawa watatu, na tabia hii (ya kuficha mambo) ni fani yao inayofahamika. Kuhusu (tabia hii ya) Bukhari na Muslim ndani ya maudhui hii, hivi punde Mwenyezi Mungu apendapo tutaifanyia uchambuzi na tutakutosheleza.

Jambo la kuzingatia ni kwamba, riwaya hizi ambazo wao wamezifanyia marekebisho, zinatosha sana kueleza mazingira halisi ya Abubakr ambaye alikanusha madai ya bibi Fatmah, jambo ambalo lilimfanya bibi Fatmah amkasirikie na kumsusa mpaka alipofariki, na mumewe akamzika usiku tena kwa siri kutokana na usia wa bibi Fatmah mwenyewe bila kumruhusu Abubakar (kuhudhuria mazishi hayo). Kama ambavyo tunafaidika kutokana na riwaya hizi kwamba Ali hakumpa baia Abubakar muda wote wa miezi sita ya uhai wa bibi Fatmah baada ya kufariki baba yake, na kwamba Ali (a.s) alilazimika kumbai Abubakar pale alipoona watu wamempuuza, basi akataka mapatano na Abubakar.

Na kitu walichokibadilisha Bukhari na Muslim miongoni mwa ukweli ni kuwa madai ya bibi Fatimah (a.s) kwamba baba yake ambaye ndiye Mtume wa Mwenyezi Mungu alimpa Fadak katika zama za uhai wake na hiyo siyo katika mirathi, na tujaalie kwamba Mitume hawarithiwi kama alivyoyaeleza hayo Abubakr kutoka kwa Mtume **(s.a.w.w)**, na bibi Fatmah akayapinga maelezo hayo na akayalinganisha maelezo ya Abubakr kwenye Qur'ani ambayo inasema kuwa "Na Sulaiman akamrithi Daud." Basi Fadak haingii katika hadithi hii inayodaiwa, kwani Fadak ni zawadi siyo miongoni mwa mirathi kwa namna yoyote ile. Kwa ajili hiyo basi utawakuta wanahistoria wote, wafasiri na watu wa hadithi wanaeleza kwamba bibi Fatmah alidai kwamba Fadak ni mali yake, na Abubakr akamkanusha na kumtaka alete ushahidi juu ya madai yake, basi akamleta Ali ibn Abi Talib na Ummu Aiman, Abubakr hakuukubali ushahidi wa hawa na akauona kuwa hautoshelezi.

Maelezo kama haya ameyakubali Ibn Hajar ndani ya As-Sawaiqul-Muhriqa pale alipoeleza kwamba bibi Fatimah alidai kwamba, Mtume **(s.a.w.w)** alimzawadia Fadak, na hakuleta shahidi juu ya hilo isipokuwa Ali ibn Abi Talib na Ummu Aiman kwa hiyo kiwango cha ushahidi wake hakikukamilika.

Na kama alivyosema Al-Imam Fakhrur-razi ndani ya tafsiri yake kuwa, Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** alipofariki bibi Fatmah (a.s) alidai kwamba Mtume alimzawadia Fadak, basi Abubakr akamwambia Fatmah, "Wewe ni mtu muhimu mno kwangu na ni mwenye kupendelewa mno kwangu mimi kuliko wengine, lakini mimi sielewi usahihi wa kauli yako kwa hiyo siwezi kukupa." Anasema. (Bibi Fatmah) akamshuhudisha Ummu Aiman huru wa Mtume wa Mwenyezi Mungu, lakini Abubakar akamtaka bibi Fatmah alete shahidi ambaye ushahidi wake utakubalika katika sheria, ikawa hakupatikana. Madai ya Fatimah (a.s) kwamba Fadak ni zawadi aliyopewa na Mtume **(s.a.w.w)** na kwamba Abubakar aliyapinga madai

hayo na hakuukubali ushahidi wa Ali na Ummu Aiman, ni jambo linalofahamika kwa wanahistoria na Ibn Taimiyyah amelieleza, na mwandishi wa Siiratul-halabiyyah, na Ibnul-Qayyim Al-jauziyyah na wengineo.

Lakini Bukhari na Muslim wamelifupisha tukio hili na hawakutaja isipokuwa ombi la bibi Fatimah juu ya mirathi peke yake, ili tu wamfikirishe msomaji kwamba bibi Fatmah alimkasirikia Abubakr mahala ambapo hapakustahiki kwani Abubakr hakufanya ila kile alichokisikia kwa Mtume **(s.a.w.w)**, kwa hiyo bibi Fatimah alifanya dhuluma na Abubakr alidhulumiwa. Bukhari na Muslim waliyafanya vote haya ili kulinda heshima ya Abubakr bila kutilia maanani uaminifu katika kunakili wala ukweli wa hadithi ambazo zilikuwa zinaumbua aibu za Makhalifa na kuondoa uzushi na vizuwizi vilivyowekwa na Banu Ummayyah na wasaidizi wa Makhalifa, hilo hawakujali japokuwa litakuwa linaharibu heshima ya Mtume mwenyewe **(s.a.w.w)** au binti yake Fatmah (a.s) (bora tu Makhalifa wao wasalimike).

Ni kwa ajili hiyo tu ndiyo maana Bukhari na Muslim wamemiliki uongozi wa wanachuoni wa hadithi kwa Masunni na hao Masunni wakavizingatia vitabu vyao (Bukhari na Muslim) kuwa ndiyo vitabu sahih mno baada ya kitabu cha Mwenyezi Mungu. Huu ni uzushi usiokuwa na dalili ya kielimu na tutauchambua katika mlango maalum mpaka tuudhihirishe ukweli kwa mwenye kuutaka apendapo Mwenyezi Mungu. Pamoja na hayo sisi tunawahoji Bukhari na Muslim ambao wamezithibitisha fadhila nyingi za Fatmah (a.s) kwa mukhtasari, lakini unatosheleza kumkosoa Abubakar ambaye alimfahamu bibi Fatimah na daraja yake mbele ya Mtume **(s.a.w.w)** zaidi kuliko walivyomfahamu kina Bukhari na Muslim. Pamoja na hayo Abubakr alimkanusha bibi Fatmah na wala hakukubali ushahidi wake wala ushahidi wa mumewe ambaye Mtume amesema kumuhusu kwamba "Ali yu pamoja na haki, na haki iko pamoja na Ali, haki inazunguka popote azungukiapo. Na hebu tutosheke na ushahidi wa Bukhari na ushahidi wa Muslim kuhusu yale aliyoyathibitisha mwenyewe Mtume **(s.a.w.w)** juu ya ubora wa binti yake bibi Fatimah.

Fatmah ni Maa'sum kwa mujibu wa maandiko ya Qur'an Muslim amethibitisha ndani ya sahihi yake juzuu ya saba, mlango wa Fadhail za Ahlul-Bait. Aisha (r.a) amesema: "Mtume **(s.a.w.w)** alitoka asubuhi mapema akiwa amejitanda guo la sufi nyeusi, basi akaja Hasan ibn Ali akamuingiza humo, kisha akaja Husein ibn Ali naye akamuingiza pamoja naye, kisha alikuja Fatmah akamuingiza na hatimaye akaja Ali naye akamuingiza kisha akasema: "Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu enyi watu wa nyumba (ya Mtume) na kukutakaseni mno." Sasa basi, ikiwa Fatmah (a.s) ni mwanamke pekee ambaye Mwenyezi Mungu amemuondolea uchafu na kumtakasa kwa kumuepusha na kila aina ya dhambi na maasi katika umma huu basi inakuwaje Abubakar anamkanusha na kumtaka ushahidi, ewe bwana unayaona hayo? Fatmah ndiye mwanamke bora miongoni mwa wanawake waumini, na ndiye mwanamke bora katika umma huu.

Bukhari amethibitisha ndani ya sahih yake juzuu ya saba katika Kitabul-isti-idhan ndani ya mlango wa Man Najaa Baina yadain-nas walam Yukhbir

Bisirri Sahibih Faidha Maata Akhbara Bih, na Muslim katika Kitabul-Fadhail, Imepokewa kutoka kwa Ummul-Muuminina Aisha amesema: "Sisi wakeze Mtume **(s.a.w.w)** wote tulikuwa mbele ya Mtume **(s.a.w.w)** hapana aliyekosekana miongoni mwetu, basi Fatmah (a.s) akaja akitembea, Wallahi hapakufichikana chochote katika mwendo wake kutokana na mwendo wa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**, basi Mtume alipomuona Fatmah akasema, karibu binti yangu, kisha akamkalisha kuliani kwake au kushotoni kwake, halafu akamnong'oneza, Fatmah akalia sana. Mtume alipoiona huzuni yake akamnong'oneza kwa mara ya pili, mara Fatmah akacheka, mimi nikamwambia, Mimi ni miongoni mwa wakeze (Mtume) lakini Mtume wa Mwenyezi Mungu amekuhusisha wewe kwa jambo la siri kati yetu kisha wewe unalia.

Mtume wa Mwenyezi Mungu aliposimama nikamuuliza Fatmah, Ni jambo gani alikunong'oneza? Akasema: Siwezi kutoa siri ya Mtume wa Mwenyezi Mungu. Mtume alipofariki nikamwambia Fatmah, Nimekukusudia wewe kwa jambo ambalo nina haki nalo juu yako hujanieleza bado. Bibi Fatmah akasema, Amma sasa ni sawa kukueleza. Akanieleza akasema, Wakati aliponinong'oneza katika jambo la kwanza alinieleza kuwa, Jibril alikuwa akija kumuaridhia Qur'an kila mwaka mara moja na kwamba mwaka huu ameniaridhia mara mbili, na wala sioni isipokuwa muda umekaribia, basi mche Mungu na uwe mvumilivu, kwani mimi ndiye mtangulizi bora kwako wewe, ndipo nilipolia kilio changu ulichokiona, na alipoiona huzuni yangu akaninong'oneza mara ya pili akasema: Ewe Fatmah huridhii kuwa wewe ndiwe mwanamke bora miongoni mwa waumini au mwanamke bora wa umma huu?"

Ikiwa Fatmah (a.s) ndiye mwanamke bora kuliko wanawake wa waumini kama yalivyothibiti hayo kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, na Abubakar anamkatalia Fatmah madai yake ya Fadak na wala hakukubali ushahidi wake, je ni ushahidi gani mwingine utakaokubalika baada yake unaoudhania ewe bwana? Fatmah ndiye mbora wa wanawake wa peponi. Bukhari amethibitisha ndani ya sahihi yake katika juzuu ya nne ndani ya Kitabu bad-il-khalq; Babu Manaqib Qarabatu Rasulillahi, Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** "Fatmah ni mbora wa wanawake wa peponi." Basi kama Fatmah ni mwanamke bora kuliko wanawake wote wa peponi, na maana yake ni kwamba yeye ni mwanamke bora ulimwenguni kwani watu wa peponi siyo ummati wa Muhammad peke yao kama inavyofahamika, sasa vipi Abubakr anamkanusha? Je, hawakudai kwamba laqab ya As-sidiq (ya Abubakr) aliipata kwa kuwa yeye alikuwa akisadikisha kila alilokuwa akilisema sahibu yake ambaye ni Mtume Muhammad, sasa ilikuwaje hakumsadiki Mtume **(s.a.w.w)** juu ya mambo aliyoyasema kuhusu bibi Fatmah?

Fatmah ni sehemuya mwili wa Mtume **(s.a.w.w)**, na Mtume hukasirika iwapo Fatmah atakasirika. Bukhari amethibitisha ndani ya sahih yake, juzuu ya nne Kitabu Bad-ilkhalq Babu Manaqib Fatmah (a.s) Bintun-nabiyyi **(s.a.w.w)** amesema: "Ametusimulia Abul-walid, ametusimulia Ibn Uyanah kutoka kwa Amr ibn Dinar kutoka kwa Abi Mulaikha, kutoka kwa Al-Musawar ibn Mukhrimah, kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: Fatmah ni sehemu itokanayo nami, yeyote mwenye kumkasirisha

basi kanikasirisha mimi." "Fatmah ni sehemu itokanayo nami kinanikera kinachomkera na kinaniudhi kinachomuudhi."

Ikiwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** anakasirika kwa kukasirika Fatmah na anaudhika kwa kuudhika kwake, basi maana ya maneno hayo ni kuwa yeye Fatmah ni ma'asum hatendi makosa, vinginevyo isingefaa kwa Mtume kusema namna hiyo, kwani mtu atendaye maasi uwezekano wa kumbughudhi na kumkera upo hata kama ana cheo kikubwa namna gani. kwani sheria ya Kiislamu haiangalii aliyekaribu au yule wa mbali, awe ni mwenye heshima (kubwa namna gani) au mnyonge, tajiri au masikini. Na iwapo mambo yatakuwa namna hiyo, iweje basi Abubakr asijali kukasirika kwa Fatmah mpaka akafa hali ya kuwa kamkasirikia, bali alimsusia kabisa na hakumsemesha mpaka alipofariki huku akimuombea dua (ya maangamizo) katika kila sala yake (aliyosali), kama yalivyo maelezo hayo ndani ya kitabu cha historia cha Ibn Qutaibah na wengineo mioneoni mwa wanahistoria.

Naam, hakika mambo haya ni ukweli wenye uchungu na ni ukweli unaouma ambao unatikisa nguzo na kutikisa imani, kwani mchunguzi muadilifu mwenye kujitenga kwa ajili ya kutafuta haki na ukweli hana njia isipokuwa kukubali kwamba, Abubakar alimdhulumu bibi Fatmah na akampokonya haki yake. Jambo hili lilikuwa ndani ya uwezo wake (Abubakr) akiwa ni Khalifa wa Waislamu angemridhia bibi Fatmah na ampe kile alichokidai, kwa kuwa alikuwa mkweli na Mwenyezi Mungu anashuhudia ukweli wake, na Mtume pia ashuhudia ukweli wake, na Waislamu wote akiwemo Abubakr wanashuhudia ukweli wake, ni siasa tu ndio inayogeuza kila kitu kwa hiyo mkweli huwa muongo na muongo huwa mkweli.

Naam, hakika hii ni aina mojawapo ya njama zilizofumwa ili kuwaweka kando Ahlilbait mbali na cheo na daraja ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwapa na zilianza kwa kumuweka Ali ibn AbiTaalib kando mbali na Ukhalifa, na kupokonya zawadi ya bibi Fatmah na mirathi yake, kumfanya muongo na kumnyanyasa ili pasibakie heshima yoyote katika mioyo ya Waislamu. Njama ziliendelea mpaka Ali, Hassan na Hussein, wakauawa. Ama kwa upande wa Hussein aliuliwa yeye pamoja na watoto wake bila huruma, na akina mama waliobakia walichukuliwa mateka. Njama hizo hazikuishia hapo tu, bali Mashia wa Ahlilbait, wapenzi wao na wafuasi wao waliuliwa, na hapana shaka zingali zinaendelea hadi leo na zinafanya kazi yake na zinatoa matunda ya kazi yake. Naam Muislamu yeyote aliyehuru na muadilifu atatambua asomapo vitabu vya historia na kutafiti ukweli na kuiweka kando batili, ataona kuwa Abubakr ni wa kwanza kabisa kuwafanyia dhulma Ahlilbait, na atatosheka na kuisoma sahihi Bukhari tu vile itakapomwekea wazi ukweli endapo atakuwa mtafiti wa kweli.

Bukhari ni huyo (umjuaye) pia Muslimu, wote wanakiri kuwa Abubakar Sidiq alimkubalia sahaba yeyote yule wa kawaida tu kwa dai lake, na akamkatalia Fatuma Zahra na kuudai kuwa ni muongo hali ya kuwa Fatumah Zahra ni mwanamke bora katika wanawake wa peponi na ni yule ambaye Mwenyezi Mungu ameshuhudia kwa kumuondolea madhambi na kumfanya mtakatifu pia Abubakr alimfanya Ali kuwa ni muongo pia Umu

Aiman naye akamfanya kuwa ni muongo. Hebu soma sasa uone wayasemayo Bukhari na Muslim. Bukhari ameandika katika sahihi yake juzuu ya tatu kitabu cha Shahadaati mlango wa Man amara bi injazil-waadi. Na Muslim katika sahihi yake ndani ya kitabu cha Al-fadha-il mlango wa Maasuila Rasulullahi shai-an qat, faqala -la, wakathurat a'taihi. Imepokewa kutoka kwa Jabir ibn Abdillah (r.a) amesema: Alipokufa Mtume **(s.a.w.w)**, kuna mali ilimfikia Abubakar kutoka kwa Al-a'laa ibn Al-Hadhrami, Abubakr akasema: Yeyote ambaye alikuwa na deni kwa Mtume **(s.a.w.w)** au alikuwa na ahadi kwa Mtume basi na aje kwetu, Jabir akasema, Mimi, nikasema, Mtume wa Mwenyezi Mungu aliniahidi kuwa atanipa hivi na hivi na hivi, akakunjua mikono yake mara tatu, basi zikahesabiwa mikononi mwangu mia tano, kisha mia tano, kisha mia tano."

Je, hivi kuna mtu atakayemuuliza Abubakr, "Ni kwa nini alimuamini Jabir ibn Abdallah katika madai yake kwamba Mtume **(s.a.w.w)** alimuahidi kumpa hivi na hivi na hivi, kisha Abubakr akaijaza mikono yake mara tatu kwa kiwango cha elfu moja mia tano bila ya kumtaka alete shahidi japo mmoja tu ili kuthibitisha madai yake? Na je Jabir ibn Abdillahi alikuwa mcha Mungu na mtakatifu mno kuliko Fatmah ambaye ni mwanamke bora ulimwenguni? Cha kushangaza kuliko yote ni kwa yeye kuukataa ushahidi wa mumewe Fatmah; Ali ibn Abi Talib ambaye Mwenyezi Mungu amemtakasa mno na akajaalia kuwa ni faradhi kwa Waislamu wote kumtakia rehma (Ali) kama wamtakiavyo rehma Mtume **(s.a.w.w)**. Na ni huyo huyo Ali ibn Abi Talib ambaye Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema kuwa, "Kumpenda Ali ni (alama ya) imani na kumchukia ni (alama ya) unafiki.

Zaidi ya hayo ni kwamba, Bukhari mwenyewe amethibitisha katika tukio jingine linalotupatia picha halisi ya dhulma aliyofanyiwa bibi Fatmah na watu wa nyumba ya Mtume **(s.a.w.w)**. Bukhari amethibitisha ndani ya sahihi yake Baku maala yahillu liahadin an yar-jia' fi hibatih wasadaqatih, Kitabul-hibat wafadhliha wat-tahridh a'laiha: Amesema kwamba, "Watoto wawili wa Suhaib rum wa Judh'an walidai nyumba mbili na chumba kimoja na kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu alimpa vitu hivyo Suhaib, basi Mar-wan akasema: Nani atakushuhudieni juu ya madai yenu? Wakasema, Ibn Umar, Akamwita akashuhudia kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** alimpa Suhaib nyumba mbili na chumba kimoja, basi Mar-wan akaukubali ushahidi wake kwa jamaa hao" Tazama ewe Muislamu matendo haya na maamuzi haya ambayo yanatekelezwa kwa wengine na wengine yanakataliwa, je, hii siyo miongoni mwa dhulma na hila? Na ikiwa Khalifa wa Waislamu anaamua kwa faida ya wanaodai kwa kiasi tu cha ushahidi wa Ibn Umar, basi je, Muislamu anaweza kujiuliza ni kwa nini basi ushahidi wa Ali ibn Abi Talib ulipingwa pia ushahidi wa Ummu Aiman (nao ulikataliwa yeye) pamoja na Imam Ali? (Lakini ni lazima pia ufahamu kwamba) ushahidi wa mwanamume na mwanamke una nguvu kuliko ushahidi wa mwanamume mmoja peke yake ikiwa hatutataka kukifikia kile kiwango ambacho Qur'ani inakitaka.

Au tuseme watoto wa Suhaib ni wakweli mno katika madai yao kuliko Binti wa Mtume **(s.a.w.w)**, na kwamba Abdallah ibn Umar ni mkweli mno mbele ya watawala hao wakati ambapo Ali siyo mkweli kwa watawala hao?

Ama madai yasemayo kwamba Mtume **(s.a.w.w)** harithiwi, nayo ni ile hadithi aliyokuja nayo Abubakar, na bibi Fatmah akaipinga kwa Kitabu cha Mwenyezi Mungu ambacho ni hoja isiyopingika kamwe, kwani imesihi hadithi kutoka kwa Mtume **(s.a.w.w)** aliposema: "Itakapokujieni hadithi kutoka kwangu basi ipimeni kwenye Kitabu cha Mwenyezi Mungu, ikikubaliana na Kitabu cha Mwenyezi Mungu itumieni na ikienda kinyume ipigeni ukutani."

Basi hapana shaka hadithi hii inapingwa na aya nyingi katika Quran, je yuko mtu atakayemuuliza Abubakr ni kwa nini ushahidi wa Abubakr peke yake unakubalika katika riwaya ambayo inapinga aya na akili, isitoshe kitabu cha Mwenyezi Mungu kinaipinga hadithi hiyo? (Lakini jambo la kushangaza ni kwamba), ushahidi wa bibi Fatmah haukukubalika hali ya kuwa unaafikiana na nukuu na akili, na haupingani na Qur'an!! Zaidi ya hapo ni kwamba, pamoja na kuwa Abubakr daraja yake ilipanda na wanaomuunga mkono na wanaomtetea wakamtengenezea chungu nzima ya ubora, bila shaka hawezi kufikia daraja ya bibi Fatmah ambaye ni mwanamke bora ulimwenguni, wala (Abubakr) hawezi kufikia daraja ya Ali ibn Abi Talib ambaye Mtume **(s.a.w.w)** amemtukuza juu ya Masahaba wote katika kila nyanja, nazitaja baadhi yake kama mfano:

Siku aliyompa bendera na Mtume akamthibitisha kwamba yeye Ali anampenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Mwenyezi Mungu na Mtume wake nao wanampehda Ali. Na siku hiyo Masahaba waliingojea kwa hamu kila mmoja akitaraji kupewa yeye, basi Mtume hakumpa isipokuwa Ali. Pia Mtume wa Mwenyezi Mungu alisema kuhusu Ali kwamba, "Bila shaka Ali anatokana nami, na mimi natokana naye, na yeye ni msimamizi wa kila Muumini baada yangu. Na kama watafanya shaka wang'ang'anizi na wenye chuki juu ya usahihi wa hadithi hizi, basi kamwe hawatakuwa na shaka kwamba kumtakia rehma Ali na Fatmah ni sehemu ya sala ya Mtume **(s.a.w.w)**, na haikubaliki sala ya Abubakr, Umar wala Uthman na wale waliobashiriwa pepo na Masahaba wote pamoja na Waislamu wote ikiwa ndani ya sala zao hakusaliwa Mtume Muhammad na kizazi cha Mtume Muhammad ambao Mwenyezi Mungu amewaondolea uchafu na akawatakasa mno, kama yalivyokuja maelezo hayo ndani ya Sihahi za Masunni zikiwemo Sahih Muslim na Bukhari na Sihah nyinginezo mpaka Imam Shafii amefikia kusema kuhusu haki yao kwamba: "Yeyote asiyekusalieni (enyi watu wa nyumba ya Mtume) mtu huyo hana sala."

Basi ikiwa watu hawa wa nyumta ya Mtume inafaa kusema uongo na kudai madai yasiyo ya kweli basi Uislamu umeingia katika mtihani Ama ukiuliza ni kwa nini ushahidi wa Abubakr unakubalika na ushahidi wa watu wa nyumba ya Mtume unapingwa? .Tawabu ni kuwa, yeye ndiye mtawala na mtawala ana uwezo wa kuamua akitakacho na kwa hali yoyote ile yeye ndiye mwenye haki, kwani madai ya mwenye nguvu ni kama madai ya mnyama mkali kwa meno na makucha aliyo nayo-kwani hiyo ndiyo-hoja yake.

Na ili ukubainikie vema ukweli wa mambo ewe msomaji mtukufu, hebu tuwe pamoja ili uyasome aliyoyathibitisha Bukhari ndani ya sahih yake kuhusu kugongana kwa suala la mirathi ya Mtume ambalo yeye Bukhari alilisema kama alivyolieleza Abubakr kwamba (Mtume kasema) "Sisi

Mitume haturithiwi tunachokiacha ni sadaka." Haya ni mapokezi ambayo Masunni wote wanayakubali na kuyatolea dalili ya Abubakr kutokubali maombi ya bibi Fatmah (juu ya mirathi yake kwa Mtume). Jambo litakachokujulisha juu ya kutosihi kwa hadithi hii na kwamba haifahamiki (kwa Waislamu) ni bibi Fatmah (a.s) kudai mirathi yake, na isitoshe wakeze Mtume ambao ni mama wa waumini nao walimtumia ujumbe Abubakr wakitaka mirathi yao. Hayo ndiyo aliyoyaandika Bukhari na ndiyo yanayotolewa dalili juu ya kutokurithiwa kwa Mitume, lakini Bukhari anajipinga mwenyewe pale alipothibitisha kwamba Umar ibn Khatab aligawa mirathi ya Mtume kwa wake zake.

Amethibitisha Bukhari ndani ya sahih yake, Kitabul-Wakala, Babul-Muzara'ah Bis-shatri. Imepokewa kutoka kwa Nafi'i kwamba, Abdallah ibn Umar (r.a) alimwambia kuwa, Mtume alimuwakilisha Khaibar kwenye sehemu ambayo kunatoka matunda au mimea, basi alikuwa akiwapa wakeze Mtume mafungu mia moja na mafungu themanini yakiwa ni ya tende na ishirini ya shairi, basi Umar akaigawa Khaibar akawakhiyarisha wakeze Mtume **(s.a.w.w)** awakatie sehemu ya maji na ardhi au yeye awaamulie, basi miongoni mwao kuna waliochagua ardhi na kuna waliochagua shehena za tende na shairi, na Aisha alikuwa miongoni mwa waliochaguwa ardhi."

Riwaya hii inajulisha wazi kwamba Khaibar ambayo ndiyo aliyoitaka bibi Fatmah apewe sehemu yake kama mirathi yake kwa baba yake na Abubakar akamkatalia maombi yake kwa kuwa eti Mtume wa Mwenyezi Mungu harithiwi, na riwaya hii inajulisha wazi pia kwamba Umar ibn Khatab aliigawa Khaibar katika zama za Ukhalifa wake kuwagawia wakeze Mtume **(s.a.w.w)** na akawakhiyarisha baina ya kumiliki ardhi au shehena, na Aisha alikuwa miongoni mwa waliochagua ardhi. Basi ikiwa Mtume **(s.a.w.w)** harithiwi ni vipi Aisha ambaye ni mke anarithi na Fatmah ambaye ni binti asiweze kurithi? Tuelimisheni juu ya mambo kama hayo enyi wenye kufahamu nanyi mtapata ujira (mwema) na thawabu.

Zaidi ya hayo ni kwamba bibi Aisha binti Abubakr aliikalia nyumba nzima ya Mtume **(s.a.w.w)** na hakuna mke yeyote wa Mtume **(s.a.w.w)** aliyepata hadhi kama aliyopata Aisha, naye Aisha ndiye aliyemzika baba yake ndani ya nyumba hiyo ya Mtume **(s.a.w.w)**, na akamzika Umar karibu ya baba yake, na ni Aisha huyo huyo aliyemzuwia Husein (a.s) asimzike nduguye Hasan pembeni mwa babu yake. Jambo hili lilimfanya Ibn Abbas aseme kama ifuatavyo juu ya bibi Aisha; "Ulipanda ngamia ukapanda na nyumbu, lau utaishi zaidi utapanda tembo, yako ni sehemu moja kati ya tisa katika thumni (moja ya nane) lakini wewe yote umeitumia."

Iwe iwavyo, mimi sikusudii kurefusha maudhui hii, bali hapana budi kwa wanaotafiti kuirejea historia, lakini si vibaya nikataja sehemu ya khutuba ambayo aliitoa bibi Fatimah (a.s) mbele ya Abubakr na Masahaba wengine, ili aangamie mwenye kuangamia miongoni mwao kutokana na ukweli (kama atakataa kuutambua) na aokoke mwenye kuokoka miongoni mwao kutokana na ukweli (iwapo ataukubali).

Bibi Fatmah alisema: "Je, hivi ni kwa makusudi mumekiacha Kitabu cha Mwenyezi Mungu mkakitupa nyuma ya migongo yenu? Kwani Mwenyezi Mungu anasema: Na Sulaiman alimrithi Daudi. Na akasema akisimulia kisa kuhusu habari ya Zakariya: Basi nipe mrithi kutoka kwako atakayenirithi

mimi na kuwarithi kizazi cha Ya'aqub na umfanye (mrithi huyo) ewe Mola wangu awe mwenye kukuridhisha. Na amesema Mwenyezi Mungu: Basi nipe mrithi kutoka kwako, atakayenirithi na kuwarithi kizazi cha Ya'aqub na umfanye ewe Mola wangu awe mwenye kukuridhisha. Na amesema tena: Mwenyezi Mungu anakuusiyeni juu ya watoto wenu, mwanamume apate sawa na sehemu ya wanawake wawili.

Na amesema pia kwamba: Na ndugu wa nasaba wanastahikiana wenyewe kwa wenyewe (katika kurithiana hivyo ndivyo ilivyo) katika kitabu cha Mwenyezi Mungu. Na amesema tena: Mmefaradhishiwa, mmoja wenu anapofikwa na mauti, kama akiacha mali, Aiusie kwa wazazi (wake) na jamaa zake kwa namna njema, haya ni wajibu kwa wamchao Mwenyezi Mungu." (Bibi Fatmah anaendelea kusema baada ya aya hizo za Qur'an) Je, hivi Mwenyezi Mungu amekuhusisheni ninyi kwa aya fulani na akamtoa baba yangu katika aya hizo? Au ninyi mnaijua mno Qur'an inapohusisha (kitu maalum) na inapozungumza kwa kuenea kuliko ajuavyo baba yangu na ibn ammi yangu (Ali)? Au mnasema kuwa watu wa mila mbili hawarithiani.

14

# WAULIZE WANAOFAHAMU

## ABUBAKR ALIWAUA WAISLAMU WALIOKATAA KUMPA ZAKA

Bukhari amethibitisha katika sahih yake Kitabustitabatil Mar-taddina, Babu qatli man abaa qabulal-faraidhi wama nusibu ilar-ridah, na Muslim naye ndani ya sahih yake Kilabul-iman babul-amri biqitalin-nas. Imepokewa kutoka kwa Abu Hurairah amesema: "Alipofariki Mtume **(s.a.w.w)** na Abubakar akatawazwa, na wakapinga waliopinga miongoni mwa Waarabu, Umar alisema: Ewe Abubakr vipi unataka kuwapiga watu na hali ya kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema kuwa, Nimeamrishwa niwapige watu mpaka waseme Lailaha Illallah, basi yeyote atakayesema Lailaha Illallah mali yake na nafsi yake imehifadhika kutokana nami isipokuwa kwa haki na hisabu yake ni juu ya Mwenyezi Mungu. Abubakar akasema: Wallahi nitampiga yeyote anayetenganisha baina ya sala na zaka kwani zaka ni haki inayostahiki katika mali, Wallahi lau wakinizuwilia mbuzi mdogo (wa zaka) waliyekuwa wakimtoa kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** basi nitawapiga kwa kuizuwia (zaka hiyo). Umar akasema basi, Wallahi sikuona isipokuwa Mwenyezi Mungu alikifungua kifua cha Abubakr (ili awapige nami nikafahamu kuwa ni haki."

Na jambo hili si geni kwa Abubakar na Umar ambao walitishia kuichoma moto nyumba ya bibi Fatmah aliye mwanamke bora, pamoja na waliokuwemo miongoni mwa Masahaba waliokataa kutoa baia. Na kama itakuwa kuwachoma moto Fatmah, Ali, Hassan, Hussein na kundi la Masahaba bora ambao walikataa kutoa baia ni jambo jepesi kwa Abubakr na Umar, basi siyo jambo zito kwao kuwaua wanaokataa kutoa zaka. Wana thamani gani Mabedui wa mbali ukiwalinganisha na kizazi kitukufu cha Mtume na Masahaba hao wema? Na zaidi ya hapo ni kwamba hawa waliokataa kutoa baia walikuwa wanaona kuwa haki ya Ukhalifa ni yao kwa mujibu wa matamko ya Mtume **(s.a.w.w)**, na hata kama tutajaalia iwe hakuna tamko linalowahusisha katika haki waliyokuwa nayo, lakini walikuwa na haki ya kupinga, kukosoa na kutoa maoni kama kweli kulikuwa na mashauriano kama wanavyodai.

Pamoja na hayo kule kuwatishia kuwachoma moto ni jambo lililothibiti, na lau si kukubaliana kwa Ali na kuwaamuru wale Masahaba watoke wakatoe baia ili kuhifadhi kumwagika kwa damu ya Waislamu na umoja wa Uislamu, basi watawala hao wasingechelewesha kuwachoma moto. Ama kwa hakika mambo yaliwanyookea kina (Abubakr na Umar) na zikaimarika nguvu zao, na hapakuwepo mtu mwenye kuwapinga baada ya kufariki kwa bibi Fatmah na baada ya Imam Ali kufanya nao Sulhu, kwa hiyo ni vipi basi watayanyamazia baadhi ya makabila ambayo yalikataa kuwapa zaka yakidai kuwa yanasubiri mpaka jambo la uongozi na mambo yaliyotokea baada ya Mtume **(s.a.w.w)** yabainike, ikwemo ule Ukhalifa ambao Umar mwenyewe amekiri kuwa ulikuwa ni wa ghafla. Kwa hiyo basi haishangazi (kumuona) Abubakr na serikali yake wananyanyuka na kuwauwa Waislamu wasiokuwa na hatia yoyote na kuwavunjia heshima zao na kuwateka wanawake zao.

Kwa hakika wanahistoria wameeleza kwamba, Abubakar alimtuma Khalid ibn Walid akaliangamize kabila la Bani Sulaim, na akamtuma kwenda Al-Yamamah, na pia kwa Bani Tamim. Khalid aliwaua watu hao kwa hila baada ya kuwafunga mikono na kuzikata shingo zao hali ya kuwa wamefungwa, na akamuuwa Malik ibn Nuwairah sahaba mtukufu ambaye Mtume wa Mwenyezi Mungu alimtawalisha kusimamia sadaka za jamaa zake kwa kumuamini, kisha Khalid akamuingilia mke wa Malik katika usiku ule ule aliomuua mumewe!!! Lahaula Wala quwwata ilia billahil-aliyyil-adhim.

Malik na jamaa zake hakuwa na kosa lolote isipokuwa ni kwamba waliposikia mambo yaliyotokea baada ya kufariki kwa Mtume **(s.a.w.w)** ikiwa ni pamoja kutengwa kwa Imam Ali na kudhulumiwa kwa bibi Fatmah mpaka akafariki hali ya kuwa amewakasirikia (kina Abubakr). Si hayo tu bali upinzani wa kiongozi wa Ansari Saad ibn Ubbadah na kujitoa kwenye baia yao, na mengineyo waliyoyanakili Waarabu miongoni mwa habari zinazotia shaka juu ya kusihi kwa baia ya Abubakar, kutokana na yote haya Malik na jamaa zake walikataa kutoa zaka. Hivyo basi hukumu iliyotoka kwa Khalifa (Abubakr) na wasaidizi wake ikawa ni kuwaua na kuwateka wanawake zao na watoto wao kisha kuvunja heshima zao na kuwaangamiza kabisa ili kusije kukatokeza miongoni mwa Waarabu wenye maoni ya upinzani au kuhoji juu ya suala la Ukhalifa. Kwa kweli linalohuzunisha mno ni kule kumkuta mtu anamtetea Abubakar na utawala wake, na anayafanya makosa ya Abubakar kuwa ni sahihi, makosa ambayo yeye mwenyewe anakiri kuwa ni makosa, na katika kumtetea anasema kama ilivyokauli ya Umar aliposema: "Wallahi sikuona isipokuwa Mwenyezi Mungu alikifungua kifua cha Abubakar (alimuongoza) ili awapige, nikafahamu kuwa hiyo ni haki."

Je, tunaweza kumuuliza Umar siri ya yeye kutosheka juu ya mauaji haya ya Waislamu, Waislamu ambao yeye mwenyewe Umar ameshuhudia kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu ameharamisha kuwauwa kwa sababu tu ya wao kusema Lailaha Illa llah? Ni huyu huyu Umar ndiye aliyemuhadithia Abubakar hadithi hii, ni vipi aligeuka ghafla na akatosheka wauawe? Alitambua kuwa hiyo ni haki eti kwa kuona Mwenyezi Mungu amemuongoza Abubakar, basi je ni vipi tendo la kuongozwa Abubakar lilitimia, na watu wengine wasilione? Ikiwa tendo la Abubakar kupewa muongozo lilikuja kimaana na siyo kwa kuthibitisha (kimaono) basi vipi Mwenyezi Mungu awaongoze watu kwenda kinyume na maamuzi yake ambayo ameyapitisha kwa kupitia ulimi wa Mtume wake **(s.a.w.w)**? Na itakuwaje Mwenyezi Mungu awaambie waja wake kupitia ulimi wa Mtume wake kwamba yeyote atakayesema Lailaha Illallah ni haramu kwenu kumuua na malipo yake yako kwangu, kisha hatimaye ampe muongozo Abubakar na Umar wawaue Waislamu hao? Je, kuna ufunuo ulioshuka kwao baada ya Mtume Muhammad? Au ndiyo ijtihadi ambayo inayohukumiwa kwa kutegemea maslahi ya kisiasa, Ijtihadi ambayo imezitupilia mbali hukumu za Mwenyezi Mungu? Ama madai ya wanaowatetea yanasema kuwa, "Watu hawa walitoka katika Uislamu, basi ilikuwa ni lazima kuwaua."

Jambo hilo siyo sahihi, na yeyote ambaye anafuatilia kwa undani vitabu vya historia ataelimika kwa elimu yakinifu kwamba anayezuwia kutoa zaka huwa hajatoka katika Uislamu, basi vipi watakuwa walitoka katika Uislamu hali ya kuwa walisali pamoja na yeye Khalid na jamaa zake walipofika kwenye maeneo yao? Kisha Abubakar mwenyewe aliyabatilisha madai haya ya uongo kwa kutoa fidia (kutokana na mauaji) ya Malik kutoka ndani ya hazina ya Waislamu na akataka radhi kwa kumuua Malik? Na mtu aliyetoka katika dini hakuna kuomba radhi kwa kumuua na wala haitolewi fidia yake kutoka ndani ya hazina ya Waislamu!! Hapana yeyote miongoni mwa viongozi wema waliotangulia aliyesema kwamba wanaozuwia zaka wametoka katika Uislamu, isipokuwa haya yamesemwa katika zama za karibuni pale yalipokuwa yametokea madhehebu na tofauti nyingi miongoni mwa Waislamu.

Masunni wamejaribu juhudi zao bila ya mafanikio kuvitakasa vitendo vya Abubakr, lakini hawakupata njia isipokuwa ni kuwapakazia Waislamu hao kuwa waliritaadi (wakatoka katika Uislamu) na hii ni kwa kuwa Masunni wanafahamu kuwa, kumtukana Muislamu ni ufasiki na kumuua ni kufru, kama yalivyoelezwa hayo ndani ya sahih za Masunni. Hata Bukhari alipoiandika hadithi ya Abubakar na kauli yake aliposema, "Wallahi nitamuua yeyote anayetenganisha kati ya sala na zaka," aliufungua mlango kwa anuani isemayo: "Mwenye kukataa faradhi na wala hakusema kuwa wameritadi." Hiyo ni dalili ya kwamba Bukhari mwenyewe haamini kuwa waliritadi, kama inavyoonekana wazi. Na wengine (miongoni mwa Masunni) wamejaribu kuitolea tafsiri nyingine hadithi hii kama alivyoitafsiri Abubakar kwamba, zaka ni haki ya mali, na hii ni tafsiri iliyowekwa mahala ambapo si pake.

**Kwanza**: Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** ameharamisha kumuua yeyote aliyesema Lailaha Illallah peke yake, na juu ya hilo ziko hadithi nyingi ambazo Sihah zimezithibitisha na tutakuletea hadithi hizo.

**Pili**: Japokuwa zaka ni haki ya mali, hadithi hii inamruhusu mtawala wa kisheria kuchukua zaka kwa nguvu kutoka kwa anayeizuwia bila kumwaga damu yake.

**Tatu**: Basi lau tafsiri hii ingekuwa sahihi, Mtume wa Mwenyezi Mungu angemuuwa Tha'alabah ambaye alikataa kutoa zaka kwa Mtume (kisa hiki ni mashuhuri hakuna sababu ya kukitolea maelezo).

**Nne**: Hebu angalia yale yaliyoandikwa na vitabu vya Kisunni kuhusu heshima ya mtu atakayesema Lailaha Illallah, nami nitatosheka na Bukhari na Muslim na baadhi tu ya hadithi ili nifupishe maelezo.

A: Muslim amethibitisha ndani ya sahih yake, Kitabul-iman Babu Tahrimi qatlil-kafir ba'ada an qala Lailaha illallah, Naye Bukhari ndani ya sahih yake, Kitabul-maghazi babu had-d thani Khalifatu anil Miq-dad ibnil-As-wad, kwamba yeye Miqdad alimwambia Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**: "Mtume waonaje ikiwa nitakutana na mtu miongoni mwa makafiri, tukapigana, kisha yeye akaupiga kwa upanga mmoja kati ya mikono yangu na akaukata, kisha akajikinga kutokana nami kwenye mti, halafu akasema, Nimesilim kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Je, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu nimuue mtu huyo baada ya kusema kauli hiyo?" Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema: "Usimuue." Miqdad akasema "Ewe

Mtume wa Mwenyezi Mungu hakika yeye ameukata mmoja kati ya mikono yangu kisha amesema hayo baada ya kuukata." Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema, "Usimuue, kwani ukimuuwa yeye atachukua mahala pako ulipokuwa kabla hujamuua na wewe utachukua mahala pake alipokuwa kabla hajasema neno lake hilo alilolisema."

Hadithi hii inafidisha kwamba, kafiri aliyesema Lailaha Illallah, japokuwa baada ya kumtendea ubaya Muislamu kwa kumkata mkono wake, ni haramu kumuua, na hapo hakuna (sharti ya) kukiri kuwa Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu wala kusimamisha sala wala kutoa zaka na wala kufunga Ramadhani wala kuhiji Makka. Basi ni wapi mwendako (katika kutetea uovu aliofanya Abubakr) na ni kitu gani mnachokitetea? B: Bukhari ameandika ndani ya sahih yake, Kitabul-Maghazi babu baathin-nabiyyi **(s.a.w.w)** Usama ibn Zaid ilal-hir-qaat min juhainah, na Muslim ndani ya sahih yake, Kitabul-iman babu tahrimi qatlil-kafir ba 'ada an qaala Lailaha illa llah.

Imepokewa kutoka kwa Usamah ibn Zaid amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu alitutuma kwenda Al-Hurqah, asubuhi tukawafika kwa jamaa hao na tukawashambulia, mimi na mtu fulani miongoni mwa Ansar tukakutana na mtu katika jamaa hao, basi tulipomvamia akasema Lailaha illa llah "Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu." Yule Muansar akamuacha asimshambulie yule mtu, mimi nikamchoma kwa mkuki wangu nikamuua. Tuliporudi, habari hizo zikamfikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema: Ewe Usamah umemuua baada ya kusema Lailah illa llah? Nikasema, alikuwa akijitetea tu. Basi Mtume hakuacha kukariri usemi wake huo mpaka nikatamani kuwa nisingekuwa nimesilimu kabla ya siku ile." Hadithi hii moja kwa moja inafidisha kwamba yeyote atakayesema Lailaha illa llah ni haramu kumuua, ndiyo maana unamuona Mtume **(s.a.w.w)** anamkemea mno Usamah mpaka Usamah anatamani kwamba asingekuwa amesilimu kabla ya siku ile ili impate ile hadithi isemayo kuwa, Uislamu unafuta yaliyopita kabla yake, ili awe na matumaini ya kupata msamaha wa Mwenyezi Mungu kuhusu dhambi hii kubwa aliyoifanya. C: Bukhari ameandika ndani ya sahih yake, Kitabul-libasi babut-thiyabil-biidh. Kadhalika Muslim ndani ya sahih yake Kitabul-imani babu man maata laa Yushriku billahi shaian dakhalal-jannah.

Imepokewa kutoka kwa Abu Dharri Al-ghifari (r.a) amesema: "Nilikwenda kwa Mtume **(s.a.w.w)** akiwa amejifunika nguo nyeupe amelala, kisha nikamwendea akawa ameamka akasema, Hapana mja yeyote atakayesema Lailaha illa llah kisha akafa hali ya kuwa yuko katika hali hiyo isipokuwa ataingia peponi. Nikasema japo atazini na ataiba? Akasema: Japo atazini na ataiba. Nikasema japo atazini na ataiba? Akasema japo atazini na ataiba hata kama Abudharri atachukia." Abudharri kila alipoisimulia hadithi hii alikuwa akisema "**Hata kama Abudharri atachukia**." Na hii ni hadithi nyingine inayothibitisha kuingia peponi kwa mtu yeyote atakayesema Lailah Illa llah na akafa. Katika hali hiyo basi haifai kumuua, na hata kama Abubakar na Umar watachukia na wote wanaowatetea ambao wanaugeuza ukweli kwa kulinda heshima ya viongozi wao waliopita na wakubwa zao ambao walizibadilisha hukumu za Mwenyezi Mungu. Ukweli halisi ulivyo ni kwamba Abubakar na Umar wanazifahamu hukumu zote hizo, kwani wao

wako karibu mno kuliko sisi katika kufahamu hukumu hizo na wako karibu mno na Mtume kuliko wengineo, lakini watu hawa kwa ajili ya (tamaa ya) uongozi walibadilisha hukumu nyingi za Mwenyezi Mungu na Mtume wake **(s.a.w.w)** hali ya kuwa wanajua wazi.

Na huenda Abubakr alipoazimia kuwaua waliozuwia kutoa zaka, na Umar akampinga kwa hadithi ya Mtume **(s.a.w.w)** ambayo inaharamisha jambo hilo, basi Abubakr alimkatiza jamaa yake kwa kumwambia kuwa (akumbuke kwamba) yeye ndiye aliyebeba kuni kwenda kuichoma nyumba ya Fatmah na kwamba Fatmah alipopeleka madai yake alikuwa akishuhudia kwamba hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, (pamoja na hali hiyo Umar akataka kwenda kuichoma nyumba ya Fatmah) kisha (Abubakr) akamkinaisha Umar kwamba, Fatmah na Ali hawakuwatendea (kina Abubakr) jambo lolote kubwa (la kuhatarisha) katika Ukhalifa, wakati ambapo makabila haya yalikataa kutoa zaka, kwa hiyo lau wangewaacha na jambo lao hilo likaenea katika miji ya Kiislamu, basi bila shaka pangetokea athari kubwa kwao kwenye makao makuu ya Ukhalifa. Basi hapo ndipo Umar alipoona kuwa eti Mwenyezi Mungu amemuongoza Abubakr awapige na akakiri kuwa hiyo ni haki.

Abubakr alikataza kuandikwa Sunna ya Mtume, pia Umar na Uthman nao walifanya hivyo baada yake. Bila shaka mtu anayetafiti akisoma vitabu vya historia na akafuatilia baadhi ya mambo ambayo utawala wa Makhalifa watatu ulikuwa umeyakusudia kuyafanya, atafahamu vilivyo kwamba wao ndiyo waliokataza kuandikwa hadithi za Mtume Mtukufu, bali walikataza hata kuzisimulia na kuzinakili kuwajulisha watu, kwani Makhalifa hao bila shaka walifahamu kwamba hazitatumikia maslahi yao au zitapingana na maamuzi yao mengi na yale waliyoyageuza kufuatia juhudi zao na kwa maslahi yao. Hadithi za Mtume **(s.a.w.w)** ambazo ndiyo msingi wa pili wa sheria ya Kiislamu, na ndizo zenye kufasiri na kuubainisha msingi wa kwanza ambao ni Qur'ani Tukufu, zilibakia ni marufuku na ni haramu (kuziandika na kuzizungumza) katika kipindi chao cha utawala na ndiyo maana wameafikiana wanachuoni wa hadithi na wale wa historia kuwa mwanzo wa kukusanywa hadithi na kuandikwa ilikuwa katika zama za Umar ibn Abdil-aziz (r.a) au baada yake kwa kipindi kifupi.

Bukhari amenakili ndani ya sahih yake, Kitabul-ilmi, babu kaifa yuqbahd-ilm, amesema, "Umar ibn Abdul-aziz alimwandikia Abubakar ibn Hazmi akamwambia, Ziangalie hadithi za Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** uziandike, hakika mimi nachelea kuhusu elimu na kutoweka kwa wanachuoni, na isikubaliwe isipokuwa iwe ni hadithi ya Mtume **(s.a.w.w)** na elimu ienezwe na watu wakae ili kila asiyejua afundishwe, kwani elimu haipotei mpaka pale inapofichwa. Basi hebu msikilize Abubakr anawahutubia watu baada ya kufariki Mtume **(s.a.w.w)** anawaambia: "Bila shaka ninyi mnasimulia hadithi kutoka kwa Mtume **(s.a.w.w)** ambazo mnakhitilafiana katika hadithi hizo, na watu watakaokuja baada yenu watahitilafiana mno, hivyo basi msisimulie chochote kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, yeyote atakayekuulizeni semeni kuwa, Baina yetu na ninyi kipo Kitabu cha Mwenyezi Mungu, halalisheni halali yake na mharamishe haramu yake.

Wallahi Abubakr ana mambo ya ajabu, ni yeye huyo huyo baada ya siku chache tangu siku ile ya kusikitisha ambayo iliitwa kuwa ni msiba wa siku ya Al-hamisi anaafikiana moja kwa moja na yale aliyoyasema jamaa yake Umar ibn Khatab pale aliposema "Bila shaka Mtume wa Mwenyezi Mungu anaweweseka, kinatutosha Kitabu cha Mwenyezi Mungu." Sasa (Abubakr) naye anasema: "Msisimulie chochote kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, yeyote atakayekuulizeni semeni kuwa, kati yetu na ninyi ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu, halalisheni halali yake na muharamishe haramu yake." Ashukuriwe Mwenyezi Mungu (kwa sababu Abubakr) amekiri wazi kwamba, wao waliitupa mgongoni Sunna ya Mtume wao na wakaifanya kuwa ni kitu kilichosahaulika kabisa. Swali lililopo hapa ni linawaelekea Masunni ambao wanawatetea Abubakr na Umar. na kuwaona kuwa wao ndiyo viumbe bora mno baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** nini hili lifuatalo: Iwapo Sihah zenu (vitabu vyenu sahihi) kama mnavyoitakidi vinaandika riwaya isemayo kwamba, Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Nimekuachieni Makhalifa wawili ambao mkishikamana nao hamtapotea kamwe, Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna zangu.**" Sisi tunajaalia kuikubali hadithi hii kuwa ni Sahihi, lakini ilikuwaje kwa hao wabora wa viumbe kwenu ninyi kuikataa sunna (ya Mtume) na wala hawakuipa uzito unaostahiki, bali wakiwazuwia watu kuiandika na kuisimulia? Je, kuna mtu atakayemuuliza Abubakar ni katika aya gani amekuta (ruhusa ya) kuwaua Waislamu wanaokataa kutoa zaka na kuwateka nyara wake zao na watoto wao?

Kitabu cha Mwenyezi Mungu ambacho ndicho kilichopo kati yetu na Abubakr kinasema wazi kuhusu watu wanaokataa kutoa zaka.

وَمِنْهُم مَّنْ عَاهَدَ اللَّـهَ لَئِنْ آتَانَا مِن فَضْلِهِ لَنَصَّدَّقَنَّ وَلَنَكُونَنَّ مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿٧٥﴾ فَلَمَّا آتَاهُم
مِّن فَضْلِهِ بَخِلُوا بِهِ وَتَوَلَّوا وَّ هُم مُّعْرِضُونَ ﴿٧٦﴾ فَأَعْقَبَهُمْ نِفَاقًا فِي قُلُوبِهِمْ إِلَىٰ يَوْمِ يَلْقَوْنَهُ بِمَا
أَخْلَفُوا اللَّـهَ مَا وَعَدُوهُ وَبِمَا كَانُوا يَكْذِبُونَ ﴿٧٧﴾

"Na miongoni mwao wapo waliomuahidi Mwenyezi Mungu kuwa, Akitupatia katika fadhila zake, tutatoa sadaka na tutakuwa miongoni mwa wanaotenda mema, lakini alipowapa hizo fadhila zake, walizifanyia ubakhili na wakakengeuka, kwa hiyo akawalipa unafiki ndani ya nyoyo zao mpaka siku ya kukutana naye kwa sababu ya wao kukhalifu waliyomuahidi Mwenyezi Mungu na kwa sababu ya kusema kwao uongo." (Qur'ani, 9:75-77).

Na kwa maafikiano ya wafasiri wote (wa Qur'an) aya hii ilishuka kumuhusu Tha'alabah, ambaye alikataa kutoa zaka katika zama za Mtume **(s.a.w.w)**, hivyo basi fahamu kwamba Tha'alaba alizuwia kutoa zaka na akakataa kumpa Mtume **(s.a.w.w)** hiyo zaka, kwani aliipinga na akasema kuwa hiyo ni kodi. Bila shaka Mwenyezi Mungu ameshuhudia ndani ya aya hizi juu ya unafiki wake (huyu Tha'alabah), pamoja na hayo Mtume **(s.a.w.w)** hakumshambulia, na wala hakuchukua mali zake kwa nguvu na hali ya kuwa Mtume alikuwa na uwezo wa kufanya hivyo.

Ama Malik ibn Nuwairah na watu wake hawakuipinga zaka kama faradhi miongoni mwa faradhi za dini, bali walimpinga Khalifa alieukalia Ukhalifa baada ya Mtume **(s.a.w.w)** kwa nguvu na shinikizo na kuchukua (kwake)

nafasi hiyo. Hakika mambo ya Abubakr ni ya kushangaza mno, bwana huyu alikipuuza kitabu cha Mwenyezi Mungu, wakati bibi Fatmah alipotoa kitabuni humo hoja dhidi ya Abubakr, na akamsomea masikioni mwake aya zilizowazi kutoka ndani ya kitabu cha Mwenyezi Mungu ambacho kinathibitisha kurithiwa kwa Mitume, lakini Abubakr hakukubali na akazitengua aya zote kwa kutumia hadithi aliyoileta yeye ili kutimiza matamanio ya nafsi yake.

Na ikiwa yeye Abubakr anasema: "Hakika ninyi mnasimulia hadithi kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu na mnahitilafiana ndani ya hadithi hizo, na watu watakaokuja baada yenu watahitilafiana mno, basi msisimulie chochote kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, yeyote atakayekuulizeni mwambieni kati yetu na ninyi ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu, ihalalisheni halali yake na muiharamishe haramu yake." Iwapo haya ndiyo maneno yake, basi ni kwa nini yeye hakufanya kama asemavyo pale yeye na Binti ya Mtume **(s.a.w.w)** walipohitilafiana kuhusu ile hadithi ya Mtume isemayo kuwa: "**Sisi Manabii haturithiwi**." Bali mbona hakuhukumiana na Bibi Fatmah kwa mujibu wa kitabu cha Mwenyezi Mungu, ili apate kuihalalisha halali yake na kuiharamisha haramu yake? Jawabu liko wazi: Katika hali hiyo (lau angekubali) bila shaka angekikuta kitabu cha Mwenyezi Mungu kiko dhidi yake, na bibi Fatmah angepata ushindi katika madai yake dhidi ya Abubakr. Na kama siku hiyo bibi Fatmah angepata ushindi, basi huenda bibi Fatmah angekuja kumuuliza Abubakr kwa kutumia maneno ya Mtume kuhusu Ukhalifa wa Ibn ammi yake (Imam Ali), na hapo Abubakr asingeweza kumpinga, na kuhusu hali hii Mwenyezi Mungu anasema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لِمَ تَقُولُونَ مَا لَا تَفْعَلُونَ ﴿٢﴾ كَبُرَ مَقْتًا عِندَ اللَّـهِ أَن تَقُولُوا مَا لَا تَفْعَلُونَ ﴿٣﴾

"Enyi mlioamini mbona mnasema msiyoyatenda, ni jambo linalochukiza mbele ya Mwenyezi Mungu kusema msiyoyatenda. (Qur'ani,61:2-3).

Naam, kwa ajili ya yote hayo, Abubakr asingestarehe iwapo hadithi za Mtume **(s.a.w.w)** zingebakia zikisambaa miongoni mwa watu, na kupeana kutoka mji huu kwenda mji ule na hali ya kuwa ndani ya hadithi hizo yamo maelezo wazi yanayopingana na siasa ambazo dola yake ilisimama (kwa kupitia siasa hizo). Kwa hiyo hapakuwa na njia aliyoiona isipokuwa ni kuzikandamiza na kuzificha bali kuzifuta na kuzichoma moto hadithi (za Mtume **(s.a.w.w)**. Huyu hapa bibi Aisha binti yake Abubakr anashuhudia hilo dhidi ya Abubakr. anasema: "Baba yangu alizikusanya hadithi za Mtume wa Mwenyezi Mungu, zilikuwa hadithi mia tano akawa anazigeuza geuza, nikasema anazigeuza geuza kwa kuwa ana mashaka fulani yaliyomfikia? Basi kulipokucha akasema: Ewe binti yangu niletee hadithi ulizonazo, nikamletea, akazichoma moto."

Umar ibn Khatab anakuwa mkali zaidi kuliko mwenzake, dhidi ya wanaosimulia hadithi kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu na anawazuia watu kuzinakili hadithi. Bila shaka tumeona siasa ya Abubakar juu ya kuzuwia hadithi kiasi kwamba alifikia wakati akazichoma moto hadithi zilizokuwa zimekusanywa katika zama zake, na zilikuwa mia tano. Kufanya hivyo ni kwa kusudio la kwamba zisije zikaenea miongoni mwa

Masahaba na Waislamu wengineo ambao walikuwa na hamu kubwa ya kuifahamu sunna ya Mtume wao. Umar alipotawalia Ukhalifa kutokana na amri ya Abubakr, aliwajibika kuendeleza siasa ile ile, lakini kwa kutumia mfumo wake unaoeleweka ambao ni ukali na ususuavu. Hakuacha kuzuwia na kukataza kuandikwa hadithi na kuzitawanya tu, bali alionya na kukemea, kupiga na alitumia (njia ya) kuwadhibiti.

Ibn Majah ameeleza ndani ya Sunan yake katika juzuu ya kwanza Babut-tawaqqi fil-hadith amesema: "Imepokewa kutoka kwa Qurzah ibn Ka'ab kwamba Umar ibn Khatab alituma kwenda Kufah na akatushindikiza, alikwenda pamoja nasi mpaka mahala paitwapo Siraar akasema, Je, mnafahamu ni kwa nini nimetembea pamoja nanyi? Tukasema ni kwa ajili ya haki ya kusuhubiana kwako na Mtume wa Mwenyezi Mungu na ni kwa ajili ya haki ya Maansari. Umar akasema, Mimi nimetembea pamoja nanyi ili nipate kuwazungumzeni mazungumzo niliyotaka kukuzungumzeni. Nimekusudia kwa ajili ya mwendo wangu huu muyahifadhi mazungumzo hayo, bila shaka ninyi mtafika kwa watu ambao wanayo Qur'an vifuani mwao ikitingishika kama unavyotingishika mtungi wenye maji, watakapokuoneni watanyoosha shingo zao kwenu na watasema (hao ni) Masahaba wa Muhammad!! Basi punguzeni kuwapa riwaya zitokazo kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** kisha kwa jambo hili mimi nitakuwa pamoja nanyi." Basi Qur'zah ibn Ka'ab alipofika huko watu hao wakasema: Tusimulie, Akasema, Umar ametukataza."

Kama alivyoeleza Muslim ndani ya sahihi yake Kitabul-adab babul isti-idhaan kwamba: Umar alimuonya Abu Musa al-Ash'ari kwamba, angempiga kwa sababu ya kusimulia hadithi aliyoipokea kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**. Abusaid Al-khudri amesema: "Tulikuwa katika kikao kwa Ubayyi ibn Ka'ab, basi akaja Abu Mussa Al-ash'ar akasimama hali ya kuwa amekasirika akasema: Nakuapieni Mwenyezi Mungu hivi kuna yeyote miongoni mwenu aliyemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akisema, Kubisha hodi ni mara tatu ukikaribishwa (uingie) vinginevyo basi rudi."

Ubayyi akasema kuna nini (kimetokea)? (Abu'Musa) akasema nilibisha hodi kwa Umar ibn Khatab jana mara tatu lakini sikuitikiwa nikarudi, kisha leo nilimwendea nikaingia kwake na nikamwambia kwamba mimi jana nilikuja na nikasalimia mara tatu kisha nikaondoka, yeye akasema, Hakika tulikusikia lakini katika kipindi hicho sisi tulikuwa tumeshughulika, lau ungeendelea tu kubisha hodi mpaka tukukaribishe. Mimi nikamwambia nilibisha hodi kama taratibu ile niliyomsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (akifundisha). Basi Umar akasema (kuniambia) Wallahi nitaujeruhi mgongo wako na tumbo lako au vinginevyo uniletee watakaokushuhudia juu ya jambo hili (ulisemalo). Ubayyi ibn Ka'ab akasema, Wallahi hatosimama pamoja nawe isipokuwa aliye mdogo wetu kwa umri, simama ewe Abu Said, nikasimama nikamwendea Umar nikasema: Bila shaka nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akisema jambo hili." Naye Bukhari amelielezea tukio hili, lakini yeye kama kawaida yake amelikata na akaondosha maonyo ya Umar kuwa atampiga Abu Mussa Al-ash'ari, kama ilivyo desturi yake kutetea heshima ya Umar.

Pamoja na hayo, Muslim ndani ya sahihi yake ameongeza kauli ya Ubayyi ibn Ka'ab kumwambia Umar, "Ewe mwana wa Khatab usiwe

mwenye kuwaadhibu Masahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**." Naye Ad-dhahabi amepokea ndani ya Tadh-kiratul-huffaadh, katika juzuu ya kwanza ukurasa wa nne. Kutoka kwa Abu Salamah amesema: "Nilimwambia Abu Hurairah, Je, katika zama za Umar ulikuwa ukiyasimulia haya? (yaani hadithi za Mtume) akasema, Lau ningekuwa nasimulia katika zama za Umar kama ninavyokusimulieni Wallahi angenipiga kwa fimbo yake." Ni kama ambavyo Umar baada ya kuzuwia kusimulia hadithi na kuonya kumpiga atakayesimulia, pia yeye alichoma moto maandiko hadithi (za Mtume **s.a.w.w**). yaliyoandikwa na Masahaba.

Siku moja aliwahutubia watu akasema: "Enyi watu hakika imenifikia habari kwamba, kumeonekana mikononi mwenu vitabu, (mimi nasema), kitabu kipendezacho mbele ya Mwenyezi Mungu ni kile chenye uadilifu na sahihi, kwa hiyo asibakishe mmoja wenu kitabu chochote ila aniletee ili nitoe maoni yangu ndani ya kitabu hicho. Watu wakadhani kwamba yeye anataka kuvisahihisha ili pasiwe na kutofautiana ndani yake, wakamletea vitabu vyao, yeye akavichoma moto."[135] Ni kama alivyoandika ibn Abdilbarri ndani ya Kitabu jaami'i hayaanil-Ilmi wafadhlih kwamba, Umar ibn Khatab alitaka kuiandika Sunna ya Mtume **(s.a.w.w)** kisha ikamdhihirikia kuwa asiandike, na hatimaye akawaandikia kwenye miji (ya Kiislamu) kwamba, "Yeyote aliyemiliki chochote kile (katika sunna ya Mtume) basi na akifute." Na alipokuwa hana njia yoyote ile pamoja na kuonya kwake, kukemea kwake, kuzuwia kwake na kuvichoma moto vitabu vya hadithi, walibakia baadhi ya Masahaba wakihadithia waliyoyasikia kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** pindi wakutanapo na watu katika safari zao nje ya Madina kila wanapowauliza juu ya hadithi za Mtume **(s.a.w.w)**. Hapa ndipo Umar alipoona awafungie watu hawa mjini Madina na awawekee vizuwizi na akaimarisha ukandamizaji dhidi yao.

Amepokea ibn Is-haq kutoka kwa Abdur-rahman ibn Auf amesema: "Wallahi Umar hakufa mpaka pale alipokuwa amewatumia ujumbe kuwaita Masahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu akawakusanya kutoka sehemu mbali mbali, (na aliowakusanya walikuwa ni) Abdallah ibn Hudhaifah, Abud-dirdai, Abudharri Al-ghifari na U'qbah ibn Amir, Umar akawaambia: Imekuwaje ninyi mmezisambaza sehemu mbali mbali hizi hadithi za Mtume wa Mwenyezi Mungu" Wakamwambia: Je,unatukataza kufanya hivyo? Akasema: Hapana, lakini bakieni kwangu (hapa hapa Madina), naapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba, hamtaachana nami muda wote wa uhai wangu.[136] Kisha baada ya Umar alikuja Khalifa wa tatu Uthman ambaye alifuata nyayo zile zile na akipita pale alipotengenezewa na jamaa yake aliyetangulia, akapanda kwenye mimbari na akatangaza bayana aliposema: "Si halali kwa yeyote yule kuleta hadithi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** ambayo mimi sikuisikia katika zama za Abubakr na Umar.

Basi hivyo ndivyo ulivyoendelea udhibiti (dhidi ya hadithi za Mtume) kwa muda wote wa uhai wa Makhalifa hao watatu, na hicho kilikuwa ni kipindi cha miaka ishirini na tano, na laiti angalau udhibiti huo ungekuwa katika kipindi hicho peke yake lakini uliendelea baada ya hapo. Kwani alipokuja Muawiyah kwenye utawala, naye akapanda juu ya minbar akasema: "Ole wenu kusimulia hadithi, isipokuwa (simulieni hadithi) zilizokuwepo wakati wa Umar, kwani Umar alikuwa akiwakhofisha watu

kuhusu Mwenyezi Mungu Mtukufu." Hadithi hii ameiandika Muslim ndani ya sahih yake katika Kitabuz-zakati babun-nahyi anil-mas-allah juzuu ya tatu. Mwenendo wa Makhalifa wa Kibani Umayyah uko katika mfumo huu, wao walizuwia hadithi sahihi za Mtume na wakabobea katika fani ya kuzusha hadithi za uongo dhidi ya Mtume **(s.a.w.w)** kiasi kwamba, Waislamu leo hii wameingia ndani ya mtihani wakati wote kutokana na (balaa la) hadithi zinazopingana na uzushi ambao kabisa hauna uhusiano wowote na Uislamu.

Hebu angalia (mifano) aliyoinakili Al-madaini jidani ya kitabu chake kiitwacho, Al-ahdath amesema: "Muawiyah aliwaandikia watendaji wake (yaani magavana) makala moja baada tu ya mwaka ule wa jamaa (akasema ndani ya makala hiyo), "Simchukulii dhamana mtu yeyote atakayeeleza kitu chochote miongoni mwa fadhila za Abu Turab ( yaani Ali) na watu wa nyumba yake." Hapo ndipo makhatibu waliposimama kwenye mimbar katika kila mji (misikitini na sehemu nyinginezo) wakawa wanamlaani Ali (a.s) na kumtukana yeye na watu wa nyumba yake." Hatimaye Muawiyah aliwaandikia tena watendaji wake sehemu zote kwamba, wasikubali ushahidi wa yeyote miongoni mwa wafuasi wa Ali (a.s) na watu wa nyumba yake, akawaandikia akasema, "Waangalieni vema (muwatunze) wafuasi na wapenzi wa Uthman walioko kwenu, ambao wanamtawalisha (Uthman) na wale wanaosimulia fadhila zake na ubora wake, yasogeleeni makazi yao na muwasogeze karibu, muwakirimu na muniandikie kila kile akisimuliacho mtu miongoni mwao, jina lake na jina la baba yake na la ukoo wake."

Basi wakafanya hayo mpaka riwaya zinazohusu ubora na utukufu wa Uthman zikawa nyingi mno. Muawiyah alikuwa akiwapelekea (magavana wake) zawadi mbalimbali ikiwemo mavazi na kuwapa nyadhifa, na aligawa mali nyingi kuwapa Waarabu. Jambo hilo likaenea kwa wingi katika kila mji, na watu wakashindania vyeo na kuipata dunia, ikawa hawezi kuja mtu kwa hawa watendaji wa Muawiyah akarudishwa bure. Kwa ajili hiyo basi walikuwa wakisimulia fadhila na ubora wa Uthman, kisha (gavana) humwandika jina (mtu huyo) na humkaribisha vizuri halafu humzawadia. Hali hiyo ilibakia kwa muda fulani, kisha Muawiyah aliwaandikia watendaji wake akasema: "Hadithi juu ya Uthman zimeshakuwa nyingi na zimetapakaa kila mji na kila mahali, basi barua yangu itakapokufikieni watakeni watu wasimulie kuhusu ubora wa Masahaba na Makhalifa wa mwanzoni, na msiiache habari yoyote inayosimuliwa na Muislamu yeyote kuhusu Abu Turab isipokuwa leteni hadithi kinyume chake kuhusu Masahaba, kwani jambo hili mimi nalipendelea mno na ndiyo nipatapo utulivu na litazima hoja ya Abu Turab na wafuasi wake na litawavunja nguvu kutokana na fadhila za Uthman na utukufu wake (tulioutengeneza).

Barua zake zikasomwa mbele ya watu, na hapo ndipo zilipoanza kusimuliwa habari nyingi kuhusu Utukufu wa Masahaba, habari ambazo ni za kuzusha zisizokuwa na ukweli wowote, na watu walifanya kila juhudi kuleta riwaya zinazokubaliana na mtazamo huu mpaka wakapata umashuhuri kwa kuyataja hayo katika mimbar na yakapelekwa kwa waalimu wa vyuoni nao wakawasomesha vijana wao na watoto wao kiasi cha kuzipokea habari hizo na kuzisoma kama isomwavyo Qur'ani. Si hivyo tu bali wanawake wao, watumishi wao na jamaa zao nao waliishi katika

mazingira hayo kwa muda mrefu. Hatimaye Muawiyah aliandika nakala nyingine moja akaipeleka kwenye miji yote (akasema ndani ya nakala hiyo): "Muangalieni yeyote ambaye utathibiti ushahidi kwamba anampenda Ali na watu wa nyumba yake, basi mumfute jina lake ndani ya diwani (daftari) na muliondoshe pato lake na riziki yake." Kisha Muawiyah alifuatisha nakala nyingine tena akasema: "Yeyote mtakayemtuhumu kuwa anawatawalisha watu hawa (Ali na watu wa nyumba yake), muadhibuni adhabu (itakayokuwa ni fundisho kwa wengine) na muibomoe nyumba yake."

Balaa hili kubwa liliwakumba watu wa Iraqi na hasa mji wa Kufah, kiasi kwamba mtu yeyote katika wafuasi wa Imam Ali alikuwa akifikiwa na mtu hamuingizi ndani mpaka awe anamuamini na kumpa siri yake, na mtu akawa anamuogopa hata mtumishi wake na mtumwa wake, na hamsimulii chochote mpaka amuapishe kiapo kizito kuthibitisha kwamba atamfichia siri yake. Kipindi hiki zilidhihiri hadithi nyingi za uzushi na uongo na zikaenea, nao wanachuoni na maqadhi na watawala wakazikubali. Watu waovu mno juu ya balaa hili (katika kuenea kwake) ni wasomi wenye kujipendekeza (kwa watawala) na wanyonge ambao huonesha unyenyekevu na ucha Mungu, hawa walikuwa wakizitumia hadithi hizo ili wapate vyeo mbele ya watawala wao, na wapate kuyakaribia mabaraza ya watawala na wapate mali, mashamba na majumba kiasi kwamba hadithi hizo za uongo zikasambaa sana mbele za watu wa dini wasiojua uzushi na uongo, nao wakazikubali hadithi hizo na kuzieleza hali yakuwa wanadhani kuwa ni za kweli, na lau wangetambua kuwa siyo za kweli wasingezipokea wala wasingezitumia. Mimi nasema kwamba, jukumu la yote hayo linabebwa na Abubakr, Umar na Uthman, hawa ndiyo ambao walizuwia hadithi sahihi za Mtume wa Mwenyezi Mungu zisiandikwe kwa madai ya kuchelea kuchanganyikana Sunna na Qur'an. Huu ndiyo usemi wausemao wanaowatetea na kuwasaidia, na madai kama hayo yanamchekesha hata mwenda wazimu.

Na je, hivi Qur'ani na Sunna ni kama sukari na chumvi ambavyo vikichanganyika inakuwa hakuna uwezekano wa kukitenganisha kimoja wapo kutokana na mwenziwe na hata hiyo sukari na chumvi havichanganyikani kwani kila kimoja huhifadhiwa ndani ya kopo lake maalum. Je, Makhalifa hawa hawakutambua kuwa waiandike Qur'an ndani ya Msahafu wake na Sunna nayo waiandike ndani ya Kitabu chake maalum kama hali ilivyo kwetu leo hii.? Na tangu hadithi zilipoandikwa katika zama za Umar ibn Abdil-azizi (r.a), basi ni kwa nini Sunna na Qur'an hazikuchanganyikana pamoja wakati ambapo vitabu vya hadithi vinahesabika kwa mamia. Sahih Bukhari haikuchanganyikana na Sahihi Muslim, na hii nayo haikuchanganyikana na Mus-nad ya Ahmad wala Muwataa ya Imam Malik, sembuse Qur'an Tukufu ichanganyikane na Hadithi? Bila shaka hii ni hoja dhaifu mfano wa nyumba ya buibui haisimami kuwa ni dalili bali kinyume chake ndiyo dalili iliyo wazi.

Amepokea Az-zuhri kutoka kwa Ur-wah kwamba, Umar ibn Khatab alitaka kuandika Sunna (ya Mtume) akataka maoni ya Masahaba wa Mtume **(s.a.w.w)** wao wakamuelekeza kuwa aiandike. Basi Umar akawa anamuomba ushauri Mwenyezi Mungu kuhusu jambo hilo kwa kadiri ya mwezi mmoja, kisha siku moja alipoamka asubuhi akasema: "Hakika mimi

nilikuwa nataka kuiandika Sunna (ya Mtume **s.a.w.w**) nami nimekumbuka kwamba, watu waliokuwa kabla yenu waliandika vitabu kisha 'WakaVithamini mno wakakiacha kitabu cha Mwenyezi Mungu 'nami kwa hiyo Wallahi siwezi kamwe kukichanganya kitabu cha Mwenyezi Mungu na kitu chochote kile. Ewe msomaji ingalie riwaya hii, ni namna gani Masahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu walivyomuelekeza Umar kwamba aiandike Sunna ya (Mtume **s.a.w.w**) naye akawapinga wote na akayategemea maoni yake kwa madai eti watu waliokuwa kabla yao waliandika vitabu kisha wakavithamini mno na wakakiacha kitabu cha Mwenyezi Mungu. Basi kama ni hivyo, yako wapi basi madai ya kuwepo mashauriano (shuuraa) ambayo Masunni wanajivunia? Kisha wako wapi hao watu waliothamini vitabu vyao na kukiacha Kitabu cha Mwenyezi Mungu? Hatujapata kuwasikia watu hao isipokuwa kutoka katika mawazo ya Omar ibn Khat-tab. Hebu tukadirie kuwepo kwa watu hawa, lakini hatuna sababu ya kuwalinganisha kwani wao waliandika vitabu vyao wenyewe ili kukipotosha kitabu cha Mwenyezi Mungu, imekuja ndani ya Qur'an Tukufu kama ifuatavyo:

فَوَيْلٌ لِّلَّذِينَ يَكْتُبُونَ الْكِتَابَ بِأَيْدِيهِمْ ثُمَّ يَقُولُونَ هَـٰذَا مِنْ عِندِ اللَّـهِ لِيَشْتَرُوا بِهِ ثَمَنًا قَلِيلًا
فَوَيْلٌ لَّهُم مِّمَّا كَتَبَتْ أَيْدِيهِمْ وَوَيْلٌ لَّهُم مِّمَّا يَكْسِبُونَ ﴿٧٩﴾

"Adhabu kali itawapata wale wanaoandika kitabu kwa mikono yao kisha wakasema, Hiki kinatoka kwa Mwenyezi Mungu ili wapate thamani ndogo ya ulimwenguni, basi ole wao kwa yale iliyoyaandika mikono yao na ole wao kwa yale wayatendayo. (Qur'an, 2:79).

Ama kuziandika Sunna za Mtume sivyo kama hivyo, kwani zenyewe zinatokana na Nabii aliyehifadhiwa, ambaye hasemi kwa matamanio yake isipokuwa ni wahyi unaofunuliwa kwake, na hii Sunna ndiye mbainishaji na mfasiri.wa Kitabu cha Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu anasema:

بِالْبَيِّنَاتِ وَالزُّبُرِ ۗ وَأَنزَلْنَا إِلَيْكَ الذِّكْرَ لِتُبَيِّنَ لِلنَّاسِ مَا نُزِّلَ إِلَيْهِمْ وَلَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُونَ ﴿٤٤﴾

"Na tumekuteremshia mawaidha ili uwabainishie watu yaliyoteremshwa kwao." (Qur'an, 16:44).

Naye Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: "**Nimepewa-Qur'an na kilicho mfano wa Qur'an pamoja nayo.**" Jambo hili halipingiki kwa kila aliyeifahamu Qur'an, kwani ndani ya Qur'an hizo sala tano (kwa namna tunavyozisali), na zaka kwa viwango vyake, hukumu za saumu na hakumu za hijja na hukumu nyingine nyingi tu zote amezibainisha Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**, na kwa ajili ya yote haya Mwenyezi Mungu amesema: "Anachokupeni Mtume kichukueni, na anachokukatazeni kiacheni." Na amesema: "Waambie, ikiwa ninyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni Mwenyezi Mungu atakupendeni."

Ilikuwa jambo jema kwa Umar kufanya bidii ili apate kujifunza na kukifahamu kitabu cha Mwenyezi Mungu na kufuata maamrisho ya Mtume wala asingeyajadili na wala kuyakosoa. Na laiti Umar angekifahamu kitabu cha Mwenyezi Mungu na akafanya bidii kujifunza hukumu ya mirathi ya ndugu kwa upande wa mama ambayo Umar hakuifahamu mpaka akafariki, (lakini masikini hakufanya hivyo) na akahukumu katika zama za Ukhalifa wake kwa hukumu mbali mbali zinazopingana. Laiti angekifahamu Kitabu

cha Mwenyezi Mungu na akafanya bidii ili ajifunze hukumu ya kutayammamu ambayo hakuifahamu hata katika siku za Ukhalifa wake, bali alitoa fat-wa kwamba mtu ambaye hakupata maji asisali.

Na laiti Umar angekifahamu kitabu cha Mwenyezi Mungu na akafanya bidii ili ajifunze kutokana na kitabu hicho ile hukumu ya talaka kuwa ni mara mbili, basi imma kukaa kwa wema au kuachana kwa wema (lakini kwa kuwa hakujifunza) Umar akaifanya kuwa ni moja na akazipinga hukumu za Mwenyezi Mungu kwa maoni yake na ijtihadi yake, kisha hukumu za Mwenyezi Mungu akazitupilia mbali.

Ukweli uliopo ambao haukwepeki ni kwamba, Makhalifa (hao) walizuwia kuenea kwa hadithi (za Mtume) na wakamuonya yeyote anayezisimulia na kuziwekea vikwazo, kwani hadithi hizo zilikuwa zinaumbua mipango yao na njama zao, na walikuwa hawana njia ya kuziawili kama walivyoiawili Qur'ani, kwani Kitabu cha Mwenyezi Mungu kimebeba namna nyingi. Amma Sunna ya Mtume yenyewe ni maneno na vitendo vya Mtume **(s.a.w.w)** haiwezekani kwa mtu yeyote kuibadilisha, na ndiyo maana Amirul-muuminina Ali (a.s) alimwambia Ibn Abbas wakati alipomtuma aende akawatolee hoja Makhawariji (akasema): "Usijadiliane nao kwa Qur'an, kwani Qur'an imebeba mengi na namna nyingi, wewe utasema na wao watasema, lakini jadiliana nao kwa Sunna (ya Mtume) basi hapo hawatapata njia ya kukwepa.

15

# WAULIZE WANAOFAHAMU

## ABUBAKR ANAMPA UKHALIFA JAMAA YAKE UMAR, NA ANAKHALIFU MAANDIKOYALIYO WAZI KUHUSU JAMBO HILO

Amesema Imam Ali kuhusiana na suala la Ukhlifa: "Ama Wallahi ameuvaa (Ukhalifa) mtoto wa Abu Quhafa hali ya kwa anajua kabisa kwamba nafasi yangu katika huo Ukhalifa ni kama nafasi ya mpini ulioko kwenye jiwe la kusagia nafaka." Akielezea kwa njia ya kinaya Imamu (a.s) anasema: "Hububujika kutoka kwangu fadhila kwa vile Mungu alinienzi kwa kuniweka karibu na materemkio ya wahyi, hivyo basi nilijizuia nikakaa mbali nao, nikawa nafikiri kati ya kuingia vitani hali nikiwa mikono mitupu, au nivute subira katika giza lililoshona hakika mtu mzima huzeeka, na mtoto huwa kijana. Muumini atataabika kwa juhudi kubwa kubakia na imani safi katika hali hiyo mpaka akutane na Mola wake." Anaendelea kusema, "Niliona kusubiri ni bora na ni hekima, basi nikasubiri hali katika macho kuna tongo tongo na shingoni kuna mwiba umenasa, naouna urithi wangu nimenyang'anywa. Wa kwanza akaenda kisha akampasia mtoto wa Khatab baada yake, ajabu ilioje kwamba yeye (Abubakr) alitaka kujitoa katika ukhalifa alipokuwa hai na ampasie mwenzake ashike baada ya kifo chake ili kudhibiti walichokigawa nusu mbili, kila mmoja akawa mgumu hagusiki na anajikwaakwaa akitaka udhuru."

Kila mwenye kuhakiki na kutafiti atafahamu kwamba, Mtume wa Mwenyezi Mungu aliutangaza ukhalifa na kumbainisha Ali ibn Abi Talib kabla ya kufa kwake kama ambavyo. wengi wa Masahaba wanalifahamu hilo na wakitanguliwa na Abubakr na Umar. Na ndiyo maana Imam Ali alikuwa akisema. "Hakika yeye anajua kabisa kwamba, nafasi yangu katika huo ukhalifa ni kama nafasi ya mpini ulioko kwenye jiwe la kusagia." Na huenda hilo ndilo lililowafanya Abubakr na Umar wazuwie kusimuliwa hadithi za Mtume **(s.a.w.w)** kama tulivyotangulia kueleza katika mlango uliopita, na wakashikamana na Qur'an kwa kuwa Qur'an japokuwa ndani yake (imo) aya ya Wilayah lakini jina la Ali halikutajwa wazi wazi kama ilivyo ndani ya hadithi za Mtume kwa mfano Mtume **(s.a.w.w)** aliposema "'Yeyote ambaye mimi nilikuwa mtawala wake, basi huyu Ali ni mtawala wake." Na alisema Mtume: "**Ali anatokana nami, nami natokana naye, naye ni mtawala wa kila muumini baada yangu**."

Na kwa ajili hiyo tunafahamu kiwango cha mafanikio ya sera aliyoiandaa Abubakr na Umar katika kuzuwia na kuchoma moto hadithi za Mtume **(s.a.w.w)**, na wakaweka vizibo juu ya vinywa ili Masahaba wasizizungumze hadithi hizo kama tulivyotangulia kueleza ndani ya riwaya ya Qurdhah ibn Ka'ab. Vizuizi hivyo viliendelea kwa robo karne ambao ni muda wa utawala wa Makhalifa watatu hadi pale alipokuja Imam Ali kwenye Ukhalifah akawashuhudisha Masahaba ile hadithi ya Ghadir.

Masahaba thelathini walishuhudia, kumi na saba miongoni mwao ni katika wale waliopigana vita ya Badri. Hii dalili wazi inayoonesha kwamba, Masahaba hawa thelathini wasingeweza kuzungumza hivyo lau kama Amirul-Muuminina Ali asingewataka kufanya hivyo, na lau Ali asingekuwa

Khalifa na ameshika nguvu za utawala, basi woga ungewafanya wakakaa chini kimya wasishuhudie hilo kama yalivyotokea hayo kwa vitendo kutoka miongoni mwa baadhi ya Masahaba ambao hofu na husuda iliwakalisha chini wasishuhudie. Mfano wa hao ni Anas ibn Malik, Bar-raa ibn Azib, Zaid ibn Ar-qam na Jarir ibn Abdillah Al-bajali. Kwa tendo lao hilo la kunyamaza waliwapatwa na madhara makubwa kutokana na dua ya Imam Ali ibn Abi Talib. Na wala Abu Turab (Imam Ali [a.s]) hakuneemeka na Ukhalifa huo kwani siku zake zote zilikuwa ni mitihani, fitina, njama na vita dhidi yake vilivyoelekezwa kwake kutoka kila pande. Zilijitokeza zile chuki na mafundo ya zama za Badri, Hunain na Khaibar, mpaka alipouawa kishahidi nahizo Sunna za Mtume hazikupata sikio lenye kuzisikiliza mbele ya hao waliotengua na kuvunja viapo vyao, bali walitoka katika dini na ni waongo (waliotumia dini kwa maslahi yao) ambao walikwisha zowea kutenda maovu, rushwa na kuipenda dunia katika zama za Ukhalifa wa Uthman. Kwa ajili hiyo mwana wa Abu Talib hakuweza kurekebisha maovu yaliyotendwa kwa robo karne katika muda wa miaka mitatu na minne ila kwa kuiangamiza nafsi yake, na haiwezekani yeye kuiangamiza nafsi yake kwani yeye anasema:

"Wallahi mimi nafahamu mno ni kitu gani kitakachowafanyeni muwe wema, lakini siwezi kukurekebisheni kwa kuiangamiza nafsi yangu." Na haukupita muda mrefu isipokuwa Muawiyah ibn Abi Sufiyan aliukalia ukhalifa, akaziendeleza sera zile kama tulivyotangulia kusema, akazuwia hadithi isipokuwa zile zilizokuwepo zama za Umar. Yeye alikwenda mbele zaidi kuliko hivyo, akateua kikundi miongoni mwa Masahaba na Tabiina ili waweke hadithi (za uzushi) na hapo ndipo Sunna ya Mtume **(s.a.w.w)** ikapotea ndani ya bahari hiyo kubwa ya hadithi za uzushi ziliundwa, na ngano zinazohusu fadhila za Masahaba. Baada ya hapo Waislamu wakaendelea hivyo kwa karne nzima wakiwa ndani ya sunna za Muawiyah na zikawa ndizo zinazofuatwa na Waislamu wote. Tunaposema sunna za Muawiyah, maana yake ni sunna aliyoiridhia Muawiyah miongoni mwa matendo ya Makhalifa watatu, Abubakr, Umar na Uthman na yale aliyoyaongeza yeye na wafuasi wake miongoni mwa uzushi na uongo, ikwemo kumlaani na kumtukana Imam Ali na watu wa nyumba yake na wafuasi wake miongoni mwa Masahaba wema.

Kwa sababu hiyo basi, ninarudia kukariri kwamba,"Abubakr na Omar walifanikiwa katika sera hii ya kufuta sunna ya Mtume kwa madai ya kuirejea Qur'an." Bila shaka utaona leo hii baada ya kupita karne kumi na nne, pale utakapotoa hoja kwa sunna madhubuti ya Mtume kuthibitisha kwamba, Mtume **(s.a.w.w)** alimbainisha Ali kuwa ndiyo khalifa wake, hapo hapo utaambiwa, "Achana na sunna ya Mtume ambayo ndani yake kunahitilafu nyingi, kinatutosha kitabu cha Mwenyezi Mungu na kitabu cha Mwenyezi Mungu hakikutaja kwamba Ali ndiyo khalifa wa Mtume bali kimesema kuwa, mambo ya Waislamu yanakwenda kwa kushauriana."

Na hii ndiyo hoja yao, kwani sijazungumza na yeyote miongoni mwa wanachuoni wa Kisunni isipokuwa, Shuraa ndicho kitambulisho chao na ndiyo mila yao. Pamoja na kwamba ukhalifa wa Abubakr ulitimia bila kutegemewa, na eti Mwenyezi Mungu aliwakinga Waislamu kutokana na shari, lakini cha ajabu ni kwamba haukupatikana kwa kushauriana kama

wanavyodai baadhi yao, bali ulipatikana kwa ghafla na tena kwa nguvu, shinikizo na vitisho, na wengi miongoni mwa Masahaba bora waliupinga wakiongozwa na Imam Ali ibn Abi Talib, Sa'ad ibn Ubbadah, Ammar ibn Yasir, Salman, Miqadad, Zubair, Abbas na wasiokuwa hawa kama walivyoeleza wanahistoria wengi waliozungumzia tukio hili.

Hebu tulipuuze tukio hili na tuone Abubakr alivyomtawaza Umar baada yake na tuwaulize Masunni ambao wanategemea msingi wa mashauriano. Je, ni kwa nini Abubakr alimbainisha Umar kuwa khalifa wake na akawalazimisha Waislamu wakubali bila ya kuwaachia washauriane kati yao kama mnavyodai? Ili ikubainikie zaidi, na kama ilivyo kawaida yetu kwamba hatutoi ushahidi isipokuwa kwa kutumia vitabu vya Masunni, sasa namletea msomaji namna Abubakr alivyomtawalisha jamaa yake. Ibn Qutaibah ameandika ndani ya kitabu chake; Tarikhul-khulafai katika mlango unaohusu maradhi ya Abubakr na kumtawaza kwake Umar (r.a) amesema: ...Kisha akamuita Uthman ibn Affan akamwambia: "Andika usia wangu." Akamtamki na Uthman akaandika; "Bismillahir-Rahmanir-Rahiim, huu ndiyo usia aliousia Abubakr ibn Abi Quhafah mwishoni mwa uhai wake duniani hali yakuwa anaondoka, na ni mwanzoni mwa uhai wake wa akhera akiwa ndiyo anaingia ndani yake. Hakika mimi nimemtawalisha juu yenu Umar ibn Khatab, iwapo mtamuona kuwa ni muadilifu miongoni mwenu basi hiyo ndiyo dhana yangu kwake na ndiyo matarajio yangu ndani yake, na iwapo atabadili na kugeuza mimi nilichokikusudia ni kheri na sijui ghaibu na hivi karibuni watajuwa wale waliodhulumu ni mgeuko gani watakaogeuka." Kisha akaufunga waraka huo na akampa.

Muhajirina na Ansari wakaingia kwake waliposikia kwamba yeye Abubakr amemtawalisha Umar wakasema: "Tunakuona umemtawalisha Umar juu yetu na bila shaka wewe unamfahamu na unaujua ukali wake kwetu sisi hali yakuwa wewe uko nasi basi itakuwaje utakapotoweka nawe utakutana na Mwenyezi Mungu na atakuuliza, sasa utasemaje?" Abubakr akasema: "Ikiwa Mola wangu ataniuliza bila shaka. nitasema kuwa, nimemtawalisha juu yao mtu ambaye ni mbora wao katika nafsi yangu. Kuna baadhi ya wanahistoria kama vile Tabari na Ibnul-athir wanaeleza kwamba, Abubakr alipomuita Uthman ili aandike usia wake, alizimia wakati akimtamkia, basi Uthman akaliandika jina la Umar ibn Khatab.

Alipozindukana akasema soma uliyoyaandika, akasoma na akataja jina la Umar, basi Abubakr akasema: "llikuwaje ukafanya hivi?" Uthmani akasema, "Hukuwa ni mwenye kumvuka Umar." Abubakr akasema, "Umepatia." Alipomaliza kuandika watu fulani miongoni mwa Masahaba waliingia kwa Abubakr, akiwemo Tal-ha na akamwambia Abubakr, "Utasema nini kwa Mola wako kesho nawe umekwisha mtawalisha juu yetu mtu mkali na msusuavu, nafsi za watu zitatawanyika na nyoyo zitamkimbia." Abubakr akasema: "Niegemesheni." alikuwa kalala, wakamuegemesha, akamwambia Tal-ha, "Hivi unanikhofisha Mwenyezi Mungu atakaponiuliza jambo hilo kesho? Nitamwambia kuwa, nilimtawalisha juu yao mbora wa watu wako.

Na ikiwa wanahistoria wanaafikiana juu ya Abubakr kumtawalisha Umar bila ya kuwashauri Masahaba, basi tunaweza kabisa kusema kwamba, "Yeye alimtawalisha Umar bila ridhaa ya Masahaba na hali ya kuwa

wamekasirika." Na ni sawa sawa Ibn Qutaibah aliposema kuwa, Muhajirina na Ansari waliingia kwa Abubakar wakambwambia: "Bila shaka wewe unafahamu ukali wake kwetu sisi." Au kama alivyosema Tabari kwamba, "Waliingia kwa Abubakar watu fulani miongoni mwa Masahaba akiwemo Tal-ha na akamwambia Abubakr, "Utasema nini kwa Mola wako kesho wakati wewe umemtawalisha juu yetu mtu mkali na msusuavu, nafsi za watu zitatawanyika na nyoyo zitamkimbia." Basi matokeo yake ni ya aina moja nayo ni kwamba mambo ya Masahaba hayakuwa ya mashauriano na hawakuwa wameridhia kutawalishwa Umar, jambo hilo alililazimisha Abubakr bila ya kuwashauri.

Kilichotokeo kile kile ambacho Imam Ali (a.s) alikizungumza wakati alipolazimishwa na Umar ibn Khatab kumbai Abubakr ambapo Imam Ali alisema, "Mnufaishe leo hii naye kesho atakurudishia." Hali hii moja kwa moja ndiyo ile aliyoisema mmoja wa Masahaba kumwambia Umar ibn Khatab pale alipotoka na ile barua ambayo ndani yake umo usia wa ukhalifa, yule Sahaba akamwambia, "Ewe Baba Hafsi kuna nini humo ndani ya barua hiyo?" Umar akasema: "Sifahamu, lakini mimi nitakuwa wa kwanza kusikiliza na kuitii." Basi yule mtu akasema: "Lakini mimi Wallahi najua kilichomo, wewe ulimtawalisha kipindi kilichopita basi na yeye amekutawalisha mwaka huu." Hii inatubainikia wazi kwamba, hapana shaka ndani yake kuwa, ule msingi wa Shuraa (mashauriano) ambao Masunni wanaupigia ngoma, hauna maana kwa Abubakr na Umar au kwa maelezo mengine ni kwamba Abubakr ndiyo wa kwanza kuubomoa msingi huu na kuupuuza na kufungua mlango kwa watawala wa Kibanu Umayyah waurudishe kuwa ni Ufalme wa Kaisari.

Watoto wanarithiana na baba zao, na vile vile ndiyo walivyofanya Banu Abbas baada ya Banu Umayyah, na hiyo nadharia ya Shuraa ikabaki kuwa ni ndoto inayowadanganya Masunni, haikuthibitika hapo zamani na wala haitathibitika. Jambo hili linanikumbusha mazungumzo yaliyofanyika kati yangu na mwanachuoni fulani miongoni mwa wanachuoni wa Kiwahabi kutoka Saudia ndani ya Msikiti mmoja mjini Nairobi Kenya. Mazungumzo yetu yalihusu utata wa ukhalifa, nami nilikuwa nikitetea maandiko yanayohusu ukhalifa na kwamba jukumu lote (la kuteua khalifa) ni la Mwenyezi Mungu na huliweka mahala atakapo na watu hawana hiyari na hawawezi kuliingilia jambo hilo.

Amma Mwanachuoni huyo yeye alikuwa akitetea shuraa kwa nguvu zote na pembeni yake lilikuwepo kundi la wanafunzi ambao wanachukua elimu kwake na wakimuunga mkono katika kila alisemalo kwa madai kwamba hoja zake ni kutoka ndani ya Qur'an Tukufu, kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu anamwambia Mtume wake **(s.a.w.w)**: "**Washauri katika jambo**." Na anasema tena: "**Na jambo lao ni kushauriana kati yao**." Niligundua ya kwamba mimi ninashinikizwa na jamaa kwa kuwa wao wamejifunza kutoka kwa waalimu zao fikra zote za Kiwahabi, kama nilifahamu pia kwamba, wao hawawezi kukubali kusikiliza hadithi sahihi na wanang'ang'ania baadhi ya hadithi walizozihifadhi na nyingi ya hizo ni hadithi zilizozushwa (na kusingiziwa kuwa Mtume alisema hivyo) basi hapo nilikubaliana na msingi wa Shuraa nikawaambia wanafunzi hao na waalimu wao kama ifuatavyo: "Je, hivi ninyi mnaweza kuitosheleza serikali ya Mtukufu Mfalme (wa

Saudia) juu ya msingi wa Shuraa ulioko kwenu mpaka (Mfalme), ajiondoe kwenye utawala wake na afuate viongozi wenu bora waliopita na awaachie Waislamu hilo bara Arabu likiwa na uhuru wa kuchagua kiongozi wao? Mimi sidhani kama (Mfalme huyo) atafanya hivyo, kwani baba zake na babu zake hawakumiliki ukhalifa peke yake bali bara Arabu nzima pia imekuwa ni milki yao mpaka ardhi yote ya Hijazi wakaipa jina la Mamlaka ya Saudia.

Basi hapo ndipo aliposema mwanachuoni wao mkuu kuwa: "Sisi hatujishughulishi na mambo ya kisiasa, sisi tumo ndani ya nyumba ya Mwenyezi Mungu ambayo ameamuru litajwe jina lake na paswaliwe ndani yake. Mimi nikasema: "Je, hali hiyo hata kwa msomi mwenye maarifa?" akasema: "Ndiyo, sisi hapa tunawafunza namna hiyo vijana. Mimi nikasema: "Sisi tulikuwa katika uchambuzi wa kielimu." Akasema: "Bila shaka wewe ndiwe uliyeuharibu (uchambuzi huo) kwa kuingiza mambo ya siasa" Basi nilitoka hapo pamoja na niliokuwa nimefuatana nao hali ya kuwa ninawasikitikia vijana wa Kiislamu ambao uwahabi umetawala fikra zao kwa kila namna mpaka wakawa ni maadui wa wazazi wao. Wazazi wao wote ni watu wanaofuata madhehebu ya Shafii, madhehebu ambayo yako karibu mno na madhehebu ya watu wa nyumba ya Mtume kama ninavyoamini mimi, (kwani hapo kabla) Masheikh walikuwa na heshima na utulivu mbele ya wasomi na wasiokuwa wasomi hasa kwa kuzingatia kwamba wengi wa Masheikh hao ni Masharifu wanatokana na kizazi kitukufu, basi hatimaye wakaja Mawahabi wakawashinikiza vijana kutokana na ufakiri wao na wakawahadaa kwa mali na nyenzo za maisha. Wakaugeuza mtazamo wao (kwa kuwaambia) kuwa wayatendayo ikiwa ni pamoja na kuwaheshimu Masharifu ni kumshirikisha Mwenyezi Mungu kwani (heshima hiyo waifanyayo) ni kumtukuza kiumbe. Basi hapo ndipo watoto hawa wakawa ni kero na balaa kwa baba zao, na hali kama hii kwa bahati mbaya ndiyo inayotokea katika miji mingi ya Kiislamu katika Afrika.

Hebu na turejee kwenye kifo cha Abubakr, kwani tunamkuta kabla ya kufa kwake anajuta kwa yale aliyoyatenda. Ibn Qutaibah ameandika ndani ya kitabu chake kiitwacho, Tarikhul-khulafai kauli ya Abubakr anasema: "Naam yamenifika, Wallahi sijuti isipokuwa kwa sababu ya mambo matatu niliyoyafanya, lau ningeyaacha mambo hayo nisiyafanye, Laiti mimi ningeiacha nyumba ya Ali, mapokezi mengine yanasema, Laiti nisingeifedhehesha nyumba ya Fatimah kwa jambo lolote lile japokuwa walikuwa wametangaza vita dhidi yangu, na laiti mimi ile siku ya Saqifah ya Bani Saidah ningeweka (mkono wangu) ndani ya mkono wa mmoja wao kati ya watu wawili, Abu Ubaidah au Umar akawa yeye ndiyo amir nami nikawa waziri, na laiti mimi pale o nilipoletewa Dhil-fujaat as-Sulami hali ya kuwa yu mateka, basi bora ningemuuwa kwa kumchinja au ningemuachia huru na nisinge mchoma moto.

Nasi tunaongezea hapo tunasema, "Laiti ewe Abubakr usingemdhulumu' bibi Fatmah na wala usingemuudhi na usingemkasirisha, na laiti wewe ungejutia kabla ya kufa kwake na umridhishe, hayo yanaihusu nyumba ya Ali uliyoifedhehesha na ukaruhusu ichomwe moto." Ama kuhusu ukhalifa, basi laiti wewe ungewaacha jamaa zako ambao ndiyo nguzo zako (yaani) Abu-ubaidah na Umar na ukaweka mkono wako ndani ya mkono wa

muhusika wake kisheria ambaye alitawalishwa na Mtume akawa yeye ndiye Amir!! Kwa kufanya hivyo ulimwengu huu tunao ushuhudia leo hii usingekuwa hivi, na dini ya Mwenyezi Mungu ingekuwa ndiyo inayoongoza ulimwengu kama alivyoahidi Mwenyezi Mungu na ahadi ya Mwenyezi ni ya kweli. Ama kumuhusu Al-fujat as-Sulami uliyemchoma moto sisi tunakwambia, "Basi laiti wewe usingezichoma moto Sunna za Mtume ambazo ulizikusanya, hapana shaka ungejifunza mengi kutokana nazo kuhusu hukumu za sheria zilizosahihi na wala usingetegemea jitihada ya maoni yako.

Na mwisho, tunakwambia ukiwa juu ya kitanda cha mauti "Laiti wewe ulipofikiria juu ya kuacha ukhalifa, ungelirejesha haki (hiyo) mahala pake kwa yule ambaye mahali pake katika ukhalifa ni sawa na mahali pa mpini wa jiwe la kusagia nafaka." Na wewe unafahamu mno kuliko watu wengine juu ya ubora wake, ucha Mungu wake, elimu yake na kwamba yeye alikuwa kama nafsi ya Mtume **(s.a.w.w)** na hasa kwamba yeye alikuachia jambo hilo na hakukupinga (yote hayo akikusudia) usalama wa Uislamu. Basi kwako kulikuwa na uhuru wa kuupa nasaha umma wa Muhammad **(s.a.w.w)** na uchagulie mtu ambaye atautengenezea mambo yake na kuuweka pamoja na akaufikisha kwenye kilele cha mafanikio. Na tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu akusamehe madhambi yako na amridhishe bibi Fatmah, baba yake, mumewe na wanawe, kwani wewe ulimkasirisha (binti ya Mtume) aliye sehemu ya mwili wa Mtume na Mwenyezi Mungu hukasirika kwa ajili ya kukasirika kwake na huwa radhi kwa kuwa radhi kwake, kama ambavyo mwenye kumuudhi Fatmah basi hakika huwa kamuudhi Baba yake kwa mujibu wa hadithi ya Mtume **(s.a.w.w)**, na Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: "Wale wanaomuudhi Mtume wa Mwenyezi Mungu, watapata adhabu kali."

Nasi tunajilinda kwa Mwenyezi Mungu kutokana na ghadhabu za Mwenyezi Mungu, na tunamuomba aturidhie sisi na Waislamu wote wa kiume na wa kike na waumini wote wa kiume na wa kike. Umar ibn Khattab anakipinga Kitabu cha Mwenyezi Mungu kwa kutumia ij tihadi yake Bila shaka khalifa wa pili anayo historia iliyojaa jitihada yake dhidi ya aya za Qur'ani tukufu zilizo wazi na Sunna tukufu ya Mtume. Masunni wanakifanya kitendo hicho (cha Umar) kuwa ni miongoni mwa sifa zake ambazo kwazo humsifia na miongoni mwao hujaribu kumtakia udhuru na kuleta taawili za kimya kimya ambazo hazikubaliki kiakili wala mantiki.

Vinginevyo basi ni vipi atakuwa yule mtu anayekipinga kitabu cha Mwenyezi Mungu na sunna ya Mtume wake kuwa yeye ni miongoni mwa Muj-tahidina, na hali Mwenyezi Mungu anasema:

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللَّـهُ وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَن يَكُونَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ ۗ وَمَن يَعْصِ اللَّـهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالًا مُّبِينًا ﴿٣٦﴾

"Haiwi kwa muumini mwanaume au muumini mwanamke, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapokata shauri wawe na hiyari katika shauri lao, na yeyote mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake hakika amepotea upotofu ulio wazi kabisa." (Qur'an, 33:36)

Na amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَمَن لَّمْ يَحْكُم بِمَا أَنزَلَ اللَّـهُ فَأُولَـٰئِكَ هُمُ الْكَافِرُونَ ﴿٤٤﴾ وَمَن لَّمْ يَحْكُم بِمَا أَنزَلَ اللَّـهُ
فَأُولَـٰئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٤٥﴾

"Na wasiyohukumu kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndiyo makafiri, na wasiyohukumu kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndiyo madhalimu, na wasiohukumu kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu basi hao ndio mafasiq (waovu)..." (Qur'an, 5:44, 45, na 47).

Bukhari ameandika ndani ya sahihi yake, Kitabul-i'tisami bil-kitab was-sunnah, mlango wa kushutumu maoni binafsi na kujitwika mzigo wa kiasi, usifuate, usiseme usiyoyajua kwamba, Mtume **(s.a.w.w)** amesema: "**Kamwe Mwenyezi Mungu haiondoi elimu baada ya kuwapa, lakini huiondoa kutoka kwao kwa kuwafisha wanachuoni pamoja na elimu yao, basi watabakia watu wajinga watakapoulizwa nao watajibu kwa mujibu wa maoni yao, hivyo watawapoteza wengine nao watapotea**."

Kama alivyoandika tena Bukhari ndani ya sahihi yake katika kitabu kile kile ndani ya mlango unaofuatia: Mtume **(s.a.w.w)** alikuwa haulizwi yale ambayo hajateremshiwa wahyi kuhusiana nayo isipokuwa husema kuwa sijuwi. Alikuwa hatoi jawabu mpaka ateremshiwe wahyi, na wala hakusema kwa maoni (yake) wala kwa kukisia, na hiyo ni kwa sababu ya kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo: "Kwa yale aliyokufunulia Mwenyezi Mungu (ndiyo uyaseme)." Na wamekwisha sema wanachuoni wa hapo kale na wa sasa hivi kwamba: "Yeyote atakayesema (lolote) kuhusu kitabu cha Mwenyezi Mungu kwa kutumia maoni yake basi bila shaka atakuwa amekufuru." Na hii bila shaka ni kuhusu aya ambazo ni muhkam na ni kuhusu kauli na matendo ya Mtume **(s.a.w.w)**. Basi ni vipi kanuni hii husahauliwa pale jambo linapohusishwa na Umar ibn Khattab au mmoja wa Masahaba au mmoja wa Maimamu wa Madhehebu manne? Inakuwaje kauli (itolewayo na hao) kwa maoni yao ikipingana na hukumu za Mwenyezi Mungu iitwe Ijtihadi ambayo mtu hupata thawabu moja kwa kufanya ijitihadi hiyo endapo atakosea, na akipatia atapata thawabu mbili? Huenda msemaji fulani akasema kuwa: "Jambo hili (la kufanya ijtihadi) umma wote wa Kiislamu Masunni na Mashia umekubaliana kutokana na hadithi ya Mtume Mtukufu ipatikanayo kwao."

Mimi nasema: "Jambo hili ni sawa, lakini wametofautiana ni mahali gani panapofaa kufanya hiyo ijtihadi, kwani Mashia wanawajibisha ijtihadi katika mambo ambayo haikuja hukumu ya wazi toka kwa Mwenyezi Mungu wala kwa Mtume wake **(s.a.w.w)** kuyahusu mambo hayo. Ama Masunni wao hawajilazimishi katika ijtihadi kwa namna hii. na kwa kuwafuata Makhalifa na viongozi wao, hawaoni ubaya kujitahidi dhidi ya maandiko (ya Qur'an wala hadithi sahihi), na bila shaka mwanachuoni mkubwa Sayyid Sharafud-din Al-musawi ameandika ndani ya kitabu chake kiitwacho, An-nassu wal-ij-tihad zaidi ya maeneo mia moja ambayo Masahaba wakiongozwa na Makhalifa watatu wa mwanzo walikwenda kinyume cha maandiko ya Qur'an na Surma zilizo wazi, basi ni juu ya wachunguzi kukisoma kitabu hicho (ili kupata ukweli huo), Na maadamu tunaichambua maudhui hii kikweli kweli, basi hatuna budi kuleta baadhi ya maandiko aliyoyakhalifu Umar ibn Khattab, na hilo imma alilifanya kwa kutoyajua

maagizo hayo, na ni jambo la ajabu kwani mjinga hawezi kuhukumu akahalalisha na kuharamisha yeye mwenyewe. Mwenyezi Mungu anasema:

وَلَا تَقُولُوا لِمَا تَصِفُ أَلْسِنَتُكُمُ الْكَذِبَ هَـٰذَا حَلَالٌ وَهَـٰذَا حَرَامٌ لِّتَفْتَرُوا عَلَى اللَّـهِ الْكَذِبَ إِنَّ الَّذِينَ يَفْتَرُونَ عَلَى اللَّـهِ الْكَذِبَ لَا يُفْلِحُونَ ﴿١١٦﴾

"Na wala msiseme kwa sababu ya uongo usemwao na ndimi zenu (kwamba) hii ni halali na hii ni haramu, msije mkamzulia Mwenyezi Mungu uwongo, hakika wale wamzuliao Mwenyezi Mungu uongo hawatafaulu." (Qur'ani 16:116).

Wala mjinga hawezi kusimama kwenye cheo cha Ukhalifa kwa ajili ya kuongoza umma kikamilifu. Mwenyezi Mungu anasema:

أَفَمَن يَهْدِي إِلَى الْحَقِّ أَحَقُّ أَن يُتَّبَعَ أَمَّن لَّا يَهِدِّي إِلَّا أَن يُهْدَىٰ فَمَا لَكُمْ كَيْفَ تَحْكُمُونَ ﴿٣٥﴾

"Basi je, aongozaye katika haki siye anayestahiki zaidi kufuatwa au (anastahiki) yule asiyeongoka (yeye mwenyewe) isipokuwa aongozwe? Basi mukoje ninyi, ni vipi mnavyohukumu?" (Qur'an, 10:35).

Na imma Umar siyo kwamba hayajui maandiko bali anayajua, lakini alifanya ij-tihadi kwa makusudi kwa maslahi fulani na hali fulani iliyolazimika kwa mujibu wa maoni yake binafsi. Jambo hili Masunni hawalichukulii kuwa ni kufru na ni kutoka katika dini, kama itakuwa hapana budi (yeye Umar) alikuwa hakutambua kuwepo kwa watu wanaozifahamu vyema hukumu miongoni mwa watu aliokuwa nao katika zama zake, na hii siyo kweli kwa sababu ya kutambua kwake Umar kwamba, Ali (a.s) alikuwa akikijua vyema Kitabu (cha Mwenyezi Mungu) na Sunna. Na kama si hivyo basi asingemuuliza maswali mengi magumu mpaka akafikia kusema juu ya Ali, "Lau kama siyo Ali, Umar angeangamia." Sasa basi ni kwa nini hakumuuliza juu ya mas-ala aliyojitahidi ndani yake kwa kutumia maoni yake ambayo anatambua kwamba yeye hayafahamu?

Mimi naamini kwamba, Waislamu waliohuru watakubaliana na hili, kwani aina ya ijtihadi kama hii ndiyo iliyoharibu itikadi ya Kiislamu, na ikaharibu hukumu, ikazipoteza na kusababisha wanachuoni wa umma huu wahitilafiane na kuwagawa makundi na madhehebu mengi. Kwa ajili hiyo kukawa na ugomvi na uhasama, na ndipo kulipotokea kushindwa kwa Waislamu na nguvu zao zikatoweka, wakabakia nyuma kiroho na kimazingira. Tunayo haki ya kuangalia hata kule kuwako kwa Abubakr na Umar juu ya kiti cha Ukhalifa na kumuondoa kwao muhusika wake kisheria. Sisi tunafikiria lau Abubakr na Umar wangezikusanya Sunna za Mtume na wakazihifadhi ndani ya kitabu makhususi, basi wangejichumia kheri nyingi mno wenyewe binafsi na juu ya umma na wala kusingeingia ndani ya Sunna ya Mtume yasiyokuwemo, na Uislamu kwa Kitabu chake (Qur'an) na Sunna yake, ungekuwa kitu kimoja, mila moja na umma mmoja wenye itikadi moja, na leo hii mazungumzo yetu yasingekuwa haya. Ama ilivyokuwa kwamba Sunna zilikusanywa kisha zikachomwa moto, zikazuiwa kuandikwa na kunakiliwa japo kwa mdomo, basi huu ndiyo msiba mkubwa na hili ndilo balaa kubwa lililotupata. Lahaula wala quwwata Ilia billahil-aliyyil-adhim.

Hebu yaangalie baadhi ya maandiko yaliyo wazi ambayo Umar alifanyia ijtihadi dhidi ya Qur'an.

A. Qur'an inasema:

وَإِن كُنتُم مَّرْضَىٰ أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ أَوْ جَاءَ أَحَدٌ مِّنكُم مِّنَ الْغَائِطِ أَوْ لَامَسْتُمُ النِّسَاءَ فَلَمْ تَجِدُوا مَاءً فَتَيَمَّمُوا صَعِيدًا طَيِّبًا ﴿٦﴾

"Na mkiwa na janaba basi ogeni, na mkiwa wagonjwa au mko safarini au mmoja wenu ametoka chooni au mmeingiliana na wanawake na hamkupata maji, basi kusudieni (mtayammamu) udongo ulio safi." (Qur'an, 5:6).

Na inavyoeleweka katika Sunna ya Mtume **(s.a.w.w)** ni kwamba, Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amewafundisha Masahaba namna ya kutayamamu na Umar mwenyewe akiwepo.

Bukhari amethibitisha hilo ndani ya sahih yake, Kitabut-tayammum, mlango wa udongo safi ni udhu wa Muislamu unamtosheleza maji, amesema: Imepokewa kutoka kwa Imran amesema: "Tulikuwa safarini pamoja na Mtume **(s.a.w.w)** nasi tulikwenda na tulipokuwa tuko mwishoni mwa usiku (alfajiri) tukalala usingizi, na hapana usingizi mzuri kwa msafiri kuliko huo, basi hakikutuamsha kitu isipokuwa joto la jua na wa kwanza kuamka alikuwa fulani kisha fulani, Abu Rajai akawataja majina A'uf alisahau, kisha Umar ibn Khattab (alikuwa) wa nne. Mtume alikuwa akilala haamshwi mpaka aamke mwenyewe kwani sisi hatujui kinachomtokea usingizini mwake. Basi Umar alipoamka na akaona yaliyowapata watu naye Umar alikuwa mtu msusuavu, akasema Allahu Akbar, na akapaza sauti yake kwa Takbira basi aliendelea kusema Allahu Akbar na kupaza sauti yake kwa Takbira mpaka Mtume akaamka kutokana na Takbira yake. Alipoamka, watu wakamshitakia yaliyowapata, akasema hapana kheri wala haidhuru, ondokeni, basi akaondoka Mtume akaenda siyo mbali kisha akatua na akaagiza maji ya kutawadha na pakanadiwa kwa ajili ya Sala, akawasalisha watu. Alipomaliza sala yake, mara alimuona mtu kajitenga hakusali pamoja na watu wengine, Mtume akasema: Ni jambo gani lililokuzuwia kusali pamoja na watu wengine ewe fulani? Akasema, nimepatwa na janaba na hapana maji, Mtume akasema, udongo unakutosha."

Lakini Umar anasema hali akipingana na Kitabu cha Mweyezi Mungu na Sunna ya Mtume wake kwamba, "Yeyote asipopata maji basi asisali" Na haya ndiyo madhehebu yake ambayo wameyasajili wanachuoni wengi wa hadithi. Muslim ameandika ndani ya sahih yake Kitabut-taharah mlango wa kutayammam, kwamba kuna mtu alimjia Umar akamwambia; "Mimi nina janaba na sikupata maji." Umar anasema: "Usisali." Ammar akasema: "Ewe Amirul-muuminina hukumbuki tulipokuwa mimi na wewe katika kikosi cha jeshi tukapata janaba na hatukuwa na maji, ama wewe hukuswali na mimi nikajigaragaza kwenye udongo na nikaswali, Mtume akasema: Ilikuwa inakutosha kupiga mikono yako juu ya ardhi kisha ukapuliza halafu ukapaka kwa mikono hiyo uso na vitanga vyako.' Umar akasema: "Muogope Mungu ewe Ammar." Ammar akasema; "Ukipenda sitaisimulia habari hiyo."

Sub-Hanallah!! Umar hakutosheka na kuyapinga maandiko yaliyowazi katika Kitabu (cha Mwenyezi Mungu) na Sunna, mpaka anajaribu kumzuwia Sahaba kwa kumpinga kufuatia maoni yake, Ammar ibn Yasir naye analazimika kumtaka radhi khalifa huyo kwa kusema: "Ukipenda

sitaisimulia habari hiyo." Basi itakuwaje mimi nishangae nanyi msishangazwe na ijtihadi hii na upinzani huu, pia kung'ang'ania huku juu ya maoni ya Umar pamoja na kuwepo ushahidi wa Sahaba (kuishuhudia Qur'an) kwani Umar hakutosheka (hakukubali) mpaka kufa kwake na hali kang'ang'ania itikadi hii, na haya Madhehebu yake yaliwaathiri Masahaba wengi ambao walikuwa wakikubaliana na maoni yake, bali huenda walikuwa wakiyatanguliza dhidi ya maoni ya Mtume wa Mwenyezi Mungu. Muslim ametoa ndani ya sahihi yake katika Kitabut-taharah, mlango wa kutayammam katika juzuu ya kwanza ukurasa wa 192 amesema: "Imepokewa kutoka kwa Shaqiq: Nilikuwa nimekaa na Abdallah na Abu Musa, Abu Musa akasema, Ewe baba Abdur-rahman waonaje lau mtu atapata janaba na hakupata maji kwa muda wa mwezi mmoja atafanyaje kuhusu sala?"

Abdallah akasema: "Hawezi kutayammam hata kama hatopata maji kwa kipindi cha mwezi mzima." Abu Musa akasema: "Itakuwaje basi kuhusu aya hii katika sura ya Maidah inayosema, Mkiwa hamkupata maji tayammamuni udongo safi." Abdallah akasema: "Lau wataruhusiwa kutumia aya hii nina shaka maji yakiwa baridi watatayammamu kwa udongo." Abu Musa akamwambia Abdallah, "Je, hukusikia kauli ya Ammar aliposema, Mtume alinituma shughuli fulani, basi huko nikapatwa na janaba nikajigaragaza kwenye udongo kama vile mnyama anavyojigaragaza, kisha nikaja kwa Mtume **(s.a.w.w)** nikamweleza jambo hilo, akasema: Bila shaka ilikuwa inakutosha ukusudie kwa mikono yako hivi, kisha akapiga mikono ardhini kwa pigo moja, halafu akapaka mkono wa kulia kwa kutumia mkono wa kushoto nje ya viganja na uso wake."

Abdallah akasema: "Je, huoni kwamba Umar hakutosheka kwa kauli ya Ammar." Nasi tukiizingatia riwaya hii ambayo ameithibitisha Bukhari na Muslim na wengineo miongoni mwa vitabu vya hadithi; tunafahamu kwa kupitia riwaya hiyo kiwango cha athari ya mwenendo wa Umar jinsi alivyowaathiri Masahaba wengi wakubwa, na kwa ajili hiyo tunafahamu pia kiwango cha kupingana kwa hukumu na kusongamana kwa riwaya na kupingana kwake, na bila shaka huenda mambo hayo ndiyo ambayo yanafasiri sababu ya watawala wa Kibanu Umayyah na Kibanu Abbasi kuzidharau hukumu za Kiislamu na kutozipa uzito, na ndipo wakaruhusu kuwepo madhehebu mengi yanayopingana katika hukumu ya jambo moja.

Hali halisi yamazingira haya inaonekana kama kwamba inawaambia kina Abu Hanifah, Malik, Ahmad na Shafii ya kwamba: "Semeni muyatakayo kwa maoni yenu, kwani ikiwa bwana wenu na Imam wenu Umar anasema ayatakayo kwa maoni yake atakavyo dhidi ya Qur'an na Sunna basi ninyi hamna lawama, kwani ninyi si cho chote ila ni wafuasi, na ni wafuasi wa wafuasi, ninyi hamna jambo jipya." Kinachoshangaza kuliko hilo ni kauli ya Abdallah ibn Mas-ud kumwambia Abu Musa: "Hawezi mtu kutayammam japo hatoyapata maji kwa muda wa mwezi mzima." Na huyu Abdallah ibn Mas-ud ni miongoni mwa Masahaba wakubwa, yeye anaona kwamba mwenye janaba iwapo hatopata maji aache kusali kwa mwezi mzima wala asitayammam, na inaonesha kwamba Abu Musa alijaribu kumkinaisha kwa aya tukufu iliyoshuka maalum kuhusu maudhui hii katika sura ya Maidah,

lakini Abdallah anajibu kwamba: "Lau wataruhusiwa kutumia aya hii nina shaka maji yakiwa baridi watatayammamu kwa udongo."

Kutokana na maelezo haya, vile vile tunafahamu namna wanavyojitahidi dhidi ya maandiko ya Qur'an kwa mujibu wa maoni yao, na kile wakionacho wao kwa bahati mbaya ni ugumu na uzito (wanaouweka) kwa umma, wakati ambapo Mwenyezi Mungu anasema:

﴿يُرِيدُ اللَّـهُ بِكُمُ الْيُسْرَ وَلَا يُرِيدُ بِكُمُ الْعُسْرَ ﴿١٨٥﴾

"Mwenyezi Mungu anakutakieni wepesi wala hakutakieni uzito." (Qur'an, 2:185).

Maskini huyu eti anasema:"Lau wataruhusiwa kuitumia aya hii nina shaka maji yakiwa baridi watatayammamu." Je, yeye alijiweka kuwa ndiyo mfikishaji wa ujumbe kwa niaba ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake? Na je, yeye ni 301 mwenye pupa (kuwaongoza) na ni mwenye huruma kwa waja kuliko Muumba wao na Mlezi wao? Na baada ya hayo Abu Musa anajaribu kumkinaisha kwa kutumia sunna ya Mtume ambayo aliisimulia Ammar na namna Mtume wa Mwenyezi Mungu alivyomfundisha kutayammam, lakini huyu Abdallah anaikataa Sunna mashuhuri ya Mtume kwa sababu Umar ibn Khattab hakutosheka na kauli ya Ammar.

Mpaka hapa tunafahamu kwamba kauli ya Umar ibn Khattab ndiyo hoja inayotosheleza kwa baadhi ya Masahaba na kwamba kutosheka kwa Umar juu ya hadithi au aya ndiyo kipimo pekee cha kusihi kwa hadithi au maana ya aya, japokuwa kutapingana na matendo na kauli za Mtume **(s.a.w.w)**. Kwa hiyo basi leo hii tunayakuta matendo ya watu wengi yanapingana na Qur'an na Sunna, sawa sawa katika kuhalalisha au kuharamisha, kwani ijtihadi ya Umar dhidi ya maandiko imekuwa ndiyo madhehebu yanayofuatwa, na ndiyo maana watu wanaojipendekeza kwa watawala, na wenye elimu walipoona hadithi ambazo zilizuwiwa katika zama za Makhalifa, baadaye zimeandikwa na wapokezi na wenye kuhifadhi wamezisajili hali ya kuwa zinapingana na madhehebu ya Umar ibn Khattab, hapo nao wakatengeneza riwaya nyingine za kwao wenyewe wakazinasibisha kwa Mtume **(s.a.w.w)** ili kuyapa nguvu madhehebu ya baba Hafsa, (miongoni mwa hayo ni) kama masala ya ndoa ya Mut'a na sala ya tarawehe na nyinginezo.

Basi riwaya zikaja zikipingana na imebakia mpaka leo kuwa ndiyo mahala pa ikhitilafu kati ya Waislamu na itabakia hivyo maadam wako wanaomtetea Umar kwa kuwa yeye ni Umar wala (mtu) hataki kuchunguza kwa ajili ya kutafuta haki na aseme kumwambia Umar Umekosea kwani sala haitenguki kwa kukosekana maji na kwamba kuna aya iliyotajwa ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu inayoruhusu kutayammam, na kuna hadithi ya kutayammam imetajwa ndani ya vitabu vyote vya Sunna. Basi kutokuzifahamu kwako wewe kunakunyima nafasi ya kukalia cheo cha Ukhalifa wala kuongoza umma, na kama ulizifahamu, hilo linakukufurisha iwapo utazipinga hukumu zake hiyo haikukufalia kitu (kuzipinga) ikiwa wewe ni muumini. Pindi Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapohukumu jambo eti wewe uwe na hiyari, ukahukumu utakavyo na kukipinga ukitakacho na hali ya kuwa unajuwa mno kuliko mimi kwamba yeyote mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake bila shaka amepotea upotevu ulio wazi.

B. Mwenyezi Mungu anasema:

إِنَّمَا الصَّدَقَاتُ لِلْفُقَرَاءِ وَالْمَسَاكِينِ وَالْعَامِلِينَ عَلَيْهَا وَالْمُؤَلَّفَةِ قُلُوبُهُمْ وَفِي الرِّقَابِ وَ الْغَارِمِينَ
وَفِي سَبِيلِ اللَّـهِ وَابْنِ السَّبِيلِ فَرِيضَةً مِّنَ اللَّـهِ وَاللَّـهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٦٠﴾

"Bila shaka sadaka hupewa mafakiri na masikini na wanaozitumikia na wanaotiwa nguvu nyoyo zao (juu ya Uislamu) na katika kuwapa uungwana watumwa na wenye madeni (yaliyowazidi uzito) na katika njia ya Mwenyezi Mungu na wasafiri (waliohawaribikiwa) ni faradhi inayotoka kwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ni mjuzi (na) mwenye hekima." (Qur'an, 9:60).

Miongoni mwa sunna maarufu ya Mtume ni kwamba, yeye Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** alikuwa akiwahusisha wanaotiwa nguvu nyoyo zao juu ya Uislamu kwa sehemu yao aliyowafaradhishia Mwenyezi Mungu kama alivyoamrisha Mwenyezi Mungu Mtukufu. Lakini Umar alikibatilisha kipato hiki kilichofaradhishwa na akajitahidi dhidi ya Qur'an katika zama za Ukhalifa wake na akawaambia "Hatuna haja nanyi Mwenyezi Mungu amekwisha uimarisha Uislamu na hana haja nanyi." Bali Umar aliipuuza hukumu hii katika zama za Ukhalifa wa Abubakr, pale walipomjia hao wanaotiwa nguvu nyoyo zao kama ilivyokuwa kawaida yao kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu.

Abubakr akawaandikia suala hilo wakaenda kwa Umar ili wakachukuwe sehemu yao, Umar akaichana barua hiyo na akawaambia: "Hatuna haja nanyi, Mwenyezi Mungu amekwisha uimarisha Uislamu na hana haja nanyi, basi kama mtasalim amri vinginevyo kati yetu na ninyi ni upanga tu." Walirudi kwa Abubakr wakamwambia, "Hivi wewe ndiwe Khalifa au yeye?" Akasema "Ni yeye apendapo Mwenyezi Mungu." Naye Abubakr alirudi nyuma kuyatekeleza yale aliyoyaandika akaafikiana na maoni ya jamaa yake Umar. Na cha ajabu vile vile ni kwamba leo hii utawakuta wanaomtetea Umar katika suala hili na kulizingatia kuwa ndiyo miongoni mwa sifa zake na uhodari wake, na miongoni mwa hawa ni Sheikh Muhammad anayejulikana kama Ad-dawaalibi, anasema katika kitabu chake Usulul-Fiqhi uk. 239 kwamba, "Huenda ijtihadi ya Umar (r.a) katika kukata kipato ambacho Qur'an imekiweka kwa ajili ya wanaoimarishwa nyoyo zao katika dini, ilikuwa katika utangulizi wa hukumu ambazo alizizungumzia Umar kufuatia mabadiliko ya maslahi kwa kubadilika zama pamoja na kwamba Qur'an kuhusiana na hilo bado imethibiti haikufutwa."

Kisha baada ya hapo (Sheikh huyu) akaanza kumtakia udhuru Umar kwamba yeye aliiangalia sababu ya kushuka kwa tamko hilo la Qur'an na siyo dhahiri yake ... mpaka mwisho wa maneno yake ambayo akili timamu haziwezi kuyafahamu. Sisi tunakubali ushahidi wake kwamba Umar alizigeuza hukumu za Qur'an kufuatia maoni yake kwamba, maslahi yanabadilika kwa mnasaba wa nyakati, na tunaipinga tafsiri yake kwamba Umar aliangalia sababu ya maandiko hayo na hakuangalia dhahiri yake na tunamwambia yeye na wengine kwamba matamko ya Qur'an na yale ya hadithi za Mtume hayabadiliki kwa kubadilika nyakati, kwani Qur'an inasema wazi kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu yeye mwenyewe hana haki kuibadilisha.

Mwenyezi Mungu anasema:

وَإِذَا تُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ آيَاتُنَا بَيِّنَاتٍ ۙ قَالَ الَّذِينَ لَا يَرْجُونَ لِقَاءَنَا ائْتِ بِقُرْآنٍ غَيْرِ هَـٰذَا أَوْ بَدِّلْهُ ۚ قُلْ مَا يَكُونُ لِي أَنْ أُبَدِّلَهُ مِن تِلْقَاءِ نَفْسِي ۖ إِنْ أَتَّبِعُ إِلَّا مَا يُوحَىٰ إِلَيَّ ۖ إِنِّي أَخَافُ إِنْ عَصَيْتُ رَبِّي عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿١٥﴾

"Na wanaposomewa aya zetu zilizo wazi wale wasioamini kukutana nasi husema, leta Qur'an isiyokuwa hii au uibadilishe, waambie, Siwezi kuibadilisha kwa hiyari yangu, sifuati isipokuwa yanayofunuliwa kwangu, hakika mimi naiogopa nikimuasi Mola wangu adhabu ya siku iliyo kuu." (Qur'an, 10:15).

Nayo Sunna tukufu ya Mtume inasema: "**Halali (aliyoihalalisha) Muhammad ni halali mpaka siku ya Qiyama, na Haramu (aliyoiharamisha) ni haramu mpaka siku ya Qiyama**."

Lakini kwa mujibu wa madai ya Ad-dawaalibi na wanaokubaliana na maoni yake miongoni mwa wanaotetea ijtihadi ni kuwa, hukumu zinabadilika kutokana na mabadiliko ya nyakati. Kama ni hivyo basi, hapana lawama kwa baadhi ya watawala ambao walizibadilisha hukumu za Mwenyezi Mungu, kwani miongoni mwao yuko aliyesema: "Kuleni ili mpate nguvu dhidi ya adui yenu hapana haja ya kufunga saumu katika zama hizi ambazo tunapambana na umasikini na ujinga na kubakia nyuma kimaendeleo, na saumu inatufanya tushindwe kuzalisha mali. Si hivyo tu bali alizuwia ndoa ya wake wengi kwani yeye anaona kuwa jambo hilo ni dhuluma, ni kuvunja haki za mwanamke." Akaendelea kusema kwamba: "Katika zama za Muhammad mwanamke alikuwa akizingatiwa kuwa ni nyenzo, ama sasa hivi tumemkomboa na kumpa haki zake zote.

Kiongozi huyu aliyaangalia maandiko kwa mujibu wa sababu asilia na wala hakuiangalia dhahiri yake kama Umar alivyoiangalia akasema: "Hakika mirathi leo hii ni lazima igawiwe kwa mwanamume na mwanamke kwa kiwango cha sawa kwa sawa, kwani Mwenyezi Mungu alimpa mwanamume sehemu mbili kwa kuzingatia kwamba yeye ndiye anayeilea familia wakati ambapo mwanamke alikuwa amepuuzwa, ama leo hii kutokana na juhudi za utawala wake sasa hivi mwanamke anajishugulisha na kuilea familia yake na aliwatolea mfano wananchi kwa mkewe ambaye alimsaidia nduguye mpaka akafikia ngazi ya waziri kutokana na ufadhili wake na uangalizi wake."

Kama ambavyo kiongozi huyo alihalalisha uzinifu na akaizingatia kuwa ni haki ya mtu binafsi aliyefikia umri wa utambuzi maadam haendi kinyume katika njia za kuendesha maisha, na akafungua majumba ya kulea watoto ambao wanazaliwa kutokana na zinaa akitetea hilo kuwa yeye ni mwenye huruma kwa watoto wa zinaa ambao walikuwa wakizikwa hali wakiwa hai kwa kuchelea fedheha, na zaidi ya hayo ni miongoni mwa ijtihadi zake zinazofahamika. Cha kushangaza ni kuwa kwa kiwango fulani rais huyu alikuwa ameathiriwa na hali ya Umar, kwani kuna kipindi alimtaja Umar kwa kumsifu, na kuna wakati akamtaja kwamba Umar hakuweza kuyabeba majukumu akiwa hai na baada ya kufa, wakati ambapo yeye atayamudu akiwa hai na baada ya kufa, na kuna wakati mwingine ni kama kwamba zilimfikia habari kuwa Waislamu wamezikosoa juhudi zake akasema: "Bila shaka Umar alikuwa mtu wa mwanzo tena mkubwa na mwenye kujitahidi

katika zama zake, basi ni kwa nini mimi nisijitahidi katika zama zangu hizi mpya, kwani Umar alikuwa kiongozi wa dola na mimi pia ni kiongozi wa dola."

Kinachoshangaza zaidi ni kuwa kila anapomtaja Muhammad Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** utaona katika maneno yake mna dharau na kejeli, kwani alisema katika hotuba yake kwamba, "Muhammad alikuwa hajui hata jiografia kwa kuwa alisema: Itafuteni elimu japokuwa itakuwa China, akidhani kwamba China ndiyo mwisho wa dunia, kwa hiyo Muhammad alikuwa hajui kuwa elimu itafikia kiwango hiki na kwamba tani nyingi za chuma (yaani ndege) zitaweza kuruka angani. unafikiri namna gani lau angetambua au kusimuliwa juu ya uranium na polasium na elimu za atom na nyukilia?" Kwa hiyo mimi simlaumu yeye maskini asiyefahamu chochote kuhusu kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna ya Mtume wake? Bali mtu huyu alijikuta tu amekwishaitawala dola kwa niaba ya Uislamu hali yakuwa anaukejeli Uislamu, anafuata utamaduni wa kimagharibi na anakusudia kuigeuza nchi yake na kuwa ni dola kama dola za Uiaya kwa kufuatia mtazamo auonao yeye.

Wako wengi miongoni mwa Marais na Wafalme waliofuata mwenendo wake, pale alipoungwa mkono na dola za Magharibi kiasi kwamba wakamsifu kuwa ni mpiganiaji haki mkubwa, kisha simlaumu kwani kila kitu kina chanzo chake na kila chombo hutoa kile kilichomo. Iwapo mimi nitakuwa muadilifu basi lawama nitazitupia kwa Abubakr, Umar na 'Uthman ambao ndio waliofungua mlango huu tangu siku aliyofariki Mtume **(s.a.w.w)** na wakasababisha ijtihadi zote ambazo watawala wa Banu Umayyah na Banu Abbas waliziimarisha kwa kipindi cha karne saba, na karne zote hizo zilitumika kuharibu miongozo ya Uislamu katika maandiko yake ya asili na hukumu zake, na mambo yalizidi zaidi kuwa mabaya katika karne zilizofuatia hapo, mpaka ikafikia kwamba kiongozi (wa Kiislamu) analihutubia taifa lake la Waislamu hali ya kuwa anamkejeli Mtume wa Mwenvezi Mungu na hapana yeyote wa kumkemea, si ndani wala nje.

Haya ndiyo niliyoyasema na ninayasema kwa baadhi ya jamaa katika harakati za Kiislamu kwamba, "Ikiwa ninyi leo hii mnampinga kiongozi kwa kutofuata Quran na Sunna ya Mtume, basi mnawajibika mumpinge aliyeleta uzushi huu wa kufanya ijtihadi dhidi ya Qur'an na Sunna, ikiwa kweli ninyi ni waadilifu na mnataka kuifuata haki kwa vitendo. Kwa bahati mbaya hawayakubali maneno haya na hunikosoa eti ni vipi nawalinganisha viongozi wa leo na Makhalifa waongofu? Nami huwajibu kwamba viongozi wa leo na wafalme wa leo ni matokeo kamili ya yale yaliyotokea ndani ya historia, na je ni lini Waislamu walikuwa huru baada ya kufariki Mtume na hata leo uhuru wao uko wapi?

Basi wao husema: "Ninyi Mashia kazi yenu ni kuwazulia Masahaba na kuwatukana, na lau siku moja tutashika madaraka tutakuchomeni moto." Basi mimi husema; "Mwenyezi Mungu asikupeni mafanikio hayo."

C. Mwenyezi Mungu anasema:

الطَّلَاقُ مَرَّتَانِ فَإِمْسَاكٌ بِمَعْرُوفٍ أَوْ تَسْرِيحٌ بِإِحْسَانٍ وَلَا يَحِلُّ لَكُمْ أَن تَأْخُذُوا مِمَّا آتَيْتُمُوهُنَّ شَيْئًا إِلَّا أَن يَخَافَا أَلَّا يُقِيمَا حُدُودَ اللَّـهِ فَإِنْ خِفْتُمْ أَلَّا يُقِيمَا حُدُودَ اللَّـهِ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا فِيمَا

افْتَدَتْ بِهِ ۗ تِلْكَ حُدُودُ اللَّـهِ فَلَا تَعْتَدُوهَا ۚ وَمَن يَتَعَدَّ حُدُودَ اللَّـهِ فَأُولَـٰئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٢٢٩﴾
فَإِن طَلَّقَهَا فَلَا تَحِلُّ لَهُ مِن بَعْدُ حَتَّىٰ تَنكِحَ زَوْجًا غَيْرَهُ ۗ فَإِن طَلَّقَهَا فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا أَن يَتَرَاجَعَا
إِن ظَنَّا أَن يُقِيمَا حُدُودَ اللَّـهِ ۗ وَتِلْكَ حُدُودُ اللَّـهِ يُبَيِّنُهَا لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿٢٣٠﴾

"Talaka ni mara mbili, kisha ni kumuweka kwa wema au kumuacha kwa wema. wala si halali kwenu kuchukua chochote mlichowapa (wake zenu) isipokuwa wote wawili wakiogopa ya kwamba hawawezi kusimamisha mipaka ya Mwenyezi Mungu, basi mukiogopa kwamba hawataweza kusimamisha mipaka ya Mwenyezi Mungu. hapo itakuwa hapana dhambi kwao kupokea ajikomboleacho mwanamke, hii ndiyo mipaka ya Mwenyezi Mungu basi musiiruke, na watakaoiruka mipaka ya Mwenyezi Mungu hao ndio madhalimu, na kama amempa talaka (ya tatu) basi si halali kwake baada ya hayo mpaka aolewe na mume mwingine, na akimuacha basi hapo hapana dhambi kwao kurejeana wakiona kuwa watasimamisha mipaka ya Mwenyezi Mungu na hiyo ndiyo mipaka ya Mwenyezi Mungu anayoibainisha kwa watu wanaojua." (Qur'an, 2:229-230).

Nayo Sunna Tukufu ya Mtume ilitoa tafsiri bila ya utata ya kwamba mwanamke hawi haramu kwa mumewe isipokuwa baada ya talaka tatu. hapo haitastahiki kwa mumewe kumrejea isipokuwa baada ya kuolewa na mume mwingine, na ikiwa atamuacha huyu mume mwingine hapo itawezekana kwa mume yule wa kwanza kumuoa upya kama wanaume wengine ambavyo wangewajibika kufanya, na ni juu yake mwanamke huyo kukubali au kukataa ni hiyari yake mwenyewe. Lakini Umar ibn Khattab kama ilivyokawaida yake, alivuka mipaka ya Mwenyezi Mungu aliyoibainisha kwa watu wenye kufahamu, akaibadilisha hukumu hii kwa kuweka hukumu yake ambayo inasema: "Talaka moja kivitendo kwa tamko la talaka tatu linamharamishia mume mkewe." Umar akawa ameipinga Qur'an tukufu na Sunna ya Mtume **(s.a.w.w)**.

Imethibiti ndani ya sahihi Muslim Kitabut-talaq Babu Talaqit-thalath kutoka kwa ibn Abbas amesema: "Katika zama za Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** na Abubakr, na miaka miwili ya Ukhalifa wa Umar, talaka ilikuwa ni talaka tatu (katika kikao kimoja) ni moja, basi Umar akasema: "Hakika watu wamelipupia jambo ambalo hapo kabla kulikuwa na utulivu kwa ajili yao kuhusiana nalo, lau tutalipitisha liwe ni hukumu juu yao, akalipitisha juu yao." Wallahi inashangaza, ni vipi Khalifa anathubutu kubadilisha hukumu za Mwenyezi Mungu mbele ya Masahaba na wanamkubalia kila anachosema na kukifanya na hakuna mwenye kukemea wala kupinga na wanatudanganya siye masikini kwamba eti Sahaba mmoja alimwambia Umar: "Wallahi lau tutaona unapotoka tutakurekebisha kwa hukumu ya upanga." Hii ni kauli ya uongo na ni uzushi ili watuoneshe kwamba Makhalifa walikuwa ni mfano bora katika kutoa uhuru na demokrasi, wakati historia inawapinga kwa ukweli wake kimatendo, na hapana mazingatio yoyote kwa maneno (kauli) ikiwa matendo yako ni kinyume chake.

Au huenda wao (Masahaba) walikuwa wanaona ndani ya Qur'an na Sunna mna upotofu na kwamba Umar ibn Khattab ndiyo alikuwa akilirekebisha na kuweka sawa. Tunajilinda kwa Mwenyezi Mungu

kutokana na kauli za kuropoka. Na nilikuwa katika mji wa Qafsah, na mara nyingi nikiwajibu wanaume ambao wamejiharamishia wake zao kwa kuwa waliwaambia wake zao mara tatu; "Wewe ni haramu (kwangu)." Na walikuwa wakifurahi pindi ninapowafahamisha hukumu sahihi za Mwenyezi Mungu ambazo Makhalifa hawakuzivuruga kutokana na ijtihadi zao, lakini wale watu wanaojidai kuwa wao ni wenye elimu huwatisha kwa kuwaambia kwamba, "Mashia kila kitu kwao ni halali."

Namkumbuka mmoja wao kuna wakati fulani alinihoji kwa njia nzuri na akaniuliza: "Ikiwa Sayyidina Umar ibn Khattab (r.a) aliibadilisha hukumu ya Mwenyezi Mungu kuhusu suala hili na nyinginezo halafu Masahaba wakamkubalia hilo, basi ni kwa nini Sayyidna Ali (a.s) hakumpinga Sayyidna Umar? Mimi nilimjibu kwa jawabu alilolitoa Imam Ali (a.s) wakati Maquraish waliposema kuwa, "Yeye ni mtu shujaa lakini hana ujuzi wa vita." Akasema (Imam Ali a.s): "Naapa kwa Mwenyezi Mungu, je, kuna yeyote miongoni mwao amebobea mno shughuli za vita! ili nimpe daraja hiyo kutoka kwangu?.

Nilisimama katika vita wakati sijafikia umri wa miaka ishirini, nami sasa nimekuwa zaidi ya miaka sitini, lakini ikimbukwe kuwa hana njia mtu ambaye watu wake hawamtii."[1].

Basi je, Waislamu waliyasikiliza maoni ya Ali? (Hakuna) isipokuwa wafuasi wake waliouamini Uimamu wake, kwa hakika (imam Ali) alipinga kuharamishwa kwa mut'a na akapinga uzushi wa tarawehe na alizipinga hukumu zote zilizobadilishwa na Abubakr, Umar na Uthman, lakini. maoni yake yalibakia kwa wafuasi wake na vipenzi wake. Ama Waislamu wengine walimpiga vita wakamlaani na wakajaribu kila njia kumuua na kufuta utajo wake.

Hakuna kitakachoweza kujulisha kupinga kwake Imam Ali (kubadilishwa kwa hukumu za Mwenyezi Mungu) zaidi kuliko msimamo wake mtukufu wa kishujaa (aliouonesha) pale Abdur-rahman ibn A'uf waliyempendekeza achague khalifa baada ya kufa Umar akamwita (Imam Ali) na kumpa masharti kwamba atakapokuwa amemchagua awe khalifa, basi awahukumu kwa mujibu wa sunna ya Makhalifa wawili (yaani) Abubakr na Umar. Imam Ali (a.s) akalikataa sharti hili na akasema: "Nitahukumu kwa mujibu wa Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna ya Mtume wake." Na kwa ajili hii basi walimuacha na wakamchagua Uthman ibn Affan ambaye alikubali sharti la kuhukumu kwa mujibu wa sunna ya 'Makhalifa hao wawili.

Kwa hiyo basi, leo hii utaona kwamba mlango wa mji wa elimu (ambaye ni Imam Ali a.s) alikuwa mjuzi mno kuliko watu wengine baada ya Mtume **(s.a.w.w)**, (na alikuwa) mfikishaji na mlinzi wa kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna ya Mtume wake, lakini amepuuzwa kwa upande wa Masunni kiasi kwamba wao wanamfuata Maliki, Abu Hanifah, Shafii na Ibn Hanbal. Wanawafuata hawa katika kila jambo la dini miongoni mwa ibada na shughuli za uhusiano na wala hawamrejei Imam Ali katika jambo lolote.

Hivyo hivyo ndivyo walivyofanya Maimamu wao katika hadithi, kama vile Bukhari na Muslim, utawaona wanapokea hadithi kutoka kwa Abu

1. Nahjul-balagha, Hotuba ya 27.

Hurairah na Ibn Umar na au kutoka kwa mtu dhaifu na asiyejulikana, aliye karibu na aliye mbali (wanapokea tu). Wakati huo huo hawapokei kutoka kwa Ali isipokuwa hadithi chache alizozushiwa na ndani yake zinachafua heshima ya nyumba ya Mtume **(s.a.w.w)**, kisha wao hawatosheki na hilo bali anayemfuata Ali (a.s) na wafuasi wema wa Imam Ali humkufurisha na kumpinga, pia (Masunni) huwatukana kwa kuwaita kuwa ni wapinzani na majina mengine mabaya, na ukweli wa mambo ni kwamba watu hawa (yaani Mashia) hawana kosa lolote isipokuwa ni kwa sababu ya kumfuata Ali ambaye alikuwa amepuuzwa na kutengwa katika zama za Makhalifa watatu, kisha baadaye akawa analaaniwa na kupigwa vita katika zama za Banu Umayah na Banu Abbas. Kila mwenye kufuatilia na akaifahamu historia, utaupata ukweli huu wazi wazi, na atafahamu yaliyopita na njama zilizopangwa dhidi yake (Imam Ali) na watu wa nyumba yake na wafuasi wake.

16

# WAULIZE WANAOFAHAMU

## UTHMAN IBN A'FFAAN ANAFUATA SUNNA YA JAMAA ZAKE KATIKA KUYAPINGA MAANDIKOYA QUR'AN NA SUNNA YA MTUME

Huenda Uthman ibn Affaan alipomuahidi Abdur-rahman ibn A'uf mwanzoni tu mwa baia yake ya Ukhalifa kwamba atawahukumu kwa mujibu wa sunna ya Makhalifa wawili Abubakr na Umar, alikuwa akikusudia kwamba naye atajitahidi kama walivyojitahidi wao kina Umar kugeuza maandiko ya Qur'an na matamko ya Sunna ya Mtume kama walivyokuwa wakifanya kina Umar. Yeyote atakayefuatilia sera yake (Uthman) zama za Ukhalifa wake, atamkuta yeye kuwa alikwenda mbele zaidi katika ijtihadi mpaka akawasahaulisha watu ijtihadi za jamaa zake kina Abubakr na Umar.

Mimi sitaki kurefusha maudhui hii ambayo imejaa ndani ya vitabu vingi vya historia vya hapo zamani na sasa hivi, yakiwemo yale aliyoyazua Uthman miongoni mwa mambo ya kutisha yaliyosababisha mapinduzi dhidi yake na yakaangamiza maisha yake. Lakini nitafupisha kwa kutoa mifano michache ili imdhihirikie msomaji na kila anayetafiti yale waliyoyazusha vvenye kutetea ijtihadi ndani ya dini ya Muhammad **(s.a.w.w)**.

A. Muslim amethibitisha ndani ya sahih yake katika kitabu Salatil-musafir kutoka kwa Aisha amesema: "**Mwenyezi Mungu alifaradhisha rakaa mbili wakati (wa mwanzo) alipoifaradhisha (sala) kisha akaikamilisha (kwa rakaa zingine mbili) ikiwa ni nyumbani, na ikathibitishwa sala ya safari kwa ile faradhi ya mwanzoni.**"

Kama ambavyo Muslim ameandika katika mlango huo huo uliotajwa hapo juu kutoka kwa Ya'ala ibn Umayyah amesema: "Nilimwambia Umar ibn Khatab, Si vibaya kwenu ninyi kupunguza sala ikiwa mtachelea kukushambulieni wale waliokufuru, lakini sasa watu wako katika amani." Umar akasema: "Nilishangazwa na yaliyokushangaza wewe, ndipo nilipomuuliza Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** kuhusu jambo hilo akasema: Hiyo ni zawadi Mwenyezi Mungu amekuzawadieni, basi ikubalini zawadi yake."

Kama ambavyo Muslim ameandika ndani ya sahihi yake ndani ya Kitabul-musafirina waqas-riha kutoka kwa ibn Abbas amesema: "Mwenyezi Mungu amefaradhisha sala kwa ulimi wa Mtume wenu kuwa ni rakaa nne nyumbani, na safarini rakaa mbili na katika khofu rakaa moja." Vile vile Muslim ndani ya sahih yake amethibitisha kutoka kwa Anas ibn Malik amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa akitoka mwendo wa maili tatu au Far-sakh tatu, husali rakaa mbili." Na kutoka kwake tena amesema: "Tulitoka pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu mjini Madina mpaka Maka, basi Mtume akasali rakaa mbili mpaka aliporudi, nikasema: Alikaa siku ngapi Maka? Akasema siku kumi." Kwa kupitia hadithi hizi ambazo amezithibitisha Muslim ndani ya sahih yake inatubainikia kwamba, aya tukufu iliyoshuka kuhusu kupunguza sala katika safari, Mtume wa Mwenyezi Mungu aliifahamu na kisha akaifasiri kwa kauli na matendo ya

kwamba ni ruhusa aliyoizawadia Mwenyezi Mungu kwa Waislamu na wanalazimika kuikubali."

Na kutokana na hali hii yanatenguka madai ya Ad-dawaalibi na walio kama yeye katika kumtakia udhuru Umar na kuyapitisha makosa yake kwamba yeye aliangalia sababu asilia ya hukumu na hakuangalia dhahiri yake, kwani Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** alimfundisha Umar lengo la kushuka aya ya kupunguza sala pale Umar aliposhangaa kwamba maandiko yaliyothibiti haisimami juu ya sababu yake ya asili, kwa hiyo sala itapunguzwa hata kama watu wako katika amani na hawachelei kushambuliwa na wale waliokufuru.

Lakini Umar, yeye anayo maoni mengine (ayajuwayo) siyo yale anayoyaona Ad-dawalibi na wanachuoni wa Kisunni kwa mujibu wa dhana zao nzuri. Na hebu tumuangalie Uthman ibn A'ffan, hapana shaka naye ni mwingine anayejitahidi dhidi ya maandiko ya Quran na Sunna, mpaka naye anaunga msafara wa Makhalifa kwani mambo yalipomkalia vizuri (kwenye Ukhalifa) akaikamilisba sala katika safari na akaigeuza kuwa rakaa nne badala ya mbili. Kwa hakika nimekuwa nikijiuliza sababu za kuzibadilisha faradhi hizi na kuongeza ndani yake, kwani ni jambo gani lililopelekea hila hii, na sikuona isipokuwa alikusudia kuwavuruga watu na hasa Banu Umayyah (wamwone) kuwa yeye ni mwema na ni mchamungu kuliko Muhammad, Abubakr na Umar. Muslim ameandika katika sahih yake ndani ya mlango wa sala ya msafiri na kupunguza sala huko Mina amesema: "Imepokewa kutoka kwa Salim ibn Abdallah, kutoka kwa Baba yake, naye kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** kwamba yeye Mtume alisali Mina na sehemu nyingine rakaa mbili nao Abubakr na Umar hivyo hivyo, na Uthman (alisali) rakaa mbili hapo mwanzoni mwa Ukhalifa wake kisha baadaye alikamilisha (rakaa) nne." Kama iliyokuja katika sahih Muslim vile vile kwamba, Az-zuhri amesema; "Nilimwambia U'r-wah ana nini Aisha mbona anakamilisha katika safari?" Akasema: "Bila shaka yeye amebadilisha kama alivyobadilisha Uthman."

*Basi hivi ndivyo ilvyofanywa dini ya Mwenyezi Mungu katika hukumu zake na maandiko yake (inafanywa kuwa) ni yenye kufuata mabadiliko ya wabadilishaji na tafsiri za wenye kufasiri.

B. Kama ambavyo Uthman alivyojitahidi kwa maoni yake kuyaunga mkono yale aliyoyafanya Umar, miongoni mwa hayo ni kuharamisha Mut'atul-hajji na ni kama alivyoiharamisha ndoa ya Mut 'a Bukhari ameandika ndani ya sahih yake katika Kitabul hajji mlango wa Tamattu'i na Iqran, kutoka kwa Mar-wan ibn Al-hakam amesema: "Niliwashuhudia Uthman na Ali (r.a). na Uthman (alikuwa) akikataza Tamatu'i na kuzikusanya baina yao, basi Ali alipoona hayo alihirimia zote Umra na Hijja na akasema siwezi kuacha Sunna ya Mtume **(s.a.w.w)** kutokana na kauli ya mtu fulani." Naye Muslim ameandika ndani ya sahih yake katika Kitabul-hajji Babu Jawazit-tamattu'i kutoka kwa Said ibn Al-musayyab amesema: "Ali na Uthman (r.a) walikutana huko Us-fan, basi Uthman akawa anakataza Tamattu'i au Umrah, Ali akasema; unataka kulifanya nini jambo alilolitenda Mtume wa Mwenyezi Mungu (unataka) kulikataza? Uthman akasema: "Achana nasi." Ali akasema, "**Hakika siwezi kukuacha." Basi Ali alipoyaona hayo yeye akazihirimia zote pamoja**."

Naam, huyu ndiye Ali mwana wa Abu Talib. amani ya Mwezi Mungu imshukie, hakuwa mwenye kuiacha Sunna ya Mtume **(s.a.w.w)** kwa ajili ya kauli ya mtu fulani miongoni mwa watu, na ile riwaya ya tatu inatufidisha kwamba, mzozo uliopita baina ya Ali na Uthman na kauli ya Uthman aliposema Achana nasi, yapo mambo ambayo miongoni mwake ni kwenda kwake kinyume (yeye Uthman) katika kila kitu na kutokufuata yale ambayo Ibn Ammi yake (Mtume **s.a.w.w**) kama ambavyo riwaya hiyo imekatwa kwani inasema: "**Ali akasema hakika mimi siwezi kukuacha**." Lakini basi alipoyaona hayo!! Je, ni mambo gani aliyoyaona Ali? Hapana shaka kwamba huyo (Uthman) pamoja na Ali kumkumbusha Sunna ya Mtume yeye aling'ang'ania kwenye maoni yake kuipinga Sunna ya Mtume na akawazuwia watu wasifanye Tamattu'i na hapo ndipo Imam Ali alipompinga Uthman na akahirimia zote pamoja yaani Hijja na Umrah.

C. Kama ambavyo Uthman alijitahidi vile vile kuhusu vifungu vya sala, basi alikuwa hasomi Takbira wakati akisujudu wala wakati anyanyukapo kutoka kwenye sijida.

Imam Ahmad ibn Hanbali ameeleza ndani ya Musnad yake juzuu ya nne ukurasa 440 kutoka kwa Imran ibn Hasin amesema: "Niliswali nyuma ya Ali sala iliyonikumbusha sala niliyosali pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu na Makhalifa wawili, akasema: Basi nikaenda nikasali pamoja naye, akawa husoma Takbira kila anaposujudu na kunyanyua kichwa chake kutoka kwenye rukuu, nikasema, Ewe baba Najiid ni nani wa mwanzo kuiacha Takbira hiyo, akasema, Uthman (r.a) wakati alipozeeka na sauti yake kuwa dhaifu aliicha[1].

Naam, hivi ndivyo ilivyopotezwa Sunna ya Mtume na ikageuzwa (toka mahala pake) ikawa ni sunna ya Makhalifa na sunna ya kifalme na ni sunna ya kisahaba na sunna ya Banu Umayyah na sunna ya Banu Abbas na zote hizo ni Bid'a zilizozushwa (na kutiwa) ndani ya Uislamu, basi (ifahamike kuwa) kila uzushi ni upotovu na kila upotovu (malipo yake) ni motoni kama alivyosema Mtume **(s.a.w.w)** Kwa ajili hiyo utaona leo hii namna na aina nyingi za sala za Waislamu, utawadhania wako pamoja lakini nyoyo zao ziko mbali mbali, kwani wanajipanga katika mstari ili wasali katika safu moja, basi utamuona huyu amenyoosha mikono yake na yule naye kakunja na mwingine naye anastaili yake peke yake katika kukunja mikono, kwani yeye anaweka mikono yake juu ya kitovu na au moyo Na mwingine utamuona amegusanisha nyayo zake na mwingine ameziachanisha. Almuradi kila mmoja anaamini kuwa yeye ndiyo yuko kwenye haki, na ukiyazungumzia hayo utaambiwa: "Ewe Bwana hizo ni aina (za sala) ambazo hazina umuhimu, wewe sali upendavyo la muhimu ni kuwa unasali basi!!

Naam, hii ni sawa kwa kiasi fulani, kwani muhimu ni kusali lakini ni lazima sala hiyo ikubaliane na sala ya Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**, bila shaka Mtume amesema "Salini kama munionavyo mimi ninasali." Basi tunalazimika kujitahidi kuitafuta sala ya Mtume **(s.a.w.w)** kwani sala ni nguzo ya dini.

---

1. Musnad Ahmadi ibn Hambali, Juzuu ya nne, uk. 440.

D. Uthman aliyestahiwa na Malaika wa Mwenyezi Mungu. Amesema Al-Balaadhuri ndani ya Ansabid-ashraf juz. 5 uk. 54. Habari za kifo cha Abudharri kutoka huko Rubdhah zilipomfikia Uthman alisema: "Mwenyezi Mungu amemrehemu (Abudharri)." Ammar ibn Yasir akasema: "Naam, amrehemu Mwenyezi Mungu kuliko nafsi zetu wote." Uthman akamwambia Ammar: Ewe muuma kwa meno dhakari ya baba yake, unadhani nimejuta kwa kumfukuza kwangu Abudharri." Kisha Uthman akaamuru aangushwe chini na alazwe chali na akasema, Nenda kajiunge mahali pake." Alipokuwa akijiandaa kutoka wakaja Banu Makhzuum kwa Imam Ali wakamwomba akaseme na Uthman juu ya Ammar, basi Imam Ali akamwambia, "Ewe Uthman mche Mungu bila shaka ulimfukuza (kutoka hapa Madina) mtu mwema miongoni mwa Waislamu akafia huko ulikomfukuzia, kisha wewe sasa hivi unataka kumfukuza mtu mfano wake?[1]".

Yakapita baina yao mazungumzo mpaka Uthman akamwambia Ali, "Basi wewe unastahiki mno kufukuzwa kuliko yeye." Ali akasema, "Ukipenda nifukuze." Hapo wakakusanyika Muhajirina kwa Uthman wakamwambia, "Ikiwa kila mtu anapokusemesha, basi wewe humtoa na kumfukuza hapana, jambo hili haliwezekani" Hakumfukuza Ammar." Katika riwaya ya Ya'aqubi ndani ya tarikh yake juz. 2 uk.147 ameandika kwamba: Ammar ibn Yasir alimsalia Miqdad na akamzika wala hakumruhusu Uthman kufanya hilo kutokana na usia wa Miqdad, basi Uthman alimkasirikia sana Ammar na akasema: "**Namuonya, Ole wangu juu ya mtoto wa mwanamke mweusi. nilikuwa namjuwa vilivyo.**"[2]

Hivi kweli inawezekana kwa mtu mwenye heshima kama hiyo ambaye malaika walimstahi aseme maneno machafu na hasa kuwahusu waumini wema? Uthman hakutosheka kumtukana Ammar na kumwambia maneno machafu kama ule usemi wake usemao: "Ewe minima meno dhakari ya babake." Kiasi kwamba aliwaamrisha vijana wake wamkamate Ammar na wakamshika miguu na mikono yake kisha Uthman akampiga Ammar kwa miguu yake ambayo alikuwa amevaa buti (akampiga) mbeleni na akamjeruhi. Kipindi hicho Ammar alikuwa keshakuwa mtu mzima tena amedhoofika, na kutokana na kipigo hicho alizimia. Hiki ni kisa mashuhuri kwa wanahistoria, matendo haya yalifanyika wakati kundi fulani la Masahaba walipoandika barua na kumuamuru Ammar aifikishe kwake (Uthman). Ni hivyo hivyo Uthman alivyomfanyia Abdallah ibn Mas-ud pale alipomuamuru mmoja wa askari wake aliyekuwa akiitwa Abdallah ibn Zum-a'h. Huyu Abdallah ibn Zum-a'h alimbeba Abdallah ibn Mas-u'ud mpaka akamfikisha kwenye mlango wa msikiti akamtupa chini akavunjika mbavu. Hapakuwa na sababu yoyote ile isipokuwa tu ni kwamba, Abdallah ibn Mas-u'd alimpinga Uthman kwa tendo lake la kuwapa waovu wa kibanu Umayyah mali za Waislamu (kwa wingi) bila hesabu.

Hatimaye yalifanyika mapinduzi dhidi yake na yakatokea yaliyotokea, Uthman akauawa na watu wakazuwia asizikwe kwa muda wa siku tatu. Hatimaye walikuja watu wanne miongoni mwa Banu Ummayyah kutaka kumsalia, baadhi ya Masahaba wakawazuwia kumsalia, basi mmoja wao

1. Ansabid-Ashraf, juz. 5 uk. 54.
2. Tarikh Al-Ya'aqubi, juz. 2 uk.147.

akasema: "Mzikeni hivyo hivyo, kwani Mwenyezi Mungu na Malaika wake wamekwisha kumsalia." Masahaba wakasema: "Wallahi kamwe hatozikwa kwenye makaburi ya Waislamu." Wakamzika mahali palipokuwa pakiitwa (Houshi Kaukah) ambako Mayahudi walikuwa wakizika maiti wao, na Banu Umayya walipotawala wakaiingiza sehemu hiyo (ya Houshi Kaukah) ndani ya Baqii.

Hii ni sehemu ndogo tu ya historia ya Makhalifa watatu (yaani) Abubakr, Umar na Uthman, nayo pamoja na kuwa ni ndogo, hiyo ni kwa sababu tumekusudia kufupisha na kutoa baadhi tu ya mifano, lakini inatosheleza kuondoa pazia kuhusu zile fadhila zinazodaiwa na sifa zilizozushwa ambazo wao hao Makhalifa watatu hawazitambui wala hawakupata kuziotea ndoto zama za uhai wao.

**Swali** linaloulizwa hapa ni hili lifuatalo: Masunni wanasemaje juu ya ukweli huu?

**Jawabu:** liko kwa wenye kumbukumbu nalo ni: Ikiwa ukweli huu munaujua na hamuupingi kwa sababu vitabu vyenu ndivyo vilivyothibitisha juu ya ukweli huu pamoja na kuunyamazia, basi mtakuwa mmeuporomosha huo uzushi uliozuliwa kuhusu Ukhalifa huo unaosemekana kuwa ni wenye uongofu. Na mkiwa mwakanusha ukweli huu na hamuamini kuwa ni ukweli, mtakuwa mmeviangusha vitabu vyenu ambavyo mnaamini kuwa ni vitabu sahihi, vitabu ambavyo vimeandika maelezo haya. Na kwa kufanya hivyo mtakuwa mmezitupa chini itikadi zenu zote.

17

# WAULIZE WANAOFAHAMU

## MLANGO WA SITA

### YANAYOHUSU UKHALIFA

**Ukhalifa**: ni kitu gani?

Ukhalifa ni kile kitu ambacho Mwenyezi Mungu amekifanya kiwe ni mtihani kwa umma, nacho ndicho kile walichokigawa na kukipupia wenye tamaa, na ni kitu ambacho katika kukigombea damu zisizo na makosa zilimwagika, si hivyo tu bali kwa sababu ya huo ukhalifa baadhi ya Waislamu walikufuru, (matokeo yake) wakahadaiwa na wakatengana wao na njia iliyonyooka na kuwaingiza ndani ya moto wa Jahiim. Hatuna budi kuleta somo kwa ufupi kuhusiana na Ukhalifa, somo ambalo pamoja na ufupi wake litazingirwa na mambo yaliyojificha na utata ambao Ukhalifa ulikuwa ndio uwanja wa utata huo muda kidogo kabla na baada ya kutawafu Mtume **(s.a.w.w)**. Kitu cha kwanza ambacho kinakuja haraka katika akili ni kwamba, suala la uongozi kwa Waarabu lilikuwa miongoni mwa mambo ya lazima katika kila zama. Utawaona wao wakimtanguliza kiongozi wa kabila au kiongozi wa familia juu ya nafsi zao (awaongoze). Basi huwa hawaamui jambo lolote wala hawatumii maoni yoyote mpaka kwanza wamshauri kiongozi wao, na wala hawamtangulii kwa kauli yoyote ile.

Basi kiongozi huyu wa ukoo mara nyingi huwa ni mkubwa kwa umri na mjuzi wao katika mambo na ni mtukufu wao kwa nasaba. Na inadhihiri kwamba, kiongozi huyu hujitokeza kufuatia matukio ndani ya ukoo wake, na miongoni mwa mambo ambayo hujitokeza kwake ni kama vile kuwa na akili tambuzi, ushujaa, ufahamu wa mambo, ukarimu kwa wageni na mengineyo miongoni mwa mambo matukufu, lakini mara nyingi (uongozi huu) hupatikana kwa njia ya kurithi na siyo kuchaguliwa. Baada ya hapo tunakuta kwamba, makabila na koo mbalimbali pamoja na kujitegemea kwake (kiuongozi), huwa yanautii uongozi wa kabila moja ambalo huenda likawa na idadi ya watu wengi, mali nyingi na linao mashujaa wanaojitosa katika vita na kuzilinda kabila nyingine. Mfano wa hilo ni Maquraishi ambao walikuwa wakiyaongoza makabila mengine ya kiarabu yaliyokuwa yakiwatii kuwa ni viongozi na mabwana ambao uongozi wao ulilazimika kutokana na wao kuwa ndiyo walinzi wa nyumba tukufu ya Mwenyezi Mungu.

Na ulipokuja Uislamu, Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** aliuthibitisha mfumo huu kwa kiwango fulani katika mahusiano, kwani alikuwa akimtawalisha juu ya makabila yaliyokuwa yakimfikia na kuukubali Uislamu, kiongozi wao na mbora wao ili awe ni msimamizi atakayewasalisha na kukusanya zaka zao na huwa yeye ndiye kiungo baina yao na Mtume. Hatimaye Mtume Muhammad **(s.a.w.w)**, kutokana na amri ya Mwenyezi Mungu alianzisha dola ya Kiislamu ambayo maamuzi yake na mafunzo yake yatatii wahyi unaomshukia Mtume kutoka kwa Mwenyezi Mungu, ukiwa ndio muongozo wa jamii na ni muongozo kwa mtu binafsi, muongozo huo ukiwa unahusu kufunga ndoa na talaka au kuuza na kununua, kupokea na kutoa, mirathi na zaka na yote yanayomhusu mtu

binafsi na jamii katika wakati wa vita na wakati wa amani. Hii ikiwa na maana kwamba mahusiano na ibada zote zitii hukumu za Mwenyezi Mungu, na jukumu la Mtume **(s.a.w.w)** ni kufikisha na kuwa macho katika kutekeleza hukumu hizo.

Na katika hali ambayo ni ya kimaumbile ni kwamba, bila shaka Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa akifikiri juu ya mtu atakayemrithi katika jambo hili muhimu na tukufu, na hilo si jingine bali ni uongozi kwa umma. Ni katika hali ile ile ya kimaumbile kwa kila kiongozi wa dola yoyote ile lazima aone umuhimu (iwapo analithamini Taifa lake) wa kuwepo mtu atakayemchagua awe naibu wake kwa kila majukumu ambayo yeye atapokuwa hayupo huyo mtu ayasimamie, na atakuwa ni waziri wake wa mwanzo na aliye karibu naye. Na ni kawaida ya maumbile vile vile, naibu wake huyu awe anatambulikana kwa mawaziri wote kadhalika mbele ya taifa. Haiwezekani kabisa, wala akili haiwezi kuamini kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** aliyapuuza yote haya na wala hakuyathamini, na hapana shaka kwamba yeye Mtume ilikuwa ndilo jambo limsumbualo. Hapana shaka kwamba hadithi zinazolihusu jambo hili ziligandamizwa kutokana na vikwazo vilivyowekwa na Makhalifa ambao walikuwa wakiongoza kwa nadharia ya Shura, na ndiyo wao waliofanya kila juhudi kuyapinga maandiko na matamko yaliyombainisha na kumtambulisha Khalifa. Na katika juhudi hizo pia kulifanyika (namna ya) kuutia kombo utukufu wa Mtume **(s.a.w.w)** na kumtuhumu kuwa anaweweseka.

Hatimaye akatiwa dosari yeye Mtume na Kiongozi aliyemtawalisha kushika uongozi wa jeshi kwa madai kwamba hafai uamiri na uongozi kwa sababu ya umri wake mdogo, kisha kuwatia shaka (watu) juu ya kufariki kwa Mtume **(s.a.w.w)** ili mambo yavurugike na watu wasije kuwahi kwenda kumpa baia Khalifa aliyebainishwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu tangu hapo kabla. Na kwa njama hizo waliweza kufanya mkutano uliojitokeza ghafla huko kwenye Saqifa, wakati Imam Ali na wafuasi wake wakishughulika kuandaa mazishi ya Mtume **(s.a.w.w)**, wao wakamchagua yule wanayemtaka na nafsi zao zikaridhika na kuimarisha mategemeo yao kwa huyo waliyemchagua. Kilichofuatia ilikuwa ni kuwalazimisha watu wote kula kiapo cha utii huku wakionywa na kutishwa na kuahidiwa (chochote kitu kwa wenye kukubali) na kuonywa (kuadhibiwa kwa watakaopinga), na kisha kuupiga marufuku upinzani wa aina yoyote katika uwanja na siasa.

Hatimaye ikafuatia kusimama imara bila samahani dhidi ya kila yule ambaye nafsi yake inamshawishi kuvunja kiapo cha utii au atakayetia mashaka kuhusu uhalali wa Ukhalifa mpya hata kama atakuwa ni Fatmah binti ya Mtume. Ilifuatia kuweka vikwazo na kuzizuwia moja kwa moja hadithi tukufu za Mtume zote, ili zisije zikasambaa miongoni mwa watu na mambo yakavurugika, hata kama jambo hilo litalazimu maisha ya mtu au mauaji ya kikundi fulani ili kuzimisha upinzani kwa madai ya kuondosha fitna kwa upande mmoja na kuritaddi kwa upande mwingine. Yote hayo tumeyatambua kwa kupitia yale waliyoyaandika wanahistoria, japo baadhi yao wanajaribu kuuficha ukweli kwa kuweka riwaya zinazogongana au kuweka tafsiri na nyudhuru ambazo utafiti na matukio vimekwisha kuuweka wazi.

Huenda baadhi yao wakasameheka, kwani kuna aliyechukua elimu yake kutoka ndani ya rejea ambazo ziliandikwa chini ya athari za kisiasa na kijamii, athari ambazo ziliachwa na ile fitina kubwa, na ikafuatiwa na matukio mbali mbali wakati Banu Umayyah walipoutawala Ukhalifa na wakawapa mali na vyeo baadhi ya Masahaba na tabiina waliofuatia ambao walikuwa wameajiriwa (kutengeneza riwaya za uongo). Kuna baadhi ya wanahistoria ambao waliochukua habari kutoka kwa watu hawa kwa dhana zao nzuri tu juu ya watu hawa, hali ya kuwa hawafahamu hiyana yao na yaliyojificha ndani ya nyoyo zao, basi ndipo zilipochanganyika riwaya sahihi na zile za uongo, na ni vigumu kwa mchunguzi kuufikia ukweli. Ili kumsogeza karibu msomaji anayetafiti kutaka kupata ukweli, hapana budi kuyaleta maswali haya ili ibainike kwa kupitia maswali hayo au majibu yake angalau sehemu ya ukweli au sehemu ya maelekezo ambayo yatamfikisha kwenye ukweli. Maswali na majibu ambayo anayetafuta ukweli haifai kuyaacha.

Zilinifikia barua nyingi kutoka miji mbali mbali, barua ambazo ndani yake kulikuwa na maswali muhimu yanayoonesha hamu kubwa ya wasomaji watukufu kutaka kuchunguza zaidi na kuufuatilia ukweli. Nami nilizijibu baadhi ya barua hizo na nyingine niliziacha siyo kwa sababu ya kuzidharau lakini ni kwa kuwa majibu yake yamo ndani ya kitabu changu kiitwacho; Thummah-tadaitu na kile kingine kiitwacho; Liakuna Maas-sadiqin. Na ili kuongeza faida basi nina yaaridhi maswali hayo ndani ya mlango huu pamoja na majibu yake na ninaambatisha pia ufafanuzi, kwani huenda msomaji akakuta baadhi ya hadithi na matukio yamerudiwa ndani ya kitabu kimoja au ndani ya vitabu vitatu kwa namna mbali mbali.

**Swali la 1**

Ikiwa Mtume alikuwa anafahamu matokeo yatakayoufika umma wake miongoni mwa migogoro na hitilafu kwa sababu ya Ukhalifa, ni kwa nini basi hakumbainisha Khalifa wake? Nimefanya hivyo makusudi nikifuata mwongozo wa Kitabu kitukufu cha Mwenyezi Mungu ambacho hukariri kueleza tukio katika sura kadhaa ili liimarike ndani ya akili ya muumini na liwe katika hali ya uwezekano wa kufahamika na wote.

**Jawabu**: Bila shaka Mtume **(s.a.w.w)** alimbainisha Khalifa wake baada ya Hijja yake ya mwisho. Khalifa huyo ni Ali ibn Abi Talib, na aliwashuhudisha-Masahaba wake ambao walihiji pamoja naye na alikuwa akitambua kwamba umma utamfanyia hiyana na utarudi kinyume nyume kwa visigino vyake.

**Swali la 2**

Ni vipi hakuna Sahaba yeyote miongoni mwa Masahaba wa Mtume aliyemuuliza Mtume kuhusu jambo hili wakati ambapo walikuwa wakimuuliza kila kitu?

**Jawabu**: Bila shaka walimuuliza na alitoa jawabu: Mwenyezi Mungu anasema:

يَقُولُونَ هَل لَّنَا مِنَ الْأَمْرِ مِن شَيْءٍ قُلْ إِنَّ الْأَمْرَ كُلَّهُ لِلَّـهِ ...﴿١٥٤﴾

"Wanasema, je sisi tunayo amri juu ya jambo hili, waambie amri yote ni ya Mwenyezi Mungu" (Qur'an, 3:154).

Na walimuuliza naye akasema:

إِنَّمَا وَلِيُّكُمُ اللَّـهُ وَرَسُولُهُ وَالَّذِينَ آمَنُوا الَّذِينَ يُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَهُمْ رَاكِعُونَ ﴿٥٥﴾

"Hakika Walii wenu (msimamizi) ni Mwenyezi Mungu na Mtume wake na wale walioamini ambao hutoa zaka hali yakuwa wamerukuu" (Qur'an, 5:55).

Na walimuuliza tena akasema: "Hakika huyu ni ndugu yangu na ni Wasii wangu na ni Khalifa wangu baada yangu".

**Swali la 3**

Ni kwa nini baadhi ya Masahaba walimpinga Mtume wa Mwenyezi Mungu pale alipotaka kuwaandikia maandiko ambayo yatawalinda wasipotee baada yake na wakasema kuwa anaweweseka?

**Jawabu**: Ni kweli kabisa kwamba Masahaba walimpinga Mtume **(s.a.w.w)** pale alipotaka kuwaandikia maandiko ambayo yatawalinda wasipotee na wakamtuhumu kuwa anaweweseka.

Hali ilitokea baada ya wao kufahamu kuwa yeye anataka kumbainisha Ali ibn Abi Talib katika maandiko hayo, kwani hapo kabla alikwisha kuwaambia wakati wa hija ya mwisho ya kuwa washikamane na kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi chake na hawatopotea kamwe, hivyo basi walifahamu kabisa kwamba madhumuni ya maandiko hayo yatakuwa ndiyo maneno yale, kwa kuwa Ali ndiye kiongozi wa kizazi cha Mtume.

Kwa hiyo walimtuhumu kuwa anaweweseka ili matokeo yake aache kuandika hasa kutokana na vurugu na hitilafu zilizotokea kuhusu maandiko hayo kabla hajayaandika, na ikiwa Mtume anaweweseka (kwa mujibu wa itikadi yao) basi bila shaka maandiko yake yatakuwa ni upuuzi, kwa namna ilivyo hapa hekima inapelekea kutokuandika.

**Swali la 4**

Kwa nini Mtume hakusisitiza (kuendelea) kuandika maandiko hayo hasa kwa kuwa yatauhifadhi umma wa Kiislamu usipotee?

**Jawabu**: Haikuwa katika wasaa wa Mtume kuendelea kutaka kuandika maandiko hayo, kwa sababu kuhifadhika kutokana na upotofu kulikwishapingwa pale Masahaba wengi walipokubaliana kuwa yeye Mtume anaweweseka. Basi ndipo hayo maandiko yalipokuwa msingi wa kupotea badala ya kuwa yawe ni mlinzi dhidi ya upotofu, na lau Mtume **(s.a.w.w)** angelazimisha kuyaandika, basi yangetokea madai batili baada yake ambayo yangeleta mashaka hata kwenye kitabu cha Mwenyezi Mungu na maandiko ya Qur'ani.

**Swali la 5**

Kabla ya kufa Mtume **(s.a.w.w)** aliusia mambo matatu kwa kuyatamka, basi ni vipi sisi yametufikia mambo mawili na la tatu likapotea? Jawabu: Mambo yako wazi kwamba ule usia wa mwanzo ndiyo uliopotea kwa kuwa unahusu Ukhalifa wa Ali, na kwa kuwa Ukhalifa uliosimama ulizuwia jambo hilo lisizungumzwe, vinginevyo mtu mwenye akili ataaminije kuwa Mtume aliusia kisha usia wake ukasahaulika kama alivyoeleza Bukhari?

**Swali la 6**

Je, Mtume **(s.a.w.w)** alikuwa akifahamu muda wa kifo chake?

**Jawabu**: Bila shaka alikuwa akifahamu tangu hapo mwanzo muda wa kufa kwake kwa wakati uliopangwa na alilifahamu hilo kabla ya kutoka

kwenda hija yake ya mwisho na kwa ajili hiyo aliita Hija ya kuaga, na kwa ajili hiyo wengi wa Masahaba walitambua kukaribia kwa mauti yake.

**Swali la 7**

Ni kwa nini Mtume **(s.a.w.w)** alitayarisha jeshi na akawajumuisha ndani ya jeshi hilo wakuu wa Muhajirina na Ansari miongoni mwa Masahaba wakubwa, na akawaamuru waende Mu'utah huko Palestina kabla ya kufa kwake kwa siku mbili?

**Jawabu**: Mtume **(s.a.w.w)** alipozitambua njama walizokuwa wamezipanga Maquraish na kwamba wameafikiana kupuuza usia wake baada yake na kumuondosha Ali kwenye Ukhalifa, alikusudia kuwatayarisha jamaa hawa ili wawe mbali na Madina wakati wa kufa kwake, basi hawatakuwa wamerudi ila baada ya kuwa jambo la Ukhalifa litakuwa limemkalia'vizuri Khalifa wake, na hawataweza baada yake kupitisha sera zao, hakuna tafsiri nyingine inayokubalika kuhusu jeshi la Usmah isipokuwa hii.

**Swali la 8**

Kwa nini Mtume **(s.a.w.w)** hakumchagua Ali kuwemo ndani ya jeshi la Usamah? Jawabu: Hiyo ni kwa sababu Mtume hawezi kuondoka ila aache Khalifa atakayeendesha mambo baada yake, na kwa kuwa Mtume **(s.a.w.w)** hakumchagua Ali kuwemo ndani ya jeshi ambalo ndani yake walikuwemo wakuu wa Kimuhajirina na Ansari ikwa ni pamoja na Abubakr, Umar, Uthman na Abdurrahman ibn A'uf, basi maamuzi haya yenye hekima yanatujulisha kuwa Ali ndiye Khalifa wa Mtume moja kwa moja, na kwamba wale wote ambao Mtume hakuwachagua kuwemo ndani ya jeshi hilo, hakuna mtu miongoni mwao aliyekuwa na tamaa ya Ukhalifa wala mwenye kumbughudhi Ali na kutaka kumfanyia hiyana.

**Swali la 9**

Kwa nini Mtume aliwawekea Kiongozi ambaye ni kijana mdogo asiyekomaa?

**Jawabu**: Ilivyokuwa mahasidi na wenye hiyana dhidi ya Ali wanalalamika juu ya umri wake mdogo na kuwa wakuu wa Kiquraishi ambao wamekwisha fikia miaka sitini hawataki kuongozwa na Ali mwenye umri ambao haujavuka miaka thelathini isipokuwa kidogo, basi Mtume **(s.a.w.w)** aliwawekea kiongozi ambaye ni Usama mwenye umri wa miaka kumi na saba wala hajakomaa na yeye alikuwa miongoni mwa watumwa waliopewa uhuru hiyo yote ilikuwa ni kuwalazimisha ili awabainishie kwanza wao wenyewe na pili Waislamu ya kwamba muumini wa kweli ndani ya Imani yake anawajibika kusikia na kutii japo atakuta ndani ya nafsi yake kuna uzito kwa yale aliyoyamua Mtume na anatakiwa atekeleze mara moja. Je, Usamaha ibn Zaid ibn Harithi anayo daraja kiasi gani mbele ya Ali ibn Abi Talib ambaye amiri jeshi wa waumini na Bwana wa Mawasii naye ndiye mlango wa Elimu ya Mtume **(s.a.w.w)** na ni simba wa Mwenyezi Mungu aliye mshindi, Haruna wa Muhammad **(s.a.w.w)**. Na kwa ajili hiyo basi walifahamu umuhimu wa Mtume kumpa Usamah uongozi juu yao ndipo walipoupinga uongozi wake na wakakataa kutoka wakamgomea, na wala hatusahau kwamba miongoni mwao walikuwemo wenye vitimbi ambao Qur'an imezungumza kuwahusu wao kama ifuatavyo:

وَقَدْ مَكَرُوا مَكْرَهُمْ وَعِندَ اللَّـهِ مَكْرُهُمْ وَإِن كَانَ مَكْرُهُمْ لِتَزُولَ مِنْهُ الْجِبَالُ ﴿٤٦﴾

"Na bila shaka walifanya hila zao (vitimbi vyao) na hila zao ziko kwa Mwenyezi Mungu (amezidhibiti) na hata kama vitimbi vyao hivyo vingeweza kuiondoa milima." (Qur'an 14:46).

**Swali la 10**

Kwa nini Mtume **(s.a.w.w)** aliwakasirikia mno wale waliogomea (jeshi la Usamah) mpaka akawalaanini?"

**Jawabu**: Bila shaka ghadhabu ya Mtume **(s.a.w.w)** ilizidi mno, pale alipofahamu kwamba wao wanamlaumu katika uteuzi wake wa amirijeshi. Lawama zilielekezwa kwa Mtume na wala siyo kwa Usamah, na hilo lilithibitika kwa Mtume pale walipokosa imani na ikhlasi kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake **(s.a.w.w)** na kwamba wao wameazimia kutekeleza sera zao kwa gharama yoyote ile itakayo wagharimu. Hali hiyo ndiyo ilyomfanya Mtume atoe laana yake ya mwisho kwa wale waliogomea ili awafahamishe wao na wafuasi wao na Waislamu wote kuwa sasa mambo yamefikia kikomo chake na aangamie mwenye kuangamia hali ya kuwa anajua.

**Swali la 11**

Je, inafaa kumlaani Muislamu hasa pale laana hiyo inapotoka kwa Mtume **(s.a.w.w)**?

**Jawabu**: Ikiwa Uislamu ni kutamka shahada mbili nazo ni mtu kusema kuwa: "Nakubali kwa moyo na ninatamka kwa ulimi kwamba, hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, na ninakubali kwa moyo na kutamka kwa ulimi kwamba Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, kisha mtu huyo asifuate maamrisho yao wala hamsikilizi wala kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake **(s.a.w.w)**, inafaa kumlaani mtu huyo, na ndani ya Qur'an tukufu zimo aya nyingi juu ya hilo, tunataja baadhi yake kama mfano: Mwenyezi Mungu anasema:

إِنَّ الَّذِينَ يَكْتُمُونَ مَا أَنزَلْنَا مِنَ الْبَيِّنَاتِ وَالْهُدَىٰ مِن بَعْدِ مَا بَيَّنَّاهُ لِلنَّاسِ فِي الْكِتَابِ أُولَـٰئِكَ
يَلْعَنُهُمُ اللَّـهُ وَيَلْعَنُهُمُ اللَّاعِنُونَ ﴿١٥٩﴾

"Bila shaka wale wanaoyaficha yale tuliyoyateremsha miongoni mwa mawaidha na uongofu baada ya kuwa tumeubainisha kwa watu, basi hao Mwenyezi Mungu anawalaani na wanalaaniwa na kila chenye kulaani." (Qur'an, 2:159).

Ikiwa Mwenyezi Mungu anamlaani mtu anayeuficha ukweli, basi unafikiria vipi kuhusu mtu anayeipinga haki na kufanya kila njia kuiharibu?

**Swali la 12**

Je, hivi Mtume **(s.a.w.w)** alimchagua Abubakar asalishe watu?.

**Jawabu**: Kwa kupitia riwaya mbali mbali zinazopingana tunafahamu ya kwamba, Mtume wa Mwenyezi Mungu hakumteua Abubakr awasalishe watu, isipokuwa kama tutayasadiki yale aliyoyasema Umar kuwa Mtume anaweweseka. Na yeyote mwenye kuyasadiki hayo basi bila shaka atakuwa kakufuru, vinginevyo ni kuwa ni vipi mtu mwenye akili atasadiki kuwa Mtume alimuamuru Abubakr awasalishe watu wakati ambapo alikuwa amemteua awemo ndani ya jeshi la Usamah na akamfanya huyu Usamah awe ndiyo Amiri na Imamu wake? Na itakuwaje ambainishe kuwa Imam kusalisha sala mjini Madina na hali yeye hakuwepo hapo, na wakati huo huo historia inashuhudia kwamba yeye Abubakr hakuwepo mjini Madina siku

Mtume alipofariki? Habari iliyothibitika ni kama walivyoeleza baadhi ya wanahistoria ambao Ibn Abil-hadid amepokea kutoka kwao kwamba, Ali (a.s) alimtuhumu bibi Aisha kuwa ndiye aliyemtumia ujumbe baba yake aje awasalishe watu, na Mtume alipolifahamu jambo hilo alikasirika na akasema: "Ninyi ndiyo wale wanawake waliomfanyia vitimbi Yusufu." Na ndipo Mtume alipotoka kwenda msikitini kisha akamuondosha Abubakr, kisha yeye mwenyewe akawasalisha watu sala ya mtu asiyejiweza ili asije akawaachia hoja baada ya hilo.

**Swali la 13**

Ni kwa nini Umar aliapa kuwa Mtume **(s.a.w.w)** hajafariki na akatishia kumuua yeyote yule atakayesema kuwa Mtume amefariki, na hakutulizana ila baada ya kuwasili kwa Abubalcr?

**Jawabu**: Umar alitishia kumuua yeyote yule atakayejaribu kusema kuwa Mtume **(s.a.w.w)** amefariki ili awatie mashaka Waislamu na awaache wakihangaika (wamechanganyikiwa) kusudi baia ya Ali isitimie, na ili wapate kufika mjini Madina wale mashujaa wa upinzani ambao walikuwa wamekubaliana naye kuuchukua uongozi, kwani walikuwa bado hawajafika. Na kwa kuwa Umar alijikuta amewatangulia wenzake, aliitumia fursa hiyo kufanya mbinu ya kuwasahaulisha kisha akachomoa upanga wake akawatisha watu. Hapana shaka kwamba yeye aliwazuwia watu kuingia kwenye chumba cha Mtume ili wakajithibitishie hali ya mambo ilivyo, vinginevyo ni kwa nini basi hakuna hata mtu mmoja aliyethubutu kuingia isipokuwa Abubakr alipofika, yeye aliingia akaufunua uso wa Mtume kisha akatoka ili aje awaambie watu kwamba: "Yeyote aliyekuwa akimuabudu Muhammad basi Muhammad amekwisha kufa, na aliyekuwa akimuabudu Mwenyezi Mungu basi Mwenyezi Mungu yu hai na hatokufa."

Hapa tunalazimika kufafanua kidogo kauli hii ya Abubakr. Je, hivi ni kweli kwamba Abubakr alikuwa akiamini kwamba miongoni mwa Waislamu yuko aliyekuwa akimuabudu Muhammad? Sivyo kabisa, isipokuwa hii ni sentensi ya majazi ambayo ilikusudiwa kuwashutumu na kuwadhalilisha Ali ibn Abi Talib kwa upande mmoja, na kwa ujumla Bani Hashim wote ambao walikuwa wakiona fahari mbele ya Waarabu wengine kwa kuwa mjumbe wa Mwenyezi Mungu Muhammad **(s.a.w.w)** anatokana nao na wao ni watu wake na ni jamaa zake na ndiyo wenye haki mno kwake kuliko watu wengine. Pia hiyo ni kauli inayotoa maelezo ya yale aliyoyatamka Umar ibn Khattab siku ile ya msiba wa siku ya al-hamisi pale Umar aliposema: "Kinatutosha kitabu cha Mwenyezi Mungu." Na ukweli halisi ulivyo ni kuwa, yeye Umar alikuwa na maana kwamba hatuna haja na Muhammad, kwani mambo yake yamefikia ukingoni na zama zake zimekwisha pita.

Bila shaka hiki ndicho alichokitilia mkazo Abubakr kwa kusema: "Yeyote aliyekuwa akimuabudu Muhammad basi yeye kisha kufa," ambapo makusudio yake yalikuwa na kwamba, Enyi mliokuwa mkijifaharisha juu yetu kwa Muhammad leo bakieni nyuma kwani mambo yake yamekwisha, sisi kinatutosha kitabu cha Mwenyezi Mungu kwani kiko hai hakitakufa. Na kwa ufafanuzi zaidi ni kuwa, Ali na Bani Hashim wao ndiyo waliokuwa wakifahamu vyema kuliko watu wengine juu ya uhakika wa Mtume **(s.a.w.w)** na walikuwa wakimheshimu mno na kumtukuza, na pia

kutekeleza maamrisho yake na waliofuatia katika hili ni wale waliopewa uhuru (baada ya kuwa watumwa) miongoni mwa Masahaba na wale waliokuwa siyo miongoni mwa Maquraish, watu hao ilikuwa Mtume akitema mate huyakimbilia na kujipangusia usoni mwao, na hugombea mabaki ya maji ya udhu wake au nywele zake na wote hawa ni wale masikini na wanyonge ambao walikuwa ndiyo Mashia (wafuasi) wa Ali tangu zama za uhai wa Mtume **(s.a.w.w)** naye ndiye aliyewaita jina hili.

Ama Umar ibn Khatab na baadhi ya Masahaba miongoni mwa vigogo wa Kiquraishi, mara nyingi walikuwa wakipinga maamuzi ya Mtume **(s.a.w.w)** na wakimjadili na kumuasi, bali wakijiepusha na matendo yake na bila shaka Umar aliukata mti wa Baia'tur-ridh-wan kwa kuwa baadhi ya Masahaba walikuwa wakitabaruku kwenye mti huo, kama walivyofanya Mawahabi katika karne hii, kwani wao wameondosha kumbukumbu za Mtume **(s.a.w.w)** hata ile nyumba ambayo alimozaliwa Mtume hawakuiacha, na sasa hivi wanajaribu kwa bidii zao na mali zao kuwazuwia Waislamu wasisherehekee kuzaliwa kwa Mtume, na wanazuwia kutabaruku kwa Mtume na kumsalia mpaka wameeneza fikra kwa watu wasiofahamu kuwa, kumsalia Mtume **(s.a.w.w)** sala yake kamilifu ni ushirikina.

**Swali la 14**

Ni kwa nini Maansari walikusanyika kwa siri ndani ya Saqifatu Bani Saidah?

**Jawabu**: Wakati Ansari walipozigundua njama zilizokuwa zimepangwa na Maquraishi za kumuondoa Ali kwenye Ukhalifa, Mtume alipofariki walikusanyika na wakataka kulipitisha suala la Ukhalifa kati yao, ili Khalifa atoke miongoni mwao. Na iwapo wakuu wa Kiquraishi ambao ndiyo muhajirina wako karibu ya Mtume na ni jamaa zake nao wanataka kutengua baia ya Ali, basi Ansari wana haki zaidi kuchukua Ukhalifa kuliko mwingine asiyekuwa wao kutokana na kuitakidi kwao kwamba Uislamu uliimarika kwa ukali wa panga zao, na kwamba Muhajirina wanawategemea wao kwani kama si wao Ansari kuuteka mji wao na makazi yao na kila walichokuwa wanakimiliki basi Muhajirina wasingeweza kuwa na ubora wala utajo wowote. Lau si kuwepo kutofautiana baina ya kabila la Ausi na Khaz-raji ambao walikuwa wakishindania uongozi ikawa kila mmoja wao anautaka Ukhalifa uende kwenye kabila lake, basi Abubakr na Umar wasingekuwa na fursa ya kuuchukua Ukhalifa kutoka kwa Maansari na wangelazimika kuwafuata Maansari.

**Swali la 15**

Kwa nini Abubakr, Umar na Abu Ubaidah walikimbilia Saqifah na wakawavamia Maansari?

**Jawabu**: Ilivyokuwa Muhajirina, yaani wakuu wa Kiquraishi wanao watu wanaofuatilia nyendo za Maansari na kile kinachofanyika katika mipango yao, basi mmoja wao hao Maquraishi ambaye ni Salim aliyekuwa mtumwa wa Abu Hudhaifah alifanya haraka kuwajulisha kina Abubakr, Umar na Abu Ubaidah kuhusu mkutano huo wa siri. Basi ndipo walipokimbilia huko Saqifah ili wakawavuruge Maansari na mipango yao waliyokwisha kuipitisha na wawavamie na kuwa wao (Maquraishi) wanajua kila kitu kinachotokea wakati wao hawapo.

**Swali la 16**

Kwa nini Umar ibn Khatab njia nzima alikuwa akiandaa kauli itakayowakinaisha Maansari?

**Jawabu**: Hapana shaka kwamba Umar ibn Khatab alikuwa akichelea upinzani wa Maansari, kama ambavyo alikuwa akichelea pia kwamba Maansari hawatakubali kumuweka mbali Ali (kwenye Ukhalifa) jambo ambalo litasababisha kubomoka kwa yale waliyoyapanga na kuyaandaa, hivyo basi juhudi zao zitapotea bure baada ya kuwa walithubutu kukifanya mbele ya Mtume mwenyewe na wakaharibu mipango yake yote kuhusu Ukhalifa. Kwa ajili hiyo basi Umar katika njia yake kuelekea Saqifa alikuwa akitunga nini atakachokisema ili wamuunge mkono na waikubali sera aliyoiandaa yeye Umar na wenzake.

**Swali la 17**

Kwa nini Muhajirina waliwashinda Maansari na wakampa Abubakr Ukhalifa?

**Jawabu**: Yako Mambo mengi yaliyotendeka katika kuwarudisha nyuma Maansari na kuwafanya Muhajirina wafaulu. Maansari walikuwa makabila mawili yanayogombea uongozi tangu zama za jahiliya (kabla ya Uislamu), na ugomvi wao ulitulizana kwa kuwepo Mtume **(s.a.w.w)** miongoni mwao. Katika kipindi hiki Mtume alikuwa kesha kufa na ummati wake unataka kuupora Ukhalifa kutoka kwa muhusika wake kisheria, basi hapo ndipo Ausi waliponyanyuka wakimpendekeza kwa ajili ya Ukhalifa kiongozi wao Sa'ad ibn Ubbadah, lakini Bashir ibn Sa'ad ambaye aliyekuwa kiongozi wa Khaz-raj akamhusudu mwana wa ammi yake na akafanya kila njia kuhakikisha kuwa Sa'ad ibn Ubbadah hatoupata Ukhalifa. Aliyavunja mapatano ya Ansari na kujiunga kwa Muhajirina na akijifanya kuwa mwaminifu na mtoa nasaha njema.

Kama ambavyo Abubakr naye aliiamsha fitna ya zama za kijahiliya kati yao alipogonga kwenye nukta dhaifu pale aliposema: "Lau jambo hili tutawapa ukoo wa Ausi, ukoo wa Khaz-raji hawatoridhia na tutapowapa Khaz-raji basi Ausi nao hawatoridhia." Kisha akawapa tamaa ya kuwagawia sehemu ya serikali akasema: "Sisi ni maamiri nanyi muwe mawaziri na kamwe hatutayaacha maoni yenu."

Hatimaye kwa kutumia akili alifanya hila ya kuwa yeye ni mtoa nasaha mwaminifu kwa umma wakati yeye alipojitoa na kuonyesha kutokuwa na haja ya Ukhalifa na kwamba yeye hapendelei kuwa Khalifa akasema: "Mchagueni mumtakaye kati ya watu hawa wawili yaani Umar au Abu Ubaidah A'mir ibn Jarrah." (Wakati huo) mipango ilikuwa imeandaliwa vizuri na utaraibu (huo) ulifaulu, basi Umar na Abu Ubaidah wakasema: "Haiwezekani sisi kukutangulia wewe, wewe ni wa mwanzo kusilimu, nawe ndiwe mwenzi wa Mtume katika pango basi kunjua mkono wako tule kiapo cha utii kwako. Hapo hapo Abubakar akanyoosha mkono wake kutokana na maneno haya, na Bashir ibn Sa'ad kiongozi wa kabila la Khaz-raj alitangulia kumpa baia Abubakr na wengine waliobakia nao wakafuatia isipokuwa Sa'ad ibn Ubbadah.

**Swali la 18**

Ni kwa nini Sa'ad ibn Ubbadah alikataa kumbai Abubakr kisha Umar naye akamtishia kumuua Sa'ad?.

**Jawabu**: Maansari walipotoa baia na wakamkimbilia Abubakr kwa ajili ya kutaka kujipatia heshima na ujamaa kwa Khalifa huyo, Sa'ad alikataa kutoa baia na alijaribu kwa juhudi zake kuwazuwia watu wake wasitoe baia, lakini alishindwa kwa sababu alikuwa mgonjwa sana kalala kitandani na sauti yake haisikiki, hapo ndipo Umar aliposema: "Muuweni, hakika huyu ndiye mwenye fitna (muuweni) ili mzizi wa upinzani ung'olewe ili asije akapinga baia hii mtu mwingine, kwani huyu atavunja umoja wa Waislamu na atasababisha kugawanyika kwa umma na ataleta fitina."

18

# WAULIZE WANAOFAHAMU

## TISHIO LA KUCHOMA MOTO NYUMBA YA BIBI FATIMA

**Swali la 19**

Ni kwa nini walitishia kuichoma moto nyumba ya bibi Fatimah?

**Jawabu**: Idadi kubwa ya Masahaba ambao hawakumpa baia Abubakr walibakia ndani ya nyumba ya Ali ibn Abi Talib, na lau Umar asingefanya haraka kuizunguka nyumba hiyo na kutishia kuichoma moto, basi jambo hilo lingepata nguvu na umma ungegawika makundi mawili moja la Ali na lingine la Abubakar. Lakini Umar kwa ajili ya kupasisha jambo lililokwisha tokea alitazama mtazamo wa mbali pale aliposema, "Lazima mtatoka kwenda kutoa baia la sivyo nitaichoma moto nyumba hii na waliomo, akikusudia Ali na Fatmah binti ya Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**." Na kwa kauli hii basi hakuweza kubakia katika watu yeyote ambaye nafsi yake inamtuma kuuvunja utiifu na akose kuingia katika baia. Basi je, ni utukufu gani mkubwa (uliokuwepo zama hizo) kuliko utukufu wa mwanamke bora ulimwenguni (Fatmah) na mumewe ambaye ni Bwana wa mawasii?

**Swali la 20**

Ni kwa nini Abu Sufiyan alinyamaza (asiseme kitu) pale Umar alipowatishia na kuwaonya?

**Jawabu**: Wakati Abu Sufiyan aliporejea Madina baada ya Mtume **(s.a.w.w)** kufariki, kwani Mtume alikuwa amempeleka Abu Sufiyan kwenda kukusanya zaka alishitukizwa na Ukhalifa wa Abubakr, na haraka alikwenda nyumbani kwa Ali ibn Abi Talib akamchochea afanye mapinduzi na awapige vita jamaa hao hali ya kuwa akimuahidi (kumsaidia) mali na watu. Lakini Ali (a.s) alimfukuza kwa kutambua nia yake, naye Abubakr na Umar walipofahamu jambo hilo walimwendea Abu Sufiyan wakamlainisha na kumuahidi kumpa kila kitu alichokikusanya katika sadaka hizo na kumshirikisha katika Ukhalifa kwa kumchagua mwanawe kuwa Gavana wa Sham. Basi Abu Sufiyan aliridhika na hayo na akawanyamazia, ndipo wakamchagua Yazid ibn Abi Sufiyan kuwa Gavana wa Sham, na alipokufa wakamteua nduguye Muawiyah ibn Abi Sufiyan achukue mahali pake na wakamuwezesha huyu Muawiyah kuufikia Ukhalifa.

**Swali la 21**

Je, Imam Ali aliridhia jambo hilo na akawapa baia jamaa hao?

**Jawabu**: Hapana kamwe Imam Ali hakuridhia jambo hilo na hakunyamaza bali alitoa hoja dhidi yao kwa kila kitu na hakukubali kuwapa baia licha ya vitisho vyao na maonyo. Ibn Qutaibah ameeleza ndani ya kitabu chake cha historia kwamba Imam Ali aliwaambia: "Wallahi sikupeni baia, ninyi ndio wenye haki kunipa baia mimi." Bali alimchukua mkewe bibi Fatmah akapita naye kwenye vikao vya Maansari, nao wakawa wanatoa sababu (kwa kusema) kwamba Abubakar amewawahi. Bukhari ameeleza kuwa Imam Ali hakutoa baia muda wote wa uhai wa bibi Fatimah, alipofariki bibi Fatmah na watu wakampuuza Imam Ali alilazimika kufanya sulhu na Abubakr, na Bibi Fatimah aliishi kwa muda wa miezi sita baada ya

kifo cha Baba yake, Sasa je, bibi Fatmah alifariki akiwa hana baia wakati ambapo baba yake ambaye ni Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: "Yeyote atakayekufa na hali ya kuwa hana baia basi atakufa mauti ya kijahiliya."

Na Je, Ali alikuwa anafahamu kwamba yeye ataishi mpaka baada ya Abubakr, basi akachelewa kumbai kwa muda huo wa miezi sita? Ifahamike kwamba, Ali hakunyamaza muda wote wa uhai wake, kwani kila alipopata fursa hukumbusha dhulma aliyofanyiwa na kuporwa haki yake, na hiyo inatosha kuwa ni dalili ya yale aliyoyasema kwenye hotuba yake inayojulikana kama hotuba ya Shaqshaqiyyah.

**Swali la 22**

Ni kwa nini walimchukiza na kumkasirisha bibi Fatmah wakati haja yao ilikuwa ni kuleta sulhu?

**Jawabu**: Bila shaka walikusudia kumchukiza bibi Fatmah kwa kumnyang'anya ardhi yake na milki zake na wakamnyima mirathi ya baba yake na wakayakanusha madai yake yote kiasi cha kumuondolea heshima yake na utukufu wake miongoni mwa watu kiasi wasimuamini endapo atachokoza kwa kuleta madai kuthibitisha matamko yanayohusu Ukhalifa. Na ndio maana Maansari walimtolea udhuru kwamba baia yao ameiwahi Abubakr, na lau mumewe (Ali) angewahi wasingempinga. Kwa ajili hiyo bibi Fatmah alimkasirikia mno Abubakr na Umar mpaka akawa huwaapiza katika kila sala anayoisali, na alimuusia mumewe kwamba asihudhurie jeneza lake yeyote miongoni mwao na amuepushe kabisa na watawala hao ambao yeye bibi Fatmah anawachukia. Na kwa hakika walikusudia kumuudhi ili wamuonyeshe Ali kuwa yeye ni dhaifu juu yao kuliko binti ya Mtume ambaye ndiye mwanamke bora ulimwenguni na ambaye Mwenyezi Mungu hukasirika kutokana na kukasirika kwake na huridhia kutokana na kuridhia kwake (Fatmah), kwa hiyo (Ali) hakuwa na la kufanya isipokuwa kunyamaza.

**Swali la 23**

Ni kwa nini wakuu wa Kiquraish waligomea jeshi la Usamah?

**Jawabu**: Pindi mambo yalipokuwa yamemkalia vizuri Abubakr na akawa ndiye Khalifa wa Waislamu kutokana na juhudi za Umar licha ya kutoridhika kwa wapinzani, Abubakr alimtaka Usamah asimchukue Umar ibn Khatab ili abakie akimsaidia kwenye mambo ya utawala, kwani yeye peke yake hawezi kuyakamilisha na hapana budi awe na watendaji ambao ni wenye nguvu na ususuavu ambao walimpinga Mtume **(s.a.w.w)** na wala hawakujali ghadhabu za Mwenyezi Mungu wala laana ya Mtume **(s.a.w.w)** kwa yule atakayegomea jeshi la Usamah miongoni mwa wale aliowateua yeye mwenyewe Mtume. Hapana shaka kwamba waliopanga kufanikisha suala hili (la Ukhalifa) ndiyo waliogomea jeshi la Usamah ili wapate kufanikisha jambo lao na kusaidiana kuimarisha misingi yao.

**Swali la 24**

Je, ni kwa nini Imam Ali (a.s) alitengwa katika kila jambo na wala hawakumshirikisha kwa lolote lile?

**Jawabu**: Halihalisini kwamba jamaa hao waliwakumbatia watu wengi miongoni mwa wale walioachwa huru (siku ya Fat-hi Makkah) na wakawapa vyeo ndani ya serikali yao kwa kuwashirikisha kwenye Ukhalifa

na wakawateua miongoni mwao wawe maamiri na watawala katika bara Arabu yote na katika kila miji ya Kiislamu. Miongoni mwa hao walioteuliwa ni Al-walid ibn Uqbah, Marwan ibn Al-hakam, Muawiyah na Yazid watoto wa Abu Sufiyan, Amri ibn Al-a's, Mughirah ibn Shu'ubah, Abu-hurairah na wengi wengineo ambao walikuwa wakimkera Mtume wa Mwenyezi Mungu. Lakini Ali walimtenga na kumpuuza wakamuacha kajifungia nyumbani kwake, wala hawakumshirikisha kwa lolote katika utawala wao kwa muda wote wa robo karne ili wamdhoofishe na kumdharaulisha na wawafanye watu wasimthamini, kwani watu ni watumwa wa dunia wanamfuata aliye na (nguvu za) utawala na cheo na mali. Na maadam Ali alikuwa hapati chakula chake cha siku moja isipokuwa kwa pato litokanalo na mkono wake na jasho lake, basi kwa vyovyote vile watu watamkimbia na wala hawatamfuata. Na ndivyo ilivyokuwa, hakika Ali alibakia katika hali hiyo kwa muda wote wa Ukhalifa wa Abubakr, Umar na Uthman akiwa ndani, na wote hawa wakifanya kila namna kumdhalilisha na kuizima nuru yake na kuzificha fadhila zake na cheo chake. hali ya kuwa Imam Ali hana chochote cha kidunia kitakacho wafanya watu wampende.

**Swali la 25**

Ni kwa nini waliwapiga vita waliozuwia zaka pamoja na kuwa Mtume alikataza jambo hilo?

**Jawabu**: Hiyo ni kwa sababu baadhi ya Masahaba walihudhuria baia ya (kula kiapo cha utii kwa) Imam Ali huko Ghadir Khum wakati walipokuwa wakirudi kutoka kwenye Hija ya kuaga hali ya kuwa wamefuatana na Mtume **(s.a.w.w)** Kwa ajili hiyo walijizuwia kutoa zaka hiyo kwa Abubakr kwa sababu wao hawakuwepo katika kifo cha Mtume wala hawakuwepo kwenye matukio yaliyofuatia kifo cha Mtume hasa juu ya kubadilika Ukhalifa kutoka kwa Ali kwenda kwa Abubakr. Hali hii ilisababishwa na wengi wao kutokuwa wakazi wa Madina, na hapana shaka kuwa baadhi ya habari ziliwafikia ya kwamba bibi Fatmah (a.s) amekosana nao na amewakasirikia, na pia kwamba Ali (a.s) amekataa kuwapa baia, na kwa yote hayo basi walikataa kutoa zaka kwa Abubakr mpaka mambo yawabainikie.

Hapo ndipo Abubakr na Umar na watumishi wa utawala wao walipoafikiana wawapelekee jeshi chini ya uongozi wa Khalid ibn Walid ambaye alikuwa ndiyo upanga wao, akaenda akazima upinzani wao na kunyamazisha fikra zao. Si hivyo tu bali aliwaua wanaume zao na kuwateka wanawake zao na watoto wao ili iwe ni onyo kwa yeyote ambaye nafsi yake itamshawishi kutotii au kuitia dosari heshima ya dola.

**Swali la 26**

Ni kwa nini walizuwia hadithi za Mtume zisiandikwe?

**Jawabu**: Tangu siku za mwanzo walifanya kila njia kuzuwia hadithi za Mtume, siyo tu kwa sababu hadithi hizo zinahusiana na suala la Ukhalifa na ubora wa Imam Ali, bali ni kwa kuwa nyingi katika hadithi hizo zinapingana na maneno yao na vitendo vyao ambavyo walikuwa wakivitumia kuendeshea mambo ya maisha na kuimarisha utambulisho wa dola mpya waliyoizusha juu ya misingi yake kwa mujibu wa ij-tihadi zao.

**Swali la 27**

Je, Abubakr alikuwa anaweza kumudu jukumu la Ukhalifa?

**Jawabu**: Abubakr hakuwa na uwezo wa kumudu uzito wa Ukhalifa, na lau Umar ibn Khatab na baadhi ya wenye hila miongoni mwa wakuu wa Kibanu Umayyah mambo yangemshinda. Historia imeandika kwamba, Abubakar siku zote alikuwa akitii maamuzi na maoni ya Umar ibn Khatab aliyekuwa mtawala mtendaji. Dalili ya hilo ni kile kisa cha wale wanaoimarishwa nyoyo zao katika dini ambao walimjia Abubakr mwanzoni mwa Ukhalifa wake, akawaandikia barua na akawatuma waende kwa Umar ambaye mambo yanayohusu mali yalikuwa mkononi mwake. Basi Umar aliichana barua ile na akawafukuza, wakarudi kwa Abubakr wakamuuliza; "Hivi wewe ndiye Khalifa au yeye?" Akawajibu: "Ni yeye kwa mapenzi ya Mungu."

Kadhalika wakati Abubakr alipoigawa sehemu ya ardhi kumgawia Uyaynah ibn Hisn na Aqra'a ibn Habis, basi Umar akakataa alipoisoma barua ya Abubakr na akaitemea mate akaifuta. Watu wale wakarudi kwa Abubakr hali ya kuwa wanalalamika kutokana na aliyoyafanya Umar na wakamwambia: "Wallahi hatufahamu hivi wewe ndiye Khalifa au Umar." Akasema; "Bila shaka yeye ndiyo Khalifa." Umar alipofika hapo hali ya kuwa amekasirika na kumuhoji Abubakr kwa maneno makali juu ya kutoa kwake ardhi hiyo, Abubakr alimwambia Umar, "Hivi sikukuambia kwamba wewe una nguvu kuliko mimi juu ya jambo hili la Ukhalifa.? Hakika wewe umenizidi nguvu."

Bukhari ameandika ndani ya sahihi yake kwamba, Umar alikuwa akiwahimiza watu wambai Abubakr na husema: "Bila shaka Abubakr ndiye Mwenzi wa Mtume wa Mwenyezi Mungu na wa pili katika wawili (pangoni) na kwamba yeye ni mbora wa Waislamu kwa mambo yenu, basi simameni mumbai." Anas bin Malik anasema: "Nilimsikia Umar anamwambia Abubakr siku hizo, panda juu ya mimbari, hakuacha kumtaka apande mpaka akapanda juu ya mimbari na watu wote wakambai."

**Swali la 28**

Kwa nini Abubakr aliusia Ukhalifa kwa Umar kabla ya kufa kwake?

**Jawabu**: Hiyo ni kwa kuwa Umar ndiye aliyefanikisha kumtupa mbali Ali kutoka kwenye Ukhalifa, na ni kutokana na (yeye Umar) kuwa mpinzani mbaya wa Mtume **(s.a.w.w)** hapo mwanzo pia kwa namna alivyowaburuta Maansari wambai Abubakr na kuwalazimisha watu kwa nguvu kutoa baia mpaka mambo yakafikia kutishia kuchoma moto nyumba ya bibi Fatmah. Pia ni kwa kuwa yeye alikuwa ndiye Khalifa mtendaji kama tulivyotangulia kusema, yeye ndiye aliyekuwa na kauli ya mwanzo na ya mwisho, na hapana shaka kwamba yeye alikuwa miongoni mwa Waarabu wenye mtazamo wa mbali, kwa hiyo alifahamu kwamba Waislamu na hasa Maansari hawatakubali kumpa baia kutokana na tabia yake ya ukali na ususuavu na hasira zake za haraka haraka. Kwa sababu hizo basi akamtangulizi Abubakr kwa kuwa tabia yake ilikuwa ya upole na huruma naye amewatangulia kusilimu. Isitoshe Aisha bint yake Abubakr alikuwa ni mwanamke shupavu anayeweza kuyakabili mambo mazito na kubadilisha mambo, katika hali hiyo Umar alikuwa akitambua vyema kwamba Abubakr ni mfuasi wake na atatii maelekezo yake kwa kila atakalolipendekeza kwake.

Jambo hili halikuwa siri kwa Masahaba wengi juu ya yeye Abubakr kuusia Ukhalifa kwa Umar kutokana na maandiko yake, bila shaka Imam Ali alikwisha mwambia Umar tangu ile siku ya kwanza kuwa: "Leo hii mwandalie sehemu yake na umuimarishie, naye kesho atakurudishia." Kama alivyosema Sahaba mwingine kumwambia Umar wakati alipotoka na yale maandiko yaliyokuwa na usia wa Abubakr,(kisha Umar akajifanya kuwa hajui kilichomo, sahaba yule) akamwambia Umar, "Mimi nafahamu kilichomo, bila shaka wewe ulimtawalisha kipindi hicho cha kwanza naye amekutawalisha mwaka huu." Hivyo basi usia wa Abubakar kwa Umar ni jambo linaloeleweka kwa watu wote, na ikiwa Abubakr katika zama za uhai wake anakiri mbele ya watu wote kwamba Umar ana nguvu kuliko yeye, basi siyo ajabu kumpa utawala wakati wa kufa kwake.

Na kwa ajili hii inatubainikia kwa mara nyingine kwamba, yale wayasemayo Masunni kuwa Ukhalifa hauwezi kukubalika isipokuwa kwa njia ya mashauriano ni jambo ambalo halipo na wala halimo kabisa ndani ya mawazo ya Abubakr na Umar. Na ikiwa Mtume **(s.a.w.w)** alifariki na akaliacha jambo hili liwe katika mashauriano kati ya watu kama wanavyodai Masunni, basi bila shaka Abubakr alikuwa ni mtu wa mwanzo kubomoa msingi huu aliipinga Sunna ya Mtume **(s.a.w.w)** kwa kumuusia Umar baada yake.

Siku zote utawaona Masunni wanajinadi kwa fahari kubwa kwamba wao wanaamini mashauriano, na eti Ukhalifa haukubaliki isipokuwa kwa njia hiyo, na hukejeli kauli ya Mashia ambao wanaamini kuwa Ukhalifa haukubaliki isipokuwa utokane na maagizo yanayotoka kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake **(s.a.w.w)**.

Masunni wengi utawasikia wanaikosoa itikadi hii na kwamba ni kitu kilichoingizwa ndani ya Uislamu kutoka kwa Waajemi/Wairani ambao wanasema kuwa uongozi wa mambo ya Mwenyezi Mungu ni suala la urithi (wa kizazi maalum). Ni mara nyingi Masunni wanatolea ushahidi aya isemayo: "Na mambo yao ni kwa mashauriano kati yao." Na wanadai kwamba aya hiyo ilishuka kuhusu Ukhalifa na kwa dalili hii sisi tunayo haki ya kusema kwamba Abubakr na Umar walikwenda kinyume na kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna ya Mtume na hawakuvithamini vitu hivyo viwili kuhusu suala la Ukhalifa.

**Swali la 29**

Ni kwa nini Abdur-rahman ibn Auf alimuwekea sharti Imam Ali ibn Abi Talib kuwa ni lazima aongoze kwa mujibu wa Sunna ya Makhalifa hao wawili?

**Jawabu**: Miongoni mwa udhalili wa dunia mbele ya Mwenyezi Mungu, ni Abdur-Rahman ibn Auf kuwa mtu atakayeamua mustakabali wa umma wa Kiislam baada ya Umar, auchagulie umma mtu amtakaye yeye na amuondoshe asiyemtaka. Kamwe hilo haliwezekani, lakini yote hayo ilikuwa ni mipango ya Umar ambaye aliupatia kura ya turufu mkono wa Abdur-Rahman juu ya Masahaba wengine, na huyu Abdurrahman ibn A'uf yeye ni miongoni mwa Waarabu wenye vitimbi. Hapana shaka kwamba yeye ni miongoni mwa wajumbe wa kundi lililopanga mipango inayohusu Ukhalifa na namna ya kuuondosha kwa muhusika wake wa kisheria. Kwa kuwa Bukhari anakiri kwamba Abdur-rahman ibn Auf alikuwa akichelea

jambo fulani kwa Ali, basi moja kwa moja naye alifanya kila njia kumtenga Imam Ali mbali na Ukhalifa kwa namna yoyote atakayoiweza. Huyu Abdur-rahman ibn Auf anafahamu kama walivyokuwa wakifahamu Masahaba wengine kwamba Ali (a.s) alikuwa hakubaliani na ij-tihadi za Abubakr na Umar na yale waliyoyabadilisha miongoni mwa hukumu za kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna za Mtume **(s.a.w.w)**, na alikuwa akijaribu kwa uwezo wake kuwapinga na kuwakemea.

Kwa sababu hiyo basi, Abdur-rahman akamuwekea sharti Imam Ali kwamba aongoze kwa mujibu wa Sunna ya Abubakr na Umar hali ya kuwa anajua tangu mwanzo kuliko mtu mwingine kwamba Ali hajipendekezi wala hasemi uongo na wala sharti hilo kamwe hatalikubali, ni kama ambavyo pia Abdur-rahman alikuwa anajua ya kwamba Uthrnan ibn Affan ambaye mkwewe, Maquraishi na wajumbe wote wa mipango hiyo watamfurahikia akichukua Ukhalifa.

**Swali la 30**

Je, hadithi ya Maimamu kumi na wawili inapatikana kwa Msunni?

**Jawabu**: Bukhari na Muslim wameithibitisha hadithi hiyo pia wanachuoni wote wa hadithi wa Kisunni wameithibitisha hadithi ya Mtume **(s.a.w.w)** isemayo "Dini haitaacha kusimama hadi siku ya Qiyama mpaka wawepo Makhalifa kumi na wawili na wote ni Maquraishi. Na hadithi hii imebakia kuwa ni mushkeli mkubwa ambao hauna jibu kwa Masunni, hapana yeyote miongoni mwa wanazuoni wao aliyethubutu kuwahesabu (Makhalifa hao) baada ya wale Khulafau-rashidina wanne, na watano ni Umar ibn Abdil-aziz, sasa wanabakia katika idadi hiyo (Makhalifa) saba ambao hawapo.

Masunni hawana njia vinginevyo nao waukubali Uimamu wa Ali na wanawe, Uimamu ambao Mashia wanaukubali na kwa kufanya hivyo wawe ni wafuasi wa watu wa nyumba ya Mtume, na au waipinge hadithi hii, jambo ambalo litavifanya vitabu vyao viwe tupu havina ukweli wowote isipokuwa uzushi mtupu. Zaidi ya hapo ni kwamba hadithi hii ambayo inahusisha Ukhalifa kwa Maquraish peke yao inapingana na ule msingi wa mashauriano ambao Masunni wanautetea, kwani uchaguzi na demokrasi inamkusanya kila mtu katika umma, na wala hailihusishi kabila maalum na kuyaacha makabila mengine bali inavuka kwenye makabila ya Kiarabu mpaka inafika kwenye makabila mengine miongoni mwa makabila ya Kiislamu yasiyokuwa ya Kiarabu.

Haya ndiyo majibu ya haraka kwa ufupi ili tumbainishie msomaji baadhi ya mas-ala ambayo huenda yakaichanganya akili yake, na hii ni kwa kuwa huenda akapata majibu kwa ufafanuzi ndani ya vitabu vya historia na vile vile ndani ya vitabu vyangu Thummah-tadaitu na Liakuuna Ma 'as-sadiqin. Basi ni juu ya mwenye kutafiti kuangalia rejea zinazo tegemewa, na ajitahidi kupata ukweli, azichambue riwaya na matukio ya kihistoria na kwa kupitia uchambuzi huo imbainikie haki ambayo imevishwa vazi la batili, alivue na aiangalie haki katika vazi lake la asili.

# WAULIZE WANAOFAHAMU

## MLANGO WA SABA

### YANAYOHUSU HADITHI TUKUFU ZA MTUME (s.a.w.w)

Nitambainishia msomaji kwamba, tatizo la hadithi ni miongoni mwa matatizo ambayo leo hii Waislamu wanakabiliana nayo na hasa katika zama zetu hizi, kwani kuna wasomi waliohitimu kutoka vyuo vikuu vya Kiwahabi ambao wamesomea fani ya hadithi. Wasomi hao utawaona wamehifadhi hadithi ambazo zinakubaliana na madhehebu yao na itikadi zao za Kiwahabi, na sehemu kubwa ya hadithi ni zile zilizowekwa na watawala wa Kibanu Umayyah ambao lengo lao pia lilikuwa ni kuizima nuru ya Utume, na kwa kupitia hadithi hizo wamfanye Mtume **(s.a.w.w)** kuwa ni mtu aliyechanganyikiwa hafahamu anachokisema wala haelewi kuwa hadithi zake na matendo yake yanapingana na huwachekesha hata wenda wazimu.

Pamoja na kuwa wahakiki na wanachuoni wa Kisunni wamesimamia kuzichambua hadithi hizo, lakini kwa bahati mbaya sana bado kuna hadithi nyingi (zilizowekwa) ndani ya vitabu vya Kisunni vinavyotegemewa, pia vitabu vya Kishia navyo havikusalimika na uharibifu na uzushi huu. Lakini Mashia wanakiri kwamba wao hawana kitabu sahihi isipokuwa Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kisichokuwa hicho basi ndani yake kuna uharibifu. Ama Masunni wao wanakubaliana kwamba sahihi mbili ya Bukhari na ile ya Muslim ni vitabu sahihi mno baada ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu. Si hivyo tu, bali wanasema kuwa kila kilichomo humo ni sahihi, na kwa ajili hiyo nitajaribu kumuwekea msomaji baadhi ya mifano katika hadithi ambazo Bukhari na Muslim wameziandika na ni hadithi ambazo yamo mambo yanayoporomosha utukufu wa Mtume Mtukufu **(s.a.w.w)** au utukufu wa watu wa nyumba ya Mtume **(s.a.w.w)**.

Nitajaribu pia katika mlango huu kuonesha baadhi ya hadithi ambazo ziliwekwa ili kuyatakasa matendo ya watawala wa Kibanu Umayyah na wale wa Kibanu Abbas, na kwa kweli kupitia hadithi hizo walikuwa wamekusudia kuitia dosari Ismah ya Mtume **(s.a.w.w)** ili tu wayahalalishe makosa yao na mauaji waliyoyafanya dhidi ya watu wasiokuwa na hatia. Hebu fuatilia maelezo yafuatayo: Eti, Mtume **(s.a.w.w)** ananyemelea Bukhari ameandika ndani ya sahihi yake, Kitabul-Istiidhan na katika Kitabud Diyat, mlango wa yeyote atakayechungulia ndani ya nyumba ya watu na wakamtoboa jicho lake hana fidia.

Muslim naye ndani ya sahihi yake, Kitabul-aadaab, mlango unaokataza kuangalia ndani ya nyumba ya wengine.

Imepokewa kutoka kwa Anas ibn Malik, "Kwamba mtu fulani alichungulia katika baadhi ya vyumba vya Mtume **(s.a.w.w)**, basi Mtume **(s.a.w.w)** akasimama akiwa na mshale au mishale, kama kwamba namuona Mtume anamnyemelea ili amchome." Bila shaka kwa mujibu wa mafunzo matukufu, hayakubaliani kuwa Mtume wa rehma ambaye ni mpole na mwenye huruma kwa waumini eti anaweza kufanya hivyo, kinachotakiwa kwa Mtume **(s.a.w.w)** ni kusimama na kumfunza adabu ya Kiislamu mtu yule aliyechungulia chumba cha Mtume na kumfahamisha kuwa kitendo

alichokitenda ni haramu. Haiwi sawa kwa Mtume achukue mshale na kumvizia kumchoma na kumpofua jicho lake, sababu mtu yule anaweza kuwa alitenda hilo kwa nia njema, kwani chumba hicho hakikuwa miongoni mwa vyumba vya wakeze Mtume **(s.a.w.w)**, na dalili ya hilo ni kuwa Anas ibn Malik alikuwemo humo. Basi ni tuhuma gani hii aliyoielekeza kwa Mtume **(s.a.w.w)** na akaiona kuwa ni ya ususuavu ambayo (eti Mtume) anamnyemelea mtu kumpofua jicho? Tosheka kwamba mshereheshaji wa sahih Bukhari aliikosoa hadithi hii kama ifuatavyo: Kumvizia kwa maana ya kumjia hali ya kuwa hamuoni, hivi ndivyo walivyoifasiri hadithi hii. Na tendo hili halipatikani kwa Mtume **(s.a.w.w)** hawezi kufanya hivyo. Mtume anaadhibu adhabu kali na kuwatesa Waislamu.

Bukhari ameandika ndani ya sahih yake, katika Kitabut-tibb juzuu ya saba uk. 13, mlango wa kuyafanya dawa maziwa ya ngamia, na katika mlango wa kufanya dawa kwa mkojo wa ngamia amesema: Ametusimulia Thabit kutoka kwa Anas kwamba kuna watu walikuwa na ugonjwa fulani wakasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu tupokee na utupe chakula." Mtume akawaamuru waende kwa mchungaji wake wa ngamia, ili wakanywe maziwa ya ngamia na mkojo wake, wale jamaa wakaenda na wakanywa maziwa ya ngamia na mkojo wake. Basi miili yao ilipotengenea walimuua yule mchungaji na wakawaswaga wale ngamia, habari hizo zikamfikia Mtume **(s.a.w.w)**, akatuma watu wawatafute jamaa hao. Walipopatikana wakaletwa, Mtume akawakata mikono yao na miguu yao na akawapiga misumari ya moto machoni mwao, basi nilimuona mtu miongoni mwao anaiuma ardhi kwa ulimi wake mpaka anakufa."

Hivi kuna Mwislamu yeyote anayeweza kuamini kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** ambaye anakataza kuadhibu kwa aina hiyo, kisha yeye mwenyewe anawaadhibu jamaa hawa kwa kuwakata mikono yao na miguu yao na kuwapigilia misumari ya moto machoni mwao kwa kuwa wao wamemuua mchungaji wake? Na lau mpokezi wa riwaya hii angesema kuwa jamaa hawa walimuadhibu vikali yule mchungaji (kabla ya kumuuwa), basi Mtume angekuwa na nafasi ya kuwaadhibu vivyo hivyo, lakini haikuja hivyo, Sasa itakuwaje Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** awaadhibu vikali namna ile bila hata ya kufanya uchunguzi wala kuwapa nafasi ya kujitetea ili abainike ni nani aliyeua miongoni mwao naye auawe? Labda baadhi ya watu watasema kuwa, wote walishiriki kumuua mchungaji yule, basi je, haikuwa sawa kwa Mtume kuwasamehe na kuwaachilia? Kwani wao walikuwa Waislamu kwa dalili ya wao waliposema "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu," hivi tuseme Mtume wa Mwenyezi Mungu hakuisikia kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo:

وَإِنْ عَاقَبْتُمْ فَعَاقِبُوا بِمِثْلِ مَا عُوقِبْتُم بِهِ ۖ وَلَئِن صَبَرْتُمْ لَهُوَ خَيْرٌ لِّلصَّابِرِينَ ﴿١٢٦﴾

"Na mkiteswa basi nanyi lipizeni kwa kiwango kilekile mlichoteswa, na mkivumilia hiyo ni kheri kwa wenye kuvumilia." (Quran, 16:126).

Na iwapo aya hii ilishuka kwa Mtume **(s.a.w.w)** wakati moyo wake ulipomuuma kutokana na kuuawa kwa ammi yake Hamzah ibn Abdil-muttalib bwana wa mashahidi ambaye makafiri walimpasua tumbo lake na wakala maini yake kisha wakamkata sehemu za siri. Mtume alikasirika sana alipomuona ammi yake akiwa katika hali hiyo na akasema, "Mwenyezi Mungu akiniwezesha nitalipiza kwa watu wapatao sabini." Hapo ndipo

iliposhuka aya hii Mtume **(s.a.w.w)** akasema: "Ewe Mola wangu nimekwishavumilia." Mtume akamsamehe muuaji aliyemuua ammi yake kwa kuwa kusamehe ndiyo tabia ya Mtume **(s.a.w.w)**. Hindu (mke wa Abu Sufiyan) ndiye aliyekitesa kiwiliwili kitukufu cha ammi ya Mtume na kula maini yake.

Na miongoni mwa yatakayokujulisha ubovu wa riwaya hii ni kwamba, mpokeaji mwenyewe ameikosoa alipoimalizia kwa kusema: "Qatadah amesema, amenisimulia Muhammad ibn Sayarin kwamba, tukio hilo lilitokea kabla ya kushuka hukumu za adhabu." Kwa hakika haiwezekani kwa Mtume kujiamulia mwenyewe kabla Mola wake hajambainishia, na ikiwa Mtume katika mas-ala madogo haamui mpaka Wahyi umshukie basi hebu fikiria kwa mambo yanayohusu kumwagika damu na hukumu za adhabu? Bila shaka ni rahisi sana kwa yeyote mwenye kuzingatia na kufahamu kwamba riwaya hiyo ni miongoni mwa riwaya za uzushi zitokanazo na Banu Umayyah na wafuasi wao, ili tu kwa kupitia riwaya hizo wawaridhishe watawala wao ambao hawaoni vibaya kuwauwa watu wasio na makosa kwa kuwadhania na kuwatuhumu peke yake, kisha huwatesa mateso makali, na dalili ya hilo ni maelezo yaliyoko mwishoni mwa -riwaya hiyo aliyoiandika Bukhari anasema: Salaam amesema "ilinifikia khabari kwamba Hajjaaj alimwambia Anasi , Hebu niambie adhabu kali aliyopata kuadhibu Mtume **(s.a.w.w)**." Anas akaisimulia hadithi hii, habari zikamfikia Hasan naye akasema, "'Natamani asingemsimulia habari hizi."

Ndani ya riwaya hii umo uzushi ili kumridhisha Hajjaj At-thaqafi ambaye alieneza uovu katika nchi na akaua maelfu ya Mashia (wafuasi) wa watu wa nyumba ya Mtume **(s.a.w.w)** wasiokuwa na hatia na aliwaadhibu vikali, kwani alikuwa akiwakata mikono na miguu na kuwatia machoni misumari ya moto na kuzitoa ndimi zao kutokea kwenye koromeo na akiwasulubu mpaka jua linawaunguza. Na riwaya kama hii inayatakasa matendo yake kwani yeye ataonekana kuwa anafuata mwendo wa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa kutumia kigezo cha kali ya Mwenyezi Mungu isemayo, "Mnacho kiigizo chema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu."- La haula wala quwwata illa billah. Na kwa ajili hiyo ndiyo maana Muawiyyah alikuwa na namna nyingi za kuwaadhibu na kuwatesa Waislamu waliokuwa wakimfuata Ali, kwani ni mara ngapi aliwachoma moto na akawazika wakiwa hai na kuwasulubu kwenye mashina ya mitende? Na miongoni mwa namna (za kuadhibu) alizozizusha waziri wa Muawiyah aitwaye Amru ibn Al-a's ni kuwa, yeye alimuadhibu vikali Muhammad ibn Abubakr kisha akamfunga ndani ya ngozi ya punda na kumtupa motoni. Na katika kuutetea wenda wazimu wao na kupenda kwao wanawake na wajakazi hebu soma yafuatayo:

(Eti) Mtume anapenda mno jimai. Bukhari ameandika ndani ya sahih yake katika Kitabul-ghusli, Babu idhaa Jaama 'a thumma A 'ada Waman Daara A 'la nisaaihi fighuslin-wahidin. Amesema:"Muadh ibn Hisham ametusimulia akasema: Amenisimulia baba yangu kutoka kwa Qataadah amesema: ametusimulia Anas ibn Malik amesema: Mtume alikuwa akiwazingukia wake zake kwa saa moja usiku na mchana na hali ya kuwa idadi yao ni kumi na mmoja, nikamwambia Anas: Hivi alikuwa anaweza

kufanya hivyo? Akasema: Sisi tulikuwa tukizungumza kwamba yeye amepewa nguvu ya wanaume thelathini." Bila shaka hii ni riwaya ya uzushi iliyokusudiwa kumtia aibu Mtume **(s.a.w.w)** ili kulihalalishia baraza la Utawala na vitendo vya Muawiyah na Yazid asiye na haya. Yawezekanaje Anas ibn Malik akafahamu kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** alikuwa akiwaingilia wakeze kumi na moja kwa muda wa saa moja? Je, Mtume ndiye aliyemwambia hivyo au alikuwepo? Najilinda kwa Mwenyezi Mungu dhidi ya maneno ya uzushi, na alizipata wapi habari za kuwa Mtume **(s.a.w.w)** alipewa nguvu za wanaume thelathini?

Kwa hakika hayo ni madhambi makubwa kwa (kumzulia) Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** ambaye uhai wake wote alipigania dini, kufanya ibada, kufundisha na kuelekeza mema kwa umma wke. Ni kitu gani wnachokiamini wapumbavu hawa pale wanapojitokeza na upuuzi kama huu? Ni kama kwamba wao kwa mujibu wa akili zao zilizochafuliwa na matamanio ya kinyama, walikuwa wakijifaharisha mbele ya jamaa zao kutokana na kuingilia mno wanawake na kuwa na nguvu nyingi za kuingilia. Na kwa kweli riwaya hizo zilizushwa ili kumchafulia Mtume **(s.a.w.w)** heshima na utukufu wake, na pili kuuhalalisha tabia ya kutokuwa haya waliyokuwa nayo watawala na Makhalifa ambao waliyajaza majumba yao wajakazi na wanawake bila ya mpaka kwa kuwa tu imewamiliki mikono yao ya kuume. Naye Anas ibn Malik msimulizi wa hadithi hii atasema nini pale Ummul-muuminina Aisha mke wa Mtume ambaye alikuwa akisema kuwa Mtume **(s.a.w.w)** yuko kama wanaume wengine kuhusu suala la jimai?

Muslim ameandika ndani ya sahih yake, Kitabut-taharah Babu naskhil-mai, minal-mai Wawujiibul-ghusli bil-tiqail-khitanain. Imepokewa kutoka kwa Abuz-zubair, kutoka kwa Jabir ibn Abdillahi naye kutoka kwa Ummukul-thuum naye kutoka kwa Aisha mke wa Mtume **(s.a.w.w)** amesema: "Kuna mtu alimuuliza Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** kuhusu mwanaume aliyemuingilia mkewe kisha hakukidhi haja yake je wakoge wote wawili? na Aisha alikuwa amekaa (hapo) basi Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema: hakika mimi hufanya hivyo na huyu ( yaani bibi Aisha) na kisha tunakoga." Kisha mwenye kuisherehesha hadithi hii katika hamish ya sahih Muslim anaongeza kauli yake anasema: "Thumma yuksilu maana yake kama ilivyo ndani ya Misbah ni Aksalal-mujamiu ni kuwa atakapotoka bila ya kutoa manii kwa ajili ya uchovu au kitu kingine."

Sasa basi ikoje hali hii kwa Mtume ambaye amepewa nguvu za wanaume thelathini (kama ilivyodai riwaya ya Anas)? Riwaya hii ni riwaya nyingine miongoni mwa riwaya ambazo ziliwekwa na wazushi, Mwenyezi Mungu awalaani na awazidishie adhabu kali mara dufu, vinginevyo ni nani mwenye akili atakayekubali riwaya kama hizi eti zimetokana na Mtume ambaye atakuwa hana haya kiasi gani mpaka amweleze mwanaume yule tena mbele ya mkewe mambo ambayo muumini wa kawaida anaona aibu kuyasema maneno kama hayo? Na kwa kutaka kuhalalisha muziki na kucheza ngoma, vitu ambavyo vilipata umashuhuri katika zama za utawala wa Banu Ummayyah hebu sikiliza maelezo yafuatayo: Mtume anachungulia ngoma na kusikiliza muziki. Bukhari ameandika ndani ya sahihi yake katika Kitabun-nikaah mlango wa kupiga dufu kwenye harusi na sherehe

amesema: Ametusimulia Bishr ibn Al-mufadhal, ametusimulia Khalid ibn Dhak-waan amesema: "Rabii binti Mu'awadh ibn Afraa, Mtume **(s.a.w.w)** alikuja akaingia wakati nikichezwa harusi akakaa kitandani kwangu kama ulivyokaa wewe na mimi, basi wajakazi wetu wakawa wanapiga dufu na wanawaombolezea wale waliouawa siku ya Badri, miongoni mwa wazee wangu, basi mmoja wao alisema: Kati yetu yupo Nabii ambaye anayajua yatakayotokea kesho, Mtume akasema: Acha maneno haya sema yale uliyokuwa ukiyasema."

Kama ambavyo Bukhari amesimulia ndani ya sahihi yake, Kitabul-jihaad babiid-darq, na pia Muslim ndani ya sahihi yake Kitabul-i'idain Babiir-rnkhsati Fil-laibi ladhi la ma'asiyala fihi. Imepokewa kutoka kwa bibi Aisha amesema: "Mtume aliingia kwangu nami nikiwa na wajakazi wawili wakiimba nyimbo ya Buatha (jina la mahali), akalala juu ya godoro na akageuza uso wake, basi Abubakar akaingia akanikemea akasema (haifai) mazumari ya shetani mbele ya Mtume, Mtume akamuelekea Abubakr akasema. Waache (wacheze) alipopuuza nikawaashiria wakatoka." Na imepokewa kutoka kwa Aisha amesema: "Ilikuwa siku ya Idi, kuna Msudani mrnoja alikuwa akicheza kwa ngoma na mikuki, sasa imma nilimuuliza Mtume wa Mwenyezi Mungu au yeye alisema, Je, unapenda kuangalia, nikasema ndiyo, basi akanisimamisha nyuma yake na shavu langu likiwa shavuni kwake na huku akisema, endeleeni enyi bani Ar-fadah mpaka nilipochoka. Akasema kuniambia; Umetosheka? Nikasema, Ndiyo, akasema, Basi nenda." Kama alivyosimulia Muslim ndani ya sahihi yake. Kitabus-salatul-i'idaini Babur-rukhsat Fillaib. Kutoka kwa Aisha amesema: "Walikuja Wahabeshi siku ya sikukuu wakiruka ruka ndani ya msikiti, basi Mtume **(s.a.w.w)** akaniita nikaweka kichwa changu begani kwake nikawa naangalia mchezo wao mpaka mimi nikawa ndiye niliyeondoka na kuacha kuwaangalia."

Vile vile Bukhari ameandika ndani ya sahihi yake, Kitabun-nikah, Babu dhihabin-nisai was-sib-yan Ilal-u'rsi. Imepokewa kutoka kwa Anas ibn Malik amesema: "Mtume **(s.a.w.w)** aliwaona wanawake na watoto wanakuja kutoka harusini, basi haraka alisimama akasema: Bila shaka ninyi ni watu mupendazao mno kwangu mimi." Mwenye kuisherehesha Bukhari, anasema: "Mum Tannan (tamko la Kiarabu) maana yake ni kuwa Mtume alisimama kwa haraka mno kwa kuwafurahia." Na ili wahalalishe uharamu dhidi ya pombe na ulevi, hebu angalia maelezo yafuatayo: (Eti) Mtume anakunywa pombe ya zabibu! Bukhari ameandika ndani ya sahih yake Kitabun-nikah katika mlango wa mwanamke kusimama mbele ya wanaume harusini na kuwahudumia maji ya zabibu, pia ndani ya mlango wa maji ya zabibu na kinywaji kisicholewesha harusini. Imepokewa kutoka kwa Abu Hazim, nave kutoka kwa Sahl amesema: "Pindi Abu Usaid As-said alipoowa, alimwita Mtume **(s.a.w.w)** na Masahaba wake, basi hakuwatengenezea chakula wala kuwasogezea isipokuwa (kazi hiyo ilifanywa na) mkewe ambaye ndiye Ummu Usaid." Kitakachokujulisha ni kwamba wao wanakusudia kwa riwaya hii kwamba Mtume **(s.a.w.w)** alikunywa Nabidh huenda makusudio siyo ile pombe ya zabibu au tende inayofahamika, bali hayo yalikuwa ni mazoweya kwa Waarabu kuziweka

tende ndani ya maji ili kuondosha harufu ya maji, kwa hiyo siyo ile Nabidhi yenyewe, na baadhi yao wanaona kuwa inafaa kuitumia.

Muslim amethibitisha riwaya hii ndani ya sahihi yake, Kitabul-ashrubah mlango unaoruhusu Nabidh ambayo haikukolezwa na haileweshi, na kutokana na hapa ndipo watawala (wa Kibanu Ummayyah) waliporuhusu pombe kwa madai kuwa ni halali madam haileweshi. Matendo waliyokuwa nayo watawala wa Kibanu Ummayyah na Banu Abbas hebu angalia maelezo yafuatayo: (Eti) Mtume hajiheshimu Bukhari amesimulia ndani ya sahih yake, Kitabul-hajji, Babu ziyarati yaumin-nahr, kutoka kwa bibi Aisha amesema: "Tulihiji pamoja na Mtume **(s.a.w.w)** tukafanya ifadha siku ya kuchinja, basi Safiya akaingia katika siku zake, Mtume **(s.a.w.w)** akamtaka Safiyyah kile ambacho mume hukitaka kwa mkewe, basi mimi nikasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu hakika yeye yumo ndani ya siku zake." Basi ni ajabu iliyoje kwa Mtume huyu ambaye anapenda kumuingilia mkewe mbele ya ushuhuda wa mkewe mwingine, kiasi mke huyo anamjulisha Mtume kuwa mke yule yumo ndani ya siku zake za hedhi hali yakuwa yule mke aliyekusudiwa na Mtume hajui kitu, kwa hiyo (Aisha) ndiye anamfahamisha Mtume wa Mungu kuwa ana hedhi!! (Eti) Mtume hana haya.

Kama alivyoandika Muslim ndani ya sahih, Kitabul-fadhail, Babu fadhail Uthman ibn Afan amesema Muslim: Kutoka kwa mama Aisha mkewe Mtume **(s.a.w.w)** na Uthman wamesimulia kwamba, "Abubakr alipiga hodi nyumbani kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** hali ya kuwa Mtume amelala kitandani kwake na amevaa shuka ya Aisha, basi Mtume akamkaribisha Abubakr naye akiwa katika hali hiyo hiyo, basi Mtume akamtimizia Abubakr shida yake (iliyomleta) kisha akaondoka, Uthman anasema, Kisha Umar alipiga hodi na akakaribishwa, hali ya kuwa Mtume yuko katika hali ile ile, Mtume akamtimizia shida yake kisha akaondoka, Uthman anasema, kisha nilibisha hodi mimi, basi Mtume akakaa na akamwambia Aisha ajifunike nguo zake. Basi nikamaliza shida yangu kisha nikatoka. Hapo Aisha akasema, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu mbona sikukuona unafadhaika kwa ajili ya Abubakr na Umar (r.a.) kama ulivyofadhaika kwa Uthman? Mtume akasema: Hakika Uthuman ni mtu mwenye haya nami nilichelea kumkaribisha nikiwa katika hali ile ili asije akashindwa kunieleza shida yake.? Ni Mtume gani huyu ambaye anawakaribisha Masahaba wake hali ya kuwa kalala amejifunika shuka ya mkewe kitandani kwake na pembeni yake yupo mkewe ambaye amevaa vazi la faragha, mpaka anapokuja Uthman akakaa ndipo Mtume anamuamuru mkewe kujifunika nguo (je, ni kweli haya)? (Eti) Mtume hajisitiri. Bukhari ameandika ndani ya sahih yake, Kitabus-salat. Babu Karahiyyat-tit-taari fis-salat, na vile vile Muslim ameandika ndani ya Kitabul-haidh, Babul-I'itinai bihifdhil-aurah.

Imepokewa kutoka kwa Jabir ibn Abdallah, kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa pamoja nao akibeba mawe kwa ajili ya Al-ka'abah akiwa amevaa shuka, basi ammi yake Mtume bwana Abbas akasema kumwambia Mtume; "Ewe mwana wa ndugu yangu lau ungeifungua shuka yake ukaifunga mabegani ili isiharibiwe na mawe, basi Mtume akaifungua na kuifunga mabegani, mara akadondoka na kuzimia,

basi Mtume kuonekana tena uchi baada ya hapo." Angalia ewe msomaji tuhuma hizi alizozushiwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**, Mtume ambaye haya ameifanya kuwa ni miongoni mwa nguzo za imani, Mtume ambaye ni mwenye haya mno kuliko hata mwali aliyeko ndani, na hawakutosheka na riwaya za Mtume kutokujiheshimu na kufunua mapaja yake mbele ya Sahaba zake, bali mpaka wamemtuhumu Mtume kuwa alikaa uchi kwa riwaya hii waliyoizusha. Hivi kweli Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa watu hawa alikuwa ni mjinga kiasi hiki cha kusikiliza maneno ya ammi yake na akafunua uchi wake mbele za watu? Namuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu aniepushe kutokana na maneno ya mashetani na maibilisi ambao wanamzulia Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Mtume huyu ambaye wakeze na watu wa karibu yake hawakupata kuona utupu wake, jambo ambalo sheria inamruhusu kuwaonesha wakeze utupu wake. Pamoja na hayo Ummul Muuminina Aisha anasema: Sikupata kamwe kuangalia wala kuuona utupu wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (**s.a.w.w)**.[169] Basi kama haya ndiyo mahusiano baina ya Mtume na wakeze ambao walikuwa wakikoga pamoja naye ndani ya chombo kimoja na Mtume hujisitiri utupu wake nao hawakupata kuuona kamwe basi vipi (itawezekana) kwa Masahaba wake na watu wengine?

Bila shaka yote hayo ni miongoni mwa uzushi na maovu ya Kibanu Ummayyah ambao walikuwa hawakuacha kufanya maovu ya kila aina, na kwa namna maovu yao yalivyokithiri kuna mmoja miongoni mwa makhalifa wa kibanu Umayyah aliyekuwa akifurahia maneno ya mshairi miongoni mwa washairi ambaye humuambia Khalifa huyo nyimbo za mapenzi kisha Khalifa huyo akasimama na kuvua nguo halafu akabusu dhakari yake, kwa hiyo siyo ajabu kwa watu hao kumvua nguo Mtume **(s.a.w.w)**.

Na maradhi haya ya kinafsi yamezagaa miongoni mwao mpaka leo hii limekuwa ni jambo la kawaida kwa baadhi ya watu wasiojali matendo yao tena hawaithamini kabisa tabia njema na kuwa na haya, hadi sasa kumekuweko na vilabu na mikusanyiko ya uchi kila mahali wanakusanyika wanaume na wanawake wakijionyesha kuwa, Ewe Mola wetu sisi ndiyo hawa kama ulivyotuumba, na kwa jinsi walivyohalalishia kuichezea dini na hukumu za sheria hebu angalia yafuatayo:- Mtume anasahau ndani ya sala yake. Bukhari ameandika ndani ya sahihi yake, Kitabul-adabi, Babu maa yajuzu Min dhikrin-nasi, na Muslim ndani ya sahih yake Kitabul-masajid wamawaadhi 'is-salat, Babus Sahwi fis-salat Was-sujudi laha. Imepokewa kutoka kwa Abu Hurairah amesema: "Mtume alitusalisha sala ya adhuhuri rakaa mbili kisha akatoa salamu, kisha akasimama kwenye gogo mbele ya msikiti na akaweka mikono yake juu yake, na miongoni mwa watu waliokuwepo ni Abubakr na Umar wao wakaogopa kumuuliza Mtume. Basi watu wenye haraka wakatoka wakasema, je, sala imepunguzwa? Katika hao alikuwemo mtu mmoja ambaye Mtume alikuwa akimwita Dhul-yadain, mtu huyo akasema. Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu umesahau au sala imepunguzwa? Mtume akasema, sikusahau na wala haijapunguzwa, watu wakasema, Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu umesahau, Mtume akasema: Amesema kweli Dhul-yadain."

Basi Mtume akasimama na kusali rakaa mbili kisha akatoa Takbira akasujudu kama anavyosujudu au akarefusha zaidi kisha akanyanyua

kichwa chake akatoa takbira kisha akasujudu sijda yake au zaidi, kisha akanyanyua kichwa chake akatoa takbira.

Haiwezekani kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kusahau ndani ya sala yake akakosa kufahamu ni rakaa ngapi amesali, na inaposemwa kwamba aliambiwa kuwa amepunguza (rakaa za) sala na akasema, Sikusahau wala haikupunguzwa, bila shaka huo ni uongo uliolenga kuwatakasa Makhalifa wao ambao mara nyingi walikuwa wakija kwenye sala hali ya kuwa wamelewa hawajui ni rakaa ngapi wanasali, na kisa kinachomhusu amiri wao aliyewasalisha rakaa nne kwenye sala ya asubuhi kisha akawageukia akawaambia, Niwaongezeni au mmetosheka? Ni kisa mashuhuri ndani ya vitabu vya historia.

Kama alivyoandika Bukhari ndani ya sahih yake, Kitabul-adhan, Balm Idha Qaamar-rajulu a'nyasaaril-Imam amesema: Imepokewa kutoka kwa Ibn Abbas (r.a) amesema: "Nililala nyumbani kwa Maimuna, na Mtume alikuwa huko usiku huo, basi Mtume akatawadha kisha akasimama anasali, nami nikasimama kushoto kwake, basi akanishika na kuniweka kulia kwake akasali rakaa kumi na tatu kisha akalala mpaka akawa anakoroma na alikuwa akilala hukoroma, kisha muadhini alimjibu na akatoka akaswali bila ya kutawadha." Amru amesema, "Nikamsimulia Bukaira akasema, Kuraibu amenisimulia habari hiyo." Riwaya kama hizi za uongo dhidi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** zinawafanya maamiri na masultani wa Kibanu Umayyah na bani Abbas na wengineo waipuuze sala na wapuuze kutawadha na wapuuze kila kitu kiasi kwamba mfano huo umeenea kwetu sisi. Mtume kuapa kisha akavunja kiapo chake Bukhari amesimulia ndani ya sahihi yake Kitabul-maghazi, kisa cha Oman na Bahrain, babu Qudumil-Ash-ariyyin wa Ahlul-Yaman. Imesimuliwa kutoka kwa Abu Qulaibah naye kutoka kwa Zuhdam amesema , "Abu Musa alipofika aliukirimu mtaa huu wa kabila la Juhrum, na sisi tulikuwa tumekaa naye huku anakula kuku. Miongoni mwa watu waliokuwepo, kuna mtu fulani alikuwa kakaa, basi akamwita aje kula akasema, mimi nimemuona anakula kitu ambacho sikukipenda. Abu Musa akasema, Njoo hakika mimi nilimuona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** akila chakula hiki.

Yule mtu akasema, Mimi nilikwisha apa kuwa sintakula chakula hicho. Yeye akasema, njoo nikueleze jambo kuhusu kiapo chako. Kwa hakika sisi tulimuendea Mtume **(s.a.w.w)** tukiwa ni kikundi cha kabila la Ash-ari, tukamuomba atupatie kipando akakataa kutupatia, hatimaye Mtume akaletewa ngawira ya ngamia akaamuru tupewe ngamia watano.

Tulipokwisha kuwachukuwa tukasema, Tumemsahaulisha Mtume kiapo chake basi kamwe sisi si wenye kufaulu. Basi mimi nikamwendea nikasema, Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu hakika wewe uliapa kwamba hutatupatia kipando na sasa umetupatia. Mtume akasema. Ndiyo lakini siwezi kuapa kisha nione kinyume chake kuwa ni bora kuliko kiapo hicho ila nitafanya kile ambacho ni bora kuliko kiapo hicho."

Hebu mwangalie Mtume huyu ambaye Mwenyezi Mungu Mtukufu ametuma ili awafunze watu kuvitekeleza viapo na wala wasivivunje isipokuwa kwa kutoa kafara. Lakini yeye mwenyewe anaamrisha kitu kisha yeye hakitendi anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

لَا يُؤَاخِذُكُمُ اللَّهُ بِاللَّغْوِ فِي أَيْمَانِكُمْ وَلَٰكِن يُؤَاخِذُكُم بِمَا عَقَّدتُّمُ الْأَيْمَانَ فَكَفَّارَتُهُ
إِطْعَامُ عَشَرَةِ مَسَاكِينَ مِنْ أَوْسَطِ مَا تُطْعِمُونَ أَهْلِيكُمْ أَوْ كِسْوَتُهُمْ أَوْ تَحْرِيرُ رَقَبَةٍ فَمَن لَّمْ يَجِدْ
فَصِيَامُ ثَلَاثَةِ أَيَّامٍ ذَٰلِكَ كَفَّارَةُ أَيْمَانِكُمْ إِذَا حَلَفْتُمْ وَاحْفَظُوا أَيْمَانَكُمْ كَذَٰلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ
آيَاتِهِ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٨٩﴾

"Mwenyezi Mungu hatakuadhibuni kwa viapo vyenu vya upuuzi, lakini atakuadhibuni kwa viapo mlivyoviapa kwa nia mliyoifunga barabara, basi (kama hamukuvitekeleza viapo vyenu) kafara yake ni kuwalisha masikini kumi kwa chakula cha kawaida mnachowalisha watu wa nyumbani mwenu au kumpa uhuru Mtumwa, lakini asiyeweza kupata hayo. Basi afunge siku tatu, hii ndiyo kafara ya viapo vyenu mnapoapa, na vilindeni viapo vyenu (msiape kisha mkakosa kuvitimiza) namna hivi ndiyo Mwenyezi Mungu anavyokubainishieni Aya zake ili mupate kushukum" (Qur'an, 5:89).

Na amesema tena Mwenyezi Mungu: "Na wala msitengue viapo baada ya kuvithibitisha". (Qur'an 16:91).

Lakini jamaa hawa hawakumuachia Mtume **(s.a.w.w)** namna yoyote ya ubora na heshima, (wakamzulia mambo chungu nzima).

20

# WAULIZE WANAOFAHAMU

## MAMA AISHA ALIACHA HURU WATUMWA AROBAINI KWA AJILI YA KUTOA KAFARA YA KUVUNJA KIAPO CHAKE

Je, ikoje daraja ya Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa mkewe Aisha ambaye alitoa kafara ya kutengua kiapo pale alipowapa uhuru watumwa arobaini. Hivi yeye bibi Aisha ni mcha Mungu mno kuliko Mtume wa Mwenyezi Mungu? Bukhari ameandika ndani ya sahih yake katika Kitabul-adab, Babul-hijrah waqaulu Rasulillahi **(s.a.w.w)** La yahillu lirajulin an yahjura akha-hu fauqa thalathi. Kwamba Aisha alisimuliwa ya kuwa Abdallah ibn Zubair alisema kuhusu kitu fulani alichonunua au alichopewa na Aisha: "Wallahi Aisha akome au sivyo nitamdhiki." Basi Aisha akasema "Je, ni yeye (Abdallah ibn Zubair) ndiye aliyesema hivi?" Watu wakasema: "Ndiyo" Aisha akasema: "Basi naweka nadhiri kwa Mwenyezi Mungu sitamsemesha kamwe mwana wa Zubair."

Ibn Zubair akawaomba (watu) waingilie kati kuwapatanisha yeye na bibi Aisha baada ya muda mrefu wa kususiana. Aisha akasema: "Wallahi sipatani naye kamwe, na wala sivunji nadhiri yangu." Basi hali hiyo ilipochukua muda mrefu kwa Ibn Zubair. aliwazungumza Mis-war ibn Makrimah na Abdur-rahman ibn Al-as-wad ibn Abdi Yaghuth, hawa ni miongoni mwa bani Zuhrah akawaambia,"Nakuapieni Mwenyezi Mungu, nawaombeni kwa haki ya Mwenyezi Mungu muniingize nyumbani mwa bibi Aisha, kwani si halali kwake kuweka nadhiri ya kuninunia." Ms-war na Abdur-rahman wakaenda naye hali ya kuwa wamejifunika shuka wakapiga hodi kwa bibi Aisha wakasema, "Amani iwe juu yako na rehma za Mwenyezi Mungu na baraka zake, je, tuingie?" Bibi Aisha akasema, "Ingieni." Wakasema: "Sote?" Akasema, "Ndiyo ingieni nyote." Lakini alikuwa hajui kwamba Ibn Zubair yuko pamoja nao.

Walipoingia Ibn Zubair naye akaingia na akapita kvvenye pazia na akamkumbatia Aisha, akawa anamnasihi bibi Aisha na huku analia naye Mis-war na Abdur-rahman wakawa wanarnnasihi bibi Aisha mpaka amkubalie na kumsemesha Ibn Zubair, na wakasema, "Hakika Mtume **(s.a.w.w)** amekataza kususiana jambo ambalo unalifahamu, kwani haifai kwa Muislamu kumsusia nduguye zaidi ya siku tatu." Basi walipomkazania bibi Aisha kumkumbusha na kumuonya, akawa naye huwakumbusha huku akilia akasema, "Hakika mimi niliweka nadhiri, na nadhiri ni jambo zito, basi nao hawakumuachia mpaka akamsemesha Ibn Zubair, na kutokana na nadhiri yake aliachia huru watumwa arobaini, na aliendelea kuikumbuka nadhiri yake baada ya hapo, basi hulia mpaka machozi yake yanalowesha ushungi wake."

Pamoja na kwamba kiapo cha bibi Aisha hakijuzu kwa sababu Mtume **(s.a.w.w)** ameharamisha kwa Muislamu kumsusia nduguye zaidi ya siku tatu, lakini yeye bibi Aisha hakukubali ila atoe kafara ya kiapo chake kwa kuwaachia huru watumwa arobaini. Jambo hili pia linatujulisha dalili nyingine kwamba bibi Aisha peke yake alikuwa ni dola tosha kabisa,

vinginevyo vipi bibi Aisha aweze kumiliki watumwa arobaini au thamani yake? Jambo hilo siyo jepesi, na wala historia haikusajili kwamba Mtume **(s.a.w.w)** alipata kuacha huru watuniwa kwa idadi kubwa kama hii katika uhai wake wote. Kwa hakika jamaa hawa hawakuacha ovu au kasoro yoyote ile isipokuwa walimpachika nayo Mtume, na yote hayo ni kwa kutaka kuyahalalisha matendo ya viongozi wao. Mwenyezi Mungu awalaani, ni wapi wanakoelekezwa? Na katika kuhalalisha kupuuza kwao hukumu za kisheria tazama maelezo yafuatayo:-

(Eti) Mtume anaziacha hukmu za Mwenyezi Mungu wakati wowote akipenda Suala hili ni kama alivyoliandika Bukhari ndani ya sahih yake katika Kitabul-aiman wan-nudhur, mlango wa kutenda dhambi kwa kusahau. Imepokewa kutoka kwa A'taa, kutoka kwa ibn Abbas (r.a) amesema: "Mtu mmoja alimwambia Mtume **(s.a.w.w)** nimezuru kabla ya kupiga." (Yaani nimetufu nyumba tawafu ya ziyarah) Mtume akasema: "Si vibaya." "Nimenyoa kabla ya kuchinja." Mtume akasema: "Hapana ubaya." Mwingine naye akasema: ."Nimechinja kabla ya kupiga." Mtume akasema "Hakuna ubaya."

Na imepokewa kutoka kwa Abdallah ibn Amr ibn Al-'as kwamba, Mtume **(s.a.w.w)** alipokuwa akihutubu siku ya kumi ya mfunguo tatu, kuna mtu fulani alisimama akasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu mimi nilikuwa nikidhania kadhaa wa kadhaa kabla kadhaa wa kadhaa (yaani nilikuwa nikidhania namna fulani kabla ya kufanya namna fulani), kisha mtu mwingine akasimama akasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu mimi nilikuwa nikidhania kadhaa wa kadhaa juu ya mambo haya matatu (kunyoa, kuchinja na kupiga)." Mtume akasema, "Fanya tu hapana ubaya kwa yote hayo kwenye kipindi hicho." Basi Mtume hakuulizwa chochote siku hizo ila alisema, "Fanya, fanya tu wala hakuna ubaya." Cha kushangaza utaposoma riwaya hizi hali ya kuwa unazipinga utaona baadhi ya wanaopinga ukweli wanakukabili kwa kusema kuwa, "Dini ya Mwenyezi Mungu ni nyepesi wala haina uzito na kwamba Mtume **(s.a.w.w)** amesema, "Fanyeni wepesi msifanye uzito (katika dini)."

Bila shaka maneno haya ni sahihi lakini lengo lake ni siyo sahihi, kwani hapana shaka yoyote kuwa, Mwenyezi Mungu anatutakia wepesi wala hatutakii uzito na wala hakufanya juu yetu uzito wowote ndani ya dini, lakini siyo kwa yale aliyokwisha kuyapitisha na kutuwekea kuwa miongoni mwa hukumu na mipaka kupitia Qur'an Tukufu na Sunna Tukufu ya Mtume, si hivyo tu bali ametupatia ruhusa ya lazima kila hali inapobidi (yaani tukikosa uwezo wa kuyatenda). Miongoni mwa mambo hayo ni kama vile kutayammam pindi maji yanapokosekana au kuchelea ubaridi wa maji, na kama vile kusali kwa kukaa inapobidi na kula mchana wa Ramadhani, kupunguza sala safarini, yote haya ni sahihi. Lakini siyo kwenda kinyume na maamrisho ya Mwenyezi Mungu, kwa mfano kuufanya utaratibu wa udhu au kutayammam kama tunavyotaka tukakosha mikono miwili kabla ya kukosha uso, au tukapaka miguu miwili kabla ya kupaka kichwa, namna hii haifai.

Lakini wazushi walitaka kumdharaulisha Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** kwa kila kitu, ili tu wapate njia (ya kufanya wapendavyo) kama wasemavyo watu wengi leo hii (ikiwa utawahoji) watasema, "Hiyo siyo juu

yako bwana, la muhimu ni kusali tu, wewe sali upendavyo." Na cha kushangaza (zaidi) ni kwamba, Bukhari mwenyewe anathibitisha katika ukurasa huo huo ambao iko hiyo (isemwayo kuwa ni) kauli ya Mtume, (Fanya, fanya tu na wala hakuna ubaya)!! Yeye anathibitisha tukio ambalo ndani yake inadhihirika kuwa Mtume **(s.a.w.w)** ni mwenye kutilia mkazo sana mipaka (ya Mwenyezi Mungu). Amesema: Imepokewa kutoka kwa Abu Hurairah ya kwamba, mtu mmoja aliingia msikitini kuswali na Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** akiwa upande fulani ndani ya msikiti, akaja yule mtu akamsalimia Mtume, Mtume akamwambia rudi kaswali tena kwani wewe hujasali, yule mtu akarudi akasali kisha akamsalimia Mtume, naye akamjibu, Mtume akamwambia rudi ukasali kwani bado hujasali. Basi yule mtu akairejea ile sala mara tatu na kila mara Mtume humwambia, "Rudi kasali kwani hujasali." Basi yule mtu akamwambia Mtume, "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu nifundishe." Mtume akamfundisha kutulizana katika rukuu na kutulizana katika sijda. Mtume akasema, "Kisha urukuu mpaka utulie hali ya kuwa umerukuu, halafu nyanyua kichwa chako mpaka usimame wima sawa sawa, kisha usujudu mpaka utulie hali ya kuwa umesujudu, kisha nyanyuka na utulie sawasawa hali ya kuwa umekaa, halafu sujudu mpaka utulizane hali ya kuwa umesujudu kisha nyanyuka mpaka usimame sawa sawa kisha fanya hivyo katika sala yako yote."

Kama ambavyo Bukhari ameandika ndani ya sahih yake, kaika Kitabut-tauhid Babu Qaulillah A 'zza wa Jalla Faqrauu ma-tayassara minal-Qur'an. Imepokewa kutoka kwa Umar ibn Khatab anasema: "Nilimsikia Hisham bin Hakim anasoma Suratul-fur-qan katika zama za uhai wa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**, basi nikamsikiliza kisomo chake, mara ghafla akawa anasoma herufi nyingi ambazo Mtume hakunisomesha, basi karibu nimshambulie ndani ya sala, nikavumilia mpaka akatoa salamu nikamvuta nguo yake nikasema, nani aliyekusomesha sura hii niliyokusikia unaisoma? Akasema: Amenisomesha Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**, nikasema, muongo wewe, mimi amenisomesha kinyume cha ulivyosoma wewe.

Basi nikamburura hali ya kuwa nimemtanguliza mpaka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**, nikasema, Bila shaka nimemsikia huyu anasoma Suratul-furqan kwa herufi ambazo mimi hukunisomesha. Mtume akasema, "Mwachilie (kwanza), ewe Hisham hebu soma." Basi akasoma kisomo nilichomsikia akikisoma. Mtume akasema: "Hivyo ndiyo ilivyoteremshwa." Kisha Mtume akasema, Ewe Umar (hebu nawe) soma, Nikamsomea kisomo alichonisomesha, Mtume akasema: "Hivyo ndivyo ilivyoteremshwa, hakika hii Qur'an imeshushwa kwa aina ya visomo saba, nanyi someni kilicho chepesi." Basi hivi baada ya riwaya hii kunabakia shaka yoyote kwamba wazushi hao walivuka mpaka katika kuchafua heshima ya Mtume **(s.a.w.w)** hadi upande wa Qur'an Tukufu na eti Mtume aliwafundisha Masahaba visomo vinavyohitilafiana na anawaambia kila mmoja wao kuwa hivyo ndivyo ilivyoshuka? Na lau kisomo kile kingekuwa na hitilafu isiyo kubwa, basi Umar asingekurubia kuikata sala ya Hishamu na kumkemea.

Jambo hili linanikumbusha wanachuoni wa Kisunni ambao wanang'ang'ania kisomo maalum, hawakubali kwa mtu yoyote kusoma

kinyume cha vile wanavyofahamu wao. Siku moja nilikuwa nasoma: Udhkuru ni'imatii al-latii an-a'mtu alaikum. Basi mmoja wao alinikemea kwa nguvu na akapiga kelele akisema, "Usiiponde Qur'an kama hujuwi kusoma." Nikasema: "Nimeiponda vipi?" Akasema: "Udhkuruu ni 'imatiya, sio Udhkuruu ni 'imati'!! Kama ambavyo Bukhari amethibitisha ndani ya sahih yake, Kitabul-istiqradh wa Adaid-dain, Babul khusumat, juzuu ya tatu ukurasa wa 88. Imepokewa kutoka kwa Abdil-malik ibn Maisarah amenieleza amesema, Nilimsikia An-nizzal, nilimsikia Abdallah anasema: "'Nilimsikia akisoma aya fulani ambayo mimi niliisikia kutoka kwa Mtume **(s.a.w.w)** kinyume cha hivyo, basi nikamshika mkono nikampeleka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, Mtume akasema: Kila mmoja wenu anasoma vizuri"

Shu'ubah amesema, "Mimi namdhania alisema: Msihitilafiane, kwani waliokuwa kabla yenu walihitilafiana na hatimaye wakaangamia." Utakasifu na sifa njema ni zake Mwenyezi Mungu!! Ni vipi Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** atazikubali hitilafu zao kwa kusema kila mmoja wenu anasoma vizuri na wala asiwarejeshe kwenye kisomo kimoja kitakachoondoa hitilafu iliyopita kati yao? Kisha baada ya hapo awaambie kuwa: "Msihitilafiane mtaangamia." Je, huku siyo kupingana? Enyi waja wa Mwenyezi Mungu hebu tutatulieni na Mwenyezi Mungu atakurehemuni. Na je, hivi kuhitilafiana kwao (kama ilivyo riwaya hiyo) si kulikubaliwa na Mtume mwenyewe na akatoa baraka zake na kuwahimiza wahitilafiane?. Haiwezekani kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (kukubali) kupingana huku na kuhitilafiana ambako akili haikubaliani nako. Basi Je, hawaizingatiii Qur'ani ambayo inasema:

وَلَوْ كَانَ مِنْ عِندِ غَيْرِ اللَّـهِ لَوَجَدُوا فِيهِ اخْتِلَافًا كَثِيرًا ﴿٨٢﴾

"Lau ingekuwa (hii Qur'an) imetoka kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu basi wangekuta hitilafu nyingi ndani yake.' (Qur'an 4:82).

Je, kuna hitilafu kubwa yenye hatari mno juu ya umma wa Kiislamu kuliko (hitilafu ya) visomo vingi ambavyo vimebadilisha maana za Qur'an vikapelekea tafsiri nyingi na maoni tofauti, mpaka ikawa ile aya ya udhu ambayo tunahitilafiana ndani yake wakati iko wazi? Mtume kufanya mambo kama mtoto mdogo!! na kumuadhibu asiyestahiki adhabu. Bukhari ameandika ndani ya sahih yake, Kitabul-maghazi, Babu maradhin-nabi **(s.a.w.w)** wawafatih. Naye Muslim ndani ya sahih yake katika Kitabus-salam Babu karahiyyatit-tadawi Bil-ladud.

Imepokewa kutoka kwa bibi Aisha amesema: "Tulimpanua mdomo Mtume wa Mwenyezi Mungu alipokuwa mgonjwa akawa anatuashiria tusimpanue mdomo, basi siye tukasema, hiyo ni chuki ya mgonjwa dhidi ya dawa, alipozindukana akasema, Je, sikukukatazeni kunipanua mdomo? Tukasema hiyo ni chuki ya mgonjwa dhidi ya dawa, Mtume akasema: Basi hatobakia mtu hapa ndani ila apanuliwe mdomo hali nami ninaangalia, isipokuwa Abbas kwani yeye hakukushuhudieni." Yanashangaza mambo aliyozushiwa Mtume huyu ambaye wazushi hawa wamemfanya kama mtoto mdogo ambaye hunyweshwa dawa chungu asiyoikubali kwa kupanuliwa mdomo na kubanwa pua, (eti Mtume huyu) anaashiria wasimpanue mdomo lakini wao wanamlazimisha tu pamoja na kutotaka kwake. Na anapozinduka anawaambia: "Je, sikuwakatazeni kunipanua mdomo?" Wao wanajitetea

kwamba, walidhania kwamba katazo hilo ilikuwa ni la mgonjwa kuichukia dawa, basi Mtume anawahukumu wote kuwa wapanuliwe midomo yao hali ya kuwa naye anaangalia ili atulize hasira zake na hatobakia miongoni mwao isipokuwa ammi yake Abbasi kwani yeye hakuwepo wakati wakimpanua mdomo.

Bibi Aisha hakukikamilisha kisa hiki, Je, Mtume alitekeleza hukumu yake kwao au hapana? Je, alimtumia Hani kutekeleza, na kilitimia vipi kitendo cha kupanuliwa midomo baina ya wanawake na wanaume waliokuwepo hapo? Mtume (eti) anaondosha baadhi ya aya za Qur'ani! Bukhari ameandika ndani ya sahih yake, Kitabu fadhailil-Qur 'an, Babu Nis-yanil-Qur'an na pia Babu man-laa yaraa ba-asan an-yaqula Suratu kadhaa wa kadhaa. Naye Muslim ameandika ndani ya sahih yake, Kitabu Salatil-musafiriina waqasriha, Babul-amri Bitaa 'hudil-Qur'an wakarahiyatu Qauli nasitu ayata kadhaa. Ametusimulia Abu Usamah kutoka kwa Hisham bin Urwah naye kutoka kwa Baba yake naye kutoka kwa Aisha amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu alimsikia mtu fulani usiku msikitini akisoma sura fulani, Mtume akasema, Mwenyezi Mungu amrehemu, kwa hakika amenikumbusha aya kadhaa wa kadhaa (yaani aya fulani) nilikuwa nimesahaulishwa katika Sura kadhaa wa kadhaa."

Vile vile Bukhari ameandika riwaya nyingine kutoka kwa Ali ibn Mushir, kutoka kwa Hisham naye kutoka kwa baba yake ambaye kapokea toka kwa Aisha (r.a) amesema, "Mtume alimsikia msomaji fulani akisoma usiku msikitini akasema, Mwenyezi Mungu amrehemu, hakika amenikumbusha kadhaa wa kadhaa hiyo ni aya fulani niliiondosha kutoka Sura kadhaa wa kadhaa." (Eti) huyu ndiye Mtume ambaye Mwenyezi Mungu alimtuma alete Qur'an ambayo ni muujiza wa kudumu, na ndiye Mtume ambaye alikuwa akiihifadhi Qur'an tangu siku ya kushuka kwake kwa jumla kabla ya kushuka kwake bayana na Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema: "Usiutikise ulimi wako kwa (kuufanyia haraka) ufunuo." Na amesema tena: "Na bila shaka hii Qur'an ni uteremsho wa Mola kwa walimwengu wote, ameteremka nao roho muaminifu (Jibril) juu ya moyo wako ili uwe miongoni mwa waonyaji, kwa lugha ya Kiarabu iliyo fasaha, na haya (yaliyomo katika Qur'an) yamo katika vitabu vya kale (walivyoteremshiwa Mitume waliopita."

Lakini waovu, wazushi na wapinzani wanapinga (ukweli huu) wanachotaka wao ni kumzulia uongo Mtume, na kumzushia mambo yasiyo na maana, mambo ambayo haiyakubaliani na akili. Ni wajibu kwa Waislamu wanaotafiti na kuchunguza wamtakase Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** kutokana na riwaya kama hizi, ambazo zimejaa katika vitabu vya hadithi na hasa vile vinavyoonekana kuwa ni eti ni sahihi. Sisi hatukuziandika riwaya hizi isipokuwa tumezitoa ndani ya kitabu cha Bukhari na Muslim ambavyo kwa Masunni ndivyo vitabu sahihi mno baada ya kitabu cha Mwenyezi Mungu. Sasa basi iwapo hali ndiyo hii kwa upande wa hivyo vitabu vinavyosemwa kuwa ni sahihi, (na tumeona ni jinsi gani vilivyoivunja heshima ya Mtume **(s.a.w.w)** na isma yake, basi hapo tena usiulize kitu kuhusu hivyo vitabu vingine vilivyobakia (yamo makubwa zaidi). Yote haya ni miongoni mwa uzushi wa maadui wa Mwenyezi Mungu na maadui wa Mtume wake **(s.a.w.w)**, maadui ambao walikuwa

wakijipendekeza kwa watawala wa Kibanu Umayyah katika zama za Muawiyah na baada yake mpaka wakavijaza vitabu kwa hadithi za uongo.

Hadithi ambazo lengo lake ni kumtia doa Mtume **(s.a.w.w)**, kwani jamaa hao hawakumuamini kwa yote aliyokuja nayo kutoka kwa Mola wake. Na hii ni kwa upande mmoja, na kwa upande wa pili walilenga kuyahalalisha matendo maovu na mabaya ya mabwana zao, matendo ambayo historia ya Kiislamu imeyanukuu. Kwa bahati nzuri Mtume wa Mwenyezi Mungu aliwabainisha watu hawa kutoka mwanzoni mwa Utume wake na alitoa tahadhari dhidi yao na wapo aliowafukuza kutoka mjini Madina na akawalaani kutokana na uovu wao. Tabari ameandika ndani ya kitabu chake cha historia amesema: "Mtume **(s.a.w.w)** alimuona Abu Sufiyan anakuja akiwa juu ya punda na Muawiyah anamuongoza, na Yazid mwanawe anamuendesha akasema: Mwenyezi Mungu na amlaani aliyepanda, anayeongoza na anayeendesha." Naye Imam Ahmad ndani ya Musnad yake kupitia kwa Ibn Abbas amesema: "Tulikuwa safarini pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**, akawasikia watu wawili wanaimba mmoja anamwitikia mwenzie, Mtume **(s.a.w.w)** akasema hebu angalieni ni kina nani hao? Watu wakasema ni Muawiyah na Amr bin Al-a's. Mtume akanyanyua mikono yake akasema: Ewe Mwenyezi wadhalilishe mno na uwashinikize motoni."

Na imepokewa kutoka kwa Abu Dharri Al-ghifari kuwa alimwambia Muawiyah kwamba, "Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu baada ya wewe (Muawiyah) kupita (mbele Mwenyezi Mungu mlaani huyu na wala usimshibishe ila kwa udongo."

Naye Imam Ali (a.s) alisema ndani ya barua aliyowaandikia watu wa Iraq kama ifuatavyo: "**Wallahi lau ningepambana nao peke yangu nao wakawa wamejaa Dunia nzima, nisingejali wala kuona upweke, na bila shaka kutokana na upotofu waliomo wao na uongofu tulionao sisi, ni jambo la wazi na uhakika na linaonekana wazi. Bila shaka mimi natamani kukutana na Mola wangu na ni mwenye kusubiri thawabu zake njema, lakini masikitiko na huzuni inayonipata ni kuhusu uongozi wa umma huu kukaliwa na watu wapumbavu na waovu ambao wataigawana mali ya Mwenyezi Mungu na kuwamiliki waja wa Mwenyezi Mungu, watawapiga vita watu wema na watakuwa katika kundi la waovu**."

Na kwa kuwa Mtume alikwisha walaani kama ulivyokiwsha ona, na walishindwa kuzichafua hadithi hizo kwa sababu Masahaba wengi walikuwa wakizifahamu, basi ndipo walipoweka hadithi nyingine kuzikabili hadithi za Mtume ambazo zitaigeuza haki kuwa ni batili na zitakazomfanya Mtume **(s.a.w.w)** kuwa mtu wa kawaida ambaye hupandwa na hasira za kijahiliyah, na ghadhabu humfanya avuke mipaka na hatimaye akatukana na kumlaani asiyestahiki kulaaniwa. Na kwa kuwatetea mabwana zao walio laaniwa (jamaa hao) walizusha hadithi hii ifuatayo: Bukhari ndani ya sahih yake ameandika katika Kitabud-da'awaat, Babu Qalin-Nabyyi **(s.a.w.w)** Man Aadhaituhn faj-al-lahu zakaatan warahmah. Naye Muslim akaandika katika sahih yake Kitabul-birri was-silah wal-aadabi Babu man La'anahun-Nabiyyu **(s.a.w.w)** an Sabbahu an Da'a alaihi walaisa hnwa ahlan Ilidhalika kaana lahu zakaatan wa-ajran warahmah.

Kutoka kwa bibi Aisha amesema: "Watu wawili waliingia kwa Mtume **(s.a.w.w)** wakamsemesha juu ya kitu fulani, mimi sikufahamu ni kitu gani walichomkasirisha, basi Mtume aliwalaani na kuwatukana, hatimaye walipotoka mimi nikasema; Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu nani aliyepata chochote cha wema ambacho hawa jamaa wamekipata? Mtume akasema: Kwani ilikuwaje? Bibi Aisha akasema, nikamwabia, umewalaani na umewatukana. Mtume akasema: Wewe hujui sharti niliyo mwekea Mola wangu, nilimwambia: Ewe Mwenyezi Mungu mimi mtu, basi yeyote katika Waislamu nitakayemlaani au kumtukana basi mfanyie (laana hiyo na tusi hilo) iwe ni zaka kwake na thawabu."

Na imepokewa kutoka kwa Abu Hurairah kwamba Mtume **(s.a.w.w)** amesema: "Ewe Mwenyezi Mungu nachukua ahadi kwako ambayo usinikengeushe kwayo, kwani hapana shaka mimi ni mtu, basi yeyote miongoni mwa waumini nitakayemuudhi, kumshutumu, kumlaani na au kumpiga, basi yafanye hayo kwake iwe ni sala na zaka, pia yawe ni mambo yatakayomsogeza karibu yako siku ya Qiyama."

Kwa kupitia hadithi hizi za uzushi Mtume anaonekana ni mwenye kukasirika siyo kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na anamtukana na kumshutumu, bali anamlaani na kumpiga asiyestahiki hilo.

Basi ni Mtume gani huyu ambaye anazukiwa na shetani mpaka anatoka nje ya ulingo wa mambo yanayokubalika kiakili? Hivi kweli mtu yeyote wa dini wa kawaida tu, atakubaliwa kufanya matendo kama hayo? Au je, haiwezi kuonekana kwake kuwa hayo ni matendo mabaya? Na kwa kupitia hadithi kama hizi watawala wa Kibanu Umayyah ambao Mtume **(s.a.w.w)** aliwalaani na kuwapiga mjeledi baadhi yao kwa sababu ya kutenda kwao machafu na wakafedheheka mbele ya watu wote, eti mara ghafla wanageuka wanakuwa ndiyo waliodhulumiwa na kutakaswa na kurehemewa pia kusogezwa karibu na rehma za Mwenyezi Mungu. Hizi ni hadithi zilizozushwa, zenyewe zinawasuta na kuwafedhehesha hao walioziunda, kwani Mtume wa Mwenyezi Mungu hakuwa na sifa ya kutukana na kulaani, wala hakuwa na uovu wala uchafu wowote ule, kamwe Mtume hakuwa hivyo. Ni maneno mabaya yatokayo vinywani mwao (hao waundaji wa hadithi za uongo) basi hasira za Mwenyezi Mungu ziwashukie na Mwenyezi Mungu amewaandalia watu hao adhabu kali.

Inatutosha riwaya moja tu waliyoiandika Bukhari na Muslim kutoka kwa bibi Aisha kwenye (riwaya hiyo itatosha) kubomoa madai haya ya uongo (dhidi ya Mtume **(s.a.w.w)**. Bukhari ameandika ndani ya sahih yake katika Kitabul-adabi, mlango usemao kuwa Mtume **(s.a.w.w)** hakuwa muovu. Imepokewa kutoka kwa bibi Aisha amesema kwamba: "Wayahudi walimjia Mtume **(s.a.w.w)** wakamwambia: As-saamu alaikum. (yaani mauti yakushukieni) Aisha akasema, mimi nikasema Alaikum, Walaanakumullah waghadhiba alaikum (yaani, Nanyi yakushukieni, Mwenyezi Mungu awalaani na awakasirikieni) Mtume akasema, tulia ewe Aisha kuwa mpole, ole wako usiwe mkali tena muovu. Mimi nikasema Je, wewe hukuwasikia walivyosema? Mtume akasema hukusikia nilivyosema? Nimewarudishia vivyo hivyo nami nitapokelewa nilichokisema wakati wao hawatopokelewa."

Kama alivyoandika Muslim katika sahih yake ndani ya Kitabul-birri was-silat wal-aadaabi kwamba: Mtume wa Mwenyezi Mungu amemkataza Muislamu kuwa mwenye kulaani, na amewakataza (Waislamu) hata kuwalaani wanyama na aliambiwa, "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu omba maombi dhidi ya washirikina." Mtume akasema, "Mimi sikutumwa ili niwe mwenye kulaani, bali nimetumwa ili niwe ni rehma."

Tabia hii ndiyo inayokubaliana na tabia tukufu na moyo wa huruma ambao Mtume wa Mwenyezi Mungu anahusika nao, kwani hakuwa akimlaani na kutukana na kumpiga asiyestahiki bali alikuwa akikasirika basi hukasrika kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na akilaani humlaani anayestahiki kulaaniwa, na akimpiga (mtu) humpiga ili kusimamisha hukumu za Mwenyezi Mungu, siyo kuwapiga wasiokuwa na makosa ambao hakuna ushahidi dhidi yao wala wale ambao hawakukiri kuwa wametenda kosa. Lakini jamaa hawa waliozusha mambo haya, hasira zao zilifura na mioyo yao kuungulia wakati riwaya zinazozungumzia kulaaniwa kwa Muawiyah na Banu Umayyah zilipoenea, wakawa hawana njia isipokuwa kutengeneza riwaya ili kuwapotosha watu na kumpandisha daraja Muawiyah ambaye ni mtu dhalili. Ndiyo maana utamkuta Muslim katika sahihi yake baada ya kuziandika riwaya hizi ambazo zinaifanya laana ya Mtume kwa Muawiyah kuwa ni zaka na ni rehma na ni vitu vya kumsogeza mbele ya Mwenyezi Mungu, Muslim akaandika hadithi iliyopokewa kutoka kwa Ibn Abbas kuwa amesema: "Nilikuwa nikicheza na watoto, Mtume wa Mwenyezi Mungu akaja, mimi nikajificha nyuma ya mlango, akaja akanipiga kwa kiganja chake na akasema, nenda kaniitie Muawiyah, Ibn 'Abbas anasema, nikaja nikamwambia Mtume, Muawiyah anakula, kisha Mtume akaniambia (tena) nenda kaniitie Muawiyah, nikarudi nikamwambia Mtume (bado) anakula, basi Mtume akasema: Mwenyezi Mungu asilishibishe tumbo lake."

Na ndani ya vitabu vya historia tunakuta kwamba, Imam Nasai baada ya kuandika kitabu cha Al-khasais ambacho ndani yake ameyaeleza mengi juu ya ubora wa Imam Ali ibn Abi Talib (a.s), Imam Nasai alipoingia Shamu, watu wa Shamu walimpinga na kumuambia "Kwa nini hukutaja sifa za Muawiyah"? Yeye aliwaambia, "Siifahamu sifa yoyote (ya Muawiyah) isipokuwa ile kauli ya Mtume aliyoisema juu yake kwamba, "Mwenyezi Mungu asilishibishe tumbo lake." Basi walimpiga mbeleni (kwenye utupu) wakamuua kifo cha shahidi. Wanahistoria wanaeleza kuwa, dua ya Mtume ilikubaliwa kwani Muawiyah alikuwa akila mpaka anachoka kula lakini hashibi. Kwa kweli mimi nilikuwa sizijui hizi riwaya ambazo zinaigeuza laana kuwa ni rehema na kikurubisho kwa Mwenyezi Mungu mpaka pale aliponifahamisha mmoja wa Masheikh wa Tunis ambaye anasifika kwa elimu na maarifa, na tulikuwa tunajadiliana juu ya hadithi mbali mbali mpaka ikafikia kumtaja Muawiyah ibn Abi Sufiyan.

Sheikh huyu alikuwa akimzungumzia Muawiyah kwa kumsifia mno na kusema: "(Muawiyah) alikuwa mwenye akili mno tena ni mashuhuri kwa utambuzi na amazingatio mazuri." Sheikh aliendelea kusema: "Muawiyah alisifika kwa siasa yake na ushindi wake dhidi ya Sayyidna Ali (k.w) katika vita." Mimi nilimvumilia kwa uchungu (Sheikh huyu) lakini hatimaye alivuka mpaka katika kumsifia Muawiyah mpaka nikashindwa tena kuvumilia na ndipo nikamwambia kwamba: "Mtume wa Mwenyezi Mungu

alikuwa hampendi Muawiyah na alimuombea dua mbaya na alimlaani." Basi jamaa waliokuwepo hapo walishangaa kuna wengine walikasirishwa na kauli yangu. Lakini yule Sheikh alinijibu kwa utulivu kunisadikisha (niyasemayo), jambo ambalo lilizidisha mshangao kwa jamaa waliohudhuria hapo na wakamwambia:"Sisi hatuelewi kinachofanyika hapa!! Wewe kwa upande fulani unamsifia Muawiyah na kumtakia radhi na kwa upande mwingine unakubaliana kuwa Mtume alimlaani, ni vipi yatawezekana mambo haya.?" Mimi na jamaa hao tukaulizana ni vipi jambo hilo litawezekana? Yule Sheikh akatujibu jawabu ambalo lilishangaza na ikawa vigumu kulikubali kwani alisema: "Hakika yule anayelaaniwa na Mtume wa Mweyezi Mungu au kutukanwa basi hiyo kwake ni zaka (utakaso) na ni rehema na kikurubisho mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu." Basi jamaa wote walijiuliza kwa mshangao, "Inawezekanaje hali hiyo?"

Yule Sheikh akasema: "Hiyo ni kwa sababu Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "**Mimi ni mtu kama watu wengine, na nimekwisha kumuomba Mwenyezi Mungu aifanye dua yangu na laana yangu iwe ni rehma na zaka**." Kisha akaongeza akasema: "Hata yule mtu aliyeuawa na Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** basi mtu huyo atatoka duniani na kuingia peponi moja kwa moja." Hatimaye nilikaa faragha na Sheikh huyu na nikamuuliza rejea ya hadithi aliyoitaja, naye akanielekeza kwenye Sahihi Bukhari na Sahih Muslim na nikazichunguza hadithi hizo, na hazikuniongezea isipokuwa uthibitisho wa njama walizozipanga Banu Umayyah ili kuufumba ukweli na kuficha aibu zao kwa upande mmoja na kuivuruga heshima ya Mtume **(s.a.w.w)** kwa upande mwingine. Baada ya hapo nilikuta riwaya nyingi zinazolenga makusudio hayo hayo. Na ili wapate kutulia wenye njama hizi, bila shaka walitengeneza riwaya nyingi kuliko hizo kwa kutumia maneno ya Mwenyezi Mungu Mola wa ulimwengu.

Bukhari ameandika katika sahihi yake ndani ya Kitabut-tawhiid mlango wa kauli ya Mungu isemayo: "Wanataka wayabadilishe maneno ya Mungu." Kutoka kwa Abu Huraira kwamba, Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** alisema: "Mtu mmoja alikuwa hajapata kutenda jambo la kheri hata kidogo alisema kuwa, Yeye akifa wamuunguze na wapeperushe nusu ya jivu nchi kavu na nusu yake baharini. Wallahi Mwenyezi Mungu akimtia mkononi mtu huyu atamuadhibu adhabu ambayo hatomuadhibu yeyote katika walimwengu. Basi Mwenyezi Mungu aliiamuru bahari ikakusanya (pvu) lililokuwa humo baharini, na aliiamuru nchi kavu ikakusanya jivu lililokuwa humo na kwa uwezo wake Mungu mtu yule aliyechomwa akawa mzima. Mwenyezi Mungu akamuuliza: Kwanini ulifanya hivi? Akajibu: Kwa ajili ya kukuogopa, kwani wewe ni mjuzi mno! Mwenyezi Mungu alimsamehe."

Kuna (habari) nyingine pia kutoka kwake (Abu Huraira) alisema: "Nilimsikia Mtume wa Mungu **(s.a.w.w)** akisema: Hakika mja alitenda dhambi na huenda alisema alifanya dhambi, akasema Ee! Mola nimetenda dhambi na huenda alisema nimefanya dhambi nisamehe, basi Mola wake atasema: Hivi mja wangu ametambua kuwa anaye Mola anaye samehe dhambi na atakayemuadhibu kwa ajili basi nimemsamehe mja wangu. Kisha atakaa kwa kipindi akitakacho Mwenyezi Mungu, halafu atatenda dhambi

au atatenda kosa kisha akasema, Mola wangu nimetenda dhambi au nimekosa kosa jingine, lisamehe kosa hilo, atasema: Hivi mja wangu ametambua kwamba anaye Mola anayesamehe dhambi na kuadhibu, basi nimemsamehe mja wangu. Kisha atakaa kwa muda autakao Mwenyezi Mungu, hatimaye atafanya dhambi na huenda alisema ametenda kosa akasema, Mola wangu nimekosa au akasema nimetenda dhambi nyingine nisamehe. Mwenyezi Mungu atasema hivi mja wangu ametambua kuwa anaye Mola anayesamehe dhambi na kuadhibu basi nimemsamehe mja wangu mara tatu, sasa na afanye atakavyo."

Lo!! Ni Mola gani huyu enyi waja wa Mungu, pamoja na kwamba mja alitambua kutokana na khofu yake ile ya mwanzo kuwa anaye Mola anayesamehe dhambi, lakini Mola wake huyo anabakia kuwa hajui ukweli huu na kila mara akajiuliza, "Hivi mja wangu ametambua kuwa anaye Mola anayesamehe dhambi?" Ni Mola gani huyu ambaye kutokana na wingi wa madhambi yanayorudiwa mara kadhaa, na wingi wa msamaha unaorudiwa mara kadhaa, basi hatimaye amechoka na kubweteka na anamwambia mja wake fanya utakavyo.? "Hayo ni maneno mazito yatokayo vinywani mwao, hawasemi isipokuwa uongo, huenda ukajiangamiza nafsi yako kwa huzuni kutokana na matendo yao iwapo hawatayaamini mazungumzo haya."

Naam, bila shaka hapo kabla walikwishadai kwamba, Mtume wa Mwenyezi Mungu alimuambia Uthmani kuwa,"Fanya upendavyo kamwe hakitakudhuru kitu baada ya leo." Maneno hayo yalisemwa wakati Uthman alipoandaa jeshi lililokuwa na zana duni za kivita (walililiita jeshi la Usrah) kulingana na usemi wao. Hapana shaka kwamba (madai kama haya) ni mfano wa kitabu cha hundi ya msamaha inayompa mtu mamlaka ya kuingia peponi inayotolewa kwa majaala ya mtawa wa Kanisa, (hundi ambayo) inamruhusu mtu kuingia katika ufalme wa mbinguni. Kwa hiyo siyo ajabu kwa Uthman kufanya matendo maovu ambayo yalisababisha mapinduzi dhidi yake na kuuawa kwake kisha akazikwa kwenye makaburi yasiyokuwa ya Waislamu tena bila kukoshwa wala kuvishwa sanda. "Hayo ni matamanio yao (siyo hukumu ya Mtume **(s.a.w.w**) basi waambie leteni hoja zenu kama ninyi mnasema kweli."

21

# WAULIZE WANAOFAHAMU

## MTUME ANAJIPINGA MWENYEWE KATIKA HADITHI ZAKE

Bukhari ameandika ndani ya sahih yake, Kitabul-fitan idhal-taqal-Muslimaini bisaifihimaa, juzuu ya 8 ukurasa 92.

Imepokewa kutoka kwa Abdillah ibn Abdil-wahab, ametusimulia Hammad kutoka kwa mtu fulani ambaye hakumtaja, naye kutoka kwa Al-Hasan amesema: "**Nilitoka na silaha yangu katika usiku wenye fitina, basi Abubakrih akakutana nami akasema: Unakwenda wapi? Nikasema nakwenda kumsaidia mwana wa ammi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w). Akasema: Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema: watakapogombana Waislamu wawili kwa panga zao basi kila mmoja wao ni mtu wa motoni. Akaambiwa basi anakosa gani huyu aliyeuawa? Akasema bila shaka alikusudia kumuua mwenzake. ..." Hammad ibn Zaidi amesema, "Niliitaja hadithi hii kwa Ayyub na Yunus ibn Ubaid nikiwa nakusudia wanifahamishe hadithi hii, basi walisema, hadithi hii ameipokea Al-Hasan kutoka kwa Ah-naf ibn Qais kutoka kwa Abubakrah**."[1]

Kama alivyoandika Muslim ndani ya sahih yake, Kitabul-fitan waashra-tus-sa'ah Babu idha tawaa-jadal-Muslimain bisaifihimaa. Hadithi ya Abibakrah kutoka kwa Al-ahnaf ibn Qais, amesema: "Nilitoka kwa ajili ya kumsaidia mtu huyu, nikakutana na Abubakrah akasema: Unakwenda wapi? Nikasema, kumsaidia mtu huyu. Akasema rudi, hakika mimi nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akisema: "Wakikutana Waislamu wawili kwa panga zao basi aliyeuwa na aliyeuawa wote wataingia motoni, nikasema, Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu huyu muuaji **(s.a.w.w)** basi vipi aliyeuawa? akasema: Hakika yeye alikuwa anapupia kumuua mwenziwe."

Kwa kupitia hadithi hii ya kuzushwa msomaji atafahamu vyema sababu zilizopelekea kuzushwa kwake na huyu Abu Bakrah anaonesha wazi uadui wake dhidi ya mwana wa ammi ya Mtume na ni jinsi gani alivyofanya ili Amirul-Muuminina (Ali [a.s]) asipate usaidizi. Hakutosheka kwa hayo, bali alianza kukosa azma za Masahaba ambao walitaka kuitetea haki dhidi ya batili. Basi akawatengenezea hadithi kama hii ambayo akili haikubaliani nayo na wala Qur'an haiikubali wala sunna sahihi ya Mtume, kwani kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo kuwa: "Lipigeni lile kundi korofi mpaka lirudi kwenye amri ya Mwenyezi Mungu" Sura Al-hujurat ay a ya 9 ni amri iliyo wazi ya kuwapiga wakorofi na madhalimu, na ndiyo maana utamuona aliyesherehesha sahihi Bukhari mwenyewe ameandika kwenye hamish ya hadithi hiyo ibara ifuatayo. "Tazama, hivi kweli ndani ya hadithi hii kuna hoja yoyote inyoruhusu kuwapiga wakorofi pamoja na kwamba kuna kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo lipigeni lile kundi korofi?" Na inapotokea hadithi kupingana na kitabu cha Mwenyezi Mungu, basi hadithi hiyo ni ya uongo itupiliwe mbali. Amma Sunna sahih ya Mtume ni ile kauli yake

1. Sahihi Al- Bukhari juzuu. 8, Uk. 92.

Mtume **(s.a.w.w)** kuhusu Imam Ali isemayo kuwa: "**Yeyote ambaye mimi nilikuwa kiongozi wake basi Ali ni kiongozi wake, ewe Mwenyezi Mungu muunge atakayemuunga (Ali) na umpinge atakayempinga na umsaidie atakayemsaidia na usimsaidie atakayeacha kumsaidia na uipeleke haki iwe pamoja naye popote atakapokuwa**."

Kwa hiyo kumuunga mkono Ali ni kumuunga mkono Mtume wa Mwenyezi Mungu, na ni wajibu kwa kila Muislamu kumsaidia Amirul-Muuumina (Ali), na kuacha kumsaidia maana yake ni kuacha kusaidia haki na ni kuitetea batili. Lau utafanya mazingatio ndani ya hadithi hii ya Bukhari utakuta kuna mlolongo wa wapokezi, mmoja wao hajulikani hawakumtaja jina lake pale aliposema; "Ametusimulia Hammad kutoka kwa mtu fulani," ambaye hakumtaja jina. Hii ni dalili wazi kwamba huyu asiyejulikana ndiye miongoni mwa wanafiki waliokuwa wakimbughudhi Ali (a.s) na wakijaribu kila namna kufuta fadhila zake au zaidi ya hapo kummaliza kabisa yeye na utajo wake kwa njia yoyote watakayoiweza.

Na amesema Sa'ad ibn Abi Waqqas ambaye naye ni miongoni mwa waliokataa kuitetea haki: "Nipeni upanga nikapigane, huyu anasema yuko kwenye haki na huyu anasema yuko kwenye batili." Na kwa mifano kama hii inayochanganya haki na batili na kuzipoteza njia za wazi ili nafasi yake ichukuliwe na njia ya giza. Sisi tunakuta ndani ya vitabu vya Kisunni vinavyotegemewa ya kwamba, Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amewabashiria Masahaba wake wengi kuingia peponi, na hasa wale kumi ambao wanaotambulikana mno miongoni mwa Waislamu kwamba wao wamebashiriwa pepo.

Ahmad, Tirmidhi na Abu Dawud wameandika kwamba Mtume **(s.a.w.w)** amesema: "Abubakr ataingia peponi, Umar peponi, Uthman peponi, Ali peponi, Talha peponi, Zubair peponi, Abdur-rahman ibn A'uf peponi, Saad ibn Abi Waqas peponi, Said ibn Zaidi peponi na Abu Ubaidah ibn Jarrah peponi. Kuna habari sahihi kutoka kwa Mtume **(s.a.w.w)** kuwa amesema: "Furahini enyi kizazi cha Yasir, bila shaka mahala penu ni peponi." Pia kuna kauli nyingine ya Mtume isemayo: "Pepo ina hamu ya watu wanne, Ali, Ammar, Salman na Miqdad."

Naye Muslim amesimulia ndani ya sahihi yake kwamba, Abdallah ibn Salaam amebashiriwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu (kuingia) peponi, na imesihi kutoka kwa Mtume aliposema: "**Hasan na Husein ni mabwana wa vijana wa peponi**." Kadhalika imesihi habari kutoka kwa Mtume kwamba, Jaafar ibn Abi Talib anaruka peponi pamoja na Malaika, na kwamba bibi Fatmah Az-zahra ndive mbora wa wanawake wa peponi, na kwamba mama yake Fatmah (bibi Khadija) alibashiriwa na Jibril kuwa atapewa nyumba huko peponi.

Pia kuna habari sahihi kutoka kwa Mtume **(s.a.w.w)** aliposema kuwa Suhaib ambaye ni mtu wa mwanzo kusilimu kutoka Rumi ataingia Peponi, na Bilal ambaye ni mtu wa mwanzo kusilimu kutoka Uhabeshi naye ataingia peponi pia Salman ambaye ni mtu wa mwanzo kusilimu kutoka Uajemi ataingia peponi.

Ikiwa mambo yako hivi basi ni kwa nini bishara za peponi zinahusika tu na hawa masahaba kumi, hukuti mkusanyiko wala kikao wanapozungumzia pepo isipokuwa kuwataja hawa kumi tu waliobashiriwa pepo.? Sisi hatuna

chuki yoyote ile kuhusu jambo hilo, na wala hatuibani rehma ya Mwenyezi Mungu ambayo ni kubwa na imekienea kila kitu. Lakini tunasema tu kwamba, hadithi hizi zinapingana na ile hadithi isemayo, "Wanapokutana Waislamu wawili na panga zao, basi aliyeua na aliyeuawa wote wataingia motoni." Kwani lau tutaikubali hadithi hiyo, basi ile hadithi ya bishara ya pepo itatoweka kwani wengi wa hawa walipigana na wakauana wao kwa wao. Tal-ha na Zubair waliuawa katika vita ya Jamal ambayo kiongozi wake alikuwa Ummul-Muumina Aisha dhidi ya Imam Ali ibn Abi Talib, na panga zao zilichomolewa na zaidi ya hapo walisababisha kuuawa kwa maelfu ya Waislamu.

Kama ambavyo Ammar ibn Yasir aliuawa katika vita vya Siffin ambavyo moto wake uliwashwa na Muawiyah ibn Abi Sufian, na Ammar alikuwa akipigana kwa upanga wake akiwa pamoja na Ali ibn Abi Talib, basi lile kundi ovu likamuua kama alivyotamka hilo Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**. Kama ambavyo Bwana wa mashahidi na Bwana wa vijana wa peponi Imam Husein alipigana kwa upanga wake yeye na watu wa nyumba ya Mtume dhidi yajeshi la Yazid ibn Muawiyah, na (jeshi hilo la Yazidi) liliwaua (watu wote wa nyumba ya Mtume) hakusalimika isipokuwa Ali ibn Husein (a.s). Na kwa mtazamo wa wazushi hawa ni kwamba, wote hawa wataingia motoni wauaji na waliouawa kwa sababu walipambana kwa panga zao. Ukweli ulivyo ni kwamba, hadithi hiyo haiwezi kusemwa kuwa ni ya (Mtume), Mtume ambaye hasemi kwa matamanio isipokuwa kwa ufunuo uliofunuliwa kwake. Na kama tulivyotangulia kusema hapo kabla kuwa inapingana na mantiki na akili, si hivyo tu bali inapingana na Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna ya Mtume **(s.a.w.w)**.

**Swali** la kujiuliza hapa ni kwamba: ni kwa kiasi gani Bukhari na Muslim wamegliafilika wasiweze kuufahamu uzushi kama huu na wala wasiweze kuzindukana?

Kupingana katika ubora Miongoni mwa hadithi zinazopingana ambazo utazikuta katika sihahi, ni ubora wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (Muhammad **s.a.w.w**) juu ya Manabii wote na Mitume wengine, na ziko hadithi nyingine zinampandisha Mtume Musa kwa daraja kuliko Mtume **(s.a.w.w)**. Mimi naamini kwamba, Mayahudi ambao walisilimu katika zama za Umar na Uthman kama vile Ka'abul-Ahbar, Tamimud-dari na Wahb ibn Munabbih ndiyo walioziweka hadithi hizo kupitia ndimi za baadhi ya Masahaba ambao walikuwa wakiwapenda kama vile Abu Hurairah na Anas ibn Malik na wengineo. Bukhari ameandika ndani ya sahih yake Kitabut-tauhid babu Qaulihi Taala Wakallamallahu Musa Taklima.

Imesimuliwa kutoka kwa Anas ibn Malik kisa kirefu inachosimulia jinsi israi ya Mtume **(s.a.w.w)** ilvyokuwa, kisha kupanda kwake mbingu saba mpaka Sidratil-Mnntaha. Kisa hicho kinaeleza pia kufaradhishwa kwa sala hamsini ambazo zilifaradhishwa kwa Mtume Muhammad na umma wake, lakini kwa ubora wa Musa zikapunguzwa na kuwa tano, na mengineyo yaliyomo ndani ya riwaya hizo miongoni mwa uongo ulio wazi kabisa na kufuru mbaya, eti kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu alisogea akateremka akawa karibu mno na Mtume, na mengineyo miongoni mwa uharibifu. Lakini kilicho muhimu kwetu katika riwaya hii ni kwamba, pale Mtume Muhammad alipoomba ruhusa afunguliwe kwenye mbingu ya saba, wakati

huo Musa alikuwa katika mbingu hiyo na kwamba Mwenyezi Mungu alimnyanyua kwenye mbingu hiyo ya saba kutokana na ubora wa yeye Musa kumsemesha Mwenyezi Mungu, hapo Musa alisema: "Ewe Mola wangu mimi sikudhani kama kuna mtu yeyote angenyanyuliwa juu yangu." Muslim ameandika katika Kitabul-iman Babu bad-il-wahyi ila Rasuli llah **(s.a.w.w)**.

Bukhari ameandika ndani ya sahihi yake Kitabu bad-il-khalqi, babu dhikril-Malaikah (a.s). Yeye ametoa kisa kingine kinachofanana na kile cha kwanza na anaeleza Israi na Mi'iraj, lakini kisa hicho kinasema kwamba, "Musa alikuwa katika mbingu ya sita na Ibrahim ya saba." Jambo la muhimu ndani ya riwaya hii ni hiki kipande kipande kisemacho kuwa: Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "Tukafika mbingu ya sita, pakasemwa ni nani huyu? Pakanenwa Jibril, pakasemwa uko pamoja na nani? Akasema, Muhammad **(s.a.w.w)**, pakasemwa, ameitwa? Akasema: ndiyo, pakanenewa karibu. Basi nikafika kwa Musa nikamsalimia akasema karibu ewe ndugu na Mtume, basi nilipopita akalia, akaambiwa nini kilichokuliza, akasema, Ewe Mola wangu kijana huyu ametumwa baada yangu katika, umma wake wataingia peponi watu wengi zaidi kuliko wale watakaoingia kutoka katika umma wangu" Kama alivyoandika Muslim ndani ya sahih yake, Kitabul-imaan babit Adnaa Ahlil-jannah Manzilatanfiiha.

Imesimuliwa kutoka kwa Abu Hurairah kwamba, Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema; "Mimi ni Bwana wa watu siku ya Qiyama, je, mnafahamu ni kwa nini? Watu watakusanywa wale wa mwanzoni na wa niwisho katika uwanja mmoja atawasikilizisha mlinganiaji na jicho litawafika wote kisha jua litasogea, na kutokana na taabu na shida itafikia hali ambayo watu hawawezi kuvumilia, hapo ndipo watakaposema, Je, mnavaona mambo yaliyokufikieni? Je, hamuangalii mtu wa kukuombeeni kwa Mola wenu? Baadhi ya watu watawaambia wengine nendeni kwa Adam, basi watamwendea Adam (a.s) watamwambia wewe ndiyo baba wa watu (wote), mwenyezi Mungu alikuumba kwa mkono wake na akakupulizia roho yake,na akawaamuru Malaika wakusujudie, tuombee kwa Mola wako. Je, huyaoni yaliyotufika? Basi Adam atasema: Leo hii Mola wangu amekasirika kiasi ambacho hajapata kukasirika mfano wake na yeye alinikataza ule mti nami nikamuasi.

Ewe nafsi yangu, nafsi yangu, nafsi yangu, nendeni kwa mwingine, nendeni kwa Nuh." Riwaya inaendelea na ni ndefu mno (nasi wakati wote tunapenda kufupisha) kiasi kwamba watu watazunguka kwa Nuhu kisha kwa Ibrahim, kisha kwa Musa, kisha kwa Isa na wote wanasema: "Ewe nafsi yangu, nafsi yangu, nafsi yangu." Kila mmoja alitaja kosa lake isipokuwa Issa hakutaja kosa lolote lakini alisema; "Ewe nafsi yangu. nafsi yangu, nafsi yangu nendeni kwa mwingine asiyekuwa mimi nendeni kwa Muhammad.1* Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema, watakuja kwangu mimi nitakwenda chini ya A'rshi nitaanguka hali ya kuwa ninasujudu kwa ajili ya Mola wangu Mtukufu kisha Mwenyezi Mungu atanifungulia baadhi ya sifa zake njema kitu ambacho hajakifungua kwa yeyote kabla yangu. Hatimaye patasemwa. "Ewe Muhammad nyanvua kichwa chako, omba utapewa, omba utakubaliwa." Nitanyanyua kichwa changu na nitasema:

"Ewe Mola wangu ummati wangu. Ewe Mola wangu ummati wangu." Patasemwa, "Ewe Muhammad waingize katika ummati wako watu bila ya hesabu katika mlango wa kulia miongoni mwa milango ya peponi, nao watashiriki na watu katika milango mingine miongoni mwa milango, kisha akasema, namuapa Mwenyezi Mungu ambaye nafsi yangu imo mikononi mwake hakika baina ya milango miwili miongoni mwa milango ya peponi ni kama baina ya Maka na Humair au ni kama baina ya Maka na Basra."

Ndani ya hadithi hizi Mtume anasema kwamba, "Yeye ni Bwana wa watu siku ya Qiyama." Na anasema kuwa, "Musa alisema, Ewe Mola wangu nilikuwa sidhani kwamba kuna mtu yeyote atakayenyanyuliwa juu yangu na pia anasema kwamba, Musa alilia na akasema: Kijana huyu aliyetumwa baada yangu wataingia peponi watu wengi katika ummati wake kuliko wale watakaoingia katika ummati wangu." Tunachokifahamu kupitia hadithi hizi ni kwamba, Manabii na Mitume wote kuanzia Adam mpaka Isa kwa kupitia Nuh, Ibrahim na Musa (amani iwashukie wao na Mtume wetu) hawatawaombea watu mbele ya Mwenyezi Mungu siku ya Qiyama na Mwenyezi Mungu amemuhusisha kwa jambo hilo Mtume Muhammad **(s.a.w.w)** peke yake, nasi tunayaamini yote hayo na tunasema kuwa, yeye Mtume ni bora wa viumbe wote, lakini Waisraili na wasaidizi wao miongoni mwa Banu Umayyah hawakuvumilia ubora huu na heshima hii kwa Muhammad **(s.a.w.w)** mpaka wakatengeneza riwaya zinazomboresha Musa juu ya Mtume **(s.a.w.w)**. Hilo tumekwishaliona hapo kabla katika kauli ya Musa kwa Muhammad kwenye ule usiku wa Israi na Mi'iraj na pale Mwenyezi Mungu alipomfaradhishia Mtume sala hamsini, Musa akamwambia Mtume, "Mimi nawajua watu kuliko wewe." Hili halikutosha wakatengeneza riwaya nyingine zinazomboresha Musa kuliko Muhammad kwa kupitia ulimi wa Muhammad mwenyewe. Basi hebu ziangalie baadhi ya riwaya hizi zifuatazo.

Bukhari ameandika ndani ya sahih yake katika Kitabut-tauhid babu fil-mashiati wal-iradah Wamaa tashauna Ilia art-Yashaa llahu. Imepokewa kutoka kwa Abu Hurairah amesema: "Mtu fulani miongoni mwa Waislamu na mwingine Myahudi waligombana, yule Mwislamu akasema, namuapa Mwenyezi Mungu aliyemteua Muhammad juu ya walimwengu. (hiki ni kiapo alichoapia) Basi yule Myahudi naye akasema: Namuapa Mwenyezi Mungu ambaye alimteua Musa juu ya walimwengu. Yule Muislamu akanyanyua mkono wake akampiga yule Myahudi, Myahudi yule akaenda kwa Mtume **(s.a.w.w)** akamuelezea yaliyojiri kati yake na yule Muislamu. Mtume **(s.a.w.w)** akasema: Msinifanye mie kuwa bora juu ya Musa, kwani siku ya Qiyama watu watazimia nami nitakuwa wa kwanza kuzindukana, basi ghafla Musa amejiangika kwa nguvu pembeni ya Arshi, mimi sifahamu je, na yeye alikuwa miongoni mwa waliozimia kisha akazindukana kabla yangu au alikuwa miongoni mwa wale ambao Mwenyezi Mungu hakuwahusisha (na kuzimia huko)."

Katika riwaya nyingine ya Bukhari amesema: "Myahudi fulani alikuja kwa Mtume **(s.a.w.w)** hali yakuwa amepigwa usoni kwake na akasema, Ewe Muhammad mtu fulani miongoni mwa wafuasi wako wa Kiansari amenipiga usoni. Mtume akasema mwite, wakamwita, Mtume akasema, Kwa nini umempiga usoni kwake? Yule mtu akasema, Ewe Mtume wa

Mwenyezi Mungu mimi nilipita kwa Myahudi huyu nikamsikia anasema;Namuapa Mwenyezi Mungu ambaye alimteua Musa juu ya watu, basi mimi nikasema, na juu ya Muhammad? Hilo likanikasirisha kisha nikampiga. Mtume akasema: Msiniboreshe mbele ya Manabii, kwani siku ya Qiyama watu watazimia nami nitakuwa wa kwanza kuzindukana, mara ghafla (nitamkuta) Musa ameshika nguzo miongoni mwa nguzo za Arshi, sasa sijui amezindukana kabla yangu au alitoshelezwa kwa mzimio ule wa (mlima wa) Tuur."

Kama ambavyo Bukhari amethibitisha ndani ya sahih yake katika Kitabu Tafsiril-Qur-an surat Yusuf (a.s) Babu qaulihi falammaa Jaa-ar-rasul. Imepokewa kutoka kwa Abu Hurairah amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**. "Mwenyezi Mungu amrehemu Lut, kwa hakika alikuwa anakimbilia kwenye pembe iliyo imara, lau ningekaa jela kiasi alichokaa Yusuph ningemwitikia mwitaji. Sisi tunastahiki zaidi kuliko Ibrahim alipoulizwa je, hukuamini? Akasema nimeamini lakini nataka roho yangu itulie. Hawakutosheka na yote hayo mpaka wamemfanya Mtume wa Mwenyezi Mungu kuwa ni miongoni mwa wenye mashaka juu ya hali yake ya baadaye mbele ya Mola wake, hana shufaa wala ile daraja tukufu, na wala hana ubora mbele ya Manabii na Mitume wengine, kwa maana hiyo hana hata ule ubashiri wa pepo kwa Masahaba wake ikiwa yeye mwenyewe hajui hali yake (itavyokuwa) siku ya Qiyama. Hebu tuisome kwa pamoja riwaya hii ambayo ameandika Bukhari, na imma utashangaa au hutashangaa.

Bukhari ameandika ndani ya sahih yake, Babu fil-janaiz, Kitabul-kusufi, juzuu ya pili ukurasa 71. Imepokewa kutoka kwa Kharijah ibn Zaid ibn Thabit, kwamba Ummul-Alai ni mwanamke wa Kiansari ambaye alimpa baia Mtume **(s.a.w.w)**. Mama huyu alimuelezea kuwa Muhajirina waligawana hisa katika hisa yetu, akatokea Uthman ibn Madh-u'n nasi tukamkaribisha majumbani mwetu, kisha aliugua maradhi ambayo kwayo alifishwa, alipofishwa na akakoshwa na kukafiniwa katika nguo zake, Mtume **(s.a.w.w)** aliingia, basi mimi nikasema: "Rehma ya Mwenyezi Mungu ikushukie ewe Abas-saaib, nashuhudia kuwa Mwenyezi Mungu amekukirimu." Mtume **(s.a.w.w)** akasema, ni lipi linalokujulisha kuwa Mwenyezi Mungu amemkirimu?" Nikasema, "Ewe Mtume wa mwenyezi Mungu ni nani basi atakirimiwa na Mwenyezi Mungu?" Mtume akasema: "Amma yeye yaqini imekwishakumfikia, namuapa Mwenyezi Mungu mimi namtakia kheri, namuapa Mwenyezi Mungu, mimi mwenyewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu lakini sijui nitafanyiwa nini?[1]"

Yule mama akasema:"Namuapa Mwenyezi Mungu kamwe sitamtakasa yeyote baada yake." Wallahi hili ni jambo la ajabu, ikiwa Mtume wa Mwenyezi Mungu yeye haujui atakachofanyiwa, basi nini kinachobakia baada ya hili? Na iwapo Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: "Bali mtu ni shahidi na nafsi yake" (Qur.75:14).

na kama Mwenyezi Mungu anamwambia Mtume wake:

---

1. Sahihi Al- Bukhari juzuu.2, Uk. 71.

إِنَّا فَتَحْنَا لَكَ فَتْحًا مُّبِينًا ﴿١﴾ لِّيَغْفِرَ لَكَ اللَّـهُ مَا تَقَدَّمَ مِن ذَنبِكَ وَمَا تَأَخَّرَ وَيُتِمَّ نِعْمَتَهُ عَلَيْكَ وَيَهْدِيَكَ صِرَاطًا مُّسْتَقِيمًا ﴿٢﴾ وَيَنصُرَكَ اللَّـهُ نَصْرًا عَزِيزًا ﴿٣﴾

"Bila shaka tumekwisha kukupa ushindi uliodhahiri, ili Mwenyezi Mungu akusamehe makosa yako yaliyo tangulia na yanayokuja na kukutimizia neema zake na kukuongoa kwenye njia iliyonyooka na akusaidie Mwenyezi Mungu msaada wenye nguvu kabisa." (Qur'an, 48:1-3).

Na iwapo kuingia peponi kwa Waislamu kunategemea kumfuata, kumtii na kumuamini Mtume **(s.a.w.w)**, basi ni vipi tutaisadiki hadithi hii ambayo ni chafu mno?.

Twajilinda kwa Mwenyezi Mungu kutokana na itikadi za Kibanu Umayyah watu ambao walikuwa hawaamini hata siku moja kuwa Muhammad ni Mtume wa haki wa Mwenyezi Mungu, bali wao walikuwa wakiitakidi kuwa ni Mfalme aliyewashinda watu kwa akili zake na ujanja wake!! Itikadi hii ndiyo ile aliyoibainisha wazi Abu Sufiyan na Muawiyah na wengineo miongoni mwa Makhalifa wao na watawala wa Kibanu Umayyah. Mtume kupingana na elimu ya tiba Bila shaka elimu inathibitisha kwa maelezo ambayo hayana shaka kuwa, kuna baadhi ya maradhi ambayo hupatikana kwa njia ya kuambukiza, jambo hili watu wengi wanalifahamu hata wale ambao hawana kiwango kikubwa cha elimu. Amma wasomi ambao wanasomea elimu ya tiba katika vyuo vikuu, bila shaka watakapoambiwa kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** anapinga hilo, hapana shaka watamdharau na watapata nafasi ya kumshambulia mno Nabii wa Uislamu. Watu wasioamini dini siku zote wanatafuta mwanya kama huu. Inasikitisha mno kwamba miongoni mwa hadithi ambazo zimethibitishwa na Bukhari na Muslim ziko zile zinazopinga kuwepo kuambukiza, na pia ziko zinazosisitiza kuwa kuna kuambukizana (maradhi).

Sisi hapa tunasajili huku kupingana kwa hadithi hizi chini ya anuani ya kuwa Mtume anajipinga, lakini hatuamini kuwa ilipata kutokea Mtume kujipinga katika maneno yake na matendo yake hata mara moja. Lakini kama kawaida (yetu) na ili kuivutia roho ya msomaji ili apate kuzindukana azitambue zile hadithi za uzushi na za uongo zilizowekwa dhidi ya Mtume **(s.a.w.w)** ambaye ni Maasum. Ili msomaji apate kufahamu lengo letu la kuziandika hadithi hizi kuwa ni kwa ajili ya kumtakasa Mtume **(s.a.w.w)** na kumpa heshima yake ya kielimu ambayo imeshinda elimu zote za kisasa, kwani hapana nadhariya yoyote ya kielimu inayopingana na hadithi sahihi za Mtume **(s.a.w.w)**. Ikiwa zitapingana basi tutajua kwamba Mtume kazushiwa hadithi hiyo kwa upande mmoja na kwa upande mwingine, bila shaka hadithi hiyo itakuwa inapingwa na hadithi nyingine inayokubaliana na nadharia ya kielimu, basi itakuwa wajibu kuikubali hii ya pili na kuiacha ile ya kwanza. Mfano juu ya hilo ninaleta hadithi ya kuambukiza kwani ni ya muhimu katika uchunguzi na itatupatia picha kamili ya kupingana kwa Masahaba na wapokezi (wa hadithi) na wale wazushi na siyo Mtume kujipinga mwenyewe kwani hilo kamwe haliwezekani.

Bukhari ndani ya sahihi yake anataja hadithi mbili, nami nitatosheka naye kwani kitabu chake ndiyo kitabu sahihi mno kwa Masunni, ili tu wenye kugeuza wasije kwenda na njia nyingi pakatokea mwenye kusema kuwa huenda ikathibiti hadithi kwa Bukhari na ikathibiti kinyume chake

kwa asiyekuwa yeye miongoni mwa wanachuoni wa hadithi. Msomaji ataona kuwa mimi katika mlango huu nimetosheka na Bukhari peke yake katika hadithi zinazopingana. Bukhari amethibitisha katika sahih yake, Kitabut-tib Babu La Hammah: Imepokewa kutoka kwa Abu Hurairah amesema: "Nabii **(s.a.w.w)** amesema: **Hapana kuambukiza wala ugonjwa wa manjano wala ndege mbaya**." Bedui mmoja akasema: "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu ni vipi kuhusu ngamia aliye mzima kisha akachanganyikana na ngamia mwenye upele na akamuambukiza? Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema: Ni nani aliyemuambukiza yule wa kwanza?" Hebu muangalie bedui huyu, ni vipi anaweza kufahamu kwa kutumia akili yake ya kuzaliwa namna ilivyo tabia ya maradhi ya kuambukiza kupitia ngamia mwenye upele ambaye anaambukiza ngamia wote akichanganyika nao, wakati ambapo Mtume anakosa jibu la kutosheleza suali la bedui na hatimaye yeye Mtume ndiyo anakuwa muulizaji?

Hadithi hii vile vile inanikumbusha daktari mmoja ambaye alimuuliza mama fulani aliyekuja na mwanawe aliyepatwa na shurua, Daktari akasema, "Je, nyumbani mwenu au jirani yenu kuna mtu anayeugua maradhi haya?" Yule mama akasema, hapana." Daktari akasema. "Basi huenda (mwanao) ameupata ugonjwa huu shuleni?" Mama akajibu haraka sana, "Hapana huyu hata shule bado hajaingia umri wake ni chini ya miaka mitano." Daktari akasema: "Kwa hiyo labda kwenye michezo." Mama akasema; "Hapana huyu haendi kwenye michezo." Yule daktari akasema: "Huenda wewe ulienda naye katika matembezi kwa baadhi ya nduguzo au walikutembeleeni baadhi ya ndugu ambao kuna ambaye alikuwa na vijidudu vya maradhi." Yule mama akakanusha, hapo ndipo Daktari alipomwambia yule mama kuwa, "Vijidudu hivyo vimetoka hewani."

Bila shaka hewa inabeba vijidudu na maradhi yanayoambukiza na huenda yakaupata mji wote au kitongoji chote na ndiyo maana kumekuweko kinga ili kuzuia vijidudu vya maradhi mabaya vitakavyobebwa na upepo kama vile kipindupindu, tauni na mengineyo. Basi iweje yote haya yasitambulikane kwa Mtume ambaye hasemi kwa matamanio yake? Bila shaka yeye ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu hakifichikani katika elimu chochote, bila shaka kwa Mwenyezi Mungu hakifichikani chochote kilichoko ardhini wala mbinguni, naye ni msikivu na ni mjuzi mno, na kwa ajili hiyo sisi tunaipinga hadithi hii na wala hatuikubali kamwe, na tunaikubali hadithi ya pili ambayo yeye mwenyewe Bukhari ameithibitisha katika ukurasa huo huo na katika mlango huo huo na ndani ya hadithi yenyewe pale aliposema:

Imepokewa kutoka kwa Abu Salamah, alimsikia Abu Hurairah baadaye akisema, Mtume **(s.a.w.w)** amesema: "**Muuguzaji asimkurubie mtu mzima (asiyeumwa)." Abu Hurairah akaikanusha hadithi yake ya kwanza sisi tukasema: "Siyo wewe uliye tusimulia kuwa hakuna kuambukizana." Basi Abu Hurairah akazungumza Kihabeshi (kupoteza lengo), Abu Salamah akasema, "Sikumuona akisahau hadithi isipokuwa hadithi hiyo**." Pamoja na kwamba hadithi hizi mbili zinapingana inayosema hakuna kuambukizana, na ile ya mtu anayeuguza asimsogelee mtu asiyeumwa, Muslim naye amezieleza ndani ya sahih yake katika

Kitabus- salam, Babu La Ad-wa walaatiirah walaa Hammah wala Safr wala Nau-u, wala Ghaulu, wala yuuridanna Mumaridhun ala musihin.

Na kwa kupitia hadithi hizi, tunafahamu kwamba ile hadithi isemayo, "Muuguzaji asimsogelee mtu mzima (asiyeumwa)" ni hadithi sahihi aliyoisema Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** kwani haipingani na elimu. Amma ile hadithi isemayo, "Hakuna kuambukizana" hiyo ni hadithi ya uongo aliyozushiwa bwana Mtume, kwani hadithi iliyosemwa na mtu asiyejuwa ukweli wa maumbile. Na kwa ajili hiyo basi baadhi ya Masahaba walitambua kupingana kwa hadithi hizi ndipo walipomkemea Abu Hurairah na wakamshangaa kwa hadithi yake ile ya kwanza, na hapo Abu Hurairah hakuwa na njia ya kukwepa mtego huu matokeo yake akaongea Kihabeshi kupoteza lengo. Kinachotuongezea nguvu kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa mbele mno kitaaluma kuliko ilivyothibitishwa na elimu za kisasa hasa kuhusu maradhi ya kuambukiza ni kwamba alikuwa akiwaonya Waislamu dhidi ya tauni, ukoma, kipindupindu na mengineyo. Bukhari ameyaandika hayo ndani ya sahih yake, Kitabul-anbiyai, Babu haddathana Abul-yaman, pia Muslim ndani ya sahih yake Kitabus-salam, Babut-taau'un wat-tirah wal-kahanah waghairiha.

Imepokewa kutoka kwa Usamah ibn Zaid amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** amesema: "Tauni ni maradhi mabaya, yalipelekwa kwa watu fulani katika wana wa Israeli, au kwa wale waliokuwa kabla yenu, basi mkiyasikia yameingia mahala fulani msiende huko, na yakiingia mahala mlipo ninyi msitoke kuyakimbia" Na katika riwaya nyingine "Kisikutoeni kitu isipokuwa kwa kuyakimbia." Na imethibiti kutoka kwake Mtume **(s.a.w.w)** kauli yake inayotoa maana hii, "Muepuke mwenye ukoma kama unavyomuepuka simba." Na kauli yake isemayo, "Mmoja wenu anapokunywa (maji au...) asipumulie ndani ya chombo." Na kauli yake nyingine isemayo, "Atakaporamba mbwa ndani ya chombo cha mmoja wenu, basi kikosheni mara saba moja wapo kwa mchanga." Yote hayo ili tu apate kuuelimisha umma wake usafi na njia za afya na kujikinga na maradhi, na siyo kuwaambia (eti) "Nzi akitumbukia ndani ya kinywaji cha mmoja wenu basi amzamishe." Hadithi hii tumekwisha izungumzia unaweza kuirejea. Sisi tunakuta kupingana kuliko wazi hata katika mambo yanayohusu Al-Hammah, kitu ambacho Waarabu walikuwa wakikiona kuwa ni mkosi, na huyo ni ndege mashuhuri anayeruka usiku na inasemekana ni bundi kwa mujibu wa tafsiri ya Malik ibn Anas.

Basi kama Mtume **(s.a.w.w)** anasema: "Hakuna Hammah basi vipi anajipinga na anajilinda kutokana naye? Bukhari ameandika ndani ya sahih yake, Kitabu Bad'il-khalq Babu yuzaffuna an-nas-lan fil-Mashyi, juzuu ya nne uk.119. Imepokewa kutoka kwa Said ibn Jubair, naye kutoka kwa Ibn Abbas (r,a.) amesema, "Mtume **(s.a.w.w)** alikuwa akiwakinga Hasan na Hussein na husema bila shaka wazee wenu Ismail na Is'haqa walikuwa wakikingwa kwayo - Najilinda kwa maneno ya Mwenyezi Mungu yaliyotimia kutokana na kila shetani na Hammah na kila jicho baya." Naam, katika mlango huu tulikuwa tunataka kutaja baadhi ya mifano ya hadithi zinazopingana ambazo zinanasibishwa kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** hali ya kuwa si zake.

Kuna mamia ya hadithi nyingine zinazopingana ambazo Bukhari na Muslim wameziandika ndani ya sahihi zao na tumezitolea mifano kama ambavyo tumemzowesha msomaji wakati wote kumletea kwa mukhtarsari na kumuashiria. Hivyo basi kwa wale watafiti wanalazimika kufuatilia kuyasoma hayo huenda Mwenyezi Mungu akaitakasa Sunna ya Mtume wake **(s.a.w.w)** kupitia kwao na kuwalipa malipo makubwa na wao wakawa ndiyo sababu ya kuitakasa haki kutokana na batili na wakaziletea zama hizi mpya utafiti madhubiti kwa kiwango kinachotakiwa na ujumbe wa Uislamu:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّـهَ وَقُولُوا قَوْلًا سَدِيدًا ﴿٧٠﴾ يُصْلِحْ لَكُمْ أَعْمَالَكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ
ذُنُوبَكُمْ وَمَن يُطِعِ اللَّـهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ فَازَ فَوْزًا عَظِيمًا ﴿٧١﴾

Enyi mlioamini, muogopeni Mwenyezi Mungu na mseme maneno ya kweli, Mwenyezi Mungu atakutengenezeeni vizuri matendo yenu na atakusameheni madhambi yenu, na yeyote anayemtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, bila shaka amefanikiwa mafanikio makubwa. (Qur'an, 33:70-71).

22

# WAULIZE WANAOFAHAMU

## MLANGO WA NANE

### YANAYOZIHUSU SIHAH MBILI, BUKHARI NA MUSLIM

Vitabu hivi viwili ni muhimu sana kwa Masunni kiasi kwamba vimekuwa ni rejea madhubiti na ni misingi ya mwanzo kwa kila mtafiti anayehusika na uchunguzi wa kidini. Imekuwa ni jambo gumu kwa baadhi ya wanaofanya utafiti kuyabainisha wazi wanayoyakuta humo miongoni mwa mambo yanayoidhalilisha dini, kupingana kwa hadithi zilizomo na mambo mengine machafu. Basi wao huyakubali tu kwa kuwa wafanyeje na wala hawawabainishii watu wao kwa kuwachelea watu hao, au kujichelea wao wenyewe kutokana na heshima na utukufu walioutengeneza kuhusu vitabu hivi.

Ukweli uliopo ni kuwa, Bukhari na Muslim hawakupata kuota ndoto hata siku moja kwamba vitabu vyao vitafikia heshima hiyo kwa wanachuoni na watu wa kawaida. Sisi tunapovikosoa vitabu hivi, siyo kwa sababu yeyote ila ni kwa kumtakasa Mtume wetu **(s.a.w.w)** ili Ismah yake isije ikavunjwa. Na kama wako baadhi ya masahaba ambao hawakusalimika na jambo hili la kukosolewa kwa lengo lile lile, kwa hiyo basi Bukhari na Muslim siyo wabora kuliko hao Masahaba ambao walikuwa karibu mno na Mtume **(s.a.w.w)**.

Na maadam bado tunalenga kumtakasa Mtume **(s.a.w.w)**, tunajaribu kwa kadiri ya uwezo wetu kuithibitisha, Ismah ya Mtume na kwamba yeye ndiye mjuzi mno na ni mcha Mungu mno kuliko watu wote kwa jumla. Tunaitakidi kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu alimteua ili awe ni rehma kwa viumbe, na akamtuma kwa viumbe wote watu na majini. Basi hapana shaka kwamba Mwenyezi Mungu anatutaka tumtakase na tumuheshimu na tusikubali afedheheshwe. Kutokana na sababu hizo basi, sisi na kila Muislamu tunatakiwa kupinga kila kinachopingana na mwenendo wake Mtukufu, na tukatae kila kinachopingana na Ismah yake ya kutokuwa na makosa au kitu chochote kinachotia dosari heshima yake tukufu ikiwa kinatoka mbali au karibu. Kwa hakika Masahaba, Tabiina (waliowafuatia Mashaba), Maimamu pamoja na Maulamaa wa hadithi na Waislamu wote na hata watu wote wanapaswa kulinda fadhila na heshima ya Mtume **(s.a.w.w)**.

Watu wanaopinga (Bukhari na Muslim wasikosolewe) na kung'ang'ania (kila kilichomo vitabuni mwao kuwa ni sahihi) bila shaka watachukia kwa kila watakachokiona kuwa ni kipya kwao. Lakini radhi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiyo makusudio (yetu) na radhi ya Mtume wake **(s.a.w.w)** ndiyo matarajio (yetu), na hiyo ndiyo akiba na hazina ya kweli siku ambayo haitamfaa (mtu) mali wala watoto ila yule atakayemfikia Mwenyezi Mungu kwa moyo ulio salimika. Pamoja na yote hayo, sisi tunaridhaa na faraja kwa waumini wa kweli ambao waliufahamu utukufu wa Mwenyezi Mungu na heshima ya Mtume wake **(s.a.w.w)** kabla ya kufahamu heshima ya watawala, Makhalifa, na hata Masultani. Nakumbuka wakati fulani nilipambana na upinzani mkali mpaka nikatuhumiwa kuwa nimekufuru na

nimetoka katika dini pale tu nilipomkosoa Bukhari kwa kosa lake la kuiandika hadithi isemayo kuwa, "Nabii Musa (a.s) alimpiga Malaika wa mauti na kumpofua jicho lake." Matokeo yake niliambiwa, "Wewe ni nani mpaka umkosoe Bukhari?" Jamaa hao walizua zogo na makelele kama kwamba mimi nimeikosoa aya fulani ndani ya kitabu cha Mwenyezi Mungu. Ukweli wa mambo ulivyo ni kwamba, pindi mchunguzi yeyote atakapojinasua kutoka kwenye kifungo cha kufuata kama kipofu na kung'ang'ania ung'ang'anizi usiokuwa na maana, bila shaka atayakuta ndani ya Bukhari na Muslim mambo ya ajabu na ya kushangaza ambayo moja kwa moja yako kinyume cha akili ya Mwarabu (Bedui) wa jangwani ambaye fikra zake bado zimeganda na anaamini kuhusu baadhi ya mambo ya uzushi na ngano za kale, na fikra zake bado zimeelemea kwenye mambo ya ajabu. Hali kama hii sio jambo la aibu, na wala hatumtuhumu kuwa yuko nyuma kimawazo kwa sababu maisha yake ya zama za kale si sawa na zama za mawasiliano ya satellite, simu na rocket.

Jambo la msingi hapa ni kwamba, sisi hatutaki mambo hayo yahusishwe na Mtume **(s.a.w.w)**, kwani tofauti iliyopo nikubwa na mwanya ni mpana sana, kwani yeye ni yule ambaye Mwenyezi Mungu alimtuma kutoka kwa wakazi wa Maka ili awasomee aya zake na awatakase na awafundishe kitabu na hekima, na kwa kuwa yeye ndiye Nabii na Mitume mwisho, basi Mwenyezi Mungu amemfunza elimu za watu wa mwanzo na wa mwisho. Kama ambavyo tunamfahamisha msomaji mtukufu ya kwamba, siyo kila kilichomo ndani ya Bukhari basi kinanasibishwa kwa Mtume, kwa hakika Bukhari hupata akaiandika hadithi ya Mtume **(s.a.w.w)** kisha akaifuatishia maoni ya baadhi ya Masahaba, kisha msomaji wake hubakia akiamini kuwa rai hiyo au hadithi hiyo ni ya Mtume wa Mwenyezi Mungu wakati ambapo siyo yake.

Ninakupigia mfano wa jambo hilo: Bukhari ameandika ndani ya sahih yake, Kitabul-hiyal Babu fin-nikah juzuu ya nane ukurasa wa 62 amesema: Imepokewa kutoka kwa Abu Hurairah kutoka kwa Mtume **(s.a.w.w)** amesema: "Mwanamke bikra haolewi isipokuwa aulizwe, wala mwanamke mkubwa (haolewi) mpaka ashauriwe." Basi pakaulizwa, "Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu kukoje kukubali kwake?" Mtume akasema: "Atakaponyamaza." Baadhi ya watu wakasema, "Kama mwanamke bikra asipoulizwa na akawa hakuolewa kisha mtu fulani akafanya hila akasimamisha mashahidi wawili wa uongo kwamba yeye amemuoa mwanamke yule kwa ridhaa yake, na kadhi akaithibitisha ndoa yake na hali mume anatambua kwamba ushahidi ule ni wa uongo, basi siyo vibaya kumuingilia nayo ni ndoa sahihi."

Basi hebu iangalie kauli ya Bukhari (baada ya kumalizika hadithi ya Mtume **(s.a.w.w)** anasema, "Baadhi ya watu wakasema." Ni kwa nini basi kauli ya baadhi ya watu, tena wasiojulikana isemayo kwamba ndoa ya ushahidi wa uongo ni ndoa sahihi? Mahala kama hapa panamchanganya msomaji na kufikiria kuwa hayo ni maoni ya Mtume kitu ambacho siyo sahihi. Mfano mwingine: Bukhari ameandika ndani ya sahihi yake, Kitabu Bad-il-khalqi Baba Manaqibul-muhajirina wafadhlihim, juzuu ya nne ukurasa wa 203. Imepokewa kutoka kwa Abdallah ibn Umar (r.a) amesema: "Katika zama za Mtume **(s.a.w.w)**, tulikuwa hatumlinganishi Abubakr na

mtu yeyote (kwa ubora), kisha (hufuatia) Umar halafu Uthman, kisha tunawaacha Masahaba wa Mtume na hatumboreshi (yeyote) baina yao." Bila shaka hayo ni maoni ya Abdallah ibn Umar na wala hawajibiki kwa maoni hayo isipokuwa yeye mwenyewe binafsi, vinginevyo atakuwa wapi Ali ibn Abi Talib ambaye ni mbora wa watu baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, lakini kwa Abdallah ibn Umar hana ubora wowote na amemuweka katika kundi la watu wa kawaida? Na kwa ajili hiyo ndiyo maana Abdallah ibn Umar alikataa kumpa baia Imam Ali na kumtawalisha, na yeyote yule ambaye Ali siyo mtawala wake basi huyo siyo muumini. Ali huyo huyo ndiye yule ambaye Mtume **(s.a.w.w)** amesema kuhusu haki ya Imam Ali, "Ali yuko pamoja na haki na haki iko pamoja na Ali." Na huyu Abdallah ibn Umar alimpa baia adui wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake na waumini aliyekuwa akiitwa Al-hajjaj ibn Yusuf ambaye ni mtu muovu na fasiki.

Lengo letu siyo kurejea kwenye maudhui hizo, lakini tunataka kumdhihirishia msomaji namna alivyo Bukhari na walio mfano wake, yeye anaiandika hadithi hii katika mlango wa sifa za Muhajirina kama kwamba yeye anataka kuwatambulisha wasomaji kwa njia ya kificho kwamba hayo ni maoni ya Mtume **(s.a.w.w)** wakati ambapo hayo ni maoni ya Abdallah ibn Umar ambaye alimfanyia uadui Imam Ali (a.s). Tutambainishia msomaji anayetumia akili msimamo wa Bukhari juu ya kila jambo linalomuhusu Ali ibn Abi Talib, na ni vipi alivyojaribu kwa juhudi zake zote kuficha ubora wake ili kumdhalilisha. Kama ambavyo Bukhari ameandika ndani ya sahih yake, Kitabu Bad-il-khalq Bahn Haddathanal-Humcridi amesema: "Ametusimulia Muhammad ibn Kathir, ametueleza Sufiyan, ametusimulia Jami'i ibn Abi Rashid, ametusimulia Abu Ya'ala kutoka kwa Muhammad ibn Al-hanafiyah amesema: "Nilimwambia baba yangu, ni mtu gani bora baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**? Akasema, "Abubakr." Nikasema, "Kisha nani?" Akasema, "Kisha Umar." Basi nilichelea kuwa atasema Uthman nikasema, "Kisha wewe." Akasema, "Mimi si lolote isipokuwa ni mtu miongoni mwa Waislamu."

Naam hadithi hii wameizusha kupitia ulimi wa Muhammad ibn Al-hanafiyyah ambaye ni mtoto wa Imam Ali ibn Abi Talib, na hii hadithi ni kama ile iliyotangulia ambayo imepokewa kwa ulimi wa Abdallah ibn Umar, na matokeo yake ya mwisho ni ya namna moja, japokuwa Ibnul-hanafiyyah alichelea kuwa baba yake angemtaja Uthman kuwa ndiyo watatu. Lakini jibu la baba yake aliposema, "Mimi si chochote isipokuwa ni mtu tu miongoni mwa Waislamu," linatosheleza kwamba, Uthman ni bora kuliko yeye (Ali), kwani hapana mtu yeyote miongoni mwa Masunni anayesema kuwa Uthmani si lolote bali yeye ni mtu miongoni mwa Waislamu tu. Masunni wanasema kuwa, kama ilivyotangulia kwamba wabora wa watu ni Abubakr kisha Umar kisha Uthmani kisha tunawaacha Masahaba wa Mtume **(s.a.w.w)** hatumboreshi yeyote baina yao, na baada ya hapo watu wote ni sawa sawa. Je, hamuzishangai hadithi hizi anazozithibitisha Bukhari, ambazo zote zina lengo moja nalo ni kumvua Ali ibn Abi Talib kila namna ya ubora (alionao)? Je, hali hii haifahamishi kuwa Bukhari alikuwa akiandika kila lile linalowaridhisha Banu Umayyah na Banu Abbas na watawala wote ambao walisimama kuwavunja watu wa

nyumba ya Mtume? Bila shaka hizo ni dalili tosha kwa yule anayetaka kupata ukweli.

Bukhari na Muslim wanaeleza kila kitu ili kuwatukuza Abu bakr na Umar Bukhari ameandika ndani ya sahihi yake katika Kitabu Bad-il-khalq, Babufadhail Abibakrs-siddiq (r.a).

Imepokewa kutoka kwa Abu Hurairah amesema: "**Mtume alisali sala ya asubuhi kisha akawaelekea watu akasema: Kuna wakati fulani mtu mmoja alikuwa anamswaga ng'ombe basi mara alimpanda kisha akampiga, yule ng'ombe akasema, Sisi hatukuumbwa kwa ajili hii, bila shaka tumeumbwa kwa ajili ya kilimo. Watu wakasema, Sub-hanallahii!! (walishangaa) Ng'ombe anazungumza? Mtume akasema: Mimi naamini jambo hili na Abubakr na Umar. Wakati huo Abubakr na Umar hawakuwepo hapo**.

Na kuna wakati fulani mtu mmoja, alikuwa akichunga mifugo yake, basi ghafla mbwa mwitu alimvamia na kuchukua mbuzi mmoja. Yule mchungaji alimtafuta mbwa mwitu na kumwokoa kondoo kutoka kwa mbwa mwitu. Yule mbwa mwitu akamwambia mchungaji; Umemuokoa kutoka kwangu basi ni nani atakayemuokoa siku ya Qiyama, siku ambayo hapana mchunga ila mimi? Basi watu wakasema, Sub-hanallah!! Mbwa mwitu anazungumza? Mtume akasema, Mimi ninaamini jambo hilo na Abubakr na Umar (nao wanaamini)." Wao hawakuwepo hapo (mahala wakati Mtume anazungumza). Na hadithi hii ni wazi kabisa kuwa ni kuazimisha na ni miongoni mwa hadithi zilizozushwa kuhusu ubora wa Makhalifa hao wawili, vinginevyo ni kwa nini watu wanapinga hali wao ni masahaba wa Mtume, (wanapinga) yale anayowaambia mpaka analazimika kukariri mara ya pili kuwa "Mimi na Abubakr na Umar tunaamini jambo hili."

Kisha hebu angalia msimuliaji wa hadithi hii anavyotilia mkazo kuwa Abubakr na Umar hawakuwepo mahala hapo mara mbili zote, kwa hakika huu ubora wanaopachikwa ni mambo ya kuchekesha na wala hayana maana yoyote. Lakini jamaa hawa ni sawa na mfa maji anayeshikilia majani (kutaka kujiokoa), na hao wazushi wa hadithi walipokosa mambo au matukio muhimu yatakayotajwa kwa ajili ya Abubakr na Umar, basi akili zao zikatunga fadhila kama hizi, na nyingi ya hizo wamezileta kama ndoto za kubuni, hazina dalili ya kihistoria wala kimantiki au kielimu. Kama ambavyo Bukhari ameandika ndani ya sahih yake, Kitabu fadhail As-habin-Nabiyyi **(s.a.w.w)**, Babu Qaidin-nabiyyi **(s.a.w.w)** Lau kiintii Mut-takhidhan khalilan. Na Muslim ndani ya sahih yake katika Kitabufadhailis-sahabah, Babu min fadhail Abibakr Siddiq (r.a.). Imepokewa kutoka kwa Amr ibn Al-a's kwamba, Mtume **(s.a.w.w)** alimtuma kwenye jeshi la Dhatus-salasil, nikamjia nikamwambia, "Je, ni watu gani wapendao mno?" Akasema ni "Aisha", Nikasema, Je, kwa wanaume? Akasema, "Baba yake "Aisha" Nikasema, "Kisha nani?" Akasema "Umar ibn Al-Khatab" Wakawaorodhesha watu wengi."

Riwaya hii imewekwa na wazushi pindi walipofahamu kwamba, historia imesajili ndani ya mwaka wa nane (yaani miaka miwili kabla ya kufariki Mtume **(s.a.w.w)** kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu alituma jeshi ambalo ndani yake alikuwemo Abubakr na Umar wakiwa chini ya uongozi wa Amr ibn Al-a's kwenda kupigana Dhatis-Salaasil, (walizusha riwaya hii)

kwa lengo la kuikata njia ya yeyote atakayesema kuwa, "Amr ibn Al-a's alikuwa akitangulizwa kwa cheo juu ya Abubakr na Umar. Utawaona waliitengeneza riwaya hii kupitia ulimi wa Amri ibn Al-a's mwenyewe ili kuitia nguvu fadhila ya Abubalcr na Umar na wakamuingiza bibi Aisha ili kumuondoa shaka kwa upande mmoja, na ili kumpa hadhi isiyo na mpaka bibi Aisha kwa upande mwingine. Na kwa ajili hiyo utamuona Imam Nawawi ndani ya sharh yake ya sahihi Muslim anasema: "Hii ni kuweka bayana ubora wa Abubakr na Umar na Aisha (r.a) na ndani yake mna dalili iliyo wazi kwa Masunni katika kumboresha Abubakr juu ya Masahaba wote na baada yake ni Umar."

Riwaya hii ni kama riwaya nyingine dhaifu ambazo mad-dajjali (wazushi) hawakuona haya kuzizua hata kwa kupitia ulimi wa Ali ibn Abi Talib mwenyewe, ili tu kwa kupitia riwaya hizo wavunje hoja za Mashia ambao wao wanasema kuwa Ali ibn Abi Talib ni bora kuliko Masahaba wengine, hii ni kwa upande mmoja.

Na kwa upande wa pili wawafikirishe Waislamu kwamba Ali mwenyewe hakuona kuwa alidhulumiwa na wala hakuwalalamikia Abubakr na Umar (kutokana na dhulma aliyofanyiwa).

Bukhari ameandika ndani ya sahihi yake, Kitabu fadhail as-habinnabiyyi **(s.a.w.w)** Babu manaqib Umar ibn Khat-taab Abi hafs. Muslim naye ndani ya sahihi yake, Kitabu fadhailis-sahabah Babu min fadhail Umar (r.a). Imepokewa kutoka kwa Ali, kutoka kwa ibn Abbas amesema: "Umar aliwekwa kitandani kwake na watu wakamzunguka wanaomba na kusali kabla hajanyanyuliwa, mimi nilikuwa miongoni mwao na mara kuna mtu fulani akanishika bega langu, kumbe alikuwa Ali, basi akamrehemu Umar na akasema: Hukumuacha mtu yeyote nimpendaye mno ili nitakapokutana na Mwenyezi Mungu niwe na amali mfano wa amali yako, namuapa Mwenyezi Mungu ninaamini Mwenyezi Mungu atakuweka pamoja na Masahaba wako wawili (Mtume na Abubakr) mara nyingi nilikuwa namsikia Mtume akisema: Nilikwenda mimi, Abubakr na Umar, nimeingia mimi, Abubakr na Umar, nimetoka mimi Abubakr na Umar." Naam hadithi hii dhahiri ni ya kubuni inasikika humo harufu ya siasa ilivyofanya kazi yake katika kumuweka mbali Fatmah asizikwe karibu na Baba yake pamoja na kuwa yeye Fatmah ni wa kwanza kumfuata Mtume katika kufa. Na muelezaji wa hadithi hii alisahau kuongeza baada ya kauli yake, Nilikwenda mimi Abubakr na Umar, niliingia mimi Abubakr na Umar na nilitoka mimi Abubakr na Umar, na nitazikwa mimi Abubakr na Umar.

Hivi watu hawa hawaoni ubaya kutolea hoja riwaya kama hizi ambazo zinapingwa na ukweli wa historia na vitabu vya Waislamu vilivyojaa (maelezo yanayohusu) dhulma dhidi ya Ali na Fatmah ambayo ilitendwa na kina Abubakr na Umar muda wote wa uhai wao? Kisha hebu izingatie kwa makini riwaya hii ili umuone mpokezi wa riwaya hii anavyomfanya Ali kuwa ni mtu kutoka mbali amekuja kuangalia maiti ya mtu asiyemtambua. Basi akawakuta watu wamesongamana (kwenye maiti huyo) wanaomba na kumsalia, akamshika Ibn Abbas begani na inakuwa kama kwamba alimnong'oneza sikioni maneno yake hayo na akaondoka, na ukweli wenyewe ni kuwa Ali katika msiba huo awe mbele ya watu na awasalishe na asimuache Umar mpaka azikwe kaburini mwake. Kwa kuwa watu katika

zama za utawala wa Banu Umayyah walikuwa wakishindana kutengeneza hadithi (za uongo) kutokana na amri ya Muawiyah ambaye alitaka kunyanyua vyeo vya akina Abubakr na Umar dhidi ya ubora wa Imam Ali ibn Abitalib, basi zilikuja hadithi nyingi zinazozungumzia ubora wao zinazochekesha, na wakati mwingine zinapingana zenyewe kwa zenyewe kufuatana na namna ya matamanio ya msimuliaji anavyotaka. Miongoni mwa hao wasimuliaji wako wale wa Kibanu Taim ambao walikuwa hawamtangulizi yeyote juu ya Abubakr, na wako wengine ni katika Banu Adiyyi ambao hawakuwa wakimtanguliza yeyote juu ya Umar, na Banu Umayyah ambao nao waliathiriwa na Umar ibn Khattab ambaye alikuwa mjeuri na msusuavu asiyejali kufanya lolote wala asiyeogopa kitu. Basi mara nyingi walimsifia na kumtengenezea hadithi ambazo zinamboresha zaidi ya Abubakr.

Hebu angalia baadhi ya mifano hiyo: Muslim ameandika ndani ya sahihi yake katika Kitabu fadhailis-sahabah Babu min fadhail Umar (r.a). Naye Bukhari ameandika ndani ya sahih yake, Kitabul-iiman Babu tafadhul ahlil-iiman fll-a 'atrial Imepokewa kutoka kwa Abu Said Al-khudri amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema, wakati fulani nilikuwa nimelala niliwaona watu wanaletwa kwangu na wamevaa kanzu, baadhi ya kanzu hizo zimefika vifuani na nyingine hazikufikia hapo, na aliletwa kwangu Umar ibn Khattab akiwa amevaa kanzu anaikokota. (Masahaba) wakasema, Ulifasiri nini juu ya hilo ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Mtume akasema: Hiyo ni dini."

Na kama tafsiri ya Mtume kwa ndoto hii itakuwa ni dini, basi maana hiyo itakuwa kwamba, Umar ni bora kuliko watu wote kwa dini, kwa mujibu wao dini haikufika vifuani na haikuingia nyoyoni mwao, wakati ambapo Umari amejaa dini kuanzia kichwani mpaka kwenye nyayo zake na zaidi ya hapo anaikokota dini nyuma yake kama inavyokokotwa kanzu. Sasa basi, Abubakr hapa ana hadhi gani, Abubakr ambaye (inasemekana) imani yake inalinganishwa na imani ya umma wote? Ni kama ambavyo Bukhari ameandika ndani ya sahih yake, Kitabul-ilmi Babu fadhil-ilmi, na Muslim naye ameandika ndani ya sahih yake Kitabu fadhailis-sahabah Babu fadhail Umar.

Imepokewa kutoka kwa ibn Umar amesema: "Nilimsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu akisema, Kuna wakati fulani nilikuwa nimelala nikakuta jagi la maziwa, basi nilikunywa mpaka nikaona manukato yanatoka vidoleni mwangu, kisha nikampa Umar ibn Khattab ziyada niliyobakisha, Masahaba wakasema, basi ulifasiri nini (ndoto yako) ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, Mtume akasema: "Maana yake ni elimu nyingi." Mimi nasema, hivi kweli wako sawa wale wanaojua na wale wasiyojua? Ikiwa ibn Khatab ameuzidi umma wote au watu wote katika dini akiwemo Abubakr, basi ni wazi kabisa ndani ya riwaya hii kwamba Umar pia amewazidi katika elimu na kuwa yeye ndiye mjuzi mno kuliko watu wengine baada ya Mtume **(s.a.w.w)**. Sasa imebaki aina nyingine ya ubora ambayo watu hushindana katika kujipamba nayo na kwamba wanahusika nayo, na ubora huo ni miongoni mwa sifa njema ambazo Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanazipenda na watu wote wanaipenda na wanajaribu kuifikia, sifa hiyo si nyingine bali ni ushujaa. Hapana budi kwa watu wanaosimulia hadithi

kuzua hadithi ambayo itakuwa ni kwa faida ya Umar ibn Khatab na hawakuacha kulifanya jambo hilo. Bukhari ameandika ndani ya sahih yake katika Kitabu fadhail as-habin-Nabiyyi **(s.a.w.w)**, Babu qaulin-Nabiyyi Lau kuntu muttakhidhan khalilan. Pia Muslim ameandika ndani ya sahih yake, Kitabu fadhailis-sahabah Babu fadhail Umar.

Imepokewa kutoka kwa Abu Hurairah amesema, "Nilimsikia Mtume **(s.a.w.w)** anasema: Kuna wakati fulani nilikuwa nimelala, basi niliona niko juu ya kisima, juu yake kuna ndoo nikachota kutoka kisimani kiasi alichotaka Mwenyezi Mungu, kisha akaichukua ndoo ile ibn Abi Qahafah (Abubakr) akachota ndoo moja au mbili na katika kuchota kwake kulikuwa na udhaifu fulani Mwenyezi Mungu amsamehe kutokana na udhaifu wake. Kisha ikageukia upande wa magharibi na akaichukua Ibn Khattab, basi sikumuona mtu hodari miongoni mwa watu aliyechota namna alivyochota Umar mpaka watu walikunywa na kutosheka."

Sasa basi ikiwa dini ni kituo cha Imani, Uislamu, Uchamungu na kuwa karibu na Mwenyezi Mungu Mtukufu, kisha Umar ndiye aliyeizingira kiasi cha kuikokota nyuma yake wakati ambapo watu wengine hawakupata isipokuwa kiasi cha kufikia kifuani na sehemu nyingine za miili yao ikabakia wazi, na pia kama elimu aliyohusishwa nayo Umar ibn Khattab haikuwabakishia watu wengine chochote katika masazo aliyoyasaza Mtume **(s.a.w.w)**, kwani yote alimpa Umar naye akayanywa yote bila hata kumkumbuka rafiki yake Abubakr, basi hapana shaka kwamba elimu hiyo ndiyo aliyoimiliki Umar katika kugeuza maamuzi ya Mwenyezi Mungu baada ya kufariki Mtume kwa Ijtihadi yake. Hapana shaka pia kwamba ijtihadi yake ndiyo matokeo ya elimu hiyo. Na kama nguvu zile na ushujaa ule amehusika nao Umar ibn Khattab, vile vile baada ya unyonge uliojitokeza kwa jamaa yake Abubakr na hii ni kweli (alikuwa dhaifu) kwani Abubakr alipata kumwambia Umar, "Bila shaka nimekwisha kukuambia kuwa kuhusu jambo hili wewe ni mwenye nguvu kuliko mimi na hakika umenishinda."

Mwenyezi Mungu na amsamehe Abubakr kwa unyonge wake na kwa kutangulia kwake kushika Ukhalifa kabla ya Umar, kwani wasaidizi wa Umar miongoni mwa Banu Adi na Banu Umayyah hawakustarehe wala kunufaika na kujipatia ngawira na ushindi mbali mbali kama walivyoyapata hayo katika zama za Ukhalifa wa Umar. Naam yote hayo basi ndiyo fadhila na ubora wa Umar ibn Khattab katika maisha ya duniani kwa hiyo ni lazima pia wamdhaminie pepo huko akhera kwa daraja kubwa na ubora mwingi zaidi ya rafiki yake Abubakr, na walifanya hayo ili kumpandisha daraja na kumpa ubora. Bukhari ameandika ndani ya sahih yake, Kitabu bad-ilkhalq Babu majaa fi sifatil-jannah wa an-nahaa mak-khluuqah, na Muslim naye ameandika ndani ya sahih yake katika Kitabu fadhailis-sahabah Babu min fadhail Umar.

Imepokewa kutoka kwa Abu Hurairah (r.a) amesema: "Wakati fulani sisi tulikuwa mbele ya Mtume **(s.a.w.w)** akasema: Kuna wakati nilikuwa nimelala, nilijiona nimo peponi, basi mara alikuja mwanamke akawa anatawadha pembeni ya jumba fulani, mimi nikasema, jumba hili ni la nani? Wakasema, ni la Umar ibn Khattab. Nikaukumbuka wivu wake (Umar), basi nikageuka nikaondoka, Umar akalia na akasema: Nikufanyie wivu wewe

Mtume wa Mwenyezi Mungu?" Ndugu yangu msomaji bila shaka umegundua mfumo wa riwaya hizi, mimi nimeziorodhesha kila moja kwenye ile ibara moja inayofanana katika kila riwaya ambayo inahusika na ubora wa Umar ibn Khattab, ibara hiyo si nyingine ila ni ile kauli ya Mtume (ambayo haiwezekani moja kwa moja kuwa aliisema) kauli inayosema: "Wakati fulani nilikuwa nimelala." Ibara hii utaikuta ndani ya riwaya zote. Wakati fulani nilikuwa nimelala niliwaona watu wakionyeshwa kwangu, wakati fulani nilikuwa nimelala nilikuta jagi la maziwa, wakati fulani nilikuwa nimelala niliona kisima, na wakati fulani nilikuwa nimelala nilijiona nimo peponi. Huenda mpokeaji wa hadithi alikuwa rnwingi wa kuota ndoto na kuchanganyikiwa akawa huzifasiri na kutengeneza riwaya kupitia ulimi wa Mtume **(s.a.w.w)**. Ni mara nyingi Mtume amezuliwa zama za uhai wake naye akiwa yupo mbele ya watu hao, basi vipi baada ya kufariki kwake (wamemzulia mengi mno) na kwa hakika watu wa umma huu walikwisha geuka na wakauana wao kwa wao, wakawa makundi na madhehebu mengi na kila kundi wakishangilia na kujivunia mambo waliyonayo.

Sasa kimebaki kitu kimoja ambacho wamekisajili wanahistoria na Masahaba waliokuwa ni mashabiki wa Umar ibn Khattab mwenyewe, kitu hicho si kingine bali ni tabia aliyokuwa akisifika nayo Umar ambayo ni ile tabia mbaya ya ususuavu na ukali kwa watu, na yeyote mwenye tabia hii mara nyingi watu huwa hawampendi. Mwenyezi Mungu anasema:

وَلَوْ كُنتَ فَظًّا غَلِيظَ الْقَلْبِ لَانفَضُّوا مِنْ حَوْلِكَ ﴿١٥٩﴾

"Na lau (wewe Muhammad) ungekuwa mkali na mgumu wa moyo wangekukimbia." (Our'an, 3:159).

Kwa bahati mbaya mashabiki wa Umar wao wanaufanya upungufu na dosari hiyo kuwa ni tendo la kusifiwa, na uovu kuwa ni ndiyo heshima. Kutokana na hali hiyo walifanya makusudi kutengeneza riwaya zinazoonesha udhaifu na udhalili ili kuipaka matope heshima ya Mtume **(s.a.w.w)** ambaye Mwenyezi Mungu anashuhudia kuwa Mtume hakuwa mkali wala mgumu wa moyo, bali Mtume ni mpole wa tabia. "Na kwa rehma itokayo kwa Mwenyezi Mungu umekuwa mpole kwao na kwa hakika wewe (Muhammad) una tabia njema ya hali ya juu, na mpole mwenye huruma kwa waumini .... na ni rehma kwa walimwengu wote." Basi hebu na tuwasikilize wajinga hawa wanasema nini kumuhusu Mtume **(s.a.w.w)**. Bukhari ameandika ndani ya sahih yake Kitabu Bad-il-khalq Babu sifati Iblis Wajunudih, naye Muslim ameandika ndani ya sahihi yake, Kitabu fadhailis-sahaba Babu minfadhail Umar.

Imepokewa kutoka kwa Sa'ad ibn Abi Waqqas amesema: "Umar alibisha hodi nyumbani kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** na mbele yake walikuweko wanawake miongoni mwa Maquraish wakizungumza naye na wakimdadisi, sauti zao zikiwa zinapaa juu. Basi alipobisha hodi Umar walisimama na mara moja wakavaa hijabu. Mtume wa Mwenyezi Mungu akamkaribisha Umar hali yakuwa Mtume anacheka. Umar akasema;Mwenyezi Mungu akufurahishe ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu. Mtume akasema; Nawashangaa wanawake waliokuwa hapa, walipokusikia sauti yako wote wamekimbilia ndani. Umar akasema, Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu wewe ndiyo ilikuwa na inastahiki

wakuogope. Kisha akasema kuwaambia wanawake hao, Enyi maadui wa nafsi zao mwaniogopa mimi na wala hamumuogopi Mtume wa Mwenyezi Mungu? Wale wanawake wakasema, Ndiyo wewe ni mkali na msusuavu mno kuliko Mtume wa Mwenyezi Mungu. Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema kumwambia Umar, Wallahi namuapa Mwenyezi Mungu ambaye nafsi yangu imo mikononi mwake kamwe shetani hawezi kukuta unapita njia fulani isipokuwa atapita njia nyingine isiyokuwa njia yako." Ni maneno machafu yatokayo vinywani mwao, hawasemi isipokuwa ni uongo.

Hebu tazama ubovu wa riwaya hii na ni vipi wanawake wale wamuogope Umar na wasimuogope Mtume wa Mwenyezi Mungu na wanyanyue sauti zao juu ya sauti ya Mtume **(s.a.w.w)** na wala wasimuheshimu na wala wasiwe na hijabu mbele ya Mtume, na kwa kiasi cha kusikia tu sauti ya Umar walinyamaza na kuharakia kuvaa hijabu. Wallahi nashangazwa na mambo ya watu hawa wajinga ambao hayawatoshi yote hayo mpaka wayanasibishie wazi wazi kwa Mtume kwamba yeye ni mkali na ni msusuavu, kwani Umar ni mkali mno na ni msusuavu mno kuliko Mtume wa Mwenyezi Mungu. Eti hayo ni miongoni mwa matendo yanayopewa ubora kama huu na hayo yaonekane kuwa ndiyo fadhila za Mtume wa Mwenyezi Mungu. Kama mambo yako hivyo basi Umar ni bora zaidi kuliko Mtume, na ikiwa hizi ni miongoni mwa tabia mbaya, ni vipi basi Waislamu wakiongozwa na Bukhari na Muslim wanazikubali hadithi hizi?

Kisha hayo hayakuwatosha mpaka wakamfanya shetani kuwa anacheza na kufurahia mbele ya Mtume **(s.a.w.w)** na wala hamuogopi Mtume. Basi hapana shaka shetani huyu ndiye aliyewafanya wanawake wanyanyue sauti zao na wavue hijabu zao, lakini shetani alikimbia na akapita njia nyingine pale tu Umar alipoingia kwenye nyumba ya Mtume **(s.a.w.w)**. Ewe Muislamu mwenye ghera, hivi unafahamu heshima ya Mtume **(s.a.w.w)** ni ya kiwango gani kwa watu hao, na jinsi gani wao wanasema hali ya kuwa wanafahamu au hawafahamu kwamba Umar ni bora kuliko Mtume **(s.a.w.w)**? Mambo kama haya bila shaka yoyote leo hii ndiyo yanayotokea kila wanapomzungumzia Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**, na huwa wanaorodhesha makosa yake wanayoyadai na kulitakasa hilo kwa kuisema (eti) yeye Mtume ni mtu tu ambaye hakuhifadhiwa dhidi ya makosa na kwamba ni mara nyingi tu Umar akimsahihisha Mtume makosa yake, na kwamba Qur'an ilikuwa ikishuka kumuunga Umar mara nyingi tu. Yote hayo wanatolea ushahidi kupitia sura ya A 'basa Watawalla. Na kupitia suala la kuzalisha mtende kwa kutia mbelewele, pia kuhusu mateka wa Badri na mengineyo.

Lakini wewe utakaposema mbele yao kvvamba Umar alifanya makosa kwa kuzuwia sehemu ya wale wanaoimarishwa nyoyo zao, au alipoharamisha mut'aa mbili (yaani mut'atul-hajji na mut'atun-nisai) au pale alipofanya upendeleo katika kugawa kipato, basi bila shaka utaiona mishipa yao ya shingo inafura na macho yao yanakuwa mekundu, bali watakutuhumu kuwa umetoka katika dini na utaambiwa wewe ni nani hata umkosoe Umar Al-faruq ambaye ndiye anayetenganisha baina ya haki na batili? Basi hapo huna jingine la kufanya isipokuwa kukubali na usijaribu kuzungumza nao tena vinginevyo yatakukuta madhara. Bukhari anazibadili hadithi ili kulinda heshima yaUmar. Naam, bila shaka mtu anayechunguza

atakapozifuatilia hadithi za Bukhari, nyingi hatozifahamu na itamdhihirikia kama kwamba hazikukamilika au zimekatwa, na kwamba yeye Bukhari huiandika hadithi hiyo hiyo kwa sanadi ile ile, lakini mara nyingi huipatia hadithi hiyo matamko yanayotofautiana katika milango mbali mbali.

Yote hayo huyafanya kwa kumpenda kwake mno Umar ibn Khatab, na huenda jambo hilo ndilo lililo wahamasisha Masunni wampende mno Bukhari mpaka wakamtanguliza mbele kuliko vitabu vingine. pamoja na kwamba Muslim ni bora zaidi kwa udhibiti, na kitabu chake kimepangwa kufuatia utaratibu wa milango. Lakini Bukhari kwa Masunni ndiyo kitabu sahihi mno baada ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu, na hali hii imechangiwa na mwenendo wa Bukhari katika kuziporomosha kwake fadhila za Ali ibn Abi Talib. Bukhari kwa upande fulani alifanya namna ya kuzikata hadithi na kuzifupisha kila pale zilipogusa (namna fulani itakayoporomosha) heshima ya Umar, kama alivyofanya njia hiyo hiyo (kuzikata na kuzifupisha) hadithi zinazotaja ubora wa Ali. Tutakutosheleza hilo kwa baadhi ya mifano hivi punde Insha-Allah.

Baadhi ya mifano ya mabadiliko ya hadithi zenye uthibitisho unaoiweka wazi hali halisi ya Umar ibn Khattab.

1). Muslim ameandika ndani ya sahih yake katika Kitabul-haidh Babut-tayamum amesema: "Kuna mtu fulani alikuja kwa Umar akasema: Hakika mimi nimepatwa na janaba lakini sikupata maji ya kuoga, Umar akasema, Usiswali, Ammar akasema. Ewe Amirul-Muuminina hukumbuki tulipokuwa mimi na wewe katika jeshi, kisha tukapatwa na janaba na hatukupata maji, amma wewe hukusali, amma mimi nilijigaragaza kwenye udongo na nikaswali. Halafu Mtume **(s.a.w.w)** akasema: bila shaka ilikuwa inakutosha upige mikono yako kwenye ardhi kisha upulize na upake uso wako na viganja vyako. Umar akasema, Ewe Ammar mche Mungu, Ammar, akasema ukitaka sitasimulia hadithi hii." Riwaya hii wameiandika kina Abu Dawood ndani ya Sunan yake, Ahmad ibn Hambal ndani ya Musnad yake, Nasai ndani ya Sunan yake, na Baihaqi na Ibn Majah pia.

Lakini Bukhari amefanya khiyana, khiyana ya kutokuwa muaminifu katika kunakili hadithi, kama ilivyo kwa ajili ya kulinda heshima ya Umar. Ameificha hadithi hii kwa kuwa hakupenda watu wafahamu ujinga wa Khalifa Umar kutokufahamu hata kanuni nyepesi za fiqhi ya Kiislamu. Hebu basi ione riwaya hiyo ambayo Bukhari amefanya khiyana ndani yake. Bukhari ameandika ndani ya sahih yake, Kitabut-tayammum hal-yiinfakhu fihimaa. Amesema: Kuna mtu fulani alikuja kwa Umar ibn Khattab akasema, "Hakika mimi nimepatwa na janaba na sikupata maji, basi Ammar ibn Yasir akasema, kumwambia Umar ibn Khattab, hukumbuki kwamba tulikuwa safarini mimi na wewe...? Al-hadithi.

Kama unavyomuona Bukhari ameondoa kwenye hadithi hiyo maneno yasemayo, "Umar akasema usiswali." Maneno haya hayapo. na hapana shaka Bukhari aliyaondoa na kuyaacha ili yasijedhihiri madh-hebu ya Umar kwa watu, madhehebu ambayo yeye alikuwa akiyaona yanamfaa hata zama za uhai wa Mtume, na alikuwa akifanya ijtihadi dhidi ya maandiko ya Qur'an na Sunna, na alibakia kwake kwenye madhehebu yake haya hata baada ya kuwa amekuwa Khalifa na akawa anayaeneza miongoni mwa watu wa kawaida katika Waislamu. Ibn Hajar amesema: "Madhehebu haya ni

mashuhuri kuwa yametokana na Umar." Na dalili ya kwamba alikuwa akiyasisistiza madhehebu hayo ni pale Ammar alipomwambia Umar, "Ukipenda sitoisimulia hadithi hiyo." Ewe msomaji soma ushangae."

2). Al-hakim An-nishapuri ameandika ndani ya Mustadrak juzuu ya pili ukurasa 514, nave Dhahabi ameiandika hadithi hiyo ndani ya Tal-khisi yake. Imepokewa kutoka kwa Anas ibn Malik amesema:"Hakika Umar ibn Khatab alisoma kwenye mimbar kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo. "Fa anbatnaa fihaa habban wai 'naban waqadhban wazaitunan wanakhlan wahadaiqa ghul-ban wafakihatan waabbaa."

Kisha akasema yote haya tunayafahamu lakini hii Abbaa ni kitu gani? Basi fuateni yale yaliyobainishwa uongofu wake kwenu ndani ya kitabu na muyatumie, na yale ambayo hamkuyafahamu basi yarejesheni kwa Mola wake." Na riwaya hii wameinakili wafasiri wengi ndani ya vitabu vyao na tafsiri walipokuwa wakifasiri sura ya A'basa, kama vile Suyutti ndani ya Ad-durru manthur, Zamakhshari ndani ya Al-kash-shaf, Ibn Kathir ndani ya tafsiri yake, Ar-razi ndani ya tafsiri yake na Khaazin ndani ya tafsiri yake. Lakini Bukhari kama kawaida yake. hadithi hii ameiondosha na kuikata ili watu wasije wakafahamu kutokufahamu kwa khalifa Umar maana ya Al-abb na ndipo alipoinakili hadithi hii kama ifuatavyo: Bukhari ameandika ndani ya sahih yake, Kitabul-I'ilisam bil-kitabi was-sunnah babu mayukrahu min kalhratatis-sual wa takalafa maalaa ya 'anih wa Qaulullahi la 'ala La las-alu a 'n ash-yaa in-tubda lakum lasn-ukum.

Imepokewa kutoka kwa Anas ibn Malik amesema: "Tulikuwa mbele ya Umar akasema, tumekatazwa kujikalifisha." Naam hivi ndivyo afanyavyo Bukhari kwa kila hadithi ambayo inazo harufu zinazomkosoa Umar. Basi ni vipi msomaji ataufahamu ukweli wa mambo kutokana na hadithi hii iliyokatwa? Bila shaka nia ya Bukhari ni kumsitiri Umar kutokufahamu kwake maana ya Al-abb na akasema tu: Tumekatazwa kujikalifisha.

3). Ibn Majah ameandika ndani ya Sunan yake Juz.2 uk.227 na Al-hakim ndani ya Mustadrak juz.2 uk.59 na Abu Dawood ndani ya Sunan yake juz.2 uk.402 na Bayhaqi ndani ya Sunan yake juz.6 uk. 264 na Ibn Hajar ndani ya Fat-hulbari na wengineo pia wameandika. Kutoka kwa Ibn Abbas kwamba amesema: "Umar aliletewa mwenda wazimu wa kike aliyezini, basi akawataka watu ushauri, kisha akaamuru apigwe mawe. Mara Ali ibn Abi Talib akapita pale akauliza ana nini huyu? Wakasema, Ni mwenda wazimu katika ukoo fulani amezini, na Umar ameamuru apigwe mawe. Ali akasema mrudisheni, kisha (Ali) alimuendea Umar akasema, Hujui ya kwamba kalamu imenyanyuliwa kwa mwenda wazimu mpaka atakaporejelewa na akili. na mwenye kulala naye mpaka atapoamka na motto mpaka atapobalehe? Basi Umar akamuachilia yule mwenda wazimu na akasema, Lau kama si Ali Umar angeangamia."[1].

Lakini Bukhari ameivuruga riwaya hii, sasa basi ni vipi watu watautambua ujinga wa Umar namna asivyoweza kuyafahamu mambo yanayohusu adhabu ambazo kitabu cha Mwenyezi Mungu kimeziweka na Mtume kazibainisha? Ilikuwaje akakikalia cheo cha Ukhalifa mtu ambaye

1. Sunan Ibn Majah, Juz.2 Uk.227. na Mustadrak Al-Hakim, Juz.2, Uk.50. Sunan Abu Dawood, Juzuu.2. 402. Na Sunan Al-Bayhaqi, Juz.6. Uk.264.

hii ndiyo sifa yake? Haiwezakani kabisa kwa Bukhari kuitaja riwaya hii kikamilifu kwa sababu tu ndani yake zimo fadhila za Imam Ali ibn Abi Talib ambaye alikuwa akikesha akiwafundisha watu wasiyoyajua, na pia hawezi kuitaja kikamilifu kwa sababu Umar mwenyewe amekiri kwamba. "Lau kama si Ali Umar angeangamia." Basi hebu tumuangalie Bukhari ni jinsi gani anavyoigeuza riwaya hii na kuificha. Bukhari amethibitisha ndani ya sahih yake katika Kitabid-Muhaaribina min ah-lil-kufri war-riddah Babu la yurjamul-majnunn walamaj-nunah. Bukhari bila ya kutaja sanad yoyote amesema. "Ali alimwambia Umar hujui kwamba kalamu imenyanyuliwa kwa mwenda wazimu mpaka azindukane na mtoto mpaka abalehe na mwenye kulala mpaka aamke?

Naam, bila shaka huu ni mfano hai unaonesha namna ya utendaji kazi wa hadithi ulivyo kwa Bukhari, kwani yeye anaikata hadithi pindi inapokuwa ndani yake kuna fedheha kwa Umar. Na pia huifupisha hadithi kama inafadhila na sifa kwa Imam Ali, basi hawezi kabisa kuiandika hadithi hiyo kikamilifu.

4). Muslim ameandika ndani ya sahih yake katika Kitabul-hudud Babu haddi shaaribil-khamri. Imepokewa kutoka kwa Anas ibn Malik, kwamba Mtume **(s.a.w.w)** aliletewa mtu aliyekunywa pombe akampiga kwa fimbo mbili kiasi (mara) arobaini, (Anas) amesema, na Abubakr pia alifanya hivyo hivyo. Amma Umar alipokuwa khalifa aliwashauri watu, basi Abdurrahman ibn A'uf akasema uchache wa adhabu ni bakora themanini, Umar akaamuru hivyo." Na Bukhari kama kawaida yake hataki kudhihirisha kutokujua kwa Umar namna hukmu ilivyo katika adhabu, kwani ni vipi anawashauri watu kuhusu adhabu inayoeleweka ambayo Mtume aliitekeleza kisha baada yake Abubakr aliifanya? Bukhari ameandika ndani ya sahih yake katika Kitabul-Hudud Babu Majaa 'a fi dharbi sharibil-khamr.

Imepokewa kutoka kwa Anas ibn Malik kwamba, Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** alipiga haddi kuhusu pombe kwa kutumia fimbo na kiatu na Abubakr alipiga mijeledi arobaini.

5). Wanahistoria na wataalamu wa hadithi ambao waliandika juu ya maradhi ya Mtume na kufariki kwake na namna alivyowataka Masahaba awaandikie maandiko ambayo kamwe hawatapotea baada yake, na tukio hilo likaitwa kuwa ni msiba wa siku ya Al-Hamisi. Na wameandika pia namna Umar alivyopinga na akasema kuwa, "Mtume anaweweseka." Mwenyezi Mungu apishe mbali. Na Bukhari ameandika ndani ya sahih yake katika Kitabul-jihad Babu Hal-Yustash-fau' Ila Ah-lid-Dhimmah wamua 'malatihim. Naye Muslim ameandika ndani ya sahihi yake katika Kitabul-wasiyyah Babu Tarkil-wasiyyah Liman laisa lahu shaiun yusii-fihi. Imepokewa kutoka kwa ibn Abbas (r.a) kwamba amesema: "**Siku ya al-khamisi, kulikuwa nini siku hiyo ya al-khamisi? Kisha akalia mpaka machozi yake yakalowanisha changarawe. Halafu akasema siku hiyo ya al-Khamisi Mtume (s.a.w.w) maumivu yake yalizidi, akasema, Nileteeni karatasi nikuandikieni maandiko ambayo kamwe hamtapotea baada ya maandiko hayo. Basi watu wakazozana, na haifai kuzozana mbele ya Mtume, kisha wakasema: Mtume wa Mwenyezi Mungu anaweweseka, Mtume akawaambia, Niacheni kwani hali niliyonayo mimi ni bora kuliko hivyo mnavyodai dhidi yangu. Aliusia wakati wa kufa kwake**

**mambo matatu: Waondoeni washirikina katika bara Arabu, na mtekeleze ridhaa ya wawakilishi kama vile mimi nilivyokuwa nawatekelezea, na lile la tatu nimelisahau**."

Naam, huu ndiyo msiba wa siku ya al-khamisi ambao Umar alichukua nafasi ya ushindi akampinga Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)** na akamzuwia kuandika kutokana na maneno yale machafu (aliyoyatamka) ambayo yanapingana na kitabu cha Mwenyezi Mungu. Maneno hayo ni kuwa: "**Eti Mtume anaweweseka**." Nao Bukhari na Muslim hapa wameinakili hadithi hii kwa ibara sahihi ambayo Umar aliitamka na hawakuibadili kwa kuwa jina la Umar halikutajwa hapa, na kuihusisha kauli hii mbaya kwa mtu asiyejulikana hapana madhara. Lakini pale linapokuja jina la Umar ndani ya riwaya ambayo inataja kuwa yeye Umar ndiye aliyetamka maneno yale inakuwa vigumu kwa Bukhari na Muslim kuiacha riwaya hiyo kama ilivyo, kwani inamfedhehesha Khalifa na inadhihirisha ukweli wake uliyo wazi na kuumbua kiwango cha yeye kutokuwa kwake na heshima mbele ya Mtume **(s.a.w.w)**.

Na Umar ndiye ambaye alikuwa akimpinga Mtume muda wote wa uhai wake katika mambo mengi, na Bukhari na wengine mfano wake walifahamu kwamba neno hili pekee linatosha kuamsha hisiya za kila Mwislamu dhidi ya Khalifa Umar hata hao Masunni wenyewe, hivyo basi wakafanya makusudi kuficha ukweli. Sasa hiyo ndiyo fani yao mashuhuri kuhusu mambo kama haya, na wakabadilisha neno Anaweweseka wakaweka neno lisemalo Maumivu yamemzidia ili waitupilie mbali ile ibara chafu. Hebu basi angalia vile Bukhari na Muslim walivyoandika kuhusu maudhui hii hii ya msiba. Imepokewa kutoka kwa ibn Abbas amesema, "Mtume wa Mwenyezi Mungu alipokaribia kufariki, na watu walikuwemo ndani ya nyumba (yake) na Umar ibn Khattab akiwa yu miongoni mwao, Mtume **(s.a.w.w)** alisema: Njooni nikuandikieni maandiko ambayo kamwe hamtapotea baada yake.

Basi Umar akasema, Bila shaka Mtume kazidiwa na maradhi nanyi mnayo Qur'an, kinatutosha Kitabu cha Mwenyezi Mungu, hapo watu waliokuwemo humo ndani wakahitilafiana na kuzozana, miongoni mwao wakasema sogeeni Mtume akuandikieni maandiko ambayo hamtapotea baada yake, na miongoni mwao wakasema alivyosema Umar.

Walipozidisha makelele na kuhitilafiana mbele ya Mtume **(s.a.w.w)**, Mtume akawaambia, Ondokeni. ... Abdallah ibn Mas-ud amesema: Ibn Abbas alikuwa akisema, Msiba mkubwa kuliko yote ni ule uliyopita baina ya Mtume wa Mwenyezi Mungu na baina ya kuwaandikia maandiko kutokana na kuhitilafiana kwao na fujo zao. Na kwa kuwa Muslim alichukua kutoka kwa mwalimu wake ambaye ni Bukhari, basi sisi tunamwambia Bukhari, "Namna yoyote ile utakavyoipinda ibara na namna utakavyojaribu kuuficha ukweli hakika hicho ulichokiandika kinatosha kuwa ni hoja dhidi yako na dhidi ya bwana wako Umar, kwani tamko la kuweweseka au maradhi yamemzidi, lina matokeo ya aina moja kwa kuwa yeyote mwenye kuzingatia atakuta kwamba watu hadi leo wanasema, "Masikini fulani homa imemzidi mpaka anaweweseka." Na hasa tutakapoongezea juu ya neno hilo, Mnayo Qur'ani, kinatutosha Kitabu cha

Mwenyezi Mungu. Na maana ya hilo ni kwamba Mtume **(s.a.w.w)** mambo yake ndiyo yamefikia kikomo na kuwepo kwake ni sawa kama hayupo.

Nami nampa changamoto kila mwanachuoni afanye mazingatio katika tukio hili peke yake bila ya mambo mengine yoyote, na bila ya kufuatilia yaliyopita, basi huenda akaamsha hisia zake mbaya mno dhidi ya Khalifa (Umar) ambaye aliunyima umma (wa Kiislamu) uongofu na ikawa ni sababu moja kwa moja ya kupotea kwa umma huu. Hivi ni kwa nini tunaogopa kusema ukweli maadam ukweli huo ni katika kumtetea Mtume wa Mwenyezi Mungu **(s.a.w.w)**? Na zaidi ya hapo tunaitetea Qur'ani na mafunzo ya Uislamu kwa ukamilifu wake. Mwenyezi Mungu anasema:"Wala msiwaogope watu, basi niogopeni mimi, wala msibadilishe aya zangu kwa thamani ndogo (ya duniani) na wale wasiohukumu kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndiyo makafiri."

Ni kwa nini baadhi ya wanachuoni hadi leo hii katika zama za elimu na nuru (bado) wanajaribu kwa juhudi zao zote kuuficha ukweli kwa kutumia tafsiri za kulazimisha ambazo wanaziunda, tafsiri ambazo hazisaidii chochote? Hebu tazama mambo aliyoyazua mwanachuoni aitwaye Muhammad Fuad Abdul-Baqii ndani na sherehe yake ya kitabu kiitwacho, Al-Lu-ulu-u Wal-mar-jaan fimat-Tafaqa Alayhis-Shaykhain, pale alipoileta hadithi ya msiba wa siku ya Al-khamis amesema akilifafanua tikio hilo. "Nileteeni kitabu, kwa maana ya vifaa vya kuandikia kama vile kalamu na wino, au alikusudia kitabu kwa maana ya kitu ambacho huandikwa ndani yake kama vile karatasi na kombe (mfupa wa begani). Jambo lililowazi hapo ni kwamba, maandiko haya aliyotaka kuandika Mtume, si mengineyo bali alitaka kumthibitisha Abubakr kwenye Ukhalifa, lakini wao walipozozana na maradhi ya Mtume yakawa yamezidia aliacha kufanya hivyo na akatumia kumbainisha kwa msingi alioufanya kupitia (kusalisha) sala."

ameenedelea kusherehesha maana ya neno Hajara (yaani anaweweseka) anasema mwanachuoni huyu, "Hajara, Ibn Bat-tal ameidhania kuwa maana yake ni Amechanganyikiwa, naye Ibn At-tiin amesema maana yake ni Kuweweseka. Na kwa maana hiyo si muafaka kuambiwa Mtume kutokana na daraja yake tukufu, na inawezekana kuwa makusudio yake ni kwamba, Mtume wa Mwenyezi Mungu amekuacheni, inayotokana na kuhama ambayo ni dhidi ya kuwepo, kutokana na yaliyomfikia miongoni mwa mambo yenye kufika yanayohusu Uungu, na ndiyo maana alisema: "Fii rafiiqil A 'ala. " Na amesema Ibnul-Athir kwamba, neno Hajara limekuja kwa njia ya kuuliza, na hamza ya kuulizia inayoleta maana ya Je, maneno ayasemayo Mtume yamebadilika na yamechanganyikana kwa ajili ya maradhi aliyo nayo? Imeondoshwa, na ndicho kilicho bora kukisema kuhusiana na maana ya Hajara. Na wala haiwezi kufanywa kuwa ni maelezo yenye kumaanisha ubaya au kuweweseka, na msemaji (wa hilo neno la Hajara) alikuwa ni Umar, na hatudhanii kuwa Umar anaweza kutamka hivyo." (Mwisho wa maneno yake).

Sisi tunakujibu ewe mwanachuoni mheshimiwa kwamba, "Dhana haitoshelezi kitu mbele ya haki, kunatutosheleza kukiri kwako kwamba, msemaji wa tamko hili baya alikuwa Umar. Nani aliyekuambia kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu alitaka kuandika juu ya ukhalifa wa Abubakr? Na Je, Umar angelipinga hilo? Je, ni Umar huyo huyo ambaye

aliyeziimarisha nguzo za Ukhalifa wa Abubakr na akawalazimisha watu wakubali kwa nguvu mpaka akatishia kuichoma nyumba ya Bibi Fatmah (a.s)? Je, yuko mwanachuoni mwingine aliyedai madai kama haya asiyekuwa wewe? Kinachofahamika kwa wanachuoni wa zamani mpaka sasa hivi ni kwamba, Ali ibn Abi Talib ndiye aliyeteuliwa na Mtume awe Khalifa japo tamko linalohusu uteuzi huo hawalikubali. Lakini yanakutosh yale aliyoyaandika Bukhari ndani ya sahih yake katika Kitabul-Wasaya, juzuu ya 3 uk. 186 amesema: "**Kuna watu fulani walizungumza mbele ya Aisha kwamba, Ali (r.a) alikuwa ndiyo wasii (wa Mtume), basi Aisha akasema, Ni wakati gani (Mtume) alipousia juu yake na hali mimi nilikuwa nimemuegemeza (Mtume) kifuani mwangu, akaomba aletewe chombo (fulani) nami nikiwa nimempakata miguuni mwangu basi mara punde alifariki, hivyo ni wakati gani aliousia juu yake**?".

Na Bukhari ameiandika hadithi hii kwamba, ndani yake imo dalili inayokanusha wasia, na hili ni jambo linalomfurahisha Bukhari. Lakini sisi tunasema kwamba, "Wale waliozungumza mbele ya mama Aisha kuwa Mtume aliusia Ukhalifa kwa Ali ni wakweli, kwa kuwa Aisha hakuwapinga na yeye mwenyewe hakukanusha wasia ule, lakini aliuliza kama mtu apingaye akasema, Ni lini aliusia? Nasi tunamjibu aliusia mbele ya Masahaba watukufu wakati yeye mama Aisha akiwa hayupo, na hapana shaka kwamba masahaba hao walimtajia mama Aisha wakati Mtume alipousia juu ya Ali kuwa Khalifa, lakini watawala na waliovamia (huo Ukhalifa) walizuia hoja kama hizi kuelezwa (hadharani) kama ambavyo jambo la tatu (miongoni mwa mambo aliyoyausia Mtume) walilisahau. Kwa hiyo siasa zilisimama kidete kuufuta ukweli huu, kwani Umar mwenyewe alipata kutamka wazi kuwa alimzuia Mtume wa Mwenyezi Mungu asiandike yale maandiko pale tu alipofahamu kwamba yanahusiana na Ukhalifa wa Ali ibn Abi Talib. Ibn Abil-hadid ameyaandika majibizano yaliyopita baina ya Umar ibn Khat-tab na Abdallah ibn Abbas, Umar alisema katika majibizano hayo kama ifuatavyo.

"Hivi katika nafsi ya Ali kumebakia kitu kuhusu Ukhalifa?" Ibn Abbas akasema: "Ndiyo." Umar akasema:"Hapana shaka Mtume wa Mwenyezi Mungu alitaka kulibainisha jina lake (Ali) wakati wa maradhi yake, mimi nikamzuia kwa kumuonea huruma na kuulinda Uislamu." Ewe mwanachuoni mtukufu, kwa nini unaukimbia ukweli? Inashangaza mno, badala ya wewe kuchangia kuudhihirisha ukweli baada ya zama za kiza pamoja na Banu Umayyah na Banu Abbas kuondoka, ninyi mnaongezea juu ya giza hilo kifuniko na mapazia ili muwazuie watu wengine wasiufahamu ukweli na kuufikia. Ikiwa wewe uliyasema hayo uliyoyasema kwa nia njema, basi bila shaka mimi namuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu akuongoze na akufungue fahamu zako.

6). Kama ambavyo Bukhari amefanya mengi kubadilisha na kufuta, na pia kuvuruga hadithi za Mtume ambazo zinaonyesha unyonge na dosari walizonazo Abubakr na Umar. Kwa mara nyingine Bukhari anakusudia kulivuruga tukio mashuhuri la kihistoria ambalo ndani yake Mtume wa Mwenyezi Mungu alizungumza jambo ambalo Bukhari hakulipenda, basi ameipuuza kabisa hadithi hiyo kwa sababu kilichomo kinampa hadhi Ali juu ya Abubakr.

Wanachuoni wa Kisunni wamesimulia ndani ya Sihahi zao na Musnad zao, kama vile Tirmidhi ndani ya Sahih yake, Al-Hakim ndani ya Mustadrak yake, Ahmad ibn Hambal ndani ya Musnad yake, Imam Nasai ndani ya Khasais yake, Tabari katika tafsiri yake, Suyuti ndani ya tafsiri yake iitwayo Ad-Durrul-Manthur na Ibnul-Athir ndani ya tarikh yake, pia Kanzul-Ummal na Zamakhishari ndani ya Al-Kash-Shaf na wengineo wengi, wote wamethibitisha kwamba:

"Mtume wa Mwenyezi Mungu alimtuma Abubakr (r.a) akamuamuru akatangaze maneno haya yafuatayo, Bara-Atun-minallahi Warasulihi, kisha akamfuatisha nyuma yake Ali (r.a) na akamuamuru Ali akatangaze maneno hayo yeye Ali, basi Ali (r.a) akasimama katika siku kumi za mfunguo tatu akatangaza akasema: Hakika Mwenyezi Mungu yuko mbali na washirikina, na pia Mtume wake (yuko mbali nao). Basi nendeni mkizunguka katika ardhi miezi minne, na asihiji mshirikina baada ya mwaka huu. Na yeyote asitufu al-Ka'aba hali akiwa uchi." Abubakr (r.a) alirudi kisha akasema,"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, kuna jambo limeshuka kuhusiana na mimi?" Mtume akasema: "**Hapana jambo, lakini Jibril amenifikia na amesema, Hawezekani kabisa mtu yeyote kutekeleza amri hii isipokuwa wewe (yaani Mtume) au mtu anayetokana na wewe**."

## SHARTI YA KUCHAPA

Sharti ya kuchapa au kusambaza ni kutaja rejeo hili. haki zote zimehifadhiwa na Taasisi ya Al-Hasanain Taasisi ya Imamu Husein (a.s)

Site ya Al-Imaamaini Al-Hassanaini (a.s) ya usambazaji wa utamaduni wa Kiislamu na mafunzo ya Kidini.

## MWISHO WA KITABU

## YALIYOMO


**1** ........................................ **WAULIZE WANAOFAHAMU**
KIMEANDIKWA NA: MUHAMMAD TIJANI AS-SAMAWI AT-
1 .............................................................. TUNISI
1 ....... KIMETARJUMIWA NA: MUSABAH SHABAN MAPINDA
2 ........................................................... DIBAJI
KWA JINA LA MWENYE ENZI MUNGU MWINGI WA REHEMA
6 ........................................ MWENYE KUREHEMU
KISHA SALA NA SALAMU ZIMSHUKIE MBORA WA MITUME
6 ..................................... NA AALI ZAKE WATUKUFU
**14** ...................................... **WAULIZE WANAOFAHAMU**
MLANGO WA KWANZA: YALE YANAYOMUHUSU MUUMBA
16 ..................................................... MTUKUFU
**27** ...................................... **WAULIZE WANAOFAHAMU**
MLANGO WA PILI KATIKA MAMBO YANAYOMUHUSU
27 ............................................... MTUME (s.a.w.w).
**49** ...................................... **WAULIZE WANAOFAHAMU**
49 ..... KAULI YA AHLU-DHIKRI KUHUSU MTUME (S.A.W.W)
49 ............................................. MLANGO WA TATU
YANAYOWAHUSU WATU WA NYUMBA YA MTUME
49 ...................................................... (S.A.W.W)
**57** ...................................... **WAULIZE WANAOFAHAMU**
57 .. UMMUL-MU'MININA AISHA ANAISHUHUDIA NAFSI YAKE
**61** ...................................... **WAULIZE WANAOFAHAMU**
**67** ...................................... **WAULIZE WANAOFAHAMU**
**73** ...................................... **WAULIZE WANAOFAHAMU**
MSIMAMO WA AISHA DHIDI YA AMIRUL-MUUMININA ALI
73 ........................................................... (A.S.)
**81** ...................................... **WAULIZE WANAOFAHAMU**
81 .................................... MWISHO WA UCHAMBUZI
84 ............................................. MLANGO WA NNE
84 ............... YANAYOWAHUSU MASAHABAKWA UJUMLA
**91** ...................................... **WAULIZE WANAOFAHAMU**
91 ............... BUKHARI AMEANDIKA KATIKA SAHIHI YAKE
**106** .................................... **WAULIZE WANAOFAHAMU**
UTENDAJI WA MASAHABA KUHUSU MAAMRISHO YA MTUME
106 ....................... (s.a.w.w) BAADA YA KUFARIKI KWAKE
NAMNA WALIVYOIPOTOSHA SUNNA YA MTUME (s.a.w.w)
106 ...........................................................

**118** ...................................... **WAULIZE WANAOFAHAMU**
KAULI YA AHLUL-DHIKRI KUHUSU BAADHI YAMASAHABA 118
**123** ...................................... **WAULIZE WANAOFAHAMU**
123 ............................................ MLANGO WA TANO
UNAWAHUSU MAKHALIFA WATATU ABUBAKR, UMAR, NA
123 ....................................................... UTHMAN
**131** ...................................... **WAULIZE WANAOFAHAMU**
131 ........... ABUBAKR BAADA YA UHAI WA MTUME (s.a.w.w)
NAMNA ALIVYOMPINGA BIBI FATMAH, KWA
131 .............................. KUMNYANG'ANYA HAKI YAKE
**140** ...................................... **WAULIZE WANAOFAHAMU**
ABUBAKR ALIWAUA WAISLAMU WALIOKATAA KUMPA
140 ............................................................ ZAKA
**153** ...................................... **WAULIZE WANAOFAHAMU**
ABUBAKR ANAMPA UKHALIFA JAMAA YAKE UMAR, NA ANAKHALIFU MAANDIKOYALIYO WAZI KUHUSU JAMBO
153 ............................................................ HILO
**170** ...................................... **WAULIZE WANAOFAHAMU**
UTHMAN IBN A'FFAAN ANAFUATA SUNNA YA JAMAA ZAKE KATIKA KUYAPINGA MAANDIKOYA QUR'AN NA SUNNA YA
170 ....................................................... MTUME
**175** ...................................... **WAULIZE WANAOFAHAMU**
175 ............................................ MLANGO WA SITA
175 ................................... YANAYOHUSU UKHALIFA
**185** ...................................... **WAULIZE WANAOFAHAMU**
185 ... TISHIO LA KUCHOMA MOTO NYUMBA YA BIBI FATIMA
**191** ...................................... **WAULIZE WANAOFAHAMU**
191 ............................................ MLANGO WA SABA
191 .. YANAYOHUSU HADITHI TUKUFU ZA MTUME (s.a.w.w)
**200** ...................................... **WAULIZE WANAOFAHAMU**
MAMA AISHA ALIACHA HURU WATUMWA AROBAINI KWA
200 .... AJILI YA KUTOA KAFARA YA KUVUNJA KIAPO CHAKE
**210** ...................................... **WAULIZE WANAOFAHAMU**
210 MTUME ANAJIPINGA MWENYEWE KATIKA HADITHI ZAKE
**220** ...................................... **WAULIZE WANAOFAHAMU**
220 ............................................ MLANGO WA NANE
220 .. YANAYOZIHUSU SIHAH MBILI, BUKHARI NA MUSLIM

235 .......................................... SHARTI YA KUCHAPA
235 .......................................... MWISHO WA KITABU
236 ........................................................ YALIYOMO